BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA HESABU ZA SERIKALI YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

FEBRUARI, 2025

YALIYOYO

UTANGULIZI..... 1

WAJUMBE NA SEKRETARIETI YA KAMATI YA PAC 2

Waheshimiwa Wajumbe:..... 2

Sekretarieti: 3

UTARATIBU WA KAZI ZA KAMATI 4

MGONGANO WA MASLAHI 4

UCHUNGUZI WA KAMATI YA PAC KUHUSU UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA TAWALA ZA MIKOA, MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023 5

BARAZA LA MANISPAA MJINI..... 5

Hoja nambari 6.3.2.1: Kutokuwepo Taarifa za Kuhesabu Mali (Stock Taking)..... 5

Majibu ya Uongozi wa Baraza.....5

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 5

Hoja nambari: 6.3.2.2: Kutokuwepo kwa mfumo maalum wa kuhifadhi taarifa za vianzio vya ukusanyaji wa mapato..... 6

Majibu ya Uongozi wa Baraza.....7

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 7

Maagizo ya Kamati ya PAC.....8

Hoja Nambari: 6.3.2.3 Kutokuwepo kwa mchanganuo wa vyanzo vya mapato katika mfumo wa makusanyo MUTM. 8

Majibu ya Uongozi wa Baraza.....9

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 9

Hoja Nambari: 6.3.2.4 Tofauti ya Bakaa ya Fedha ya Kufunga na Kufungulia Mwaka shilingi 178,446,089 9

Majibu ya Uongozi wa Baraza.....10

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 10

Maagizo ya Kamati ya PAC.....10

Hoja Nambari: 6.3.2.5 Kutofanyika kwa usulihishi wa kibenki Bank reconciliation na taarifa za matumizi.....11

Majibu ya Uongozi wa Baraza.....11

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 12

Maagizo ya Kamati ya PAC.....12

HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI UNGUJA.....13

Hoja nambari 6.3.7.1: Tofauti ya Bakaa ya Fedha kwenye hesabu ya mwisho wa mwaka na bakaa iliopo benki shilingi 44,622,028.94 13

Majibu ya Uongozi wa Halmashuri 13

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 13

Maagizo ya Kamati ya PAC.....14

Hoja nambari 6.3.7.2: Kukosekana kwa mapato ya leseni za skuli binafsi shilingi 1,500,000 14
Majibu ya Uongozi wa Halmashuri 15
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 15
Hoja nambari 6.3.7.3: Kutokuwekewa alama za Utambulisho kwa samani za Ofisi. 15
Majibu ya Uongozi wa Halmashuri 16
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 16
Maagizo ya Kamati ya PAC.....16
Hoja nambari 6.3.7.4: Kutokufanyika kwa tathmini ya utendaji kazi (Performance Appraisal)....16
Majibu ya Uongozi wa Halmashuri 17
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 17
Maagizo ya Kamati ya PAC.....17
Hoja nambari 6.3.7.5: Kutokuwepo kwa Mpango Maalum wa Mafunzo. 17
Majibu ya Uongozi wa Halmashuri 19
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 19
Maagizo ya Kamati ya PAC.....19
BARAZA LA MJI WETE 20
Hoja nambari 6.3.8.1: Kukosekana kwa Nyaraka za uchambuzi wa madeni shilingi 33,486,026.74. 20
Majibu ya Uongozi wa Baraza la Mji Wete 20
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 21
Maagizo ya Kamati ya PAC.....21
Hoja nambari 6.3.8.2: Malipo ya Fedha ambayo Hayajawafikia Wadai shilingi 3,165,220.74. 22
Majibu ya Uongozi wa Baraza la Mji Wete 23
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 23
Maagizo ya Kamati ya PAC.....23
Hoja nambari 6.3.8.3: Hati za Malipo zenye nyaraka pungufu shilingi 5,005,220.74. 24
Majibu ya Uongozi wa Baraza la Mji Wete 25
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 25
Maagizo ya Kamati ya PAC.....25
Hoja nambari 6.3.8.4: Kutokulipwa kwa deni la muda mrefu la ukodishwaji wa Bekari shilingi 6,200,000 26
Majibu ya Uongozi wa Baraza la Mji Wete 26
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 26
Maagizo ya Kamati ya PAC.....26
Hoja nambari 6.3.8.5: Dosari katika mradi wa ujenzi wa vituo vya daladala 27
Majibu ya Uongozi wa Baraza la Mji Wete 27
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 28
Maagizo ya Kamati ya PAC.....28
BARAZA LA MANISPAA CHAKE CHAKE - PEMBA. 29
Hoja nambari 6.3.9.1: Kutokuwiana kwa fedha za bajeti zilizorikodiwa baina ya mipango kazi na ripoti ya utekelezaji Shilingi 65,064,069 29
Majibu ya Uongozi wa Baraza.....29
Uchunguzi wa Kamati PAC.....30

Hoja nambari 6.3.9.2: Kukosekana kwa mkataba wa ununuzi wa mafuta shilingi 69,050,540.....30
Majibu ya Uongozi wa Baraza.....32
Uchunguzi wa Kamati ya PAC.....32
Hoja nambari 6.3.9.3: kukosekana kwa usawa wa taarifa za Mapato yaliokusanywa Baina ya Mfumo wa MUTM na Taarifa Nyengine za Mapato shilingi 22,247,000.....32
Majibu ya Uongozi wa Baraza.....34
Uchunguzi wa Kamati ya PAC.....34
JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU).....35
Hoja namba 7.1.2.1: Kutokuwepo kwa mpango maalumu wa mafunzo.....35
Majibu ya Uongozi wa JKU.....35
Uchunguzi wa Kamati ya PAC.....35
Maagizo ya Kamati ya PAC.....36
Hoja namba 7.1.2.2: Ucheleweshwaji wa vifaa vya ujenzi.....36
Majibu ya Uongozi wa JKU.....38
Uchunguzi wa Kamati ya PAC.....38
Hoja namba 7.1.2.3: Kukosekana kwa uhalisia katika utayarishwaji wa nyaraka za makisio ya gharama za ujenzi (BOQ) zilizopelekea kuwepo tofauti shilingi 258,747,000.....38
Majibu ya Uongozi wa JKU.....41
Uchunguzi wa Kamati ya PAC.....41
Maagizo ya Kamati ya PAC.....42
Hoja namba 7.1.2.4: Dosari zilizobainika katika ujenzi wa majengo ya Afisi na Mahanga ya Askari.....42
Majibu ya Uongozi wa JKU.....42
Uchunguzi wa Kamati ya PAC.....42
Maagizo ya Kamati ya PAC.....43
Majibu ya Uongozi wa JKU.....43
Uchunguzi wa Kamati ya PAC.....43
Maagizo ya Kamati ya PAC.....44
Majibu ya Uongozi wa JKU.....44
Uchunguzi wa Kamati ya PAC.....44
Maagizo ya Kamati ya PAC.....44
Hoja namba 7.1.2.5: Malipo ambayo hayakufuata taratibu za manunuzi shilingi 144,966,683....45
Majibu ya Uongozi wa JKU.....46
Uchunguzi wa Kamati ya PAC.....46
Maagizo ya Kamati ya PAC.....46
JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU) - PEMBA.....47
Hoja namba 7.1.2.6: Uwepo wa mashine ambazo hazitumiki zenye thamani ya shilingi 44,918,400.....47
Majibu ya Uongozi wa JKU.....47
Uchunguzi wa Kamati ya PAC.....48
Maagizo ya Kamati ya PAC.....48
Hoja nambari 7.1.2.7: Nyaraka za gari za JKU kuonesha umiliki wa watu binafsi.....48
Majibu ya Uongozi wa JKU.....49
Uchunguzi wa Kamati ya PAC.....50

Majibu ya Uongozi wa JKU....51
Uchunguzi wa Kamati ya PAC....52
Maagizo ya Kamati ya PAC....53

CHUO CHA MAFUNZO....53

Hoja nambari 7.1.3.1: Utambuzi wa mapato kinyume na Muongozo....53
Majibu ya Uongozi wa Chuo cha Mafunzo....53
Uchunguzi wa Kamati ya PAC....54
Maagizo ya Kamati ya PAC....54

Hoja nambari 7.1.3.2: Utumiaji usioridhisha wa rasilimali za Chuo cha Mafunzo....54
Majibu ya Uongozi wa Chuo cha Mafunzo....55
Uchunguzi wa Kamati ya PAC....56
Maagizo ya Kamati ya PAC....56

Hoja nambari 7.1.3.3: Dosari zilizobainika katika zabuni nambari SMS/DO4/G/RNCB/2022/2023/02 ya Ununuzi wa Chakula cha Askari na Wanafunzi....56
Majibu ya Uongozi wa Chuo cha Mafunzo....57
Uchunguzi wa Kamati ya PAC....58
Maagizo ya Kamati ya PAC....58

Hoja nambari 7.1.3.4: Dosari zilizobainika katika zabuni nambari SMS/DO3/G/RNCB/2022/2023/03 ya Ununuzi wa Mafuta....58
Majibu ya Uongozi wa Chuo cha Mafunzo....59
Uchunguzi wa Kamati ya PAC....59
Maagizo ya Kamati ya PAC....59

Hoja nambari 7.1.3.5: Mazingira yasiyoridhisha ya Makaazi ya Askari wa Chuo cha Mafunzo....60
Majibu ya Uongozi wa Chuo cha Mafunzo....60
Uchunguzi wa Kamati ya PAC....60
Maagizo ya Kamati ya PAC....61

KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU)....62

Hoja nambari 7.1.5.1: Ukiukwaji wa taratibu za malipo ya posho mbali mbali....62
Majibu ya Uongozi wa KZU....63
Uchunguzi wa Kamati ya PAC....63
Maagizo ya Kamati ya PAC....64

Hoja nambari 7.1.5.2: Kutokuandaliwa kwa Sera za Kikosi cha Zimamoto na Uokozi....64
Majibu ya Uongozi wa KZU....64
Uchunguzi wa Kamati ya PAC....65

Hoja nambari 7.1.5.3: Kukosekana kwa uhalisia wa Makadirio ya Matumizi na utekelezaji wake wa shilingi 2,197,000,298....65
Majibu ya Uongozi wa KZU....67
Uchunguzi wa Kamati ya PAC....67

Hoja nambari 7.1.5.4: Dosari katika utekelezaji wa Mkataba wa ununuzi wa Vifaa vya Ujenzi TZS 3,480,000,000....67
Majibu ya Uongozi wa KZU....68
Uchunguzi wa Kamati ya PAC....68
Maagizo ya Kamati ya PAC....68

Hoja nambari 7.1.5.5: Dosari katika usimamizi wa Miradi ya Maendeleo ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi 69
Majibu ya Uongozi wa KZU 70
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 71
Maagizo ya Kamati ya PAC 71

Hoja nambari 7.1.5.6: Upungufu wa vifaa vya kuzimia moto 71
Majibu ya Uongozi wa KZU 75
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 75
Maagizo ya Kamati ya PAC 75

UCHUNGUZI WA KAMATI YA PAC KUHUSU UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA TAASISI ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023 76

MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO 76

Hoja nambari 4.1.2.1: Kukosekana kwa umiliki wa Mifumo ya Wakala wa Serikali Mtandao kuwa ni Mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar 76
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao 77
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 78
Maagizo ya Kamati ya PAC 78

Hoja nambari 4.1.2.2: Seva za uzalishaji wa Data za Mifumo ya Serikali Mtandao zipo katika Kituo cha Data kilichopo Dar-es-Salaam 78
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao 79
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 79
Maagizo ya Kamati ya PAC 80

Hoja nambari 4.1.2.3: Kushindwa kuwasilisha Mfumo wa Manunuzi uliohitajika kulingana na hadidu za rejea za mkataba 80
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao 80
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 81
Maagizo ya Kamati ya PAC 81

Hoja nambari 4.1.2.4: Mifumo wa e-Proz unatekelezwa na kufanya kazi kwa njia ya Mfumo kama Huduma (System-as-a-Service) 81
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao 82
Uchunguzi na Maagizo ya Kamati ya PAC 83

Hoja nambari 4.1.2.5: Ukiukwaji wa Taratibu za malipo uliosababisha gharama kubwa za malipo ya tozo ya huduma ya Mfumo wa e-Proz shilingi 4,500,873,948.53 83
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao 84
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 85
Maagizo ya Kamati ya PAC 85

Hoja nambari 4.1.2.6: Malipo ya tozo ya huduma yaliyofanywa kabla ya muda wa malipo shilingi 1,459,562,114 85
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao 86
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 86

Hoja nambari 4.1.2.7: Kuwepo kwa tofauti baina ya fedha zinazodaiwa na Ozone International pamoja na kiwango halisi kinachotakiwa kulipwa na Serikali 86

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao....89
Uchunguzi wa Kamati ya PAC....89

Hoja nambari 4.1.2.8: Kutokukatwa tozo ya huduma ya Mfumo wa e-Proz kwa Wasambazaji waliotunukiwa zabuni....89
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao....90
Uchunguzi wa Kamati ya PAC....90

Hoja nambari 4.1.2.9: Kuwepo kwa zabuni ambazo hazikutekelezwa kwenye orodha ya malipo ya matumizi ya mfumo wa e-Proz....90
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao....91
Uchunguzi wa Kamati ya PAC....91

Hoja nambari 4.1.2.10: Kutokubainishwa kwa uwazi wa Hakimiliki ya kodi asili za utengenezwaji wa Mifumo (Software source codes)....91
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao....92
Uchunguzi wa Kamati ya PAC....92

Hoja nambari 4.1.2.11: Kutokuwepo kwa Kifungu cha uanzishwaji wa makubaliano ya Escrow .92
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao....93
Uchunguzi wa Kamati ya PAC....93
Maagizo ya Kamati ya PAC....93

Hoja nambari 4.1.2.12: Aina ya Mkataba na njia za malipo kutoendana na asili ya kazi zinazotekelezwa na mkataba (nature of assignment)....93
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao....94
Uchunguzi wa Kamati ya PAC....94
Maagizo ya Kamati ya PAC....95

Hoja nambari 4.1.2.13: Gharama za malipo ya Mkataba wa UBX zitabebwa na walipaji wa huduma....95
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao....95
Uchunguzi wa Kamati ya PAC....95
Maagizo ya Kamati ya PAC....95

Hoja nambari 4.1.2.14: Kutokuzingatiwa kwa Mpango wa Manunuzi ndani ya Mfumo wa e-Proz....96
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao....96
Uchunguzi wa Kamati ya PAC....96
Maagizo ya kamati ya PAC....96

Hoja nambari 4.1.2.15: Kuwepo kwa zabuni zisizokuwa na thamani ya fedha alizolipwa Msambazaji kupitia Mfumo wa e-Proz. 97
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao....97
Uchunguzi wa Kamati ya PAC....97

Hoja nambari 4.1.2.16: Kuwepo kwa zabuni zisizo na uhalisia wa thamani ya fedha katika Mfumo wa e-Proz....97
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao....98
Uchunguzi wa Kamati ya PAC....98
Maagizo ya kamati ya PAC....98

Hoja nambari 4.1.2.17: Mfumo wa e-Proz kushindwa kubaini vyeti vilivyomaliza muda 98
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao....99

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 100
Maagizo ya kamati ya PAC 100

Hoja nambari 4.1.2.18: Kuwepo kwa vyanzo vya mapato ambapo makusanyo yake hayapiti kwenye Mfumo wa ZanMalipo 101
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao 101
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 101
Maagizo ya kamati ya PAC 102

Hoja nambari 4.1.2.19: Kukosekana kwa kipengele cha "Bajeti Reallocation" kwenye Moduli ya Bajeti 102
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao 103
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 103

Hoja nambari 4.1.2.20: Kukosekana kwa kipengele cha "Supplementary Budget" kwenye Moduli ya Bajeti 103
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao 104
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 104
Maagizo ya kamati ya PAC 104

Hoja nambari 4.1.2.21: Kukosekana kwa kipengele cha "Version Carryover" kwenye Moduli ya Bajeti 104
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao 105
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 105

Hoja nambari 4.1.2.22: Mfumo kutofanyiwa majaribio na watumiaji (User Acceptance Testing) Wakuu (Core Team Users) wa Moduli ya Bajeti 105
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao 106
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 106
Maagizo ya kamati ya PAC 107

Hoja nambari 4.1.2.23: Kukosekana kwa nyaraka muhimu za utengenezwaji wa Mfumo wa BAMAS 107
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao 108
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 108
Maagizo ya kamati ya PAC 108

Hoja nambari 4.1.2.24: Kukosekana kwa sehemu kubwa ya Ripoti za Bajeti katika Mfumo wa BAMAS 108
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao 109
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 110
Maagizo ya Kamati ya PAC 110

Hoja nambari 4.1.2.25: Kutokamilika kwa Moduli ya Mapato katika Mfumo wa BAMAS 110
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao 110
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 111
Maagizo ya kamati ya PAC 111

Hoja nambari 4.1.2.26: Kukosekana kwa ufahamu wa kutosha wa namna Mfumo unavyofanya kazi kwa watumishi wa Idara ya Bajeti na Muhasibu Mkuu wa Serikali 111
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao 111
Uchunguzi na Maagizo wa Kamati ya PAC 112

Hoja nambari 4.1.2.27: Kukosekana kwa Ripoti za Kihasibu (final accounts) katika mfumo wa BAMAS zinazoendana na mahitaji ya sasa ya Serikali.....112
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao..... 112
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 112

OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI, NA UTAWALA BORA (OR-KSUUB).....114

Hoja Nambari 4.1.3.1: Kukosekana kwa nyaraka muhimu za Utengenzwaji wa Mfumo 114
Majibu ya Uongozi wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora 115
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 115
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 116

Hoja Nambari 4.1.3.2: Kuchelewa kukamilika kwa Mradi wa Utengenezwaji wa Mfumo 116
Majibu ya Uongozi wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora 117
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 117
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 117

Hoja Nambari 4.1.3.3: Dosari katika Mfumo wa HR-Payroll Information System 118
Majibu ya Uongozi wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora 120
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 121

Hoja nambari 4.1.3.4: Dosari katika Mfumo wa Legal Aid Database System (LADS) 121
Majibu ya Uongozi wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora 124
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 124

Hoja nambari 4.1.3.5: Dosari katika Mfumo wa e-Library System.....124
Majibu ya Uongozi wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora 126
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 126
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 126

Hoja nambari 4.1.3.6: Kutokuwepo kwa leseni katika kanzidata "database" ya Mfumo wa HR-Payroll Information System 127
Majibu ya Uongozi wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora 127
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 128

Hoja nambari 4.1.3.7: Kutofanyika kwa usanidi katika sehemu zinazoweka kumbukumbu za shughuli za watumiaji wa kanzidata ya Mfumo "database Audit logs" 128
Majibu ya Uongozi wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora 129
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 130

Hoja nambari 4.1.3.8: Kukosekana kwa usalama katika Seva inayoendesha Mfumo wa HR-Payroll Information System (Application Server) 130
Majibu ya Uongozi wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora 131
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 131

Hoja nambari 4.1.3.9: Dosari za kiusalama zilizobainika katika Chumba cha Mitambo (Server Room).....131
Majibu ya Uongozi wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora 133
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 133
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 134

MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI ZANZIBAR (ZAECA).....135

Hoja Nambari 4.1.4.1: Kukosekana kwa Mkataba wa Viwango vya Huduma (SLA Agreement) baina ya ZAECA, ZICTIA na TTCL 135

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar 135
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 136

Hoja Nambari 4.1.4.2: Kutozingatiwa kwa Utaratibu wa Utengenezaji wa Mifumo ya TEHAMA (Software Development Life Cycle 136
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar 137
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 138

Hoja Nambari 4.1.4.3: Mapungufu yaliyobainika katika chumba cha seva (Server room) 138
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar 140
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 140
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 141

Hoja Nambari 4.1.4.4: Udhaifu wa udhibiti wa ufikiaji na mgawanyo wa majukumu ndani ya Mfumo wa usimamizi wa Kesi (Access control).....141
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar 143
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 143
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar 144
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 144

Hoja Nambari 4.1.4.6: Malipo ya ziada yaliyofanyika kwa wazabuni kupitia mfumo wa eProz shilingi 13, 883,600.....144
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar 148
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 149
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 149

Hoja Nambari 4.1.4.7: Kutokushindanishwa kwa watoa huduma mbalimbali kwenye Zabuni ya Ununuzi wa Huduma ya Chakula nambari RFQ_21374 yenye thamani ya shilingi 45,360,000 ...149
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar 150
Uchunguzi wa kamati ya PAC 151

Hoja Nambari 4.1.4.8: Upatikanaji hafifu wa mfumo wa manunuzi wa kielektroniki (eProz) katika mtandao wa ZAECA 151
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar 151
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 152
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 152

Hoja Nambari 4.1.4.9: Kutotumika kwa mfumo wa e-Offi ce katika Afi si za Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi.....152
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar 153
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 153

Hoja Nambari 4.1.4.10: Kukosekana kwa Mfumo wa Kielektroniki wa kufanya Uchunguzi wa Kimahkama (Forensic Audit Software) na kukusanya Ushahidi wa Kidijitali (Digital Evidence) .153
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar 155
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 155

Hoja Nambari 4.1.4.11: Kukosekana kwa “Sophos Firewall” katika Afisi za Mikoa za Mamlaka ya Kuzuia na Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibaar.....155
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar 156
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 156

Hoja Nambari 4.1.4.12: Kutokufanyika kwa Mafunzo ya Kujikinga na Uhalifu wa kimtandao (Cyber Security Awareness Training) kwa watumishi wa ZAECA. 157

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar 157
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 158

Hoja Nambari 4.1.4.13: Kutofungwa kwa Mfumo wa Kamera za Ulinzi katika Afisi za ZAECA ...158
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar 159
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 159

MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR (ZRA) 160

Hoja Nambari 4.1.10.1: Kutoshirikishwa kikamilifu Kitengo cha TEHAMA cha ZRA katika mchakato wa Utengenezwaji wa Mfumo wa ZIDRAS 160
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar..... 161
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 161
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 162

Hoja Nambari 4.1.10.2: Dosari katika utendaji kazi wa Mfumo wa ZIDRAS 162
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar..... 163
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 164

Hoja Nambari 4.1.10.3: Dosari katika Ukusanyaji wa Mapato yatokanayo na Kodiza Bandari na Viwanja vya Ndege.....164
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar..... 165
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 166

Hoja Nambari 4.1.10.4: Dosari katika Muunganiko wa Mfumo wa ZIDRAS na Mfumo wa Ikram Sealine Company 166
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar..... 166
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 167

Hoja Nambari 4.1.10.5: Kuchelewa kuunganishwa kwa Mifumo ya Makusanyo ya Mapato ya Kampuni ya AZAM, ZAN FAST FERRIES na Mfumo wa ZIDRAS 167
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar..... 167
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 168
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 168

Hoja Nambari 4.1.10.6: Kukosekana kwa leseni ya Kanzidata ya Mfumo wa ZIDRAS (Oracle Database) 168
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar..... 170
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 170
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 171

Hoja Nambari 4.1.10.7: Tathmini ya Miundombinu ya Mtandao (Review of Network infrastructure).....171
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar..... 171
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 172

MFUKO WA HIFADHI YA JAMII (ZSSF) 173

Hoja Nambari 4.1.11.1: Dosari katika Maboresho ya Mfumo wa FuMIS kwa mwaka wa fedha 2022/2023.....173
Majibu ya Uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii 173
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 174
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 174

Hoja Nambari 4.1.11.2: Mapitio ya mfumo wa kugundua, kutoa ishara na kuzima moto (Fire Detection and Suppression System) 174
Majibu ya Uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii 175
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 176

Hoja Nambari 4.1.11.3: Dosari katika Mchakato wa Usimamizi wa Matukio (Inadequate Incident Management Process) 176
Majibu ya Uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii 177
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 177
Maagizo ya Kamati ya PAC 177

Hoja Nambari 4.1.11.4: Udhaifu katika utendaji kazi wa Mifumo ya ZSSF kwa upande wa Pemba 178
Majibu ya Uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii 178
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 178

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR (ZURA) 179

Hoja Nambari 4.1.14.1: Kukosekana kwa Mpango wa Matengenezo wa kuzuia uharibifu (Preventive Maintenance Plan) 179
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) 179
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 180
Maagizo ya Kamati ya PAC 180

Hoja Nambari 4.1.14.2: Kukosekana kwa Mpango wa Kusimamia Matukio ya TEHAMA (ICT Incident Management Plan) 180
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) 180
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 181
Maagizo ya Kamati ya PAC 181

Hoja Nambari 4.1.14.3: Utekelezaji wa Mradi wa kutengeneza mfumo wa ZIRS nje ya muda wa mkataba 181
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) 182
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 183
Maagizo ya Kamati ya PAC 183

Hoja Nambari 4.1.14.4: Kutokamilika kwa Utengenezwaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Malalamiko (CMS) 183
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) 184
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 185

Hoja Nambari 4.1.14.5: Kukosekana kwa nyaraka muhimu za Utengenzwaji wa Mifumo ya ndani ya TEHAMA 185
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) 186
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 186
Maagizo ya Kamati ya PAC 186

Hoja Nambari 4.1.14.6: Mapungufu yaliyobainika katika Mradi wa Ufungaji wa chumba cha kuhifadhia Mitambo (Mini Data Center) ZURA 187
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) 188
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 189

Hoja Nambari 4.1.14.7: Dosari katika mfumo wa Ulinzi wa kamera (CCTV camera system) 189
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) 190

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 190

Hoja Nambari 4.1.14.8: Kusitishwa kwa Mfumo wa Kuchunguza (Scanning) Mafuta ya kimagendo na Uchakachuaji (Fuel Marking System) ZURA 190

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) 191
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 191
Maagizo ya Kamati ya PAC 191

Hoja Nambari 4.1.14.9: Kutokufanya kazi kwa Mfumo wa kukagua vihatarishi (Walthrough Scanners) 191

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) 192
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 192
Maagizo ya Kamati ya PAC 192

Hoja Nambari 4.1.14.10: Udhaifu katika udhibiti wa utoaji wa Leseni kupitia Mfumo wa ZIRS 193

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) 194
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 194
Maagizo ya Kamati ya PAC 194

Hoja Nambari 4.1.14.11: Kujirudia kwa Taarifa zinazoingizwa kwenye Mfumo wa ZIRS (Data Redundancy) 194

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) 195
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 195

Hoja Nambari 4.1.14.12: Kuwepo kwa Taarifa zisizo sahihi ndani ya Mfumo (incorrect data) 195

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) 196
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 196
Maagizo ya Kamati ya PAC 197

Hoja Nambari 4.1.14.13: Mapitio ya Mfumo wa Usimamizi wa Malalamiko (Complaint Management System) 197

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) 199
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 199

Hoja Nambari 4.1.14.14: Kutofanya kazi ipasavyo "Logs/ Audit Trails" ndani ya Mfumo wa ZIRS 199

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) 200
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 200

Hoja Nambari 4.1.14.15: Dosari ya kiusalama katika upatikanaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Malalamiko (SSL Certificate issue) 200

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) 202
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 202

Hoja Nambari 4.1.14.16: Kukosekana kwa zana za kisasa za kufuatilia utendaji wa Mtandao (Modern Network Monitoring Tools) 202

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) 203
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 203

MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI ZANZIBAR (ZMA) 204

Hoja Nambari 4.1.26.1: Udhibiti duni katika chumba cha Seva cha Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA).....204
Majibu ya Uongozi wa ZMA..... 204
Uchunguzi wa Kamati ya PAC..... 204
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 205

Hoja Nambari 4.1.26.2: Udhaifu katika mfumo wa kusajili Meli na Mabaharia (Vessels & Seafarers Registration Systems).....205
Majibu ya Uongozi wa ZMA..... 206
Uchunguzi wa Kamati ya PAC..... 207

Hoja Nambari 4.1.26.3: Udhaifu katika mfumo wa Bill Portal kutokuonesha Status za "Control Number" zilizoghairika (Cancelled) na zilizokwisha muda (Expired).....207
Majibu ya Uongozi wa ZMA..... 208
Uchunguzi wa Kamati ya PAC..... 208

Hoja Nambari 4.1.26.4: Udhaifu katika mfumo wa kutoa Leseni wa Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA).....208
Majibu ya Uongozi wa ZMA..... 209
Uchunguzi wa Kamati ya PAC..... 209

Hoja Nambari 4.1.26.5: Kuweza kusajili jina la Kampuni zaidi ya mara moja.....209
Majibu ya Uongozi wa ZMA..... 209
Uchunguzi wa Kamati ya PAC..... 209

Hoja Nambari 4.1.26.6: Kutotumika kwa mifumo ya Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA) kwa upande wa Pemba.....210
Majibu ya Uongozi wa ZMA..... 210
Uchunguzi wa Kamati ya PAC..... 210
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 211

UCHUNGUZI WA KAMATI YA PAC KUHUSU UKAGUZI WA TAARIFA ZA SERIKALI KUU KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023.....212

MFUKO WA FEDHA WA HUDUMA ZA AFYA ZANZIBAR (ZANZIBAR HEALTH BASKET FUND) 212

Hoja nambari 4.5.1.1: Kuchelewa kuingizwa kwa fedha za Mradi.....212
Majibu ya Uongozi..... 212
Uchunguzi wa Kamati ya PAC..... 212
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 213

Hoja nambari 4.5.1.2: Kuchelewa kuingizwa kwa fedha za Walengwa wa Mradi 213
Majibu ya Uongozi..... 214
Uchunguzi wa Kamati ya PAC..... 214
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 214

Hoja nambari 4.5.1.3: Kutoingizwa kwa fedha za Mradi kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar shilingi 800,000,000.....214
Majibu ya Uongozi..... 214
Uchunguzi wa Kamati ya PAC..... 215

Hoja nambari 4.5.1.4: Vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye daftari la ghalani shilingi 37,687,635 215

Majibu ya Uongozi 222
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 222
Maagizo ya Kamati ya PAC 222

PROGRAMU YA CHANJO - EPI (GAVI) 223

Hoja nambari 4.5.2.1: Kutotelekelezwa kwa shughuli zilizopangwa zenye thamani ya shilingi 1,001,913,061.43 223
Majibu ya Uongozi 223
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 224
Maagizo ya Kamati ya PAC 224

Hoja nambari 4.5.2.2: kiasi cha dawa kilichokwisha muda wa matumizi 224
Majibu ya Uongozi 225
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 225
Maagizo ya Kamati ya PAC 225

Hoja nambari 4.5.2.3: Ushuru wa Ongezeko la Thamani kwa miamala ya benkiyenye thamani ya shilingi 1,216,542.41 225
Majibu ya Uongozi 226
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 227
Maagizo ya Kamati ya PAC 227

Hoja nambari 4.5.2.4: Matumizi yaliyofanywa bila ya kuzingatia matumizi ya risiti za kielektroniki (EFD) shilingi 5,184,270 227
Majibu ya Uongozi 228
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 228

Hoja nambari 4.5.2.5: Ununuzi uliofanywa bila ya kutumia mfumo wa E-Proz shilingi 39,340,503.78 228
Majibu ya Uongozi 229
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 229
Maagizo ya Kamati ya PAC 229

Hoja nambari 4.5.2.6: Upotevu wa ziada wa chanjo za Rotavan 230
Majibu ya Uongozi 236
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 236
Maagizo ya Kamati ya PAC 236

OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO 237

Hoja Namba 5.4.1.1 Ununuzi wa mafuta bila ya kuwepo mkataba shilingi 191,446,790. 237
Majibu ya Uongozi wa Fedha na Mipango 237
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 237
Maagizo ya Kamati ya PAC 238

Hoja Namba 5.4.1.2 malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslim shilingi 107,451,300 238
Majibu ya Uongozi wa Fedha na Mipango 238
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 238

Hoja Namba 5.4.1.3: Malipo yaliyofanyika kinyume na miongozo ya ufungaji wa hesabu shilingi 248,361,770 239
Majibu ya Uongozi wa Fedha na Mipango 239
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 239

Hoja Namba 5.4.1.4 Malipo yaliyolipwa kinyume na utaratibu shilingi 35,000,000 239
Majibu ya Uongozi wa Fedha na Mipango 240
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 240

KAMISHENI YA UTALII ZANZIBAR.....241

Hoja nambari 5.8.2.1: Tofauti iliyojitokeza baina ya Hesabu ya Mwisho wa mwaka na Mikataba halisi iliyofungwa shilingi 87,126,930 241
Majibu ya Uongozi wa Kamisheni..... 242
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 242
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 243

Hoja nambari 5.8.2.2: Tofauti iliyobainishwa kati ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka na Taarifa za Mapato shiling 724,427,202.....243
Majibu ya Uongozi wa Kamisheni..... 244
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 244
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 245

Hoja nambari 5.8.2.3: Kutokuingizwa kwa makusanyo yatokanayo na Tamasha la ZTITE katika Taarifa za Hesabu za Mwisho wa Mwaka U$D 3,465.....245
Majibu ya Uongozi wa Kamisheni..... 245
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 245

Hoja nambari 5.8.2.4: Kutoonekana kwa maeneo halisi ya miradi 10 ambayo imepata lesseni kutoka Kamisheni ya Utalii 246
Majibu ya Uongozi wa Kamisheni..... 246
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 247
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 247

Hoja nambari 5.8.2.5: Dosari katika uazishwaji wa kikosi cha Polisi Utalii pamoja na matumizi yaliyofanyika shilling 181,691,420.....247
Majibu ya Uongozi wa Kamisheni..... 248
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 248
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 248

Hoja nambari 5.8.2.6: Mapungufu katika Mpango wa Manunuzi wa Mwaka (Annual Procurement Plan) 248
Majibu ya Uongozi wa Kamisheni..... 249
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 249
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 249

Hoja nambari 5.8.2.7: Malipo kwa watoa huduma ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 136,536,485. 62.....249
Majibu ya Uongozi wa Kamisheni..... 250
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 251
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 251

Hoja nambari 5.8.2.8: Matumizi yaliyokiuka Taratibu za Manunuzi Shilingi 136,536,485. 62 251
Majibu ya Uongozi wa Kamisheni..... 252
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 253
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 253

Hoja nambari 5.8.2.9: Kukosekana kwa nyaraka za makubaliano ya kuwasafirisha wageni kutoka Arusha shilingi 6,814,800.....253

Majibu ya Uongozi wa Kamisheni 253
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 254
Maagizo ya Kamati ya PAC 254

Hoja nambari 5.8.2.10: Fedha zilizotumika bila ya kuidhinishwa katika Mpango kazi wa Mwaka shilingi 247,706,500 254
Majibu ya Uongozi wa Kamisheni 255
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 255
Maagizo ya Kamati ya PAC 255

Hoja nambari 5.8.2.11: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu shilingi 27,570,000 255
Majibu ya Uongozi wa Kamisheni 256
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 256
Maagizo ya Kamati ya PAC 257

Hoja nambari 5.8.2.12: Kutelekezwa kwa majengo ya Mradi wa Bi Khole yaliyogharimu shilingi 1,791,715,81 5.36 257
Majibu ya Uongozi wa Kamisheni 258
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 258
Maagizo ya Kamati ya PAC 258

Hoja nambari 5.8.2.13: Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia Mfumo wa kielektroniki (e-Proz) shilingi 38,835,048 259
Majibu ya Uongozi wa Kamisheni 259
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 259
Maagizo ya Kamati ya PAC 260

KAMISHENI YA UTALII - PEMBA 260

Hoja nambari 5.8.2.14: Mtumishi anaekaimu nafasi kinyume na utaratibu 260
Majibu ya Uongozi wa Kamisheni 261
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 261
Maagizo ya Kamati ya PAC 261

UCHUNGUZI WA KAMATI YA PAC KUHUSU UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023 262

MRADI WA MAENDELEO WA ZESTA 262

Hoja nambari 4.1.1.1: fedha za mradi ambazo hazikutolewa USD 2,401,605.98 262
Majibu ya Uongozi wa Shirika 262
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 263
Maagizo ya Kamati ya PAC 263

Hoja nambari 4.1.1.2: kuchelewa kuwasilishwa kwa Rasimu ya Mkataba kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali 263
Majibu ya Uongozi wa Shirika 264
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 264
Maagizo ya Kamati ya PAC 265

MRADI WA MAENDELEO WA ZESS 266

Hoja nambari 4.1.2.1: upungufu wa fedha za kugharamia shughuli za mradi 266
Majibu ya Uongozi wa Shirika 267
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 267

Maagizo ya Kamati ya PAC..... 268

Hoja nambari 4.1.2.2: ukaguzi katika maeneo ya utekelezaji wa mradi 268

Majibu ya Uongozi wa Shirika..... 268

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 268

MRADI WA UIMARISHAJI WA ELIMU YA SEKONDARI ZANZIBAR (ZISP).....269

Hoja nambari 4.3.1.1: Fedha za mradi zilizokopwa ambazo hazijarejeshwa U$D 130,464.....269

Majibu ya Uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali..... 269

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 270

Maagizo ya Kamati ya PAC..... 270

Hoja nambari 4.3.1.2: Fedha ya mradi ambazo hazikutumika U$D 140,399.97.....270

Majibu ya Uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali..... 270

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 271

Maagizo ya Kamati ya PAC..... 271

Hoja nambari 4.3.1.3: Dosari iliyojitokeza katika kituo cha Limbani - Pemba 271

Majibu ya Uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali..... 271

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 272

Maagizo ya Kamati ya PAC..... 272

MRADI WA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA WA ELIMU AWAMU YA PILI (GPE II).....273

Hoja nambari 4.3.2.1: Kasoro zilizobainika katika utekelezaji wa Mradi 273

Majibu ya Uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali..... 273

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 273

Maagizo ya Kamati ya PAC..... 274

MRADI WA ELIMU YA JUU KWA MABADILIKO YA KIUCHUMI (HEET) 275

Hoja nambari 4.3.3.1: Fedha za mradi ambazo hazikutumika shilingi 3,140,485,688 275

Majibu ya Uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali..... 275

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 277

Maagizo ya Kamati ya PAC..... 277

MRADI WA UJENZI WA KITUO CHA MABASI KINOWE (HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI).....278

Hoja nambari 5.1.4.1: Kukosekana kwa Ripoti ya Utekelezaji Mradi.....278

Majibu ya uongozi wa Halmashauri..... 278

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 278

Maagizo ya Kamati ya PAC..... 279

Hoja nambari 5.1.4.2: Kukosekana kwa Ripoti ya Mkaguzi wa Ndani.....279

Majibu ya uongozi wa Halmashauri..... 279

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 279

Maagizo ya Kamati ya PAC..... 280

Hoja nambari 5.1.4.3: Kutokuwasilishwa kwa hati ya dhamana ya utendaji kazi (Performance security) shilingi 104,622,450.....280

Majibu ya uongzi wa Halmashauri..... 281

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 281

Maagizo ya Kamati ya PAC..... 281

Hoja nambari 5.1.4.4: Kutokufanyika kwa upembuzi yakinifu kabla ya utekelezaji mradi.....281
Majibu ya uongozi wa Halmashauri..... 282
Uchungiwa Kamati ya PAC..... 282
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 283

Hoja nambari 5.1.4.5: Malipo ya awali yaliyolipwa kinyume na utaratibu 283
Majibu ya uongozi wa Halmashauri..... 283
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 284
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 284

Hoja nambari 5.1.4.6: Kutokukatwa malipo ya kitangulizi katika vyeti vya malipo (interim payment certificate) shilingi 128,050,000 284
Majibu ya uongozi wa Halmashauri..... 285
Uchungi wa Kamati ya PAC..... 285
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 285

Hoja nambari 5.1.4.7: Mapungufu katika Mkataba wa Ujenzi wa Kituo cha Mabasi Kinoe 286
Majibu ya uongozi wa Halmashauri..... 286
Uchungi wa Kamati ya PAC..... 287
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 287

Hoja nambari 5.1.4.8: Mradi kutekelezwa bila ya uwepo wa hati ya dhamana ya benki.....287
Majibu ya uongzi wa Halmashauri..... 288
Uchunguzi na Maagizo ya Kamati..... 288

UCHUNGUZI WA KAMATI YA PAC KUHUSU UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA NA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023 289

SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR.....289

Hoja nambari 4.1.1.1: ukosefu wa mita inayotumika kupima umememem unaoingia na kutoka katika vituo vidogo vya usambazaji umeme na transfoma 289
Majibu ya Uongozi..... 289
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 290
Magizo ya Kamati ya PAC 290

Hoja nambari 4.1.1.2: ucheleweshaji mkubwa wa kushughulikia malalamiko ya wateja 291
Majibu ya Shirika la Umeme..... 291
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 291

Hoja nambari 4.1.1.3: kutokukusanywa kwa mwaka mzima madeni ya wateja wanaolipa baada ya kutumia umeme shilingi bilioni 7,596,399,436.42.....292
Majibu ya Shirika la Umeme..... 294
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 294
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 295

Hoja nambari 4.1.1.4: kuchelewa kwa kiasi kikubwa kwa huduma ya unganishaji umeme kwa wateja.....295
Majibu ya Shirika la Umeme..... 296
Uchunguza wa Kamati ya PAC 296

Hoja nambari 4.1.1.5: Ucheleweshaji mkubwa wa kutafuta ufumbuzi wa miamala isiyo ya kawaida iliyomo katika taarifa ya usuluhishi wa kibenki 296

Majibu ya Shirika la Umeme 297
Uchunguza wa Kamati ya PAC 297

Hoja nambari 4.1.1.6 mchakato wa ununuzi usio wa ushindani wenye thamani ya shilingi 3.24 bilioni na USD milioni 138.07. 297
Majibu ya Shirika la Umeme 298
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 302
Maagizo ya Kamati ya PAC 302

Hoja nambari 4.1.1.7: Kutumia njia ya ununuzi isiyosahihi shilingi bilioni 11.63 302
Majibu ya Shirika la Umeme 303
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 304
Maagizo ya Kamati ya PAC 304

SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR (ZPC) 305

Hoja nambari 4.1.2.1: Kukosekana kwa Mshauri Elekezi katika miradi ya ujenzi ya Shirika la Bandari yenye thamani ya shilingi 12,500,530,762 305
Majibu ya Uongozi wa Shirika 305
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 306
Maagizo ya Kamati ya PAC 307

Hoja nambari 4.1.2.2: Kuchelewa kuanza kwa mradi wa ujenzi wa bandari ya Shumba 307
Majibu ya Uongozi wa Shirika 307
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 308
Maagizo ya Kamati ya PAC 308

Hoja nambari 4.1.2.3: Kumaliza muda wa dhamana ya Utendaji kazi (Performance security) ... 308
Majibu ya Uongozi wa Shirika 309
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 310
Maagizo ya Kamati ya PAC 310

Hoja nambari 4.1.2.4: Kutokujumuishwa kwa maoni ya Mwanasheria Mkuu katika mkataba wa ujenzi wa Bandari ya Shumba 310
Majibu ya Uongozi wa Shirika 311
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 311
Maagizo ya Kamati ya PAC 312

Hoja nambari 4.1.2.5: Kutokuwepo kwa usimamizi mzuri wa madeni ya wadaiwa wa Shirika shilingi 1,692,860,807.5 312
Majibu ya Uongozi wa Shirika 315
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 316
Maagizo ya Kamati ya PAC 316

Hoja nambari 4.1.2.6: Kukosekana kwa kumbukumbu za vikao vya kamati ya misamaha na madai 316
Majibu ya Uongozi wa Shirika 317
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 318

Hoja nambari 4.1.2.7: Kushindwa kukusanya tozo ya mizigo na ada ya kukodisha ghala shilingi 546,795,243.75 319
Majibu ya Uongozi wa Shirika 320
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 321
Maagizo ya Kamati ya PAC 321

SHIRIKA LA BANDARI PEMBA 322

Hoja nambari 4.1.2.8: Malimbikizo ya Madeni ya Mapato shilingi 226,165,354.96.....322

Majibu ya Uongozi wa Shirika..... 322

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 323

SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA ZANZIBAR 324

Hoja nambari 4.1.5.1: Mkataba unaotekelezwa bila ya kuwasilishwa dhamana ya utendaji kazi (perfomance Security) 324

Majibu ya Uongozi wa Shirika..... 325

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 325

Maagizo ya Kamati ya PAC..... 325

Hoja nambari 4.1.5.2: Wasiwasi juu ya ulipwaji wa deni kutoka Kampuni ya GBP Tanzania shilingi 1,406,195,716.28.....326

Majibu ya Uongozi wa Shirika..... 326

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 327

Maagizo ya Kamati ya PAC..... 328

Hoja nambari 4.1.5.3: Kutokuwepo kwa Mkataba baina ya Shirika la Meli Zanzibar na Kampuni ya ZALAGACO.....328

Majibu ya Uongozi wa Shirika..... 328

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 329

Maagizo ya Kamati ya PAC..... 329

Hoja nambari 4.1.5.4: Malipo yaliyofanywa bila ya upatikanaji wa huduma zilizokusudiwa Shilingi TZS 32,260,00 329

Majibu ya Uongozi wa Shirika..... 330

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC..... 330

Hoja nambari 4.1.5.5: Malipo yaliyofanyika kinyume na bajeti iliyoidhinishwa shilingi 174,865,205 330

Majibu ya Uongozi wa Shirika..... 331

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 331

Maagizo ya Kamati ya PAC..... 331

SHIRIKA LA NYUMBA (ZHC) 332

Hoja nambari 4.1.7.1: Kutokuchukuliwa hatua za kisheria kwa Wapangaji wenye malimbikizo ya madeni ya muda mrefu shilingi 833,023,000 332

Majibu ya Uongozi wa Shirika..... 335

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 335

Maagizo ya Kamati ya PAC..... 335

Hoja nambari 4.1.7.2: Uwepo kwa idadi kubwa ya wapangaji ambao hawana mikataba halali 335

Majibu ya uongozi wa Shirika 336

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 336

Maagizo ya Kamati ya PAC..... 336

Hoja nambari 4.1.7.3: Kukosekana kwa sera za bima (insurance policies) kwa nyumba za biashara zenye mikataba ya upangaji wa muda mrefu (long lease contracts) 337

Majibu ya Uongozi wa Shirika..... 337

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 337

Hoja nambari 4.1.7.4: Kutotenganishwa kwa thamani ya Ardhi na Majengo katika kutafuta gharama za uchakavu 338
Majibu ya Uongozi wa Shirika 338
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 338
Maagizo ya Kamati ya PAC 339

Hoja nambari 4.1.7.5: Kushindwa kuondoa thamani ya majengo mawili yaliyobomolewa katika taarifa za mwaka wa fedha 2022/2023 339
Majibu ya Uongozi Wa Shirika 340
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 340
Maagizo ya Kamati ya PAC 340

SHIRIKA LA NYUMBA PEMBA 340

Hoja Nambari 4.1.7.6: Malipo yaliyofanywa nje ya mfumo wa manunuzi shilingi 17,310,740 ... 340
Majibu ya Uongozi wa Shirika 341
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 342

Hoja Namabari 4.1.7.7: Kutokununua vifaa vya kuandikia kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji shilingi 3,419,504.70 342
Majibu ya Uongozi wa Shirika 343
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 343
Maagizo ya Kamati ya PAC 343

Hoja nambari 4.1.7.8: Hali ya Uchakavu wa majengo ya Shirika 344
Majibu ya Uongozi wa Shirika 344
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 344

Hoja nambari 4.1.7.9: Kukosekana kwa hatimiliki kwa baadhi ya mali za Shirika 345
Majibu ya Uongozi wa Shirika 345
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 345

Hoja nambari 4.1.7.10: Deni la Mapato la ukarabati wa nyumba zilizotolewa fidia shilingi 57,900,000 346
Majibu ya Uongozi wa Shirika 347
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 347
Maagizo ya Kamati ya PAC 347

MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR (ZAA) 349

Hoja nambari 5.1.3.1: Kutowasilishwa katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa Tozo ya Usalama (Safety Fee) inayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kwa niaba ya Mamlaka, shilingi 684,050,000 349
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka 349
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 350
Maagizo ya Kamati ya PAC 350

Hoja nambari 5.1.3.2: Kutowasilishwa katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa Tozo ya Huduma kwa abiria (Passenger Service Charge) inayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kwa niaba ya Mamlaka 351
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka 351
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 351
Maagizo ya Kamati ya PAC 352

Hoja nambari 5.1.3.3: Malipo ya kukodi mabasi manne kwa ajili ya wafanyakazi bila ya kuzingatia thamani ya fedha (Value for money), shilingi 237,600,000 352
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka 353
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 353
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 353

Hoja nambari 5.1.3.4: Kutokuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Viwanja vya Ndege 353
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka 354
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 354
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 354

Hoja nambari 5.1.3.5: Kutokuwepo kwa Sera na Miongozo ya Uendeshaji na Usimamizi wa Mamlaka..... 355
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka 355
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 355
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 356

Hoja nambari 5.1.3.6: Kutokuwepo kwa usimamizi mzuri wa madeni ya Mamlaka 356
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka 357
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 357

MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE PEMBA 357

Hoja nambari 5.1.3.7: Kutokukamilika kwa Ufungaji wa Taa za kuongozea Ndege (Approach light) 357
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka 358
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 358

MAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI ZANZIBAR (ZIPA) 359

Taarifa fupi kuhusu utekelezaji wa Kazi za Kamati kwa Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA)..... 359

MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA ZANZIBAR UNGUJA . 360

Hoja nambari 5.1.9.1: Mapato yaliyokusanywa nje ya mfumo shilingi 70,989,688 360
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka 361
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 361
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 361

Hoja nambari 5.1.9.2: Kushindwa kuthibitisha uwepo wa mali za ghalani za jumla ya shilingi 52,059,922.59 zilizoainishwa katika Taarifa za Fedha za Mwisho wa Mwaka 362
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka 363
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 363

Hoja nambari 5.1.9.3: Kukosekana kwa Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi (Risk Management Framework) 363
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka 364
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 364
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 364

Hoja nambari 5.1.9.4: Kuchelewa kukamilika kwa mradi wa ujenzi 364
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka 365
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 365

Hoja nambari 5.1.9.5: Dosari katika mradi wa Ujenzi Kidimni 366
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka 366
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 366

Hoja nambari 5.1.9.6: Uhifadhi usioridhisha wa vielelezo vya dawa za kulevya zilizokamatwa.366
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka 367
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 367

Hoja nambari 5.1.9.7: Malimbikizo ya Madeni ya muda mrefu shilingi 55,421,635 368
Majibu ya Uongozi wa Mamlaka 368
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 368
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 369

Hoja Nambari 5.1.9.8: Dosari zilizobainika katika utekelezaji wa Sheria 369
Majibu ya Uongozi wa Tume 371
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 372

MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA ZANZIBAR - PEMBA.372

Hoja nambari 5.1.9.9: Kukosekana kwa usafiri wa uhakika wa ufuatiliaji wa kazi za mamlaka za utoaji taaluma kwa wananchi 372
Majibu ya Uongozi wa Tume 372
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 372
Magizo ya Kamati ya PAC 373

Hoja nambari 5.1.9.10: Kukosekana kwa usiri katika utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ...373
Majibu ya Uongozi wa Tume 373
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 374
Magizo ya Kamati ya PAC 374

Hoja nambari 5.1.9.11: Kukoseka kwa vifaa vya kisasa vya ukaguzi wa Dawa za Kulevya. 374
Majibu ya Uongozi wa Tume 374
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 375
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 375

MAMLAKA YA MAWASILIANO ZANZIBAR (ZICTIA) 376

Hoja nambari 6.1.2.1: Dosari katika uandaaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka 376
Majibu ya Uongozi ZICTIA. 376
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 376
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 377

Hoja nambari 6.1.2.2: Tofauti iliyojitokeza katika taarifa za fedha shilingi 2,672,032,699.....377
Majibu ya uongozi wa ZICTIA..... 387
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 388
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 388

Hoja nambari 6.1.2.3: Uwepo wa deni la shilingi 2,605,582,800 ambalo halijalipwa 388
Majibu ya Uongozi wa ZICTIA 393
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 394
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 394

Hoja nambari 6.1.2.4: Kushindwa kukusanya jumla ya shilingi 44,007,687 kutokana na usimamizi usioridhisha wa Mkataba baina ya Wakala na TTCL 394
Majibu ya Uongozi wa ZICTIA 396

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 396
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 396

Hoja nambari 6.1.2.5: Kutokulipwa kwa kiasi cha shilingi 859,233,085 kutoka kwa Mteja TTCL 397
Maijbu ya Uongozi wa ZICTIA 398
Uchunguzi na Maagizo ya Kamati ya PAC..... 398

Hoja nambari 6.1.2.6: Malipo yenye vielelezo pungufu shilingi 89,032,790.....398
Majibu ya Uongozi wa ZICTIA 407
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 407
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 408
Hoja nambari 6.1.2.7: Malipo yaliofanywa kwa njia ya Fedha Taslim (Cash Payment) shilingi 39,925,000 408
Majibu ya Uongozi wa ZICTIA 409
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 410
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 410

Hoja nambari 6.1.2.8: Ongezeko la matumizi kwa baadhi ya vifungu vya bajeti shilingi 932,427,527 410
Majibu ya Uongozi wa ZICTIA 412
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 412
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 412

WAKALA WA KARAKANA KUU YA MAGARI YA ZANZIBAR 413

Hoja nambari 6.1.8.1: Dosari katika utayarishaji wa Hesabu za Mwisho wa mwaka.....413
Majibu ya Uongozi wa Karakana 413
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 414

Hoja nambari 6.1.8.2: Kukosekana kwa makadirio ya mapato ya shilingi 55,340,658 415
Majibu ya Uongozi wa Karakana 415
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 415
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 416

Hoja nambari 6.1.8.3: Dosari katika uwasilishaji wa taarifa za fedha shilingi 12,066,650.....416
Majibu ya Uongozi wa Karakana 416
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 416
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 417

WAKALA WA KARAKANA YA MAGARI YA SERIKALI- PEMBA.....417

Hoja nambari 6.1.8.4: Ukosefu wa mafundi wenye taaluma ya kutosha. 417
Majibu ya Uongozi wa Karakana 417
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 417

Hoja nambari 6.1.8.5: Uwepo wa upungufu wa watumishi 418
Majibu ya Uongozi wa Karakana 419
Uchunguzi na Maagizo ya Kamati. 419

Hoja nambari 6.1.8.6: Kutokuuzwa au kufanyiwa matengenezo kwa gari chakavu 419
Majibu ya Uongozi wa Karakana 420
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 420

Hoja nambari 6.1.8.7: Kukosekana kwa kitengo cha unyoshaji, upigaji rangi na usafishaji wa magari 420

Majibu ya Uongozi wa Karakana. 420
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 421

Hoja nambari 6.1.8.8: Kutokutayarishwa kwa Mpango wa Matengenezo ya Mali.....421
Majibu ya Uongozi wa Karakana 421
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 421

Hoja nambari 6.1.8.9: Uwepo wa muitiko mdogo wa Taasisi za Umma wa kufanya Matengenezo ya magari ya karakana Kuu. 421
Majibu ya Uongozi wa Karakana. 422
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 422

WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA MALI (BPRA) 423

Hoja Nambari 6.1.9.1: Dosari katika Uandaaji wa Taarifa za Hesabu za Mwisho wa Mwaka shilling 15,495,019.86 423
Majibu ya Uongozi 423
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 424
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 424

Hoja Nambari 6.1.9.2: mapato yaliyokusanywa nje ya mfumo wa ZanMalipo Shillingi 726.954,846 424
Majibu ya Uongozi 425
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 426
Maagizo ya Kamati ya PAC..... 426

Hoja Nambari 6.1.9.3: Kukosekana kwa Taarifa ya Mapato shilingi 2,693, 743 638 katika mfumu wa ZanMalipo 426
Majibu ya Uongozi 427
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 427

Hoja Nambari 6.1.9.4: Usimamizi usioridhisha wa Fedha za TIRKA 427
Majibu ya Uongozi 429
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 429

WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA MALI (BPRA) - PEMBA 430

Hoja nambari 6.1.9.5: Dosari Uwepo wa upungufu wa watumishi.....430
Majibu ya Uongozi wa Wakala 430
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 431
Magizo ya Kamati ya PAC 432

Hoja Nambari 6.1.9.6: Kukosekana kwa gari kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za wakala.....432
Majibu ya Uongozi wa Wakala 432
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 433

BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ).....434

Hoja nambari 7.1.1.1: Kutokuripotiwa kwa orodha kamili ya mikopo iliyofanyiwa maboresho 434
Majibu ya Uongozi wa PBZ 434
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 434

Hoja nambari 7.1.1.2: Dosari zilizobainika katika majalada ya mikopo (PBZ Convetional) 435
Majibu ya Uongozi wa PBZ 435
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 436

Hoja nambari 7.1.1.3: Dosari zilizobainishwa katika Shariah (PBZ Islamic) 437
Majibu ya Uongozi wa PBZ 437
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 438
Hoja nambari 7.1.1.4: Kutokuzingatiwa kwa matakwa ya kisheria katika utoaji wa mikopo 438
Majibu ya Uongozi wa PBZ 439
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 439
Hoja nambari 7.1.1.5: Kutokufanyika kwa marekebisho ya thamani ya mikopo iliyorekebishwa 439
Majibu ya Uongozi wa PBZ 440
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 440
Hoja nambari 7.1.1.6: Uwepo wa Akaunti za dharura katika matawi ya benki 441
Majibu ya Uongozi wa PBZ 442
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 442
Hoja nambari 7.1.1.7: Kutokutambulika kwa ada ya upangaji wa mikopo na mapato 442
Majibu ya Uongozi wa PBZ 443
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 443
Hoja nambari 7.1.1.8: Kutokuzingatiwa kwa utaratibu wa kushughulikia Malalamiko ya Wateja 443
Majibu ya Uongozi wa PBZ 444
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 444
Hoja nambari 7.1.1.9: Malipo ya posho la usumbufu yaliyolipwa bila ya kuzingatia taratibu za kiutumishia shilingi 30,000,000 445
Majibu ya Uongozi wa PBZ 445
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 446
Maagizo ya Kamati ya PAC 446
Hoja nambari 7.1.1.10: Kutokufuatwa kwa taratibu za utoaji wa mikopo kwa watumishi waliopo katika muda wa majaribio (probation Period) shilingi 1,036,785,631 446
Majibu ya Uongozi wa PBZ 447
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 447
Maagizo ya Kamati ya PAC 448
Hoja nambari 7.1.1.11: Mikopo iliyotolewa bila ya kuzingatia kizingiti cha ukomo wa Utumishi shilingi 1,036,785,631 448
Majibu ya Uongozi wa PBZ 449
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 450
Maagizo ya Kamati ya PAC 450
Hoja nambari 7.1.1.12: Mikopo iliyoidhinishwa kinyume na sera ya mikopo ya Benki shilingi milioni 458,086,631 450
Majibu ya Uongozi wa PBZ 451
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 451
Taarifa za ukaguzi wa Benki ya Mucoba kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba, 2022 452
Majibu ya Uongozi wa PBZ 453
Uchunguzi wa Kamati ya PAC 454
Maagizo ya Kamati ya PAC 454

CHUO KIKUU CHA TAIFA ZANZIBAR (SUZA) *455*

Hoja nambari 7.1.9.1: Manunuzi wa vifaa vya kuandikia kinyume na sheria ya wakala wa Serekali wa Uchapaji Zanzibar shilingi 34,579,297 ..... **455**

Majibu ya Uongozi wa SUZA 455

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 456

Hoja nambari 7.1.9.2: Matumizi madogo ya Fedha za Skuli ya Biashara **456**

Majibu ya Uongozi wa SUZA 457

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 457

Hoja nambari 7.1.9.3: Malipo ya fedha taslim kwa wafanyakazi wa kigeni 163,944,000 ..... **458**

Majibu ya Uongozi wa SUZA 459

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 459

Maagizo ya Kamati ya PAC 460

Hoja Nambari: 7.1.9.4 Changamoto zinazolikabili eneo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lilioko Wilaya ya Bagamoyo **460**

Majibu ya Uongozi wa SUZA 460

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 461

Hoja nambari 7.1.9.5: Kutokutumika kwa mashine na vifaa vya jikoni kwa muda mrefu **461**

Majibu ya Uongozi wa SUZA 462

Uchunguzi wa Kamati ya PAC 463

Maagizo ya Kamati ya PAC 463

HITIMISHO *464*

UTANGULIZI

Kijumla, Kamati ya Hesabu za Serikali hutekeleza majukumu yake chini ya Kanuni ya 119(1) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2024) pamoja na Jaduwali lake la Kwanza lililoainishwa katika Kanuni hiyo. Aidha kwa mujibu wa Kanuni ya 124, Kamati ya Hesabu za Serikali hutakiwa kuwasilisha mbele ya Baraza ripoti ya utekelezaji wa shughuli zake katika mkutano wa mwezi wa Febuari au wakati mwengine ambapo Kamati ya Uongozi na Shughuli za Baraza itaamua

Kwa mnasaba huo, Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati ya PAC imefanikiwa kufanya uchunguzi wa Vitabu Vitatu kati ya Sita vya Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufuatia uwasilishwaji wake uliofanywa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Haroun Ali Suleiman mbele ya Baraza la Kumi Mkutano wa Kumi na Tano wa Baraza katika kikao cha tarehe 27 Juni, 2024.

Katika uchunguzi wa Vitabu vilivyowasilishwa, jumla ya Ripoti Tano zilifuatiliwa na kuchunguzwa.

Mheshimiwa Spika, Ripoti ambazo Kamati ya PAC imezifanyia kazi ni hizi zifuatazo:

1. Ripoti ya Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023;
2. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika na Taasisi Zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023;
3. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa Mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023;
4. wa Taarifa za Fedha za Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha Mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023; na
5. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa kwa kipindi cha Mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2023.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya PAC kwa kipindi hicho haikuweza kukamilisha kuzifanyia kazi Ripoti Tatu zilizobakia ambazo zilizowasilishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Ripoti zenyewe ni:

1. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Kiufundi wa Ukarabati wa Uwanja wa Michezo wa Gombani Chake Chake Pemba kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023;
2. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Hospitali Kumi za Wilaya na Moja ya Mkoa kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023; na
3. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Kiufundi wa Mradi wa Usambazaji wa Miundombinu ya Maji Safi na Salama Unguja na Pemba kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023.

Kamati ya PAC tayari imeanza kuzifanyia kazi Ripoti hizo lakini bado haijakamilisha kazi yake ya uchunguzi kwa kutokana na ukweli kwamba Ripoti hizo zinahitaji kufuatiliwa na kuchunguzwa kwa undani zaidi hasa ukizingatia zinagusa maslahi ya moja kwa moja ya umma. Kamati yetu itakamilisha kuzifanyia kazi Ripoti hizo haraka iwezekanavyo na kuwasilisha Ripoti yake kama itakavyoelekezwa na Kamati ya Uongozi na Shughuli za Baraza.

WAJUMBE NA SEKRETARIETI YA KAMATI YA PAC

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati hii imeundwa na Wajumbe Wanane (8) na Sekretarieti ya Watendaji Kumi na Sita (16).

Waheshimiwa Wajumbe:

Mhe. Juma Ali Khatib	-	Mwenyekiti;
Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	M/Mwenyekiti;
Mhe. Bakar Hamad Bakar	-	Mjumbe;
Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Mjumbe;
Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Mjumbe;
Mhe. Kombo Mwinyi Shehe	-	Mjumbe;
Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Mjumbe;
Mhe. Abdulla Hussein Kombo	-	Mjumbe;

Sekretarieti ya Kamati hii ilikuwa na Maofisa Wanne (4) ambao ni Makatibu wa Kamati na Maofisa kadhaa wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama wafuatao:

Sekretarieti:

Ndg. Fatma Omar Ali	-	Katibu.
Ndg. Maryam Haji Ali	-	Katibu.
Ndg. Said Khamis Ramadhan	-	Katibu.
Ndg. Adam Maulid Simai	-	Katibu.
Ndg. Akida Hamad Akida	-	Mkaguzi – Mkurugenzi Ofisi ya Mdhibiti (Taasisi Zinazojitegemea)
Ndg. Juma Mohammed Juma	-	Mkaguzi – Mkurugenzi Ofisi ya Mdhibiti (Mifumo)
Ndg. Ramadhan Iddi Hassan	-	Mkaguzi – Mkurugenzi Ofisi ya Mdhibiti (Madeni)
Ndg. Nassor Mdachi Mwinyi	-	Mkaguzi - Ofisi ya Mdhibiti (Unguja)
Ndg. Maryam Ali Khamis	-	Mkaguzi - Afisi ya Mdhibiti (Mifumo)
Ndg. Shehe Abdalla Ali		Mkaguzi - Afisi ya Mdhibiti (Taasisi Zinazojitegemea)
Ndg. Said Othman Suleiman		Mkaguzi - Afisi ya Mdhibiti (Mifumo)
Ndg. Maryam Othman Juma		Mkaguzi - Afisi ya Mdhibiti (Mifumo)
Ndg. David George Kazi		Mkaguzi - Afisi ya Mdhibiti (Taasisi Zinazojitegemea)
Ndg. Abdulhamid A. Haji		Mkaguzi - Afisi ya Mdhibiti (Taasisi Zinazojitegemea)

Ndg. Issa Faki Ali		Mkaguzi - Afisi ya Mdhibiti (Pemba)
Ndg. Moh'd Suleiman Amour	-	Mkaguzi - Ofisi ya Mdhibiti (Pemba)

UTARATIBU WA KAZI ZA KAMATI

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ya PAC imezingatia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambazo hutumika kuwa ni Hadudi Rejea, matakwa ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Sheria ya Kinga, Uwezo na Fursa za Wajumbe pamoja na Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2024).

Sambamba na hilo, Kamati ilikutana na Watendaji wa Wizara na Taasisi za Serikali zilizohusika na hoja zilizoibuliwa katika Ripoti ya Mdhibiti kwa kufanya mahojiano, kupitia vielelezo na hatimae kufanya ziara katika maeneo mbali mbali kushuhudia uhalisia wa majibu yaliyotolewa na Wizara au Taasisi husika. Aidha, Kamati kwa kuzingatia haja iliyokuwepo, ilifanya ziara katika maeneo husika na baadae ilifanya mijadala ya hoja mbali mbali.

Shughuli hizi zilifanyika ndani ya mizunguko mitano kama ifuatavyo:

1. Mzunguko wa Kwanza: Ulianzia tarehe 05/08/2024 hadi 09/08/2024 - Pemba na kumalizia tarehe 12/08/2024 hadi 23/8/2024 - Unguja
2. Mzunguko wa Pili: Ulianzia tarehe 28/10 hadi Tarehe 01 Novemba, 2024 - Pemba na kumalizia tarehe 04/11/2024 hadi 22/11/2024; na
3. Mzunguko wa Tatu: Ulianzia tarehe 10/12/2024 hadi tarehe 20/12/2024 Unguja na kumalizia tarehe 23/12/2024 hadi tarehe 23/01/2025 – Pemba.

MGONGANO WA MASLAHI

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ya PAC ilifuata matakwa ya Kanuni na] Sheria za nchi zilizoelekeza uwekaji wazi Mgongano wa Maslahi kwa Wajumbe dhidi ya jambo linalojadiliwa ili kuepusha kujitokeza kwa upendeleo hususan wakati wa kufanya maamuzi na kusababisha uonevu au ubatilishaji wa haki. Kwa bahati nzuri, Katika majadiliano ambayo Kamati imeyafanya, hakujajitokeza aina yoyote ya mgongano wa maslahi kwa Wajumbe dhidi ya maamuzi waliyoyatoa.

UCHUNGUZI WA KAMATI YA PAC KUHUSU UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA TAWALA ZA MIKOA, MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023

BARAZA LA MANISPAA MJINI

Hoja nambari 6.3.2.1: Kutokuwepo Taarifa za Kuhesabu Mali (Stock Taking)

Kifungu cha 71(1) cha Sheria namba 6 ya Uanzishwaji wa Ofisi ya Msajili wa hazina na Usimamizi wa mali za kudumu ya 2021 kinaelezea Taasisi kufanya zoezi la utambuzi wa vifaa vya taasisi kwa lengo la kujua idadi na thamani halisi ya vifaa hivyo, aidha Ukaguzi umebaini baraza la manispaa kwa mwaka unaoishia Juni, 2023 hawakufanya zoezi hili licha ya kuwa baraza lina bakaa ya vifaa mbali mbali ambavyo havikutumika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria namba 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina pamoja na kanuni na miongozo inayotolewa na Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa Mjini kukuhakikisha miongozo inafuatwa ili kuendelena na hisabu ya mwisho ya mwaka ambao umetolewa na muhasibu mkuu.

Majibu ya Uongozi wa Baraza

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 zoezi la kuhesabu mali halikufanyika kutokana na ukosefu wa taaluma kwa watendaji. Baada ya kubaini kasoro hiyo Baraza limechukua juhudi ya kutoa elimu kwa watendaji kupitia kitengo cha Mkaguzi wa ndani.

Hali halisi kwa sasa

Kwa mwaka wa fedha 2023/24, Baraza limefanikisha kufanya zoezi la kuhesabu mali kama utaratibu unavyoelekeza. Kiambatanisho nambari 1 kinahusika.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Baraza la Manispaa Mjini kukiri kuwepo kwa kasoro hiyo ya kutokufanya zoezi la utambuzi wa vifaa vya taasisi kwa kila mwaka kama sheria namba 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina pamoja na kanuni na miongozo inayotolewa na Serikali, kamati ua PAC imebaini mapungufu hayo yametokana na kutokuwa na wataalum katika kitengo hicho.

Kamati ya PAC baada ya kupitia vielelezo vilivyowasilishwa mbele ya kamati juu ya hatua mbali mbali zilizochukuliwa na Baraza katika kuhakikisha

kasoro hiyo inaondoka kamati imeridhishwa na utekelezaji wa hoja hii na kuiondoa hoja.

Hoja nambari: 6.3.2.2: Kutokuwepo kwa mfumo maalum wa kuhifadhi taarifa za vianzio vya ukusanyaji wa mapato

Kifungu nambari 70 cha sheria namba 7 ya Serikali za Mitaa ya 2014 kimelipa fursa Baraza kukusanya mapato mbalimbali yatokanayo na kodi, vianzio mbalimbali pamoja na fedha zinazotokana na vitega uchumi, miradi n.k.

Kanuni nambari 27(3) ya kanuni za usiamamizi wa fedha za umma za 2021 inaeleza kwamba Mamlaka ya Serikali za Mitaa itakuwa na uwezo wa kuweka malengo ya mapato.

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Manispaa Mjini hawana mfumo maalum wa kuhifadhia kumbukumbu zinazotokana na vianzio mbalimbali vya mapato kama vile fomu za leseni za biashara, mabango, ada ya usajili wa wafanyabiashara ndogo ndogo, n.k jambo ambalo linapelekea Baraza kushindwa kuweka na kufikia malengo halisi ya ukusanyaji wa mapato kutokanwa na kutojulikana kwa vianzio halisi vya ukusanyaji wa mapato.

Aidha, ukaguzi umeshindwa kujiridhisha na uhalisia wa makusanya ya mapato yanayotokana na vianzio hivyo kutokana na Barza hilo kutojua idadi halisi ya vianzio vyake.

Kukosekana kwa mifumo ya kuhifadhia kumbukumbu zilizoainishwa hapo juu kunapelekea:

- Kutojuwa uhalisia na mtiririko mzima wa fedha zilizokusanywa.
- Kutojulikana kwa takwimu halisi za vianzio vya mapato kama viel idadi ya mabango ya matangazo yanayotakiwa kulipiwa mapato, leseni, maduka yanayokusanywa taka, mahoteli yanayokusanywa taka, maskuli na taasisi zikiwemo makanisa na miskiti, idadi ya fomu za leseni zilizopokelewa na Baraza n.k.
- Kuwepo kwa ugumu wa ufuatiliaji wa mapato hayo hali ambayo imepelekea kuchukua muda mrefu kwa ajili ya kufuatilia kumbukumbu kwenye mafaili hususan kumbukumbu za miaka ya nyuma.
- Kuwepo kwa ugumu wa ufuatiliaji wa mapato hayo hali ambayo imepelekea kuchukua muda mrefu kwa ajili ya kufuatilia kumbukumbu kwenye mafaili hususan kumbukumbu za miaka ya nyuma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza kuhakikisha kwamba unachukua hatua za makusudi za kuanzisha mfumo wa kuhifadhia taarifa mbalimbali ili uweze kuwasaidia watendaji katika kutekeleza majukumu yao kwa urahisi.

Majibu ya Uongozi wa Baraza

Mfumo ulioridhiwa na kutumika kwa ukusanyaji wa mapato kwa Manispaa ya Mjini ni mfumo wa MUTM. MUTM ni Mfumo wa Ukusanyaji wa Taarifa za Mapato, ulianzishwa mwaka 2017/18 na Halmashauri ya Kaskazini A. Baada ya kuwepo viashiria vingi vya upotevu wa mapato katika nyaja mbali mbali, Serikali iliona kuna haja ya kuongeza udhibiti wa makusanyo kwa kutumia njia za mifumo, ndipo Wizara ikapendekeza mfumo huo utumike katika Halmashauri na Manispaa zote, na kwa Manispaa ya Mjini umeanza kutumika mwaka wa 2020. Baada ya changamoto nyingi keundelea kujitokeza kutokana na mfumo huo ikiwemo kutotafautisha vyanzo vya mapato, kutotoa taarifa za makusanyo kwa uwazi, kutokuwa na mahusiano ya taarifa za makusanyo kwa malipo yanayopitia benki na mfumo nakadhalika. OR TAMISEMI imeamua kuuboresha mfumo huo ambao kwa sasa unajuilikana kwa jina la ZAN MUTM.

Kwa upande wa Baraza, ZAN MUTM umeanza kutumika mwezi wa Septemba mwaka 2023. Pamoja na jitihada mbali mbali zinazofanywa, Baraza linaendelea na kufanya tathmini ya mfumo huo ili kuhakikisha taarifa za vyanzo vya makusanyo zinakuwemo.

Hali halisi kwa sasa

ZAN MUTM ni mfumo ambao umeanzishwa na kusimamiwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ (OR – TAMISEMIM). Wajibu wa Baraza ni kufuata maelekezo juu ya utaratibu wa kuingiza na kutumia taarifa za mfumo, hivyo changamoto zinazojitokeza zinawasilishwa OR - TAMISEMIM kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi ikiwemo kuweka mapato kulingana na vyanzo husika.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ua PAC katika kufuatilia utekekelezaji wa hoja hii, imebaini pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuanzisha mfumo mpya wa ZAN MUTM ila bado mfumo huo mpya katika tendaji kazi wake una mapungufu mengi ambayo yanaadhiri utendaji mzima wa kazi za Baraza. Mapungufu hayo ni kama ifuatavyo:-

- Mfumo kutokufanya usuluhishi wa taarifa za Makusanyo (Reconcilliation).
- Mfumo huu pia hauna identification yoyote ya mapato yanayokusanywa na Baraza.
- Maafisa Mapato wa Baraza kutokuwa na uelewa juu ya utumiaji wa mfumo.
- Mfumo huu kutokufanyiwa mapitio ya mara kwa mara ili kuweza kusuluhisha changamoto zinazojitokeza za makusanyo.
- Mfumo kutokutoa taarifa za makusanyo ya kila mwezi.

Kwa mnasaba huo, Kamati ya PAC haikuridhishwa na utekelezaji wa Mfumo huu na kupelekea hoja hii kubakia kwa hatua za utekelezaji.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauagiza Uongozi wa Baraza la Manispaa Mjini kufanya kikao cha pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-gaz) na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ili kutafuta ufumbuzi wa haraka wa changamoto zilizopo katika Mfumo wa Zan MUTM ili kuondokana na upotevu wa fedha za Serikali zitokanazo na Makusanyo.

Hoja Nambari: 6.3.2.3 Kutokuwepo kwa mchanganuo wa vyanzo vya mapato katika mfumo wa makusanyo MUTM.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 27(2)(a) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa fedha za Umma ya mwaka 2016 pamoja na kanuni nambari 25(1-2) na kanuni nambari 122(1)(a-d) ya kanuni ya usimamizi wa fedha za umma ya 2021, zinahimiza usahihi na uwazi wa taarifa za mapato/fedha za Taasisi.

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Manispaa Mjini lina vianzio vya makusanyo ya mapato visivyopongua 19 vya ukusanyaji wa mapato ambayo yanasaidia katika utekelezaji wa majukumu ya Baraza kama vile mapato yatokanayo na huduma za ada ya usafi, leseni, fomu, masoko, nk.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kwamba mapato yote yanaingizwa katika mfumo wa MUTM kupitia hesabu ya mapato yenye nambari 0404007000 bila ya kuwepo mchanganuo au kutofautisha aina na kiwango cha kila chanzo cha mapato kilicho kusanywa kwa kipindi husika jambo ambalo limepelekea ukaguzi kushindwa kutathmini na kujua hali halisi ya ukusanyaji wa mapato kwa kila chanzo kulinga na makadirio yaliyowekwa.

Aidha, ukaguzi umeshindwa kujiridhisha na kuthibitisha taarifa za mapato zilizoainishwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka kutokana na kukosekana kwa uwazi wa taarifa za kila kianzio husika.

Kukosekana kwa mchanganuo wa vyanzo mbalimbali vya mapato katika mfumo wa makusanyo unaotumiwa na Baraza unaweza kupelekea:

1. Kukosekana kwa uwazi na takwimu usahihi za mapato kulingana na vyanzo husika.
2. Kushindwa kufanya tahtnini juu ya mwenendo mzima wa ukusanyaji mapato
3. Kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa Mapato ya Serikali kutokana na kutojulikana kima halisi cha fedha kinakusanywa kwa kila chanzo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa Mjini kuweka alama za utambulisho “code” ambazo zitainisha na kutofautisha aina na kiwango halisi cha mapato yaliyokusanywa na kwa chanzo kwa mwaka husika.

Majibu ya Uongozi wa Baraza

MTUM ni mfumo ambao umeanzishwa na kusimamiwa na (OR) TAMISEMIM. Wajibu wa Baraza nikufuata maelekezo juu ya namna gani wataweza kuingiza na kutumia taarifa za mfumo hivyo, kwa upande wa Baraza changamoto ambazo zinakabiliana nazo kutokana na mfumo zinawasilishwa Wizarani. Baada ya jitihada mbali mbali Wizara imeandaa mfumo unaoainisha vyanzo vya mapato ingawa bado haujatatua changamoto ya kutambua taarifa za malipo zinazofanywa kwa kutumia uhaulishaji wa kibenki “transfer” jambo ambalo linapelekea kushindwa kupata taarifa sahihi kwa wakati na pia kufanya suluhisho kwa hesabu kuanzia ngazi za chini.

Baraza linaendelea kuliona jambo hilo linachangia kushidwa kukamilisha kuandaa hesabu kwa mujibu wa sheria zilizopo hivyo, Baraza linampango wa kuandaa mfumo wa ndani ambao linaamini litapunguza changamoto hizo zinazojitokeza kwa kiwango kikubwa.

Hali halisi kwa sasa

Kutokana na maboresho ya mfumo wa ZAN MTUM vianzio mbali mbali vya mapato na mchanganuo wake vinaonekana katika mfumo huo. Kama inavyoonekana kwenye kiambatanisho namba 3.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Uchunguzi wa kamati ya PAC katika hoja hii unaenda sambamba na Hoja Nambari: 6.3.2.2.

Hoja Nambari: 6.3.2.4 Tofauti ya Bakaa ya Fedha ya Kufunga na Kufungulia Mwaka shilingi 178,446,089

Ukaguzi umekagua kumbukumbu mbalimbali za kurikodia taarifa za fedha zikiwemo daftari la kurikodia fedha taslim, taarifa za Benki pamoja na hesabu ya mwisho wa mwaka na kubaini kwamba bakaa ya fedha zilizowasilishwa kwenye hesabu ya kufungia mwaka imetofautiana na bakaa ya kufungulia mwaka ambapo hesabu ya mwisho wa mwaka inonyesha bakaa ya kufungia mwaka 2021/2022 shilingi **383,292,684.38** na bakaa ya kufungulia mwaka 2022/2023 ni shilingi **561,738,773.29** hivyo kupelekea tofauti ya shilingi **178,446,089** baina ya bakaa ya kufungia na kufungulia mwaka. Aidha ukaguzi umebaini kuwa bakaa ya kufungulia mwaka ilyoainishwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka shilingi **561,738,773.29** inakwenda sambamba na bakaa iliopo benki katika

akaunti ya mapato. Hata hivyo ukaguzi umeshindwa kujua sababu zilizopelekea kutowiana kwa bakaa za fedha hizo.

Kutokuwepo kwa usawa baina ya hesabu ya mwisho wa mwaka pamoja na mabuku ya kurikodia fedha taslim za mapato kunapelekea kukosekana kwa ithibati ya taarifa za hesabu ya mwisho wa mwaka iliyowasilishwa kwa Mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa baraza uhakikishe unarekebisha mapungufu yaliyo kwenye hesabu za nyuma (mwaka 2021/2022) na kuweka bakaa sahihi ili kuwe na usawa baina ya taarifa zinazowasilishwa kwenye hesabu ya mwisho wa mwaka 2022/2023

Majibu ya Uongozi wa Baraza

Baraza linakiri kuwa bakaa ya kufungia hesabu iloainishwa kwa mwaka wa fedha 2021/22 ni TZS 383,292,684.38 ambapo fedha za uanzilishi kwa mwaka wa fedha 2022/23 ni TZS 561,738,773.29. Hali hii imekuja baada ya kufanya upembuzi wa taarifa za mapato na matumizi na kuona tofauti mbali mbali za hesabu baina ya mfumo wa baraza na taarifa zilizoingizwa katika daftari la kurekodia fedha taslim"Cash book" liliopo (OR) Fedha na Mipango. Kutokana na hali hiyo, Baraza liliamua kufanya mabadiliko ya kuweka bakaa la awali katika kitabu cha hesabu za mwaka kwa mujibu wa hesabu za kibenki.

Hali halisi kwa sasa

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kuwepo kwa tofauti ya bakaa ya fedha ya kufunga na kufungulia mwaka imerekebishwa. Kama inavyoonekana kwenye kiambatanisho namba 3.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, kamati ya PAC imebaini kuwa utofauti uliojitokeza wa bakaa ya fedha katika kufunga na kufungulia mwaka umetokana na muhasibu wa baraza kutumia mfumo wa kufunga hesabu katika daftari la kurekodia fedha taslim (cash book) liliopo (OR) Fedha na Mipango na bila kufanya usuluhishi wa taarifa za bank.

Wakati wa uchunguzi wa hoja hii, kamati imebaini kuwa changamoto hizo zimetokana na mfumo wa EPICAL ulianzishwa na (OR) Fedha na Mipango ambao haufanyi usuluhishi wa taarifa za kifedha.

Kwa msingi huo, Kamati ya PAC imeridhika na hatua zilizochukuliwa za marekebisho na imeiondoa hoja hii.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauagiza Uongozi wa Baraza la Manispaa Mjini kuhakikisha wanafuata miongozo ya ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka ili kuondokana na upotevu wa fedha za Serikali.

Hoja Nambari: 6.3.2.5 Kutofanyika kwa usulihishi wa kibenki Bank reconciliation na taarifa za matumizi

Section 105(1) cha kanuni za 2021 za sharia ya usimamizi wa fedha za umma za nambari 12 ya 2016 kinamtaka Afisa Masuuli kufanya usuluhishi wa kibenki kila mwezi au mara kwa mara kutegemea na miongozo ya Hazina au matoleo mengine yaliyotolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali.

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Manispaa Mjini halifanyi usulihishi wa kibenki kama kanuni zinavyoelezea jambo ambalo limepelekea Baraza kushidwa kugundua sababu zilizopelekea kutowiana kwa taarifa zilizorikodiwa katika mabuku ya kurikodia fedha Taslim na taarifa za fedha zilizopo katika taarifa za benki (Bank statements).

Kutofanyika kwa usuluhishi wa kibenki kwa mujibu wa kanuni za usimamizi wa fedha za umma kumepelekea kutopatikana kwa usahihi wa taarifa za fedha zilizoainishwa katika vitabu vya kumbukumbu, taarifa zililoingizwa kwenye mfumo pamoja na taarifa zilizopo benki.

Aidha, Taasisi kushindwa kugundua makosa katika hatua za awali na kupelekea kuendelea kufanya makossa hayo kwa muda mrefu jambo ambalo linapepekea ugumu katika utatuzi wake.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza kufanya usuluhishi wa kibenki kila wiki ili kuweza kugundua mapema, kupunguza au kuzuia matatizo yanayopelekea kutopatikana kwa usahihi wa taarifa za mapato pamoja na matumizi zinazorikodiwa katika vitabu vya hesabu za Taasisi.

Majibu ya Uongozi wa Baraza

Changamoto za mfumo wa MUTM ni miongoni mwa sababu kubwa ya kutoweza kuandaa taarifa za kufanya usuluhishi baina ya mapato na matumizi wakati wa kufunga hesabu. MUTM ni mfumo ambao si tu unashindwa kutoa taarifa za makusanyo kulingana na chanzo husika bali hata kupokea taarifa za makusanyo yanayofanywa kwa njia nyengine ukiachana na POS. Itakumbukwa kuwa MUTM upo chini ya usimamizi wa Afisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ hivyo, Baraza linaendelea kuwasilisha changamoto hizo ili kupata ufumbuzi ingawa si kwa njia ya maadishi. Pamoja na maboresho yaliofanywa katika mfumo wa ZAN MUTM, Baraza linaendelea kufuatilia taarifa za mfumo wakati likitafakari uwezekano wa kuandaa mfumo wa ndani ambao utaweza kuondosha changamoto za taarifa za makusanyo na matumizi jambo litarahisisha kufanya zoezi la usuluhishi wa hesabu kwa urahisi zaidi.

Vile vile, Baraza linatarajia kununua vitendea kazi pamoja na kuandaa mafunzo kwa wakuu wa mapato yatakayo wawezasha kupata taarifa kupitia mfumo husika, kuhifadhi kumbukumbu na vielelezo ili Baraza liweze kufanya usuluhishi wa hesabu kuanzia ngazi za chini.

Hali halisi Kwa sasa

Baraza tayari limeshawapatia mafunzo watendaji wa mapato lakini bado kuna changamoto ya kutokusomana kwa mifumo ya ZAN MTUM na mfumo ya kibenki.

Aidha, kwa upande wa usuluhishi wa matumizi, Baraza linashindwa kufanya usuluhishi huo kwa sababu Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGA) za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinatumia akaunti ya pamoja kwa ajili ya kufanya matumizi kupitia akaunti iliyoko Benki Kuu ya Tanzania, ambapo msimamizi wa akaunti hiyo ni Afisi ya Rais Fedha na Mipango. Vile vile Usuluhishi huu unafanywa kwa pamoja kupitia wasimamizi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambao wapo Afisi ya Raisi Fedha na Mipango Zanzibar.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, imebaini kuwa changamoto ya kutokusomana kwa mifumo ya ZAN MTUM na mfumo ya kibenki inaendelea licha ya juhudi mbali mbali zilizochukuliwa na uongozi wa Baraza la Manisspa Mjini, Kamati haikuridhika na utekelezaji na kuibakisha hoja hii kwa ajili ya ufumbuzi.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauagiza Uongozi wa Baraza kukaa pamoja na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhakikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGA) zinafanya usuluhisi wa taarifa za matumizi ili kuepusha kujitokeza kwa changamoto ya kutokusomana kwa taarifa.

HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI UNGUJA

Hoja nambari 6.3.7.1: Tofauti ya Bakaa ya Fedha kwenye hesabu ya mwisho wa mwaka na bakaa iliopo benki shilingi 44,622,028.94

Ukaguzi umekagua kumbukumbu mbali mbali za kurikodia taarifa za fedha zikiwemo katika daftari la kurikodia fedha taslim, taarifa za benki pamoja na hesabu ya mwisho wa mwaka na kubaini kwamba bakaa ya kufungia mwaka 721,660,979.13 na bakaa ya fedha za kwenye taarifa za benki inayoishia Juni 2023 766,283,008.07 kuna tofauti ya shilingi 44,622,028.94 katika akaunti ya mapato ya Halmashauri jambo ambalo limepelekea ukaguzi kushindwa kuthibitisha usahihi wa taarifa zilizoainishwa katika hesabu hizo. Hata hivyo ukaguzi haukuweza kujua sababu zilizopelekea kutowiana kwa bakaa za fedha hizo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Halmashauri uhakikishe unarekebisha mapungufu yaliyomo kwenye hesabu na kuweka bakaa sahihi ili kuwe na usawa baina ya taarifa zinazowasilishwa kwenye hesabu ya mwisho wa mwaka 2022/2023 na zile za benki.

Majibu ya Uongozi wa Halmashuri

Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja mnamo tarehe 23 Juni, 2023 ilifanya uhaulisho wa fedha kutoka katika hesabu yake ya Mapato (A/C NO 0765272001) na kupeleka hesabu ya matumizi ya maendeleo (AC/ NO 9928210204), kutokana na kosa (error) lililojitokeza Benki ya PBZ ilishindwa kuhamisha fedha hizo na ikazihamisha tarehe 11/07/2023 na kupelekea tofauti hiyo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kwamba ni kweli wakati Mkaguzi anafika Halmashauri ya Wilaya ya Kusini kulijitokeza kasoro ya kuwepo tofauti ya fedha zilizopo katika hesabu ya mwisho wa mwaka na bakaa iliyopo benki shilingi 44,622,028.94. hali hiyo ilisababishwa na Watendaji wa Halmashauri kufunga hesabu zao kwa kutumia kumbukumbu ziliopo katika Mfumo (balance as per Bank) badala ya kutumia fedha halisi walizofanyia matumizi (balance as per cash flow). Hata hivyo, Kamati ilipitia kielelezo cha barua kutoka Halmashauri kilichothibitisha kwamba fedha hizo zilishindwa kuhamisha na kurekebishwa kasoro hiyo tarehe 11/07/2023 na kwasasa tayari kasoro hiyo imesharekebishwa. Kwa mnasaba huo, Kamati imeiondoa hoja hii.

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati pia imebaini kwamba licha ya utekelezaji mzuri wa majukumu yake lakini, kwa kipindi kirefu Halmashauri ya Wilaya ya Kusini haina Mkurugenzi badala yake kazi zote zinasimamiwa chini ya uongozi wa Kaimu wa Halmashauri hiyo ambae ameanza kutumikia nafasi

hiyo kwa barua yenye kumbukumbu nambari CAC.48/179/01/61 ya tarehe 19 Oktoba, 2023 takriban mwaka mmoja na miezi mitatu imepita hivi sasa ambapo ni kinyume na Sheria Nambari 11 ya 2016 na Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 ambayo inamtaka mtu anayekaimu nafasi asizidi mwaka mmoja bila ya kuthibitishwa au kuondolewa.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini ufunge hesabu zake za mwisho wa mwaka kwa umakini mkubwa ili kusijitokeze utafauti wowote wa bakaa ya fedha kati ya benki na kwenye hesabu yenyewe.
2. Waziri anayehusika na Tawala za Mikoa ahakikishe anawasiliana na Mamlaka Teule ili uteuzi wa nafasi ya Murugenzi uweze kufanyika kama zinavyoelekeza Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma.

Hoja nambari 6.3.7.2: Kukosekana kwa mapato ya leseni za skuli binafsi shilingi 1,500,000

Kwa mujibu wa sheria namba 7 ya mwaka 2014 kifungu namba 70 (b) (ii) pamoja na kanunni ya mwaka 2020 ya kanununi za huduma zinazotolewa na Serikali za mitaa kifungu namba 31(2) na 32 vinavyoelezea juu ya namna ya kufanya biashara na ukataji wa lesseni za biashara.

Ukaguzi umefanya mapitio na tathmini ya mapato yanayotokana na ukataji wa leseni zitokanazo na uwepo wa skuli binafsi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja na kubaini mara baada wamiliki wa skuli binafsi kupata kibali cha usajili kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya amali wanatakiwa kulipia mapato ya leseni kwa viwango vifuatavyo:-

i. Skuli za Maandalizi (nursery) 100,000
ii. Skuli ya Msingi na Mandalizi 250,000
iii. Skuli ya Maandalizi, Msingi na Sekondari 500,000

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni uwepo wa skuli nne (4) ambazo zimeshindwa kutekeleza agizo la kukata leseni kwa mujibu wa muongozo uliotolewa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kupelekea kuikosesha Serekali Jumla ya shilingi 1,500,000 ikiwa ni ada ya ukataji leseni.

Orodha ya skuli ambazo hazijakata lesseni za biashara ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Nam.	**Jina la skuli**	**Malipo ya leseni**
1.	Bwejuu charity school	500,000.
2.	Assalaam International school	250,000.
3.	South East Cost	250,000

4.	Dallalul Khairat	500,000
Jumla		**1,500,000**

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini kuongeza mikakati imara ya kusimamia vyanzo vya mapato ikiwemo kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuweza kujiendesha kiufanisi pindipo baadhi ya vyanzo vitakaposhindwa kukidhi makusanyo halisi kwa mujibu wa makadirio ya bajeti.

Majibu ya Uongozi wa Halmashuri

Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja tayari imekutana na baadhi ya wahusika wa skuli hizo na kuwapa elimu na inaendelea kutoa msisitizo kwa baadhi ya skuli ambazo hazijaitikia wito wetu tuliowapelekea.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia majibu ya utekelezaji wa hoja hii, Kamati ya PAC imegundua kuwa ni kweli kasoro alizobaini Mkaguzi zilikuwepo. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba baadhi ya skuli hazikuitikia wito kutokana na kuwepo uelewa mdogo wa kujua kwamba kwa vile wamepatiwa leseni na Wizara hawalazimiki kulipa gharama nyengine yoyote katika maeneo wanayofanyia kazi (Halmashauri). Hali hiyo imepelekea skuli ya Jamii ya Bwejuu Charity kushindwa kulipia leseni zao.

Sambamba na hilo, skuli ya moja ya South East Cost imeitikia wito na kuahidi ikifika mwezi wa Januari, 2025 kufanya malipo ya leseni. Kwa vile hoja hii hakuteklezwa kwa asilimia kubwa, Kamati imeibakisha kwa hatua za utekelezaji wake.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini iendelee na juhudi zake za utoaji uelewa kwa wananchi na wamiliki wa skuli ili waweze kufanya malipo ya leseni na kuchangia katika mapato ya Halmashauri zao ambayo ndio chachu ya maendeleo yao.
2. Uongozi wa Halmashauri uhakikishe madeni ya malipo ya leseni yanalipwa kwa skuli zote zilizokuwa hazijalipwa ili Serikali na Halmashauri iweze kujiendeshe.

Hoja nambari 6.3.7.3: Kutokuwekewa alama za Utambulisho kwa samani za Ofisi.

Kifungu namba 58(d) cha sheria ya Uanzishwaji wa Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali kinaleza' "Afisa Masuuli wa Taasisi ya umma atahakikisha utaratibu wa kuhifadhi unawekwa ili kuondosha wizi, hasara, kupotea na matumizi mabaya".

Ukaguzi umebaini Halmashauri ya Wilaya ya Kusini inamililki samani kwa ajili ya matumizi ya kuendeshea shughuli zake lakini hazijaekewa alama za utambulisho, hali hiyo inaweza kupelekea samani hizo kutotambulika na kuweza kupotea kwa urahisi au kuhamishwa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini kuchukua juhudi za haraka kuziwekea alama samani zake zote zilizokosa alama ili kuziepusha na upotevu.

Majibu ya Uongozi wa Halmashuri

Halmashauri imepokea ushauri na tayari imeweza kuziwekea alama za utambulisho samani zake zote mpya.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Ni kweli kwamba wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake katika Halmashauri ya Wilaya ya Kusini, kulikuwa na kasoro ya kutowekewa alama za utambulisho samani za Ofisi hiyo. Hata hivyo, kwasasa kasoro hiyo imeshafanyiwa kazi.

Sambamba na hilo, Kamati imetaka kujua kuwa Halmashauri inayo kitengo cha 'Asset Management Unit' kama ilivyoelezwa na Sheria ya Msajili wa Hazina na kuelezwa kwamba tayari Halashauri imeshaunda kitengo hicho na kinao watumisihi wake. Hivyo, Kamati imeondoa hoja hii.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inautaka uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini kuchukua juhudi za kuziwekea alama samani zake zote inazonunua ili kuepusha upotevu wake.

Hoja nambari 6.3.7.4: Kutokufanyika kwa tathmini ya utendaji kazi (Performance Appraisal)

Kifungu nambari 93 (1) cha kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 kinachoelekeza "Kila taasisi ya umma italazimika kumfanyia tathmini ya utendaji wa kazi mtumishi wake kila mwaka. Fomu ya tathmini itatolewa na Afisi Kuu ya Utumishi wa Umma".

Ukaguzi umebaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini haifanyi tathmini ya utendaji kazi kwa watumishi wake kama ilivyoelekezwa katika kanuni ya utumishi.

Kutokufanyika kwa tathmini ya utendaji kazi kwa watumishi kunapelekea kuwakosesha haki zao za msingi kwa mujibu wa sheria ikiwemo kupata nyongeza ya mwaka, kupandishwa madaraja pamoja na stahiki nyenginezo zinazohusiana na mtumishi wa Umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja kufanya tathmini ya utendaji kazi kwa watumishi wake kila mwaka (performance appraisal) kama kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 inavyoelekeza ili kuweza kupima ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa miongozo na taratibu za kiutumishi.

Majibu ya Uongozi wa Halmashuri

Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja imepokea pendekezo na imelifanyia kazi, hadi sasa watumishi takriban asilimia themanini 80% tayari wameshafanyiwa tathmini ya utendaji kazi na miongoni mwao tayari wameshapata nyongeza ya mwaka (incriment) kupitia mishahara yao.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kwamba ni kweli kulikuwa na kasoro ya kutokufanyika kwa tathmini ya utendaji kazi (Performance Appraisal) wakati Mkaguzi anatekeleza kazi zake. Hali hiyo ilisababishwa na Watendaji wa Halmshauri waliopo Ofisini wakati huo kutokuwa na uelewa wa kufuatilia na kuwafanyia tathmini Watumishi wao ili waweze kupata haki zao za nyongeza ya mshahara.

Kwasasa, Watumishi wengi wameshawafanyia tathmini na tayari wameshapata nyongeza zao isipokuwa kuna Wakuu wa Vitengo sita bado hawajawafanyia tathmini hiyo, Kutokana na utekelezaji uliofanyika, Kamati imeamua kuiacha hoja hii kwa hatua za Mkaguzi kwenda kujiridhisha.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inautaka Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini kufanya tathmini ya utendaji kazi kwa watumishi wake kila mwaka (performance appraisal) ikiwemo Wakuu wake sita wa Vitengo waliobakia ili kuweza kupima ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yao na kuwapatia stahiki zao wote wanaohusika.

Hoja nambari 6.3.7.5: Kutokuwepo kwa Mpango Maalum wa Mafunzo.

Kanuni ya 74(1) ya kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014 inazitaka “Taasisi zote za Serikali kuandaa mpango maalum wa mafunzo pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya mafunzo hayo”. Aidha kwa mujibu wa waraka OR/UUU CAB.40/158/01/54 na CAB.40/158/01/37 unazitaka Wizara na Taasisi za umma zinatakiwa kufanya maandalizi ya mpango wa mafunzo ili kujua mahitaji (Training Needs Assessment) na kuwasilisha mpango wa mafunzo.

Ukaguzi umebaini kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2023 limetumia jumla ya shilingi 21,248,400 kwa ajili ya mafunzo ya muda mrefu na mfupi bila ya kuwepo kwa Mpango Mkuu wa mafunzo hivyo ukaguzi umeshindwa kuthibitisha

watendaji waliopatiwa fursa za mafunzo hayo kama yalikuwa na mahitaji kama sheria na miongozo inavyoelekeza. Jadweli lifuatalo linaonyesha orodha ya watumishi hao:

Nam	**Jina**	**Muda wa mafunzo**	**Mafunzo aliyopata**	**Muda wa mafunzo**
1.	Moh'd Kh. Abdalla	Miaka mine	Computer engineering and information technology	2025
2.	Faida M Makame	Miaka mitatu	Business human resources	2023
3.	KhatibM.Khatib	Miaka miwili	Master on Economic and Finance	2025
4.	Hilda KhJuma	Miaka mitatu	Degree on Economic and Development	2025
5.	Abdulwarith K. Fatawi	Wiki 2	Monitoring and Evaluation	2023
6.	Hassan P. Ali	Wiki 2	Waste Management	2023
7.	Shemsa Kh. Yussuf	Wiki 1		2023
8.	Hamid S Ali	Wiki 1		2023
9	Sibadili Z. Arafat	Wiki 1	Record and Archive Management	2023
10.	Subira Kh. Fadhil	Wiki 1	Record and Archive Management	2023
11.	Mtumwa S Ali	Wiki 1	Record and Archive Management	2023

12.	Saleh A Seif	Wiki 2	Monitoring and Evaluation	2023

Majibu ya Uongozi wa Halmashuri

Halmashauri imepokea pendekezo na italifanyia kazi ili iendane na taratibu na Sheria za usimamizi wa Rasilimali watu.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kuchunguza utekelezaji wa hoja hii, Kamati ya PAC imetaka kujua hao wafanyakazi waliopo masomoni walipelekwa kwa utaratibu gani na kuelezwa kwamba Halmashauri ilikuwa inasikiliza matakwa ya Wafanyakazi wao wanaotaka kwenda kusoma bila ya kuzingatia kwamba kuna Mpango wao wa Mafunzo wanatakiwa waufuate. Hata hivyo, kwasasa wanajipanga kutekeleza Mpango wao mpya watakaouandaa. Kwa mnasaba huo, hoja hii inabakia hadi Mkaguzi atakapokwenda kujiridhisha katika ukaguzi wake wa mwaka 2023/2024.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inautaka uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini kuhakikisha unaandaa Mpango wake wa mafunzo na kuutekeleza ili kuondoa malalamiko ya kuonekana wepo wa upendeleo fursa za kusoma kwa Wafanyakazi wao.

BARAZA LA MJI WETE

Hoja nambari 6.3.8.1: Kukosekana kwa Nyaraka za uchambuzi wa madeni shilingi 33,486,026.74.

Ukaguzi ulipitia hesabu ya mwisho wa mwaka iliyowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Baraza la Mji Wete na kubaini kwamba kuna madeni ya wafanyakazi na wasambazaji wa bidhaa mbalimbali kwa ajili ya Baraza yenye thamani ya shilingi 75,615,790.74. Hadi ukaguzi huu unakamilika mnamo Februari, 2024 madeni yaliyokuwa na nyaraka za uthibitisho ni shilingi 42,129,764 na hivyo kutokupatiwa nyaraka za uthibitisho wa deni la shilingi 33,486,026.74 kwa ajili ya ukaguzi jambo ambalo limepelekea ukaguzi kushindwa kuthibitisha uhalali wa madeni hayo. Kukosekana kwa kumbukumbu za kuthibitisha uhalali wa kuwepo kwa madeni hayo kunaweza kupelekea taarifa za hesabu zilizowasilishwa kutoonyesha sura halisi na sahihi. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Wete kuhakikisha nyaraka hizo zinapatikana kwa ajili ya kufanyiwa uhakiki wa uhalali wa madeni hayo ili hatua za kuombewa malipo ziweze kuchukuliwa kwa lengo la kuepusha kujitokeza kwa malalamiko kwa watumishi wa umma na watoa huduma mbali mbali. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 38: Madeni yaliyokosa Nyaraka za Uchambuzi

Nam	**Mdai**	**Kiasi Cha Deni (Tshs)**
1.	Wasambazaji/Watoa huduma	1,927,189.74
2.	Wafanyakazi	13,698,000.00
3.	Taasisi Nyengine za Serikali	17,860,837.00
Jumla		**33,486,026.74**

Majibu ya Uongozi wa Baraza la Mji Wete

Mheshimiwa Mwenyekiti ni kweli baadhi ya vielelezo vya madeni havipo na mpaka sasa vyengine bado havijakamilika na hii ni kutokana na kwamba madeni mengi ambayo hayana vielezo ni ya miaka ya nyuma sana na hii inapelekea kutopata ithibati sahihi ambazo zinaonesha uhalisia wa madeni haya .

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC baada ya kufanya uchunguzi na ufuatiliaji wake kuhusiana na hoja hii ilibaini mambo yafuatayo:

1. Licha ya majibu ya uongozi wa Baraza la Mji Wete kuonesha kukiri kwamba ni kweli wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake katika Taasisi hiyo, baadhi ya vielelezo vya madeni vilikosekana kwa ukaguzi. Hata hivyo, watendaji wa Baraza walikuwa wakitofautiana juu ya uwepo wa majibu hayo ambapo Muhasibu wa Baraza alidai kuwa vielelezo vilikuwepo.
   Hatimae, Kamati ilibaini kwamba baadhi ya vielelezo hivyo (Fomu za malipo/vocha) vilikuwepo na Mkaguzi aliviona wakati wa ukaguzi ila vilikosa uhalali kwa vile vilikuwa havija kamilika na ndio maana Mkaguzi hakuvitia alama ya usahihi. Vielelezo vilivyokosekana ni pamoja na kutokuambatanishwa kwa mikataba ya malipo ya vikundi vya usafi katika vocha husika, kukosekana kwa 'invoice' ya vifaa vilivyonunuliwa na vielelezo vya malipo ya 'overtime'.
2. Kukosekana kwa umakini katika utekelezaji wa hoja za Mkaguzi. Hali hii imejitokeza baada ya Kamati kuuliza kwamba licha ya vielelezo kuwepo na Mkaguzi kutoridhika navyo, Watendaji wanakijua kilichosababisha Mkaguzi kushindwa kuvikubali vielelezo walivyompatia. Kamati imegundua kuna changamoto katika hilo na kupelekea majibu yanayotolewa kushindwa kuakisi hoja ya Mkaguzi.
3. Kuwepo kwa ukiukwaji wa Sheria na Kanuni za Fedha kwa vile Watendaji wa Baraza walikuwa wamepatiwa huduma lakini walishindwa kuwa vielelezo vinavyothibitisha uhalali wa malipo yanayostahiki. Hali hiyo inaweza kukosesha haki za Watoa Huduma husika.
4. Kuendelea kuwepo kwa madeni ya shilingi takribani milioni 15 kutoka Mamlaka ya Maji ZAWA kufuatia Baraza kupatiwa huduma za maji. Aidha, Tume ya Utangazaji Zanzibar nayo ilikuwa inalidai Baraza takribani shilingi milioni Kumi na Tano kufuatia uwepo wa 'online Television' lakini kwasasa deni hilo limeshalipwa

Katika kuhitimisha majadiliano ya hoja hii, Kamati ya PAC haikuridhika na majibu yaliyowasilishwa kwake hasa ukizingatia kwamba bado vielelezo husika havikuwepo wakati wa majadiliano. Hivyo, hoja hii inaendelea kubakia.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Uongozi wa Baraza la Mji Wete uwe makini katika ufuatiliaji hoja zinazoibuliwa na Mkaguzi hususan kwa kujua vitu vyote ambavyo amevikosa wakati wa ukaguzi na kuvitafutia ufumbuzi haraka iwezekanavyo.
2. Uongozi wa Baraza la Mji Wete uhakikishe unafuata kikamilifu Sheria na Kanuni za Fedha kwa kuambatanisha vielelezi stahiki kwa ununuzi stahiki uliofanyika.

Uongozi wa Baraza la Mji Wete ukamilishe malipo yanayodaiwa na ZAWA ili huduma ya maji iweze kupatikana kwa uendelevu wake.

Hoja nambari 6.3.8.2: Malipo ya Fedha ambayo Hayajawafikia Wadai shilingi 3,165,220.74.

Kwa mujibu wa kifungu namba 29(3)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 kinaleza kwamba "Katika kusimamia madeni Afisa Muhasibu atalipa madeni yote ya mikataba na fedha zote zinazodaiwa ndani ya muda ulioelezwa au uliokubaliwa". 81 Baada ya kupitia kumbukumbu za Afisi ya Baraza la Mji Wete zikiwemo daftari la fedha taslim na hati za malipo ukaguzi umebaini uwepo wa shilingi 3,165,220.74 ambazo zimelipwa kwa watoa huduma na taasisi mbali mbali kupitia mfumo wa ulipaji wa Baraza lakini fedha hizo hazijawafikia wadai. Hali hii inaweza kupelekea watoa huduma kutokupata haki yao ya malipo kwa wakati jambo ambalo linaweza kupelekea kukosa imani ya kufanya kazi na Baraza. Ulipwaji wa fedha usiomfikia mdai kwa muda muafaka ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu. Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Wete kuhakikisha unafanya juhudi za makusudi ili kuweza kuwalipa wadai hao. Mchanganuo wa malipo ya fedha hizo ni kama unavyoonekana katika jadweli lifuatalo:

Jadweli Nambari 39: Malipo ya fedha ambayo hayajawafikia Wadai

Hati Nam.	**Hundi Nam.**	**Thamani ya Fedha (Tshs)**	**Aliyelipwa**	**Maelezo**
27/6 26/6/2023	TISS	160,633.74	Amos Industries ltd	Malipo ya ununuzi wa maji ya kunjwa kwa matumizi ya ofisi
28/6 27/06/2023	TISS	2,980,000	Chasasa Services Station	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Diesel kwa matumizi ya Baraza la Mji Wete.
29/6 26/6/2023	TISS	24,587.00	ZRB	Malipo ya zuio la kodi kwa mfanyabiashara.
Jumla	**3,165,220.74**			

Majibu ya Uongozi wa Baraza la Mji Wete

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli malipo tajwa hapo juu yameshindwa kuwafikia walengwa kutokana na changamoto za kimfumo ambazo ziko nje ya uwezo wa ofisi kwani taratibu zote za malipo hayo zilikamilika ila BOT walishindwa kukamilisha malipo hayo hadi sasa.

Katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili ofisi ilimuandikia barua Afisa Mdhamini Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango yenye kumbukumbu namba REF: NO. BLMW/OR/TMSMIM/SMZ/P/F.10/VOL.II/126, ambapo nae Afisa Mdhamini alijibu aandikiwe Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na Ofisi ikamuandikia barua yenye kumbukumbu namba

REF: NO. BLMW/OR/TMSMIM/SMZ/P/F.10/VOL.XII/137

ambapo inendelea kufanyiwa kazi barua hiyo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia ukweli wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa kitengo cha Uhasibu hakikuwa makini katika utekelezaji wa majukumu yake hasa ukizingatia kwamba Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango huwa inatoa muongozo kuhusiana na tarehe za mwisho za kufanya malipo kupitia mfumo wa 'epica' ambapo Wahasibu wote wanatambua changamoto zinazoweza kujitokeza. Aidha, Wahasibu hawkufanya ufuatiliaji vizuri (Verification) haraka iwezekanavyo kwa malipo waliyoyafanya hasa ukizingatia mfumo wa Benki Kuu huwa unarudisha majibu ndani ya saa 24 iwapo kuna muamala haukukamilika.

Licha ya juhudi zote zilizochukuliwa na Baraza, Kamati imegundua kwamba bado Wadai hawajapokea malipo yao wakati huduma tayari imeshapokelewa na Baraza. Kwa mnasaba huo, Kamati inaendelea kuibakisha hoja hii hadi majibu kamili ya fedha zilizolipwa zimeishia wapi yatakapopatikana. Hivyo, hoja inaendelea kubakia.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Watendaji wa Baraza Mji Wete wafuate miongozo inayotolewa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ili kuepuka changamoto za ufanyaji wa malipo katika muda usiopendekezwa.
2. Uongozi wa Baraza la Mji Wete uhakikishe Wadai wote wanalipwa fedha zao kulingana na huduma waliyotoa.
3. Kitengo cha uhasibu kiwe makini katika utekelezaji wa majukumu yake ikiwemo kufuatilia kwa haraka changamoto zinazojitokeza za utumaji miamala ya fedha kupitia mfumo ili kuweza kurekebisha kasoro zilizopo kwa urahisi.

Hoja nambari 6.3.8.3: Hati za Malipo zenye nyaraka pungufu shilingi 5,005,220.74.

Kanuni ya 57(1)(2)(b) ya kanuni ya usimamizi ya fedha za umma ya mwaka 2021 inaeleza kuwa malipo yote lazima yaambatanishwe na hati ya malipo ambayo imekamilika nyaraka zote kwa mujibu wa maelekezo ya Hazina na kuidhinishwa na Afisa Mhasibu. Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya shilingi 5,005,220.74 zimetumika kwa ajili ya malipo mbali mbali ya Baraza la Mji Wete lakini baadhi ya nyaraka husika hazikuambatanishwa katika hati za malipo ili kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Hali hii inaweza kuwa imesababishwa na uwepo wa udhibiti wa ndani usioridhisha wa uhifadhi wa vielelezo vya fedha na vielelezo vyengine vinavyohusiana na uendeshaji wa kazi za Baraza au washika fedha wameshindwa kutimiza kikamilifu majukumu yao ya kuweka udhibiti mzuri wa uwekaji wa kumbu kumbu za nyaraka muhimu hasa vielelezo vya hati za malipo jambo ambalo linaweka uwezekano wa kutokea kwa matumizi yasiyoridhisha ya fedha za umma kwenye shughuli mbalimbali za Baraza.

Kutokuambatanishwa nyaraka kamili katika hati za malipo ni kwenda kinyume na Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Wete kuhakikisha wanaambatanisha vielelezo vyote husika vya malipo katika hati za malipo kwa wakati. Mchanganuo wa hati za malipo zenye nyaraka pungufu ni kama unavyoonekana katika jadweli lifuatalo:

Jadweli Nambari 40: Hati za Malipo Zenye Nyaraka Pungufu

Hati Nam.	**Hundi Nam.**	**Thamani ya Fedha (Tshs)**	**Aliyelipwa**	**Maelezo**
18/8 15/8/2022	TSS	1,840,000	Salim Awadh Salim	Malipo ya gharama za chakula.
27/6 26/6/2023	TISS	160,633.74	Amos Industries ltd	Malipo ya ununuzi wa maji ya kunjwa kwa matumizi ya ofisi
28/6 27/06/2023	TISS	2,980,000	Chasasa Services Station	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Diesel kwa matumizi ya Baraza la Mji

				Wete.
29/6 26/6/2023	TISS	24,587.00	ZRB	Malipo ya zuio la kodi kwa mfanyabiashara.
Jumla	**3,165,220.74**			

Majibu ya Uongozi wa Baraza la Mji Wete

Mheshimiwa Mwenyekiti, hati za malipo zenye nyaraka pungufu za Tsh 3,165,220.74 zenye vocha namba 27/6, 26/6/2023, 28/6 27/06/2023 na 29/6 26/6/2023ambazo malipo yake hayakukamilika kutokana na matatizo ya kimfumo kati ya BOT na walipwaji ilishindikana na kupelekea kukosekana kwa nyaraka hizo,na vocha namba 18/8 15/8/2022 yenye thamani ya Tsh 1,840,000 nyaraka zake zipo na zimekamilika.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imegundua kwamba msingi wa hoja hii unatokana na hoja nambari 6.3.8.2 inayohusiana na Malipo ya fedha ambayo hayajawafikia Wadai. Hali hiyo ilipelekea Wakaguzi kushindwa kupata vielelezo vya hati za malipo kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanywa. Hata hivyo, Kamati ilifanikiwa kupata kielelezo cha malipo ya gharama za chakula (risiti ya tarehe 18/8/2022) iliyoambatanishwa na vocha na dokezo la malipo hayo.

Katika kuchunguza kwa undani risiti hiyo, Kamati imebaini kulikuwa na kasoro kadhaa zilizokuwa zikiipatia mashaka Kamati kwani tarehe ya maombi ya barua ya ununuzi wa chakula cha kikao cha Wanafunzi kutoka kwa Bwana Salim Awadh Omar iliandikwa tarehe 28/4/2022 wakati kikao cha matumizi ya chakula hicho kilikuwa tarehe 28/4/2022, lakushangaza ‘comment’ za Mkurugenzi katika barua hiyo zilikuwa tarehe 27/4/2022 na muhuri wake ulikuwa tarehe 27/4/2022. Kwa mnasaba huo, kulikuwa na utofauti katika tarehe ambapo ‘comment’ za Mkurugenzi zilitakiwa ama ziwe tarehe 28 au zaidi ya tarehe hiyo.

Kwa vile Kamati imejiridhisha kwamba ni kweli malipo yaliyofanyika bila ya kuwepo vielelezo vilivyokamilika, Kamati ya PAC haikuridhika na malipo haya na kupelekea hoja kubakia.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Baraza la Mji Wete lihakikishe linatunza vizuri vielelezo vyake ili vitakapohitajika viweze kupaikana.
2. Mkurugenzi awe makini anapopitia na kuweka ‘comments’ zake katika barua anazoletewa na Watendaji ili kuepusha kuwepo shaka kwa watumizi wa barua hyo.

Hoja nambari 6.3.8.4: Kutokulipwa kwa deni la muda mrefu la ukodishwaji wa Bekari shilingi 6,200,000

Kwa mujibu wa kifungu namba 29(3)(b) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Namba 12 ya mwaka 2016 kinamtaka Afisa Muhasibu kulipa madeni yote ya mikataba na fedha zote zinazodaiwa ndani ya muda ulioelezwa au uliokubaliwa. Ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Mji Wete linadaiwa na Bwana Salum Ali Moh'd wa Wete deni ambalo limetokana na kulikodisha Baraza bekari iliopo Bomani Wete kwa bei ya shilingi 150,000 kwa mwezi. Aidha, ukaguzi umebaini Baraza liliingia katika makubaliano ya ukodishwaji wa bekari hiyo tangu mwaka 2017 na kulipa deni la miaka mitatu hadi mwaka 2019. Kuanzia tarehe 01.01.2020 hadi ukaguzi unakamilika mnamo mwezi Disemba, 2023 Baraza imelipa shilingi 1,000,000 kwa hati nambari 33/5 ya tarehe 29/5/2023 na hivyo kubakiza deni la shilingi 6,200,000.

Kutokuwalipa wafanyabiashara kwa wakati kunawadhoofisha wafanyabiashara hao na hivyo kukosa imani na Baraza na Serikali kwa ujumla na pia ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu. Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza kuhakikisha madeni yote yanafuatiliwa na kulipwa kwa wakati ili kuepusha uzorotaji katika utoaji wa huduma.

Majibu ya Uongozi wa Baraza la Mji Wete

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Ofisi ya Baraza la Mji Wete ilikuwa inalipa kodi ya bekari iliyopo kwa ajili ya matumizi ya KMKM jambo ambalo lilikuwa ni mzigo usiokuwa na tija kwa Baraza, na wakati ukaguzi ulipopita Ofisi ya Baraza la Mji Wete ililipa shilingi 1,000,000 kwa sababu kipindi hicho kulikuwa na mazungumzo yanaendelea ila kwa sasa tumeshalipa deni na tumeshavunja mkataba kwa maslahi ya Baraza.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa ni kweli Baraza la Mji Wete lilikuwa likidaiwa shilingi 6,200,000 na Bwana Salim Ali Moh'd. Hata hivyo, deni hilo limeshalipwa na kwasasa Baraza tayari limeshavunja Mkataba huo kupitia barua ya tarehe 10/9/2024 yenye kumbukumbu nambari BLMW/OR/TMSMIM/SMZ/P/A/8 Vo. 1/10.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Baraza la Mji Wete lihakikishe linakamilisha malipo ya fedha inazodaiwa mara tu baada ya huduma kupatiwa.

Hoja nambari 6.3.8.5: Dosari katika mradi wa ujenzi wa vituo vya daladala

Katika kuhakikisha utoaji wa huduma bora kwa jamii, Baraza la Mji Wete wameanzisha mradi wa ujenzi wa vituo sita (6) vya kusubiria daladala (Bus Shed) katika maeneo mbali mbali ya Wilaya ya Wete.

Katika mradi huo Baraza la Mji Wete limeingia mkataba wenye kumbu kumbu namba SMZ/D11/W/Q/2022-23/19 na KHC Company Limited kwa thamani ya shilingi 29,700,000 kwa ajili ya ujenzi wa vituo sita (6) vya kusubiria daladala (bus shed) ambavyo vimejengwa maeneo ya Amani road, Mchangamdogo, Madenjani, Maziwani road, Mzambarau Karim na Mtambwe Kidundo road.

Dosari zilizojitokeza ni kama zifuatazo:

- Kukosekana kwa barua ya kumpata (kumuomba) mkandarasi kuja kufanya kazi ya ujenzi.
- Kukosekana kwa ushindani wa bei kwa Wakandarasi tofauti (Three quotation).
- Kutopelekwa Rasimu ya mkataba kwa Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) ili kupatiwa ushauri wa kitaalamu.
- Kwa mujibu wa kifungu nambari 1 cha Masharti Maalum ya Mkataba (SCC 1) kinaeleza kwamba kipindi cha uangalizi wa kazi (defect liability period) ni siku 360 ambapo mkandarasi atamaliziwa 3% ya malipo lakini malipo yote yamefanyika ndani ya miezi minne (malipo ya kwanza yamefanyika 28/10/2022 na ya mwisho yamefanyika tarehe 10/01/2023).
- Kwa mujibu wa muhtasari wa tarehe 16/09/2022 wa kikao cha mapatano (Negotiation Meeting Minutes) unaeleza kua malipo yatafanyika sehemu tatu ambapo 50% baada ya kusaini mkataba, 45% baada ya kumaliza kazi na 3% baada ya kipindi cha uangalizi wa kazi (defect liability period). Ukaguzi umebaini kwamba malipo yamefanyika mara mbili tu ambapo malipo ya awali ni 50% na malipo ya mwisho ni 50%.

Majibu ya Uongozi wa Baraza la Mji Wete

Mheshimiwa Mwenyekiti katika kipindi cha ukaguzi wa mradi wa vituo vya daladala timu ya ukaguzi ilishindwa kubaini uwepo wa barua ya kumualika mkandarasi (Invitation Letter). Kwa kuzingatia mpangilio wa nyaraka ya zabuni barua hiyo huwa inakaa mwanzo wa nyaraka ya zabuni na wala haikuwa sehemu katika nyaraka zinazohitajika kwenye mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti jumla ya wakandarasi watatu ambao ni Alghassan Company Limited, KHC Company Limited na Micheweni Engineering and Contractors Partneship walialikwa katika mchakato wa zabuni ya mradi wa ujenzi wa vituo vya daladala kupitia "Invitation Letter". Mpaka kufikia

ukomo wa muda wa kupokelewa kwa zabuni hizo ni mkandarasi mmoja tu KHC Company LIMITED ambae aliwasilisha zabuni yake na wakandarasi wawili hawakuwasilisha zabuni zao. Kwa mnasaba huo Bodi ya Zabuni ilikubaliana kuendelea na zabuni hiyo kwa sababu kusitisha mchakato na kuanza upya kunaweza kuiletea hasara Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti wakati wa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa vituo vya daladala ilikuwa hakuna muongozo wa kupeleka rasimu ya mkataba kwa wakala wa majengo (ZBA). Muongozo huo ulifika ofisini mnamo tarehe 03/10/2023 kwa barua yenye kumbukumbu namba WN/OR/TMSMIM.SMZ/P/M.10/9/VOL.111/15 na kupokelewa tarehe 04/10/2023 wakati mradi wa ujenzi ulitekelezwa Septemba 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti ni kweli kwamba malipo yaliyofanywa katika mradi wa ujenzi wa vituo vya daladala yalikuwa ni tofauti na kifungu cha kwanza cha masharti ya mkataba (SCC 1) pamoja za kikao cha majadiliano. Jambo hili limefanyika kimakosa ingawa katika kipindi cha (defect liability period) hakukutokea dosari yoyote katika mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti ni kweli malipo yalifanyika kwa awamu mbili badala ya awamu tatu jambo ambalo limefanyika kimakosa.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia ukweli wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kwamba baadhi ya Watendaji wa Baraza la Mji Wete walishindwa kutekeleza majukumu yao kutokana na kutofuata Sheria, miongozo pamoja na mkataba wa Ujenzi wa Vituo vya Daladala. Hili limethibitishwa kwa kufanya malipo ya gharama za ujenzi kwa awamu mbili kinyume na Mkataba (awamu tatu) pamoja na kuvunja masharti maalum ya mkataba kwa kufanya malipo yote ya asilimia tatu (3%) ya kipindi cha uangalizi wa kazi (defect liability period) ndani ya miezi minne badala ya siku 360.

Kutokana na uzembe uliofanyika, Kamati ya PAC haikuridhishwa na majibu ya utekelezaji wa hoja hii na kusisitiza kwamba Baraza la Mji Wete litekeleze majukumu yake kwa kuzingatia matakwa ya sheria, miongozo na masharti yaliyoelezwa katika mikataba yao.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Baraza la Mji Wete lihakikishe linapotekeleza kazi zake hususan Miradi yake ya Maendeleo linafuata Sheria, kanuni, miongozo pamoja na masharti yaliyomo katika mikataba yao ili kuepusha kubeba dhima iwapo kutajitokeza changamoto.

BARAZA LA MANISPAA CHAKE CHAKE - PEMBA.

Hoja nambari 6.3.9.1: Kutokuwiana kwa fedha za bajeti zilizorikodiwa baina ya mipango kazi na ripoti ya utekelezaji Shilingi 65,064,069

Katika ukaguzi uliofanyika kupitia taarifa za utekelezaji zilizoandaliwa na Baraza la Manispaa Chake Chake zimebainisha uwepo wa tofauti wa taarifa za fedha zilizoainishwa na kuwasilishwa baina ya mpango kazi wa Baraza na ripoti ya utekelezaji.

Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya shilingi 100,000,000 zilibainishwa katika taarifa ya mpango kazi na shilingi 165,064,609 zilibainishwa katika ripoti ya utekelezaji kwa lengo la ukamilishaji wa Mradi wa ujenzi wa maduka 20 katika soko la Chake Chake. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuwiana kwa taarifa za fedha za bajeti zilizorikodiwa na kuonesha uwepo wa tofauti ya shilingi 65,064,609.

Kutokana na tofauti iliyobainika hapo juu ukaguzi umepata shaka juu ya uhalisia wa taarifa mbili hizo jambo ambalo linaweza kupelekea kwa kiashiria cha ukiukwaji wa taratibu za ufungaji wa hesabu kukosa kuakisi viwango vya uhasibu kitaifa na kimatifa hatimae taarifa za hesabu kutokuonyesha sura halisi na sahihi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Chake Chake Pemba kuhakikisha kwamba kunakuwa na uwiano wa taarifa za fedha zinazotayarishwa na kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Majibu ya Uongozi wa Baraza

Baraza la Manispaa Chake Chake lilianzisha mradi wa ujenzi wa maduka 20 katika mwaka wa fedha 2021/2022 hatua za malipo yalifanyika kwa mikataba miwili kwa awamu tofauti, fedha iliyobaki ililipwa katika mwaka 2022/2023 hivyo kutofautiana kwa fedha kati ya mpango kazi na ripoti ya utekelezaji kumetokana na makadirio yaliyokadiriwa kulingana na makusanyo ya mapato, hivyo uhalisia wa utekelezaji kutokuwiana na taarifa za fedha za bajeti zilizokadiriwa katika mpango kazi na kuonyesha uwepo wa tofauti wa shilingi 65,064,069, kikawaida makisio ya bajeti huwa hayaendani na uhalisia wa bajeti.

Ni kweli kwamba ukaguzi wa fedha kwa mwaka 2022/23, ulibaini kuongezeka matumizi ya Tzs. 165,064,069 ambapo kwa mujibu wa mpango kazi wa bajeti ujenzi wa milango 20 soko la matunda Chake Chake ilipangwa kutumika Tzs. 100,000,000. Hii inatokana na bakaa ya shilingi 195,916,353 ambayo ilipitiwa na mwaka (2020/2021) na kufanya nyongeza katika mwaka uliofuata 2022/2023 na kupelekea fedha hizo kufanyiwa maamuzi katika kikao cha Baraza la Madiwa cha tarehe 9/10/2021 ili ziweze kutumika kwa ajili ya miradi tofauti ukiwemo mradi wa maduka 20 katika soko la matunda

chake chake. Na katika mradi wa maduka 20 wajumbe waliamua kutenga jumla ya shilingi 65,064,069 ili kuengezea katika ujenzi huo na fedha nyengine zitumike kutekeleza miradi mengine, kwa bahati mbaya Baraza la Manispaa Chake Chake baada ya maamuzi ya Kikao cha Madiwani lilighafilika kufanya marekebisho ya mpango kazi ili kuendana na maamuzi ya Kikao na hatimae lilianza utekelezaji wa mradi huo moja kwa moja.

Uchunguzi wa Kamati PAC

Pamoja na kukiri kwa Baraza la Manispaa Chake Chake kuwepo kwa kasoro hiyo ya kutokuiwiyana kwa taarifa za fedha za bajeti baina ya Mpango Kazi na Ripoti ya Utekelezaji. Kamati ya PAC imebaini kasoro hii imetokana na kutokufanyika kwa mapitio ya mpango kazi kwa mwaka husika ambao maamuzi hayo yalitokana na Baraza la Madiwani juu ya utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Maduka Ishirini katika Soko la Matunda Chake Chake.

Kamati ilipata fursa ya kupitia baadhi ya vielelezo vikiwemo Muhtasari wa Kikao cha Baraza la Madiwani kilichojadili Taarifa ya Mapato na Matumizi cha tarehe 09/10/2021 na kupelekea kamati kuiondoa hoja.

Hoja nambari 6.3.9.2: Kukosekana kwa mkataba wa ununuzi wa mafuta shilingi 69,050,540

Kwa mujibu wa kifungu nambari 42(2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kwamba “Taasisi ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma itapanga mpango wake wa ununuzi na uondoshaji kwa kutumia vigezo vinavyokubalika na hususan utazingatia kutumia mfumo wa mikataba maalumu kwa namna inavyohitajika kutoa huduma bora, zenye gharama nafuu na kwa njia inayoweza kubadilika kwa bidhaa zinazohitajika kila mara au zinzojirudia kila baada ya muda.

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 69,050,540 zimelipwa na Baraza la Manispaa Chake Chake kwa kituo cha mafuta cha Chake Petrol Station kwa ajili ya ununuzi wa mafuta bila ya kuwepo kwa mkataba. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kutokupa huduma iliyo bora nay a uhakika pamoja na uwezekano wa kutokea kwa ununuzi holela wa mafuta. Aidha, ni kwenda kinyume na kifungu nambari 42(2)(b) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016,

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza kuhakikisha wanafunga mikataba kwa ununuzi wa bidhaa zote wanazotumia kila mara au zinazojirudia kila baada ya muda kama Sheria inavyooelekeza. Mchanganuo wa mafuta yaliyonunuliwa bila kufungiana mkataba na mtoa huduma ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 41: Malipo yasiyokuwa na mkataba wa ununuzi wa mafuta

Hati Namba	Hundi Namba	Kiasi Kilicholipwa (Tsh)	Alielipwa	Maelezo
30/07 27/7/2022		5,907,220		
48/08 26/08/2022		5,907,220		
01/10 27/10/2022		5,907,220		
13/11 02/11/2022		5,907,220		
36/12 22/12/2022	IT	5,907,220		Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Ununuzi wa mafuta kwa matumizi ya kazi za Baraza
39/01 24/01/2023		5,907,220		
26/02 07/02/2023		5,907,220	Chake Petrol Station	
54/03		9,000,000		

28/03/2023				
05/14 **13/04/2023**		**9,000,000**		
45/05 **24/05/2023**		**5,000,000**		
06/06 **13/06/2023**		**4,100,000**		
		69,050,540		

Majibu ya Uongozi wa Baraza

Ni kweli kwamba katika ukaguzi wa mwaka 2022/2023, kulibainika ununuzi wa mafuta wa Tzs. 69,050,540 yaliyonunuliwa bila ya

kwa kuwepo mkataba wa ununuzi wa mafuta hayo, kwasababu manunuzi yote yanayofanywa na Serikali kwa njia moja au nyengine kama Local Purchase Order (LPO) ambapo tayari huo ni mkataba, kilichobainika ni kukosekana kwa mkataba wa utumizi wa mafuta baina ya Ofisi ya Baraza la Manispaa Chake Chake na Chake Petrol Station, kutokana na hali hiyo Baraza la Manispaa Chake Chake Pemba limechukua juhudi za makusudi kuandaa mkataba wa matumizi kwa ajili ya matumizi ya bidhaa hii ili kuepukana na changamoto zilizojitokeza awali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia utekelezaji wa majibu ya hoja hii, Kamati ya PAC imeridhika na juhudi zilizochukuliwa na Uongozi wa Baraza la Manispaa ya Chake Chake za kufunga Mkataba Mpya baina yao na Msambazaji Chake Petrol Station wa tarehe 01/7/2022 hadi 30/6/2025 na kupelekea Kamati kuiondoa hoja hii.

Hoja nambari 6.3.9.3: kukosekana kwa usawa wa taarifa za Mapato yaliokusanywa Baina ya Mfumo wa MUTM na Taarifa Nyengine za Mapato shilingi 22,247,000

Kanuni ya 105(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inamtaka Afisa Mhasibu wa taasisi ya Umma kufanya usuluhishi wa kibenki kila mwezi au wakati wowote kama itakavyoelekezwa na miongozo kutoka Hazina au toleo lolote ambalo litatolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali.

Baada ya kupitia taarifa mbali mbali za mapato ukaguzi umebaini kwamba taarifa za mapato za Baraza la Manispaa Chake Chake zinatofautiana, Utofauti wa mapato yaliyokusanywa unadhihirisha kwamba baadhi ya mapato yanaweza kuwa yanakusanywa nje ya mfumo na hivyo kushindwa kuonekana kwenye taarifa zinazotoka kwenye mfumo. Tofauti hizi pia zinapelekea taarifa za mapato zinazoandaliwa kutoaminika na hesabu za mwisho wa mwaka za Baraza zinazoandaliwa kwa kutumia taarifa hizo huweza zisiwe sahihi. Taarifa za mapato tulizozipitia ni pamoja na taarifa za mfumo wa ukusanyaji mapato (MUTM), taarifa za benki (Bank Statement), taarifa za mapato ya kila mwezi pamoja na daftari la kukusanyia mapato ya kila siku (Daily Analysis Book). Utofauti uliobainika kwa kiasi kikubwa ulitokana na kutokufanyiwa kwa usuluhishi baina ya taarifa kama ilivyoelekezwa katika kanuni.

Kutowiana kwa taarifa za makusanyo ya mapato ya mwaka kunapelekea kutokupatikana kwa uhalisia wa mapato yaliokusanywa katika Baraza.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Chake Chake kuhakikisha kwamba taarifa zinazohusiana na fedha za mapato zinakuwa sahihi ili kuwezesha wadau wa taarifa hizo kuwa na Imani nazo. Mchanganuo wa utofauti wa taarifa hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 42: Tofauti ya taarifa za Mapato baina ya Mfumo wa MUTM na Taarifa nyengine za Mapato

Namba	**Taarifa zenye utofauti**	**Tofauti (Tshs)**
1.	Taarifa ya Mfumo wa Ukusanyaji Mapato (MUTM) na Daftari la kukusanyia mapato ya kila siku. (587,803,420 – 592,817,920)	5,014,500
2.	Taarifa ya Mfumo wa Ukusanyaji Mapato (MUTM) na Taarifa za Benki (Bank Statement). (587,803,420 – 596, 419, 420)	8,616,000
3.	Taarifa ya Mfumo wa Ukusanyaji Mapato (MUTM) na Taarifa za kila mwezi za mapato. (587,803,420 – 596, 419, 920)	8,616,500
	Jumla ya tofauti iliyobainika	**22,247,000**

Majibu ya Uongozi wa Baraza

Ni kweli kwamba kulikuwa na tofauti kati ya mfumo wa MUTM na taarifa nyengine za mapato kwa mfano taarifa za benk (bank statement) na MUTM, jambo lilisababishwa na baadhi ya wateja wetu kulipa fedha bila ya kutumia Control number. Hata hivyo, hatukuweza kufanya upatanisho kwenye mfumo wa MUTM kwasababu ya mfumo wenyewe kutokubali kufanya upatanisho wa fedha (Bank reconciliation statement).

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC baada ya kupitia majibu ya hoja hii, imegundua kwamba licha ya kuanzinshwa kwa mfumo mpya wa ulipaji wa malipo wa ZAN MUTM na Ofsi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa Mabaraza yote ya Manispaa za Unguja na Pemba, lakini bado mfumo huo una changamoto nyingi ambazo Kamati imezibaini zikiwemo-:

- Mfumo kutokubali kufanya upatanisho wa fedha (Bank Reconciliation Statement).
- Mfumo kutokuwa na kodi yenye kuonesha mapato ya kila chanzo (Blok Manangement System).
- Maafisa Mapato kutokuwa na uwelewa juu ya matumizi wa mfumo huo.
- Mfumo huo kukosa wataalam wa kuusimamia uendeshaji wake.

Kutokana na changamoto hizo Kamati ya PAC haikuridhishwa na hatua za utekeleza na kuibakisha hoja hii kwa ufuatiliaji zaidi.

JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU)

Hoja namba 7.1.2.1: Kutokuwepo kwa mpango maalumu wa mafunzo

Kanuni ya 74(1)ya Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 inazitaka "Taasisi zote za Serikali kuandaa Mpango Maalum wa Mafunzo pamoja na kuteng fedha kwa ajili ya mafunzo hayo". Aidha, kwa mujibu wa Waraka wenye kumbukumbu namba CAB.40/158/01/54 na CAB.40/158/01/37 kutoka Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora unazitaka Wizara na Taasisi za Umma kufanya maandalizi ya Mpango wa Mafunzo ili kujua mahitaji (Training Needs Assessment)na kuwasilisha Mpango wa Mafunzo.

Ukaguzi umebaini kwamba Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar halikuandaa Mpango Mkuu wa Mafunzo ambao ungesimamia masuala yote yanayohusiana na na mafunzo kwa Watendaji wake na kuwasilisha kwa mujibu wa kanuni na toleo nililolinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar kuhakikisha unaandaa Mpango wa Mafunzo, Mpango wa Tathmini ya mahitaji pamoja na bajeti ya mafunzo ili kuepusha kujitokeza kwa mizozo au malalamiko kwa watumishi wa umma watakaonyimwa nafasi ya kushiriki katika mafunzo.

Majibu ya Uongozi wa JKU

JKU ina mpango wake maalumu kwa ajili ya mafunzo kama ifuatavyo:

a) Mpango wa mafunzo ya vijana wa mujibu wa sheria. Mafunzo haya yanajumuisha mafunzo ya kijeshi, ujasiriamali, uzalendo, michezo, sanaa na utamaduni.
b) Mpango wa mafunzo ya kiaskari unaojumuisha mafunzo ya awali na uongozi wa ngazi tofauti.

Tanbihi: Kwa upande wa mafunzo ya kiaskari, mafunzo haya ni siri kwa sababu yanaambatana na mbinu mbali mbali za kiulinzi na medani za kivita (Kiambatanisho cha mpango wa mafunzo)

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imegundua kuwa majibu ambayo Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar imeyatoa kwa Kamati ya PAC yaliekezwa zaidi kuhusiana na Mpango wa Mafunzo ya Kiaskari jambo ambalo Mkaguzi hakukusudia huko.

Hata hivyo, baada ya Kamati kulieleza Jeshi Mpango uliokusudiwa kuwepo ni ule unaohusu uendelezwaji na upatikanaji wa mafunzo kwa Watumishi wa Jeshi la Kujenga Uchumi, Kamati ilielezwa kwamba Mpango huo upo ambapo kutokana na upatikanaji wao wa fedha, utekelezwaji wake

hufanywa kwa kuwapatia ruhusa wale wote wanaoomba. Kwasasa wanao watumishi ambao wanajiendeleza kimasomo katika kada za uhasibu katika Jiji la Arusha.

Kwa mnasaba huu, hoja hii inaendelea kubakia kwa hatua za utekelezaji.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Jeshi la Kujenga Uchumi lihakikishe linakuwa na Mpango wake halisi wa Mafunzo kwa Watumishi wake, Mpango wa Tathmini ya mahitaji pamoja na bajeti ya mafunzo ili kuepusha malalamiko kwa watumishi watakaokuwa hawakupatiwa nafasi ya kujiendeleza kimafunzo licha ya kuwa na Mpango wao wa Mafunzo ya Kiaskari.

Hoja namba 7.1.2.2: Ucheleweshwaji wa vifaa vya ujenzi

Kwa mujibu wa barua ya tarehe 8 Agosti, 2023 kutoka Idara ya Majenzi na Viwanda JKU Pemba kwenda kwa Mkuu wa Zoni Pemba inaeleza mahitaji ya vifaa vya ujenzi kwa jengo la Afisi ya Wawi Pemba.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Idara ya Ujenzi na VIwanda JKU Pemba inayotekeleza mradi wa ujenzi wa jengo la Afisi Kuu ya JKU Wawi Pemba imesitisha ujenzi wa jengo hilo kutokana na kuchelewa kuletwa vifaa vya ujenzi ambavyo wameviomba ili kukamilisha ujenzi huo kwa wakati.

Aidha, imebainika kwamba Idara ya Ujenzi na Viwanda iliomba kuwasilishiwa vifaa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi mnamo tarehe 08 Agosti, 2023 lakini hadi ukaguzi unakamilika, vifaa hivyo havijawasilishwa jambo ambalo linaweza kupelekea kutokukamilika kwa mradi huo kwa wakati uliopangwa na hatimae kuiingiza hasara Serikali kutokana na mabadiliko ya bei za bidhaa siku hadi siku.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar kuhakikisha linafanya ufuatiliaji wa vifaa hivyo kwa lengo la kuweza kupatikana haraka vifaa ili kutimiza malengo yaliyokusudiwa kwa ufanisi na kwa wakati. Aidha, ni vyema kuzingatia masharti ya mkataba ikiwemo kuangalia uwezekano wa kutoza adhabu ya fidia kulingana na idadi ya siku alizochelewa kwa mujibu wa mkataba husika. Mchanganuo wa vifaa vilivyochelewa kuwasilishwa ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli Nabmari 53: Vifaa vilivyochelewa kuwasilishwa katika eneo la ujenzi

Namba	**Vifaa vya Umeme**	**Kiwango**
1.	Main Switch 3 phase	1 pc 6*12

2.	Waya 40mm	9 Rolls
3.	Taa za ukutani	100
4.	Silling holder	15 pcs
5.	Connector Box	100 pcs
6.	Angle holder	20 pcsw
7.	Intermediate Switch	4 pcs
8.	Engle Server Lamp	35 pcs
9.	Two Gang Two Way	8 pcs
10.	Grout	Box 2
11.	Wall Taiz	Srm 430
12.	Gypsum	100 pkt
13.	Rangi nyeupe	Ndoo 50
14.	Rangi Cream ya mafuta	Ndoo 15
15.	Rangi ya Antifangas ya Cream	Ndoo 12
16.	Rangi nyeusi	Ndoo 4
17.	Rangi ya Cream ya maji	Ndoo 25
18.	PVC	Pipe 4
19.	Sim Tank	5000 ltr
20	PPR Pipe	1
21.	PPR Gate Valve	Valve 1
22.	Flexible Pipe	3 FTS
23	Misumari ya kufungia basen	9 Pcs
24.	Bash	Ps 1

Majibu ya Uongozi wa JKU

Ni kweli mpaka CAG anakagua vifaa vilivyoorodheshwa kwenye kitabu vilikua havijafika kwenye ujenzi. Hata hivyo, vifaa hivi vilishafika katika maeneo ya ujenzi na kutumika ambapo ujenzi wa mahanga na afisi Bambi Kim tayari umeshakamilika na kufunguliwa rasmi katika sherehe za kutimiza miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Vile vile ujenzi wa Afisi JKU Wawi pamoja na ujenzi wa mahanga na Afisi Chambani tayari imekamilika na inatarajiwa kufunguliwa rasmi katika sherehe za kutimiza miaka 61 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ifikapo mwezi Januari, 2025.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Mkaguzi kubaini kwamba kulikuwa na ucheleweshwaji wa vifaa vya ujenzi vinavyohitajika kutumika katika ujenzi wa miradi ya JKUZ. Kamati ilitaka kujua sababu ya kutokea changamoto hiyo, ilielezwa kwamba hali hiyo ilitokana na kutoingizwa fedha za miradi hiyo kwa wakati kutoka Serikalini. Hata hivyo, Kamati imejiridhisha kwamba vifaa hivyo tayari vimeshafika maeneo husika na tayari vimetumika kwa shughuli za ujenzi zilizokusudiwa kutekelezwa. Kamati imejiridhisha hayo baada ya kuangalia baadhi ya miradi hiyo na kupitia vielelezo (Store Ledger) vya upokeaji na utoaji vifaa hivyo vinapoingizwa ghalani.

Kwa vile Kamati imejiridhisha kwamba vifaa hivyo vimeletwa licha ya kuchelewa kwake, uzito wa hoja hii unaondoka na kuamua kuiondosha.

Hoja namba 7.1.2.3: Kukosekana kwa uhalisia katika utayarishwaji wa nyaraka za makisio ya gharama za ujenzi (BOQ) zilizopelekea kuwepo tofauti shilingi 258,747,000

Ukaguzi ulitembelea Mradi wa Afisi Kuu Wawi, Chambani pamoja na Bambi Kim na kubainika uwepo wa mapungufu mbali mbali katika utayarishwaji wa BOQ na mahitaji halisi ya ujenzi huo, jambo ambalo linaweza kuathiri gharama halisi zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. Kuwepo kwa ongezeko la gharama za makadirio ya kazi kutapelekea kuathiri bajeti ya ujenzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi kuhakikisha kuwa unazingatia kwa pamoja nyaraka za makisio ya gharama za ujenzi (BOQ) baina ya Watayarishaji, Idara ya Majengo na Viwanda. Mchanganuo wa gharama zilisababisha tofauti kujitokeza baina ya nyaraka za makisio ya gharama za ujenzi (BOQ) pamoja na gharama halisi zilizotumika ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 54: Kutokuwepo kwa uhalisia katika utayarishwaji wa nyaraka za BOQ

Mahitaji	**Kiwango cha BOQ**	**Kiwango halisi**	**tofauti**	**Thamani (Tzs.)**	**Tofauti (Tzs.)**
Congrete Blocks Grade A 6	6,200	13,000	6,800	3,000	20,400,000
Aggregate Trip	65	89	24	750,000	18,000,000
Reinforcement of Yield:					
16mm diameter	32	33	1	2,900,000	2,900,000
12mm diameter	22	24	2	2,900,000	5,800,000
8mm diameter	4	5	1	3,000,000	3,000,000
Binding wire	6	58	52	100,000	5,2000,000
Gypsum Powder	280	300	20	40,000	800,000
Saw	2	6	4	5,000	20,000
Safety Helment	90	100	10	20,000	200,000
Wooden Float	4	34	30	30,000	900,000
Sprit level Small size	25	26	1	20,000	20,000
Cane machine with all Accessories:					
2*8*20	4,250	8,000	3,750	25,000	93,750,000
2*2*20	3,250	6103	2,853	17,000	48,501,000
1*10*18 ficial board	350	1,150	800	50,000	40,000,000

Roof Sheet nails of 5’	100	400	300	7,000	2,100,000
Roof Sheet nails of 4’	100	450	350	7,000	2,450,000
Roof Sheet nails of 3’	75	325	250	7,000	1,750,000
Roof Sheet nails of 2.5’	25	75	50	7,000	350,000
Concrete nails 4”	10	250	240	6,500	1,560,000
Congrete nails 3”	5	454	449	6,5000	2,918,500
2G1W Switch	-	15	15	20,000	300,000
Box Screw	2	50	48	9,500	456,000
Conduit Pipe 20mm (Oman)	40	1,050	1,010	4,000	4,040,000
PPR pipe (UK)	2	25	23	25,000	575,000
Wall Puty	-	4	4		-
4mm wire	-	6	6	1,300,000	7,800,000
Connector Bar	-	30	30	24,000	720,000
Marine Board	-	550	550	100,000	55,000,000
Props	-	1,000	1,000	15,000	15,000,000
Vishoka	-	20	20	35,000	700,000
Nyundo	-	10	10	18,000	180,000

Kopla	-	2	2	86,000	172,000
Reflactor	-	60	60	15,000	900,000
Disc	-	2	2	15,000	30,000
Cut out	-	3	3	42,000	126,000
Single Switch Socket	-	10	10	10,000	100,000
Nondo 10mm	-	30	30	40,000	1,200,000
2*6	-	4,400	4,400	40,000	176,000,000
Union Box	-	4	4	36,000	144,000
Nipple Socket	-	27	27	25,000	675,000
Jumla					**258,747,000**

Majibu ya Uongozi wa JKU

Ni kweli hali hii ilijitokeza. Uongozi wa JKU ulichukua hatua ya kukaa na wataalamu wake wa majengo kwa lengo la kuyafanyia kazi mapungufu haya ili yasije yakajitokeza tena. Hata hivyo, JKU ilizibeba gharama zote za ujenzi kupitia faida ya miradi mbali mbali inayotekeleza kwa lengo la kukamilisha ujenzi kwa wakati.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imegundua kwamba wakati Mkaguzi anafika JKU kutekelezaji majukumu yake ni kweli alibaini nyaraka za makisio ya gharama za ujenzi (BOQ) ziliyokuwa zikitumika zilikuwa na kasoro hususan za kutokuwemo kwa baadhi ya vifaa vya kutekelezea shughuli za ujenzi. Hali hiyo ilichangiwa na kutokufanyika kwa upembuzi yakinifu kwa Miradi yao ya Bambi Kim, Chambani na Wawi jambo ambalo lingepelekea kutambua makisio au vifaa husika kwa mujibu wa mahitaji yao.

Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba makisio yote ya vifaa vilivyoorodheshwa na Mkaguzi tayari vimeshanunulia na kutumika kwa ujenzi wa Miradi hiyo.

Maagizo ya Kamati ya PAC

JKU ihakikishe inafanya upembuzi yakinifu kabla ya kuanza utekelezaji wa Miradi yake ya Maendeleo.

Hoja namba 7.1.2.4: Dosari zilizobainika katika ujenzi wa majengo ya Afisi na Mahanga ya Askari

Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar linatekeleza miradi mbali mbali ya ujenzi ikiwemo ujenzi wa majengo ya Ofisi pamoja na ujenzi wa Mahanga ya Askari Unguja na Pemba. Katika uteelezaji wa miradi hiyo, ukaguzi ulitembelea maeneo mbali mbali ya utekelezaji na kubaini uwepo wa dosari zifuatazo:

a. Kutozingatiwa kwa huduma za uzimaji moto na usalama katika majengo yanayojengwa na JKU

Ukaguzi ulitembelea maeneo ya ujenzi wa Mahanga na Ofisi za Jeshi la KUjenga Uchumi Zanzibar na kujionea ujenzi unaoendelea kufanyika ambapo ukaguzi umebaini kwamba JKUZ haikuzingatia huduma za uzimaji wa moto na usalama kwa watumiaji wa majengo hayo. Majengo hayo ni kama yafuatayo:

i. Jengo moja la Ofisi na Mahanga mawili ya Wanafunzi Bambi Kim Unguja.
ii. Jengo la Ofisi ya Zoni ya JKU Wawi Pemba.
iii. Jengo moja la Ofisi na Mahanga mawili ya Wanafunzi Chambani Pemba.

Majibu ya Uongozi wa JKU

Ni kweli katika ujenzi huu JKU haikuzingatia huduma za uzimaji wa moto na usalama. Hata hivyo baada ya kubainika mapungufu haya JKU kwa kushirikiana na Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar imeanza mchakato wa kufanya makisio ya vifaa hivyo na kuviagiza ili vifungwe na hali ya usalama ipatikane kama ilivyoshauriwa. Aidha, kwa upande wa zabuni za majengo mengine yanayojengwa na JKU kwa sasa suala la uwekaji wa huduma za uzimaji wa moto na usalama limezingatiwa.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya PAC imebaini bado Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar halijakamilisha mchakato wa kuweka vifaa vya kuduma ya uzimaji moto na usalama kwani Jeshi hilo lipo katika hatua ya kufanya makisio ya vifaa hivyo. Kwa mnasaba huo, hoja hii inabakia kwa hatua za ufuatiliaji na ukamilishaji wa uwekaji wa vifaa vya kuzimia moto na usalama katika majengo ambayo wameyajenga kwa gharama kubwa.

Hoja hii inabakia hadi JKU watakapokamilisha urekebishaji wa kasoro ya kuweka huduma za uzimaji moto na usalama na Kamati kujiridhisha.

Maagizo ya Kamati ya PAC

JKU lihakikishe linaweka vifaa vya kuzimia moto na usalama katika majengo yake yote matatu ya Ofisi na Mahanga mawili ya Wanafunzi Bambi Kim Unguja, Jengo la Ofisi ya Zoni ya JKU Wawi Pemba pamoja na Jengo moja la Ofisi na Mahanga mawili ya Wanafunzi Chambani Pemba.

a. Kuanza kuharibika kwa dari za majengo

Mnamo tarehe 28 Novemba, 2023. Ukaguzi ulitembelea miradi ya ujenzi wa Mahanga ya Wanafunzi pamoja na Afisi ya Kambi ya JKU Bambi na kubaini kuwepo kwa dosari katika dari za majengo ambazo zimeshaanza kuharibika kabla ya majengo kutumika.

Kitendo cha kuaza kuharibika kwa dari kabla ya mradi kukamilika na kukabidhiwa kinatia ishara ya utekelezaji wa mradi uliofanywa chini ya kiwango kubalifu jambo ambalo huenda likapelekea kuchakaa kwa majengo kwa haraka, kuendelea kuvuja na kuharibika kwa vifaa na samani, kutapelekea kutumika kwa gharama ya ziada ya kufanya ukarabati kwa muda mfupi jambo ambalo ni kuisababishia hasara Serikali ya kufanya matumizi nje ya bajeti.

Majibu ya Uongozi wa JKU

Hali hii imetokana na kukosekana kwa miundombinu ya mifereji ya bati (gutter) kutowekwa awali kwenye majengo imesababisha ‘Gypsum Boards’ kuchukuwa unyevu pamoja na maji yanayosababisha kuvimba kwa ‘Gypsum Boards’ na hatimae kuanguka. Hatua zilizoanza kuchukuliwa na JKU ni:

i) Miundombinu ya gutter imeanza kufungwa kwenye majengo yote kuepusha kiwango cha unyevu na maji yanayotoka kwenye bati yasiharibu.
ii) Kutokana na eneo la bambi kuwa ni eneo lenye baridi kali, hivyo JKU imeona ni vyema mfumo wa ‘PVC boards’ uanze kutumika kwani hata kama ‘Gypsum Boards’ zitafungwa nyengine hali ya uharibifu inaweza kujirejea. Mfumo huu utaanza kuwekwa kuanzia robo hii ya pili ya mwaka wa fedha 2024/2025.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC baada ya kuchambua majibu ya hoja hii imebaini kwamba wakati Mkaguzi anafanya ukaguzi katika Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar ni kweli kulikuwa na changamoto ya kuanza kuharibika kwa baadhi ya dari za Majengo ya Jeshi hilo. Hali hiyo ilisababishwa na kutokuwekwa kwa mikingo ya maji mvua (gutter). Hata hivyo, tayari Jeshi hilo limeanza mchakato wa kurekebisha hali hiyo ili isiweze kujitokeza kwa mara nyengine. Hoja hii inabakia hadi JKU watakapokamilisha urekebishaji wa kasoro hii na Kamati kujiridhisha.

Maagizo ya Kamati ya PAC

JKU iongeze juhudi katika kuyafanyia marekebisho majengo yote yaliyopata athari ya kuharibika kwa 'Gypsum Boards' zilizowekwa awali ili liweze kuyafanya majengo hayo kuishi kwa muda mrefu.

b. Uwekaji usioridhisha wa viluva

Katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Mahanga ya Askari pamoja na majengo ya Ofisi ya Kambi ya Bambi Kim, ukaguzi ulijionea utekelezaji huo ukiwa upo katika uwekaji wa Viluva (Interlock Paving Block) katika eneo la nje ya majengo hayo.

Dosari iliyobainika ni utekelezaji usioridhisha wa upangaji wa viluva ambavyo baadhi yake kuonekana kufanya shimo na vyengine kutokupangika vizuri na kupelekea kujitokeza kwa tatizo la kutuwama kwa maji, kufanyika kwa mabonde na miinuko na vyengine kubainika vikiwa vimeota majani na kutokuonesha taswira nzuri ya utekelezaji wa mradi huo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa JKUZ kuongeza umakini wa usimamizi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo kufanya usimamizi wa kila hatua ili kuepusha kujitokeza kwa kitendo cha kufanya ukarabati kabla ya kukabidhiwa kwa miradi ya Serikali.

Majibu ya Uongozi wa JKU

Hali hii imesababishwa na kuwepo kwa ushindiliaji mdogo (compaction of hard core) kwa baadhi ya maeneo kwa upande wa kifusi kilichowekwa chini ya interlocks jambo lililochangia kwa kiasi kikubwa kufanyika kwa mbonyeo huo kutokana na kupita kwa gari zenye ujazo mkubwa. Hatua zilizoanza kuchukuliwa ni kuanza kuzitoa interlocks zilizobonyea sambamba na zoezi la uwekaji wa kifusi kigumu kwa maeneo yaliyoathirika ili kuongeza uimara.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kutafuta ukweli wa hoja hii, Kamati ya PAC imegundua kuwa ni kweli wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake ya ukaguzi katika Jeshi la JKU, kulikuwa na kasoro ya uwekaji usioridhisha wa viluva katika eneo la nje la ujenzi wa Mahanga ya Askari pamoja na majengo ya Ofisi ya Kambi ya Bambi Kim. Hata hivyo, JKU bado wapo katika hatua ya utoaji wa 'interlock' hizo na uwekaji wa kifusi katika maeneo hayo. Kamati imeendelea kuibakisha hoja hoja hii kwa hatua za utekelezaji zaidi na Kamati itakapolitembelea eneo husika kujiridhisha.

Maagizo ya Kamati ya PAC

JKU ihakikishe inakuwa makini katika utekelezaji wa miradi yake ya maendeleo kwa kuviondoa viluva vyote vilivyobonyea na kuweka kifusi vizuri ili kuiwezesha miradi hiyo iweze kudumu kwa muda mrefu.

Hoja namba 7.1.2.5: Malipo ambayo hayakufuata taratibu za manunuzi shilingi 144,966,683

Kwa mujibu wa Kanuni ya 57(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2020, inaeleza kwamba Taasisi ya Ununuzi haitoruhusiwa kuvunjavunja matumizi (Split Contract) kwa lengo kukwepa uitishaji wa Zabuni.

Ukaguzi umebaini kwamba JKUZ imefanya matumizi ya shilingi 144,966,683 kwa utaratibu wa kuvunjavunja kwa mtoa huduma Green Land General Supply Company kinyume na kanuni iliyonakiliwa hapo juu.

Kufanya ununuzi kwa njia ya kuvunjavunja kunapelekea kuikosesha Serikali mapato yatonayo na malipo ya Wazabuni wanaoingia mikataba ya kazi au usambazaji wa vifaa au huduma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa JKUZ kuweka msisitizo katika usimamizi wa ununuzi unaofanyika kwa lengo la kuzingatia matakwa ya sheria ya Ununuzi ili kuepuka athri inayoweza kujitokeza kutokana na kushindwa kusimamia matakwa ya Sheria hiyo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika Jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 55: Malipo ambayo hayakufuata utaratibu wa manunuzi

Tarehe ya malipo	**aliyelipwa**	**Kiasi (Tzs.)**
20/7/2022	Green Land General Supply Company	2,847,762
22/7/2022		40,497,056
30/7/2022		46,715,732.08
19/7/2022		13,436,088
5/10/2022		4,660,764.72
12/10/2022		9,164,201.04
19/1/2023		151,725,50
6/2/2023		735,000
10/2/2023		24,019,607.86

9/3/2023		2,638,746,14
Jumla		**144,966,683.34**

Majibu ya Uongozi wa JKU

Ni kweli hali hii ilijitokeza kutokana na ugeni wa taratibu za kimanunuzi kulikosababishwa na watendaji wetu ambao hawakua na uzoefu wa kutosha hali iliyopelekea kuvunja vunja matumizi ili kuepuka mikwamo hali ambayo haikuwa sahihi kisheria. JKU imechukua hatua za kuajiri na kusomesha Maafisa husika wa manunuzi kwa lengo la kufuata taratibu zote na kuepukana na ukiukwaji wa taratibu za kimanunuzi. Aidha, kwasasa JKU baada ya kukiimarisha kitengo cha manunuzi inafanya matumizi yake kwa kufuata taratibu zote za kimanunuzi na pale inapobidi kukwama, watendaji wa kitengo cha manunuzi huchukua hatua ya kwenda Afisi za manunuzi Mazizini kwa lengo la kuuliza na kupata ufumbuzi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Jeshi la Kujenga Uchumi kukiri juu ya kuwepo kwa kasoro ya kuvunjavunja kwa matumizi (Split Contract) wakati wa kupatiwa huduma kutoka kwa Mtoa Huduma 'Green Land General Supply Company' kinyume na kanuni ya 57(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2020. Kamati imebaini kwamba JKU haikuwa na Watendaji wenye ueledi katika utekelezaji wa masuala ya manunuzi jambo lililosababishwa na kutokuwepo Mpango mzuri wa matumizi Rasilimali Watu kwa vile Watendaji waliokuwa wataalamu na wazoefu hawakuwepo Ofisini katika kipindi husika. Kamati inasisitiza kwamba kutokujua taratibu sio sababu ya kuiachia Taasisi kutekeleza majukumu yake kinyume na utaratibu.

Kamati ya PAC, baada ya kufuatilia na kugundua kwamba Maafisa Manunuzi wamesharejea kazini na kwamba wanauzoefu wa kutosha kutekeleza masuala ya manunuzi kwa mujibu wa taratibu. Kamati inaendelea inaibakisha hoja hii kwa hatua za ufuatiliaji hadi Mkaguzi atakapojiridhishwa katika ukaguzi unaofuata.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Kamati inaliagiza Jeshi la Kujenga Uchumi kuhakikisha linatekeleza majukumu yake kwa umjibu wa SHeria na Kanuni za Manunuzi ili kupeuka hoja za ukaguzi.
2. JKU itumie njia mbadala katika utekelezaji wa majukumu yake kwa kuazima Watumishi katika Idara Maalum nyengine iwapo itatokea ukosefu wa wataalamu na wazoefu ndani ya Jeshi ili utekelezaji huo ufanyike kwa mujibu wa Sheria.

JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU) - PEMBA

Hoja namba 7.1.2.6: Uwepo wa mashine ambazo hazitumiki zenye thamani ya shilingi 44,918,400

Kifungu cha 61(2) cha Sheria ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma, Namba 6 ya 2021 kinawataka Maafisa Masuuli kuhakikisha kwamba mali za umma zinatumika kwa tija na manufaa kulingana na jukumu litakalotekelezwa.

Ukaguzi umebaini kwamba Jeshi la Kujenga Uchumi Zoni ya Pemba limefanya malipo ya shilingi 44,918,400 kwa ajili ya ununuzi wa mashine ya kufyatulia matofal iliyogharimu shilingi 25,500,000 pamoja na mashine ya kufanyia mikate ya bekari kwa shilingi 19,418,400 kwa ajili ya kuanza kazi. Hadi ukaguzi unakamilika mashine hizo bado hazijafanyiwa kazi kama ilivyokusudiwa jambo ambalo limepelekea kutokupatrikana kwa tija iliyokusudiwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi Pemba kuhakikisha unatenga fedha za kutosha katika bajeti ili kuiendeleza miradi inayoibuliwa na kuweza kuleta tija iliyokusudiwa.

Majibu ya Uongozi wa JKU

Ni kweli mpaka kipindi ambacho CAG anakagua mashine zenye thamani ya TZS 44,918,400 zilizonunuliwa zikiwemo mashine ya kufyatulia matofali na mashine ya kufanyia mikate zilikua bado hazijatumuika kwasababu zifuatazo:

Mosi, mashine ya kufyatulia matofali ilihitaji umeme wa three phase ili iweze kufanya kazi kitu ambacho mpaka CAG anakagua JKU ilikua kwenye hatua za kufuatilia kupata huduma hii Shirika la umeme. Aidha, mara tu baada ya kupatikana umeme wa three phase mashine hii imeanza kufanya kazi kwa lengo la JKU kujiongezea kipato pamoja na kuwapa mafunzo ya ujasiriamali Vijana wanojenga Taifa waliopo katika Kambi ya JKU Msaani.

Pili, mpaka CAG anakagua ni kweli mashine ya kutengenezea mikate ilikua bado haijatumika kwa sababu ya kukosekana mashine nyengine ndogo ndogo zilizokua zinanunuliwa kulingana na upatikanaji wa fedha kutoka serikalini. Hadi tunaleta taarifa hii kwako, mashine hii ina zaidi ya mwaka mmoja imeanza kufanya kazi na kwa zoni hii ya Pemba JKU hainunuwi mikate kutoka bekari za nje kitu kinachoihakikishia JKU na Taifa kwa ujumla usalama wa askari na vijana wa mujibu wa sharia

JKU ipo tayari baada ya kikao hiki ikupeleke wewe na kamati yako katika kambi yake ya JKU - Msaani ukajionee kwa jinsi gani mashine hizi zinavyofanya kazi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufanya uchunguzi wa hoja hii, Kamati ya PAC ilibaini mambo yafuatayo:

1. Ni kweli wakati ukaguzi unatembea katika Jeshi la Kukenga Uchumi Pemba, mashine za kutengenezea mikate na mashine za kufyatulia matofali zilizokuwa hazijafungwa na kuanza kufanya kazi. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba mashine hizo zimeshafungwa na kutumika kwa kutengenezea mikate na matofali.
2. Mradi huo uliamuliwa na kuandaliwa bila ya kuwa na 'concept note' itakayitumika kama dira katika utekelezaji wake. Hali hiyo ingelilisaidia Jeshi kujua mahitaji yepi yanatakiwa yaanze mwanzo na yepi yatafanywa mwisho na kuepuka kununua mashine kwanza bila ya kuandaa mazingira ya ufanyaji kazi zake.
3. Mradi ilikuwa inatumia fedha zinazotoka Serikali (OC) badala ya kutumiwa fedha za miradi ya maendeleo na kusababisha kusuasusa katika utekelezaji wake.

Licha ya kujitokeza kasoro ya uwepo wa mashine ambazo hazitumiki zenye thamani ya shilingi 44,918,400 ambayo Mkaguzi alizibaini wakati wa utekelezaji wa majukumu yake, kwasasa kasoro hiyo imesharekebishwa na tija kupitia mashine hizo inapatikana. Kwa mnasaba huo Kamati imeiondoa hoja hii.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Jeshi la Kujenga uchumi lihakikishe linaandaa 'concept note' kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi yake ya maendeleo.
2. JKUZ itumie fedha zake za miradi ya maendeleo katika utekelezaji wa miradi yake ili fedha za matumizi mengineyo ziweze kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Hoja nambari 7.1.2.7: Nyaraka za gari za JKU kuonesha umiliki wa watu binafsi

Kwa mujibu wa kifungu cha 64(1) cha Sheria Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma, Namba 6 ya 2021kinaeleza kwamba "Taasisi ya Umma itahifadhi nyaraka zilizothibitishwa kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali".

Ukaguzi umebaini kuwa Jeshi la Kujenga Uchumi Pemba linamiliki gari aina mbali mbali lakini baadhi ya gari hizo nyaraka zake zinaonesha kuwa na umiliki wa watu binafsi katika nambari za usajili badala ya Jeshi hilo. Nyaraka za gari kuonesha zinamilikiwa na watu binafsi kunaweza kusababisha mgogoro baina ya Jeshi na wananchi na pia kunaweza kupelekea matumizi mabaya ya gari hizo. Hali hii inaweza kuwa imetokana na ununuzi wa gari zilizokuwa zishatumika au kutokubadilisha ununuzi baada ya kununununua.

Nyaraka za gari kuonesha umiliki wa watu binafsi ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokitaja hapo juu. Ushauri unaushauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi Zoni ya Pemba kuhakikisha kwamba gari zake zote wanazipatia nyaraka zinazoonesha zinamilikiwa na Jeshi ikiwa ni pamoja na kushirikiana na Wakala wa Usajili wa Mali na Biashara kwa lengo la kufuatilia utaratibu mzima wa upatikanaji wa nyaraka hizo.

Mchanganuo wa gari ambazo nyaraka zake zinaonesha kumilikiwa na watu binafsia ni kama unavyoonesha katika Jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 56: Gari za JKU zinazoonesha kumilikiwa na watu binafsi

Namba	**Aina ya Gari**	**Jina la Umiliki**	**Namba ya Usajili**	**Namba inayotumika**
1	PRADO S/WAGON	Rashid Moh'd Soud	Z912FY	JKU 140
2	SUZUKI ESCUDO	Kombo Ali Hamdu	Z164JA	JKU 143
3	MAZDA	Ali Azizi Ali	Z387GJ	JKU 141
4	COASTER BUS	Mariam Shaaban Chavala	Z593 KA	JKU 150
5	CARRY SUZUKI	Taarifa za Umiliki zimekosekana	Z971 JG	Namba haikupatikana

Majibu ya Uongozi wa JKU

Ni ukweli usiopingika mpaka CAG anaikagua JKU gari hizi zilikua na umiliki wa watu binafsi kama ilivyoelezwa kwenye hoja ya msingi. Hali hii ilisababishwa na ucheleweshwaji wa ununuzi wa magari kutoka Wizara ya Fedha kufuatia agizo la Serikali kuu. Hivyo, kwa kukidhi mahitaji ya wakati huo wa uchaguzi wa mwaka 2020, JKU ililazimika kununua magari haya na kuyatumia. Aidha, kwasasa JKU tayari imeshakamilisha mchakato wa kubadilisha umiliki wa kadi za gari kutoka kwa watu binafsi na kumilikiwa na JKU (Kiambatanisho cha nyaraka za kuomba umiliki wa kadi za gari za JKU).

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya ukaguzi kubaini kuwa nyaraka za baadhi ya gari za Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar zilikuwa zikionesha umiliki wake unamilikiwa na watu binafsi badala ya Jeshi lenyewe. Hata hivyo, wakati Kamati yetu inafanya uchunguzi wake juu ya hoja hii ilibaini kuwa mnamo tarehe 4 Novemba, 2024 gari zote hizo zilikuwa tayari zimeshabadilishwa umiliki wake kama inavyojionesha hapa chini:

Na.	**Aina ya Gari**	**Jina la Umiliki**	**Namba ya Usajili**
1.	PRADO S/WAGON	Jeshi la Kujenga Uchumi	SMZ1238A
2.	SUZUKI ESCUDO	Jeshi la Kujenga Uchumi	SMZ1239A
3.	MAZDA	Jeshi la Kujenga Uchumi	SMZ1260A
4.	COASTER BUS	Jeshi la Kujenga Uchumi	SMZ743B
5.	CARRY SUZUKI	Jeshi la Kujenga Uchumi	SMZ744B

Aidha, Kamati imejiridhisha kwamba taarifa kamili za umiliki wa mali hizo zimeshaingizwa katika Daftari la Mali za Kudumu za Jeshi (Fexed Asset Register). Kutokana na hoja hiyo kufanyiwa kazi ipasavyo, Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi na kuamua kuiondoa hoja hiyo.

Hoja nambari 7.1.2.8: Kufanya matumizi ya fedha za makusanyo ya mapato kinyume na utaratibu shilingi 190.151,180.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Jeshi la Kujenga Uchumi Zoni ya Pemba kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilimekusanya jumla ya shilingi 190,151,180 kutokana na vyanzo vyake mbali mbali vya mapato.

Dosari iliyobainika ni kutokuwepo kwa makadirio ya mapato pamoja na kutoingizwa kwa mapato hayo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali jambo ambalo limepelekea Jeshi hilo kufanya matumizi ya mapato hayo bila ya kuwa na kibali kutoka Baraza la Mapinduzi.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa matumizi yasiyoridhisha ya fedha za Serikali, aidha ni kwenda kinyume na Kanuni ya 39(1) ya kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi Pemba kufuata taratibu, miongozo na sheria zilizowekwa ili kupata uhalali wa kutumia fedha wanazokusanya. Mchanganuo wa makusanyo na matumizi hayo ni kama unavyoonekana katika Jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 57: Makusanyo ya mapato yaliyotumika kinyume na taratibu

Namba	**Muda wa Makusanyo**	**Kiasi cha Fedha kilichokusanywa na Kutumika (Tzs.)**
1.	Julai, 2022	700,000
2.	Agosti, 2022	12,482,692
3.	Septemba, 2022	19,560,586
4.	Oktoba, 2022	15,645,362
5.	Novemba, 2022	20,405,950
6.	Disemba, 2022	5,200,000
7.	Januari, 2022	11,247,084
8.	Februari, 2022	52,286,932
9.	Machi, 2022	13,571,792
10.	April, 2022	22,991,952
11.	Mei, 2022	5,467,938
12.	Juni, 2022	10,590,892
Jumla		**190,151,180**

Majibu ya Uongozi wa JKU

Jeshi la Kujenga Uchumi lina vyanzo vyake vya ndani vinavyotumika kuwasilisha au kuchangia fedha katika Mfuko Mkuu wa Serikali kila mwaka wa fedha kama ifuatavyo:-

a. Mapato ya kodi za maduka
b. Mapato ya Karafuu
c. Mapato ya Mpunga
d. Mapato ya mazao ya Bustani
e. Mazao ya Baharani
f. Mapato ya kazi ya Useremala
g. Ada ya Mafunzo/Wanafunzi
h. Mapato ya mifugo

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 JKU imevuka lengo la makusanyo kutokana na sababu ya ustawi mzuri wa mazao ya uzalishaji. Lifuatalo ni

jeduweli linaloonyesha makadirio na makusanyo pamoja na asilimia ya makusanyo kwa kila fungu. Fedha hizi zimekusanywa na kambi za JKU Unguja na Pemba na kuwasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

Mpango wa Ukusanyaji Mapato ya JKU kwa Mwaka 2022/2023

Gfs code	**Chanzo cha mapato**	**Makadirio ya mapato kwa 2022/2023**	**Makusanyo halisi 2022/2023**	**Asilimia ya makusanyo kwa mwaka**
1415004	Kodi ya Maduka	8,386,000	10,657,000	127.0
1415010	Karafuu	10,000,000	10,000,000	100.00
1421004	Mapato ya Mpunga	10,000,000	10,000,000	100.00
1421006	Mapato ya mazao ya Bustani	15,000,000	15,000,000	100.00
1422027	Mazao ya Baharani	5,000,000	5,000,000	100.00
1422052	Mapato ya Viwanda Vidogo vidogo	10,000,000	10,000,000	100.00
1422088	Ada ya Mafunzo/Wanafunzi	35,500,000	45,500,000	128.17
1421011	Mapato ya mifugo	10,000,000	10,000,000	100.00
Jumla		**105,386,000**	**117,657,000**	**112**

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia ukweli wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kwamba licha ya JKU kuwa na vyanzo vyake na makisio yake ya makusanyo ambayo huchangia katika Mfuko Mkuu wa Hazina, lakini bado JKUZ inakuwa na shughuli zake za ndani ambazo huhitaji fedha za kuziendeleza kila siku. Hivyo, kwa vile utekelezaji wa hoja hii unahitaji muda wa ufuatiliaji,

inabakia hadi pale ufumbuzi wake utakapopatikana na Kamati kujiridhisha zaidi juu ya utekelezaji wake.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inalitaka Jeshi la Kujenga Uchumi kwa kushirikiana na Afisi ya Rais, Fedha na Mipango, kufungua akaunti nyengine ya mapato yake ambayo itakua inatumika kwa utekelezaji wa shughuli zao.

CHUO CHA MAFUNZO

Hoja nambari 7.1.3.1: Utambuzi wa mapato kinyume na Muongozo

Kwa mujibu wa maelezo ya taarifa za fedha za hesabu za mwisho wa mwaka Chuo cha Mafunzo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 zimefungwa kwa kuzingatia msingi na muongozo wa uandaaji wa hesabu za kimataifa “IPSAS cash basis”. Aidha baadhi ya Msingi hiyo ni “IPSAS 1” ambayo inatoa muongozo wa ufungaji wa hesabu kwa njia ya “Cash basis” ambayo inaitaka taasisi husika kuripoti taarifa zake za mapato ya mwaka husika.

Muongozo wa Uandaaji wa hesabu (IPSAS Cash Basis) unaelekeza kuwa kumbukumbu za mapato na matumizi yataingizwa kwenye vitabu vya mahesabu wakati malipo halisi yanapopokelewa au kutolewa, ukaguzi umebaini kuwa Chuo cha Mafunzo kinatambua mapato yao baada ya kutoa matumizi (Profit) jambo ambalo ni kwenda kinyume na Muongozo wa ufungaji wa hesabu (IPSAS Cash Basis).

Kufanya hivyo kunapelekea Chuo cha Mafunzo kushindwa kutoa hesabu sahihi ya mapato waliokusanya kwenye vyanzo vyao vya mapato.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha kwamba unaandaa hesabu zake kwa mujibu wa Viwango vya hesabu vinavyoelekeza.

Majibu ya Uongozi wa Chuo cha Mafunzo

Chuo cha Mafunzo katika mwaka wa fedha 2022 /2023 kimetayarisha taarifa za mwisho wa mwaka kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta za Umma (IPSAS) pamoja na muongozo wa ufungaji wa hesabu kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango (ORFM) ambao hutolewa kila mwaka na kuelekeza vitu (items) ambavyo zitatambuliwa kama mapato ambazo zitajumuishwa katika taarifa hizo.

Muongozo wa ufungaji wa hesabu wa mwisho wa mwaka kutoka ORFM umeonesha mapato yanayotakiwa kutambuliwa na kuoneshwa katika taarifa za mwisho wa mwaka ni yale ambayo tunayotakiwa tuyachangie katika Serikali kuu kutokana na faida inayopatikana kutoka miradi mbali mbali inayotekelezwa na Chuo cha Mafunzo, Mapato hayo yatokanayo na kilimo na Ujenzi, ambayo chuo cha Mafunzo kiliyatambua na kuyaingiza katika taarifa za mwisho wa mwaka 2022/2023 kwa mujibu wa muongozo kutoka ORFM,

badala ya kuingiza mapato ghafi kama mdhibiti na mkaguzi wa hesabu za Serikali alivyosema.

Hivyo Chuo cha mafunzo kinaomba kushauri Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kukaa pamoja kukubaliana juu ya muongozo sahihi wa kutumia katika ufungaji wa hesabu. Vile vile katika kulitatua hili Chuo cha Mafunzo kinaomba kutayarisha vitabu viwili vya taarifa za mwisho wa hesabu kwa fedha za kutoka Serikali kuu, na taarifa kutoka miradi yetu mbali mbali ya ndani.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia majibu ya hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016 chini ya kifungu cha 119 kinazitaka Taasisi za Serikali kuandaa taarifa za fedha za hesabu za mwisho wa mwaka zinazohusiana na mapato yake. Hata hivyo, Chuo cha Mafunzo ni Taasisi ya kijeshi ambayo huweka utaratibu wa kuchangia Serikalini fedha zinazotokana na Miradi yake inayoitekeleza ambapo baadhi ya kiasi cha fedha hutumika kugharamia utekelezwaji wa Miradi hiyo.

Kamati imegundua kuwa ili Chuo cha Mafunzo kiweze kujiepusha na hoja za Mkaguzi Chuo kinalazimika kufungua hesabu nyengine itakayoshughulika na mapato yanayorokana na Miradi yao. Kwa msingi huu, hoja hii inabakia kwa hatua za utekelezaji.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inautaka Uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha unaandaa hesabu zake kwa mujibu wa Viwango vya hesabu vinavyoelekeza kujumuishwa kwa mambo yote yanayohusiana na mapato ya Chuo.

Chuo cha Mafunzo kihakikishe kinaadaa hesabu inayojitegemea ya Miradi yao ya Maendeleo pekee ili kuepusha hoja za Ukaguzi kujitokeza.

Hoja nambari 7.1.3.2: Utumiaji usioridhisha wa rasilimali za Chuo cha Mafunzo

Ukaguzi umepitia taarifa mbali mbali za Chuo zikiwemo taarifa za kibajeti kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Chuo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo mapato yote ya Chuo yalikadiriwa kuwa ni shilingi 125,690,855.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 Chuo kilikusanya jumla ya shilingi 102,251,500 sawa na asilimia 81 ya makadirio kutoka katika vyanzo vyake, vile vile kwa kupitia mpango kazi umeeleza kuwa Chuo kitaweka miundombinu ya umwagiliaji katika makambi na kuipatia idara ya uzalishaji Pembejeo za kilimo na ufugaji na utumiaji mzuri wa ardhi kwa ajili ya kilimo.

Ukaguzi ulitembelea Kambi za Chuo cha Mafunzo zilizopo Ubago, Hanyegwa Mchana, Langoni, Kinumoshi, kiwanda cha Ushoni pamoja na Idara mbali mbali za uzalishaji na kubaini kwamba licha ya kuwa na mipango mizuri Chuo cha Mafunzo bado kumekuwa na ufanisi wa chini wa ukusanyaji wa mapato jambo ambalo linatia shaka kwa ukaguzi kujihakikishia kuwa Chuo cha Mafunzo kinaweza kutekeleza dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba vikosi vya Ulinzi na Usalama vinajitegemea kutokana na shughuli zake za uzalishaji.

Kushindwa kutumia Rasilimali zake vizuri inaweza kupelekea kwa Chuo cha Mafunzo kushindwa kutumia vyema raslimali ya ardhi na watu katika uzalisahaji na hatimae kukosekana kwa mapato.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kufanyia kazi Mapendekezo ya ukaguzi ili kwenda sambamba na dhamira ya Serikali ya awamu ya nane ya kuhakikisha kwamba vikosi vya Ulinzi na Usalama vinajitegemea kutokana na shughuli zake za uzalishaji.

Majibu ya Uongozi wa Chuo cha Mafunzo

Chuo Cha Mafunzo kinajitahidi katika utumiaji wa rasilimali watu na Ardhi katika kuleta maendeleo endelevu. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Chuo Cha Mafunzo kimetumia ipasavyo rasilimali watu na ardhi katika shughuli za kilimo kama ifuatavyo:

- Tumefanikiwa kulima ekari mia mbili (200) za miwa katika kambi ya Langoni na Kinumoshi.
- Tumefanikwa kulima kilimo cha miparara chichi ekari sita 6 katika kambi ya H/Mchana.
- Tumefanikiwa kulima kilimo cha mihogo jumla ya ekari ishirini na tatu 23, kati ya hizo ekari saba 7 langoni, ekari sita 6 tungamaa na ekari kumi 10 Kinumoshi.
- Tumefanikiwa kulima jumla ya ekari kumi na mbili 12 za mahindi, kati ya hizo ekari sita 6 kambi ya langoni, ekari mbili 2 kambi ya Kinumoshi na ekari nne 4 kambi ya H/Mchana.
- Tumefanikiwa kulima ekari ishirini na moja 21 ya kilimo cha mpunga, kati ya hizo ekari nane 8 kambi ya langoni, ekari mbili2 kambi ya Kinumoshi, ekari sita 6 kambi ya tungamaa na ekari tano 5 kengeja.
- Tumefanikiwa kupanda mikarafuu ekari 10 katika kambi ya langoni na Kinumoshi.
- Vilevile Chuo Cha Mafunzo kinaendelea na kilimo cha mbogamboga katika kambi zake mbali mbali za Unguja na Pemba

Pia Chuo Cha Mafunzo kinaendelea kusomesha Wapigana watano 5 katika fani ya kilimo na ufungaji katika vyuo tofauti ndani na nje ya nchi sambamba na hilo Chuo Cha Mafunzo kimeajiri wataalamu watuta katika fani ya kilimo na ufungaji kwa ajili ya kuhakikisha rasilimali watu na ardhi

tunatumia ipasavyo. Mabadiliko ya tabia ya nchi yamepelekea kuathiri shughuli za kilimo katika Chuo Cha mafunzo kama ifuatavyo;-

- Tumefanikiwa kuvuna ekari 117 za miwa kati ya ekari 200 tulizo lima
- Tumefanikiwa kuvuna ekari 15 za mihogo kati ya ekari 23
- Tumefanikiwa kuvuna ekari tano za mahindi kati ya ekari 12
- Tumefanikiwa kuvuna ekari 11 za mpunga kati ya ekari 21.

Kutokana na changamoto ziliopo hapo juu zimepelekea Chuo Cha Mafunzo kutofikia 100% ya makadirio ya uchagiaji wa mapato Serekalini. Ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi Chuo Cha Mafunzo kimechimba visima katika kambi zake mbambali za Unguja na Pemba.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imegundua kuwa ni kweli Chuo cha Mafunzo kimeandaa Mpango mzuri utekelezaji wa shughuli zake za uzalishaji Pembejeo za kilimo na ufugaji na utumiaji mzuri wa ardhi kwa ajili ya kilimo. Hata hivyo, Kamati imejaribu kupima Mpango uliopo kwa kulinganisha na utekelezaji wake na imebaini kuwa Chuo cha Mafunzo kimefanikiwa kwa asilimia kubwa kuutekeleza kivitendo Mpango huo kwa kulima ekari mia mbili (200) za miwa, ekari sita za Miparara chichi pamoja na ekari ishirini na tatu 23 za Mihogo.

Sambamba na hilo, Chuo kimechukua juhudi za kuyavuna ipasavyo mavuno waliyolima na kupelekea kuongeza mapato yao. Licha ya mafanikio hayo, bado Chuo hakijafikia uwezo wa kujitosheleza kimahitaji na kutegemea baadhi ya fedha zitoke Serikalini. Hata hivyo, Kamati imeridhika na majibu ya Chuo na kuiondosha hoja hii na kusisitiza juhudi zaidi zichukuliwe ili kujinasua na utegemezi.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inautaka Uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuchukua juhudi za makusudi katika kupango mipango mizuri itakayowawezesha kufikia lengo la kujitegemea kikamilifu hususan katika masuala ya uzalishaji.

Hoja nambari 7.1.3.3: Dosari zilizobainika katika zabuni nambari SMS/DO4/G/RNCB/2022/2023/02 ya Ununuzi wa Chakula cha Askari na Wanafunzi

Kanuni ya 125 (1)(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2021 inaeleza kuwa kutakuwa na makadirio ya thamani ambayo ni misingi ya kazi za ununuzi; na zabuni yoyote iliyotathiminiwa na iko juu au chini ya makadirio ya thamani ya manunuzi, kadiri itakavyokuwa, haitaidhinishwa isipokuwa ikiwa inakidhi masharti kama ilivyoainishwa katika miongozo iliyotolewa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji Zanzibar.

Aidha, kifungu cha 43(2) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza “ununuzi au uondoshaji wa mali za umma utaanzishwa au kuendelea baada ya kuthibitishwa kwamba fedha zote kwa kiwango kamili na kwa muda wote zitakuwepo wakati wa kuingia mkataba”.

Chuo cha Mafunzo kilitangaza zabuni ya ununuzi wa Chakula cha Askari na Wanafunzi kwa njia ya ushindani usio wa wazi ikiwa na makadirio ya shilingi 1,440,000,000. Nyaraka za Wazabuni Watatu zilifunguliwa tarehe 13 Septemba 2022 na kufanyiwa tathmini. Tarehe 23 Novemba 2022, Chuo cha Mafunzo kilisaini mkataba na Mkangas General Supplies wa pendekezo la ununzi na usambazaji wa Chakula cha Askari na Wanafunzi kwa jumla ya shilingi 2,625,439,045 kuwa ndie Mzabuni aliyekuwa na kiwango cha chini. Hii imepelekea kuwepo kwa ongezeko la shilingi 1,185,439,045 sawa na asilimia 82.32 ukilinganisha na makadirio ya awali. Kwa mujibu wa taratibu za manunuzi Zabuni hiyo haikupaswa kuidhinishwa na ilitakiwa kutangazwa upya ili kupata bei shindani.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha kwamba, unafanya tathmini ya kina pale wanapoamua kufanya makadirio ya hesabu kwa mahitajio ya ununuzi mbali mbali ili kupata hesabu sahihi.

Majibu ya Uongozi wa Chuo cha Mafunzo

Chuo cha Mafunzo kilianzisha utaratibu wa ununuzi wa chakula cha Askari na Wanafunzi baada ya kuthibitisha kuwa fedha zote kwa kiwango kamili na kwa muda wote zitakuwepo baada ya kuingia mkataba na Mkangas General Supplies kwa ajili ya usambazaji wa chakula chenye jumla ya TZS 1,440,000,000 kama kifungu namba 43(2) cha sheria ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma (2016) kinavyoelekeza.

Kutokana na changamoto zilizojitokeza mwanzoni mwa mwezi wa Novemba 2022, la ongezeko la kesi za uzalilishaji na madawa ya kulevya ilipelekea ongezeko la wanafunzi na mahabusu na ilikua tayari tumeshaweka bajeti ya chakula, Msambazaji wa mwanzo RM2 Food Stuff ikiwa Mkataba wake wa mwanzo na Nyongeza (Extension) yote imeisha na uharaka wa upatikanaji wa chakula cha kuwalisha wanafunzi na mahabusu, Chuo ili kuweza kufidia ongezeko hilo iliona ni vyema kuongeza kiwango kwa kila chakula, Zabuni ilirudishwa katika bodi ya Zabuni kwa ajili ya kuidhinishwa taratibu za kuongezeka kwa bajeti ya TZS 2,625,439,045, kwa kuwa chakula hicho kilihitajika kwa wakati, tungeifuta zabuni hii na kuitangaza upya, ingepelekea kuchukua muda mrefu hadi kukamilika kwake, hivyo ingepelekea kuathirika kwa wanafunzi na mahabusu.

Kwa kukabiliana la tatizo hili Chuo cha Mafunzo kuanzia mwaka wa fedha 2024-2025 baada ya mkataba wa msambazaji wa chakula kuisha, tutakuwa tunaandaa mkataba wa mfumo (Framework Contract) ambao utaonesha

kiwango cha chakula na bei yake bila kuathiri kiwango cha fedha kilichobajitiwa awali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC katika kulichunguza kwa undani suala hili, imebaini kuwa ni kweli kulikuwa na ongezeko la matumizi ya kutoka shilingi 1,440,000,000 na kufikia shilingi 2,625,439,045 ambapo ni sawa na zaidi ya asilimia 100. Hata hivyo, kutokana na uwepo wa dharura ya kuongezeka kwa Wanafunzi na Mahabusu katika Vyuo hivyo kumelazimika kutumika fedha zaidi kwa kwa lengo jema la kuhami maisha ya Ndugu zetu waliokuwa wakisubiri kuhukumiwa au kumaliza muda wao wa kutumikia katika Vyuo hivyo.

Kutokana na dharura iliyojitokeza na unyeti wa suala la ununuzi wa vyakula kwa Taasisi za Kijeshi, Uongozi wa Chuo cha Mafunzo ulitakiwa kuomba kibali cha matumizi ya fedha hizo kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali ili kupata idhini ya matumizi ya fedha hizo hasa ukizingatia sababu ya kuwasilisha maombi hayo ilikuwepo. Kwa mnasaba huu, Kamati imeamua kuicha hoja hii kwa hatua za ufuatiliaji ili kusijitokeze kasoro kama hizo baadae.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inautaka Uongozi wa Chuo cha Mafunzo iwapo kutatokezea dharura yenye sababu za msingi za kufanya matumizi ya dharura ufuate taratibu za matumizi ya fedha za Serikali ikiwemo kuomba ridhaa ya matumizi ya fedha nje kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Hoja nambari 7.1.3.4: Dosari zilizobainika katika zabuni nambari SMS/DO3/G/RNCB/2022/2023/03 ya Ununuzi wa Mafuta

Kanuni ya 125 (1)(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya 2021 inaeleza kuwa kutakuwa na makadirio ya thamani ambayo ni misingi ya kazi za ununuzi, na zabuni yoyote iliyotathiminiwa na iko juu au chini ya makadirio ya thamani ya manunuzi, kadiri itakavyokuwa, haitaidhinishwa isipokuwa ikiwa inakidhi masharti kama ilivyoainishwa katika miongozo iliyotolewa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji Zanzibar.

Aidha, kifungu cha 43(2) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza “ununuzi au uondoshaji wa mali za umma utaanzishwa au kuendelea baada ya kuthibitishwa kwamba fedha zote kwa kiwango kamili na kwa muda wote zitakuwepo wakati wa kuingia mkataba”.

Chuo cha Mafunzo kilipanga kupitia mpango wake wa Manunuzi kuwepo kwa Zabuni nambari SMS/DO3/G/RNCB/2022/2023/03 ya ununuzi wa Mafuta yenye jumla ya shilingi 55,281,473.

Aidha, ukaguzi umepitia taarifa za malipo yaliyofanywa kwa ajili ya ununuzi wa Mafuta na kubaini kuwepo jumla ya shilingi 121,318,500 zimetumika

kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Petrol na jumla ya shilingi 55,281,473 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Diesel kutoka Kijangwani Petrol Station kwa Unguja na Chasasa Service Station Pemba.

Kufanyika kwa matumizi hayo kumepelekea kuwepo kwa ongezeko la jumla ya shillingi 121,318,500 ambapo sawa na asilimia 219.46 ukilinganisha na makadirio ya awali. Kwa mujibu wa taratibu za manunuzi Zabuni hiyo haikupaswa kuidhinishwa na ilitakiwa kutangazwa upya ili kupata bei shindani.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha kwamba, unafanya tathmini ya kina pale wanapoamua kufanya makadirio ya hesabu kwa mahitajio ya ununuzi mbali mbali ili kupata hesabu sahihi.

Majibu ya Uongozi wa Chuo cha Mafunzo

Chuo cha Mafunzo kilianzisha utaratibu wa ununuzi wa mafuta baada ya kuthibitisha kuwa fedha zote kwa kiwango kamili na kwa muda wote zitakuwepo baada ya kuingia mkataba na vituo vya mafuta kwa ajili ya usambazaji wa mafuta jenye jumla ya TZS 121,318,500 kwa mafuta ya Petrol na TZS 55,281,473 kwa mafuta ya Diesel kama kifungu namba 43(2) cha sheria ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umama (2016) kinavyoelekeza.

Aidha kiasi cha TZS. 121,318,500 ambacho kilikuwa haikuanishwa katika mpango wa manunuzi, kilikuwemo katika mpango kazi na bajeti kuu ya Chuo cha mafunzo, hii inaonesha kuwa kiasi hicho kilikuwa katika bajeti na sio ziada, hivyo katika kulifanyia kazi hali hii Chuo cha Mafunzo umehuisha (update) mpango wa manunuzi ili kuendana na mpango kazi na bajeti.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Ni kweli wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake ya kiukaguzi katika Chuo cha Mafunzo alibaini uwepo wa dosari ya kutokuingizwa katika Mpango wa Manunuzi fedha ya ununuzi wa mafuta ya Petroli yenye jumla ya shilingi 121,318,500. Hata hivyo Kamati imefanikiwa kuuona Mkataba wa Ununuzi wa Mafuta pamoja na Mpango wa Manunuzi uliohuishwa na kubaini kuwemo kwa kiasi hicho cha fedha. Kamati ilitaka kujua kwanini Makaguzi hakupatia nyaraka hiyo na kuelezwa uhuishaji huo ulifanyika wakati Mkaguzi ameshamaliza kazi zake. Kwa msingi huu, Kamati imeridhika na majibu ya uongozi wa Chuo cha Mafunzo na kuiondosha hoja hii kwa vile hakukuwa na upotevu wowote wa fedha.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Chuo cha Mafunzo uhakikishe unakuwa makini kwa kufanya uhuishaji wa Mpango wake wa Ununuzi kwa wakati na kumpatia Mkaguzi wakati wa anapofanya kazi zake.

Hoja nambari 7.1.3.5: Mazingira yasiyoridhisha ya Makaazi ya Askari wa Chuo cha Mafunzo

Mnamo tarehe 06 Disemba, 2023 ukaguzi ulifanya ziara ya kutembelea Kambi za Vyuo vya Mafunzo Zoni ya shamba kwa Upande wa Unguja kwa lengo la kuangalia utekelezaji wa mipango na kazi za Chuo cha Mafunzo kilichojipangia kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Aidha,ukaguzi ulibaini kuwepo kwa Mazingira yasiyoridhisha ya Makaazi ya Askari wa Chuo cha Mafunzo katika maeneo ya Makambi ya Chuo cha Mafunzo yaliyokuwepo katika maeneo mbali mbali kwa upande wa Unguja.Kambi hizo ni kama zifuatazo:-

- Kambi ya Chuo cha Mafunzo Hanyengwa Mchana
- Kambi ya Chuo cha Mafunzo Ubago
- Kambi ya Chuo cha Mafunzo Kinu Moshi
- Kambi ya Chuo cha Mafunzo Langoni

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha kwamba, unafanya juhudi za maksudi ili kuinusuru hali hiyo inazikabili nyumba za Maaskari hao kwa ajili ya maakazi yao.

Majibu ya Uongozi wa Chuo cha Mafunzo

Chuo cha Mafunzo kinaelewa umuhimu wa makaazi bora kwa Maafisa na Askari wake ndio maana tukaandaa na kuutekeleza mradi wa ujenzi na uboreshaji wa nyumba za Maafisa na Askari kwa zoni zote na Unguja na Pemba, hadi hivi sasa mradi huu umefanya marekebisho makubwa ya nyumba tatu za ghorofa za Maafisa na Askari zilizoko Makao Makuu ya Chuo cha Mafunzo Kilimani Zanzibar na kwa upande wa Pemba tayari tumesha kamilisha nyumba za kisasa katika kambi zote.

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 mradi huu umetengewa jumla ya TZS 2,550,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba tisa (9) za familia 18 katika kambi ya Hanyegwa Mchana na Hanga lenye vyumba 20 katika kambi ya Bumbwini kwa ajili ya kuweka mazingira mazuri ya Makaazi kwa Maafisa na Askari wa Chuo cha Mafunzo. Mradi huu utakuwa endelevu katika kambi zote za Chuo cha Mafunzo kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa ni kweli kuna kasoro ya kuwepo kwa mazingira yasiyoridhisha kwa ajili ya Wapiganaji wa Chuo cha Mafunzo Unguja na Pemba. Hata hivyo, changamoto hiyo imeanza kurekebishwa ambapo Kamati imeshuhudia uwepo wa Majengo mengi mapya katika Vyuo tofauti vya Mafunzo Unguja na Pemba. Kamati imebahatika kuona majengo hayo mapya katika Makao Makuu ya Chuo hicho.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inautaka uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuendelea na juhudi za kutekeleza miradi ya ujenzi wa nyumba mpya za makaazi ya askari wake ili waweze kufanya kazi katika mazingira mazuri zaidi.

KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU)

Hoja nambari 7.1.5.1: Ukiukwaji wa taratibu za malipo ya posho mbali mbali

Kwa mujibu wa kifungu namba 60 cha Kanuni ya kimeeleza kuwa: Maafisa na askari wa Idara Maalumwatapaswa kulipwamaposho mbalimbali kama yatakavyokuwa yakipangwa na Tume kipindi baada ya kipindi kwa mujibu wa ujuzi, vyeo na mazingira mengineyo kama yalivyofafanuliwa katika kifungu nambari 60(a-i) cha Kanuni ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum ya 2007.

Ukaguzi umefanya mapitio katika hati za malipo, mfumo wa malipo (payroll), maandalizi na utekelezaji wa bajeti pamoja na kanuni, miongozo na sheria mbali mbali zinazohusiana na ulipwaji wa stahiki kwa watumishi wa Idara Maalum.

Ukaguzi umebaini Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimefanya malipo ya maposho kwa Maafisa na Askari wake mbali mbali ambapo malipo hayo hulipwa kinyume na utaratibu uliowekwa na Tume ya Utumishi Idara Maalum. Katika dosari hiyo ilibainika uwepo wa baadhi ya wapiganaji kulipwa malipo pungufu ya posho la mazingira magumu la asilimia 15 na posho la nyumba la asilimia 10 ambapo thamani ya fedha inayolipwa hailingani na asilimia ya fedha iliyotakiwa kulipwa kwa mujibu wa miongozo na kanuni za Tume ya Utumishi ya Idara Maalum ya 2007.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kufanya mapitio mapya ya stahiki za wapiganaji wake ili kuweza kufanya maboresho ya bajeti ya stahiki za maafisa na wapiganaji kuendana na uhalisia wa fedha wanayotakiwa kulipwa. Mchanganuo wa posho zinazolipwa kwa baadhi ya wapiganaji hao ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 1:Ukiukwaji wa taratibu za malipo ya Posho mbali mbali

Namba ya Uajiri	Posho linalostahiki kulipwa kulingana na mshahara kwa mwezi (Tsh.) (A)	Posho linalolipwa (Tsh.) (B)	Tofauti ya Posho (Tsh.) (A-B)
POSHO LA MAZINGIRA MAGUMU (15% YA MSHAHARA)			
938730	162,150	75,000	87,150

738689	175,500	75,000	100,500
738801	162,150	75,000	87,150
139103	139,700	75,000	64,700
138707	212,550	75,000	137,550
Jumla Ndogo (X)	**852,050**	**375,000**	**477,050**
Namba ya Uajiri	**Posho linalostahiki kulipwa kulingana na mshahara kwa mwezi (Tsh.) (C)**	**Posho linalolipwa (Tsh.) (D)**	**Tofauti ya Posho (Tsh.) (C-D)**
POSHO LA NYUMBA (10 % YA MSHAHARA)			
938730	108,100	10,000	98,100
738689	175,500	20,000	155,500
738801	108,100	10,000	98,100
139103	139,700	20,000	119,700
138707	141,700	20,000	121,700
Jumla Ndogo (Y)	**673,100**	**80,000**	**593,100**
Jumla Kuu (X+Y)	**1,525,150**	**455,000**	**1,070,150**

Majibu ya Uongozi wa KZU

Kikosi kinalipa posho kwa maafisa na askari wake kutokana na miongozo iliyotolewa na Ofisi ya Raisi Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora. Barua yenye Kumbukumbu Na. CCB.90/446/0/4 ya tarehe 17/03/2022 kutoka Utumishi wa Umma inafafanua. na imeambatanishwa.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia majibu ya hoja hii, Kamati ya PAC imebaini mambo yafuatayo:

1. Hakukuwepo ukiukwaji wa muongozo wa ulipaji wa posho la mazingira magumu kwa Watendaji wa Idara Maalum za SMZ. Hali hiyo imetokana na kuwepo kwa barua yenye Kumbukumbu nam. CCB.90/446/0/4 ya tarehe 17/03/2022 ambayo imeelekeza viwango sahihi vinavyotakiwa kulipwa kwa Watumishi hao.
2. Kuwepo ukiukwaji wa utaratibu katika ulipwaji wa posho la nyumba kwa Maaskari wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ambapo muongozo wa ulipaji posho hilo umeelekeza kwamba kila Askari akatwe asilimia 10 ya mshahara wake bila kujali cheo. Hata hivyo, Kamati imegundua utaratibu unaotumika unafanywa kwa kuzingatia cheo cha Askari na sio asilimia ya mshahara. Ili kuthibitisha hilo, Kamati ilihitaji kupatiwa vielelezo vya malipo yaliyofanyika kwa kuzingatia vyeo lakini hadi Kamati inakamilisha kazi zake vielelezo hivyo havijawasilishwa.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kikozi cha Zimamoto na Uokozi uhakikishe unafanya malipo ya posho hususan posho la nyumba kwa kuzingatia miongozo inayotolewa na Serikali.

Hoja nambari 7.1.5.2: Kutokuandaliwa kwa Sera za Kikosi cha Zimamoto na Uokozi

Kifungu cha 6 (1) na (2) cha Sheria namba 9 ya mwaka 1999 ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimezitaja kazi za Kamishna wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ikiwa ni pamoja na Uandaaji wa Sera za Kikosi zinazohusiana na masuala ya Viwango, Mafunzo, Uongozi na mambo mengine yanayohusiana na utendaji wa shughuli za kikosi cha Zimamoto na Uokozi.

Timu ya ukaguzi ilifanya mahojiano na Maofisa na Askari wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi juu ya uwaandaji wa sera hizo na matumizi yake na kubaini Kikosi hakikuandaa Sera ambazo zingetumika katika ufanyaji wa kazi za kikosi za kila siku kinyume na matakwa ya sheria tajwa hapo juu, hali ambayo imepelekea kutokufanyika kwa baadhi ya shughuli za Kikosi kwa ufanisi na uweledi.

Kazi za Kikosi cha Zimamoto na Uokozi zinategemea kuwepo kwa sheria, kanuni, miongozo na sera mbali mbali ambazo zitakwenda kurahisisha shughuli za ufanyaji wa kazi za Kikosi hivyo basi kutokuwepo kwa baadhi ya sera na miongozo kunaweza kupelekea baadhi ya kazi za Kikosi kutokufanyika kwa ufanisi na uweledi.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kuchukua jitihada za haraka za ufanikishaji wa uandaaji wa sera na miongozo ya Kikosi ili kuweza kufanya kazi katika viwango vinavyohitaji.

Majibu ya Uongozi wa KZU

Ni kweli Kikosi hadi sasa hakina sera yake mwenyewe kutokana na taratibu za Kitaifa na Kimataifa, sera inayotumika kwa kukabiliana na majanga ya

moto ni Sera ya Maafa, Aidha Kikosi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kimetenga bajeti yake kwa ajili ya uandaji wa Sera, sheria na kanuni.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kuchunguza hoja hii, Kamati ya PAC imegundua yafuatayo:

1. Kifungu cha 6(1) na (2) cha Sheria Nambari 9 ya mwaka 1999 imeeleza kwamba Kamishna wa Zimamoto na Uokozi aandae Sera ya Kikosi inayohusiana na masuala ya viwango, mafunzo na uongozi. Hata hivyo, Kikosi hakijaandaa Sera hiyo badala yake inatumia Sera ya Taifa ya Majanga. Hali hiyo imepelekea Kikosi kutekeleza majukumu yake kinyume na Sheria na ndio msingi wa hoja ya Mkaguzi.
2. Kamati pia imebaini kuwa tayari Kikosi kimeshatenga jumla ya shilingi milioni 20,600,000 katika bajeti yake ya mwaka 2024/2025. Kamati ilitaka kujua kwamba kiutaratibu Sera ya Taasisi ikitaka kuundwa ni lazima iendane na Sera Kuu ya Taifa ambayo kwa Zanzibar husimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kikosi tayari kimefanya mazungumzo na Ofisi hiyo ili kupatiwa maelekezo juu ya uwezekano wa kuwa na Sera yake.
3. Kikosi kifuatilie Afisi ya Mwanasheria Mkuu juu ya uhalali wa kuwa na uwezo au mamlaka ya kuandaa Sera ya Uokozi wakati Sera ya Taifa ya Maafa ipo na wanaendelea kuitumia.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kihakikishe kinachukua juhudi za makusudi kufuatilia kwa karibu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Afisi ya Mwanasheria Mkuu juu ya mamlaka ya uandaaji wa Sera yao ili waweze kuondoa utata uliopo.
2. Iwapo Kikosi kitakuwa hakina mamlaka ya kuandaa Sera yao, wahakikishe wanafuata taratibu zote za uhauilishaji wa fedha zilizopangwa kwa ajili ya uandaaji wa Sera ya kikosi.

Hoja nambari 7.1.5.3: Kukosekana kwa uhalisia wa Makadirio ya Matumizi na utekelezaji wake wa shilingi 2,197,000,298

Katika kupitia nyaraka mbalimbali, ikiwemo ripoti ya utekelezaji wa mpango kazi wa Kikosi wa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2023 na kubaini kuwepo fedha zilizoingizwa kwa shughuli makhususi ambazo zimepindukia fedha za makadirio ambazo zilipangwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali ziliomo kwenye mpango kazi wao.

Aidha, ukaguzi umebaini kuwepo kwa ongezeko la shilingi2,197,000,298 ambalo limetokana na kuingizwa kwa fedha kinyume na kilichoombwa kwenyeshughuli makhususi zilizoainishwa katika Kikosi hicho. Hata hivyo ukaguzi umeshindwa kupata maelezo ya kina kuhusiana na kuwepo kwa ongezeko hilo.

Kutokana na tofauti ya kima kikubwa cha fedha kilichobainika ukaguzi umefanya tathmini ya kina baada ya kuwasilisha hoja hii kwa uongozi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi na kutokupatiwa majibu toshelevu, hivyo dosari hii huwenda ilisababishwa na kukosekana kwa umakini wa utekelezaji wa miongozo ya bajeti pamoja na uhalisia wa kinachofanyika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kuongeza umakini katika upangaji wa Mpango Kazi ili uweze kuendana na uhalisia wa taarifa za utekelezaji wake. Jadweli lifuatalo linaonyesha ongezeko la fedha hizo:

Jadweli Nambari 2:Tofauti iliyobainika baina ya fedha halisi na makisio

Idara husika	Huduma/shughuli	Kupitia mpango kazi	Kupitia ripoti ya utekelezaji	Tofauti
Utawala na Fedha	S.1.1: Kutoa huduma za uokozi na uzimajimoto kwa wakati	388,400,000	523,690,947	135,290,947
	S.1.2: Kuwajengea uwelewa wananchi na Taasisi kuhusu tahadhari ya majanga ya moto	10,000,000	243,576,002	233,576,002
	S.1.5: Kuwapatia maafisa na wapiganaji mafunzo ya uzimaji moto na uokozi ndani na nje ya nchi	20,000,000	133,942,004	113,942,004
	S.2.3: Kuziwezesha timu kushiriki katika michezo	70,000,000	208,418,953	138,418,953
	S.2.4: Kuwapatia maafisa na	20,000,000	50,000,000	30,000,000

	wapiganaji posho na likizo			
	S2.2.1: Ujenzi wa vituo vya uokozina uzimaji moto nyumba na mahanga ya kulala Maafisa na Askari.	1,230,000,000	2,792,772,392	1,562,772,392
Jumla		**1,755,400,000**	**3,952,400,298**	**2,197,000,298**

Majibu ya Uongozi wa KZU

Kikosi kimeweza kupitia mpango kazi na Mpango wa Utekelezaji wake na kubaini kuwa hakuna tofauti ya fedha zilizopindukia, fedha za makisio kama ilivyoonyeswa na mdhibiti. Ripoti ya Utekelezaji na Mpango kazi imeambatanishwa. Vile vile Ushauri uliotolewa na mdhibiti tumeupokea.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa ni kweli wakati wa ukaguzi kulikuwa na tofauti ya makadirio ya matumizi na Mpango kazi. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba changamoto iliyojitokeza imesharekebishwa kwa kufanya mapitio ya Mpango Kazi wao na kubaini kasoro hiyo. Baada ya kupitia taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka (Financial statement), Kamati ilijiridhisha usahihi wa taarifa hizo. Kwa msingi huo, Kamati ya PAC imeiondoa hoja hii.

Hoja nambari 7.1.5.4: Dosari katika utekelezaji wa Mkataba wa ununuzi wa Vifaa vya Ujenzi TZS 3,480,000,000

Kanuni ya 20(1-2) (f) na 58(1) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma, 2020 inaeleza Kipindi cha mkataba kinachoruhusiwa kitatoa tathmini ya kweli ya wakati ambapo mzabuni anayefaa anaweza kutarajiwa kukamilisha uwasilishaji wa bidhaa, kukamilisha kazi, au kukamilisha kutoa huduma, kwa kuzingatia tarehe inayotarajiwa ya kukamilika na eneo husika.

Ukaguzi ulipitia Mkataba wa ununuzi wa vifaa vya Ujenzi uliongiwa baina KZU na M/S Osaju Company ltd wenye kumbukumbu nambari SMZ/DO5/G/NCB/2021-2022/11 wa tarehe 31/12/2021 kwa thamani ya shilingi 3,480,000,000 pamoja na kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na kubaini kwamba mkataba huo haukuainisha muda wa kukamilisha ununuzi wa vifaa hivyo.

Aidha, katika kupitia hati za malipo ukaguzi ulibaini kuwepo kwa muda mrefu wa uwasilishwaji wa Vifaa vya Ujenzi kwa ajili ya Unguja na Pemba ambapo Mkataba umeendelea kutumika kwa muda wa miaka miwili (2) kutokana na kutokuanishwa kwa muda wa umalizikaji wa Mkataba.

Kuwepo kwa muda mrefu wa uwasilishwaji wa Vifaa vya Ujenzi kwa ajili ya Unguja na Pemba Kunaweza kupelekea kutofikiwa lengo la Serikali kutokana na kutokukamilika kwa wakati shughuli zilizopangwa kufanyika kwa wakati husika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozikuwa makini wakati wa uandaaji na utekelezaji wa mikataba ili kuona shughuli zote zilizopangwa zinakamilika kwa wakati husika kwa mujibu wa Mipango ya Serikali. Aidha, ni vyema Kikosi kuunda timu ya ufuatiliaji wakati wa mchakato wa manunuzi na wakati wa uandaaji na utekelezaji wa Mkataba.

Majibu ya Uongozi wa KZU

Kikosi kiliingia mkataba na kampuni ya Osaju Company Ltd kwa kipindi cha miaka miwili kwa ajili ya Usambazaji wa vifaa vya Ujenzi . makubaliano hayo yalifanyika 31/12/2021. Hii ilitokana naupatikanaji wa Fedha kutoka Serikali kuu. Hata hivyo ushauri uliotolewa na Mdhibiti tunauchukua na kuufanyia kazi kwa lengo la kukuza ufanisi katika utendaji wetu. Mkataba husika umeambatanishwa.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati imebaini kwamba kulikuwa na Mkataba wa ununuzi wa vifaa vya ujenzi baina ya Kikosi cha Zimamoto na M/S Osaju Company Limited wenye jumla ya shilingi bilioni 3,480,000,000 ambao kiuhalisia ulikuwa na muda wa kuanza (tarehe 31/12/2021) lakini haukuwa na muda wa kumalizika kwake. Kamati ilipotaka kujua kuhusiana na ukweli huo ilielezwa kwamba Mkataba huo ulikuwa wa “Framework Contract” ambao huwa unategemea na mahitaji ya aina ya kifaa na kuwasilishwa kwake.

Katika kufuatilia ukweli wa hoja hiyo, Kamati ilitaka ipatiwe barua pamoja na maoni au ushauri kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu ili kuthibitisha kwamba Mkataba huo ulifuata masharti yanayotakiwa kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, Namba 11 ya mwaka 2016. Lakushangaza, hadi Kamati inakamilisha kazi zake, hakuna kielelezo chochote kilichowasilishwa mbele ya Kamati na kupelekea hoja hii kubakia.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kihakikshe kinafuata utaratibu katika uandaaji wa Mikataba yao ili kuepuka matumizi ya fedha yasiyokuwa halali.

Hoja nambari 7.1.5.5: Dosari katika usimamizi wa Miradi ya Maendeleo ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi

Ukaguzi ulipitia Mkataba wa ununuzi na usambazaji wa vifaa vya Ujenzi uliongiwa baina Kikosi cha Zimamoto na Uokozi na M/S Osaju Company Ltd wenye kumbukumbu nambari SMZ/DO5/G/NCB/2021-2022/11 wa tarehe31/12/2021 kwa thamani ya shilingi 3,480,000,000 pamoja na kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Baada ya kufanyika kwa hatua hiyo Ujenzi ulianza rasmi katika maeneo yaliyoainishwa ndani ya Mkataba kama ifuatavyo:-

- Ujenzi wa Hanga la Askari Mahonda
- Ujenzi wa Ofisi za Kanda Kaskazini Unguja Mahonda
- Ujenzi wa Hanga na Nyumba za Askari Finya
- Ujenzi wa Kituo cha Zimamoto na Uokozi Wete

Ukaguzi ulitembelea Miradi hiyo katika maeneo yaliyoainishwa kwa kuangalia hatua za utekelezaji pamoja na hali ya usimamizi wa miradi na kubaini kuwepo kwa dosari zifuatavyo:-

1. Kuta za Majengo hazikujengwa kwa viwango vinavyohitajika

Ukaguzi ulitembelea Mradi wa Hanga na Nyumba za Askari Finya Pemba na kubaini uwepo wa kuta zilizojengwa kwa viwago visivyoridhisha hali inayoweza kupelekea Majengo kutokuwa na ubora kwa matumizi ya baadae.

2. Kutumika kwa Matofali yasiyokuwa na viwango vinavyohitajika

Ukaguzi ulitembelea Mradi wa Hanga na Nyumba za Askari Finya Pemba na kubaini kuwepo kwa matofali ambayo hayakuwa na viwango kwa ajili ya matumizi ya ujenzi huo. Matofali hayo yaliyopokelewa na Kikosi kutoka kwa Mzabuni aliyepewa kazi hiyo. Aidha ukaguzi ulifanya mahojiano na baadhi ya Mafundi na kututhibitishia kuhusu kuyakataa Matofali hayo kutokana na kutokukidhi viwango vinavyohitajika katika aina ya ujenzi iliyopo pamoja na baadhi ya tofali hizo kuwa na dosari mbali mbali.

3. Uwezekaji usioridhisha wa Paa la majengo yaMahanga ya Askari

Ukaguzi ulibaini hali ya kuharibika kwa dari za majengo (Roof) kwa Jengo la Kituo cha Zimamoto na Uokozi Wete na Hanga la Askari Mahonda, hali iliyosababishwa na uwezekaji usioridhisha wa mapaa ya majengo hayo, hali iliyopelekea kuanza kuvuja wakati wa Mvua.

4. Utunzaji wa vifaa vya Ujenzi usioridhisha vikiwa Ghalani

Ukaguzi ulitembelea bohari za Vifaa vya Ujenzi katika maeneo ya Ujenzi na kubaini kuwepo kwa uhifadhi usioridhisha wa Vifaa vya Ujenzi ambavyo vimepokelewa kwa muda mrefu jambo ambalo huwenda likapelekea kuharibika vifaa hivyo kabla ya kuanza kutumika na hatimae

kukisababishia Kikosi kutumia gharama za ziada kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vilivyoharibika na kupelekea kuingiza hasara Serikali na hatimae kupelekea kutokufikiwa kwa lengo lililokusudiwa.

5. Kupitwa kwa muda kwa Bidhaa kutokana na kutotumika kwa muda mrefu

Ukaguzi ulitembelea maeneo ya Kikosi kwa Unguja na Pemba na kubaini kuwepo kwa vifaa vya ujenzi ambavyo vimepitwa na mudawa matumizihali iliyosababishwa na kutotumika kwa wakati kwa vifaa hivyo.

Aidha, ukaguzi ulifanya mahojiano na Maafisa wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Kituo cha Kigunda na kubaini kuwepo kwa ujenzi uliosimama wa Ofisi za KZU ambapo vifaa vya Ujenzi huo ikiwemo ndoo za rangi, gypsum boards, pamoja na vifaa vyenginevyo vikiwa vimemaliza muda wa matumizi kutokana na tarehe zilizobainishwa katika vifunganishio vyake, hii imetokana na kusimama kwa ujenzi wa kituo cha Kigunda Kanda ya Kaskazini Unguja kwa muda mrefu jambo ambalo litapelekea kutumika kwa gharama ya ziada pale ujenzi huo utakapoanza kwa awamu nyengine na kuisababishia hasara Serikali kwa kuibebesha mzigo wa matumizi ya fedha yasiyokuwa na tija.

Kutokana na dosari zilizoainishwa hapo juu ukaguzi umebaini dosari hizo zimesababishwa na uwepo wa vitendo vya uzembe wa kutokuzingatia miongozo na taratibu za ujenzi zinavyoelekeza na hatimae kupelekea upotevu wa fedha za umma kwa kununua vifaa kwa wingi kabla ya mahitaji ya matumizi ya vifaa hivyo na hasa ukizingatia vifaa hivyo vina muda maalum wa matumizi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kuongeza umakini katika usimamizi wa miradi ya maendeleo kwa kufanya matumizi kulingana na upatikanaji wa fedha pamoja na kununua vifaa kulingana na mahitaji wakati wa utekelezaji wa kazi husika ili kuepuka kujitokeza kwa kumalizika muda wa matumizi wa vifaa hivyo kabla ya mahitaji.

Majibu ya Uongozi wa KZU

Naomba ifahamike kuwa Kikosi kinatumia askari wake katika ujengaji wa Majengo yake, kwa upande wa kuta za majengo kikosi kimejitahidi kuona ujenzi wake unajengwa kwa kufuata viwango vinavyostahiki ili kupata Jengo lililoimara na Madhbuti, hata hivyo dosari ndogo ndogo zinarekebishwa wakati wa kumalizia jenga (Finishingi). Kwa upande wa matufali, Kikosi kinatumia matufali ambayo ni mazima na sio mabovu ambayo hayakukizi viwango. Kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti matufali ambayo yapo chini hayakutumika kutoka na kutokizi viwango.

Ni kweli kwamba kuna sehemu moja ya paa letu ilikuwa inapitisha maji kwa kiwango kidogo sana, hii ilitokana na mafundi wetu kutokuwa na utaalamu

wa kuezeka paa la design ya ndani (kulala), hata hivyo kikosi tayari kimesharekebisha kasoro hiyo kwa kushirikiana mafundi kutoka nje ya Kikosi. Vile vile Dosari ya Vifaa kupitwa na muda, hivi ni vifaa vilivyobaki katika mradi wa ujenzi wa Makarakana na sio ujenzi wa mahanga ya KZU ambapo KZU ilipanga kuvitumia kwa ajili ya Kurekebisha vituo vyake, hata hivyo kutokana na ufinyu wa bajeti hakikuweza kukamilisha zoezi hilo kwa wakati.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya majibu yaliyowasilishwa na uongozi wa Kikosi, Kamati imebaini kuwa wakati wa ukaguzi utekelezaji wa ujenzi ulikuwa na changamoto za kuvuja kwa majengo, gypsum kuharibika pamoja na kuwepo kwa rangi zilizopitwa na wakati. Kamati ilitaka kujua kwanini rangi hizo zilikuwa zimeharibika (expired goods) na kuelezwa kwamba bidhaa hiyo ilibakia wakati wa ujenzi wa mradi wao uliopita. Hata hivyo, Kamati ya PAC baada ya mahojiano ya kina ilijiridhisha kwamba kasoro hizo zimerekebishwa na kupelekea hoja hiyo kuondolewa.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kiwe makini katika utekelezaji wa miradi yao ya ujenzi ili kuepuka kasoro kama hizo zisijitokeze tena.

Hoja nambari 7.1.5.6: Upungufu wa vifaa vya kuzimia moto

Katika kutembelea miradi mbalimbali ya maendeleo pamoja na mali za kikosi, ikiwa ni pamoja na zana za kuzimia moto, ukaguzi umebaini kuwa kikosi kina upungufu mkubwa wa vifaa vya kuzimia moto kama vile magari ya kuzimia moto, Bwiza, water relay jambo ambalo linapelekea kikosi kushindwa kutekeleza dhamira yake ya kusogeza huduma karibu kwa jamii na kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi mkubwa.

Magari yaliyopo ni yenye ujazo wa lita 1500 za maji ambapo baada ya muda mfupi gari inashindwa kuendelea kutoa huduma kutokana na ukosefu wa maji, jambo ambalo linaondosha ufanisi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi.

Ukosefu wa vifaa vya kuzimia moto unaweza kupelekea kupunguza ufanisi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi katika kutekeleza majukumu yake pindipo majanga ya moto yanapotokezea.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kuhakikisha unaandaa bajeti maalum (ya dharura) inayohusiana na ununuzi wa magari na vifaa vya zimamoto vya kisasa na kuiwasilisha Serikalini kwa lengo la kupewa kipaombele cha haraka ili kunusuru utokeaji wa majanga ambayo hawatakuwa na uwezo wa kuyakabili kulingana na vifaa vilivyopo sasa. Mchanganuo wa magari hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 3: Hali halisi ya Magari katika vituo vya Zimamoto na Uokozi

Namba	Namba ya Gari	Aina ya Gari	Hali Halisi ya Gari
Kituo cha Zimamoto Mjini			
1.	KZU 279	Man	Nzuri
2.	KZU 271	Isuzu	Afadhali
3.	KZU 238	Fuso	
4.	KZU 193	Fuso	
5.	KZU 236	Rav 4	
6.	KZU 275	Land Crusser	
Kituo cha Zimamoto M/Kwerekwe			
1.	KZU 227	Nissan	Afadhali
2.	KZU 265	Land Crusser (Pampa)	
Kituo cha Zimamoto Bandarini			
1.	KZU 252	Nissan	Afadhali
Kituo cha Zimamoto Buyu			
1.	KZU 202	Canter	Afadhali
2.	KZU	Toyota Hilax	
Kituo cha Zimamoto Uwanja wa Ndege Unguja			
1.	KZU	Nafco 01	Afadhali
2.	KZU	Nafco 02	
3.	KZU 256	Noah	
4.	KZU 262	Ambulance	
Kituo cha Zimamoto Kitogani			
1.	KZU 239	Fuso	Afadhali

2.	KZU 258	Ashok	
3.	KZU 266	Land Crusser (Pampa)	
4.	KZU 213	Eveco	
5.	KZU 277	Navara	
Kituo cha Zimamoto Marumbi			
1.	KZU 194	Fuso	Afadhali
Kituo Cha Zimamoto Mahonda			
1.	KZU 192	Fuso	Afadhali
2.	KZU 274	Rav 4	
Kituo Cha Zimamoto Kigunda			
1.	KZU 250	Nissan	Afadhali
Kituo Cha Zimamoto Nungwi			
1.	KZU 231	Fuso	Afadhali
Ofisi ya Chanjaani Pemba			
1.	KZU 240	Prado	Afadhali
2.	KZU 219	Rav 4	
3.	KZU 217	Pickup	
4.	KZU 223	Issuzu	
5.	KZU 218	Canter	
6.	KZU 195	Tata	
Kituo cha Zimamoto Chanjaani Pemba			
1.	KZU 248	Nissan	Afadhali
2.	KZU 246	Issuzu	
3.	KZU 261	Pamper	

Kituo cha Zimamoto Mkoani Pemba			
1.	KZU 260	Isuzu	Afadhali
Kituo Cha Zimamoto Wete Pemba			
1.	KZU 233	Fuso	Afadhali
Kituo cha Zimamoto Kijichame Pemba			
1.	KZU 271	Benz	Afadhali
Kituo cha Zimamoto Uwanja wa Ndege Pemba			
1.	KZU 278	Man	Nzuri
2.	KZU 265	Scania	
3.	KZU 270	Caravan	Afadhali
Gari Mbovu			
1.	SMZ 3599	Eveco	Mbovu
2.	KZU 213	Eveco	
3.	SMZ 3603	Ambulance	
4.		Ambulance	
5.		Toyota Hilax	
6.		Curmbas	
7.		Titano	
8.		Isuzu	
9.		Canter	
10.		Canter	
11.		Toyota Rav A4	
12.		Toyota Rav A5	
13.		Ditroet	

14.		Tata	
15.		Fuso	
16.		Isuzu	
17.		Ditroet	
18.		Amarok	

Majibu ya Uongozi wa KZU

Ni kweli kwamba Kikosi kimekabiliwa na Upungufu mkubwa wa vitendea kazi, hii imesababishwa na kuwa na bajeti ndogo ambayo haikidhi kununua vifaa vya kutosha. Kwa sasa Kikosi kimo katika hatua ya Kupata mkopo "Soft Loan" Euro 10,000,000 kutoka Serikali ya Austra kwa ajili ya kununua Magari ya kuzimia moto na Uokozi yasiopungua 21, boti moja na vifaa mbali mbali vikiwemo vya uokozi katika mwaka wa fedha 2024/2025 na 2025/2026 mradi huu tunategemea utakamilika ndani ya miaka miwili. Mbali na hayo tunategemea Kikosi kupitia bajeti yake ya ndani kwa mwaka wa fedha 2024/2025 itanunua gari mbili za kisasa za kuzimiamoto. Hata hivyo Kikosi kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 kimepanga kununua gari mbili za uendeshaji.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa ni kweli wakati wa ukaguzi Kikosi kilikuwa na upungufu wa vifaa vya kuzimia moto. Hata hivyo, Kikosi kimeshachukua juhudi za kuomba mkopo wa jumla ya shilingi bilioni 27,200,000 kwa ajili ya ununuzi wa gari za kuzimia moto. Kupitia fedha hizo, Kikosi kinategemea kununua zaidi ya gari 20 za aina tofauti zikiwemo za kuzimia moto.

Sambamba na hilo, Kamati ilipopitia taarifa ya hesabu ya nwisho wa mwaka imebaini kuwa jumla ya shilingi milioni 700,000,000 zimetumika mwaka 2022/2023 na kuelezwa kwamba fedha hizo zilitumika kwa kulipia deni la ununuzi wa gari mbili za kuzimia moto ambazo zinaendelea kutumika (moja ipo Unguja na nyengine Pemba). Kamati ilitaka kupatiwa vielelezo vya ununuzi huo ili kujiridhisha na matumizi yaliyofanyika lakini hadi Kamati inakamailisha kazi zake haikuweza kupatiwa vielelezo hivyo. Kwa msingi huu, Kamati imeibakisha hoja hii kwa hatua za Mkaguzi kwenda kujiridhisha kama kweli vielelezo hivyo vipo.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inakitaka Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kuhakikisha wanahifadhi vizuri vielelezo vya matumizi yao ili vikihitajika viweze kupatikana kwa wakati.

UCHUNGUZI WA KAMATI YA PAC KUHUSU UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA TAASISI ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023

MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO

Hoja nambari 4.1.2.1: Kukosekana kwa umiliki wa Mifumo ya Wakala wa Serikali Mtandao kuwa ni Mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

Kifungu nambari 62 na 64 cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 vinaeleza kwamba Taasisi za Umma kutumia mbinu sahihi za kupata mali za umma na kutunza nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zinamilikiwa kisheria. Aidha, mali hizo zinapaswa kuwekwa katika daftari la Mali za Kudumu.

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kuwa Wakala wa Serikali Mtandao inamiliki kwa njia ya usimamizi mifumo mbali mbali ambapo mifumo hiyo hutumika kwa Taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kufanya shughuli zao kuu ikiwemo shughuli za kukusanya mapato, kufanya manunuzi na matumizi, kupanga bajeti ya kuidhinisha fedha za matumizi kwa Taasisi za Umma, kutoa nambari za udhibiti wa malipo, kufanya mawasiliano ya ndani na nje ya Taasisi, kutuma barua na nyaraka mbali mbali kwa Taasisi ambapo nyaraka hizo baadhi yao ni siri za Serikali. Baadhi ya mifumo hiyo ndiyo inayotekeleza dhana ya Serikali Mtandao kama vile Mfumo wa Afisi Mtandao kwa Serikali (e- Office), Mfumo wa Barua pepe za Serikali (GMS), Mfumo wa manunuzi ya Serikali (e-Proz), Mfumo wa Bajeti na Matumizi wa Serikali (BAMAS), Mfumo wa Kutoa nambari za Udhibiti wa malipo ya Serikali (ZanMalipo) n.k.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini baadhi ya mifumo hiyo ni mali ya Kampuni binafsi za Nje na mengineyo ni Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo SMZ inatumia kwa mujibu wa makubaliano ya Ushirikiano (MoU) na sio mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa maana ya kuwa SMZ haina umiliki halisi (source codes) kwa mifumo hiyo, licha ya kuwa shughuli zote kuu za Taasisi za SMZ zinafanyika kupitia mifumo hiyo ikiwemo shughuli za kukusanya mapato, matumizi, manunuzi, barua na nyaraka za siri, mawasiliano ya Viongozi wa Umma n.k.

Kutumika mifumo hiyo bila ya kuwa na umiliki kamili kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kunaweza kupelekea kukosekana kwa usiri na usalama wa taarifa muhimu za Serikali jambo ambalo linaweza kusababisha kuvuja kwa Taarifa za Serikali na kusababisha kukosekana kwa usalama wa Nchi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kwa kuzingatia kwamba Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) hayafungamani na sheria, hivyo uongozi wa Wakala unapaswa kuanzisha mchakato wa kuwa na mifumo yake au kupata umiliki halisi kutoka kwa washirika waliowapatia na kuitambua mifumo hiyo kama Mali ya Umma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama ilivyoagizwa kupitia vifungu nilivyovinakili hapo juu.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Mamlaka ya Serikali Mtandao imepewa jukumu na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar la kuhakikisha Zanzibar inakua ya kidijitali katika uendeshaji wa shughuli za Serikali na Utoaji wa Huduma kwa Umma. Ili kutekeleza jukumu hilo kwa haraka na katika muda uliopangwa. Mamlaka ya Serikali Mtandao imekuwa ikitumia taratibu mbali mbali ili kufanikisha lengo lililopangwa kama ifuatavyo: -

1. Utaratibu wa Mifumo kama Huduma (Software as a Service - SAAS),
2. Utaratibu wa Miundombinu kama Huduma (Infrastructure as a Service - IAAS),

Utaratibu wa Mifumo inayomilikiwa Miundombinu na Huduma (On Premises - Hosting the Software on One's Own Hardware).

Taratibu hizo zimeiwezesha Mamlaka kuingia katika hati za makubaliano na Taasisi za Tanzania bara pamoja na kuingia mikataba na kampuni binafsi kwa ajili ya utengenezaji wa mifumo. Utaratibu huu tayari umekubalika Serikalini kwa Taasisi za Serikali kuingia mikataba kwa njia ya(PPP) Public- Private Partnership kupitia (Zanzibar Public- Private Partnership Department).

Ni kweli kuwa Mifumo ya eoffice, GMS na ZanMalipo haina umiliki wa ***Source Code*** Kwa hivi sasa kwa sababu Mifumo hii inaingia katika aina ya umiliki wa Miundombinu kama huduma (Infustructure as a Service

- IAAS) ambayo kwa mujibu wa Taratibu za uendeshaji wa Mifumo inakubalika kwani Mamlaka ya Serikali Mtandao inauwezo wa kuifikia Mifumo hiyo muda wowote inapohitajika. Aidha kwa upande wa Mfumo wa Bajeti na Matumizi Serikalini (BAMAS), Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina umiliki wa ***Source Code.***

Mamlaka ya Serikali Mtandao imeshaanza mazungumzo na Mamlaka ya Serikali Mtandao ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusiana na kukamilisha taratibu za upatikinaji wa “Source Code” na umiliki wa Mifumo ya eoffice, GMS na ZanMalipo kwa ajili ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imeelezwa ni kweli muelekeo ni kwamba Mamlaka iwe na umiliki na mifumo yote lakini changamoto ilikua wataalamu ambao ni “developers” na wana uwezo mkubwa wa kutengeneza mifumo ambayo inahitajika kwa kipindi hicho.

Kamati imejiridhisha kwamba kweli kwa kipindi hicho eGaz haikua na wataalamu wanaojitosheleza ambao wangeweza kutengeneza mifumo hiyo ambayo ilikua ikihitajika na badala yake wakashirikiana na eGa (TZ) ili kuweza kushirikiana katika utengenezaji wa mifumo hiyo.

halkadhalika, Kamati imejiridhisha kwamba kulikua na changamoto ya wataalamu wa kutengeneza mifumo “System Developers” ambapo awali kulikua na wataalamu wanne (4) na sasa wapo kumi na nane (18), jambo ambalo limeweza kuimarisha Taasisi ambapo sasa eGaz inaweza kutengeneza mifumo kwa kutumia uwezo wake wa ndani.

Aidha, kamati imebaini kwamba kuna muelekeo kupitia “MoU” baina ya eGa (TZ) na eGaz ambayo kuna mazungumzo yanafanyika ili sasa mifumo yote ambayo “source code” zake bado hazijawasilishwa eGaz iweze kukabidhiwa kwa Mamlaka Serikali Mtandao Zanzibar.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaielekeza Mamlaka Serikali Mtandao Zanzibar kuhakikisha mifumo yote ambayo “source code” zake zipo katika taasisi nyengine inawasilishwa na kukabidhiwa kwa Mamlaka ili kuhakikisha umiliki wa mifumo yote ya serikali.

Hoja nambari 4.1.2.2: Seva za uzalishaji wa Data za Mifumo ya Serikali Mtandao zipo katika Kituo cha Data kilichopo Dar-es-Salaam

Serikali Mtandao imebainika kuwa Seva za uzalishaji wa data za mifumo ya Serikali Mtandao (ZANMALIPO, e-Office na GMS) zimewekwa katika kituo cha data kinachosimamiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao ya Tanzania (eGA) kilichopo Jijini Dar-es-Salaam.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na malengo ya Uanzishwaji wa Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar (ZICTIA) ambapo imepewa jukumu la kusimamia Kituo cha Data cha Serikali ya

Zanzibar kinachotoa huduma za miundombinu ya seva za mifumo kwa taasisi za Umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kutumia kituo cha Data cha Serikali ya Zanzibar kama ilivyoelekezwa katika kifungu nambari 4 cha Sheria ya Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar ya 2020 ili kwenda sambamba na malengo ya uanzishwaji wa Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar (ZICTIA) pamoja na kuongeza usiri na uadilifu wa matumizi ya taarifa za Serikali.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Ni kweli baadhi ya mifumo ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGAZ) imewekwa katika kituo kinachosimamiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (eGA). Mamlaka imechukua hatua hizo kwa kuzingatia vigezo vya Bodi ya Viwango ya Kimataifa (International Organization for Stanadard - ISO) vinavyohusu uhifadhi wa mifumo ya TEHAMA (***A.8.13 Information Backup ensures systematic compliance with ISO 27001:2022***) ambayo imesisitiza kutohifadhi taarifa katika kituo kimoja.

Mamlaka imechukua hatua hizo kwa kuwa kwa sasa ZICTIA haina kituo chengine cha kuhifadhi data (***Disaster Recovery site***) hali inayoweza kuleta athari iwapo kituo kikuu kitakabiliwa na changamoto yoyote na kupelekea kukosekana kwa huduma muhimu za Serikali Mtandao. Katika kukabiliana na Changamoto hiyo Mamlaka ya Serikali Mtandao tayari imeshachukua juhudi za kuhakikisha kuwa inafanikiwa kupata kituo chake cha kuhifadhia Taarifa.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba katika malengo ya awali ya eGaz, Taasisi ilipanga kutengeneza kituo chake cha kuhifadhia “data” (Data Centre) kama sehemu ya kituo mbadala cha kuhifadhia “data” endapo itatokea hitilafu katika vituo vyengine. Kutokana na changamoto mbali mbali mpango huo haukuweza kutekelezeka kwa kipindi hicho. Kutokana na jitihada zilizofanywa na eGaz, kwa sasa tayari wameshapata eneo TTCL na tayari taratibu zote zimeshakamilika na hatua za ujenzi zimeanza ambapo “data centre” hiyo itamilikiwa moja kwa moja na eGAZ wenyewe na inatarajiwa itakidhi haja ya mahitaji yote ya sasa. Kwa mnasaba huo seva zilizopo eGA Dar es Salaam zitaondolewa na kuletwa katika vituo vyao ambavyo vipo katika hatua ya ujenzi kwa sasa.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaielekeza Mamlaka Serikali Mtandao kuhakikisha ujenzi wa kituo hicho cha kuhifadhia "data" kinakamilika kwa wakati ili kupunguza ama kuondoa uwezekano wa taarifa muhimu na nyeti za Serikali kuvuja.

Hoja nambari 4.1.2.3: Kushindwa kuwasilisha Mfumo wa Manunuzi uliohitajika kulingana na hadidu za rejea za mkataba

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Kampuni ya Ozone International imeshindwa kutengeneza mfumo uliohitajika na badala yake imeleta na kuweka mfumo wa manunuzi ukiwa katika muundo wa huduma (System-as-Service)

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 2 cha makubaliano ya mkataba, ambapo kwa mujibu wa Hadidu za Rejea (ToR), Mamlaka ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma (User department) ilihitaji kutengenezewa mfumo kupitia njia bora za utengenezaji wa mifumo ya kielektroniki na sio kununua huduma ya mfumo.

Kwa vile mshauri elekezi ameshindwa kutekeleza makubaliano ya msingi wa mkataba, ukaguzi unaishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kupitia Wakala wa Serikali Mtandao kuchukua hatua stahiki, ikiwemo kusitisha utekelezaji wa mkataba kwa mujibu wa kifungu nambari 19.1 cha mkataba huo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kusimamia vyema utekelezaji wa mikataba ili kuhakikisha kwamba mifumo inayonunuliwa au kutengenezwa inazingazingatia mahitaji ya watumiaji wa Mifumo hiyo.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Ni kweli mfumo wa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali unaohusiana na manunuzi (eProz) unapatikana kwa utaratibu wa "***Software As A Service (SAAS)".***

Hadidu rejea zilizowasilishwa za upatikanaji wa mfumo zilihusu kutumia njia bora za utengenezaji wa mfumo wa kieletroniki ambapo mambo mbali mbali yanahitaji kuzingatiwa yakiwemo mchakato wa kina unaojumuisha mipango, usanifu, utekelezaji, na usimamizi ili kuhakikisha kuwa mifumo hiyo inakidhi mahitaji ya watumiaji na viwango vya usalama.

Kutokana na uharaka wa upatikanaji wa mfumo na baada ya kupata uzoefu wa changamoto na ugumu wa mfumo wa ununuzi kutoka Tanzania Bara (TANePS), Wakala wa Serikali Mtandao

(eGAZ) kwa ushirikiano na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji Mali za Umma (ZPPDA) iliona kwanza kuna haja ya kutengeneza mfumo kwa kutumia njia ya ***Software as a service (SAAS).*** Wakala wa Serikali Mtandao ilichukua hatua muafaka katika kuhakikisha kuwa mfumo wa ununuzi unapatika kwa wakati na katika kila hatua iliwashirikisha watendaji wa ZPPDA. **Kiambatanisho namba (01)**

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba mfumo wa eProz wa sasa ambao unatumika kwa njia ya "software as a Service SAAS" una changamoto nyingi ambazo zinapelekea kutopatikana kwa tija ambayo ilikusudiwa.

Aidha, kutokana na changamoto za mfumo huu, Kamati imeelezwa kwamba eGaz ina mpango wa kuchukua mfumo wa manunuzi unaotumika Tanzania bara na kuufanyia "customization" ili uweze kutumika Zanzibar.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaiagiza Mamlaka Serikali Mtandao kuchukua hatua stahiki ili kuhakikisha changamoto nyingi zinazoikumba mfumo wa manunuzi zinaondolewa ili kupatikane kwa huduma bora.

Hoja nambari 4.1.2.4: Mifumo wa e-Proz unatekelezwa na kufanya kazi kwa njia ya Mfumo kama Huduma (System-as-a-Service)

Ukaguzi uliofanyika kwa eGAZ umebaini kwamba Mfumo wa e-PROZ uliowekwa na Ozone International unafanyakazi kwa njia ya huduma (System-as-a Service), hii ina maana kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inauziwa huduma ya mfumo badala ya kuwekewa mfumo wenyewe (On-premises System).

Matumizi ya mfumo wa e-Proz kwa njia ya huduma, yanahatarisha usiri wa taarifa za manunuzi ya Serikali kwa vile seva za mfumo huo zipo nje ya Mipaka ya Jamhuri ya Tanzania ambapo kuna utofauti katika utekelezaji wa sheria, kanuni na sera za ulinzi wa taarifa. Aidha, Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Muongozo wa Utengenezaji, Uendeshaji na Usimamizi wa Tovuti za Serikali, toleo la 1.0 mwaka 2022, ambapo aya ya 7.1 inaelekeza kuwa tovuti zote zihifadhiwe kwenye kituo kikuu cha kuhifadhi taarifa cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kuandaa utaratibu wa kusitisha mkataba wa Ozone International

Limited bila ya kuathiri shughuli za kiutendaji za Serikali kutokana na hoja zifuatazo:

a) Mahitajio ya Mfumo wa e-Proz kupitia njia ya Huduma (System- as-a Service) hayakutajwa wala kujadiliwa katika Majadiliano ya Mkataba yaliyofanyika baina ya Ozone International, Wakala wa Serikali Mtandao na Mamlaka ya Manunuzi (Kiambatisho nambari A cha Mkataba).
b) Mahitajio ya Mfumo wa e-Proz kupitia njia ya Huduma (System-as a-Service) hayakubainishwa katika Hadidu za Rejea zilizobainisha msingi wa mahitaji ya mfumo, upeo na matokeo ya kazi (Kiambatisho nambari B cha Mkataba).
c) Hakuna ushahidi wa kuidhinishwa kwa manunuzi ya Mfumo wa e-Proz kupitia njia ya Huduma kutoka kwa Wakala wa Serikali Mtandao kama ilivyoelekezwa kupitia Viwango vya Utengenezaji, Upatikanaji, Uendeshaji na Utunzaji wa Mifumo ya Serikali Mtandao (Hati Namba. eGAZ/EXT/ESG/003, sehemu ya 2.2.2.1.2).

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Ni kweli mfumo wa ePROZ uliotengenezwa na Ozone International na kutumiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kufanya manunuzi unafanyakazi kwa njia ya huduma kama ***(System-As-A Service),*** na kwa sasa haukuhifadhiwa kwenye miundombinu iliyopo Nchini.

a) Uwekaji wa mfumo kwa njia hii umezingatia Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao kwa wakati huo nambari 12/2019 ambayo imefutwa na kuanzishwa Sheria mpya ya Mamlaka ya Serikali Mtandao ya nambari 1/2024 ambayo imesisitiza kuhakikisha usalama wa taarifa zinazohifadhiwa kwenye mifumo na haina kikwazo cha uhifadhi wa Taarifa nje ya mipaka ya Zanzibar (Rejea sehemu ya sita (6) ya Sheria No.1/2024).
b) Utaratibu wa kutumia mfumo kama huduma ***Software as Service*** unakubalika na tayari Wakala wa Serikali Mtandao kupitia muongozo wa utengenezaji mifumo ***Guidelines for Development Acquisition Operation Maintenance for e-Government Applications*** kifungu cha **2.2.2.1 Guideline for Software** imeruhusu uwepo wa mifumo ambayo inapatikana kama huduma kwa kuweka utaratibu.
c) Aidha, kuhusiana na kwenda kinyume na Muongozo wa Utengenezaji, Uendeshaji na Usimamizi wa Tovuti za Serikali, toleo la 1.0 mwaka 2022, ambapo aya ya 7.1 inaelekeza kuwa tovuti zote zihifadhiwe kwenye kituo kikuu cha kuhifadhi taarifa cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, sio sahihi kwani eProz ni mfumo wa manunuzi ni tofauti na mfumo wa tovuti hasa ukizingatia kuwa tovuti ni jukwaa au ukurasa wa

mtandao ambao unapatikana kwenye mtandao na unakuwa na habari, taarifa tofauti pamoja na maudhui mbalimbali ambayo yanaweza kufikiwa na watumiaji. Hivyo, mfumo wa manunuzi sio sawa na tovuti kwa sababu ni mfumo ambao unatoa huduma kuhusiana na manunuzi tu na hauna taarifa nyengine.

Mamlaka ya Serikali Mtandao haijakiuka Muongozo wa Tovuti na inahifadhi tovuti za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kituo cha kuhifadhia taarifa kinachosimamiwa na Shirika la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA).

Uchunguzi na Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba uchunguzi na Maagizo ya Hoja hii unalingana na Hoja Na. 4.1.2.3.

Hoja nambari 4.1.2.5: Ukiukwaji wa Taratibu za malipo uliosababisha gharama kubwa za malipo ya tozo ya huduma ya Mfumo wa e-Proz shilingi 4,500,873,948.53

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023, imebainika jumla ya shilingi 4,500,873,948.53 zimelipwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kampuni ya Ozone International kupitia Hesabu nambari 0828583001 ya PBZ kutoka Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali, ikiwa ni malipo ya tozo za huduma ya matumizi ya mfumo wa e-Proz kuanzia mwezi wa Oktoba 2022 hadi Juni 2023.

Baada ya kufanyika tathmini ya fedha zilizolipwa kwa kulinganisha na thamani ya huduma ya mfumo inayotolewa (Value for Money) ukaguzi umebaini kwamba gharama zenye jumla ya shilingi 4,500,873,948.53 zilizolipwa kwa kipindi cha muda wa miezi tisa (9) kuanzia Oktoba 2022 hadi Juni 2023 ni kubwa kulinganisha na huduma yenyewe iliyokuwa ikipatikana kwa kipindi hicho.

Hivyo, ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao pamoja na Uongozi wa Afisi ya Rais Fedha na Mipango kusitisha malipo ya huduma ya mfumo wa e-Proz ili kuokoa kiasi kikubwa cha fedha zinazolipwa kwa kipindi cha miaka mitano (5) ya utekelezaji wa mkataba, na badala yake fedha hizo ziwekezwe kwenye kutengeneza Mfumo wa manunuzi mwengine unaohitajika kwa mujibu wa Hadidu za Rejea za Mkataba.

Hali halisi ya malipo yanayolipwa kwa Mshauri elekezi (OZONE International Limited) kutokana na huduma za mfumo wa eProz

anazotoa kwa kila mwezi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 25: Mchanganuo wa malipo yaliyofanywa kwa Ozone International Limited

Namba	Hati ya Malipo	Nambari ya Ankara	Maelezo	Tarehe ya Malipo	Kiasi kilicholipwa (Tshs)
1.	13/12	OZN/2022/003	Malipo ya e-Proz kwa mwezi wa Novemba 2022.	8/12/2022	92,452,158.90
2.	57/12	OZN/2022/002	Malipo ya e-Proz kwa mwezi wa Okto-ba 2022.	13/12/2022	27,978,385.40
3.	92/01	OZN/2022/004	Malipo ya e-Proz kwa mwezi wa Disemba 2022.	17/01/2023	144,110,705.28
4.	89/02	OZN/2023/001	Malipo ya e-Proz kwa mwezi wa Janu-ari 2023.	21/02/2023	111,066,832.30
5.	212/03	OZN/2023/002	Malipo ya e-Proz kwa mwezi wa Febuari 2023.	22/03/2023	191,177,953.50
6.	219/04	OZN/2023/003	Malipo ya e-Proz kwa mwezi wa Ma-chi 2023.	18/04/2023	1,294,290,852.80
7.	61/05	OZN/2023/004	Malipo ya e-Proz kwa mwezi wa Aprili 2023.	11/05/2023	507,209,116.35
8.	37/06	OZN/2023/005	Malipo ya e-Proz kwa mwezi wa Mei 2023.	9/6/2023	673,025,830.00
9.	203/06	OZN/2023/006	Malipo ya e-Proz Kuanzia 1 hadi 15 Juni)	30/06/2023	1,459,562,114.00
Jumla					**4,500,873,948.53**

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Malipo jumla ya shilingi 4,500,873,948.53 ambayo yamelipwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yamefanyika ikiwa na imani kwamba jumla ya shilingi 4,500,873,948.53 zitalipwa na watowa huduma (suppliers). Serikali ipo katika hatua ya kuhakikisha kwamba jumla ya shilingi 4,500,873,948.53 zinakusanywa kutoka kwa watowa huduma. Ufuatiliaji wa malipo haya unafanywa kwa ushirikiano wa karibu baina ya Mamlaka Serikali Mtandao (eGAZ),

Ofisi ya Raisi Fedha na Mipango, na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, imebaini kwamba ni kweli kulikua ukiukwaji wa taratibu za malipo uliosababisha gharama kubwa za malipo ya tozo ya huduma ya Mfumo wa e-Proz shilingi 4,500,873,948.53. hali imesababishwa na kutokuwepo kwa uunganushwaji (integration) wa mifumo ambapo inapelekea kutojulikana kimfumo fedha ambazo zinatakiwa kukusanywa na Serikali na tozo ambazo zinatakiwa kulipwa mtoa huduma. Kwa mnasaba huo, Kamati imeamua kuibakisha hoja hii kwa hatua za utekelezaji.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Kamati ya PAC inaiagiza Mamlaka kuchukua hatua za makusudi ili kuhakikisha inaunganisha mfumo wa eProz na mifumo mengine ya Serikali ikiwemo mfumo wa Bamas na Zanmalipo.
2. Kamati inaitaka Mamlaka kuhakikisha mfumo wa eProz una uwezo wa kutoa risiti za kielektroniki (digital Invoice) ili kuthibitisha malipo kamili ambayo yamefanyika kupitia mfumo.

Hoja nambari 4.1.2.6: Malipo ya tozo ya huduma yaliyofanywa kabla ya muda wa malipo shilingi 1,459,562,114

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kuwa jumla ya shilingi 1,459,562,114 zimelipwa kwa Ozone International kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kupitia hati namba 203/06 ya tarehe 30/06/2023 ikiwa ni malipo kwa ajili ya huduma ya mfumo wa e-Proz kuanzia tarehe 1 hadi 15 Juni, 2023.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na utaratibu wa malipo jambo ambalo linaashiria kuwa huduma ya mfumo wa e-Proz ina muelekeo zaidi wa kibiashara badala ya kuwa suluhisho la kazi za manunuzi ya Umma kama ilivyoanishwa kwenye dhamira ya utengenezaji wa mfumo ndani ya Mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kusimamia utekelezaji wa makubaliono ya mikataba kwa kuhakikisha Serikali inapatiwa Mfumo wa manunuzi uliohitajika, ili kuepusha usumbufu wa upatikanaji wa huduma endapo Serikali itachelewa kulipia huduma hiyo.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Ni kweli kiwango cha fedha kilichoainishwa kililipwa mapema tarehe 30/06/2023 ikiwa ni malipo kwa ajili ya huduma ya mfumo wa e-Proz kuanzia tarehe 1 hadi 15 Juni, 2023. Mamlaka ilifanya malipo hayo kutokana na utaratibu unaotumika serikalini katika kipindi cha mwisho wa mwaka kwa kutakiwa kufunga hesabu mapema ifikapo mwisho mwaka 2022/2023.

Mamlaka ya Serikali Mtandao ikiwa na jukumu la kuhakiki na kuthibitisha malipo ya matumizi ya mfumo wa eProz iliona ni vyema kufanya malipo mapema kukimbia changamoto zinazoweza kujitokeza ya ucheleshwaji wa malipo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba uchunguzi na Maagizo ya Hoja hii unalingana na Hoja Na. 4.1.2.5.

Hoja nambari 4.1.2.7: Kuwepo kwa tofauti baina ya fedha zinazodaiwa na Ozone International pamoja na kiwango halisi kinachotakiwa kulipwa na Serikali

Katika ukaguzi uliofanyika umebaini uwepo wa tofauti ya fedha zinazotozwa na Ozone International na kiasi halisi cha tozo kinachopaswa kulipwa kwa Ozone kutokana na matumizi ya mfumo kwa mujibu wa makubaliano.

Tofauti hiyo, imetokana na kwamba mfumo hautoi ankara za malipo kiotomatiki na badala yake huandaliwa baada ya uchakachuaji wa ripoti za tenda zilizoidhinishwa ndani ya mfumo huo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao, kupitia na kuthibitisha kiwango cha fedha za tozo zinazowasilishwa kwenye ankara ya Ozone International kabla ya kupelekwa Ofisi ya Rais Fedha na mipango kwa ajili ya malipo. Aidha, katika kupitia ankara hizo, ukaguzi unashauri mambo yafuatayo kuzingatiwa:

- Idadi ya zabuni halisi zilizoidhinishwa ndani ya mfumo katika mwezi husika, kwa sababu umebaini uwepo wa nakala za zabuni (dublicate tenders).
- Kiasi halisi cha thamani ya zabuni alicholipwa msambazaji wa huduma, kwa sababu tumebaini uwepo wa zabuni zisizo na thamani (ZERO & NULL values).
- Kuthibitisha utekelezaji wa tenda zilizoidhinishwa ndani ya mfumo katika mwezi husika, kwa sababu tumebaini baadhi ya zabuni zilizoidhinishwa hazikutekelezwa kwa malipo.
- Kiwango cha ubadilishaji fedha, kinachotumika kwa ajili ya kubadili fedha za thamani ya zabuni zilizolipwa kwa shilingi

kwenda kwenye dola za kimarekani, sababu makubaliano ya malipo yapo kwa dola za kimarekani. Mchanganuo wa tofauti hiyo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 26: Fofauti ya fedha zinazolipwa kwa kila mwezi

Namba	Nambari ya Ankara ya Ozone	Mwezi wa malipo ya huduma	Tozo ya Huduma iliyoombwa	Tozo halisi ya huduma inayopaswa Kudaiwa kwa kuzingatia Thamani za Zabuni. (TZS)	Tofauti ya fedha (TZS)
1.	OZN/2022/003	November 2022	97,318,062.00	101,194,574.43	(3,876,512.43)
2.	OZN/2022/002	October 2022	29,450,932.00	31,167,664.59	(1,716,732.59)
3.	OZN/2022/004	December 2022	144,110,705.28	157,941,043.78	(13,830,338.50)
4.	OZN/2023/001	January 2023	116,912,455.00	117,734,049.91	(821,594.91)
5.	OZN/2023/002	February 2023	201,239,951.00	64,204,539.78	137,035,411.22
6.	OZN/2023/003	March 2023	1,362,411,424.00	1,592,469,472.12	(230,058,048.12)
7.	OZN/2023/004	April 2023	533,904,333.00	425,041,956.94	108,862,376.06
8.	OZN/2023/005	May 2023	708,448,242.00	1,122,995,496.23	(414,547,254.23)
9.	OZN/2023/006	June 2023, (from 1st to 15th)	1,536,381,173.00	1,256,318,645.41	280,062,527.59
Total Amount				**4,869,067,443.18**	**(138,890,165.90)**

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Ni kweli mfumo wa eProz hautoi Ankara za malipo kiotomatiki hali iliyopelekea malipo ya huduma kutolewa kwa njia ya kuangalia ripoti ya kumalizika kwa tenda na mzabuni kupewa mkataba.

Tofauti ya tozo ya Tzs 138,890,165.90/= zilizoainishwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali inatokana na kuangalia ripoti za ***RFQ (awarded tenders)*** na sio hatua ya mwisho wa kupewa mkataba ambayo ndio tozo inapotolewa na kufanyiwa malipo.

Hata hivyo Mamlaka ya Serikali Mtandao tayari imeshachukua hatua ya kuunganisha mfumo wa eProz na Mfumo wa Serikali wa Mapato (ZanMalipo) pamoja na mfumo wa Bajeti na Matumizi Serikalini (BAMAS). Utekelezaji wa hatua hii utarahisisha kuweza kujua uhalisia wa zabuni zilizofanikiwa kufikia hatua ya mwisho na kuweza kupewa mkataba.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Makubaliano baina ya Ozole na eGaz ni kwamba ukokotoaji unafuata mkataba ambao utatolewa kwa alieshinda zabuni. Mamlaka imeeleza kwamba kwa sasa eGAz tayari wapo katika hatua za kuiunganisha mifumo ya BAMAS na ZANMALIPO kwa eProz ili sasa tozo zote ziweze kukokotolewa automatic na mfumo wenyewe tofauti na inavyofanywa sasa. Kamati imeamua kuibakisha hoja hii kwa ufuatiliaji wa utekelezaji wake.

Hoja nambari 4.1.2.8: Kutokukatwa tozo ya huduma ya Mfumo wa e-Proz kwa Wasambazaji waliotunukiwa zabuni

Katika ukaguzi uliofanyika, imebainika kwamba wasambazaji wa huduma hawakukatwa kiwango cha fedha kubalifu kwa mujibu wa zabuni walizotunukiwa, ili kuzuia fedha zinazopaswa kulipwa Ozone International kwa ajili ya tozo ya huduma ya matumizi ya mfumo wa e- Proz.

Kushindwa kukata na kuzuia tozo ya huduma ya mfumo wa e-Proz kwa wasambazaji, ni kukiuka makubaliano ya mkataba na kunapelekea Serikali kubeba mzigo wa gharama za matumizi ya mfumo huo na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kusimamia utekelezaji wa makubaliano ya mikataba kwa kuhakikisha wasambazaji waliotunukiwa zabuni zilizopitia kwenye mfumo wa e-Proz wanawasilisha fedha za matumizi ya huduma hiyo kama ilivyokubalika kupitia mkataba wa utekelezaji wa mfumo huo.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Ni kweli kumetokea changamoto za kutokukatwa na kuzuia tozo ya huduma ya mfumo wa e-Proz kwa wasambazaji. Katika kuhakikisha mfumo wa manunuzi hautoingizia gharama za uendeshaji Serikalini, Mamlaka ya Serikali Mtandao ilichukua hatua ya kuindikia barua yenye kumbukumbu namba **CBA.164/289/01/75** ya tarehe **29 Septemba 2021** ikimuarifu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuwajuulisha Afisa Masuuli wote wa Taasisi za Umma, kuhusiana na uwepo wa gharama za huduma (service charge) kwa zabuni ambazo zinahitajika kulipwa kila mwisho wa mwezi. **Kiambatanisho namba 2 kinahusika.**

Kutokana na barua hiyo Mamlaka ya Serikali Mtandao ilitarajia kuwa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa kuwa wao ndio wenye jukumu la kulipa na ndio msimamizi Mkuu wa wahasibu wote ingechukua hatua ya kufungua akaunti na kuwataka wahasibu wote kuwakata wazabuni gharama za huduma ya kutumia mfumo kulingana na makubaliano ya mkataba ili kuhakikisha udhibiti wa upatikanaji wa mapato ya Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba uchunguzi na Maagizo ya Hoja hii unalingana na Hoja Na. 4.1.2.5.

Hoja nambari 4.1.2.9: Kuwepo kwa zabuni ambazo hazikutekelezwa kwenye orodha ya malipo ya matumizi ya mfumo wa e-Proz

Baada ya kupitia orodha ya zabuni zilizowasilishwa na Ozone International kwa ajili ya malipo, ukaguzi umebaini uwepo wa zabuni zilizopo katika hatua za uanzishwaji, utangazwaji, zilizositishwa na zilizopitwa na wakati.

Hii inamaana kuwa kiasi cha tozo ya huduma kinachowasilishwa na Ozone hakina uhalisia wa thamani ya zabuni zilizoidhinishwa na kutekelezwa kwa mwezi husika, na kupelekea kulipwa malipo yasiyostahiki jambo ambalo ni kinyume na kifungu nambari 41.2 cha mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Serikali Mtandao kusimamia utekelezaji wa makubaliano ya mikataba kwa kuhakikisha tozo ya huduma inakatwa kwa zabuni ambayo imeidhinishwa katika mfumo na kutekelezwa kwa malipo ya zabuni hiyo.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Mamlaka ya Serikali Mtandao inakubaliana na hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na imechukua hatua ya kutoa elimu kwa Maafisa ununuzi wa Taasisi zote za Umma kuhakikisha Mikataba wanayoingiza katika mifumo ni yenye kukamilika katika hatua zote nne ili kuepuka uwepo wa zabuni ambazo hazikutekelezwa kwenye orodha ya malipo ya matumizi ya mfumo wa e-Proz. Hata hivyo huduma za malipo ambazo zimewasilishwa baada ya kutolewa katika hatua za awali zilithibitishwa kua ni miamala halali ambayo imefanywa na Taasisi husika.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba uchunguzi na Maagizo ya Hoja hii unalingana na Hoja Na. 4.1.2.5.

Hoja nambari 4.1.2.10: Kutokubainishwa kwa uwazi wa Hakimiliki ya kodi asili za utengenezwaji wa Mifumo (Software source codes)

Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar imeingia mkataba na Kampuni ya UBX (Tanzania) Limited kwa ajili ya kazi ya utengenezaji na uwekaji wa mifumo inayohusisha malipo ya huduma mbali mbali zinazotolewa na taasisi za Umma, Zanzibar

Kifungu nambari 3 cha mkataba huo, kinaelekeza kwa kila taasisi ya Serikali inapohitaji mfumo unaohusisha malipo italazimika kuwasilisha mahitaji yao kwa Wakala wa Serikali Mtandao ili kuyatengenezea nyongeza ya mkataba (addendum) kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hiyo.

Katika ukaguzi uliofanyika umebaini kifungu nambari 28 cha mkataba Mkuu wa UBX hakijatosheleza katika kueleza Hakimiliki ya kodi za utengenezwaji wa Mifumo (Source Codes) ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kutokubainisha umiliki wa kodi hizo za utengenezwaji wa mifumo, kunatoa fursa kwa mtengenezaji (UBX) kuendelea kuwa na udhibiti wa mifumo hiyo hadi baada ya kumalizika kwa utekelezaji wa mkataba, jambo ambalo ni kwenda kinyume na Viwango vya Utengezaji, Upatikanaji, Uendeshaji na Utunzaji wa Mifumo ya Serikali Mtandao (Hati Na. eGAZ/EXT/ESG/003), aya nambari 2.2.2.1.3 ambapo inaelekeza mkataba lazima uwe na kifungu kinachotoa umiliki wa viasili vya programu (source codes)

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa eGAZ kuzingatia ulinzi wa hakimiliki ya kodi asili za utengnezwaji wa mifumo ya TEHAMA

katika kila mkataba unaohusisha utengenezaji wa mifumo kama ilivyoelekezwa katika kifungu nambari 3(1)(b) cha Sheria ya Hakimiliki ya Zanzibar, 2003 pamoja na muongozo wa viwango wenye kumbukumbu nambari eGAZ/EXT/ESG/003.

Vile vile katika Mktaba wa UBX, Wakala inapaswa kuhakikisha kwa kila nyongeza ya mkataba itakayofanywa izingatie kuboresha kipengele cha Umiliki (Kifungu cha 28) ili kulinda umiliki wa viasili vya kodi za mifumo kwa taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Ni kweli mkataba ambayo Mamlaka ya Serikali Mtandao inayoingia na Kampuni binafsi kwa ajili ya utengenezaji wa mifumo katika Taasisi za Umma hueka utaratibu wa kuweza kuweka nyongeza ya mkataba (addendum).

Utaratibu huu unatokana na mahitaji na uwezo wa Taasisi husika ikiwa inataka kutengenezewa mfumo kupitia kampuni ambazo tayari zina mkataba na Mamlaka ya Serikali Mtandao, hivyo kuweza kuweka mahitaji yake yakiwemo:

- Iwapo Taasisi husika itaweza kulipa “lupsum” ya gharama na kuweza kumiliki source code pale mtengezaji atakapomaliza utengenezaji wa mfumo.
- Iwapo Taasisi haitakuwa na uwezo wa kulipa “lupsum” basi itaingia mkataba wa kuweza kumlipa mtengenezaji kwa utaratibu watakaokubaliana na kwa muda maalum na muda huo ukimalizika mfumo unakuwa ni mali ya Taasisi pamoja na source code zake.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kwamba ni mkataba baina ya UBX na eGaz umebainisha kwamba Taasisi yoyote ya Serikali inaweza kumilikki kodi asili (source code) iwapo itakamilisha utaratibu wa malipo mara baada ya utengenezaji wa mfumo husika. Utaratibu huo wa malipo ni ama kulipia kwa jumla ama kulipia kidogo kidogo, ambapo Taasisi itakayolipia kwa jumla ina uwezo wa kumiliki kodi asili mara tu baada ya utengenezaji wa mfumo na Taasisi itakayolipia kidogo kidogo itamiliki kodi asilia mara baada ya kukamilisha malipo hayo. Kamati imeridhika na majibu na kuiondosha hoja hii.

Hoja nambari 4.1.2.11: Kutokuwepo kwa Kifungu cha uanzishwaji wa makubaliano ya Escrow

Ukaguzi umebaini kwamba Mkataba Mkuu wa UBX haujajumuisha kipengele cha Uanzishwaji wa Makubaliano ya

Escrow, ambapo ni makubaliano ya kulinda na kutunza “source codes” kwenye Taasisi ya Tatu (third party) hadi kukamilika kwa utekelezaji wa mkataba wa utengenezaji wa mifumo hiyo.

Kushindwa kusimamia ulinzi na usalama wa viasili (source codes) vya mifumo ya Serikali, kunatoa fursa kwa mtengenezaji wa mifumo (UBX) kuendelea kuvitumia (re-uses) viasili hivyo kwa kuviboresha (customization) kwa ajili ya manufaa ya kibiashara.

Ili kudumisha uendelevu wa mifumo ya Serikali Mtandao, ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kufanya maboresho ya Mkataba Mkuu wa UBX kwa kuweka nyongeza ya kifungu cha uanzishwaji wa Makubaliano ya Escrow kwa mifumo yote itakayotekelezwa kupitia mkataba huo.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Mamlaka ya Serikali Mtandao imepokea ushauri wa Mdhibiti na Mkauguzi wa Hesabu za Serikali kuhusiana na suala la kuboresha Mkataba mkuu wa UBX.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imeelezwa kwamba Mamlaka tayari ina mpango wa kufanya kikao na UBX kwa ajili ya kujadili na kukubaliana kuhusu kipengele cha Escrow ambacho kimsingi kinamtaka mtengenezaji mfumo kuhifadhi na kudhibiti kodi asili. Kwa mnasaba huo, Kamati imeibakisha hoja hii kwa hatua za ufuatiliaji.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaielekeza Mamlaka ya Serikali Mtandao kuhakikisha kipengele cha Escrow kinaingizwa katika mkataba mkuu ili kulinda kodi asili za mifumo ya Serikali wakati wa utengenezaji wa mifumo hio na hatimae kodi asili zote ziweze kumilikiwa na Serikali pindi mifumo ikimalizika kutengenezwa.

Hoja nambari 4.1.2.12: Aina ya Mkataba na njia za malipo kutoendana na asili ya kazi zinazotekelezwa na mkataba (nature of assignment)

Kanuni ya 181 ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2021 inaelekeza kwamba kazi za utengenezaji wa programu (mifumo) zitumie Mkataba wa Mkupuo (Lump sum contract) na malipo yake yatokane na bei isiyobadilika (fixed price) itakayokubalika.

Ukaguzi umebaini Mkataba Mkuu wa UBX ni wa aina ya kubakiza (Retainer contract) ambapo malipo yake yanatokana na mikato ya asilimia ya thamani ya miamala ya malipo itakayopitishwa kwenye

mifumo itakayo tengenezwa kwa muda wa miaka minne (4) ya utekelezaji wa mkataba huo. Kufanya hivyo, ni kwenda kinyume na kifungu cha kanuni nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kuzingatia sheria, na kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma katika kuingiza mikataba ya utengenezwaji wa mifumo kwa kampuni ya UBX. Aidha rasimu za mikataba hiyo ni vyema kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu kabla kwa ajili ya kupatikana ushauri na maoni ya kisheria kabla ya kuanza kusainiwa na kutumika rasmi kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Mifumo.

Jadweli lifuatalo linaonyesha mchanganuo wa malipo kwa Kampuni ya UBX, yanayotokana na mikato ya asilimia ya thamani ya miamala ya malipo.

Jadweli Nambari 27: Mchanganuo wa malipo kwa Kampuni ya UBX, yanayotokana na mikato ya asilimia ya thamani ya miamala ya malipo.

Kuanzia Shilingi (Tsh.)	Hadi Shilingi (Tshs)	Asilimia Itakayolipwa kwa UBX (%)	Asilimia atakayochukuwa eGAZ (%)	Jumla ya Asilimia zitazokatwa (%)
1	100,000	2.0	0.5	2.5
100,001	500,000	1.6	0.4	2.0
500,001	1,000,000	1.0	0.3	1.3
1,000,001	5,000,000	0.2	0.1	0.3
5,000,001	10,000,000	0.1	0.05	0.15

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Ni kweli Kanuni ya 181 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2021 inaelekeza kwamba kazi za utengenezaji wa programu (mifumo) zitumie Mkataba wa Mkupuo (Lump sum contract)

Aidha, Mkataba Mkuu wa UBX ni wa aina ya kubakiza (Retainer contract) ambapo umetumia kifungu nambari 182 cha kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2021 kinachohusiana na Time Based Contract.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba mkataba mkuu baina ya eGaz na UBX ni wa aina ya kubakiza (Retainer contract). Aidha, Kamati imebaini kwamba kulikua na upungufu wa mkataba huo kwani kichwa cha habari (Heading) cha mkataba kinaeleza kwamba mkataba utakua wa mkupuo balada ya kubakiza.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaielekeza Mamlaka ya Serikali Mtandao kuhakikisha kichwa cha habari cha mkataba kinabadilishwa ili kuendana na maudhui yaliyokuepo ndani ya mkataba wenyewe.

Hoja nambari 4.1.2.13: Gharama za malipo ya Mkataba wa UBX zitabebwa na walipaji wa huduma

Katika ukaguzi uliofanyika, imebainika kuwa kifungu nambari 10.4 cha mkataba mkuu wa UBX kinaelekeza malipo ya utekelezaji wa mkataba yatatozwa kwa walipaji wa huduma.

Kufanya hivyo, kunapelekea kuongezeka kwa ada, tozo au bei ya huduma zitakazotolewa kwa wananchi kutoka Serikalini ambapo malipo yake yatapitishwa kwenye mifumo itakayotengenezwa na UBX.

Ukaguzi unaushauri uongozi Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kufanya maboresho ya Mkataba Mkuu wa UBX kupitia nyongeza iliyotajwa katika kifungu nambari 3 ili kubatilisha kifungu nambari 10.4, na hivyo Kampuni ya UBX ilipwe kiasi cha mkupuo kulingana na asili ya kazi inayokwenda kutekelezwa.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Ni kweli gharama za malipo ya Mkataba wa UBX zitabebwa na walipaji wa huduma hii ni kutokana na gharama za uendeshaji wa Mifumo jambo ambalo ni kawaida katika utoaji wa huduma , kwa mfano tozo ya Shilingi 70 kwa kila lita moja ya mafuta ya gari anayokatwa mwanachi katika uendeshaji wa huduma za barabara(Service Charge) kupitia ununuzi wa mafuta (Petrol na Disel).

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati haijaridhika na uhalisia kwamba kifungu namba 10.4 cha mkataba mkuu baina ya UBX na eGaz kinamtaka mnufaika wa huduma kulipia ada ya huduma, hali ambayo inaweza kupelekea mripuko wa bei kwani hali hii itasababisha kungezeka kwa bei kwa huduma zote ambazo zitatolewa kutokana na matokeo ya mkataba mkuu wa UBX

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaielekeza Mamlaka ya Serikali Mtandao kuangalia namba ambayo kifungu namba 10.4 cha mkataba mkuu wa UBX kinaweza kufutwa ama kufanyiwa marekebisho na badala yake taasisi zote zilipie ada kwa mkupuo (Lumbsum payment) kwa UBX badala ya kuruhusu malipo kubakiza (Retainer payment) ambapo mfumo huu unaenda kuwaumiza zaidi watumiaji wa huduma wa mwisho.

Hoja nambari 4.1.2.14: Kutokuzingatiwa kwa Mpango wa Manunuzi ndani ya Mfumo wa e-Proz

Ukaguzi umebaini kuwa, mfumo wa e-Proz haujazingatia kuwepo kwa Mpango wa Manunuzi unaoandaliwa na kuidhinishwa na taasisi inayofanya manunuzi (PDEs) kwa kila mwaka kulingana na bajeti husika.

Kuwepo kwa dosari hiyo, kunawezesha mfumo kuruhusu manunuzi ya bidhaa au huduma ambazo hazikuainishwa katika mpango wa manunuzi na kupelekea kuathiri utekelezaji wa bajeti iliyopangwa kwa mwaka husika, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria, kanuni na miongozo ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kusimamia uboreshwaji wa mfumo kwa kujumuisha Mipango ya Manunuzi inayoandaliwa na taasisi za Umma ili kuweka udhibiti wa kiotomatiki kwa kuzuia zabuni zilizo nje ya mpango wa manunuzi uliowasilishwa katika Mamlaka ya Manunuzi ya Umma kama ilivyoelekezwa kupitia Kanuni ya 64(1) ya kanuni za Manunuzi ya Umma.

Vile vile utaratibu huu utaweza kurahisisha jukumu la kufanya ukaguzi wa Manunuzi ya Umma linalotekelezwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Ni kweli wakati wa ukaguzi mfumo wa e-Proz ulikuwa haujaunganishwa na mfumo wa BAMAS ambapo ungeweza kuzingatia mpango wa manunuzi. Kwa sasa Mamlaka tayari imeshaanza hatua za kuunganisha mfumo wa e-Proz na mfumo wa BAMAS kwa lengo la kuhakikisha kuwa mfumo wa e-Proz unazingatia mpango wa manunuzi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, Kamati ilitaka kujua ni kwa asilimia ngapi Mfumo wa BAMAS umeanza kuunganishwa na Mfumo wa e-Proz na kuelezwa kwamba kwasasa umeshafikia asilimia 80 ambapo kwasasa Wakala upo katika hatua ya kufanya majaribio (testing of System) ili kuona au kubaini changamoto na kuweza kuzipatia ufumbuzi.

Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ifikapo mwanzoni mwa mwezi wa Januari Mfumo huo utakuwa umekamilika. Kwa msingi huu, Kamati inaendelea kuibakisha hoja hii kwa hatua za utekelezaji na kujiridhisha juu ya kukamilika kwake.

Maagizo ya kamati ya PAC

Kamati ya PAC inautaka Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuchukua juhudi za

makusudi zitakazohakikisha Mfumo wa BAMAS unaunganishwa na Mfumo wa Manunuzi e-Proz kwa wakati uliopangwa.

Hoja nambari 4.1.2.15: Kuwepo kwa zabuni zisizokuwa na thamani ya fedha alizolipwa Msambazaji kupitia Mfumo wa e-Proz.

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa zabuni ambazo hazina thamani ya fedha alizolipwa msambazaji, hii maana yake ni kwamba mfumo wa e-Proz hauna udhibiti wa kuzuia uingizaji wa zabuni isiyo na thamani ya fedha atakazolipwa msambazaji. Kuwepo kwa dosari hii, kunatilia mashaka uhalisia wa malipo ya tozo ya huduma yanayofanywa kila mwisho wa mwezi, kwa vile ukokotoaji wa kiasi cha fedha hizo hutegemea thamani ya zabuni zilizoidhinishwa na kulipwa ndani mwezi husika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kusimamia maboresho ya huduma za mfumo wa e-Proz, ili kuweza kujengewa udhibiti wa kulazimisha uingizwaji wa taarifa ya thamani ya zabuni wakati wa uandaaji wa zabuni hizo ndani ya mfumo.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Ni kweli kasoro hii ilikuwepo ya kukosekana bei kwenye nyaraka kutokana na kukosekana muongozo kutoka Mamlaka ya Manunuzi na Uondoshaji Mali Zanzibar. Maafisa Manunuzi wengi walikua wanatumia Muongozo kutoka Tanzania Bara ambao ulikua haulazimishi kuweka bei, Aidha kulikua na utaratibu wa kuhakiki bei kabla malipo kufanyika.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kuishughulikia hoja hii, Kamati ilitaka kujua kwamba katika hatu za awali za utengenezaji Mfumo wa Manunuzi (e-Proz) Mamlaka ya Serikali Mtandao haikuweza kuiona changamoto ya kuwepo kwa zabuni zisizokuwa na thamani ya fedha alizolipwa Msambazaji na Uongozi wa Mamlaka kueleza kuwa hawakuelewa kama changamoto hiyo ingeweza kujitokeza. Hata hivyo, changamoto hiyo tayari imesharekebishwa. Kwa mnasaba huo, Kamati imeamua kuiondoa hoja hii.

Hoja nambari 4.1.2.16: Kuwepo kwa zabuni zisizo na uhalisia wa thamani ya fedha katika Mfumo wa e-Proz

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa zabuni zisizo na uhalisia wa thamani ya fedha (Tender values) alizolipwa msambazaji aliyetunukiwa zabuni, ukilinganisha na kiasi cha fedha kilichotangazwa (RFQ values).

Kuwepo kwa dosari hii, kunatilia mashaka uhalisia wa malipo ya tozo ya huduma yanayofanywa kila mwisho wa mwezi, kwa vile ukokotoaji wa kiasi cha fedha hizo hutegemea thamani ya zabuni zilizoidhinishwa na kulipwa ndani mwezi husika Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali

Mtandao Zanzibar kusimamia maboresho ya mfumo kwa kuweka udhibiti wa kuthibitisha na kuzuia uingizwaji wa thamani ya zabuni iliyo nje ya kiwango cha bajeti ya manunuzi ya zabuni hiyo.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Sababu ya kuonenaka kwa tofauti ya zabuni zisizo na uhalisia wa thamani ya fedha anazolipwa msambazaji aliyeshinda zabuni, ukilinganisha na kiwango cha fedha halisi zilizoainishwa, inatokana na makosa yanayofanywa na Maafisa manunuzi wa Taasisi husika na sio Mfumo. Kwa mfano “Tenda” nambari RFQ _15081 ambapo imetangazwa kama ni “Tenda” ndogo kwa mujibu wa jaduali namba tano ya sheria 11/2016 kiwango cha zabuni kubwa kinaanzia 15,000,001/-. Muhusika wa zabuni hii ametumia “Tenda” ndogo badala ya “tenda” kubwa na kuandaa mkataba katika sehemu isiyohusika.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imegundua kuwa licha ya juhudi ambazo Mamlaka imezichukua lakini bado Mfumo wa Manunuzi hauwezi kutambua zabuni zisizo na uhalisia wa thamani ya fedha. Mamlaka inaendelea kuifanyia kazi suala hili ili iweze kulitatua. Kwa msingi huu, Kamati imeibakisha hoja hii kwa hatua za utekelezaji.

Maagizo ya kamati ya PAC

Kamati inautaka Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao kuhakikisha inaufanyia marekebisho Mfumo wa e-Proz ili uweze kutambua zabuni zisizo na uhalisia wa thamani ya fedha kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa na Sheria.

Hoja nambari 4.1.2.17: Mfumo wa e-Proz kushindwa kubaini vyeti vilivyomaliza muda

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa e-Proz unashindwa kuwazuia wasambazaji walio na vyeti vya usajili vilivyopitwa na wakati kuingia katika mashindano na kutunukiwa zabuni, kufanya hivyo ni kinyume na Kanuni nambari 87 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma.

Ukaguzi umebaini Msambazaji “OSAJU COMPANY LIMITED” mwenye nambari ya usajili G000394 ulioishia tarehe 19 /01/2023, alishiriki na kutunukiwa zabuni mbali mbali bila ya kuzingatia umalizikaji muda wa vyeti vyake vya usajili

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kusimamia maboresho ya Mfumo kwa kuweka udhibiti wa kiotomatiki wa kumzuia Msambazaji mwenye nambari ya usajili iliyopitwa na wakati ashindwe kushiriki na kutunukiwa zabuni kama ilivyoelekezwa kwenye

Kanuni za Manunuzi ya Umma. Mchanganuo wa Taarifa za cheti cha Msambazaji ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 28: Mfumo kushindwa kuzuwia wasambazaji walio na vyeti vya usajili vilivyomaliza muda wake wa kushiriki mashindano ya zabuni

S/N	RFX Code	RFX Tiltle	Division	RFX Publish RFx Date	RFX AwardDate	Supplier Awarded
1.	rfq_ 14781	UNUNUZI WA NGUO ZA WATOTO MAZIZINI WAMJJWW	MINISTRY OF COMMUNITY DEVELOPMENT	3/16/2023	01/04/2023 16:38	15,730,000.
2.	rfq_ 13753	UNUNUZI WA KARATASI ZA KUANDIKIA (A4 PAPER)	PUBLIC PROCUREMENTAND DISPOSALOF PUBLIC ASSETS	3/8/2023	13/03/2023 12:16	800,000.
3.	rfq_ 14853	UNUNUZI WA KOMPYUTA	PUBLIC PROCUREMENTAND DISPOSALOF PUBLIC ASSETS	3/20/2023	09/05/2023 11:09	6000,000.
4.	rfq_ 14863	UNUNUZI WA KOMPYUTA (DESKTOP)	PUBLIC PROCUREMENTAND DISPOSALOF PUBLIC ASSETS	3/20/2023	09/05/2023 12:27	6000,000.
5.	rfq_ 18021	TUNAOMBA KUSAMBAZIWA KOMPUTA ZA MEDANI DESKTOP COMPUTER KWA MATUMIZI YA	ZANZIBAR HIGHER EDUCATION LOAN BOARD (ZHELB)	4/28/2023	04/05/2023 21:10	19,000,000.
6.	rfq_1896	SBD FOR SUPPLY OF XONSTRUCTION AND BUILDING MATERIAL FOR JKU SECURITY	NATIONAL SERVICES BRIGADE (JKU)	1/19/2023	30/03/2023 10:14	2,632,042,250.
7.	rfq_ 8696	ZABUNI KWA AJILI YA KUJENGA VIBANDA PUMPING HOUSE PAMOJA NA FENSI JUMLA	ZANZIBAR WATER AUTHORITY (ZAWA)	1/16/2023	12/05/2023 11:27	1,279,576,434.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Ni kweli mfumo wa manunuzi huchukua taarifa za awali pale Mzabuni anapofanya usajili kwa mara ya kwanza na kuweka taarifa sahihi

zinazotakiwa ili kuweza kukamilisha usajili. Uwekaji wa taarifa umezingatia leseni za aina mbili kuu kulingana na utaratibu unaotumiwa na Mamlaka ya Manunuzi kama ufuatao:

- Leseni ambazo hutolewa mara moja na kupewa cheti za kuruhusiwa kufanya biashara. Mfano ZRA, BPRA na TIN. Aina hii ya leseni haitaji kuwekewa muda wa kumalizika.
- Leseni zinazotolewa na Mamlaka ya Manunuzi kwa ajili ya kuruhusiwa kufanya biashara na Taasisi za Umma. Cheti hichi hutolewa kila mwaka na kinahitaji kulipiwa kila mwaka.

Kutokana na mahitaji tofauti ya uwepo wa vyeti mfumo umeweka utaratibu maalamu wa uwekaji cheti cha ZPPDA ambapo Mzabuni anahitajika kuweka tarehe ya mwisho ya usajili wa cheti. Muda wa cheti unapomalizika muda wake. Afisa manunuzi ana uwezo wa kujua na kuweza kumtambulisha Mzabuni kuwa cheti chake kimemaliza muda.

Aidha kuhusiana na kupewa zabuni kwa OSAJU COMPANY LIMITED kuwa cheti chake kimeisha muda wake, Mamlaka ya Serikali Mtandao imechukua hatua ya kufuatilia suala hilo na kubaini kuwa katika kipindi ambacho OSAJU COMPANY LIMITED amepewa zabuni cheti chake kilikuwa hakijamaliza muda wake. kiambatanisho namba 4 cha Ripoti ya Mkaguzi kinahusika.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kwamba ni kweli kasoro iliyobainishwa na Mkaguzi ya Mfumo wa e-Proz kushindwa kubaini vyeti vilivyomaliza muda wake ilikuwepo na inaendelea kuwepo kwani bado kasoro hiyo Mamlaka haijaifanyia kazi ipasavyo.

Kuhusiana na kumaliza muda kwa cheti cha usajili wa Kampuni ya OSAJU, Kamati imebaini kuwa katika kipindi cha ukaguzi cheti hicho kilikuwa kimemaliza muda wake wa usajili. Hata hivyo, uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao ilifuata utaratiba wa kuhuisha muda wake. Hoja hii inaendelea kubakia kwa vile utekelezaji wake haujakamilika.

Maagizo ya kamati ya PAC

1. Kamati inaitaka Mamlaka ya Serikali Mtandao kuhakikisha unaingia mikataba na Wasambazaji waliokuwa hawajasajili na Mamlaka ya Manunuzi na Ununuzi wa Mali za Umma.
2. Mamlaka pia ihakikishe inaandaa utaratibu ndani ya Mfumo wa e-Proz utakaodhibiti vyeti vya Wasambazaji vilivyomaliza muda wake wa usajili kutotambuliwa na Mfumo.

Hoja nambari 4.1.2.18: Kuwepo kwa vyanzo vya mapato ambapo makusanyo yake hayapiti kwenye Mfumo wa ZanMalipo

Kifungu nambari 55(a) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaelezea kwamba "Fedha zote za Umma zitakusanywa kupitia mfumo wa malipo wa kielektroniki uliowekwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali".

Katika kutekeleza agizo hilo Serikali ilianzisha rasmi mfumo wa 'ZanMalipo' ili kuweza kukusanya fedha zote za Serikali kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mapato ya Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali mtandao kwa kushirikiana na Ofi si ya Rais Fedha na Mipango, kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma kwa kuunganisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ili kuhakikisha fedha zote zinakusanywa kupitia mfumo wa malipo wa kielektroniki kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mapato ya Serikali.

Jadweli nambari 29: Tofauti ya mapato yanayokusanywa baina yamfumo wa ZanMalipo na mifumo mwengine.

Namba	Taasisi ya Umma	mapato katika Taarifa za Hesabu.	Mapato yalikusanywa ZANMALIPO	Mapato yaliyokusanywa kwa mifumo mwengine	Mifumo iliyohusika kukusaya mapato
1.	Wizara ya Afya	2,814,099,739.68	861,065,009.00	1,953,034,730.68	Mfumo wa Usimamizi wa Vipimo na Chanjo ya Uviko-19 Zanzibar.
2.	Wizara ya Maji, Nishati na Madini.	12,574,306,012.00	768,321,103.00	11,805,984,909.00	Mfumo wa Usimamizi wa Vibali (RAHISI SOLUTION).

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Ni kweli kwamba kuna baadhi ya vyanzo vya mapato ambapo makusanyo yake hayapiti kwenye Mfumo wa ZanMalipo. Mamlaka ya Serikali Mtandao inaendelea na jitihada ya kuhakikisha kuwa Mapato yote ya Serikali yanapitia katika Mfumo wa ZanMalipo, kazi ya kuunganisha Mifumo inaendelea kwa kushirikiana na Mtengenezaji wa Mifumo hiyo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Mamlaka ya Serikali Mtandao kukir kwamba kuna baadhi ya mapato hayapitii katika Mfumo wa ZanMalipo. Hata hivyo, Kamati ya PAC imebaini kuwa changamoto kubwa inayosababisha hilo kutokea ni Taasisi

husika hazitaki kutumia Mfumo wa ZanMalipo kwa maslahi binafsi yanayopelekea kujinufaisha na kuzuia baadhi ya mapato kuingia Serikalini.

Katika kuhakikisha hilo linatatuliwa, Mamlaka imekuwa ikichukua hatua zifuatazo:

a) Kufanya vikao na Taasisi Tumizi ili kuwalazimisha kutumia Mfumo wa ZanMalipo katika ukusanyaji wa Mapato yao.
b) Mamlaka huwaadikia barua Taasisi Tumizi ili kuwakumbusha juu ya utekelezaji wa matakwa ya sheria. Kwa mfano, Mamlaka iliwaandikia barua Kampuni ya Uvuvi ya ZAFICO, Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka pamoja na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ya tarehe 30/12/2024 yenye kumbukumbu nambari CAB.202/397/01-G/53. Aidha, tarehe hiyo hiyo pia waliwaandikia barua yenye kumbukumbu nambari CAB.202/397/01-G/54 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo, Jeshi la Kujenga Uchumi, Chuo cha Mafunzo, Kikosi cha Valantia

Changamoto hiyo pia inaikabili Kamisheni ya Utaii kupitia fedha ambazo Wageni hulipa moja kwa moja Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) na kuacha kutumia Mfumo wa ZanMalipo unaotoa 'control number' za kufanyia malipo hayo. Kwa msingi hu, hoja hii bado haijatekelezwa ipasavyo, hivyo inabakia.

Maagizo ya kamati ya PAC

Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao uhakikishe unafuatilia kwa karibu taasisi zote ambazo hazifanyi makusanyo yake kupitia Mfumo wa ZanMalipo ili kunusuru mapato ya Serikali kupotea.

Hoja nambari 4.1.2.19: Kukosekana kwa kipengele cha "Bajeti Reallocation" kwenye Moduli ya Bajeti

Ukaguzi ulibaini kwamba mfumo wa BAMAS haujawekewa kipengele (functionality) cha "Budget Reallocation" ambacho ni muhimu katika hatua ya kufanya mabadiliko ya mgawanyo wa bajeti kwenye mfumo ambapo bila ya kipengele hicho watumiaji wa mfumo hawawezi kubadilisha mgawanyo (reallocation) kutoka fungu moja la bajeti kwenda fungu jengine kulingana na mabadiliko yanayohitajika.

Kukosekana kwa Kipengele cha "budget reallocation" katika mfumo wa BAMAS kunaweza kupelekea kushindikana kutekelezwa kwa mabadiliko yanayopendekezwa kwa Serikali na Baraza la Wawakilishi wakati wa vikao vya Bajeti za Mapato na Matumizi Barazani. Aidha, utekelezaji wa "budget reallocation" unatakiwa kufanyika ndani ya "Vote" kutokana na makosa ya kibinadamu (human errors) katika kuweka bajeti kwenye mafungu tofauti na mpango.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kutengeneza na kuweka kipengele cha "Budget Reallocation" katika Mfumo wa BAMAS ili

kuwezesha watumiaji wa mfumo katika Idara ya Bajeti kutekeleza majukumu yao kulingana na taratibu za kazi.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Wakati wa ukaguzi wa Mfumo wa BAMAS kulikuwa na baadhi ya vipengele ambavyo havikupitiwa kwa ufasaha suala hili limetokana na kuwa mfumo ulikuwa bado haujaanza kutumika na ulikuwa katika kipindi cha majaribio.

Hata hivyo Mfumo wa BAMAS umezingatia moduli ya "*Budget reallocation*" na Mamlaka ya Serikali Mtandao ilichukua hatua ya kuwapatia mafunzo watendaji wa Idara ya Bajeti na kuwaonyesha jinsi moduli hii ya "Budget Reallocation" namna inavyofanyakazi katika mfumo wa BAMAS.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Mfumo huu wa BAMAS kwa muda mrefu (mwaka 2022) ulishindwa kuanza kutumika. Hata hivyo, tarehe 1 Julai, 2024 rasmi Mfumo huo umeanza kutumika na kabla ya matumizi, Mamlaka kupitia Idara ya Hazina ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango iliandaa mafunzo kwa Watendaji wa Idara ya Bajeti pamoja na Wahasibu Wakuu wa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Kwasasa moduli ya 'reallocation' tayari imeshaandaliwa na inafanyakazi katika Mfumo huo. Kwa msingi huo, Kamati imeamua kuiondoa hoja hii kwa vile tayari imeshatekelezwa ipasavyo.

Hoja nambari 4.1.2.20: Kukosekana kwa kipengele cha "Supplementary Budget" kwenye Moduli ya Bajeti

Ukaguzi ulibaini kwamba mfumo wa BAMAS hauna kipengele cha Bajeti ya Nyongeza (Supplimentary Budget) ambacho ni maalumu kwa ajili ya kuwezesha uingizaji wa bajeti ya nyongeza ambayo inaidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa sababu maalumu tofauti na bajeti kuu inayopitishwa kila mwaka.

Kukosekana kwa kipengele cha "Supplementary Budget" katika mfumo wa BAMAS kunaweza kupelekea Serikali kushindwa kuingiza bajeti iliyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kutekeleza kazi maalumu au dharura iliyosababishwa na majanga kama vile Mafuriko, Tetemeko la Ardhi, ugonjwa wa mlipuko n.k na kulazimu bajeti pamoja na matumizi hayo kufanyika nje ya mfumo jambo litakalo ondoa udhibiti wa bajeti na matumizi unaopatikana kupitia mfumo na kuhatarisha ufanyaji wa matumizi yasiyozingatia idhini na udhibiti uliopo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kukamilisha vipengele vyote muhimu kulingana na "business processes" za Idara ya Bajeti ikiwa ni pamoja na uundaji wa kipengele cha "Supplementary Budget" kwa kizingatia miongozo ya Kitaifa. O T I.

Aidha, ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kuhakikisha unafanya ushirikishaji wa karibu wa watumiaji wa mfumo wa BAMAS katika Idara ya Bajeti kwa hatua zote kuanzia kukusanya na kuandika mahitaji ya watumiaji (user requirements), kuthibitisha mahitaji (validation of documented user requirements), kufanya mafunzo ya watumiaji, kutoa nafasi kwa watumiaji wa mfumo kufanya majaribio ya mfumo na kutoa ruhusa au kuzuia mfumo kuanza kutumika ikiwa haujakidhi mahitaji (User Acceptance and Testing).

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Ni kweli wakati wa ukaguzi Mfumo wa BAMAS ulikuwa unakosa baadhi ya module suala hili limetokana na kuwa Mfumo ulikuwa bado haujaanza kutumika na ulikuwa katika kipindi cha majaribio.

Aidha, miongoni mwa kipengele muhimu ni kipengele cha "*Supplementary Budget*" ambacho ni moja ya moduli mpya ambazo Mamlaka ya Serikali Mtandao imeweka katika mfumo wa BAMAS, kutokana na mahitaji ya watumiaji.

Mamlaka ya Serikali Mtandao tayari wameweka moduli hii katika mfumo na maboresho yake yatafanyika wakati wa utekelezaji wa "*Phase*" inayofuata baada ya kukamilika kwa moduli ambazo hivi sasa zinazifanyiwa kazi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa ni kweli hoja hii ilikuwa haijatrekelezwa wakati Mkaguzi anafanya jukumu lake la kikatiba. Hata hivyo, kwasasa kipengele cha "*Supplementary Budget*" tayari kimeandaliwa moduli yake ndani ya Mfumo wa BAMAS na hatua inayoendelea ni kuufanyia majaribio. Kwa vile majaribio hayajakamilika, hoja hii inabakia kwa hatua za kuthibitisha utekelezaji wake.

Maagizo ya kamati ya PAC

Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango uhakikishe unakamilisha majaribio ya moduli ya "*Supplementary Budget*" ili iweze kutumiwa na wahusika.

Hoja nambari 4.1.2.21: Kukosekana kwa kipengele cha "Version Carryover" kwenye Moduli ya Bajeti

Ukaguzi ulibaini kwamba mfumo wa BAMAS hauna kipengele cha "*Version Carryover*" ambacho ni muhimu katika kufanikisha mchakato wa utayarishaji wa bajeti kwa kurahisisha kupeleka mbele katika mwaka mpya wa bajeti usanidi uliofanyika katika mwaka uliotangulia au kutoka "version" moja kwenda "version" nyengine ndani ya mwaka mmoja.

Kukosekana kwa kipengele hiki kunaongeza ugumu wa kazi ya maandalizi ya bajeti na kupelekea kutumia muda mrefu katika uandaaji wa bajeti hali

inayoweza kusababisha ucheleweshaji wa mchakato wa bajeti na kufanya utekelezaji wa bajeti husika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kuhakikisha kwamba unatatua mapungufu hayo kwa kuzingatia umuhimu wake katika kukamilisha mchakato wa kuandaa bajeti ya Serikali ili mfumo wa BAMAS usaidie kupatikana kwa ufanisi kwa watumiaji wake na sio kuwa kikwazo cha ufanisi.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Ni kweli wakati wa ukaguzi Mfumo wa BAMAS ulikuwa unakosa baadhi ya ripoti suala hili limetokana na kuwa mfumo ulikuwa bado haujaanza kutumika na ulikuwa katika kipindi cha majaribio.

Aidha, miongoni mwa kipengele muhimu ni kipengele cha "*Version Carryover*" ambacho ni moja ya moduli mpya ambazo Mamlaka ya Serikali Mtandao imeingiza katika mfumo wa BAMAS kutokana na mahitaji ya watumiaji. Mamlaka ya Serikali Mtandao tayari imeweka moduli hii katika mfumo na maboresho yake yatafanyika wakati wa utekelezaji wa "*Phase*" inayofuata baada ya kukamilika kwa zile moduli amabazo kwa sasa Mamlaka ya Serikali Mtandao inazifanyia kazi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya kuwepo kwa kasoro hii wakati wa ukaguzi, hata hivyo Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango tayari imeshaingiza moduli ya "*Version Carryover"* na inaendelea kufanya kazi. Hivyo, Kamati imeamua kuiondoa hoja hii kwa vile tayari imeshatekelezwa na inafanya kazi.

Hoja nambari 4.1.2.22: Mfumo kutofanyiwa majaribio na watumiaji (User Acceptance Testing) Wakuu (Core Team Users) wa Moduli ya Bajeti

Ukaguzi ulibaini kwamba utengenezaji wa mfumo wa BAMAS haukuzingatia Miongozo ya Viwango Bora Kubalifu (best practice) katika utengenezaji wa mifumo ya TEHAMA kama vile "Software Development Life Cycle (SDLC)".

Hali hii ilibainika kupitia mahojiano na majadiliano yaliyofanywa na ukaguzi kwa watumishi wa Idara ya Bajeti ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ambapo ilifahamika kwamba miongoni mwa hatua muhimu katika utengenezaji wa mifumo ya TEHAMA ni hatua ya kufanya majaribio ya mfumo (UAT) ili kubaini kama mfumo umekidhi mahitaji ya watumiaji, hali hii haikuzingatiwa ipasavyo na kwamba eGAZ iliunda mfumo kwa kushirikisha watumishi wachache katika Idara ya Bajeti na kupelekea watumishi waliobaki kukosa uelewa wa kutosha wa utendaji wa mfumo wa BAMAS katika eneo la kusimamia Bajeti ya Serikali (Budget Management).

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kuzingatia Miongozo ya Viwango Bora kubalifu vya TEHAMA katika utengenezaji wa mifumo kama vile “SDLC” ambayo inahakikisha kwamba mifumo inayotengenezwa inatumia gharama ndogo na kukamilika kwa wakati pamoja na kuzingatia hatua zote muhimu kwa uzito unaostahili na kuepusha kufanya kazi moja zaidi ya mara moja (double works) zitakazoigharimu taasisi muda mrefu na fedha nyingi bila sababu.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ziliteua wataalam ambao wanafahamu taratibu zote zinazohusiana na matumizi na bajeti. Wataalam hao walitoka katika vitengo tofauti kwa ajili ya utengenezaji wa Mfumo wa BAMAS.

Mfumo ulipokamilika mafunzo yalitolewa kwa wataalamu wanaohusika (core fuction) na walipitishwa kipengele kwa kipengele ili kupata mapendekezo zaidi na hayo ndio ilikua majaribio ya moduli ya bajeti kwa Core Team ambayo yalifanyika kuanzia tarehe 17/08/2022 mpaka 25/08/2022.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia ukweli wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa Mfumo wa BAMAS ulitarajiwa kutumika tangu mwaka 2022 lakini ulishindikana kutumika kutokana na kuwepo baadhi ya Wafanyakazi waliokuwa hawapo tayari kuacha kutumia Mfumo wa awali. Vile vile, Mkaguzi aliomba ripoti ya majaribio pamoja na orodha ya watumiaji katika majaribio yaliyofanyika ili zweze kutathmini kufanyika kwa majaribio hayo lakini hakuweza kupatiwa.

Ili kuondoa utata uliojitokeza katika majibu na maelezo ya Mkaguzi, Kamati ya PAC imetaka ipatiwe vielelezo vya orodha ya waliohudhuria kikao cha mafunzo hayo pamoja na kukutana na baadhi ya Maafisa kutoka katika Taasisi zifuatazo waliohudhuria ili iweze kufanya tathmini juu ya kufanyika kwa mafunzo husika:

a) Mfanyakazi mmoja kutoka Idara ya Bajeti.
b) Mfanayakazi mmoja kutoka Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali.
c) Muhusika kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.
d) Muhusika kutoka Wizara ya Afya.
e) Muhusika kutoka Wizara inayohusiana na Tawala za Mikoa.
f) Muhusika kutoka Manispaa ya Mjini.
g) Muhusika kutoka Baraza la Mji Chake Chake.
h) Muhusika kutoka Halmashauri ya Micheweni.

Wengine ni Wahusika kutoka Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar:

a) Muhusika kutoka Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo;
b) Muhusika kutoka Jeshi la Kujenga Uchumi; na

c) Muhusika kutoka Chuo cha Mafunzo.

Kamati pia imeelezwa kwamba Mfumo huu ni mzuri ukilinganisha na Mfumo uliopita kwa vile unaweza kupatikana muda wowote katika sehemu ambayo muhusika yupo (haina haja ya kwenda Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango). Kamati imeibakisha hoja hii hadi itakapokutana na Wahusika waliopatiwa mafunzo hayo ili kuthibitisha kilichoelezwa na Mamlaka.

Maagizo ya kamati ya PAC

Kamati inautaka uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao kuendelea kuwapatiwa mafunzo wahusika pamoja na kuwafuatailia ipasavyo ili kuhakikisha matumizi mazuri ya Mfumo huu.

Hoja nambari 4.1.2.23: Kukosekana kwa nyaraka muhimu za utengenezwaji wa Mfumo wa BAMAS

Ukaguzi uliomba nyaraka mbalimbali zilizotumika kutengeneza Mfumo wa BAMAS, hadi ukaguzi unakamilika Uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao haukuweza kuupatia ukaguzi nyaraka zilizoombwa ikiwemo Nyaraka ya Usanifu wa Mfumo, nyaraka zinazoonesha mahitaji ya watumiaji wa mfumo, nyaraka za kufanya majaribio ya mfumo, pamoja na nyaraka mbali mbali za usanifu wa mfumo wa BAMAS kwa ajili ya kufanya mapitio ya namna mfumo ulivyosanifiwa ili kupima utekelezaji wa miongozo ya viwango bora kubalifu vya TEHAMA (best practices) katika hatua ambayo mfumo ulikuwa umefika.

Kukosekana kwa Nyaraka hizi muhimu kumepelekea kutofanyika kwa mapitio ya usanifu na usanidi wa mfumo wa BAMAS, aidha hali hii imekwamisha ufanyaji wa tathmini za majaribio yaliyofanyika wakati wa utengenezaji wa Mfumo huo ili kuthibitisha ushiriki wa makundi mbalimbali ya watumiaji wa mfumo katika hatua za utengenezaji wa mfumo jambo ambalo linapelekea kuinyima Serikali fursa ya kushauriwa kuhusiana na Usalama, Usiri, Uadilifu na upatikanaji wa taarifa za kibajeti, mapato na matumizi pamoja na madeni ya Serikali katika mfumo wa BAMAS.

Aidha, Serikali imekosa fursa ya kupata ushauri sahihi kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na matumizi endelevu ya mfumo huu yatakayohakikisha kwamba Serikali inanufaika na uwekezaji uliofanyika katika mfumo wa BAMAS kwa kutumia fedha za Umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kuhakikisha kwamba unaandaa Nyaraka zote ambazo ni muhimu sana katika kuendeleza mfumo wa BAMAS na kuhakikisha kwamba Serikali inaweka mikakati ya matumizi endelevu ya Mfumo ambayo yanazingatia usalama, usiri, uadilifu na upatikanaji wa taarifa za kibajeti, mapato na matumizi pamoja na madeni ya Serikali.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Wakati wa ukaguzi ni kweli baadhi ya nyaraka zilikua hazipo hii inatokana na mfumo ulikua upo katika majaribio,kwa sasa nyaraka zote muhimu za Mfumo zinapatikana.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa wakati ukaguzi unafanyika, Mfumo wa BAMAS ulikuwa katika hatua ya utengenezaji. Hivyo, kuna nyaraka hazikuwepo. Hata hivyo, Kamati imegundua kuwa kuna baadhhi ya nyaraka ambazo huhitajika katika kipimdi cha awali (cha utengenezaji Mfumo) nazi hakupatiwa Mkaguzi. Kamati imelitambua hilo baada ya kutaka kupatiwa nyaraka hizo lakini haikupatiwa zikiwemo nyaraka ya Usanifu wa Mfumo, nyaraka zinazoonesha mahitaji ya watumiaji wa mfumo, nyaraka za kufanya majaribio ya mfumo, pamoja na nyaraka mbali mbali za usanifu wa mfumo wa BAMAS.

Kwa upande wa nyaraka ya majaribio ya Mfumo, Kamati imeelezwa kwamba majaribio yamefanyika na yanaendelea kufanywa kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na mafunzo ya utumiaji Mfumo kwa Watendaji wa Idara ya Bajreti na Idara ya Muhasibu Mkuu wa Serikali (Hazina) tayari yameshafanyika.

Maagizo ya kamati ya PAC

Uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao uhakikishe unakuwa na mashirikiano ya karibu na Mkaguzi wakati anapotekeleza majukumu yake ya ukaguzi na anapohitaji nyaraka apatiwe ili asiweze kuandika hoja zenye majibu.

Kamati inautaka Uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kuhakikisha unaandaa nyaraka zote ambazo ni muhimu zaidi katika kuendeleza mfumo wa BAMAS.

Uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao iweke mikakati ya matumizi endelevu ya Mfumo ambayo yanazingatia usalama, usiri, uadilifu na upatikanaji wa taarifa za kibajeti, mapato na matumizi pamoja na madeni ya Serikali.

Hoja nambari 4.1.2.24: Kukosekana kwa sehemu kubwa ya Ripoti za Bajeti katika Mfumo wa BAMAS

Ukaguzi ulibaini kwamba sehemu kubwa ya Ripoti mbali mbali za Bajeti hazikuwa tayari katika mfumo wa BAMAS kwa ajili ya matumizi ambapo tuligundua kwamba kati ya Ripoti 122 zinazohitajika na watumiaji wa mfumo ni ripoti 15 pekee ndizo zilizokuwepo katika mfumo wa BAMAS sawa na asilimia 12 ya ripoti zote.

Uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao Kukosekana kwa ripoti hizo kunapelekea mfumo wa BAMAS kutokuwa tayari kwa ajili ya kuanza kutumika kwa kuingiza bajeti za Serikali kwasababu hautaweza kutoa ripoti zinazotakiwa kupelekwa katika Baraza la Wawakilishi kujadiliwa na hatimaye kuidhinishwa kabla ya kuanza kutumika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kufanya tathmini ya mahitaji ya watumiaji wa mfumo katika maeneo yote kuanzia Bajeti, Mapato, Matumizi na Ripoti mbalimbali zinazohitajika ikiwa ni pamoja na ripoti za Bajeti kama zilivyofanyiwa uchambuzi hapo juu na kuchukuwa hatua stahiki za kutekeleza mapungufu yote yaliyomo katika mfumo huo kwa kuwashirikisha watumiaji wa mfumo katika kila kitengo/ seksheni hatua kwa hatua na kuhakikisha kwamba inaandaa taarifa za utekelezaji ambazo zitapatikana kwa ajili ya ukaguzi.

Hali halisi iliyopo ya upatikanaji wa ripoti dhidi ya mahitaji ya ripoti za Mfumo wa BAMAS ni kama inavyoonekana katika Mchoro hapo chini:

Jadweli Nambari 30: Hali halisi ya utekelezaji wa mahitaji ya ripoti ya watumiaji wa mfumo wa BAMAS



Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Mfumo wa BAMAS ni mfumo unaotatua changamoto nyingi za Ripoti hasa katika maeneo ya mipango na bajeti. Mfumo huu kutokana na ukubwa wake kwa “Phase” hii ya awali umelenga zaidi kuangalia mahitaji yanayoendelea kutumika na baada kukamilika kwa mahitaji hayo, mfumo utakwenda mbali zaidi kwa kuleta maboresho ya maeneo mengine yanayohitajika.

Kwa upande wa Ripoti mfumo umekamilisha ripoti zote zinazohitaji kwa matumizi ya bajeti na tayari zimepitiwa na wataalamu kutoka Idara ya bajeti ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango. Ripoti hizo zinapatikana kwenye mfumo kwa “sever” za “Live” na “sever” za majaribio yaani “Test Sever”.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake katika Wakala huu, ni kweli Ripoti za Mfumo zinazohitajika na watumiaji wa mfumo wa BAMAS zilikuwa hazipo. Hali hiyo ilisababishwa na kutokukamilika kwa Mfumo huo. Hata hivyo, kwasasa zaidi ya asilimia 80 ripoti zake zinapatikana ndani ya Ripoti husika na Kamati imeridhks nayo. Hoja hii inabakia kwa hatua za kujiridhisha kukamilishwa mchakato wa upatikanaji wa Ripooti hizo.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inautaka Uongozi wa Wakala kuhakikisha unakamilisha upatikanaji wa asilimia 20 liyobakia ya Ripoti zinazohitajika na watumiaji wa mfumo ili hoja iweze kuondoka.

Hoja nambari 4.1.2.25: Kutokamilika kwa Moduli ya Mapato katika Mfumo wa BAMAS

Ukaguzi ulibaini kwamba Moduli ya kuratibu masuala ya Mapato (Revenue Management Module) haijakamilika katika mfumo wa BAMAS, aidha, ilibainika pia kwamba watumiaji wa Mfumo katika eneo hili hawana uelewa wa kutosha kuhusiana na utendaji kazi wa Mfumo wa BAMAS jambo linalotilia shaka mpango wa Wakala wa Serikali Mtandao katika kuhakikisha kwamba watumiaji wote wa mfumo huu wanashirikishwa ipasavyo na kwamba wanapata uelewa kamili wa namna mfumo unavyofanya kazi katika vitengo/ seksheni zao kulingana na mahitaji yao.

Kutokamilika kwa Moduli ya kusimamia mapato ni kikwazo kikubwa katika uratibu, udhibiti na usimamizi wa mapato unaofanywa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kupitia Idara ya Muhasibu Mkuu wa Serikali jambo linaloweza kuathiri kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa taarifa sahihi za mapato ya nchi ambazo huwasilishwa kupitia ripoti za mwisho wa mwaka zinazoandaliwa na Muhasibu Mkuu wa Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kuyafanyia kazi mapungufu hayo kwa kuzingatia umuhimu wa usimamizi wa ukusanyaji wa mapato pamoja na upatikanji wa taarifa sahihi zilizokamilika kwa wakati muafaka.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Wakati wa ukaguzi Moduli ya Mapato ilikua haijakamilika. Kwa sasa Mfumo wa BAMAS tayari umefanya muunganiko baina ya Mfumo wa Mapato wa

ZanMalipo na tayari majaribio yamefanyika ya kuhamisha taarifa hizo za mapato na kuzihamisha kwenye mfumo wa BAMAS.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Hoja hii tayari imeshatekelezwa ambapo kwasasa Moduli ya kuratibu masuala ya Mapato (Revenue Management Module) imeshaandaliwa na kupelekea Mfumo wa Mapato wa ZanMalipo kusomana vizuri na Mfumo wa BAMAS. Kukamilika kwa Moduli hiyo imesababisha Mapato ya Serikali kuongezeka kwa vile imepunguza mwanya wa upotevu wa mapato yetu. Hoja hii imeondolewa na Kamati kwa vile imeshatekelezwa.

Maagizo ya kamati ya PAC

Kamati inautaka Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao inaisimamia vyema Moduli ya kuratibu masuala ya Mapato (Revenue Management Module) ili iweze kuongeza zaidi mapato yetu.

Hoja nambari 4.1.2.26: Kukosekana kwa ufahamu wa kutosha wa namna Mfumo unavyofanya kazi kwa watumishi wa Idara ya Bajeti na Muhasibu Mkuu wa Serikali

Ukaguzi ulifanya mapitio kwa watumiaji wa mfumo wa BAMAS katika Idara ya Bajeti na Mhasibu Mkuu wa Serikali na kubaini kwamba wafanyakazi wa Idara hizo bado hawana uwelewa mzuri wa matumizi ya mfumo huo pamoja na kuwa wao ndio wanaotakiwa kuendesha na kutoa elimu kwa wengine kwa upande wa Bajeti, Mapato na Matumizi pamoja na Hesabu za mwisho wa mwaka (final accounts). Aidha, Idara ya bajeti na Idara ya Muhasibu Mkuu wa Serikali imedai kutokupatiwa mafunzo ya kutosha juu ya matumizi ya mfumo huo.

Kutokuwa na ufahamu wa kutosha wa mfumo wa BAMAS kwa Idara hizo ambazo ndizo watumiaji wakuu wa mfumo wa BAMAS kunaweza kupelekea Serikali kupata hasara kubwa kwa kuingia gharama nyingi za kutengeneza mfumo wa BAMAS ambao unaweza kutotumika ipasavyo na kutoongeza tija na ufanisi uliokusudiwa Serikalini. Aidha, hali hii inaweza kuwa chanzo kikuu cha kukosekana kwa matumizi endelevu ya mfumo huu wa BAMAS Serikalini.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao, kufanya tathmini ya uhitaji wa mafunzo ya mfumo wa BAMAS kwa wafanyakazi wa Idara ya Bajeti, Idara ya Muhasibu Mkuu wa Serikali na kuwapatia mafunzo ili kuhakikisha kuwa mfumo huo utakapoanza kutumika hakuna mapungufu ya uelewa wa mfumo kwa watumiaji.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Idara ya bajeti imeshafanyiwa mafunzo juu ya utumiaji wa mfumo wa BAMAS na kila mtendaji tayari amepatiwa “Account” itakayomuezesha

kuingia kwenye mfumo wa majaribio “Test App” na kufanya majaribio yatakayomuezesha ufahamu zaidi wa mfumo, Kwa muduli ya Bajeti vile vile mfumo huu wa BAMAS tayari umeanza kutumika kwa uingizaji wa taarifa za mipango na kibajeti ambapo zoezi hili la uingizaji linapofanyika, watumishi wa idara ya Bajeti ndio wanaohusika na usimamizi wa “user”

Kwa upande wa Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, watumishi wameshapatiwa mafunzo ya kutosha juu ya utumiaji wa mfumo wa BAMAS.

Uchunguzi na Maagizo wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa uchunguzi na Maagizo wa Kamati ya PAC kuhusiana na hoja hii unalingana na hoja nambati 4.1.2.22 (rejea hoja husika).

Hoja nambari 4.1.2.27: Kukosekana kwa Ripoti za Kihasibu (final accounts) katika mfumo wa BAMAS zinazoendana na mahitaji ya sasa ya Serikali

Ukaguzi ulibaini kuwa Mfumo wa BAMAS haujawekewa ripoti za “final accounts” ambazo zinaendana na matakwa ya sasa ya utendaji yaani” Cash Basis Final Accounts”.

Kukosekana kwa ripoti hizo ambazo ni za lazima katika uhasibu zinazotolewa kila mwisho wa mwaka kunarudisha nyuma utendaji wa Idara ya Muhasibu Mkuu wa Serikali na kupelekea mfumo utakapoanza kutumika watumishi waandae Ripoti hizo kwa mikono (manually).

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kujipanga vyema kwa kuandaa mpango kazi utakaozingatia mapungufu yote yaliyomo katika mfumo wa BAMAS na kuonesha muda utakaotumika kutatua mapungufu hayo kwa kila eneo la watumiaji wa mfumo na kuyatatua kwa haraka iwezekanavyo Kabla mfumo haujaanza kutumika (Live Operations).

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Ni kweli wakati wa ukaguzi mfumo wa BAMAS ulikuwa unakosa baadhi ya ripoti kwa kuwa mfumo ulikuwa katika hatua za majaribio na ulikuwa haujaanza kutumika rasmi.

Kwa sasa mfumo umekamilika na tayari ripoti za “final accounts” zinapatikana katika Mfumo wa BAMAS.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Ni kweli kwamba wakati Mkaguzi anafika Mamlaka ya Serikali Mtandao kutekeleza kazi zake, Ripoti za Kihasibu (final accounts) katika Mfumo wa BAMAS zinazoendana na mahitaji ya sasa ya Serikali zilikuwa hazimo katika Mfumo huo. Hili lilitokana na kutokukamilika kwa matengenezo yake, ila kwasasa RIpoti zote zinazohitajika kwa matumizi wa Wahasibu zinapatikana

ndani ya Mfumo wa BAMAS. Miongoni mwa Ripoti hizo ni “user manual” inayotumiwa na waandaaji wa Bajeti, ‘Operational’ za “Cash Management Report”, “Ananlytical Report” pamoja na “Consolidation Report”. Kwa msingi huu, hoja hii imeondolewa na Kamati.

OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI, NA UTAWALA BORA (OR-KSUUB)

Hoja Nambari 4.1.3.1: Kukosekana kwa nyaraka muhimu za Utengenzwaji wa Mfumo

Kwa mujibu wa Muongozo wa eGA nambari eGA/EXT/BSA/008 wa Utekelezwaji wa Miradi ya TEHAMA, wa mwaka 2020 unahitaji mradi wa TEHAMA unapotekelezwa lazima ufuate taratibu na mbinu "Methodology" ya Project Development Life Cycle – PDLC. Mbinu hiyo imekusanya hatua tofauti za mchakato wa utengenezwaji wa mfumo.

Aidha, kifungu nambari 2.3 cha muongozo huo kimefafanua kwamba kwa kila hatua kutakuwa na matayarisho ya nyaraka ambazo zitasaidia katika utengenezwaji, uendeshaji, usimamizi na udumishaji wa mfumo. Baada ya kukamilika kwa mradi kutakuwa na mpango wa kusimamia na kudumisha mradi ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi na kuendelea kutoa huduma bora kama ilivyokusudiwa.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya Mradi wa TEHAMA wa Uanzishwaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Mishahara na Rasilimali Watu (HR and Payroll Information Management System) uliotengenezwa na Kampuni ya ENGO kupitia Mradi wa PFMRP mwaka 2021 kwa gharama za shilingi 59,000,000. Mfumo huo unatumika katika Wizara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na unasimamiwa na OR-KSUUB kwa kushirikiana na eGAZ.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa dosari mbali mbali kwenye mchakato wa utengenezaji, uendeshaji, usimamizi na udumishaji wa mfumo wa HR-Payroll Information System, baadhi ya dosari zilizobainika ni kama zifuatazo: -

Ukaguzi uliomba nyaraka mbali mbali za utengenezwaji wa mfumo wa HR-Payroll Information System, lakini hadi ukaguzi unakamilika baadhi ya nyaraka hazikuweza kupatikana. Miongoni mwa nyaraka zilizokosekana ni kama zifuatazo:-

1. Ripoti ya Pendekezo la Mradi (Project Proporsal Report / Business Case) kuhusiana na uanzishwaji wa Mfumo inayoeleza kwa ufupi hatua mbali mbali za utengenezwaji wa mfumo pamoja na kuchambua kwa kina gharama zote za fedha zitakazotumika kwenye kila kipengele cha mradi huo (Project Breakdown Cost).
2. Ripoti ya kufanyika kwa Tathmini ya Vihatarishi vya Mradi (Risk Assessment Report).
3. Mpango wa kusimamia, kuzikabili na kuziepuka hatari zinazoweza kujitokeza kwenye utekelezaji wa Mradi (Risk Management Plan).
4. Ripoti ya hali ya Mradi iliyofikia (Progress Project Report) pamoja na gharama zilizokuwa zimetumika kabla ya kumalizika kwa mradi huo

wa utengenezwaji wa mfumo kwa mujibu wa kifungu cha 6.4(a) cha Masharti Maalum ya Mkataba (SCC).

5. Ripoti ya uthibitisho wa kukubalika kwa utendaji kazi katika majaribio ya mifumo (UAT Report).
6. Ripoti ya Kuhakiki Ubora wa Mfumo (Quality Assurance Report) kwa mujibu wa Mpango wa kusimamia Ubora (Quality Management Plan) uliopo.
7. Kodi za kutengenezea Mfumo “Source Codes”.
8. Barua ya kukubalika Mfumo (Acceptance Letter).
9. Muongozo wa mtumiaji wa Mfumo (Application User Manual).

Kukosekana kwa nyaraka hizo kunatoa ishara kwamba kuna udhaifu katika mchakato wa utengenezwaji wa mfumo wa TEHAMA kutokana na kutokuzingatiwa kwa Muongozo wa utekelezaji wa miradi ya TEHAMA wa eGA nambari eGA/EXT/BSA/008 pamoja na miongozo ya kimataifa ya utengenezwaji wa Mifumo ya TEHAMA (SDLC).

Aidha, kukosekana kwa nyaraka hizo kunaweza kusababisha hatari (risk) ya kutengenezwa mifumo isiyokuwa na tija na ufanisi wa utendaji kazi na kupelekea kushindwa kufi kia malengo yaliyokusudiwa jambo ambalo linaweza kusababisha Ofisi kuingia gharama za ziada za marekebisho ya mfumo na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB kuhakikisha unazingatia na kufuata kikamilifu miongozo na viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa katika utekelezaji wa miradi ya TEHAMA. Vile vile, Ofisi kuhakikisha nyaraka zote zinazohusika kwenye mfumo zinatengenezwa na kuwekewa kumbukumbu kwa kila hatua ili kupatikana ufanisi katika usimamizi na udumishaji na mifumo ya TEHAMA ya Ofisi.

Majibu ya Uongozi wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora

Mfumo wa HR-Payroll wakati wa utengenezwaji wake ilikidhi miongozo yote iliowekwa na Serikali Mtandao. Nyaraka zilizokosekana hazikuwa zikihitajika wakati kwa utengenezaji wake kwa wakati huo.

Kwa upande wa Muongozo wa mtumiaji wa Mfumo (Application User Manual) bado zinaendelea kutayarishwa kutokana na maboresho makubwa yaliyofanyika katika Mfumo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati haijaridhishwa na majibu ya Wizara kutokana na kwamba hoja ilijumuisha aina ya nyaraka ambazo wakati wa ukaguzi zilikosekana, na badala yake Wizara ilitakiwa kueleza uwepo ama kutowepo kwa nyaraka hizo na sababu zilizopelekea kutokuwepo kwa nyaraka ambazo hazipo.

Aidha, Kamati katika uchunguzi wake imebaini kwamba ripoti ama nyaraka zifuatazo hazikuatikana kwa uchunguzi :-

- Ripoti ya Pendekezo la Mradi (Project Proporsal Report / Business Case) kuhusiana na uanzishwaji wa Mfumo inayoeleza kwa ufupi hatua mbali mbali za utengenezwaji wa mfumo pamoja na kuchambua kwa kina gharama zote za fedha zitakazotumika kwenye kila kipengele cha mradi huo (Project Breakdown Cost).
- Ripoti ya kufanyika kwa Tathmini ya Vihatarishi vya Mradi (Risk Assessment Report).
- Mpango wa kusimamia, kuzikabili na kuziepuka hatari zinazoweza kujitokeza kwenye utekelezaji wa Mradi (Risk Management Plan).
- User acceptance test (UAT Report)

Kamati imebaini kwamba wizara ilimuachia “vendor” kila kitu bila ya kuhakikisha kwamba kuna miongozo, taratibu na tathmini ambazo zinahitaji kufanyika kwa wakati ili mfumo uweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaielekeza Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora kuhakikisha inafuata miongozo ya kitaifa, kikanda ama kimataifa katika kutengeneza mifumo ili kuhakikisha mifumo hiyo inaleta tija iliyokusudiwa

Hoja Nambari 4.1.3.2: Kuchelewa kukamilika kwa Mradi wa Utengenezwaji wa Mfumo

Kwa mujibu wa kifungu nambari 2.2 cha Masharti Maalum ya Mkataba (SCC) wa Uboreshaji wa Mfumo wa Mishahara wa Serikali (GPS), muda wa maboresho ya mfumo ulikuwa ni miezi minne (4) kuanzia tarehe 20 Mei 2021 hadi kumalizika mwezi wa Septemba, 2021.

Aidha Jadweli la Mpango Kazi wa Mradi limethibitisha kuwa kazi hiyo itafanyika kwa kipindi cha miezi minne (4) tu kuanzia mwezi wa Mei, 2021 hadi mwezi wa Septemba, 2021.

Moja kati ya maboresho makuu yaliyopangwa kufanyika ni kuingizwa taarifa kamili za rasilimali watu katika Mfumo wa zamani wa Mishahara (GPS) ili kwenda sambamba na mahitaji na kuweza kupatikana taarifa zote za watumishi pamoja na maslahi yao kwa ufanisi na kwa wakati.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba mradi huo umechelewa kumalizika kwa kipindi kirefu cha zaidi ya miezi 22 (mwaka mmoja na miezi kumi) na kuanza rasmi kutumika baada ya kumalizika kwa mafunzo ya mfumo mnamo mwezi wa Julai, 2023 badala ya mwezi wa Septemba, 2021.

Hali hii imesababishwa na kuwepo kwa udhaifu katika kukusanya mahitaji na kushirikisha ipasavyo watumiaji wa mfumo (user requirements) ili

kuweza kupata taarifa sahihi na kwa wakati katika kipindi cha utengenezwaji wa mfumo.

Kuchelewa kukamilika kwa mradi huo kumepelekea Taasisi za Umma kuchelewa kupata huduma za rasilimali watu kwa ufanisi kupitia mfumo wa HR-Payroll Information System na hatimae kudhoofisha utendaji kazi wa Taasisi hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB katika miradi ijayo kuhakikisha unakuwa makini katika kuanzisha miradi ya TEHAMA kwa kufuata kikamilifu miongozo na taratibu zote za utengenezwaji wa mifumo pamoja na nyaraka husika.

Majibu ya Uongozi wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora

OR-KSUUB inakiri kuwepo na kasoro zilizojitokeza ambazo zimechelewesha mfumo kufanya kazi kwa wakati uliopangwa. Zipo sababu nyingi ambazo zimepelekea kuchelewa kutumika kwa mfumo wa Mshahara wa Serikali (GPS). Miongoni mwa sababu hizo ni hizi zifuatazo -

Mfumo ulikua unamilikiwa na Wizara ya Fedha na shughuli zote zilifanyika huko;

Baada ya hapo mfumo ukawa unamilikiwa na Serikali Mtandao “eGaz”, pia shuguli zote zilikuwa zinafanyika huko;

Ilipofika mwaka 2023, mfumo ulikabidhiwa Ofisi na baada ya kukabidhiwa hakukuwa na ucheleweshaji na mara moja shughuli zote zilifanikishwa na mfumo kuanza kutumika ndani ya Serikali kama ilivyo kusudiwa.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba mfumo huu kabla ya kukabidhiwa kwa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora ulikua unamilikiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao, ambapo OR-KSUUB haikukabidhiwa rasmi nyaraka zote zinazohusiana na mfumo huo.

Aidha, Kamati inaipongeza OR-KSUUB kwa kusimamia vyema utengenezaji wa mfumo huo ambapo mfumo huo tayari imeshafanyiwa majaribio kwa kuunganishwa na mfumo wa BAMAS ambapo mfumo uliweza kutoa mpaka vocha. Kamati halkadhalika imebaini kwamba mfumo huo tayari imeshakamilika kwa asilimia Zaidi ya tisini (90%).

Hivyo, kamati imeridhika na jitihada zilizochukuliwa na OR-KSUUB katika kuhakikisha mfumo huo unaendelea ili uweze kuja kuleta tija iliyokusudiwa.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaiagiza Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGaz) kuhakikisha inakabidhi mfumo wa HR-Payroll Information System kwenda kwa OR-KSUUB kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa.

Hoja Nambari 4.1.3.3: Dosari katika Mfumo wa HR-Payroll Information System

Ukaguzi ulifanya mapitio ya Mifumo ya OR-KSUUB kwa kuangalia udhibiti wa taarifa uliopo ndani na nje ya mifumo hiyo. Baadhi ya mifumo mikuu iliyopitiwa kwa mwaka wa fedha 2022-2023 ni pamoja na Mfumo wa HR-Payroll Information System, Mfumo wa LADS, Mfumo wa elibrary na Tovuti ya Ofisi.

Katika ukaguzi huo dosari mbali mbali zimebainika na kutolewa na matokeo ya mapitio hayo ni kama ifuatavyo: -

Katika ukaguzi uliofanyika wa mfumo wa HR-Payroll Information System imebainika kwamba mfumo bado una mapungufu mengi katika utendaji kazi wake ambapo mapungufu hayo yasipofanyiwa kazi kuwepo yanawea kuathiri ufanisi wa mfumo na kusababisha kusababisha kukosekana kwa tija iliyokusudiwa. Baadhi ya mapungufu yaliyobainika ni kama ifuatavyo: -

a) Kutokafanya kazi kwa baadhi ya moduli za mfumo wa HR-Payroll System

Mfumo wa HR-Payroll Information Management System umekusanya jumla ya moduli kumi na sita (16) ambazo hutumika kwa shughuli zote za taarifa za rasilimali watu na mishahara kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuna baadhi ya moduli hazifanyi kazi licha ya kwamba mfumo unaendelea kutumika, moduli hizo ni kama zifuatazo:

• Moduli ya kutoa Ripoti “Reporting Module”

Moduli hii ilitarajiwa kutoa ripoti za aina zote zinazohusiana na taarifa za kiutumishi kama vile taarifa binafsi za mtumishi, mishahara, maposho, mikato, nyongeza, kupandishwa cheo, kushushwa cheo, masomo, adhabu, uhamisho, likizo, safari za kikazi n.k.

Aidha moduli hii ilitarajiwa kuweza kutoa ripoti hizo kwa vipindi tofauti vinavyohitajika kama vile kwa mwezi, miezi mitatu, miezi sita, kwa mwaka n.k ambapo ripoti hizo zilitarajiwa kupatikana katika mifumo tofauti kama vile mfumo wa pdf, spreadsheet, text file, JSON file, html file, Word file n.k.

Hivyo kutokana na kutofanya kazi kwa moduli hii kunapelekea Taasisi za Serikali kutoweza kupata ripoti za aina tofauti kama zilivyotajwa hapo juu.

• Moduli ya Kusimamia Bajeti “Budgeting Management Module”

Moduli hii ilitarajiwa kusimamia taarifa zote zinazohusiana na bajeti ya mishahara zinazotolewa kutoka katika Mfumo wa BAMAS ambapo taarifa hizo zingeonesha kiasi gani cha fedha kinachoombwa na Taasisi husika kwa ajili ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi kwa kila mwezi, kiasi gani kilichopo sasa na kiasi gani kinahitajika kwa ajili ya malipo ya area,

maposho, nyongeza n.k. ambapo taarifa hizo zingesaidia taasisi kupanga mikakati ya ajira kwa watumishi wanaostaafu na wanaohitajika.

• Moduli ndogo ya likizo

Sehemu hii ilitarajiwa kuonesha taarifa za likizo za mtumishi kama vile idadi ya siku za likizo alizonazo, tarehe ya kuanza likizo, tarehe ya kumaliza likizo n.k. ambapo taarifa hizo zingesaidia kuweka kumbukumbu nzuri ya likizo za wafanyakazi katika Taasisi za Umma.

Kutofanya kazi kwa moduli hizo kunasababisha kukosekana kwa baadhi ya Taarifa muhimu kama zilivyobainishwa hapo juu jambo ambalo linaweza kupelekea mfumo kuonekana hauna tija kama ilivyokusudiwa licha ya fedha nyingi kutumika katika utengenezwaji wake.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB kufanya jitihada za makusudi ili kuweza kuukamilisha mfumo huo na katika moduli zote kwa lengo la kuweka taarifa za kiutumishi na bajeti kama ilivyokusudiwa na hatimae kupatikana kwa tija na ufanisi wa utendaji kazi wa mfumo.

b) Kutokuwepo kwa Rejista la Mishahara "Salary Register" ndani ya Mfumo wa HR-Payroll Information System

Ukaguzi umebaini kwamba Mfumo wa HR-Payroll Information Management System hauna Rejista la Mshahara "Salary Register" ambapo lingeweza kuhifadhi taarifa zote za mishahara ya mfanyakazi kuanzia alipoajiriwa hadi atakapostaafu ili kuweza kusaidia kutoa taarifa za mishahara kwa usahihi wakati mfanyakazi anapostaafu.

Kutokuwepo kwa Rejista la Mishahara ndani ya mfumo kumepelekea kazi ya ujazaji wa taarifa za mishahara ya watumishi kwa kila mwezi kuendelea kufanyika nje ya mfumo kwenye makaratasi "manually" jambo ambalo husababisha ugumu na changamoto katika ujazaji na uwekaji wa kumbukumbu za taarifa hizo kwa Taasisi za Umma na kuonekana mfumo bado haujasaidia katika eneo hilo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB kufanya jitihada za kurekebisha dosari zinazobainika katika mfumo huo ili kuweza kupatikana ufanisi na tija iliyokusudiwa katika utendaji kazi wa mfumo.

c) Mfumo kushindwa kutoa "Notification"

Mtumishi anaekaribia kustaafu Sheria na taratibu za kiutumishi zinamtaka Mtumishi wa umma kupewa barua ya notisi ya kustaafu kazi miezi sita kabla, aidha inapofi ka siku chache kabla ya kustaafu mtumishi hukumbushwa tena na kutakiwa kurejesha rasilimali zilizochini ya umiliki wa Afi si pamoja na kuzuiliwa mshahara wake "block" ili kutoendelea kulipwa mshahara baada ya kustaafu kazi, kwa sasa mchakato wa kutoa taarifa za kustaafu kazi hufanyika kwa njia ya kawaida "manually".

Kwa mujibu wa mahitaji ya watumiaji, Mfumo wa HR-Payroll Information Management System ulitakiwa kuweza kutoa taarifa ya ukumbusho “Notifi cation information” kwa mtumishi wa umma anaekaribia kustaafu kazi ambapo taarifa hiyo ingetumwa kwa njia ya ujumbe mfupi “sms” kwenye simu ya mkononi au kwa njia ya barua pepe “email” ili kumkumbusha mtumishi husika siku zake chache alizobakisha kustaafu kazi. Aidha, kupitia taarifa hiyo uongozi wa Taasisi husika ungeweza kufanya maandalizi ya kustaafu kwa wakati bila ya kuchelewesha.

Ukaguzi umebaini kwamba Mfumo wa HR-Payroll Information System bado haujaweza kutoa taarifa ya ukumbusho wa kustaafu kazi (Notification Information) kwa njia ya “sms” au “email” kwa mtumishi wa umma anaemaliza muda wake wa utumishi ili kupata ukumbusho mapema na kufanya taratibu zote za kustaafu zinazotakiwa kwa wakati.

Mfumo kushindwa kutoa taarifa ya ukumbusho (Notification) kwa mtumishi anaekaribia kustaafu kunaweza kujitokeza ucheleweshwaji wa utengenezwaji wa maslahi ya mtumishi endapo wahusika, ya mtumishi akichelewa kupata taarifa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB kufanya marekebisho hayo mapema ili mfumo uweze kufanya kazi kama ilivyokusudiwa kwa kuweza kumjuulisha mtumishi kwa njia ya sms au baruapepe kabla ya kustaafu kazi ili kufanya maandalizi yanayohitajika kwa wakati bila ya kuchelewa.

Majibu ya Uongozi wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora

Dosari ya mfumo wa “HR-Payroll Information System”.

Kwa upande wa moduli ya kutoa Report inaendelea kufanyiwa kazi kulingana na mahitaji na kuweza kupatikana kwa vipindi tofauti ambapo kwa sasa zile report za msingi zinapatikana kwa kipindi cha mwezi mmoja kwa mfumo wa Pdf na spreadsheet.

Module ya kusimamia Bajeti tayari kwa sasa inafanya kazi na kama kutahitajika maboresho yoyote kipindi ambacho Mfumo unaendelea kutumika, moduli hiyo itaendelea kufanyiwa kazi.

Pia Mfumo wa HR-Payroll utengenezwaji wake ni kwa vipindi (Phases) mbili, kipindi cha kwanza kimekamilika kilichojumuisha uingizwaji wa taarifa za Wizara na Taasisi zinazolipwa na mfumo wa zamani wa ulipaji mishahara uliopo Wizara ya Fedha na tunatarajia kuanza kwa kipindi (phase) ya pili hivi karibuni ambayo imekusanya module ya likizo, mafunzo, kujumuisha mashirika ya serikali na mobile application ambayo itaweza kutoa taarifa binafsi za Mtumishi kupitia simu yake ya mkononi kwa njia ya sms au email, pia itaweza kutoa notifications zikiwemo za kustaafu kazi, siku za likizo zilizobaki na nyenginezo.

Dosari katika tovuti ya “www.utumishismz.go.tz"

ORKSUUB tayari imeshatengeneza Tovuti mpya ya Ofisi ambayo imekidhi viwango na miongozo yote iliowekwa na Serikali Mtandao. Utumiaji wa TOVUTI hii mpya itaondoa dosari zote zilizoainishwa hapo juu

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati kinsingi imeridhika na majibu ya Wizara pamoja na jitihada zilizofanyika katika kuifanyia kazi hoja hii ikiwa ni pamoja na kuweza kuongeza upeo na kuunganisha mfumo huo na mfumo wa BAMAS. Aidha, Kamati imebaini kwamba changamoto iliyotokea na ikapelekea mpaka hoja hii kuwepo ni ukweli kwamba OR-KSUUB imekabidhiwa mfumo kwa njia zisizo rasmi ambapo hakukua na nyaraka zozote muhimu ambazo zingeweza kuiongoza Wizara katika kuuendeleza mfumo huu.

Hoja nambari 4.1.3.4: Dosari katika Mfumo wa Legal Aid Database System (LADS)

Mfumo wa LADS ni mfumo ulioanzishwa na Wizara ya Katiba na Sheria mwaka 2020 na unasimamiwa na OR-KSUUB. Mfumo huo umetengenezwa na mtaalamu kutoka Dar es Salaam kwa gharama za shilingi 18,000,000 ukiwa na malengo ya kusajili na kuweka kumbukumbu za watoa huduma za msaada wa kisheria (legal service providers) kama vile Taasisi na Jumuiya za Kisheria, Wanasheria, Mawakili, Mavakili, Wasaidizi wa Kisheria n.k. ambapo taarifa zao za usajili, biashara, aina za huduma wanazotoa hupatikana kidijitali kupitia mfumo huo.

Ukaguzi ulifanya uhakiki wa mfumo na kubaini uwepo wa mapungufu mbali mbali, baadhi ya mapungufu hayo ni kama ifuatavyo: -

a) Kukosekana kwa msaada wa kiufundi “Technical Support” kutoka kwa mtengenezaji wa mifumo wakati zinapojitokeza changamoto kwenye mfumo, vile vile kutokuwepo kwa msimamizi wa mfumo “System Administrator” kwa upande wa Afi si jambo ambalo limepelekea umiliki wa mfumo wote (ownership) kubakia kwa mtengenezaji wa mfumo licha ya kwamba ORKSUUB ina wataalamu katika kitengo cha TEHAMA wanaoweza kusimamia mfumo huo na fedha nyingi zimelipwa kwa ajili ya utengenezaji wa mfumo.

b) Mfumo kukosa sehemu ya kusajili na kuingiza viambatisho (attachment) vya taarifa za Vituo vya Msaada wa Kisheria jambo ambalo limesababisha baadhi ya vituo kuendelea kutoa huduma za msaada wa kisheria bila ya kusajiliwa, kwa mfano kituo cha Msaada wa Kisheria cha M/Kwerekwe kinachosimamiwa na Zanzibar University pamoja na kituo cha Msaada wa Kisheria kinachosimamiwa na Mkurugenzi wa Mashtaka.

c) Kutokuwepo kwa taarifa muhimu (mandatory *) zinazohitajika wakati wa usajili ambazo taarifa hizo hujazwa kwa njia ya kuchaguliwa kutoka kwenye sehemu ya orodha na sio kuingizwa kwa mkono, kwa mfano taarifa za Shehia ambapo baadhi yao hazimo kama vile Tumbatu, Kiembe Samaki, Donge Mchangani n.k. Hali hii husababisha kujitokeza kwa ugumu kwa wanaosajili kutoka maeneo hayo.

d) Mfumo kukosa sehemu ya kuingiza tarehe, mwezi na mwaka wa usajili kwa Taasisi/Jumuiya. Aidha mfumo hauna taarifa za jinsia kwa Wanasheria, Mawakili na Mavakili ambazo zitaonesha utambuzi wao kwa vile kuna baadhi ya majina hutumika katika jinsia zote mbili, hivyo ripoti zinazotoka kwenye Mfumo hazioneshi jinsia ya mtoa huduma na wala tarehe kamili ya kusajiliwa jambo ambalo linasababisha ugumu kwa watendaji wa Afi si katika kuwafahamu na kuweka kumbukumbu za kiutendaji.

e) Cheti cha usajili kinachotolewa na OR-KSUUB kwa ajili ya kupewa watoa huduma baada ya kukamilika usajili hakina udhibiti wa utambulisho kama vile QR Code, Barcode n.k. ambapo udhibiti huo utasaidia kubainisha cheti feki na halisi.

f) Mfumo wa LADS haujaunganishwa na Mfumo mkuu wa malipo (ZANMALIPO) kwa ajili ya kutoa nambari za udhibiti wa malipo “Control Numbers”, vile vile wahasibu wa Afi si hawafanyi ulinganisho wa kibenki (Bank Reconcilliation) ili kuweza kulinganisha baina ya taarifa za kifedha kutoka katika akaunti na taarifa za kwenye mfumo.

g) Baadhi ya malipo hufanyika kwa Wakala, lakini mfumo hautambui uwepo wa Wakala katika orodha yake ya njia za malipo kutokana na kutoingizwa taarifa hizo, hivyo watoa huduma wanaolipia usajili kupitia wakala hupata ugumu wa kufanya usajili kwenye mfumo kutokana na risiti zao kushindwa kutambulika kwenye mfumo.

h) Kukosekana kwa udhibiti mzuri katika kufanya uhakiki “Verifi cation” na utambuzi “Validation” wa uhalali wa vyeti na risiti za malipo zinazowasilishwa na watoa huduma wakati wa usajili. Mchakato huo hufanyika kwa njia ya kawaida “manually” bila ya kutumia Control Numbers. Vile vile wakati wa (re-registration) mfumo unashindwa kutambua ikiwa kiambatisho cha risiti za malipo kishawahi kutumika nyuma kabla.

i) Watoa huduma wanaoendelea kufanya usajili kwa mwaka unaofuata (re-registration) mfumo huwalazimisha kuingiza baruapepe mpya na sio ya awali ambayo ilitumika wakati wa usajili wa mwanzo, hivyo watoa huduma hulazimika kutengeneza baruapepe mpya kila wanapofanya re-registration kwa mwaka mwengine jambo ambalo husababisha changamoto za mawasiliano kwa wateja wao kutokana na kubadilisha taarifa hizo kila muda.

j) Watoa huduma za msaada wa kisheria kila mwaka hutakiwa kuwasilisha ripoti za utendaji kazi katika Idara ya Msaada wa Kisheria iliyopo ORKSUUB ambapo ripoti hizo huwasilishwa kwa njia ya kielektroniki kwa kufanyiwa “attachment” kupitia mfumo wa LADS, dosari iliyobainika ni kwamba mfumo huo hauna sehemu ya kufanya “attachment” kwa ajili ya kuwasilisha ripoti za utekelezaji, kwa hivyo kunakuwa na changamoto kubwa katika kuwasilisha ripoti hizo kupitia mfumo ambapo watoa huduma hulazimika kutumia njia ya kudanganya kufanya usajili mpya ili kupatikana sehemu ya “attachment” ya vyeti na risiti za malipo na ndio hutumika kwa kuwasilisha ripoti zao. 2022 - 2023 2022 - 2023 Ripoti ya Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Taasisi za SMZ kwa mwaka wa fedha.

k) Mfumo haujazingatia mahitaji na vigezo vya kiusalama vya utengenezwaji wa nenosiri “password requirement” kutokana na kubainika mfumo kuweza kutengeneza nenosiri kwa kutumia nambari pekee.

l) Baadhi ya Ripoti zinazotolewa katika mfumo hazioneshi uhalisia na usahihi wa taarifa zake, hadi ukaguzi unakamilika ripoti za waliosajiliwa zilikuwa zinaonesha kwamba jumla ya taasisi na watoa huduma wote waliosajiliwa katika mfumo ni 318 ambapo idadi hiyo sio sahihi na usahihi ni kwamba idadi iliyopo ni 272, Changamoto hiyo imejitokeza kutokana na mfumo kuchanganya taarifa za watoa huduma wapya wanaojisajili na wanaoendelea kujisajili katika sehemu moja na kuwahesabu kama wasajiliwa wapya bila ya kuwatenganisha jambo ambalo watendaji wa Wizara wanaohusika na kazi hii hupata tabu ya kuwahesabu katika mfumo njia wanayotumia kuwahesabu ya mkono “manually” kwa kutumia vidole.

m) Baadhi ya nyaraka zinazohusiana na utengenezwaji wa mfumo wa LADS zimekosekana kwa ukaguzi jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 2.3 cha Muongozo wa eGA nambari eGA/EXT/BSA/008 wa Utekelezwaji wa Miradi ya TEHAMA, wa mwaka 2020. Nyaraka zilizokosekana ni kama zifuatazo: -

- Inception Report.
- User Requirement Document.
- System Requirement Specifi cation
- System Design Document.
- System Quality Assurance Report.
- User Acceptance Test Report.
- Training Report.

Kwa ujumla uwepo wa changamoto zilizotajwa hapo juu umesababishwa na ukosefu wa usimamizi, udhibiti na msaada wa kiufundi wa mfumo na vile vile kutokuwepo kwa mashirikiano baina ya Afi si na mtengenezaji wa mfumo ambapo dosari zake ni kwamba mfumo huo unaweza kupoteza taarifa au kuharibika na kusababisha hasara kwa Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB kuandaa mkakati imara wa kufanya marekebisho ya dosari zote zilizobainika katika mfumo huo kwa kushirikiana na mtengenezaji wa mfumo ili kuweza kuimarisha ufanisi na utendaji kazi wa mfumo na vile vile kuongeza usalama wa taarifa zilizomo.

Majibu ya Uongozi wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora

Mfumo wa Usajili wa Watoaji Msaada wa Kisheria umetengenezwa mwezi Januari mwaka 2020 kwa lengo la kuwasajili Watoaji wa Msaada wa Kisheria pamoja na Taasisi zao. Aidha, hatua mbali mbali zimechukuliwa zikiwa na lengo la kuondosha dosari zilizojitokeza kwa utaratibu ufuatao: -

Hatua kuhusu umiliki wa mfumo zimechukuliwa ambapo Mtengenezaji wa Mfumo ametakiwa kuondoa umiliki wa Mfumo kutoka kwa Mtengenezaji na kukabidhi kwa Kitengo cha TEHAMA cha Ofisi.

Bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 imezingatia kufanyiwa kwa mapitio Mfumo wa Usajili wa Watoaji wa Msaada wa Kisheria na hatua zimechukuliwa kwa kuwashirikisha Maafisa wa Kitengo cha TEHAMA kwa lengo la kuziondoa dosari zote zilizoonekana katika Taarifa ya CAG ikiwemo vipengele vyote kuanzia (a-l).

Kuhusu kipengele (m), wakati mfumo unataarishwa kwa upande wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar hakukuwepo na Mwongozo wa Utekelezwaji wa Miradi ya TEHAMA, hata hivyo, Ofisi itahakikisha inafuata Muongozo uliotolewa na Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar wakati itakapokuwa inafanya Mapitio ya Mfumo huo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Wizara imekiri kuwepo kwa mapungufu ambayo yamebainishwa na mkaguzi, na kuahidi kwamba mapungufu hayo tayari yameshaanza kuanyiwa kazi. Aidha, Kamati imeridhika na juhudi ambazo Wizara imezichukua katika kuhakikisha mapungufu hayo yanafanyiwa kazi.

Hoja nambari 4.1.3.5: Dosari katika Mfumo wa e-Library System

Mfumo wa Elibrary ni mfumo ambao umeanzishwa na OR-KSUUB kwa lengo la kuweka taarifa za kisheria katika sehemu moja ikiwa kama ni kitovu cha kitaifa cha taarifa za kisheria (One Stop Centre).

Aidha, mfumo huo husaidia kuweka mazingira ya maktaba katika hali ya kidijitali ili kuwawezesha majaji na maofisa wa sheria kupata taarifa kwa njia ya kielektroniki na kufanya tathmini kuhusiana na rasilimali mbalimbali za kisheria pamoja na ripoti za sheria, uamuzi wa mahakama, sera za Serikali n.k.

Mfumo huo umetengenezwa na mshauri elekezi (consultant) kutoka Zanzibar kwa gharama za shilingi 9,300,000 sawa na USD 4,026. Hata

hivyo, mkataba wa makubaliano haukupatikana kwa ukaguzi. Ukaguzi ulifanya jitihada za kupitia mfumo huo na kubaini uwepo wa dosari kama ifuatavyo: -

A) Kutofanya kazi kwa Mfumo wa e-library System

Mfumo wa e-library System umetengenezwa kwa lengo la kutumika katika Taasisi nne (4) za kisheria ambazo ni Mahkama ya Zanzibar, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Afisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na Skuli ya Sheria ya Zanzibar.

Ukaguzi ulifanya jitihada za kutaka kuhakiki mfumo huo kwa lengo la kupima utendaji wa kazi na kuangalia ikiwa unaenda sambamba na malengo ya Taaisisi yaliyokusudiwa. Hadi ukaguzi unakamilika mfumo ulikuwa umelala haufanyi kazi licha ya kuwa gharama za shilingi 9,300,000 zilikuwa tayari zimeshalipwa kwa mtengenezaji.

Kutofanya kazi kwa mfumo huo kumesababisha Taasisi nne (4) za Kisheria kukosa huduma za kisheria zilizopangwa kutolewa kupitia mfumo, aidha kumesababisha hasara ya shilingi 9,300,000 kutokana na kukosekana kwa tija iliyokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB kufanya jitihada za makusudi za kuufufua mfumo huo, kuusimamia na kuudhibiti ili uweze kudumu na kufanya kazi kwa weledi na ufanisi na hatimae kupatikana kwa tija iliyokusudiwa.

B) Kukosekana kwa baadhi ya taarifa za Utengenezwaji wa mfumo wa e-library System

Ukaguzi uliomba nyaraka zinazohusiana na utengenezwaji wa mfumo wa e-library System kwa lengo la kuweza kuzifanyia uhakiki ikiwa zimefuata vigezo kwa mujibu wa “TOR” pamoja na “Concept Note”. Hadi ukaguzi unakamilika baadhi ya nyaraka zilizoombwa hazikuwasilishwa kwa ukaguzi, nyaraka zilizokosekana ni kama zifuatazo: -

- Signed Contract/Agreements/Statement of Commitment for maintanance.
- Inception Report.
- System Quality Assurance Report.
- User Acceptance Test Report.
- Training Manual for the system.
- Work Report.

Kukosekana kwa nyaraka hizo kumepelekea ukaguzi kushindwa kufahamu na kutoa ushauri kwa Ofisi ikiwa mfumo umetengenezwa kwa mujibu wa mahitaji ya watumiaji “user requirements”, umekidhi vigezo vilivyohitajika, taratibu nzuri zilitumika katika kufanya majaribio ya utendaji kazi wa

mfumo, wadau wameshirikishwa ipasavyo na mafunzo yalifanyika kwa ufanisi.

Aidha kukosekana kwa nyaraka hizo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 4.0 cha matakwa ya “TOR” na vile vile kwenda kinyume na kifungu nambari 2.3 cha Muongozo wa eGA nambari eGA/EXT/BSA/008 wa Utekelezwaji wa Miradi ya TEHAMA, wa mwaka 2020.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa (OR) KSUUB kufanya mawasiliano ya karibu na mshauri elekezi kwa kumtaka atayarishe nyaraka zote zilizokosekana kwa mujibu wa hadidu rejea na kwa mujibu wa vigezo vya kitaifa na kimataifa. Nyaraka hizo zitasaidia katika kutatua changamoto za usimamizi na uendeshaji wa mfumo zinazojitokeza pamoja na kuwepo kumbukumbu zitakosaidia katika uimarishaji wa mfumo baadae

Majibu ya Uongozi wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora

Mfumo wa Elibrary ni mfumo ambao umeanzishwa na OR-KSUUB kwa lengo la kuweka taarifa za kisheria katika sehemu moja ikiwa kama ni kitovu cha kitaifa cha taarifa za kisheria (One Stop Centre).

Wizara imekuwa ikichukua juhudi mbali mbali za kuzifanyia kazi kasoro zilijitokeza katika uandaaji na matumizi ya mfumo huo ambao imebainika kwamba una kasoro kadhaa katika matumizi yake, kama ilivyobanishwa na kupendekezwa katika taarifa hii. Ofisi kupitia maafisa TEHAMA wa ndani imeanza kazi ya kuziondoa dosari zilizopo katika mfumo huo kulingana na mahitaji “Requrements” zinazoendana na miongozo iliyowekwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba ni kweli fedha za Tsh 9,300,000/- zimelipwa kwa mtengenezaji mfumo kutoka Zanzibar. Aidha, Kamati imesikitishwa na ukweli kwamba Wizara imelipa fedha hizo na mpaka Kamati inamaliza uchunguzi wake, mfumo huo bado haujaanza kufanya kazi.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaiagiza uongozi wa (OR) KSUUB kufanya mawasiliano ya karibu na mshauri elekezi kwa kumtaka atayarishe nyaraka zote zilizokosekana kwa mujibu wa hadidu rejea na kwa mujibu wa vigezo vya kitaifa na kimataifa. Aidha, Kamati inaielekeza Wizara kuhakikisha mfumo huo unakamilika na kuanza kutumika kwa wakati ili ulete tija iliyokusudiwa.

Hoja nambari 4.1.3.6: Kutokuwepo kwa leseni katika kanzidata "database" ya Mfumo wa HR-Payroll Information System

Mfumo wa HR-Payroll System hutumia "database" aina ya SQL Server 2019 kutoka kwa kampuni ya Biashara ya Microsoft ambapo kanzidata hiyo hutumika kwa ajili ya kuhifadhia taarifa zote za kiutumishi pamoja na mishahara kwa watumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa mujibu wa sera ya makubaliano ya leseni za Microsoft (End User License Agreement - EULA), ili utumie kanzidata ni lazima Taasisi ilipie leseni ya matumizi, baada ya kulipiwa kanzidata inakuwa halali na kupatiwa ulinzi, usalama na udhibiti mkubwa kutoka kwa kampuni hiyo na kulinda taarifa zilizomo dhidi ya mashambulizi ya virusi, udukuzi n.k.

Ukaguzi umebaini kwamba database ya mfumo wa HR-Payroll Information System haina leseni ya matumizi licha ya kwamba imehifadhi taarifa muhimu za watumishi na Viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa sasa kanzidata iliyoingizwa humo inatumia leseni ya majaribio tu ambayo haina muda mrefu wa matumizi na vile vile haina usalama wa kutosha.

Picha Nambari 1: Kanzidata ya toleo la majaribio ambayo inamaliza muda Januari, 2024

	SERVER NAME	INSTALLATION_DATE	VERSION	EXPIRY DATE
1	WIN-218IHV0KO35\MSSQLSERVER2019	2023-07-26 23:36:06.640	Enterprise Evaluation Edition (64-bit)	2024-01-22 23:36:06.640

Hali hii inaweza kusababisha hatari ya upotevu wa taarifa za kiutumishi na mishahara kwa viongozi na watumishi wa umma ikiwa kanzidata itashambuliwa, kuharibiwa na virusi au kudukuliwa kupitia mitandao jambo ambalo litapelekea kuingiza hasara kubwa Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB kuhakikisha unafanya jitihada za makusudi za kununua leseni ya matumizi ya kanzidata ya mfumo wa HR Payroll System ili kuziweka taarifa zake katika hali ya usalama dhidi ya hatari zilizopo.

Majibu ya Uongozi wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora

Mfumo wa HR-Payroll System hutumia "database" aina ya SQL Server 2019 kutoka kwa kampuni ya Biashara ya Microsoft ambapo kanzidata hiyo hutumika kwa ajili ya kuhifadhia taarifa zote za kiutumishi pamoja na mishahara kwa watumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Ripoti ya ukaguzi imekuwa na wasiwasi kuhusu hali ambayo inaweza kusababisha hatari ya upotevu wa taarifa za kiutumishi na mishahara kwa

viongozi na watumishi wa umma ikiwa kanzidata itashambuliwa, kuharibiwa na virusi au kudukuliwa kupitia mitandao jambo ambalo litapelekea kuingiza hasara kubwa Serikali.

OR-KSUUB imeshanunua leseni na tayari zimeshaingizwa katika “Softwares” zote zinazotumika kwa mfumo wa HR-Payroll System ikiwemo kanzidata ambayo imekusanya taarifa za Watumishi. Hivyo basi, hivi sasa Mfumo huu upo salama dhidi ya vihatarishi vinavyoweza kushambulia kanzidata na Mfumo kwa ujumla.

Aidha, katika kuongeza usiri, uadilifu na usalama wa kulinda taarifa za kiutumishi, mfumo unao uwezo wa kuchunguza shughuli zote zinazofanyika kuweka rekodi inayobainisha tarehe, muda, na akaunti ya kila kitende kitakachofanyika. Hali hii itaweza kusaidia kugundua vitendo chochote kitakachofanyika ambacho sio cha uadilifu ndani ya kazidata.

Ili kuepusha Kazidata kuchezewa, kufuta au kuharibu taarifa kwa wasiokuwa waadailifu, Ofisi imemuandaa mtu pekee ”Adiministrator” wa kusimamia na kuzifikia taarifa za uchunguzi zilizomo ndani ya kazidata ya mfumo “Data base Audit Logs”.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya Wizara na hatua ilizozichukua katika kuhakikisha mapungufu ambayo yameainishwa katika hoja hii yanafanyiwa kazi.

Hoja nambari 4.1.3.7: Kutofanyika kwa usanidi katika sehemu zinazoweka kumbukumbu za shughuli za watumiaji wa kanzidata ya Mfumo “database Audit logs”

Moja kati ya sehemu muhimu zinazopewa kipaumbele cha udhibiti kwenye kanzidata ni sehemu ya kuhifadhi kumbukumbu za shughuli za watumiaji “database audit logs”.

Sehemu hii hurikodi shughuli “activities” zote zinazofanywa na watumiaji wa kanzidata “database administrators and database users” ambapo hutumika kwa kuangalia ushahidi endapo tukio la kihalifu likifanywa kupitia kanzidata ya mfumo.

Ukaguzi ulifanya uhakiki wa kanzidata “database” ya mfumo wa HR-Payroll Information System na kubaini kwamba sehemu ya kuhifadhi “Audit logs” haijasanidiwa (not configured) kwa ajili ya kuchunguza na kuweka kumbu kumbu za matukio yanayofanyika ndani ya kanzidata.

Picha ifuatayo inaonesha kanzidata ya mfumo wa HR-Payroll Information System haijafanyiwa usanidi (not configured) katika sehemu ya Audit logs, kwa ajili ya kurekodi shughuli zote zinazofanyika ndani ya database.

Picha Nambari 2: Kanzidata ya Mfumo wa HR-Payroll Information System haijasanidiwa kwa ajili ya kunasa Audit Logs



Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB kuhakikisha kanzidata ya mfumo wa HR-Payroll Information System inasanidiwa ili kuweza kuchunguza, kubaini matumizi halisi na kuweka kumbukumbu za shughuli zote zinazofanyika ndani yake na akaunti yoyote inayohusika kufanya shughuli hizo. Hali hii itasaidia kupatikana kwa ushahidi wa kubaini tarehe, muda na akaunti iliyotumika kufanya kitendo kisichokuwa na uadilifu ndani ya kanzidata hiyo.

Aidha, katika kuongeza usiri, uadilifu na usalama wa kulinda taarifa za kiutumishi Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB kuhakikisha unamuandaa mtu pekee atakaetunza, kusimamia na kuzifikia taarifa za uchunguzi zilizo ndani ya kanzidata za mifumo “database audit logs” ili kuepusha kuchezewa, kufutwa au kuharibiwa na wasiokuwa waadilifu.

Majibu ya Uongozi wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora

Kuhusu kuhifadhi kumbukumbu na shughuli za watumiaji ORKSUUB tayari inaendelea kuyafanyia kazi maelekezo na mapendekezo yaliyotolewa kuhusu mfumo kuwa na uwezo wa kuhifadhi kumbukumbu za shughuli za watumiaji, ambapo hivi sasa tayari imeshatengeza “database ya audit logs” . Kwa hivyo, mfumo na uwezo wa kuweka ushahidi wa kumtambua aliyehusika kufanya vitendo vyenye kukiuka misingi ya uadilifu kama vile wizi, udukuzi, ufutaji wa taarifa bila ya idhini, ubadilishwaji wa data n.k.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imeridhika na jitihada ambazo OR-KSUUB katika kuhakikisha changamoto iliyoibuliwa na Mkaguzi inatatuliwa ili kuweza kudhibiti matumizi mabaya ya watu wasiokua na uadilifu katika mfumo wa HR-Payroll Information System.

Hoja nambari 4.1.3.8: Kukosekana kwa usalama katika Seva inayoendesha Mfumo wa HR-Payroll Information System (Application Server)

Ukaguzi umebaini kompyuta aina ya Seva ambayo imeingizwa Mfumo wa HRPayroll Information System haiko salama kiutendaji "Vulnerable" kutokana na kubainika kuwa haina leseni katika "Window Operating System". Vile vile imebainika haina programu ya kuzuwia mashambulizi ya virusi, programu hatarishi na udukuzi "antivirus software" licha ya kuwa kompyuta hiyo imeungwa na mtandao wa Internet. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika picha hapo chini: -

Picha Nambari 3: Mapunfugu ya usalama katika Seva ya Mfumo wa HR – Payroll Information System haiko salama



Seva yenye mfumo wa HR-Payroll System ambayo haina leseni ya Window Operating System, badala yake inatumia ya Window ya majaribio tu, vile vile ina ujazo mdogo wa nafasi, haina antivirus na inatumia internet

Aidha, imebainika kuwa Seva hiyo ina ujazo mdogo wa nafasi ya kuendesha mfumo wa HR-Payroll Information System kulingana na mahitaji ya mfumo wenyewe (System Requirement Specifi cation) ambapo kwa kiasi kikubwa

imesababisha mfumo kuwa na kasi ndogo ya utendaji kazi “slow performance” kwa vile mfumo huo unatumika takriban Taasisi zote za SMZ. Vile vile hali hii imepelekea baadhi ya taarifa kushindwa kuhifadhiwa kwa ufanisi ndani ya kanzidata za mfumo kama vile taarifa za application logs.

Kuwepo kwa usalama mdogo wa Seva hiyo kunaweza kusababisha hatari kubwa ya mfumo wa HR-Payroll Information System kupata mashambulizi ya virusi, udukuzi, utendaji mdogo wa kazi na hatari nyengine zisizojulikana jambo ambalo litapelekea mfumo kuharibika na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB kufanya jitihada za kuhakikisha Seva hiyo inaekewa leseni halisi “Original Window license” katika mfumo wa uendeshaji “Operating System” na vile vile inaingizwa programu ya kusaidia kuzuwia mashambulizi na hatari mbali mbali zinazotokana mashambulizi ya mitandao kama vile virusi, udukuzi n.k. na pia kuongeza uwezo ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Majibu ya Uongozi wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora

ORKSUUB imeshachukua hatua mbali mbali kwa ajili ya kuzifanyia kazi changamoto ziilizobainishwa hapo juu. Hivi saa, tayari imeshanunua leseni “Windows Server licence” kwa ajili ya seva inayotumia Mfumo wa HR-Payroll Information System na zimeshafanyiwa “installation” na Ofisi imeshanunua antivirus software ya ESET PROTECT COMPLETE (COMPLETE, MULTILAYERED PROTECTION FOR ENDPOINTS, CLOUD APPLICATIONS AND EMAIL, THE NUMBER ONE THREAD VECTOR) kwa ajili ya usalama wa Seva na Taarifa zinazohifadhiwa na Seva hiyo.

Pia Ofisi ipo katika hatua za kutengeneza miundo mbinu ya TEHAMA ndani ya Serikali. Miundo hii inatarajiwa kumtambua afisa “ICT Security Officer”, pamoja na kupewa majukumu yanayohusiana na kazi hizo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imeridhika na Majibu ya Wizara pamoja na juhudi zilizochukuliwa katika kuhakikisha mapungufu yaliyoonekana kwenye hoja hii yanafanyiwa kazi.

Hoja nambari 4.1.3.9: Dosari za kiusalama zilizobainika katika Chumba cha Mitambo (Server Room)

Ukaguzi ulitembelea katika chumba cha Mitambo (Server Room) cha OR-KSUUB Unguja kilichopo katika ghorofa ya sita ambapo chumba hicho vile vile hutumika kusimamia na kuendesha mitambo ya kamera za ulinzi (CCTV Camera) zilizofungwa kwa ajili ya kuweka usalama wa Afisi. Katika chumba hicho ukaguzi umebaini uwepo wa dosari mbali mbali kama zifuatazo: -

- Mitungi ya kuzimia moto (fire extenguishers) imekwisha muda wa matumizi (expired).
- Mfumo wa kugundua na kutoa ishara ya hatari ikiwa khitilafu za moto zikitokea katika jengo haufanyi kazi “Addressable Smoke & Heat Detector and Fire Alarm System”.
- Kipooza Hewa (Air Condition) kilichomo ndani ya chumba cha Seva hakifanyi kazi vizuri kutokana na kutofanyiwa “service” kwa muda mrefu.
- Kutokuwepo kwa kifaa cha usalama kinachodhibiti uingiaji wa watu mlangoni (door security device).

Hivyo, kuwepo kwa dosari za kiusalama zilizotajwa hapo juu kunaweza kusababisha upotevu wa taarifa na uharibifu wa mifumo na miundombinu ya Afisi iliyowekwa ndani ya chumba hicho.

Aidha, kwa upande wa CCTV kamera katika jengo la OR-KSUUB lenye ghorofa nane (8) ukaguzi umebaini kati ya kamera (16) zilizofungwa, kamera (11) zinaonesha na kamera (5) hazioneshi kutokana na changamoto mbali mbali.

Hata hivyo ukaguzi umebaini mtambo wa kuhifadhia kumbukumbu za matukio (NVR) yanayorikodiwa na CCTV kamera haufanyi kazi, kwa hivyo hakuna rikodi yoyote inayoingizwa katika mtambo huo licha ya kwamba kamera 11 zinaonesha. Jadweli lifuatalo linaonesha idadi ya kamera zilizofungwa na hali halisi ya utendaji kazi: -

Jadweli Nambari 4: Idadi ya Kamera zilizofungwa na Afisi

Eneo Husika	**Idadi ya Kamera zilizofungwa**	**Idadi ya kamera zinazofanya kazi**	**Idadi ya kamera zisizofanya kazi**
Nje ya jengo la Afisi	7	4	3
Ground Floor	4	3	1
1st Floor – 5th Floor	0	0	0
6th Floor	5	4	1
7th Floor – 8th Floor	0	0	0
Jumla ya Kamera	**16**	**11**	**5**

Kwa mujibu wa jadweli hapo juu kunaonesha kwamba idadi ya kamera zinazofanya kazi ni kidogo kulinganisha na ukubwa wa jengo ambapo baadhi ya ghorofa hazijafungwa kamera, kwa mfano ghorofa ya kwanza hadi ya tano na ya ghorora ya saba hadi ya nane.

Vile vile ukaguzi umebaini ufungaji wa kamera haukuzingatia vipaombele vya usalama wa maeneo waliopo Viongozi Wakuu wa Afisi katika jengo hilo, kwa mfano afisi za Mhe. Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na baadhi ya Wakurugenzi zipo katika ghorofa ya nne (4) lakini hakuna kamera

iliyofungwa kwenye ghorofa hiyo kwa ajili ya kuangalia usalama wao endapo tatizo lolote likitokea dhidi yao.

Kutofanya kazi kwa kamera za Afisi kunaweza kusababisha kukosekana kwa ushahidi endapo tukio lolote la wizi, uhalifu au uharibifu likitokea katika Afisi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB kuimarisha dosari zote zilizotajwa hapo juu zinazohusu CCTV kamera na chumba cha Mitambo ili kuongeza usalama, ulinzi na utendaji kazi wa vifaa vilivyomo katika chumba cha Mitambo kwani chumba hicho ni muhimu sana katika kusimamia na kuendesha mifumo na miundombinu ya Afisi.

Aidha, Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi kufanya jitihada za makusudi za kutengeneza au kubadilisha mtambo wa kuhifadhia kumbukumbu za matukio ya CCTV kamera na vile vile kuongeza idadi ya ufungaji wa kamera hususan katika ghorofa ya nne (4) ambayo viongozi wakuu wa Ofisi wapo hapo.

Majibu ya Uongozi wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora

Ofisi inaendelea kuzifanyia kazi changomoto zote hizi za kiusalama wa mifumo, jengo na ustawi wa viongozi zilibainika kwenye ukaguzi na zilikuwepo kabla ya kutolewa ushauri huo. Ofisi imefanya jitihada ya kubadilisha kipoza Joto (AC) kilicho bora na kinachofanya kazi vizuri zaidi katika kulinda ubora wa vifaa vilivyomo kwenye chumba cha mitambo kutokana na vumbi pamoja na hali ya joto hali ambazo ni hatarishi kwa uhai na utendaji kazi wa vifaa hivyo,

Kwa upande wa CCTV kamera.

katika kuimarisha usalama wa Jengo la Ofisi, Uongozi umefanya jitihada za makusudi za kutengeneza na kubadilisha mtambo wa kuhifadhi kumbukumbu za matukio ya CCTV kamera. Vilevile idadi ya kamera zimeongezwa na kufikia 44 ambapo mwanzo zilikuwa kamera kumi na sita (16). Aidha, katika kuzingangatia usalama wa jengo na maeneo muhimu ambayo Wakuu wa Ofisi wanapatikana pia tumeweka kamera kwa jengo zima, ambapo hivi sasa kila floor ina kamera za usalama zisizopungua nne (4). kamera zote arobaini na nne (44) zinafanya kazi vizuri.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imeridhika na hatua za utekelezaji zilizochukuliwa katika kuhakikisha kamera zote katika Jengo la Wizara zinafanya kazi vizuri pamoja na kuengeza idadi za kamera kutoka 16 hadi 44.

Aidha, Kamati haijaridhishwa na uhalisia kwamba mitungi ya kuzimia moto ambayo imekwisha muda wake bado haijabadilishwa, jambo ambalo

linapelekea kutokua na njia za utatuzi za haraka endapo majanga kama ya moto yakitokea.

Halkadhalika, Kamati imebaini kwamba mfumo wa kugundua na kutoa ishara ya hatari katika jengo bado haufanyi kazi, jambo ambalo linapelekea usalama mdogo kwa jengo kwa ujumla.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaiagiza Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora kuhakikisha wanaandaa bajeti kwa ajili ya ununuzi wa mitungi mipya ya kuzimia moto (fire extinguisher) pamoja na uwekaji wa mfumo wa kugundua na kutoa ishara ya hatari katika jengo la Wizara

MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI ZANZIBAR (ZAECA)

Hoja Nambari 4.1.4.1: Kukosekana kwa Mkataba wa Viwango vya Huduma (SLA Agreement) baina ya ZAECA, ZICTIA na TTCL

Mkataba wa Viwango vya huduma ni aina ya mkataba unaowekwa kati ya mtoa huduma na mteja, ukielezea viwango vya utendaji na ahadi zinazohusiana na utoaji wa huduma fulani.

Mkataba huu hua ni chombo cha kusimamia na kuhakikisha ubora wa huduma ambapo pande zote mbili zinakubaliana juu ya viwango maalum vya utendaji, mara nyingi vikiwa na vigezo vya kiufundi, muda wa kurekebisha matatizo (downtime), na mambo mengine yanayohusiana na huduma inayotolewa. Viwango vya Utendaji, Muda wa Ufikiaji (Downtime) Maelezo ya Huduma, Malipo na Adhabu, Muda wa Mkataba, Mchakato wa Kupima Utendaji.

Aidha ukaguzi uliofanyika ulibaini ZAECA haina Mkataba wa viwango vya huduma na Watoa huduma wao ambao ni ZICTIA na TTCL jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 4.3, nambari 4.1.6 na 4.1.7 cha Viwango bora vya kimataifa (Best Practice) ISO/IEC 20000 vinavyoelekeza uwepo wa Mkataba wa viwango vya huduma (SLA agreement) katika Huduma za TEHAMA kwenye Mashirika na Taasisi mbali mbali.

Kutokuwepo kwa Mkataba wa Viwango vya Huduma (SLA) kunaweza kuwa na athari mbali mbali haswa kwa wateja na watoa huduma, ikijumuisha kutokuwa na uhakika wa viwango vya utendaji, migogoro ya kuelewa vigezo vya huduma, kutokuwa na malalamiko yanayoweza kushughulikiwa kisheria pamoja na kutokuwa na kipimo wazi cha utendaji wa huduma fulani.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kuhakikisha unaandaa utaratibu wa upatikanaji wa Mkataba wa Viwango vya huduma (SLA Agreement) kutoka kwa watoa huduma wake wote.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar

ZAECA imefanya jitihada za kupata SLA baina yake na watoa huduma hao. Kwa upande wa ZICTIA baada ya kuwasiliana nao walieleza kuwa wataweka SLA kwenye mkataba mama wa huduma.

Hayo ni kwasababu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imewashauri bora waingize tu kwenye mkataba mama kama walivyokuwa wakifanya zamani kuliko kuwa na nyaraka mbili tofauti, hivyo wamefanya hivyo na tayari wametupa mkataba wao na wameingiza ndani yake vipengele vya SLA.

Kwa maelezo hayo ZAECA na ZICTIA sasa tayari tunayo SLA kwa huduma ya intaneti. **Kiambatanisho A**.

Upande wa TTCL nao tayari tumewasiliana nao na kuwapelekea rasimu ya SLA ambayo ni **kiambatanisho B** ili waipitie hatimae tuipitishe kwa pamoja.

TTCL wametueleza kuwa wameipeleka rasimu yetu Makao Makuu yao Dar es Salaam kwa mwanasheria wa kampuni, bado tunasubiria majibu kutoka kwao.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imeridhika kwa hatua ya utekelezaji ambao imechukuliwa na Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar. Kamati imeamua kuifuta hoja hii kwani tayari imeshatekelezwa.

Hoja Nambari 4.1.4.2: Kutozingatiwa kwa Utaratibu wa Utengenezaji wa Mifumo ya TEHAMA (Software Development Life Cycle

“Software Development Life Cycle – SDLC” ni mchakato wa kina unaotumika katika utengenezaji wa Programu za TEHAMA ambapo utaratibu huu wakitaalamu unajumuisha hatua tofauti ambazo hufuatwa kipindi cha uanzishwaji mpaka kumalizika kwa Mfumo husika.

Lengo kuu la SDLC ni kutengeneza mfumo unaokidhi matarajio ya watumiaji, kusaidia kutengeneza na kukamilisha Programu kwa wakati na bajeti iliyokusudiwa huku ikizingatia ubora wa mfumo husika.

Aidha, ukaguzi ulibaini kwamba utengenezaji wa mfumo wa “Case Distribution System” haukuzingatia utaratibu na mbinu za “SDLC” kwa sababu ya kukosekana kwa nyaraka mbalimbali zilizotakiwa kuwepo kama ushahidi wa kuzingatiwa kwa “SDLC”.

Hali hii inakwenda kinyume na matakwa ya viwango bora kubalifu (Best practice) ISO/IEC 12207:2017 kifungu nambari 7-24, kinachozungumzia utaratibu uliobora katika hatua za utengenezaji wa Mifumo ya TEHAMA katika Taasisi, ili kuhakikisha utekelezaji ulio bora na wa uhakika wa utengenezaji wa Mifumo ya TEHAMA.

Miongoni mwa hatua za Msingi za Utengenezaji wa Mifumo ya TEHAMA ambazo hazikuzingatiwa wakati wa utengenezwaji wa Mfumo wa Case Distribution System ni pamoja na: -

- Uchambuzi na Mahitaji ya watumiaji (Requirements Analysis).
- Ubunifu wa Mfumo (System Design).
- Upimaji/ Majaribio ya Mfumo (System Testing).
- Uwasilishaji wa Mfumo (System Deployment).
- Uendeshaji na Matengenezo (Operation and Maintenance).

Kutozingatiwa kwa hatua za Kitaalamu za utengenezwaji wa Mifumo ya TEHAMA (SDLC) kunachukuwa sehemu kubwa ya kuwa ni chanzo cha matatizo na changamoto mbali mbali za mifumo ya TEHAMA ikiwemo: -

- Ucheleweshwaji wa kukamilika kwa mifumo ya TEHAMA.
- Ubora hafifu wa mifumo ya TEHAMA inayotengenezwa.
- Mifumo kutengenezwa kwa gharama kubwa zaidi ya uhalisia wake
- Mifumo kutokukidhi mahitaji ya watumiaji.
- Kutokufikiwa kwa malengo ya Serikali katika uwekezaji kwenye TEHAMA

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kuhakikisha unazingatia taratibu za utengenezwaji wa mifumo ya TEHAMA kama vile “Software Development Life Cycle (SDLC), Project Development Life Cycle (PDLC)” n.k ili kuisadia Serikali kufikia malengo ya uwekezaji kwenye TEHAMA ambayo ni kuongeza tija, ufanisi, uwazi na uwajibikaji kwa wakati.

Aidha, katika mfumo huo uliotengenezwa, ukaguzi unashauri kuandaliwa kwa nyaraka zake zote muhimu kama vile nyaraka ya mahitaji, nyaraka ya usanidi, nyaraka ya namna mfumo unavyofanya kazi (operations manual), n.k na kwamba nyaraka hizo zipatikane kwa ajili ya ukaguzi

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar

ZAECA haina mfumo wa kielectroniki inaotumia katika kazi zake, isipokuwa katika kupunguza changamoto za kuhifadhi taarifa, ZAECA iliamua kutumia programu ya “access” ambayo ni kanzidata (database) inayopatikana kwenye programu za Microsoft office kutunzia taarifa zake. Ili uwe mfumo uwe unaweza kuisadia Taasisi kuhifadhi taarifa zake, kuchakata na kusaidia katika kufanya maamuzi kutokana na ripoti zinazopatikana kwenye mfumo.Mfumo wa aina hiyo ZAECA haupo.

Programu hii haina sifa za kuwa mfumo kwasababu zifuatazo;

- Haihusishi vipengele (components) vingi kwa pamoja, ina kanzidata peke yake, haina software applications, hardware na udhibiti wa namna ya ufanyaji kazi wake.
- Ipo kwenye computer moja peke yake haitumiki kwenye computer nyengine wala kupitia mfumo wa mawasiliano kama intaneti.

Programu hii inaweza kutumika kuwa ni moja kati ya vipengele vingi vinavyounda mfumo, programu hii kwa vile ni programu ya kanzidata basi nayo huweza kutumika kama kanzidata ya mfumo wa kielektroniki.

Hivyo, programu hizi za Microsoft Office kama vile word, excel na power point ZAECA imekuwa ikizitumia bila ya kuhitaji utaratibu wa utengenezaji

wa mifumo, ndio hivyo hivyo inatumia programu hiyo ya “access” kujisaidia kuhifadhi taarifa huku ikiendelea na maandalizi ya kutengeneza mfumo wake.

Hata hivyo hatua za utengenezaji mfumo zimeanza na taratibu za utengenezaji wa mifumo ya TEHAMA unazingatiwa. Tayari ZAECA imewasilisha kwa Mamlaka ya Serikali mtandao EGAz nyaraka za kusudio la utengenezaji wa mfumo yaani “concept note” **kiambatanisho C** kinahusika.

Aidha, kwavile mfumo huo ZAECA iliona unaweza kuchelewa kutokana na changamoto za upatikanaji wa rasilimali fedha ikaamua kutumia rasilimali watu wa ndani kufanya kwanza mfumo mdogo ambao utahusisha Idara ya Uchunguzi peke yake, jambo ambalo EGAz walitushauri kutumia template mpya kwa vile tuna lengo la kufanya wenyewe **kiambatanisho D** kinahusika. Kazi hii inaendelea kwa ushirikiano wa karibu na EGAz.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imeridhika na majibu ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar na kubaini kwamba “case distribution system” haikua ni mfumo bali ni program ambayo inatumika katika kuisaidia ZAECA kuweza kufanya shughuli zake kwa urahisi zaidi, kama jinsi zinavyotumika program za Microsoft Excel na Microsoft Word. Hivyo, kwa mnasaba huo Kamati imeiondoa hoja hii.

Hoja Nambari 4.1.4.3: Mapungufu yaliyobainika katika chumba cha seva (Server room)

Chumba cha Seva ni eneo maalum ambalo hutumiwa kuhifadhi na kusimamia vifaa vya kompyuta na miundombinu inayosaidia utoaji wa huduma za mtandao, uhifadhi wa data, na mifumo mengine muhimu katika Mamlaka au biashara.

Katika kufanya ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA ya ZAECA ukaguzi ulibaini uwepo wa mapungufu mbali mbali yakiwemo kukosekana kwa mfumo wa kuzima moto, kuharibika kwa UPS inayotumika kuimarisha ulinzi juu ya mabadiliko ya umeme katika Vifaa ndani ya Seva, kutokuwepo kwa daftari la kusajili watu wanaoingia kwenye chumba cha Seva, kutokuwepo kwa kamera za ulinzi, udhaifu wa udhibiti kupitia geti/ mlangoni, kutokuwepo kwa mashine ya “Biometric” kwa ajili ya kuchukuwa kumbukumbu za watu wanaoingia, Maelezo ya kina ya dosari hizo ni kama ifuatavyo:-

A) Kukosekana kwa mfumo wa kiautomatiki wa kuzima moto (Fire Suppression System) katika chumba cha Seva

Ukaguzi ulibaini ZAECA kutokua na Mfumo wa dharura wa kuzima Moto katika Chumba cha Seva kilichopo ndani ya Mamlaka hiyo jambo ambalo ni kwenda kinyume na Matakwa ya Miongozo na Viwango vya kimataifa vya

TEHAMA wa ISO 9001 (Fifth edition 15/9/2015) katika kifungu nambari 5.15, ambacho kinasisitiza uhitaji wa utaratibu wa udhibiti wa taarifa ili kulinda vifaa na mifumo ya TEHAMA inayohifadhiwa katika Seva na kuweza kufanya kazi hiyo kwa masaa 24 kwa siku zote za wiki.

Kukosekana kwa mfumo wa kuzima moto katika chumba cha Seva kunaweza kusababisha hatari kwa vifaa, miundombinu na taarifa zilizo ndani ya chumba Seva kama vile ongezeko la joto na kusababisha mripuko wa moto, kuharibika kwa miundombinu na kukosa huduma, kuongezeka kwa gharama za matengenezo baada ya kutokea kwa moto n.k.

Ukaguzi unaushauri viongozi ea ZAECA Kuweka Mfumo wa kuzima moto wa kiautomatiki (fire suppression system) katika chumba cha Seva ili kuweza kulinda vifaa na mifumo ya TEHAMA inayohifadhiwa.

B) Kutokuwepo kwa daftari la kusajili watu wanaoingia katika chumba cha Seva

Ukaguzi ulibaini kukosekana kwa Daftari la kuweka rikodi za Watu wanaingia na kutoka katika chumba cha Seva, hali hii inaenda kinyume na viwango kubalifu vya kimataifa vya TEHAMA vinavyohitaji uwepo wa daftari maalum litakalotumika kwa ajilli ya kurikodi watu watakaoingia na kutoka katika chumba cha Seva kwa ajili ya usimamizi mzuri na udhibiti wa chumba cha Seva.

Kukosekana kwa Daftari la kuhifadhia watu wanaoingia na kutoka katika chumba cha Seva kunaweza kusababisha kushindwa kudhibiti na kufahamu aina ya watu wanaoingia na kutoka katika eneo hilo, muda pamoja na shughuli wanazofanya hali ambayo inaweza kuhatarisha usalama wa rasilimali zilizomo ndani yake.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kuweka utaratibu imara kwa kuweka kumbukumbu za wanaoingia na kutoka katika chumba cha seva pamoja na kufuatilia shughuli wanazofanya ndani ya chumba hicho ili kuhakikisha kunakuwepo kwa usalama wa taarifa na miundombinu iliyomo.

C) Udhaifu wa udhibiti wa Mlango wa chumba cha Seva kilichopo ZAECA (Absence of reinforced Door)

Ukaguzi ulibaini ZAECA kutokuweka ulinzi wa kutosha katika Mlango wa kuingilia katika chumba cha Seva hali ambayo ni kinyume na Matakwa ya kifungu nambari 2.9.2.1 cha Muongozo wa utengenezaji wa Sera ya Ulinzi wa TEHAMA katika Afisi za Umma kutoka Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar eGAZ unaoelekeza kwamba kuwepo na udhibiti imara wa uingiaji katika vyumba vya kuhifadhia Mitambo kwa lengo la kuboresha Usalama.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kuweka mlango wa geti la chuma katika chumba cha Seva pamoja na kuboresha madirisha ya chumba hicho kwa ajili ya kulinda na kudhibiti rasilimali zilizopo katika chumba hicho

dhidi ya vihatarishi vinavyoweza kusababisha upotevu wa vifaa, taarifa pamoja na mifumo.

D) Kutokuwepo kwa kifaa cha kusimamia kumbukubu za wanaoingia na kutoka katika chumba cha Seva (biometric door security device)

Kwa mujibu wa muongozo na viwango kubalifu vya kimataifa vya TEHAMA wa ISO 9001 (Fifth edition 15/9/2015) katika kifungu nambari 7.1, 7.2, 7.3 inasisitiza uhitaji wa udhibiti wa taarifa katika sehemu za Afisi, vyumba, juu ya uwekaji wa kifaa maalum cha kuchukua kumbukumbu ya watu wanaoingia na kutoka katika chumba cha Seva, kwani kufanya hivyo kunasaidia udhibiti na usalama wa juu katika upatikanaji na ufikiaji wa mifumo na vifaa katika chumba cha Seva.

Kukosekana kwa kifaa hicho kunaweza kupelekea Mamlaka kushindwa kupata kumbukumbu sahihi za waliongia na kutoka katika chumba hicho ili kuweza kusaidia katika kufuatilia matumizi na kubaini matendo yasiyo ya kawaida.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kuweka mashine ya Biometric ili kusaidia udhibiti na usalama katika upatikanaji na ufikiaji wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika chumba hicho.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar

a) Ni kweli mfumo wa kiautomatiki wa kuzima moto sio tu kwenye chumba cha seva bali kwenye afisi zote za Mamlaka bado ZAECA haijafanikiwa kuweza kuweka mfumo huo.

10. ZAECA imepokea ushauri wa kitaalamu na itatekeleza ushauri huo kwa kadri rasilimali fedha itakavyokuwa inaruhusu.

b) Ni kweli kipindi cha ukaguzi daftari halikuwepo, ZAECA imekubaliana na hoja ya CAG na kwa sasa tayari daftari lipo na linatumika vizuri.

c) Ni kweli wakati wa ukaguzi mlango wa gril kwenye chumba cha seva haukuwepo, ZAECA tayari imelifanyia kazi na mlango tayari ushawekwa.

d) Ni kweli kifaa cha kusimamia kumbukumbu za wanaoingia na kutoka katika chumba cha Seva (Biometric door security device) bado ZAECA haijafanikiwa kuweka kutokana na upatikanaji wa rasilimali fedha.

Hata hivyo Mamlaka imeanza uwekaji wa kifaa hicho kwa ajili ya mahudhurio kwenye Afisi ya Makao Makuu, na itaendelea kuweka kifaa hicho kwenye Afisi zake zote pamoja na vyumba vyote vya seva kadiri ya upatikanaji wa rasilimali fedha utakavyoruhusu.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

a) Kamati imebaini kwamba ni kweli katika chumba cha seva hakuna mfumo wa kuzimia moto bali chumba kina mitungi ya gesi ya

kuzimia moto “fire extinguisher” ambayo ndio inatumika endapo kutatokea majanga.

Kamati imeelezwa kwamba changamoto kubwa ni upatikanaji wa fedha, jambo ambalo kamati imeshindwa kupata kielelezo chochote kinachoonesha kwamba ZAECA hua wanapanga katika bajeti yao kifungu ambacho kitapelekea kupatikana kwa mfumo wa kuzimia moto katika chumba cha seva.

b) Kamati imebaini kwamba ZAECA haiku ana uelewa wa kuwepo kwa daftari linaloweka kumbukumbu ya watu walioingia katika chumba cha seva, na baada ya mkaguzi, Uongozi wa ZAECA umetatua hoja hii kwa kuweka daftari hilo.

c) Kamati imebaini kwamba hoja hii tayari imeshatekelezwa.

d) Kamati imeridhika na utekelezaji wa hoja hii.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inaielekeza Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar kuhakikisha kwa bajeti ijayo wanaandaa fedha kwa ajili ya kuweka mifumo ya kuzimia moto hususani katika vyumba vya seva ili kuhakikisha usalama wa vifaa pamoja na taarifa zinazohifadhiwa katika vifaa hivyo.

Hoja Nambari 4.1.4.4: Udhaifu wa udhibiti wa ufikiaji na mgawanyo wa majukumu ndani ya Mfumo wa usimamizi wa Kesi (Access control)

Miongozo ya Wakala wa Serikali Mtandao, 2022 (ICT Gudelines 2022) kifungu nambari 4.1, pamoja na kifungu nambari 3.4.4.7 cha Sera ya TEHAMA ya Taifa Zanzibar, ambacho kinazitaka Mamlaka za Umma kutengeneza utaratibu wa udhibiti wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwa watumiaji kwa lengo la kudumisha Usalama, Usiri, Uadilifu wa taarifa za Serikali pamoja na upatikanaji wa mifumo.

Ukaguzi ulibaini kwamba Mfumo wa Usimamizi wa Kesi (Case Distribution Sysytem) wa ZAECA una udhibiti duni wa ufikiaji katika makundi ya watumiaji wake ambapo kundi la watumiaji wa kawaida (Information Center Officer) wamepatiwa uwezo mkubwa wa ufikiaji wa Moduli zote zinazowawezesha watumiaji hao kuingiza taarifa za aina zote katika mfumo, kuona taarifa mbalimbali katika mfumo, kusanidi pamoja na kufuta taarifa mbali mbali ndani ya Mfumo huo. Hivyo kundi hili ni la “super users” ambalo linaweza kukamilisha hatua zote bila ya kumuhusisha mtu mwengine katika ngazi tofauti za uongozi wa Mamlaka.

Udhibiti duni wa ufikiaji wa mfumo, hususan mfumo wenye taarifa nyeti kama huu unaweza kupelekea kuwepo kwa dosari mbali mbali kwa Mamlaka na Serikali kwa ujumla, miongoni mwa hizo ni pamoja na:-

- Kuondoa Usiri unaotakiwa kuwepo katika taarifa mbali mbali zinazohusiana na kesi za Rushwa na uhujumu uchumi.
- Kuhatarisha Uadilifu wa taarifa za Kesi pamoja na mienendo yake katika hatua mbali mbali za upatikanaji wa haki kwa watuhumiwa.
- Kudhoofisha hali ya upatikanaji wa mfumo husika pamoja na usalama wa taarifa zilizomo.

Hali halisi ya utumiaji ya mfumo inayoonesha mtumiaji wa kawaida kupewa uwezo wa kuzifuta modeli zote ni kama inayoonekana katika picha ifuatayo:-

Picha Nambari 4: Mfumo wa Usambazaji wa Kesi ukionesha Afisa wa Kitengo cha IC (Information Center) kufikia katika Moduli zote za Mfumo



Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kuzingatia mgawanyo wa majukumu na makundi ya watumiaji katika kufikia moduli mbali mbali za Mfumo na kuhakikisha kwamba hakuna mtu mmoja mwenye ufikiaji wa maeneo yote ya mfumo ili kuimarisha Usiri, Uadilifu, na Usalama wa taarifa mbali mbali za Kesi zinazohusiana na Rushwa na Uhujumi Uchumi

Aidha, ili kuhakikisha kuwa mfumo unazingatia uwazi na uwajibikaji Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kutengeza makundi ya watumiaji yanayowahusisha viongozi wa Mamlaka ambao pia watapatiwa ufikiaji katika mfumo ili waweze kuona na kupata taarifa zote kupitia ripoti mbali mbali kwenye mfumo.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar

Kama jibu la hoja 4.1.1.2 lilivyoweka wazi kuwa programu inayotumika kusaidia kuhifadhi taarifa haikuwa mfumo wezeshi, ila ni kisaidizi cha wakati huu ZAECA ikiwa haina mfumo hadi hapo itakapokuwa na mfumo wake.

Programu yenyewe inapatikana kwenye computer ya mtu mmoja ambae ana uwezo wa kufanya kila kitu kwenye computer yake.

Dosari ambazo zimefikiriwa kuweza kutokea hazina athari kwa namna ya utendaji wa sasa uliopo,

- Mwenye computer iliyomo programu hiyo ndie anaepokea malalamiko yote na majalada ya kesi zote yeye ndie anaeyahifadhi, hakuna usiri ambao umedhoofishwa kwa kuwepo programu hiyo.
- Hakuna uadilifu na upatikanaji wa haki unaoweza kuathirika kwasababu kimsingi programu hiyo iwepo au isiwepo yeye bado ndio mwenye kuhifadhi kesi zote.
- Programu hiyo haidhoofiki kwasababu imo kwenye computer moja (local based) na hakuna mwengine anaeweza kuitumia nje ya computer hiyo.

Hata hivyo programu hii sasa imekuwa haitumiki tena kwa matarajio ya kuja kuanza kutumika mfumo mdogo ambao ZAECA inauandaa kwa matumizi ya Idara moja pekee.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini utekelezaji wa hoja hii unaendana na hoja namba 4.1.4.2 ambapo program iliyokusudiwa haikua mfumo bali program ambayo inatumika na Afisa TEHAMA wa ZAECA. Hivyo, Kamati imeridhika na majibu ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar.

Hoja Nambari 4.1.4.5: Dosari ya kiusalama katika Uhifadhi wa Mfumo wa Usambazaji Kesi

Ukaguzi ulibaini kuwa Mfumo wa Usambazi Kesi umehifadhiwa katika Kompyuta ya Mamlaka kama Seva, hata hivyo Kompyuta hiyo inatumiwa na mmoja wa maafisa wa ZAECA kama kitendea kazi chake katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na miongozo ya viwango bora kubalifu vya TEHAMA (best practice) ambayo kwa sababu za kiusalama ambazo ni njia muhimu za kuhakikisha taarifa za Serikali zinaendelea kubaki na Usiri, Uadilifu na kupatikana muda wote inatakiwa Kompyuta/ Seva inayotumika kuhifadhi mifumo ya TEHAMA kuwekwa katika mazingira salama kama vile chumba cha Seva (Sever Room) ambayo yanaudhibiti wa ufikiaji unaohakikisha kila anayefikia vifaa hivyo (Kompyuta/ Seva) anafahamika muda wote na kuhifadhiwa kwa kumbu kumbu za alichofanya kupitia “audit

trails/logs" mazingira ambayo ZAECA haijaweka katika Kompyuta inayotumika kuhifadhi mfumo wa "Case Distribution".

Aidha, hali hii inaweka rehani Usiri, uadilifu na upatikanaji wa taarifa nyeti za kesi mbali mbali zinazohusu wahalifu na watuhumiwa wa masuala ya rushwa na uhujumu uchumi jambo ambalo linaweza kupelekea kuchelewesha au kukwamisha juhudi na jitihada za Serikali katika kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kuchukuwa hatua za makusudi za kuboresha mazingira ya TEHAMA katika Mamlaka ikiwemo upatikanaji wa Seva maalum itakayotumika kwa ajili ya kuhifadhi mifumo mbali mbali ya TEHAMA ya Mamlaka na kuhakikisha kwamba Seva hiyo inawekwa katika chumba maalumu cha Seva (Server Room) ambacho kitazingatia matakwa ya kiusalama, utendaji, usiri, uadilifu na upatikanaji wa mifumo katika ngazi ya Taifa na Kimataifa (best practice).

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar

Kama jibu la hoja 4.1.1.2 lilivyoweka wazi kuwa programu inayotumika kusaidia kuhifadhi taarifa sio mfumo wezeshi, ila ni kisaidizi cha wakati huu ZAECA ikiwa haina mfumo hadi hapo itakapokuwa na mfumo wake.

Hata hivyo programu hii sasa imekuwa haitumiki tena kwa matarajio ya kuja kuanza kutumika mfumo mdogo ambao ZAECA inauandaa kwa matumizi ya Idara moja pekee kwa ushirikiano wa karibu wa EGAz.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Utekelezaji wa hoja hii unaendana na hoja namba 4.1.4.2 na 4.1.4.4, hivyo kamati imeridhika na kuiondoa hoja hii.

Hoja Nambari 4.1.4.6: Malipo ya ziada yaliyofanyika kwa wazabuni kupitia mfumo wa eProz shilingi 13, 883,600

Ukaguzi ulifanya mapitio ya taratibu za manunuzi yaliyofanywa na ZAECA kupitia mfumo wa eProz na kubaini zaidi ya asilimia 34 ya Zabuni za "Minor Value" zilitolewa na ZAECA kwenda kwa wasambazaji (suppliers) kwa ajili ya malipo ya huduma mbali mbali.

Ukaguzi ulibaini uwepo wa dosari katika mchakato wa manunuzi yaliyofanyika ikiwemo ukiukwaji wa taratibu za manunuzi ambapo ni kinyume na Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016. Baadhi ya dosari zilizobainika ni kama zifuatazo:-

a) Utoaji wa Zabuni kwa waombaji "biders" waliokuwa na bei za juu zaidi na kuwaacha waombaji waliokuwa na bei ndogo ambao walichaguliwa na mfumo na kuwekwa katika nafasi 3 bora (3 Lowest biders) bila ya kuwepo kwa sababu za msingi zenye ushahidi.

b) Mfumo wa eProz kushindwa kutumika katika kutoa taarifa za matokeo kwa waombaji zabuni hususan kwa wazabuni ambao hawakuchaguliwa (hawakushinda zabuni) ya kusambaza bidhaa zilizohitajika ili kuweka kumbu kumbu na ushahidi wa kutoridhishwa na uwezo pamoja na vigezo vyao kabla ya kuwanyima zabuni husika.

Hivyo, kutokana na dosari zilizopo hapo juu, tathmini iliyofanyika imebainisha ZAECA imefanya malipo ya ziada ya shilingi 13,883,600 kwa zabuni 15 kati ya zabuni 41 zilizofanyiwa tathmini bila ya kuzingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma pamoja na matakwa ya mfumo wa eProz. Hali halisi ya taarifa za malipo ya ziada yaliyofanyika ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 32: Zabuni zilizotolewa kwa watoa huduma ambao bei zao ni kubwa ukilinganisha na watoa huduma waliochaguliwa na mfumo wenye bei nafuu

Namba	Nambari ya Zabuni	Gharama halisi za mzabuni mwenye bei ndogo kwa mujibu wa mfumo (TZS)	Gharama za aliyepewa tuzo ya zabuni (TZS)	Nafasi ya aliyepewa tuzo ya zabuni kwa mujibu wa mfumo	Ziada ya fedha (TZS)	Asilimia ya ziada (%)
1.	rfq_22651	150,000	212,000	4	62,000	29.25
2.	rfq_22649	148,000	210,000	3	62,000	29.52
3.	rfq_22648	596,500	707,500	2	111,000	15.69
4.	rfq_22503	5,015,000	11,512,100	4	6,497,100	56.44
5.	rfq_18233	4,761,000	5,475,000	2	714,000	13.04
6.	rfq_16914	385,000	591,000	5	206,000	34.86
7.	rfq_16900	2,457,000	2,700,000	3	243,000	9.00
8.	rfq_12147	1,600,000	2,450,000	2	850,000	34.69
9.	rfq_10830	800,000	850,000	2	50,000	5.88
10.	rfq_22540	600,000	1,680,000	5	1,080,000	64.29
11.	rfq_222	4,277,000	7,880,000	5	3,603,000	45.72

	70					
12.	rfq_16578	1,800,000	2,200,000	2	400,000	18.18
13.	rfq_22245	210,500	216,000	2	5,500	2.55
Jumla		**22,800,000**	**36,683,600**		**13,883,600**	

Kufanyika kwa malipo ya ziada kunaweza kusababisha hasara kwa Serikali kutokana na upotevu wa fedha unaotokana na kutozingatiwa kwa Sheria na taratibu za manunuzi kupitia mfumo wa kielektroniki wa eProz. Vile vile kunaweza kusababisha dosari zifuatazo:-

- Kuondoa imani kwa wazabuni kutokana na kutopatiwa taarifa zozote kwenye mfumo kuhusiana na zabuni walizoomba ikiwa wamekosa na sababu zilizowafanya kukosa zabuni hizo.
- Kukosekana kwa tija na kupunguza ufanisi wa ununuzi na uondoshaji wa mali za umma kwa sababu ya kutozingatia taratibu zilizowekwa kupitia mfumo wa eProz.
- Kuongeza gharama kwa Serikali na kuisababishia Serikali hasara kwa kufanya manunuzi ya bidhaa na huduma kwa bei za juu zaidi ya uhalisia wa soko
- Kuchochea mazingira ya rushwa hususan katika mazingira ambayo wazabuni wenye bei ndogo wasipopatiwa zabuni na badala yake kupewa wazabuni wenye bei za juu zaidi

Vile vile jadweli hapo chini linaonesha taarifa nyengine ya mzabuni ambae amechaguliwa na kupewa tuzo ya zabuni kwa thamani ya shilingi 14,880,000 kwa ajili ya kusambaza huduma kwa ZAECA lakini nafasi yake kwa mujibu wa orodha ya mfumo ni mtu wa kumi na sita (16) kulingana na bei za zabuni zilizowasilishwa ambapo mzabuni mwenye bei ndogo alikuwa ni shilingi 7,636,000. Ukaguzi haukupatiwa ushahidi wa vigezo vilivyotumika kumpata mzabuni huyo.

Hali halisi ya mchakato wa zabuni ni kama inavyoonekana katika picha hapo chini:-

Jadweli Nambari 33: Kukosekana kwa vigezo vilivyotumika kumpata mzabuni wa 16 na kuwaacha wazabuni wa nafasi za awali wenye bei nafuu

AWARDING DECISION: Awarded

Rank	Supplier	Awarding Decision	Total Price	Confirmed Price
1	MULTI HOME FURNITURE		7,636,000	7,636,000
2	TRINITY GENERAL SUPPLIES		7,751,000	7,751,000
3	ZAN PRINTINGS		7,830,000	7,830,000
4	AMO COMPUTER SERVICES		8,336,000	8,336,000
5	New Home Furniture		9,030,000	9,030,000
6	AKHAKAMU GENERAL SUPPLIES COMPANY LIMITED		9,920,000	9,920,000
7	SAMOI TRADER & GENERAL SUPPLY COMPANY LIMITED		10,112,000	10,112,000
8	SALEH DECORATION		10,374,000	10,374,000
9	Storatoet General Supply		11,720,000	11,720,000
10	KADON COMPANY LIMITED		12,319,200	12,319,200
11	Z & M (T) GENERAL TRADERS LIMITED		12,430,000	12,430,000

Page 53 of 59

Report run from: Report Area, at: 22/12/2023 12:10

Rank	Supplier	Awarding Decision	Total Price	Confirmed Price
11	DILAIYA PRINTING AND GENERAL SUPPLIES		12,430,000	12,430,000
12	ABRAS GENERAL TRADER		13,420,000	13,420,000
13	KICHAN GENERAL SUPPLIERS COMPANY LIMITED		13,908,000	13,908,000
14	4 PEOPLE GENERAL SUPPLIER		14,038,000	14,038,000
15	DREAM LINER GENERAL TRADERS LIMITED		14,330,000	14,330,000
16	F & AS EQUIPE AND GENERAL	Awarded	14,880,000	14,880,000

Picha Nambari 5: Wazabuni ambazo wamekosa tuzo ya zabuni na hawakupewa taarifa ya sababu ya kukosa kupitia mfumo kwenye zabuni ya RFQ_2637

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa ZAECA kuhakikisha kwamba unasimamia kitengo cha Manunuzi kwa karibu na kuhakikisha kwamba taratibu za Manunuzi zinazingatiwa muda wote katika aina zote za manunuzi kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo ya manunuzi

Aidha, kwa upande wa matumizi ya mfumo wa e-Proz ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kuhakikisha kwamba unawawezesha watumishi wa Kitengo cha manunuzi kwa kupatiwa mafunzo stahiki katika baadhi ya maeneo ambayo hawana uelewa wa kutosha ili waweze kuutumia mfumo ipasavyo na kuepuka kufanya malipo ya ziada yatakayosababisha hasara kwa Serikali

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar

Kwa mujibu wa jadweli la tano katika sheria ya ununuzi na uondoaji wa mali za umma Zanzibar Sheria namba 11 ya mwaka 2016, linaeleza kuwa minor value inaanzia kuanzia zero hadi kufikia shilingi milioni kumi na tano. Utekelezaji wake ni kupata kotesheni zisizopungua tatu kwa lengo la kushindanisha bei na ubora wa bidhaa husika. Sambamba na hilo, pia sheria hiyohiyo ya Manunuzi ya mwaka 2016, kifungu namba 127(a)(b) kinaeleza kuhusu mzabuni atakae kuwa ni mshindi yaani Successful bids, *"coted the bid with the best evaluated bid in case of goods or work or service, but not necessarily the lowest or highest submitted price subject to any margin of preference applied".*

Aidha kifungu namba 124 kinaelezea kuwa kuna vigezo vyengine mbalimbali ukiacha cha bei ya mzabuni kinachoweza kumpata mzabuni wa kwanza au wachini kabisa.

Pia, kifungu No, 126 kinaeleza kuwa mzabuni aliekubalika lazima vigezo vyake alivyoipa taasisi viendane na matakwa ya taasisi husika yaani viendane na vigezo vilivyomo ndani ya nyaraka ya zabuni ya taasisi husika.

Kadhalika kifungu No, 128 kinakitaka kitengo cha manunuzi kuwa makini wakati wa kufanya uchambuzi yakinifu (Evaluation to bids) sio kuangalia bei iliotolewa na mzabuni tu badala yake kufuata vigezo vyengine kama vilivyokwisha kuainishwa katika kifungu hichohicho.

Kutokana na vifungu vichache vilivyokwisha elezwa hapo juu hiyo ndio sababu kubwa ambayo iliopelekea maafisa hao wa ununuzi kumuacha mzabuni mwenye bei ndogo na kumchagua wa pili au wa sita katika orodha hiyo ya zabuni husika na si vyenginevyo.

Kuhusu hasara ya shilling millioni 13,883,600, hii kwa mujibu wa kanuni za ununuzi na uondoaji wa mali za Umma ya mwaka 202 haikuwa hasara bali ni tija kwasababu vifaa vimefika ghalani na vimewafikia walengwa kwa wakati vilipo hitajika bila ya kuchelewa kufika, na vikiwa katika hali ya ubora uliohitajika, vifaa vipo na vinaendelea kutumika kwa kazi za ZAECA na vinaleta ufanisi na vizima hadi sasa .

Hata hivyo ZAECA ilianza kutumia vifaa hivyo bila ya kulipa hata kiasi kidogo cha fedha hadi hapo ilipoingia OC.

Hii ina maana kwamba unapochagua mzabuni wa chini sio kuangalia bei pekee bali uangalie na

- Wakati wa kuleta bidhaa (delivery time),
- Uwezo wake wa kifedha kabla ya kulipwa na taasisi (Financial capacity),
- Ubora wa bidhaa (Quality based), na
- Uhalali wa biashara (Eligibility) n.k.

Mfumo umeweka sehemu ya mazungumzo ya moja kwa moja na mzabuni, bali baadhi ya wazabuni hawajibu kwa wakati komenti hizo jambo ambalo linazorotesha ufanisi wa kazi, wakati mwengine vifaa vinahitajika kwa haraka huwezi kumsubiri kujibu komenti bali utaendelea na hatua ili kuokoa hali ya tatizo iliopo.

Mzabuni mwengine ukimpigia simu anapokea na anajibu kuwa hawezi kufanya kazi hiyo kwa pesa aliojaza bali alikuwa anabahatisha tu.

Wengine hawana hata ofisi za biashara ikitokezea hasara tutawapata wapi lengo nikuijenga taasisi sio kuiangusha ofisi na hata vigezo vyao vinakuja tofauti na tulivovianisha katika nyaraka ya zabuni.

Wapo wengi wanaotoa bei ndogo kisha wanasema hawawezi kufanya biashara mpaka walipwe kwanza kitendo ambacho kwa Serikali yetu ni kigumu, maranyingi mwanzo tunachukua bidhaa mpaka pesa itakaporuhusu tunalipa, hivyo ofisi yetu ndivyo inavyofanya manunuzi yake. Sio mara nyingi kulipwa papo hapo ni mara chache tu kutokea hivyo. Maelezo hayo na vigezo vyote vilivyoelezwa hapo juu ndivyo ambavyo vinatufanya tuwawache wenye bei ndogo na kuwachukuwa wenye bei kubwa.

Hayo yote yana simamiwa na muhimili mkuu wa Manunuzi unasema kuwa Thamani ya fedha kwa bidhaa husika (Value for Money)

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati kimsingi imeridhika na majibu ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar ambapo kama sheria inavyoeleza, mshindi wa zabuni halazimiki kua mwenye bei ndogo bali awe na uwezo wa ziada ambao utaleta tija (win-win) kwa pande zote mbili.

Aidha, Kamati imebaini kwamba msingi wa hoja hii ni kwamba Afisa manunuzi wa ZAECA hawakua wanaweza sababu katika mfumo ya kuonesha uhalali wa kumchagua Mzabuni Fulani badala ya mwengine ambae alionekana katika mfumo akiwa na bei ndogo zaidi.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inaiagiza Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar kuhakikisha inaweka sababu za kumchagua mzabuni katika mfumo wa eProz ili kuwezesha ukaguzi kufanyika kwa urahisi na kupata vielelezo vyote ili kuepusha hoja nyengine zisitokee

Hoja Nambari 4.1.4.7: Kutokushindanishwa kwa watoa huduma mbalimbali kwenye Zabuni ya Ununuzi wa Huduma ya Chakula nambari RFQ_21374 yenye thamani ya shilingi 45,360,000

Ukaguzi ulibaini kwamba ZAECA haikuwaalika watoa huduma mbalimbali katika zabuni ya Ununuzi wa Huduma ya Chakula kupitia Zabuni nambari

RFQ_21374 ya tarehe 07/06/2023 ambapo Kampuni ya 2R&2N Supplier ndio pekee iliyoalikwa kushiriki katika Zabuni hiyo kinyume na Sheria namabri 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 na Kanuni zake.

Ukiukwaji wa taratibu za manunuzi unaweza kupelekea uwepo wa mianya ya rushwa na uhujumu uchumi na kuisababishia Serikali hasara kwa kununua bidhaa au huduma kwa bei kubwa zisizokuwa na ushindani.

Kudhoofisha uchumi kwa kuondoa ushindani na mzunguko wa fedha kwa kupunguza wafanya biashara ambao hawapati kazi kama hiyo ya Zabuni ya kutoa huduma ya chakula.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kusimamia kitengo cha Manunuzi kwa karibu na kuhakikisha kwamba watumishi wanazingatia matakwa ya Sheria na Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ili kufanya manunuzi yenye tija katika matumizi ya fedha za Serikali na kupunguza gharama zisizo za lazima kwa Serikali kupitia ushindani wa wazabuni na watoa huduma mbali mbali watakao wezesha kupatatikana bei shindani ambazo ni himilivu kwa Serikali

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar

Hii ni pesa ambayo ilitumika katika mafunzo ya kijeshi ya ZAECA yaani Mafunzo ya awali ya uchunguzi BIC.

Kiukweli haya mafunzo yanahitaji usiri, uangalifu na usalama katika kuendesha kwake. Hivyo panahitajika usalama wa mtumiaji na mlaji kijumla kama vile ilivyo kwa vyombo vya ulinzi na usalama wanakuwa na mpishi maalum wanaye muamini na kumfanyia vetting kama ambavyo tulivyofanya ZAECA.

Kupitia sheria ya Manunuzi ya mwaka 2016 iliweweka wazi njia mbalimbali za manunuzi ikiwemo hiyo ambayo ZAECA ilioitumia yaani njia ya manunuzi ya kununua moja kwa moja (Single Source Method). Njia hii inafanyakazi katika mazingira ya dharura tunazuia ushindani (yaani ni exceptional circumstance). Maelezo haya yanapatikana katika kifungu No.75 katika sheriya ya Manunuzi namba 11 ya mwaka 2016.

Hivyo ZAECA nayo kutokana na kozi hiyo kuwa nyeti na siri ndipo uongozi ulipo amua kutumia njia hiyo ya mojakwamoja na kwa vile muhusika alikwisha fanyiwa vetting na kujaza mkataba.

Zabuni hii ilikuwa ni ya upishi kwenye mafunzo ya BIC (basic investigation course) ambayo ni mafunzo ya kijeshi yalofanyika kwenye kambi ya kijeshi. Kutokana na unyeti, kutunza siri za kambi na usalama wa chakula cha maafisa, ZAECA ililazimika kutumia mtoa huduma wa kuchagua na sio wa

kushindanishwa na hivi ndivyo viwango vya juu vya ubora kamilifu ("best practice") ilivyo, vikosi vyote vya ulinzi na usalama ndivyo wanavyofanya.

Uchunguzi wa kamati ya PAC

Kamati imeridhika na majibu ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar.

Hoja Nambari 4.1.4.8: Upatikanaji hafifu wa mfumo wa manunuzi wa kielektroniki (eProz) katika mtandao wa ZAECA

Ukaguzi ulibaini kwamba mfumo wa eProz haupatikani kupitia mtandao wa ZAECA katika mazingira ya Makao Makuu ya Afisi, ambapo ukaguzi uliweza kugundua chanzo kikuu cha tatizo la kutokupatikana kwa mfumo wa eProz kupitia mtandao wa Afisi ni kuwepo kwa matumizi makubwa ya "bandwith" yanayofikia kikomo cha "bandwith" iliyolipiwa (20Mbps) na ZAECA kutoka ZICTIA yakiwa ni sababu kuu ya kukwamisha ufikiaji wa mfumo wa eProz.

Aidha, ukaguzi uliweza kufanya tathmini ya matumizi ya "internet" na kubaini kwamba ZAECA haijaweza kuzuia matumizi katika "sites" zisizokuwa na tija na zenye vihatarishi vya usalama wa taarifa za kompyuta kama vile Torrent, Netflix, Ticktok, adult sites, gambling site, download sites n.k ambazo kwa kawaida hutumia "Bandwith" kubwa na kunyima Programu nyengine kufanya kazi wakati wa masaa ya kazi.

Kukosekana kwa leseni za udhibiti na usalama katika kifaa cha ulinzi wa mawasiliano ya mtandao (sophos firewall) kunaweza kupunguza ufanisi wa Kitengo cha Manunuzi katika matumizi ya mfumo wa manunuzi (eproz).

Vile vile kuongezeka kwa gharama binafsi kwa watumishi kutokana na watumishi kutumia simu zao za mkononi kwa ajili ya kupata huduma za Internet na kuweza kuufikia mfumo wa eProz.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kufanya malipo ya Leseni za kifaa cha Sophos XG Firewall ili kupata uwezo wa kufanya usanidi wa Sera za Usalama ikiwemo kuzifungia Programu ambazo zimepigwa marufuku katika Muongozo wa Internet Usage Guideline, 2022 wa eGAZ.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar

Ni kweli mfumo huu wa manunuzi wa kielektroniki (eProz) ambao unapatikana kwa kiunganishi "https://eprocurement.zppda.go.tz" umekuwa na changamoto kiasi fulani si tu kwenye ofisi zetu za ZAECA pekee bali hichi ni kilio cha Afisi nyingi za Serikali na binafsi.

ZAECA tuna changamoto ya kukosa leseni kwenye kifaa chetu cha ulinzi na uchujaji wa mfumo wetu wa mawasiliano "firewall" matokeo yake kushindwa kuchuja baadhi ya mitandao ambayo haina tija wakati wa kazi, ili

kupunguza matumizi ya intaneti na kuiwacha intaneti itumike kwa masuala muhimu ya kazi tu.

Mara nyengine hufanya majaribio jioni sana kipindi ambacho takriban wafanyakazi wengi washaondoka, na bado hushindwa kufanya kazi kupitia mfumo huu wa Eproz, mara nyengine hujaribu kwa kutumia intaneti ya simu zetu lakini bado changamoto inakuwa palepale.

Afisa mananuzi wetu wamekuwa na kawaida ya kwenda kuufuata mfumo kule ulipo Michenzani mall, na kwa mujibu wao ukifika pale mfumo unafunguka kiwepesi sana na wala hauna changamoto, cha ajabu wakifika pale huwa hawapo peke yao, wanakutana na afisa manunuzi wa sehemu mbali mbali wakiwa na changamoto kama yao.

Hivyo, ukizingatia kuwa mifumo mengine yote inafunguka vizuri isipokuwa huu tu wa Eproz, na maelezo tulioyaeleza juu hapo, ni dhahiri tatizo hili kamwe halihusiani tu na ZAECA pekee bali kwa asilimia kubwa mfumo wenyewe ndio changamoto.

Hata hivyo, kwasiku za karibuni ZAECA imeanza kuona wepesi katika kufungua mfumo wa Eproz, na baadhi ya kazi zinafanyika hapahapa ofisini, matarajio ya ZAECA baada ya kupata leseni ya kifaa chetu cha ulinzi intaneti itaimarika sana na tatizo hili litapungua sana kama si kuondoka kabisa.

Mchakato wa kutafuta leseni tayari umeanza, kupitia bajeti ya mwaka huu wa fedha 2024/2025 tumejipanga kununua leseni hiyo, **kiambatanisho E** kinahusika.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC kimsingi imeridhishwa na majibu ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaielekeza Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar kuhakikisha inalipia leseni ya kifaa cha “firewall” ili kusaidia katika kudhibiti usalama na kuepusha majanga. Aidha, Kamati inaitaka ZAECA kuhakikisha inadhibiti matumizi ya tovuti na “application” ambazo hazina tija ili kuuwezesha mtandao wa ofisi kuanya kazi kwa kasi iliyokusudiwa.

Hoja Nambari 4.1.4.9: Kutotumika kwa mfumo wa e-Offi ce katika Afi si za Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi

Ukaguzi ulibaini kwamba ZAECA haijaanza matumizi ya mfumo wa Serikali wa Afisi Mtandao (e-Office) licha ya kupatiwa Kompyuta na “Scanner” maalumu kwa ajili ya kuendesha mfumo kwa zaidi ya miezi 4 sasa.

Aidha, ukaguzi ulibaini kwamba watumishi wa Masjala pamoja na watumishi wengine wanaotakiwa kutumia mfumo wa e-Office hawajapatiwa mafunzo ya namna ya kuutumia mfumo ambapo mpaka tunakamilisha Ukaguzi ZAECA haikuwa na mpango wa mafunzo ya mfumo ya e-Office.

Kukosekana kwa dira na mpango madhubuti wa utekelezaji wa miongozo halali ya Serikali kupitia Wakala wa Serikali Mtandao na Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kumepelekea mapungufu katika mipango na mikakati ya Serikali ya kutekeleza Serikali Mtandao ili kuongeza tija, ufanisi, uwazi na uwajibikaji.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZAECA kuhakikisha kwamba unasimamia kitengo cha Masjala na TEHAMA kwa kushirikiana na eGAZ na Mamlaka ya Nyaraka na Kumbu kumbu Zanzibar ili kuwezesha utolewaji wa mafunzo kwa watumishi wote wanaotarajiwa kutumia mfumo wa e-Office na kutekeleza mahitaji yote muhimu yatakayowezesha kuanza kutumika kwa mfumo wa e-Office katika Afisi zote za ZAECA Unguja na Pemba kwa uharaka unaostahili.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar

Ni kweli kipindi Mkaguzi anapita ZAECA ilikuwa haijaanza kutumia mfumo wa E-office kutokana na changamoto za mafunzo japokuwa mfumo ulikuwa tayari unapatikana.

Hata hivyo, mfumo wa E-office sasa unatumika vizuri katika ofisi ya Makao Makuu baada ya kupatiwa mafunzo, na mpango wa kupeleka mikoani unaendelea, **kiambatanisho F**.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imeridhika na majibu ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar.

Hoja Nambari 4.1.4.10: Kukosekana kwa Mfumo wa Kielektroniki wa kufanya Uchunguzi wa Kimahkama (Forensic Audit Software) na kukusanya Ushahidi wa Kidijitali (Digital Evidence)

Mfumo wa Kielekroniki wa kufanya Uchunguzi wa Kimahkama (Forensic Audit Software) na kukusanya Ushahidi wa Kidijitali (Digital Evidence) ni mfumo wa Kielektroniki uliotengenezwa na kutumika kwa lengo la kuhifadhi na kusimamia ushahidi wa kesi au nyaraka nyingine muhimu zinazotumika katika Muktadha wa kimahakama. Ushahidi huu unaweza kuwa wa aina mbalimbali, ikiwa ni pamoja na nyaraka za elektroniki, picha, sauti, au taarifa nyingine inayoweza kutumika kuthibitisha na kuelezea ukweli juu ya suala fulani.

Mfumo huu unaweza kujumuisha programu, taratibu, na vifaa vinavyosaidia uhifadhi wa ushahidi kwa njia inayohakikisha usalama, uhakika, na upatikanaji wa haraka wa taarifa. Lengo kuu la mfumo wa kuchunguza ushahidi ni kutoa njia rasmi na yenye utaratibu wa kisheria wa kuhifadhi, kusimamia, na kuwezesha utumiaji wa ushahidi katika muktadha wa kisheria na kiupelelezi.

Ukaguzi ulibaini ZAECA haina Mfumo wa Kielekroniki unaotumika katika kusaidia kuchunguza ushahidi kutokana na Kesi mbalimbali zinazo ripotiwa katika Mamlaka. Hata hivyo, hadi ukaguzi unakamilika haukuweza kupatiwa njia zinazotumika kuhifadhi ushahidi wa kidijitali (Digital Evidence).

Baadhi ya nyaraka za kidijitali ambazo zinatakiwa kuwa na mfumo wa kusimamia na kulinda matumizi yake ni pamoja na:-

- Barua pepe, Maandishi na Ujumbe Mfupi (Emails, text and instant messages).
- Picha za Kidijitali na Video (Digital photographs and video footage).
- Faili za Uhasibu na Miamala (Accounting files and transactions).
- Historia ya kivinjari na kumbukumbu za mtandao (Browser history and Internet logs).
- Taarifa za Eneo (GPS tracks and location data)
- “Databases Logs”

Kukosekana kwa mfumo wa kuchunguza na kuhifadhi ushahidi wa kidijitali au kutumia mifumo isiyo rasmin kunaweza kusababisha dosari mbali mbali, hasa katika muktadha wa kimahakama, kiuchunguzi na kiupelelezi kama zifuatazo:

Kuharibu ubora wa Ushahidi: Hali hii inaweza kujitokeza katika mazingira ambayo ushahidi uliochukuliwa na Mamlaka ukatofautiana na ushahidi halisi japo kwa sehemu ndogo sana kama vile mkato, nukta, urefu wa sentensi, “format of data” na kupelekea ushahidi kukataliwa katika vyombo vya kutolea haki.

Upotevu wa Ushahidi: Kukosekana kwa Mfumo imara wa Kielekroniki unaotumika kuhifadhia Ushahidi kunaweza kupelekea kupotea kwa nyaraka na vielelezo mbalimbali ambavyo ni muhimu katika kufanikisha hatua za kupatikana kwa haki juu ya kesi fulani katika vyombo vya haki.

Kuchelewesha Kesi na Uchunguzi: Kutokana na upotevu na kuharibika kwa ubora wa ushahidi kunaweza kupelekea ucheleweshwaji wa Kesi na kukamilika kwa uchunguzi jambo linaloweza kuchelesha upatikanaji wa haki.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kupanga bajeti itakayowezesha upatikaji wa mfumo wa Kielektroniki wa kuhifadhi ushahidi wa kidijitali kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa na kimataifa.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar

Ni sahihi kwamba ZAECA kwa sasa haina mfumo maalum kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa kimahakama na kukusanya ushahidi wa kidigitali (digital evidence), hata hivyo ZAECA imekuwa na ushirikiano na taasisi mbali mbali za kiuchunguzi ndani na nje ya Zanzibar zinazoiwezesha ZAECA kupata taarifa na ushahidi wa kidigitali ambao utatumika Mahakamani kila itapoonekana kuna uhitaji wa ushahidi huo.

Kwa upande wa upatikanaji wa ushahidi wa kielektroniki na kidigitali ikiwemo nyaraka za kielektroniki na data, ZAECA kwa kuzingatia mnyororo wa kiushahidi “chain of custody”, imekuwa ikishirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa “TAKUKURU” pamoja na Jeshi la Polisi Tanzania katika ukusanyaji wa ushahidi kutokana na kwamba Taasisi hizo zina mfumo wezeshi kwa ajili ya upatikanaji wa ushahidi wa kitaalamu. Mashirikiano hayo yanakuja kutokana na kuwepo kwa hati ya maelewano “Memorandum of Understanding” kati ya ZAECA na TAKUKURU ambapo pamoja na mambo mengine moja ya eneo la mashirikiano ni kuwepo kwa msaada wa kiuchunguzi baina ya Taasisi hizo.

Kwa kawaida ushahidi wa kielektroniki zao lake ni kupatikana kwa hati ngumu “hard copy” ya taarifa zilizohifadhiwa katika mfumo husika wa kielektroniki unaofanyiwa uchunguzi, nakla hiyo kwa kawaida ndio inayotumika Mahkamani kama sehemu ya ushahidi katika kuthibitisha taarifa inayochunguzwa katika mfumo wa kielektroniki husika.

Katika hatua nyengine, ZAECA kupitia mradi wa BSAAT-Z unaofadhiliwa na Serikali ya Uingereza, imepanga kununua vifaa maalum kwa ajili ya uchunguzi, uhifadhi na unyonyaji wa taarifa za kielektroniki kutoka katika mifumo ya kidigitali inayofanyiwa uchunguzi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imeridhika na hatua za utekelezaji wa hoja hii pamoja na mipango ambayo ZAECA imekua ikifanya ili kuweza kukusanya Ushahidi kidijitali.

Hoja Nambari 4.1.4.11: Kukosekana kwa “Sophos Firewall” katika Afisi za Mikoa za Mamlaka ya Kuzuia na Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibaar.

Ukaguzi ulibaini kutokuwepo kwa Firewall katika Afisi za Mikoa za Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA Regional Offices).

Hali hii inapelekea matumizi yote ya kimtandao katika Afisi za Mikoa kwa upande wa Unguja kutokuwa na usalama wa kutosha jambo ambalo ni kinyume na Matakwa ya Miongozo ya Serikali 2022, kifungu nambari 6.3.1 Kinachozitaka Taasisi za Umma kuweka njia za kiusalama katika Matumizi ya Kimtandao katika Afisi za Umma.

Kukosekana kwa kifaa cha kuweka usalama wa mtandao (Network) kunaweza kupelekea kuvuja au kudukuliwa kwa taarifa muhimu za Serikali na hivyo kusababisha hatari ya kukosekana kwa Usiri, Uadilifu, na Upatikanaji wa taarifa za Serikali zinazochakatwa, kusafirishwa na kuhifadhiwa katika mifumo na vifaa nyengine vya TEHAMA vinavyotumika ZAECA na kusababisha kupotea, kuharibiwa ama kudukuliwa kirahisi na watu wasiohusika na kutokuwa na nia njema na Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kuchukuwa hatua za makusudi za kuboresha Teknolojia ya kimtandao ya Mamlaka ili kuimarisha usalama na kuongeza tija na ufanisi wa ZAECA kupitia matumizi ya TEHAMA.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar

ZAECA ina Afisi 5 katika mikoa 5 ya Unguja na Pemba. Baadhi ya afisi zake zinazo huduma za mifumo ya mawasiliano na mtandao na nyengine hazina kama ifuatavyo;

- Afisi ya HQ na mkoa wa Mjini magharibi → huduma ipo
- Afisi ya mkoa wa kusini Unguja → huduma ipo nusu
- Afisi ya mkoa wa kaskazini Unguja → huduma haipo kabisa
- Afisi ya mkoa wa kusini Pemba → huduma ipo nusu
- Afisi ya mkoa wa kaskazini Pemba –→ huduma ipo

Kwa afisi ambazo huduma ipo na kifaa cha ulinzi “Sophos Firewall” pia kipo, maana yake afisi ya makao makuu na ya mkoa wa kaskazini Pemba kifaa kipo na hizi ndio afisi kongwe ambazo ZAECA inazitumia.

Afisi zilizobaki ni afisi mpya ambazo tumehamia karibuni, huduma ipo nusu maana yake hakuna mfumo wa mawasiliano ndani ya afisi na kunatumika intaneti ya dharura ya TTCL huku mchakato wa kupeleka mkonga wa taifa tayari umeanza kiambatanisho G kinahusika. Mara tu baada ya mkonga kufika na kifaa kitalazimika kuwepo ili watumishi wa afisi hizo nao wapate kuweza kutumia huduma za Serikali kama E-office na nyenginezo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imeridhika na hatua za utekelezaji zilizochukuliwa na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar.

Hoja Nambari 4.1.4.12: Kutokufanyika kwa Mafunzo ya Kujikinga na Uhalifu wa kimtandao (Cyber Security Awareness Training) kwa watumishi wa ZAECA.

Mpango wa mafunzo ya uelewa juu ya masuala ya ulinzi na usalama wa matumizi ya TEHAMA ni mpango mahsusi ulio na lengo la kuwajengea uwezo watumiaji wa mifumo pamoja na vifaa vya TEHAMA dhidi ya matokeo ya uhalifu wa kimtandao (cyber crime) pamoja na uingizwaji wa programu hatarishi “malicious software” unaoweza kuiathiri Mamlaka.

Aidha, ukaguzi ulibaini ZAECA kutokua na mpango mahsusi wa kutoa mafunzo ya usalama wa Kimtandao (Cyber Security Awareness Training) kwa watendaji wake licha ya kuwa watendaji hao hutumia vifaa vya kielektroniki, miundombinu ya Kimtandao pamoja na mifumo ya TEHAMA katika kazi zao za kila siku.

Hali hii inaenda kinyume na Matakwa ya Muongozo wa utengenezaji wa Sera za ulinzi wa TEHAMA kutoka Wakala wa Serikali mtandao Zanzibar kipengele nambari 2.8.4.1 kinachozungumzia utowaji wa elimu kuhusiana na Makosa na Usalama wa kimtandao kwa watumishi wa Taasisi za Umma katika ngazi zote.

Kushindwa kuilinda Mamlaka dhidi ya wahalifu wa mitandao (hacker) pamoja na programu hatarishi (malicious software) hali inayoweza kusababisha uvujaji wa taarifa (data breach) nyeti za Mamlaka na hivyo kuisababishia Serikali Gharama kubwa katika kupambana dhidi ya Uhalifu wa aina hiyo pamoja na kukosekana kurejeshwa kwa taarifa muhimu ambazo zilipata mashambulizi au kupotea kwa njia ya mitandao.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kuandaa Mpango wa mafunzo ya Usalama wa Kimtandao kwa watumishi wake katika ngazi zote ili kuhakikisha kwamba kila mtumishi anachukuwa tahadhari za mashambulizi ya kimtandao kupitia matumizi ya mifumo na vifaa mbali mbali vya TEHAMA. Aidha, mafunzo haya yanatakiwa kutolewa angalau mara moja kila mwaka kwa watumishi wote Unguja na Pemba.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar

Kwenye hoja hii 4.1.4.12 ZAECA tunakubali hatukuweza kuwapa mafunzo ya uhalifu wa kimtandao watumishi wetu wote na badala yake tumempatia mtumishi mmoja tu kutoka kitengo cha TEHAMA ambae tayari ameshawashirikisha wenzake kwenye kitengo cha TEHAMA na sasa wako tayari kutoa Elimu na ujuzi huo kwa watumishi waliobaki.

Hivyo kutokana na umuhimu wa mafunzo haya tayari tumepanga kupitia mpango wetu wa mafunzo wa mwaka wa fedha 2024/2025 kuwapatia

mafunzo hayo watumishi wote Unguja na Pemba kadri ya rasilimali wakati itakavyo ruhusu.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati baada ya kupitia mpango wa Mafunzo wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar imeridhika na majibu yaliyowasilishwa mbele ya Kamati

Hoja Nambari 4.1.4.13: Kutofungwa kwa Mfumo wa Kamera za Ulinzi katika Afisi za ZAECA

Mfumo wa Kamera za CCTV unasaidia kuonesha kumbukumbu za matukio yote yanayofanyika katika mazingira ya Afisi kwa lengo la kutunza ushahidi kwa ajili ya hatua nyengine za haki kwenye vyombo husika ikiwa kumetokezea uhalifu wa aina yoyote.

Kwa kuzingatia Kifungu nambari 4.3.4 cha muongozo wa Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ), 2022, Taasisi inatakiwa kuhakikisha uwepo Usanifu wa Usalama wa Mamlaka (Institutional Security Architecture) ambao utahakikisha upatikanaji wa usalama wa taarifa na nyenzo muhimu za TEHAMA.

Katika kufanya mapitio ya mfumo wa Ulinzi kwa kutumia kamera katika Afisi kuu pamoja na Afisi za Mikoa za ZAECA Unguja, ili kuangalia utendaji kazi wa mfumo huo, ukaguzi ulibaini kutokufungwa kwa mfumo wa CCTV camera katika Afisi hizo licha ya kubainika katika Afisi Kuu uwepo wa vifaa vinavyoweza kuwezesha kufanya kazi kwa mfumo huo ikiwemo Mashine ya kurikodia matukio (NVR) pamoja na kamera.

Hali hii imesababisha kukosekana kwa taarifa za ulinzi na ushahidi kwa njia za kidijitali katika maeneo yote ya Afisi kuu za ZAECA yaliyopo Kilimani.

Vile vile kwa kuzingatia umuhimu wa usalama katika mazingira ya Afisi za ZAECA ambazo pamoja na mambo mengine hushikilia mali na vitu mbali mbali vya thamani kama ushahidi wa matukio ya Rushwa na Uhujumu Uchumi kutoka kwa wananchi kunaweza kuongeza hatari (risk) ya mali hizo kuharibiwa, kuibiwa, au kupotezwa ushahidi katika maeneo ya himaya ya ZAECA na hatimae kushindwa kujulikana waliohusika kuondoa ushahidi huo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kuandaa mpango na kutekeleza ufungaji wa Kamera za Ulinzi kuanzia katika hatua ya kuandaa michoro ya mtandao wa Kamera hadi Nyaraka ya Usanifu wa kiusalama kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa na kimataifa ikiwa ni hatua muhimu za kuboresha usalama na kuhakikisha upatikanaji wa ushahidi wa uhakika endapo uhalifu wa aina yoyote utatokea katika mazingira ya Afisi.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar

ZAECA ilifanya jitihada za kutaka kufunga kamera za ulinzi katika jengo la afisi ya Makao makuu, ilitafuta mshauri elekezi ambae alifanya BOQ na kutukabidhi, **kiambatanisho H** kinahusika.

Hata hivyo kutokana na gharama kubwa na upatikanaji wa rasilimali fedha, na kwa kuwa tayari mpango wa ujenzi wa jengo lake la makao makuu umeanza, kamera za ulinzi zitafungwa kwenye jengo hilo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imeridhika na hatua za utekelezaji ambazo zimechukuliwa na Mamlaka ambapo kwa ujenzi wa jengo jipya masuala yote ya usalama yamezingatiwa ikiwemo ufungwaji wa kamera katika maeneo yote ya jengo.

MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR (ZRA)

Hoja Nambari 4.1.10.1: Kutoshirikishwa kikamilifu Kitengo cha TEHAMA cha ZRA katika mchakato wa Utengenezwaji wa Mfumo wa ZIDRAS

Kwa mujibu wa utaratibu unaokubalika (best practice) kwenye uanzishwaji wa Miradi ya Mifumo ya TEHAMA kwa Taasisi za Umma unahitaji kuwepo kwa ushirikishwaji uliokamilika kwa watumiaji na wasimamizi wa Mifumo wa TEHAMA kuanzia hatua za awali hadi hatua za mwisho za utengenezaji wa Mifumo ya TEHAMA. Vivile taratibu zinahitaji wasimamizi wa ndani wa mfumo wa TEHAMA kupatiwa elimu kuhusiana na aina ya kodi asili (source codes) zilizotumika kutengeneza mifumo, lugha na jukwaa lililotumika kwenye utengenezaji wa Mifumo (programming language & framework/platform) na vile vile kupatiwa mazingira ya majaribio ya kutengeneza Mifumo (Test Environment) ili kuwaandaa vyema wasimamizi kwa kuwapatia uelewa mkubwa wa kusimamia, kuendesha na kudumisha Mifumo hiyo ili kupunguza gharama kubwa za utegemezi pindipo watakapokabidhiwa rasmi baada ya kukamilika hatua za utengenezwaji.

ZIDRAS ni mfumo wa TEHAMA uliotengenezwa na wataalamu wa ICT kutoka Kampuni ya UBX chini ya usimamizi wa eGAZ, ambapo eGAZ ilisaini mkataba na UBX kwa ajili ya utengenezwaji wa Mfumo huo utakaotumiwa na ZRA kwa shughuli kuu za biashara ya makusanyo ya kodi. Aidha mfumo wa ZIDRAS, umekuja ili kuondosha changamoto na dosari za kiutendaji na kiusalama zilizokuwa zikitokea katika Mfumo wa awali wa ZITAS.

Ukaguzi uliofanyika ulibaini kuwa kitengo cha TEHAMA cha Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) hakikushirikishwa kikamilifu katika mchakato wa utengenezwaji wa Mfumo wa ZIDRAS ambapo imebainika mchakato huo ulikuwa ukifanyika baina ya eGAZ na UBX pekee kwa kipindi kirefu cha utengenezwaji licha ya kuwa Wasimamizi wakuu wa mfumo huo baada ya kukamilika ni Kitengo cha TEHAMA cha ZRA.

Hadi ukaguzi unakamilika, mfumo wa ZIDRAS ulikuwa umeanza kutumika kwa kipindi cha zaidi ya miezi sita nyuma kwa baadhi ya Taasisi lakini Kitengo cha TEHAMA hakikuwa na uelewa juu na Usimamizi, Uendeshaji, Udumishaji na hali ya Usalama wa taarifa za makusanyo ndani ya mfumo pamoja na kanzidata yake.

Kutoshirikishwa kikamilifu kwa Kitengo cha TEHAMA katika michakato ya utengenezwaji wa mifumo ya ndani ya Mamlaka kunaweza kusababisha wataalamu wa ndani ya Kitengo cha TEHAMA kushindwa kudhibiti mifumo ya Mamlaka kikamilifu na kuondokewa na ari, imani, morali na nguvu ya kusimamia mifumo hiyo jambo ambalo litapelekea kushindwa kutoa msaada wa kiufundi kwa watumiaji wa mifumo ndani ya Afisi na

hatimae kusababishakuzorota kwa kazi, kuendelea kutegemea watu wa nje ya Mamlaka jambo ambalo litachochea kuongeza gharama za uendeshaji na kuingiza hasara Serikali bila ya kupatikana tija iliyokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) katika Miradi yake ijayo kuchukuwa jitihada kubwa za kuhakikisha watendaji wake wa Kitengo cha TEHAMA wanashirikishwa kikamilifu kwenye michakato yote ya Miradi ya TEHAMA inayohusiana na Mamlaka ili kuepusha dosari zinazoweza kujitokeza baadae na kuigharimu Mamlaka na Serikali kutokana na udhaifu unaoweza kujitokeza kwenye Usimamizi, Uendeshaji na Udumishaji wa Mifumona Miundombinu ya TEHAMA ya Mamlaka.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar

Mfumo wa ZIDRAS unatengenezwa na kampuni ya UBX Tanzania Limited chini ya usimamizi wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kwa kuzingatia Mkataba Mkuu baina ya pande hizo mbili. Kwa kuzingatia umuhimu wa ushirikishwaji wa watendaji wa TEHAMA wa ZRA, Mamlaka ilifanya mchakato wa kuumiliki mfumo wa ZIDRAS Kwa kuhakikisha inafunga mkataba moja Kwa moja na kampuni inayotengeneza Mfumo wa ZIDRSA. Hatimae, mnamo mwezi March 2024 Mamlaka ilifanikiwa kufunga mkataba baina baina ya ZRA na UBX Kwa ajili ya kutengeneza mfumo huo kulingana na mahitaji ya Mamlaka. Moja ya miongoni mwa vipengele muhimu vilivyozingatiwa ni utaratibu wa uwezeshwaji wa wataalamu wa utengenezaji mifumo wa Mamlaka ili waweze kuusimamia na kutengeneza mfumo wa ZIDRAS kulingana na mahitaji yatakavyojitokesha.

Hivyo, baada ya kukamilika Kwa uundwaji wa mfumo wa ZIDRAS hatua inayofata ni kuhaulisha taaluma (knowledge transfer) kutoka Kwa wataalamu wa UBX kuja Kwa wataalamu wa ZRA.

Hata hivyo, watendaji wa Idara ya TEHAMA walishiriki Kwa kuandaa mahitaji ya mfumo wa ZIDRAS baada ya kupokea kutoka Kwa idara tumizi za mfumo huo na kuziwasilisha Kwa UBX Kwa ajili ya kutengenezwa.

Sambamba na hayo, Idara ya TEHAMA Kwa kushirikiana na Kamati ya Mfumo wa ZIDRAS (ZIDRAS Steering committee) imeshawakilisha pendekezo la kupatikana watendaji wa ziada katika divisheni ya uandaaji na uchambuzi mifumo watakao tumika kwa ajili uendelezaji wa ujenzi wa mfumo wa ZIDRAS.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba ni kweli wataalamu wa kitengo cha TEHAMA cha Mamlaka ya Mapato Zanzibar hawakushirikishwa tangu kuanza kwa utengenezaji wa mfumo wa ZIDRAS. Kutoshirikishwa kwa watendaji wa TEHAMA kunapelekea kwa wataalamu hao taarifa ndogo ndogo na muhimu wakati wa utengenezaji wamfumo Pamoja na changamoto zinazotokea,

jambo ambalo lingewajengea uzoefu wataalamu hao kwa kiasi kikubwa sana. Kamati inashauri kwamba kwa miradi ijayo Mamlaka ya Mapato Zanzibar ihakikishe wataalamu wa TEHAMA wanashiri.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaielekeza Mamlaka ya Mapato Zanzibar kuhakikisha kwa miradi ijayo watendaji wa TEHAMA wanashirikishwa kwa hatua zote ili kuwajengea uwezo na ufahamu wa mifumo ambayo itatengenezwa.

Hoja Nambari 4.1.10.2: Dosari katika utendaji kazi wa Mfumo wa ZIDRAS

Ukaguzi ulifanya mapitio ya Mfumo wa ZIDRAS kwa lengo la kuhakiki na kutathmini ufanisi wa utendaji kazi wa mfumo hususan katika eneo la usalamana michakato ya usimamizi wa makusanyo ya kodi. Licha ya mfumo kuendelea kufanya kazi kwa zaidi ya miezi sita baada ya kukamilika kwa utengenezwaji wake, hadi ukaguzi unakamilika ulibaini kuwepo kwa dosari za kiutendaji katika mfumo huo, baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Kushindwa kufanya kazi kwa moduli ndogo ya Uhakiki wa Marejesho ya Kodi (Tax Return Vetting)

Katika Mfumo wa ZIDRAS, moduli ndogo ya Uhakiki wa Marejesho ya Kodi (Tax Return Vetting) imegawika katika vipengele (section) vikuu viwili ambavyo ni Marejesho ya Ushuru wa Ndani (Domestic Tax Return - DTR) na Marejesho ya Mapato Yasiyo ya Kodi (Non Tax Income Return - NTR). Ukaguzi ulibaini kuwa kipengele cha Marejesho ya Mapato Yasiyo ya Kodi (NTR) hakiwezi kuonyesha taarifa zozote kuhusiana na mapato yasio ya kodi, jambo ambalo linawapa ugumu watendaji wa Idara ya NTR wanapohitaji kupata taarifa za Mapato yasiyo ya Kodi kutoka kwenye mfumo wa ZIDRAS. Hali hii husababishawatendaji hao kutumia kipengele chengine cha Marejesho ya Ushuru wa Ndani (DTR) ili kuweza kuzivuta data za NTR na kuzipata taarifa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zao.

- Kutokuwepo kwa moduli ya kuweka Taarifa za makusanyo ya Ndege Binafsi (Private Charters)

Ukaguzi ulibaini kuwa Mfumo wa ZIDRAS hauna moduli/sehemu ya kuingiza taarifa za mapato (marejesho) kutoka kwa Kampuni zenye kutumia ndege Binafsi na sio Ndege za Biashara. Hali hii hupelekea taarifa za makusanyo kwa ndege hizo kuingizwa kwa njia ya kawaida kwenye mfumo wa zamaniwa ZITAS kutokana na Mfumo mpya wa ZIDRAS kukosa sehemu za kuingiza Taarifa za Ndege hizo.

- Kutokufanya kazi kikamilifu kwa moduli ya Ripoti kwenye Mfumo wa ZIDRAS

Ukaguzi ulibaini kuwa moduli ya Ripoti katika mfumo wa ZIDRAS bado ina changamoto ya utendaji kazi kutokana na kushindwa kutoa ripoti muhimu za makusanyo ya mapato na madeni. Baadhi ya ripoti ambazo bado hazipatikanikatika mfumo wa ZIDRAS ni pamoja na Ripoti za Marejesho ya Ritani, Ripotiza Madeni, Ripoti za Walipa kodi kwa Kila mwezi, miezi mitatu, miezi sita, mwaka, Ripoti za makusanyo ya kila siku zinazotokana na huduma za tozo zaViwanja vya Ndege na ada za usalama n.k.

- Mfumo kushindwa kutoa taarifa za ukumbusho "Notification Message" kwa Walipakodi kuhusu tarehe zao za kuwasilisha Ritani zinapofika (due date)

Ukaguzi umebaini kuwa ZIDRAS haiwezi kuwakumbusha wateja kwa kutumianjia ya barua pepe, SMS au njia nyingine yoyote kuhusu kuwasilisha marejesho yao pindipo tarehe za malipo zitakapofikiwa jambo ambalo ni kinyume na mahitaji ya mfumo.

- ZIDRAS kushindwa kuchuja na kuonyesha taarifa kwa mujibu wa mahitaji ya watumiaji wa Mfumo

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya Kampuni za Ndege kama KLM, QATAR, FLY DUBAI, KENYA, UGANDA, TURKISH na ETHIOPIA tayari zimetoa tamko rasmi kwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kwamba Kampuni hizo zitalipia ada za tozo (ushuru) kwa kutumia shilingi ya Kitanzania (Tsh.) na sio Dola yaKimarekani (USD).

Hata hivyo, Mfumo wa ZIDRAS unashindwa kubagua taarifa za malipo ya USD na malipo ya Tshs. Katika moduli ya NTR, na badala yake huonyesha aina zote mbili za taarifa za malipo (Tsh & USD) katika sehemu ya Ritani za Ushuru wa Uwanja wa Ndege, hivyo wakati mwingine inaleta mkanganyiko wa taarifa za mapato kwa upande wa watendaji wa Idara ya NTR ambao hushughulika na Taarifa hizo wakati wanapofanya kazi ya kuthibitisha na kuidhinisha taarifa za malipo.

Kuwepo kwa changamoto hizo kunaweza kusababisha kutopatikana kwa ripoti sahihi zinazotolewa na ZIDRAS na hatimae kukosekana kwa tija na ufanisi wa utendaji wa Mfumo huo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZRA kuhakikisha kuwa mfumo wa ZIDRAS unafanyiwa marekebisho haraka iwezekanavyo kutokana na mapungufu yote yaliyobainika ili kuweza kutumika kwa ufanisi na kupatikana kwa tija iliyokusudiwa.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar

Mamlaka inakubaliana na mapendekezo ya Mkaguzi.

- Mamlaka ilishayabaini mapungufu yaliyoibuliwa na Mkaguzi kabla ya zoezi la ukaguzi na kuanza kuupitia upya mfumo wa ZIDRAS wote ili

kuboresha utendaji kazi wake Kwa kuhakikisha mfumo unaendana na utendaji kazi wa sasa wa Mamlaka.

- Mamlaka imeshafanya mapitio ya mfumo mzima wa ZIDRAS ili kuboresha utendaji kazi wake Kwa Kwa kueka vipengele vyote muhimu katika mfumo wa ZIDRAS.
- Kipengele cha tax return vetting kwa sasa kinafanya fanya kazi vyema, na kinatumika kupokea ritani zote zinazowasilishwa mwisho wa mwezi.
- Mamlaka limefuatilia suala hili na sasa Mfumo wa ZIDRAS una moduli inayojitegemea kwa ajili ya kupokea makusanyo yanayotokana na biashara ya Ndege Binafsi (Private Charters)
- Mfumo wa ZIDRAS sasa una uwezo wa kutoa ripoti tofauti kwa mujibu wa mahitaji yaliyotolewa na watumiaji ripoti hizo, Kama vile ripoti za Marejesho ya Ritani, Ripoti za Madeni n.k.
- Mfumo Kwa sasa umeshaanza kutoa taarifa za ukumbusho Kwa walipakodi ikikaribia “due date”.
- Baada ya kuonekana mapungufu ya kutoweza kuchuja kwa mujibu wa mahitaji, Mamlaka umeurekebisha Mfumo wa ZIDRAS na sasa watumiaji wana uwezo wa kuchukua taarifa kama vile kubaguwa malipo ya ritani yaliyolipwa kwa kutumia TZS na USD
- Baada ya kukamilika Kwa mapitio ya mfumo wote wa ZIDRAS, Module ya report ni miongoni mwa module mpya zilizoingizwa kwenye mfumo wa ZIDRAs ili watumiaji waweze kuvuta taarifa wanazizihitaka.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC baada ya kufanya uchunguzi imethibitisha kwamba dosari zilizoibuliwa na Mkaguzi zimeshafanyiwa kazi ambapo katika mfumo kilaanina ya mlipa kodi anaonekana katika “column” yake ambapo wakipa kodi wakubwa wanaonekana katika sehemu zao, walipa kodi wa kati na wadogo wanaonekana katika sehemu yao pamoja na mapato yasiokua ya kodi yanaonekana katika “column” yake.

Kwa mnasaba huo, Kamati imeridhika na majibu ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar na kufanya maamuzi ya kuiondoa hoja hii.

Hoja Nambari 4.1.10.3: Dosari katika Ukusanyaji wa Mapato yatokanayo na Kodiza Bandari na Viwanja vya Ndege

Moja kati ya aina za mapato yanayokusanywa na ZRA ni Mapato Yasiyo ya Kodi (Non Tax Revenues) ambapo mapato hayo hutokana na vyanzo mbali mbali kama vile Ada za Bandari na Uwanja wa Ndege, Ada za leseni, Ada za Usajiliwa Vyombo vya Moto n.k.

Mapato yasiyo ya kodi hukusanywa kila mwezi kupitia taarifa zinazowasilishwa ZRA (Files Returns) kutoka kwa Wateja wake ambao ni

Kampuni za Meli za Abiria na Migizo, Kampuni za Ndege, waombaji wa leseni za udereva, wanaosajili vyombo vya moto n.k.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba taarifa nyingi za mapato (File Retuns) zinazoingizwa kwenye mfumo wa ZIDRAS kuhusiana na makusanyo ya ada za Bandari na Uwanja wa Ndege hazina uhakika wa usahihi wake kutokana na taarifa hizo kukusanywa na kuingizwa kwenye mfumo wa ZIDRAS kwa njia ya kawaida (manually) badala ya kupitia muunganiko wa mifumo (systems integration).

Hali hii imebainika kutokana na kuwepo kwa tofauti baina ya taarifa za idadi ya abiria zinazowasilishwa kutoka kwa Wateja (Airlines & Marine Ferries) kupitia "Manifest" na taarifa za abiria zinazowasilishwa na watendaji wa ZRA kwa njia ya "Excel Files" kutoka maeneo hayo ya makusanyo (Uwanja wa Ndege na Bandarini) jambo ambalo ZRA hupata tabu katika kuthibitisha usahihi wa taarifa hizo.

Aidha hali hii imetokana na kukosekana kwa muunganiko wa moja kwa moja (integration) baina ya Mfumo wa ZIDRAS na mifumo ya wateja wanaolipa ada za Bandari (Kampuni za Meli na Ndege).

Kuwepo kwa utofauti kwenye taarifa za abiria wanaosafiri kunaweza kusababisha ZRA kushindwa kufikia malengo ya makusanyo yasiyo ya kodi kutokana na kutopatikana kwa taarifa sahihi jambo ambalo linaweza kuingiza hasara kwa Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZRA kufanya jitihada za kuunganisha moja kwa moja mfumo wa ZIDRAS pamoja na mifumo ya wateja wao wanaolipa ada za bandari (Kampuni za Meli na Ndege) ili kupatikana taarifa sahihi za abiria waliosafiri na hatimae kuepuka udanganyifu unaoweza kujitokeza kwenye taarifa za abiria kutokana na mchakato huo kufanyika manually kwa sasa.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar

ZRA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) kwa kutumia watengenezaji wake wa ndani imetengeza wigo wa utendaji kazi katika mfumo wa VFMS wa kunasa taarifa zote za mgeni anayefika na kuondoka (**GADIS**) katika uwanja wa ndege wa Zanzibar ili kupata taarifa sahihi kwa madhumuni ya kuepusha hitilafu yoyote katika faili ya maelezo, Jaribio la Kukubalika kwa Mtumiaji limekamilika na utumiaji wa kipengele hiki umeshakamilika Kwa ajili ya matumizi. Mfumo wa VFMS tayari umeunganishwa na mfumo wa ZIDRAS, hivyo basi kuondoa ukusanyaji wa ushuru wa bandari mwenyewe.

Mfumo huo Kwa sasa umeaza kutumika

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imeridhishwa na hatua ambazo ZRA imechukua katika kuhakikisha inaunganisha mfumo wake na mifumo ya Viwanja vya ndege na Bandari ambapo mpaka sasa tayari mfumo ya Viwanja vya ndege pamoja na mfumo wa Kampuni ya Meli ya IKRAM.

Halkadhalika, Kamati imeelezwa kwamba kwasasa ZRA inafanya jitihada za kuweza kuunganisha mifumo ya Kampuni za Azam Marine pamoja na ZanFast Ferries.

Kwa hatua hizo, Kamati imeridhika na hatua zilizochukuliwa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar.

Hoja Nambari 4.1.10.4: Dosari katika Muunganiko wa Mfumo wa ZIDRAS na Mfumo wa Ikram Sealine Company

Ukaguzi ulifanya uhakiki wa muunganiko (Integration) uliopo baina ya Mfumo wa ZIDRAS na Mfumo wa Meli ya **Ikram Sealine Company** kwa lengo la kuangalia aina gani ya taarifa za makusanyo zinazoingia kwenye mfumo wa ZIDRAS kutoka kwenye mfumo wa Ikram Sealine Company.

Kwa mujibu wa maelezo ya watendaji wa Idara ya NTR kutoka ZRA taarifa za makusanyo zilizohitajika kuunganishwa kwenye mfumo wa ZIDRAS ni pamoja na taarifa za makusanyo yatokanayo na idadi ya abiria waliosafiri, makusanyo yanayotokana na migizo (cargo and parcels) pamoja na taarifa za magari yaliyopakia mizigo (Freight Shipping Trucks).

Dosari iliyobainika katika muunganiko huo ni kwamba mfumo wa Ikram Sealine Company unaingiza taarifa za makusanyo ya mizigo midogo midogo tu (parcel) na sio taarifa zote kwa mujibu wa makubaliano ya uunganishwaji kama vile taarifa za idadi ya abiria waliosafiri na idadi ya mizigo mikubwa (cargo).

Hali hii husababisha kuwepo kwa upotevu wa mapato kutokana na kutopatikana kwa taarifa za idadi ya abiria wanaosafiri, idadi ya mizigo (cargo) iliyosafirishwa pamoja na taarifa za magari yaliyopakia mizigo katika Meli hiyo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZRA kufanya jitihada za makusudi za kuhakikisha taarifa zote za makusanyo ya Meli ya Ikraam Sealine zinaingizwa katika Mfumo wa ZIDRAS jambo ambalo litapelekea kuimarika kwa makusanyo na hatimae Serikali kupata fedha nyingi za maendeleo.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar

Uunganishaji kati ya kampuni ya Ikram sea line na mfumo wa VFMS umekamilika kikamilifu na taarifa zote za abiria na vifurushi huhamishiwa kwenye mfumo wa VFMS kwa kuunganishwa.

Muunganiko baina ya Mfumo wa Meli ya Ikram Sealine Company umekamilika na unafanya kazi kikamilifu kwa kutuma taarifa za abiria wanao panda meli Pamoja na taarifa za mizigo (parcel)

Taarifa hizo hupelekwa kwenye mfumo ZIDRAS kupitia muungalniko uliopo baina ya VFMS na ZIDRAS kwa ajili ya matumizi ya “return filing”

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar ambapo tayari ZRA imeshafanya muunganisho baina ya mfumo wa Kampuni ya Meli ya Ikram na mfumo wa ZIDRAS.

Hoja Nambari 4.1.10.5: Kuchelewa kuunganishwa kwa Mifumo ya Makusanyo ya Mapato ya Kampuni ya AZAM, ZAN FAST FERRIES na Mfumo wa ZIDRAS

AZAM MARINE na ZAN FAST FERRIES ni miongoni mwa kampuni kubwa zilizopo Zanzibar zinazofanya biashara ya usafirishaji wa abiria na mizigo yao kupitia njia ya Bahari (Coastal Travel).

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kampuni hizo bado zinakwepa kuunganisha mifumo yao yenye taarifa za makusanyo ya abiria na mizigo pamoja na mfumo wa ZIDRAS, badala yake taarifa zao huziwasilisha ZRA kwa njia ya kawaida (manually) kupitia ‘manifest paper’ zilizojazwa kwa mkono. Aidha, imebainika kwamba hii ni moja kati ya mbinu zinazotumiwa na kampuni hizo kukwepa kodi kwa kutokuwasilisha idadi halisi ya abiria waliosafiri pamoja na mizigo iliyomo jambo ambalo ZRA hushindwa kufahamu na hupata changamoto nyingi katika kubaini idadi halisi ya abiria waliosafiri pamoja na mizigo yao.

ZRA kushindwa kutambua idadi halisi ya makusanyo inayohitajika kupatikana kutokana na makusanyo ya Kampuni hizo kunapelekea kushindwa kufahamu mapato halisi na hatimae kujitokeza kwa upotevu wa mapato kwa Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZRA kwa kushirikiana na uongozi wa Shirika la Bandari na Serikali kuchukuwa jitihada za makusudi za kuyataka makampuni ya AZAM MARINE, ZAN FAST FERRIES na nyenginezo kuunganisha moja kwa moja mifumo yao na Mfumo wa kukusanya Mapato wa ZRA kwa utaratibu maalum ili taarifa za abiria, mizigo na nyenginezo zinazohitajika ziweze kuingizwa kwenye mfumo wa ZIDRAS na kupatikana mapato halisi.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar

ZRA imetoa barua za utekelezaji kwa barua ya Azam Marine Ltd yenye namba rejea ZRB/TS/A.1/VOL.1/90 ya tarehe 21 Septemba, 2023 na barua ya Zan Fast Ferries Ltd yenye namba za kumbukumbu ZRB/TS/Z.1/

VOL.1/55 ya tarehe 21 Septemba 2023, zaidi ya hayo ZRA imechukua hatua zaidi kwa kupanga mikutano ya mtandaoni na ya kimwili kati ya timu za ufundi za ZRA ICT na mafundi wa TEHAMA wa Azam Marine Ltd kwa ajili ya kupata msaada wa kiufundi ili kuharakisha mchakato wa muunganisho. Kwa sasa Mamlaka imeshatoa barua ya mwisho ya ukumbusho wa kukamishiasha muunganisho Kwa kampuni hizo mbili na kuwataka wakamilishe ndani ya mwezi wa August 2024.

Kwa upande wa Azam Marine, mfumo wao haukuwa umetengenezwa ili na watu wengine waweze kuvuta taarifa(consumable) ulikuwa ni Kwa ajili ya matumizi ya Azam marine tu. Hivyo baada ya kupokea takwa la kujiunga na Mfumo wa VFMS ndipo walipoanza kufanya mawasiliano na Mtengenezaji mfumo wao ambae yupo nje ya nchi" alisema mtaalamu wao wa ICT".

Kwa sasa Agizo wamelitekeleza Kwa kurekebisha mfumo wao ili uweze kuunganishwa na mfumo wetu na wameshaanza kuungamnisha na ziko mwishoni kumalizia ujengwaji wa muunganiko baina ya mifumo yao na mfumo wa VFMS Kwa sasa wamefikia asilimia 85% Kwa mujibu wa barua yao yenye kumbukumbu No. Fef: AM.ZRA-INT-10/24.

Kwa upande Zan Fast Ferries, wako ukingoni kumalizia muunganisho kupitia Kampuni ya Rahisi iliyopo kilimani, wameshaliza na wanataka kufanya UAT.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imeridhika na hatua zilizochukuliwa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar katika kufanya jitihada za kuiunganisha mifumo ya Kampuni za AZAM MARINE na ZANFAST FERRIES ambapo mpaka Kamati inapita mifumo hiyo imeshaunganishwa kwa asilimia zaidi ya 85. Aidha, Kamati imeelezwa kwamba ifikapo tarehe 31 Disemba 2024, Mamlaka itachukua hatua za mwisho endapo itatokea Kampuni hizo kushindwa kuunganisha mifumo yao na ZRA kikamilifu.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaielekeza Mamlaka ya Mapato Zanzibar kuhakikisha kabla ya Tarehe 31 Disemba 2024 mifumo yote ya Azam Marine na ZanFast Ferries inaunganishwa kikamilifu. Aidha ikitokea mpaka tarehe hiyo mifumo hiyo haijaunganishwa kikamilifu basi hatua stahiki zichukuliwe kama Mamlaka ilivoiahidi Kamati katika kikao kilichofanyika tarehe 11/12/2024.

Hoja Nambari 4.1.10.6: Kukosekana kwa leseni ya Kanzidata ya Mfumo wa ZIDRAS (Oracle Database)

Oracle, kama mifumo mingine iliyotengenezwa na makampuni mbalimbali duniani, huwa na makubaliano maalum katika matumizi ya kanzidata zake za aina ya "Oracle Database".

Kanzidata hizo ili zitumike kwa matumizi ya biashara katika taasisi za Umma na Kampuni binafsi zinapaswa kulipiwa leseni halali ya matumizi. Baada ya kulipiwa leseni Oracle Database inakuwa halali kutumika kibiashara, kupata ulinzi, usalama na inaimarisha udhibiti mzuri wa taarifa zinazoingizwa ndani yake kutokana na vitendo vya uhalifu vinavyofanywa dhidi ya kanzidata hiyo, kwa kupata "online updates and security patches" kupitia mtandao.

Aidha, ukiukwaji wa masharti ya leseni ya matumizi kwa taasisi zinazotumia database hiyo unaweza kusababisha taasisi za umma au kampuni binafsi kuingia katika hatari ya kukosa usalama wa taarifa zake zilizomo na vile vile kuweza kushtakiwa mahakamani ikibainika.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 3.16 cha Toleo la 2 la Sera ya TEHAMA ya ZRB ya mwaka 2021 kinachohusu Usimamizi Bora wa TEHAMA kinaeleza kwamba "Mifumo yote (programu zote) ya ZRA lazima iwe na makubaliano halali ya leseni ambayo yataendana na Sera Kuu ya Programu".

Aidha kifungu nambari 5.2 cha sera hiyo kinachohusu General Software

kinaeleza yafuatayo: -

- Watumiaji wa mifumo lazima watii hakimiliki "copy rights" na matakwa ya leseni "licensing restrictions" pamoja na Sera za ZRA zinazotumika. Rasilimali za TEHAMA haziwezi kutumika kwa kukiuka hakimiliki au mashartiya makubaliano yoyote ya leseni.
- ZRA itatumia programu zenye leseni ambapo Idara ya TEHAMA inawajibika kushughulikia utoaji leseni katika programu hizo kwa usahihi na zilizosasishwa.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba ZRA imekuwa ikitumia kanzidata ya Oracle (Oracle Database) iliyounganishwa na Mfumo Mkuu wa Makusanyo ya Mapato (ZIDRAS) kwa muda mrefu ambapo taarifa zote za makusanyo ya mapato ya walipakodi zinahifadhiwa ndani ya kanzidata hiyo kupitia mfumo wa ZIDRAS.

Dosari iliyobainika ni kwamba kanzidata hiyo imekuwa ikitumika kuhifadhia taarifa za makusanyo ya mapato ya walipakodi bila ya kuwa na leseni ya matumizi kwa kipindi kirefu (expired licences) jambo ambalo linapelekea taarifa za walipakodi kuwa katika hatari kubwa ya kukumbwa na athari kutokana na kutokuwepo kwa ulinzi imara na usalama katika matumizi ya kanzidata hiyo.

Baadhi ya athari zinazoweza kuikumba ZRA kutokana na kutumia kanzidata isiyo na leseni ya matumizi ni kama vile kufutika kwa taarifa za makusanyo ya walipakodi zilizoingizwa, kushambuliwa na virusi au programu hatarishi, kuvamiwa au kudukuliwa kupitia wizi wa mitandao na hatimae kuingizia hasara Serikali.

Aidha, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na vifungu vya sera ya TEHAMA ya ZRA vilivyonakiliwa hapo juu pamoja na kukiuka Makubaliano ya Leseni ya Mtumiaji kwa Kampuni ya Oracle (End User Lisence Agreements - EULAs) ambapo inaweza kusababisha dhima kubwa kwa ZRA.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar kuhakikisha unafanya jitihada za makusudi za kununua leseni halali za matumizi ya rasilimali zote za TEHAMA zinazotumika kwa Taasisi hiyo ikiwemo mifumo, kanzidata, programu pamoja na miundombinu ya TEHAMA ili kuziweka taarifa zake katikahali ya usalama.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar

Uongozi wa ZRA unakubaliana na ushauri wa mkaguzi na taratibu za kununua leseni ya “Oracle” zilifanyika na kubaini kuwa leseni hiyo ni ghali sana. Aidha, ZRA imeomba ushauri kutoka kwa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kwa barua yenye kumbukumbu namba ZRA/FA.61/162/01/57 ya Desemba 20, 2023 ili kupendekeza kanzidata itakayoongeza ulinzi pamoja na kufanya kazi kwa gharama nafuu. gharama kwa mifumo ya ZRA.

Aidha, taratibu za kubadilisha hifadhidata ya oracle zinachukuliwa na zinatarajiwa kukamilika kabla ya kumalizika December 2024.

Baada ya kupata ushauri kutoka taasisi mbali mbali zinazosimamia kodi, washauri wa usalama wa taarifa, serikali mtandao, Mamlaka imefanya maamuzi ya kuwatafuta kampuni ya oracle moja Kwa moja ili kuomba punguzo la gharama za leseni.

Hivyo, Mamlaka imefanikiwa kupata punguzo zuri sana na kurejesha majibu Kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar.

Baada ya kuona punguzo hilo na sababu nyengine za kiusalama, Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar ilipendendekeza tuendelee na hatua za kununua leseni ya oracle na Kwa sasa tayari tenda imeshatangazwa.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwama ni kweli Mamlaka ya Mapato Zanzibar ilikua ikitumia Kanzidata ya Oracle bila kuwepo kwa leseni “Active lisence” ambapo inapelekea kuweka taarifa za mfumo wa Zidras katika hali ya hatari ya kudokolewa.

Halkadhalika, Kamati imebaini sababu zilizopelekea kutonunuliwa kwa leseni ni gharama kubwa ya leseni hiyo ambayo inauzwa kwa gharama ya dola za kimarekani laki sita ($600,000). Mamlaka imeieleza Kamati kwamba kutokana na bei hiyo kuwa kubwa, imefanya jitihada za kuonana na uongozi wa Oracle ili kuomba punguzo la bei na hatimae kukubaliwa kupunguziwa bei kwa kiasi kikubwa sana.

Kamati imeelezwa kwamba tayari Zabuni imeshatolewa na “vendors” tofauti ambao wanatambulika na Oracles wanategemewa kushiriki.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inaielekeza Mamlaka ya Mapato Zanzibar Zabuni hiyo inakamilika kwa wakati na kwa bei sahihi ili taarifa muhimu za mfumo wa ZIDRAS zinakua na udhibiti mzuri na usalama wa uhakika.

Hoja Nambari 4.1.10.7: Tathmini ya Miundombinu ya Mtandao (Review of Network infrastructure)

Ukaguzi ulifanya mapitio ya miundombinu ya Mtandao (Network Infrastructures)na kubaini uwepo wa Swichi aina ya CISCO Small Business 200 zinazotumiwa na Mamlaka kwa shughuli za mawasiliano ya usafirishaji wa taarifa (data) kupitia mifumo yake ya ZIDRAS na VFMS.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini Swichi hizo zimepitwa na wakati ambapo mudawake wa mwisho wa matumizi (End of Life) ni tarehe 04 Oktoba, 2018 na muda wa mwisho wa kupatiwa msaada wa sasisho (End Of Life Support) ni tarehe 31 Oktoba, 2023.

Kuendelea kutumia miundombinu hiyo kunaweza kuathiri hali ya upatikanaji na ufikiaji wa taarifa za kwenye mifumo, aidha kunaweza kuhatarisha usalamawa mifumo ya ndani ya Mamlaka kama vile Mfumo wa VFMS, ZIDRAS na mifumo mingine inayotumika kwa matumizi ya ndani na nje ya Mamlaka.

Matumizi ya vifaa vilivyopitwa na wakati haviwezi tena kupokea sasisho (updates) za kiusalama mtandaoni, na hivyo kuwa na uwezekano wa kuathiriwa na wavamizi wa nje wa kupitia mitandao.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kuhakikisha kuwa unanunua na kufunga vifaa na miundombinu ya kisasa ya mtandao ili kuimarisha ulinzi na usalama wa taarifa dhidi ya mashambulizi yanayotokana na vihatarishi vya mtandao na hatimae kupatikana kwa ufanisi wa utendaji kazi wa vifaa na miundombinu hiyo.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar

ZRA imefanya mapitio ya mtandao kwa ofisi zake zote za ZRA ikiwa ni pamoja na vituo vya mikoa na huduma kwa kuimarisha miundombinu ya ofisi zake kisasa. Kwa sasa vituo vyote vya mikoa na huduma vinatumia swichi mahiri za hivi karibuni, na kwa ZRA HQ ombi la kununua swichi na ruta za hivi karibuni. inawasilishwa kwa Kamishna Jenerali kwa idhini.

Vifaa vimeshanunuliwa na Kwa sasa tunaendelea kubadilisha

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imeridhika na majibu ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar na kujithibitishia kwamba tayari vifaa vyote vimeshanunuliwa na vinaendelea kufungwa. Hivyo, kwa utekelezaji huo hoja hii imeondolewa.

MFUKO WA HIFADHI YA JAMII (ZSSF)

Hoja Nambari 4.1.11.1: Dosari katika Maboresho ya Mfumo wa FuMIS kwa mwaka wa fedha 2022/2023

ZSSF imefunga Mkataba na Kampuni ya Real Tech Limited terehe 28 Novemba, 2022 wenye nambari SMZ/F0308/C/ NCB/2021-2022/06 uliogharimu shilingi 195,290,000 pamoja na VAT kwa ajili ya uboreshaji wa Mfumo Mkuu unaosimamia Mafao ya Wanachama wa ZSSF (FuMIS).

Kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba kazi hiyo ya maboresho ilitakiwa kufanyika kwa kipindi cha miezi sita (6) kuanzia tarehe 01 Disemba, 2022 hadi tarehe 30 Mei, 2023. Hadi ukaguzi unakamilika mnamo mwezi wa Novemba, 2023 kazi hiyo ilikuwa bado haijakamilika ukizingatia kwamba kuna miezi sita (6) mengine ya ziada ilikuwa tayari imeshapita bila ya kuwepo kwa mkataba wa nyongeza (addendum). Licha ya kuongezeka kwa muda huo ukaguzi umebaini kuwa ZSSF haikujumuisha kipengele cha kutoa adhabu (penalt) au tozo kwa mtoa huduma pindipo akishindwa au akichelewa kukabidhi kwa wakati kazi hiyo kwa mujibu wa mkataba.

Kutokamilika kwa maboresho hayo kunapelekea kuchelewa kupatikana kwa huduma bora zilizotarajiwa kutolewa kwa wanachama wa Mfuko kutokana na kufanyika kwa maboresho hayo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZSSF kupitia Idara ya TEHAMA kufuatilia kwa kina juu ya sababu za ucheleweshaji wa maboresho ya mfumo wa GuMIS na kuweka mpango imara wa kufanya upembuzi yakinifu na kuondoa dosari zote zilizopo ambazo zinakwaza kwa njia moja au nyengine zoezi la ukamilishaji wa mfumo huo.

Majibu ya Uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii

Kazi ya kuboresha Mumo wa FUMIs haikukamilika kwa wakati kulingana na muda wa Mkataba kutokana na sababu zifuatazo: -

1. Kutokea utofauti kati Maboresho ya Mfumo na matakwa ya uboreshwaji wa Mfumo kimkataba

Wakati wa uwasilishwaji wa Toleo la kwanza la mfumo ulioandaliwa na Kampuni iliyoshinda zabuni hiyo, Mfuko uligundua kuwa maboresho ya Mfumo yaliyofanywa hayaendani na mahitaji ya kimkataba yaliyowasilishwa katika kikao hicho, hivyo, Uongozi wa Mfuko uliwataka wafanye marekebisho ili maboresho ya mfumo yaendane na mahitaji ya mkataba kabla ya kuanza majaribio ya matumizi ya Mfumo mpya. Hali hii ilipelekea mmiliki wa kampuni hiyo kuwabadilisha wataalamu wake wa awali na kuleta wengine ambao nao iliwachukua muda kufahamu mahitaji na hatimae kuchelewa maboresho ya mfumo huo.

2. Kampuni husika kuondokewa na watalaamu tegemewa kwa mradi huo

Wakati maboresho ya mfumo yanaendelea, baadhi ya wataalam waliacha kazi katika Kampuni hiyo kutokana na kupata kazi kwenye taasisi nyengine kwa kufuata maslahi Zaidi. Hali ambayo ilisababisha mradi kutokamilika kwa wakati.

Kutokana na hali zilizojitokeza hapo juu, Uongozi wa Mfuko uliwaandikia barua (**Kumbukumbu Nambari: ZSSF/AB.218/265/01/62 ya Tarehe 14 JUNI, 2023)** ya kutokuridhishwa na mwenendo na ucheleweshaji wa maboresho ya Mfumo kulingana na muda uliowekwa kimkataba. Hali kadhalika, Mfuko ulisitisha malipo baada ya malipo ya awali ya asilimia 30, kutokana na kuwa yalikuwa yashalipwa kabla ya tatizo hili kutokea kwa mujibu wa Mkataba. Sambamba na hayo, Uongozi wa Mfuko utaichukua ya kuipa adhabu Kampuni hiyo kwa mujibu wa Mkataba.

Pamoja na hayo, kwa sasa utekelezaji wa mradi huo umeshakamilika na upo katika hatua za kuthibishwa na watendaji kabla ya kukabidhiwa rasmi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba mfumo huu upo tangu mwaka 2012 na unakua unafanyiwa marekebisho “upgrades” kila inapohitajika. Kila ikitokea kufanyiwa marekebisho mfumo huo, utaratibu ni kwamba kunatakiwa kuwepo kwa “change management document” ambayo inaelezea kuwepo kwa haja ya kufanyiwa marekebisho mfumo huo ambayo nyaraka hiyo inathibitishwa na Kamati ya Uongozi ya TEHAMA “IT Steering Committee”.

Kamati imetaka kupatiwa nyaraka ya “change manegement document” lakini mpaka inamaliza kikao chake haikufanikiwa kuipata nyaraka hiyo.

Aidha, Kamati imebaini mfumo huo bado haujaanza kufanya kazi, jambo ambalo linapelekea kuchelewa kutolewa kwa huduma bora iliyokusudiwa.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaielekeza Mfumo wa Hifadhi ya Jamii kuhakikisha inatafuta njia sahihi za kuweza kukamilisha uboreshaji wa mfumo huo ili lengo la kutoa huduma iliyobora inafanikiwa ndani ya muda uliokusudiwa.

Hoja Nambari 4.1.11.2: Mapitio ya mfumo wa kugundua, kutoa ishara na kuzima moto (Fire Detection and Suppression System)

Mfumo wa kugundua na kuzima Moto (Fire Detection and Suppression System - FDSS), ni mfumo wa kisasa ambao umejumuisha vifaa na miundombinu mbali mbali yenye uwezo wa kubaini chanzo cha moto (fire detection), kutoa ishara ya hatari ya moto (fire alarm) na vile vile kuweza kuzima moto wakati unapotokea kwenye majengo mbali mbali (fire extenguisher).

Faida kuu ya Mfumo huu ni kuweza kubaini mapema, kutoa ishara kwa binadamu na kuweza kuuzima moto wenyewe (automatic) bila ya kuingiliwa na binaadamu wakati janga la moto linapotokea katika jengo au eneo la Afisi, ambapo pia husaidia kwa kiasi kikubwa kuzima moto maeneo ambayo binaadamu hatoweza kuyafi kia mapema wakati wa dharura ya moto.

ZSSF imefanikiwa kuweka teknolojia na miundombinu ya mfumo wa kugundua, kutoa ishara na kuzima moto (FDSS) katika Ofisi zake mbali mbali ikiwemo chumba cha Seva na Mitambo ya Mawasiliano (Datacenter) kilichopo katika Makao Makuu Kilimani Unguja, Vile vile miundombinu hiyo imefungwa katika Afi si ya Pemba pamoja na Hoteli ya Mkoani Pemba.

Hata hivyo, katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba pamoja na ZSSF kuweka vifaa na miundombinu ya kisasa ya kuzima moto lakini kumekuwa na uhaba kwa miundombinu hiyo kufanyiwa huduma za matengenezo na maboresho kwa wakati “services and maintanance”. Hadi ukaguzi unakamilika baadhi ya miundombinu hiyo ilikuwa bado haijafanyiwa maboresho kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja.

Kushindwa kufanya huduma za matengenezo na maboresho kwa wakati kwenye mifumo ya kuzimia moto kunaweza kusababisha mifumo hiyo kutoweza kufanya kazi ipaswavyo kama ilivyotarajiwa pindipo janga au dharura ya moto ikitokea katika majengo ya ZSSF, jambo ambalo litapelekea kujitokeza kwa uharibifu mkubwa wa vifaa, mali na taarifa za afisi na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZSSF kuhakikisha unaandaa na kutekeleza vizuri mkakati wa kusimamia mfumo na miundombinu ya uzimaji wa moto katika majengo yake na vile vile kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika vifaa hivyo kwa lengo la kuhakikisha vinafanya kazi ipasavyo pamoja na kuvifanyia huduma za maboresho na matengenezo “services and maintanance” kwa wakati ili kuweza kudumisha utendaji kazi wa vifaa hivyo.

Majibu ya Uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii

Kabla ya ukaguzi kufanyika, Uongozi ulikuwa umeshagundua kuwa vifaa vya kuzimia moto vilivyotajwa si tu muda wake wa kufanyiwa maboresho umepitwa muda bali vifaa hivyo vilikuwa vimeshapitwa na muda kutokana na kasi ya ukuaji wa teknolojia. Wakati wa ukaguzi, Mfuko ulikuwa umeshatanganaza tenda ya kumpata Mzabuni wa kuleta vifaa vya kisasa kupitia Zabuni namba SMZ/F0308/G/ICB/LOT1-2/2022-2023/04 Kwasasa Mfuko umeshampata na kuingia Mkataba na Mzabuni Emerging Communications na vifaa vinaendelea kufungwa kwa mujibu wa Mkataba na zoezi la uboreshaji huo linategemewa kukamilika mwezi January 2025.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imeridhika na majibu ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ambapo Kamati imejiridhisha kuwepo kwa hatua ya zabuni ambayo itaenda kufunga vifaa vipya vinavyoendana na wakati. Kamati inaiachia hoja hii kwa ufuatiliaji ili kujihakikishia kwa tarehe za mbeleni kwamba hoja hii ilifanyiwa kazi kikamilifu.

Hoja Nambari 4.1.11.3: Dosari katika Mchakato wa Usimamizi wa Matukio (Inadequate Incident Management Process)

ZSSF ni moja kati ya Taasisi zilizofanikiwa kwa kiasi kikubwa katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutumia mifumo na miundombinu mbali mbali ya TEHAMA kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zake za Mfuko. Ukaguzi ulifanya ufuatiliaji kwa ofisi zake zote kuhusiana na njia zinazotumika katika kuripoti na kusimamia matukio na changamoto za kwenye mifumo kuanzia hatua zinapojitokeza, hatua ya ufuatiliaji hadi hatua ya kupatiwa ufumbuzi na kubaini uwepo wa udhaifu katika mchakato mzima wa usimamizi wa matukio na utatuzi wa changamoto za mifumo.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba ZSSF kwa kiasi kikubwa bado inaendelea kutumia utaratibu wa njia ya kawaida (manual) kupitia uandishi wa madokezo, simu na mahojiano ya moja kwa moja katika kukusanya changamoto za mifumo kutoka kwa watumiaji na kuwasilishwa Idara ya TEHAMA kwa ajili ya ufumbuzi ambapo changamoto hizo hutakiwa kuekewa kumbukumbu na kupangiwa vipao mbele vya kufanyiwa kazi kwa mujibu wa uhalisia wake, umuhimu wake, madhara yake, tarehe na muda ulioripotiwa na Idara ya Mtumiaji. Ni maoni ya mkaguzi kuwa utaratibu wa utendaji kazi wa uongozi unahitaji kuimarishwa kwani siku hizi kuna njia za kiotomatiki za kudhibiti Mchakato ambao huleta majibu ya haraka kwa changamoto, dosari na hatari mbalimbali zinazoweza kujitokeza na kuripotiwa na wafanyakazi. Aidha, imebainika kutokuwepo kwa mkataba wa utoaji wa huduma (SLA) baina ya Idara ya TEHAMA na Vitengo vengine vya watumiaji wa mifumo katika Mfuko (Business Units) jambo ambalo linaweza kupelekea kutokuwepo kwa maelewano mazuri katika utoaji na upatikanaji wa huduma za kibiashara. Kuendelea kutumia njia ya kawaida (manual system) kunaweza kusababisha Mfuko kupungua ufanisi wake katika utendaji kutokana na mifumo iliyopo kushindwa kufanyiwa marekebisho kwa wakati juu ya changamoto, dosari na Vihatarishi mbali mbali vinavyoweza kujitokeza na kuripotiwa na wafanyakazi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZSSF kuanzisha utaratibu wa kutumia mfumo wa TEHAMA (Helpdesk System) ikiwa kama dawati kuu kwa ajili ya kupokea, kukusanya, kusimamia na kuwasilisha matukio na changamoto

na Vihatarishi vyote vinavyojitokeza kwenye mifumo ili kuwezesha watumiaji wa mifumo (system users) katika tawi lolote la ZSSF kuripoti moja kwa moja kwenye Idara ya TEHAMA kwa lengo la kufanyiwa kazi haraka iwezekanavyo na kubakia kumbukumbu zote za taarifa zake. Zaidi ya hayo, makubaliano ya kiwango cha huduma (SLA) kati ya Idara ya TEHAMA na vitengo vya Biashara yanapaswa kutekelezwa ili kudumisha uwajibikaji na utatuzi wa matukio kwa wakati. Vile vile uongozi wa Mfuko kwa kushirikiana na Idara ya TEHAMA unashauriwa kuandaa mkakati maalum wa kupitia, kuchambua, kufanyia tathmini na kuzitatua hatari zote zilizopo katika mifumo na miundombinu ya TEHAMA ya Mfuko kwa kuzingatia umuhimu na aina ya hatari zilizobainika.

Majibu ya Uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii

Kwa sasa utaratibu wa Mfuko linapowasilishwa tatizo au suala linalohitaji utatuzi wa changamoto za mifumo hutatuliwa na watendaji wa Divisheni ya TEHAMA. Hadi sasa Uongozi wa Mfuko haujapokea malalamiko ya ucheleweshwaji wa utatuzi wa changamoto zinazowasilishwa kwa utatuzi kutokana na Mfumo uliopo sasa. Hata hivyo, Uongozi wa Mfuko unaendelea kusimamia na kufuatilia utendaji kazi wa mfumo wa utatuzi changamoto za mifumo uliopo sasa, pale ambapo ikibainika unaleta changamoto za utatuzi wa changamoto za mifumo ikiwa utahitaji kuboresha zaidi ikiwemo kuwa na mfumo maalumu wa TEHAMA wa utatuzi wa changamoto hizo yatafanyika maboresho kulingana na mahitaji.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii umekiri kwamba ni kweli mpaka sasa wanaendelea kutumia mfumo ya “manual” katika kusajili na kufuatilia matukio. Aidha ZSSF imekiri kwamba makubaliano ya kiwango cha huduma “SLA” baina ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na watumiaji mfumo katika Mfuko “business Unites” bado mkataba huo haupo jambo ambalo linaweza kupelekea kutoelewana katika maeneo kadhaa baina ya ZSSF na business units hizo.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaielekeza Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kuhakikisha inakamilisha mipango yake ya kua na “help desk” ambayo changamoto zote zitakazo ripotiwa zinakua zinasajiliwa “automatic” na mfumo ambapo mfumo wenyewe utakua na uwezo wa kujisomea njia bora za utatuzi kwa baadae na kuweza kutoka mapendekezo ya utatuzi kwa aina ya changamoto ambazo zimesajiliwa sana.

Halkadhalika, Kamati inaielekeza Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kuhakikisha inaandaa mkataba wa kiwango cha huduma (SLA) ili kuepusha changamoto ambazo zinaweza kutokea kwa kukosekana kwa mkataba huo.

Hoja Nambari 4.1.11.4: Udhaifu katika utendaji kazi wa Mifumo ya ZSSF kwa upande wa Pemba

Ukaguzi ulifanya uhakiki wa utendaji kazi wa mifumo ya ZSSF kwa upande wa Pemba na kubaini kuwa kasi ya utendaji kazi wa mifumo kwa Pemba ni ndogo (slow speed). Hali hii imesababishwa na kuwepo kwa udhaifu katika miundombinu iliyotumika kuunganisha mawasiliano ya mtandao (VPN Connection) kutoka kwa kampuni ya Zanlink. Aidha imebainika kunapokuwa na changamoto ya hali ya hewa kwa mfano uwepo wa mvua kubwa hupelekea mifumo kushindwa kupatikana na kutumika kwa ufanisi. Kuwepo kwa udhaifu katika miundombinu ya mawasiliano ya mtandao kunaweza kusababisha kupungua kwa ufanisi wa utendaji kazi wa Mfuko kwa upande wa Pemba na hatimae kupelekea kujitokeza kwa malalamiko kwa watumishi wa ZSSF kwa upande wa Pemba na wanachama kutokana na huduma duni zinazoweza kutolewa na Mfuko kwa upande wa Pemba zilizosababishwa na changamoto ya mawasiliano ya mtandao. Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZSSF kuweka na kutumia njia mbadala ya miundombinu ya Mkonga wa Taifa kutoka ZICTIA (Fiber Connectivity and Infrastructure) kwa upande wa Pemba kama ilivyoungwa katika Ofi si za Zanzibar kwa lengo la kuendelea kupatikana huduma bora na ya uhakika, yenye kasi kubwa (higher speed) na iliyo salama (secure) dhidi ya mashambulizi na vihatarishi vinavyotokana na mitandao (cyber-attacks).

Majibu ya Uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii

Kabla ya ukaguzi na mpaka sasa, Ofisi za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) zote Unguja na Pemba zinatumia mitandao ya ZICTIA na Zanlink. ZICTIA ni Mtoa Huduma za Mtandao Mkuu kwa ZSSF na Kampuni ya Zanlink ni Mtoa Huduma za Mtandao mbadala wakati ambao Mtandao wa ZICTIA utakuwa na changamoto zozote ili kuhakikisha kuwa huduma za Mfuko zinapatikana wakati wote kwa wanachama wake.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imeridhika na majibu ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na kujithibitishia kwamba ni kweli ofisi za ZSSF Unguja na Pemba zimeunganishwa na mitandao ya ZICTIA na Zanlink ambapo mtandao wa ZICTIA ndio unaotumika kutoa huduma na mtandao wa Zanlink unatumika endapo itatokea hitlafu kwa mtandao wa ZICTIA.

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR (ZURA)

Hoja Nambari 4.1.14.1: Kukosekana kwa Mpango wa Matengenezo wa kuzuia uharibifu (Preventive Maintenance Plan)

Katika ukaguzi uliofanyika ZURA Unguja na Pemba ilibainika kwamba ZURA haina mpango wa matengenezo wa kuzuia uharibifu wa vifaa na vitendea kazi mbali mbali ikiwemo mifumo na miundombinu ya TEHAMA.

Mpango huu huainisha ratiba ya matengenezo ya vifaa/ vitendea kazi husika kulingana na vigezo mbali mbali ambavyo taasisi husika itaviona vinafaa kwa makundi tofauti kama vile hali ya vifaa, umri wa vifaa, kiwango cha matumizi ya vifaa, unyeti wa vifaa, gharama na umuhimu wa vifaa husika n.k.

Lengo la mpango wa matengenezo ni kuhakikisha kwamba vifaa vyote vya Taasisi ambavyo vinagharimu fedha nyingi kuvinunua vinatumika katika namna endelevu kwa muda uliopangwa na kuepusha hasara kwa Serikali kupitia ununuzi wa vifaa vyengine kama hivyo kwa sababu ya ubovu wa vifaa vilivyopo uliosababishwa na kukosa matengenezo ya kuzuia uharibifu mara kwa mara kulingana na mpango husika.

Kukosekana kwa mpango huo kumepelekea ZURA kuwa na vifaa mbali mbali vilivyoharibika na kushindwa kutengenezwa kwa Unguja na Pemba ambapo vifaa hivyo vimejumuisha Printers, Kompyuta, UPS, Kamera za Ulinzi za CCTV, mtandao (Network), routers, vipoza joto (ACs) n.k, ambavyo vimeharibika na kukosekana kwa utaratibu na ratiba rasmi wa matengenezo yake na kukosekana kwa tija na kupunguza ufanisi wa Shirika katika utekelezaji wa majukumu yake.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kuandaa mpango wa matengenezo ya kuzuia uharibifu na kuhakikisha unafuatwa kwa kutenga rasilimali fedha na muda kwa ajili ya utekelezaji mipango husika kwa wakati.

Aidha, kwa upande wa vifaa ambavyo tayari vimekwisha haribika tunashauri vifanyiwe tathmini ya ubovu ili kubaini kama vinaweza kutengenezwa au vinahitaji kubadilishwa na kuchukua hatua stahiki mara moja ili kurejesha hali ya utendaji wa Taasisi na kuongeza tija na ufanisi.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)

Hoja imepokelewa, Mamlaka tayari imeshaanda ratiba ya matengenezo ya vifaa vya TEHAMA (Preventive Maintenance Plan) kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na utekelezaji wake umeshanza kufanyakazi katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2024/2025.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba kitengo cha TEHAMA cha ZURA kwa kipindi cha ukaguzi wa CAG hawakua na uwezo wa kitaalamu na nguvu kazi kuweza kuifanya kazi hiyo. Lakini kwa sasa ZURA imekiri inao wataalamu wa kutosha ambao wanaweza kuifanya kazi hiyo.

Aidha, kamati ilihitaji kuiona tathmini ya ubovu wa vifaa ambapo mpaka Kamati inamaliza kikao chake Tathmini hiyo haikuweza kupatikana.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaiagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar kuhakikisha inaandaa mpango Tathmini ya ubovu wa vifaa ili kujua vifaa ambavyo havifai tena kwa ajili ya matumizi na kuanza kuandaa Mpango wa matengenezo ili kuweza kuzuia uharibifu wa vifaa ambavyo Serikali inatumia fedha nyingi kuvinunua.

Hoja Nambari 4.1.14.2: Kukosekana kwa Mpango wa Kusimamia Matukio ya TEHAMA (ICT Incident Management Plan)

Mpango wa usimamizi wa matukio (Incident Management Plan) ni utaratibu maalumu wa utambuzi, usajili, uhakiki, ufuatiliaji na utatuzi wa matukio mbali mbali ya TEHAMA katika Miundombinu na Vifaa vya TEHAMA pamoja na Programu Tumizi ambayo yanaweza kuathiri utendaji wa Taasisi kupitia TEHAMA na kuondoa Usiri, Uadilifu na Upatikanaji wa Taarifa mbali mbali za Serikali kwa wakati.

Ukaguzi umebaini kwamba ZURA haina Mpango rasmi wa kusimamia matukio ya TEHAMA katika kutambua, kusajili, kuhakiki, kufuatilia, kutatua na kutunza kumbu kumbu za matukio mbali mbali ya TEHAMA, tofauti na matakwa ya Kifungu nambari 9.2.2 cha ZURA ICT Guideline pamoja na matakwa ya miongozo ya viwango bora kubalifu vya TEHAMA kama vile **ISO/IEC 27001 Clause 10.2**. Hali hii inaweza kusababisha ucheleweshwaji wa kubaini na kutatua changamoto za TEHAMA.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati kusimamia uandaaji wa mpango wa kusimamia matukio ya TEHAMA kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa na kimataifa (best practice) na kuhakikisha kwamba mpango huo unatumika katika usimamizi wa matumizi ya Miundombinu, vifaa na Programu zote za TEHAMA katika taasisi.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)

Hoja imepokelewa, Mamlaka tayari imeshaandaa rasimu ya mpango wa usimamizi wa matukio ya TEHAMA (ICT Incident Management Plan) ambayo

inasimamia utaratibu mzima wa usajili na utekelezaji wa matukio ya TEHAMA. Hata hivyo Mamlaka kupitia Kitengo cha TEHAMA imetengeneza mfumo wa kidigitali wenye uwezo wa kusajili matukio ya TEHAMA na utekelezaji wake ambapo kwa sasa mfumo huo upo katika hatua ya majaribio (Testing).

Pamoja na maelezo haya nambatanisha rasimu ya mpango wa usimamizi wa matukio ya TEHAMA (ICT Incident Management Plan).

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba mpango wa usimamizi wa matukio ya TEHAMA (ICT Incident Management Plan) kwa sasa upo, aidha Uongozi wa Taasisi umekiri kwamba kwa kipindi ambacho wakaguzi wanapita mpango huo haukuwepo.

Hali hiyo ilitokana na kwamba ZURA kupitia Kitengo chake cha TEHAMA hakikikua na uwezo wa kutosha kuweza kuandaa Mpango huo pamoja na mipango mengine ambayo ilihitajika.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaielekeza Mamlaka kwamba kuwepo kwa mpango huo peke yake haitajitosheleza bali kuwepo na vitendea kazi “tools” ambavyo vitawezesha kwa mpango huo kufanya kazi vizuri kwa kuweka kumbukumbu za changamoto zote ambazo zitajitokeza za TEHAMA na kuweza kutoa ripoti.

Hoja Nambari 4.1.14.3: Utekelezaji wa Mradi wa kutengeneza mfumo wa ZIRS nje ya muda wa mkataba

Kwa mujibu wa Mkataba nambari ISPG/DRMNRG/ZNZ/AFDB/QCBS/10/2019 uliongiwa baina ya mtoa huduma na Afisi ya Rais Fedha na Mipango kwa niaba ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA), Mkataba huo ulisainiwa tarehe 29/05/2020 na ambapo ulitakiwa kuanza kutekelezwa ndani ya siku 15 ambayo ni sawa na tarehe 13/06/2020 na kwamba ulitakiwa kukamilika ndani ya miezi 6 kuanzia tarehe 13/06/2020 sawa na tarehe 12/12/2020.

Ukaguzi umebaini kwamba sehemu kubwa ya mradi huu ilitekelezwa nje ya muda wa mkataba, yaani mradi huu ulitekelezwa pasipokuwa na mkataba hai kuanzia tarehe 13/12/2020 mpaka tarehe 30/12/2022 mradi ulipokamilika, sawa na ucheleweshaji wa mradi kwa zaidi ya miaka 2 na siku 18.

Aidha, hadi ukaguzi unakamilika haukupatiwa “addendum” ya kuongeza muda wa mkataba ili kuhalalisha kazi za mradi kuendelea kufanyika na Serikali kuwa na nguvu za kisheria za kuidhinisha malipo ya Mtoa huduma,

hali hii inaweza kupelekea athari mbali mbali kwa Serikali/ Umma na mtoa huduma ikiwemo ukiukwaji wa Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 pamoja na kanuni zake kwa kuidhinisha malipo kwa mtoa huduma pasipokuwa na mkataba hai. Vile vile kunaweza kupelekea kuchelewesha manufaa ya mradi husika kwa ZURA hali iliyoikosesha ZURA fursa ya kupata tija na kuongeza ufanisi kwa kipindi chote ambacho mradi ulichelewa jambo ambalo linaweza kuongeza gharama za utekelezaji wa mradi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kwa kushirikiana na uongozi wa Afisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha kwamba unazingatia matakwa ya Sheria za Nchi katika Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma bila kujali chanzo cha fedha zinazotumika kutekeleza kazi/ mradi husika kwakuwa Sheria za Nchi hazibagui aina ya chanzo cha fedha.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)

Hoja imeopokelewa, Mamlaka itazingatia ushauri uliotolewa na Mkaguzi. Aidha, Mradi wa ZIRS umezaminiwa na “African Development Bank (AfDB Bank)” ulioratibiwa na Afisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar kwa niaba ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA), wakati mradi unaanza ZURA haikuwa na nyenzo za kutosha zitakazo msaidia mtoa hudumu kutengeneza mfumo wa ZIRS kwa kuzingatia kanuni na sheria za Mamlaka, ikiwemo miongozo na kununi za maji, umeme na gesi, na kutokana na ZURA inaendeshwa na kanuni na Sheria Zanzibar, ilipaswa kwamba mfumo wa ZIRS utengenezwe kwa kuzingatia kanuni, miongozo na sheria ya Mamlaka. Hivyo, Mamlaka haikuwa na chaguo zaidi ya kupokea fursa hiyo na kuanza zowezi la kuanda kanuni pamoja na miongozo mbali mbali ya Mamlaka kwa kushirikiana na Ofisi tofauti ikiwemo EWURA, BRELA, ZAWA na ZECO.

Zoezi hili limechukuwa muda mrefu mpaka kupatikana kwa nyaraka hizo, na kutokana na muda ushaenda kulingana na mkataba, Mamlaka imeona kuna ulazima wa kusogeza mbele kipengele cha “System Development” katika hatua ya uzamini “Warranty and After Sales Service” ambayo mtoa huduma alipaswa kuendelea kutoa huduma “Support” kwa muda wa miaka miwili baada ya mkataba kumaliza kama ilivyoainishwa katika Mkataba uliosainiwa **May, 2020** wenye nambari **ISPG/ZNZ/AfDB/QCBS/10/2019** katika ukurasa 43, kipengele namba 5 cha “Approach and Methodology” kinachosema kwamba “*Provide after sales services support for a period of 24 months including 6 months of liability period*”, na baada ya muda huo kumaliza ndipo mtoa huduma atapokea malipo ya asilimia 5% kwa kuzingatia mkataba.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba “concept note” pamoja na nyaraka nyengine ikiwemo mkataba zimefanywa na Afisi ya Rais, Fedha na Mipango. Aidha, Kamati imebaini kwamba ZURA walikua na jukumu la kufuatilia na kuhakikisha taratibu zote zinafuatwa kama Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 pamoja na kanuni zake inavyoeleza.

Kamati haijaridhika na uhalisia kwamba ZURA hawakuweza kusimamia Sheria ambapo walitakiwa kabla ya kuendelea na utengenezaji wa mfumo wa ZIRS kuhakikisha taratibu zote zimefuatwa ikiwa ni pamoja na kupatikana kwa mkataba wa ziada “addendum” ambayo kimsingi ndio ZURA walitakiwa kufanya ukizingatia mkataba wa awali ulikua tayari umeshakwisha muda wake.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inaielekeza ZURA kuhakikisha kwa miradi ijayo inafuata Sheria na taratibu zilizowekwa ili kupatikane kwa miradi yenye tija na kwa muda uliokusudiwa, ikiwemo kuandaa mkataba wa ziada “addendum” endapo mkataba wa awali utaisha muda wake bila ya mradi kukamilika.

Hoja Nambari 4.1.14.4: Kutokamilika kwa Utengenezwaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Malalamiko (CMS)

“Software Development Life Cycle – SDLC” ni mchakato wa kina unaotumika katika utengenezaji wa Programu za TEHAMA ambapo utaratibu huu wakitaalamu unajumuisha hatua tofauti tofauti ambazo hufuatwa kipindi cha uanzishwaji mpaka kumalizika kwa Mfumo husika. Hatua hizo zikijumuisha: -

- Uchambuzi na Mahitaji ya Mfumo (Requirements Analysis).
- Ubunifu wa Mfumo (System Design).
- Matengenezo ya Mfumo (System Development).
- Upimaji (Testing).
- Uwasilishaji wa Mfumo (System Deployment).
- Uendeshaji na Matengenezo (Operation and Maintenance).

Lengo kuu la SDLC ni kuzalisha programu inayokidhi matarajio ya wateja, kusaidia kuzalisha programu kwa wakati uliokusudiwa pamoja na kusaidia kupatikana kwa programu ndani ya bajeti iliopangwa.

Aidha, ukaguzi umebaini kutokufuatwa kwa utaratibu wa utengenezaji wa mifumo ya TEHAMA (SDLC) katika utengenezaji wa Mfumo wa Malalamiko wa Mamlaka ya udhibiti wa huduma za Maji na Nishati (ZURA).

Hali hii inakwenda kinyume na matakwa ya viwango bora kubalifu (Best practice) **ISO/IEC 12207:2017 Clauses 7-24** pamoja na kifungu nambari **7.0** cha ZURA ICT guideline, kinachozungumzia utaratibu uliobora katika hatua za utengenezaji wa Mifumo ya TEHAMA katika Taasisi au Mashirika, ili kuhakikisha utekelezaji uliobora na wa uhakika wa utengenezaji wa Mifumo ya TEHAMA.

Kutokana na kutokuzingatiwa kwa taratibu za utengenezaji wa mifumo ya TEHAMA (SDLC) katika matengenezo ya Mfumo wa Malalamiko (Complaint Management System), kumesababisha kutokukamika kwa hatua za matengenezo ya Mfumo husika kwa kipindi kirefu ambapo matengenezo ya awali yalianza mnamo mwaka 2020.

Baadhi ya vipengele muhimu ambavyo bado havijakamilika katika utekelezaji wa Mfumo wa “Complaint Management System” inajumuisha moduli zifuatazo;

- Uwezo wa Mlalamikaji kutuma ombi lake mwenyewe kupitia Mtandao.
- Uwezo wa Mhandisi wa ZURA kuona na kuweka “Update” juu ya lalamiko Fulani.
- Uwezo wa Mfumo kutuma SMS za kawaida kwa walalamikaji kuonyesha kupokelewa kwa malalamiko yao.
- Uwezo wa Mfumo kumuwezesha Mlalamikaji kuingiza taarifa ya muendelezo wa lalamiko lake.
- Uwezo wa Mfumo kutoa ripoti za utekelezaji wa utatuzi wa malalamiko ya Wananchi.

Hali hii inaonesha udhaifu kwa Kitengo cha TEHAMA cha ZURA kutokana na kutofanya upembuzi yakinifu wa mahitaji ya watumiaji wa mifumo (user requirements) kabla ya kuanza kutengeneza mfumo huo jambo ambalo limepelekea kuchelewa kukamilika kwa Mfumo husika.

Aidha, Kutokukamilika kwa mfumo katika wakati muafaka kunaweza kupelekea kujitokeza kwa ongezeko la gharama za ziada zisizotarajiwa na hatimae kutofikia malengo na kutopatikana tija iliyokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kufuata njia za Kitaalamu katika matengenezo ya Mifumo ya TEHAMA ili kuendana sambamba na matakwa ya miongozo bora kubalifu ya Kitaifa na Kimataifa.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)

Hoja imepokelewa, Mamlaka itazingatia taratibu za utengenezaji wa mifumo ya TEHAMA (SDLC), aidha Mamlaka kupitia Kitengo cha TEHAMA imefanya maboresho ya mfumo kwa kuwawezesha kitengo cha uhusiano kusajili malalamiko wanayopokea kwa wateja na kuyapeleka Idara/kitengo husika kwa mujibu wa uhalisia wa lalamiko kupitia mfumo. Hata hivyo, Mamlaka

kupitia Kitengo cha TEHAMA kinaendelea kufanya maboresho ya mfumo huo kwa kuwawezesha walalamikaji kusajili malalamiko yao wenyewe, pamoja na kuunganisha "Integration" mfumo wa SMS ili waweze kupokea maendeleo ya malalamiko yao. Maboresho hayo yamepangwa kufanyika ndani ya robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2024/2025 kuanzia tarehe 1/1/2025 hadi 31/03/2025, sambamba na kumaliza maboresho hayo kitengo cha TEHAMA kitaendelea kuwajengea uwezo wadau wa ndani na wa nje.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba katika changamoto ambazo zimeainishwa na Mkaguzi kutoka CAG bado ZURA hawajatekeleza na kutatua changamoto izo na wanaendelea kuwa katika mchakato wa kutekeleza kadhia hizo.

Kamati imebaini chimbuko la hoja hii ni uwezo mdogo wa Kitengo cha TEHAMA cha ZURA ambacho kimsingi mpaka Kamati inamaliza uchunguzi wake Kitengo hicho kilikua na watendaji watatu (3), ambapo wawili (2) ni wa Mifumo na mmoja (1) ni wa hardware.

Kamati imeibakisha hoja kutokana na kutokamilika kwa mambo ambayo yamebainika katika ukaguzi.

Hoja Nambari 4.1.14.5: Kukosekana kwa nyaraka muhimu za Utengenzwaji wa Mifumo ya ndani ya TEHAMA

Katika kufanya Mapitio ya Mifumo ya TEHAMA iliotengenezwa na Mamlaka ya Udhibiti ya Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Ukaguzi umebaini kukosekana kwa nyaraka muhimu za utengenezwaji wa mifumo hiyo, ambapo mpaka kumalizika kwa ukaguzi ZURA ilishindwa kutupatia nakala za nyaraka mbali mbali zilizotumika katika michakato ya utengenezaji wa mifumo tajwa hapo chini:-

1. Mfumo wa usimamizi wa Malalamiko (Complaint Management System (CMS))
2. Mfumo wa usimamizi wa Rasilimali Watu (Human Resource - Instify Management System (HRMIS)

Miongoni mwa nyaraka zilizohitajika kwa ajili ya ukaguzi ambazo hazikupatikana ni pamoja na nyaraka zifuatozo: -

1. Approved User Requirements Documents
2. Approved Project Plan or Project Schedule
3. Approved Project Cost Management Plan.
4. Approved User Acceptance Testing (UAT) reports.
5. Approved System Configuration Documents.
6. Approved System Operations Manual/ document.
7. System training Reports for different user groups.

8. User matrix documents.
9. Approved System sustainability plan.

Kukosekana kwa Nyaraka muhimu za utengenezaji wa Mifumo ya TEHAMA kunaenda kinyume na matakwa ya kifungu nambari **2.5** cha Muongozo wa viwango vya mahitaji ya uanzishwaji wa programu za TEHAMA kutoka Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ), pamoja na viwango bora kubalifu (Best Practice) **ISO/IEC/IEEE 15289:2011.** Ambayo imeweka umuhimu wa utengenezaji wa nyaraka mbali mbali katika hatua tofauti za utengenezaji wa programu za TEHAMA.

Utaratibu wa kutengeneza Mifumo ya TEHAMA pasipo kuzingatia uwepo wa nyaraka muhimu kunachangia katika kupatikana kwa Mifumo isiyokuwa na tija katika taasisi, kupatikana kwa Mifumo iliyokosa ufanisi katika utendaji kazi pamoja na kupatikana kwa Mifumo inayochukua mda mrefu kukamilika ambapo kwa ujumla hali hii inachangia katika kudumaza maendeleo ya TEHAMA katika Taasisi za Umma pamoja na kuongezea Serikali mzigo na hasara ya kudhamini mifumo isiokua rasmi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kuhakikisha unafuata njia za kitaalamu katika kutengeneza mifumo ya TEHAMA ya ndani, kama inavyoelekezwa kupitia miongozo mbali mbali ya kitaifa na kimataifa.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)

Hoja imepokelewa, Mamlaka itazingatia miongozo ya kutengeneza mifumo ya TEHAMA. Hata hivyo Mamlaka tayari imeshaandaa nyaraka zote muhimu zilizoorozeshwa katika hoja hii. Aidha Mamlaka imeanza kutumia mfumo wa ERMS ambao unasimamiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGAZ) unaojumuisha majukumu ya HRIMS (System Fuctionality) na taarifa zote za HRIMS kuhamishwa katika mfumo wa ERMS.

Pamoja na maelezo haya, nambatanisha nyaraka zinazohusu mfumo wa CMS.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamti imeridhika na majibu kuhusu mfumo wa HRIMS. Aidha, Kamati ilipokea nyaraka za mfumo wa CMS ambazo ZURA wamewasilisha kwa Kamati na kubaini kwamba nyaraka hizo hazikufuata “templates” ambayo imetolewa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGaz), ambayo kimsingi ndio “template” ambazo taasisi zote za Serikali zinatakiwa kufuata katika kuandaa nyaraka mbali mbali.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaiagiza ZURA kuhakikisha inafuata Miongozo ambayo imewekwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao ili kuhakikisha Mifumo ambayo

inatengenezwa imezingatia viwango vya kitaifa, kikanda na kimataifa na hatimae kupatikana kwa tija iliyokusudiwa.

Hoja Nambari 4.1.14.6: Mapungufu yaliyobainika katika Mradi wa Ufungaji wa chumba cha kuhifadhia Mitambo (Mini Data Center) ZURA

Mradi wa Usambazaji na Ufungaji wa vifaa kwa ajili ya chumba kidogo cha kuhifadhia mitambo (Mini Data Center) ulitekelezwa kupitia Mkataba nambari **SMZ/FO118/W/NCB/2021/22/20,** baina ya Mamlaka ya Udhibiti wa huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) na Kampuni ya Neymon Investiment LTD, ambapo mradi huo uligharimu kiasi cha shilingi 177,000,000.

Mradi huo ulianza mnamo tarehe 1 Oktoba, 2022 na kumalizika tarehe 30 Novemba, 2022 ambapo ulijumuisha usambazaji wa vifaa na ufungaji wa mifumo ifuatayo:-

1. Ufungaji wa sakafu ya chuma ilioinuliwa (Steel Raised Floor Tiles).
2. Ufungaji wa Mfumo wa kufuatilia hali ya kimazingira ya chumba cha kuhifadhia Mitambo (Monitoring System).
3. Ufungaji wa Mfumo wa hali ya hewa (Air conditional System).
4. Ufungaji wa Mfumo wa Umeme na Mfumo wa umeme wa hakiba (Main Power System and Redundant Power Supply).
5. Ufungaji wa Mfumo wa Ulinzi kwa kutumia Kamera (Surveillance System).
6. Ufungaji wa Mfumo wa kudhibiti uingiaji wa chumba cha kuhifadhia Mitambo (Door Access Control).
7. Uwekaji wa Mazingira Bora ya mpangilio wa waya za mawasiliano katika chumba cha mitambo (Cable Management).
8. Utayarishaji wa Nyaraka za Matumizi kwa ajili ya chumba cha Kuhifazia Mitambo (Documentation and Control).

Katika utekelezaji wa Mradi huu ukaguzi umebaini mapungufu mbali mbali yanayoendana kinyume na matakwa ya Mkataba wa Mahitaji na Ufafanuzi wa kiufundi (Requrement and Technical Specification) kama ifuatavyo:-

1. Kutofanya Kazi kwa Mfumo wa Ufatiliaji wa hali ya kimazingira ya Chumba cha Seva

Kwa kuzingatia matakwa ya Mkataba uliosainiwa baina ya ZURA na Mtoa Huduma katika kipengele nambari 7 cha Waraka wa Vipimo vya Mahitaji na Ufafanuzi wa kiufundi (Requirement and Technical Specification) kinachozungumzia uwekaji wa mfumo wa ufatiliaji ambao utakua na uwezo wa kufatilia hali halisi katika chumba cha Mitambo ikiwemo kufatilia hali ya joto, mzunguko wa hewa, uwezo wa kugundua uvujaji wa maji, ufuatiliaji wa usalama, ufuatiliaji wa hali ya nishati na umeme, uwezo wa kugundua uwepo wa moshi nakadhalika.

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa kufuatilia hali ya hewa katika “Mini Data Center” haujakamilika kwa mujibu wa mkataba japokuwa mtoa huduma ameshalipwa fedha zote, aidha ukaguzi umebaini kutokufungwa kwa baadhi ya vifaa muhimu ambavyo ni:-

1. “Screen Monitor” ya inchi 55 iliyokusudiwa kuonesha hali halisi ya hewa katika chumba hicho.
2. “Sensors” ambazo kazi yake ni kufuatilia kiwango cha joto, kiwango cha umeme na mzunguko wa hewa na kupeleka taarifa hizo kwenye “Screen Monitor” kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Kutokufanya kazi kwa Mfumo wa ufatiliaji wa hali ya kimazingira katika chumba cha kuhifadhia Mitambo kunaweza kusababisha kuharibika kwa vifaa vilivyomo ndani ya chumba hicho kutokana na kuongezeka kwa joto kali pindipo mfumo huo ukiharibika na kushindwa kutoa ripoti na ukumbusho (notification) kwa wakati.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kufanya uhakiki wa kina kabla ya kupokea miradi ya TEHAMA kutoka kwa wakandarasi katika hatua za kuhakikisha utekelezaji wa Mradi kwa mujibu wa makubaliano. Aidha, ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kufunga Skrini za ufatiliaji wa mfumo kwa lengo la kuondoa athari zitakazoweza kujitokeza kutokana na kukosa tarifa za hali ya chumba cha seva kwa wakati husika

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)

Hoja imepokelewa, Mamlaka imeshafanya mawasailiano na Mkandarasi “**Neymon Investiment Limited**” kwa njia ya barua Nam: “**AB.334/760/05/09” tarehe 14/02/2024** kwa ajili ya kufanya marekebisho ya kamera. Hata hivyo, Maboresho hayo tayari yameshafanyika kwa kuwekwa kamera zenye sifa kulingana na mkataba. Aidha kwa upande wa TV ya nchi 55 ipo tokea mwanzo na imeunganishwa na mfumo wa ufuatiliaji wa kamera “**CCTV Monitoring**” tangu kukamilika kwa ujenzi wa chumba hicho.

Kwa upande wa “Sensors”, chumba cha seva kimefungwa sensa mbili ikiwemo sensa ya kugundua ikiwa kuna unyevu wa maji, na ya pili kufatilia hali ya chumba “Temperature”. Sensa hizi zinatumia mifumo miwili tofauti ni hali ambayo ilishindikanwa kuweka mifumo mitatu ikiwemo ya CCTV katika TV moja, na katika hali kikawaida TV huwa haina uwezo wa “Split Screen” na kuonyesha vitu vitatu kwa wakati mmoja.

Aidha, tayari Mamlaka imeshafunga kamera tatu katika chumba cha seva kwa ajili ya ufuatiliaji wa matokeo na usalama.

Hata hivyo, kitengo cha TEHAMA kinaendelea kutafuta njia bora ya kuweza kufanya “Monitoring” ya mifumo yote mitatu itakayosaidia ufatiliaji wa hali ya kimazingira katika chumba cha seva.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imefanya ufuatiliaji wa hoja hii na kubaini kwamba kamera zote zimebadilishwa na zinafanya kazi vyema. Halkadhalika “sensors” tayari zimeshafungwa, hivyo hoja hii imefanyiwa kazi kikamilifu.

Kwa mnasaba huo, Kamati imeridhika na hoja hii.

Hoja Nambari 4.1.14.7: Dosari katika mfumo wa Ulinzi wa kamera (CCTV camera system)

Mfumo wa Kamera za CCTV unasaidia kuonesha kumbukumbu za matukio yote yanayofanyika katika mazingira ya Afisi kwa lengo kuu la kutunza ushahidi kwa ajili ya hatua nyengine za Mashtaka kwenye vyombo vya kutoa haki ikiwa kumetokezea uhalifu wa aina yoyote.

Kwa kuzingatia Kifungu namba 4.3.4 cha muongozo wa Serikali Mtandao wa mwezi Machi mwaka 2022, Taasisi inatakiwa kuhakikisha uwepo Usanifu wa Usalama wa Taasisi (Institutional Security Architecture) amabo utahakikisha upatikanaji wa usalama wa Taarifa na nyenzo muhimu za TEHAMA.

Kwa kuzingatia hayo Ukaguzi umebaini dosari mbali mbali katika mfumo wa Ulinzi kwa kutumia Kamera katika Ofisi za ZURA upande wa Unguja na Pemba kama zifuatazo;

I. Kutokufanya kazi kwa Asilimia 22.2 za kamera katika Ofisi Kuu ya ZURA Unguja

Katika kufanya mapitio ya mfumo wa Ulinzi kwa kutumia kamera katika Ofisi kuu za ZURA Unguja, ili kuangalia utendaji kazi wa mfumo huo, Ukaguzi umebaini uwepo wa Kamera 12 kati ya 54 sawa na asilimia 22.2 ambazo hazifanyi kazi kwenye jengo la ZURA Unguja. Hivyo kusababisha kukosekana kwa tarifa za ulinzi na ushahidi kwa njia ya kamera katika maeneo hayo kwa kipindi kisichopungua miezi 6.

Hata hivyo ukaguzi ulishindwa kupatiwa ushahidi juu ya hatua zilizochukuliwa katika utengenezaji wa Kamera zilizoharibika. Jambo linaloenda kinyume na kifungu nambari **10.5 cha ZURA ICT GUIDELINE** kinachohitaji uwepo wa utaratibu endelevu wa kufanya matengenezo ya nyenzo za TEHAMA hali hiyo inaweza kusababisha dosari zifuatazo:-

Uhalifu Usiothibitishwa: Bila kamera za ulinzi, ni vigumu kuthibitisha uhalifu na kuchukua hatua dhidi ya wale wanaohusika. Kamera zinasaidia

katika kurekodi matukio ya uhalifu na kuwafanya wahalifu wawe na wakati mgumu kuepuka kukamatwa pamoja na kupinga mashtaka.

Kupotea kwa Mali: Kamera za ulinzi zinasaidia kulinda mali za thamani za Ofisi. Kutokuwepo kwa ulinzi wa kamera kunaweza kutengeneza mwanya wa wizi wa mali za Taasisi na hivyo kusababisha upotevu na hasara kubwa kwa Taasisi na Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kuhakikisha kwamba unayafanyia kazi mapungufu yote yaliyobainika katika hoja hii.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)

Hoja imepokelewa, Aidha tatizo hili limejitokeza kutokana na muingiliano wa Taasisi kutumia chumba cha TEHAMA kimoja (ICT Room) Pamoja na vifaa vyake kama (Switch, PBX, NVR) ambapo chumba hicho kinapokea muunganiko (Connection) ya Kamera ya majengo yote mawili. Hali hii imepelekea vifaa hivyo kuzidiwa na kupoteza uhalisia wake kwa baadhi ya kamera.

Kwa kulizingatia hilo, Mamlaka ipo katika hatua ya kutafuta mtoa huduma wa kufanya maboresho ya miundombinu ya kamera ya jengo la ZURA ikiwemo kutenganishwa vya TEHAMA vilivyokuwepo katika chumba cha TEHAMA (ICT room Basement" ndani ya robo ya pili ya mwaka fedha 2024/2025.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imeridhika na hatua za utekelezaji wa hoja hii ambazo zimechukuliwa na Mamlaka. Kamati imebaini kwamba tayari mamlaka imeshatoa Zabuni na wapo katika hatua za kumpata mtoa huduma "supplier".

Hoja Nambari 4.1.14.8: Kusitishwa kwa Mfumo wa Kuchunguza (Scanning) Mafuta ya kimagendo na Uchakachuaji (Fuel Marking System) ZURA

Ukaguzi umebaini uwepo wa usitishwaji wa Mfumo uliokua ukitumika katika Kupima na kuhakikisha Nishati ya Mafuta inayopatikana kwa Wananchi imefata Sheria na Taratibu zilizoekwa katika Nchi. Mfumo huo ulianza kufanya kazi mnamo tarehe 1 Novemba, 2022. Kwa kuzingatia makubaliano yaliofikiwa katika zabuni yenye kumbukumbu namba **SMZ/FO118/NC/ICB/2019- 20/17** ya Huduma ya upimaji wa mafuta ilitarajiwa kumaliza muda wake mnamo 31 Octoba, 2023.

Aidha ukaguzi ulishindwa kujiridhisha njia madhubuti zilizowekwa na ZURA katika kuhakikisha zinasaidia Serikali katika kuzuia na kupambana

na vitendo vya kimagendo vya Mafuta katika visiwa vya Unguja na Pemba baada ya kusitisha matumizi ya mfumo wa upimaji wa Mafuta (Fuel Marking Sysytem).

Kupungua makusanyo ya Kodi za Serikali: Kutokana na kukosekana kwa njia ya kuthibitisha uhalali wa Mafuta endapo yakifikishwa katika vituo vya kuuzia mafuta (Filling Stations) Hii inaweza kupelekea mafuta hayo kupanda na hivyo kupunguza Pato la Serikali linaloingia kupitia Tozo zitokanazo na uingizaji wa Mafuta.

Kuhatarisha Usalama wa vyombo vya Wananchi na kuingizia Serikali Hasara ya Fidia: Kukosekana kwa njia madhubuti za kupambana na uingizwaji wa mafuta bila ya kufata taratibu katika nchi kunaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa kupatikana kwa mafuta yasiokidhi vigezo na hivyo kupelekea uharibifu katika vyombo vinavyotumia mafuta hayo, Hali hio inaweza kuisababishia Serikali mzigo wa ulipaji wa fidia endapo ikibainika mafuta yaliotumika ndio chanzo cha matatizo yaliojjitokeza.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kutengeneza mikakati thabiti ya kuzuia na kudhibiti upatikanaji wa huduma za maji na nishati katika viwango vilivyo tarajiwa ili kufikia lengo la utengenezwaji wa Mamlaka hii na Serikali.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)

Hoja imepokelewa, Mamlaka baada ya kupata uwezo wa kitaalamu kwa kushirikiana na ZBS imeona hakuna haja ya kuendelea na huduma inayotolewa na kampuni ya GFI, jambo ambalo limesaidia kupunguza gharama za uendeshaji kwa kiasi kikubwa kwa Mamlaka na mtumiaji wa mafuta (mwananchi) kwa kupungua bei ya mafuta.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imeridhika na majibu ya Mamlaka.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inaielekeza ZURA kuhakikisha inatengeneza MoU baina yake na ZBS ili kuwepo kwa nyaraka ambayo inaonesha makubaliano hayo.

Hoja Nambari 4.1.14.9: Kutokufanya kazi kwa Mfumo wa kukagua vihatarishi (Walthrough Scanners)

Mfumo wa kukagua vihatarishi ni mfumo wa kiusalama unaotumika kuchunguza vihatarishi ambavyo vimeambatana na mtu wakati wa kuingia katika maeneo tofauti ikiwemo katika Viwanja vya Ndege, vituo vya Treni, majengo ya Serikali na kadhalika.

Ukaguzi umebaini mfumo huo haukuwahi kutumika kwa kuchunguza vihatarishi (Walkthrough scanner) katika lango kuu la kuingilia katika jengo la Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) tokea kipindi cha kukamilika kwa uwekwaji wa Mfumo huo mnamo mwaka 2020.

Aidha, ukaguzi ulishindwa kujiridhisha kutokana na kutopatiwa vielelezo vya uwepo wa kompyuta inayohifadhi na kuonesha uchambuzi wa matukio ya watu wanaopita na kukaguliwa na Mfumo huo wa kiusalama, hii ni kutokana na kutokuepo kwa sehemu iliokusudiwa kuwekwa kwa seva ya kuongoza Mtambo huo (Control Center).

Vile vile, ukaguzi ulishindwa kujiridhisha kutokana na kutopatikana vielelezo vinavyoonesha uwepo wa mafunzo yaliopatiwa wataalam (Security personel) kwa lengo la kuongoza na kusimamia Mfumo huo wa Ulinzi.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na lengo la Serikali la kuwekeza katika Mifumo ya kisasa ambayo ina lengo la kutumika katika kuboresha huduma za kiusalama katika ofisi na majengo ya Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi kuhakikisha utekelezaji wa matumizi ya mifumo ya usalama ya ndani kwa lengo la kuboresha uendeshaji na kulinda usalama kama ilivyo kadiriwa.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)

Hoja imepokelewa, Mfumo wa kukagua vihatarishi uliwekwa kwa ajili ya matumizi maalumu ya ZURA. Hata hivyo baada ya matumizi ya jengo kubadilika na kuruhusiwa taasisi nyengine kutumia jengo, mfumo huo umeshinda kutumika kama ilivokusudiwa hapo awali. Hata hivyo, Mamlaka imekusudia kutumia mashine hiyo katika jengo lake jipya la ofisi ya Pemba inayotarajiwa kujengwa hivi karibuni.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati haijaridhishwa na majibu ya Mamlaka ambapo Kamati imebaini mashine hiyo iligharimu ZURA Tsh 18,000,000, ikiwa na lengo la kutumika siku moja tu ambayo ni siku ya ufunguzi wa jengo.

Kamati imeshangazwa kuwepo kwa mashine ambayo imenunuliwa kwa fedha nyingi kwa ajili ya udhibiti na usalama lakini mashine hiyo isitumike kabisa kwa sababu ya kwamba jengo hilo linatumika na taasisi nyengine pia.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaiagiza ZURA kuhakikisha mashine hiyo inatumika kwenye jengo la ZURA liliopo Maisara ili kuleta usalama na udhibiti kwani dhamana ya jengo hilo bado lipo chini ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma

za Maji na Nishati Zanzibar licha ya kua kuna taasisi nyengine inatumia jengo hilo.

Hoja Nambari 4.1.14.10: Udhaifu katika udhibiti wa utoaji wa Leseni kupitia Mfumo wa ZIRS

Baada ya kufanya mapitio ya Mfumo wa ZIRS na kuangalia hatua zinazotumika katika utowaji wa Leseni za uendeshaji wa Biashara za Mafuta kwa Wadau wa ZURA, Ukaguzi umebaini uwepo wa udhaifu katika udhibiti wa upatikanaji wa Leseni hizo, ambapo mfumo unamuwezesha Mtumishi wa ZURA kuwa na uwezo wa kuiona na kuipakua Nyaraka ya Leseni kabla ya kukamilika kwa hatua za malipo. Hali hii inaweza kupelekea uwepo wa mianya ya rushwa na kuikosesha Serikali mapato kwa mtumishi asiyekuwa muadilifu kwa kupakuwa na kumkabidhi mteja nyaraka ya leseni kabla hajafanywa malipo.

Aidha, ukaguzi umebaini Mfumo kutokua na uwezo wa kubaini endapo Leseni iliyopakuliwa na kutumika katika vituo vya mafuta kuwa imekamilika katika hatua za malipo au laa.

Picha Nambari 12: Leseni ambayo haijamaliza taratibu za malipo katika mfumo wa ZIRS ambapo Afisa wa ZURA ana uwezo wa kuipakua kabla ya kufanyiwa malipo



Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kuhakikisha unaongeza udhibiti katika eneo hili kwa kuhakikisha kwamba Leseni inaonekana katika mfumo baada ya kukamilisha hatua za Malipo, na kwamba leseni ikishatolewa katika mfumo mara ya kwanza (original) na kama itatakiwa kutolewa tena kwa mara nyingine itambulike kama nakala (Copy 1,2,3 etc.).

Aidha, kuwekwe mgawanyo wa majukumu ambapo afisa anayehusika na leseni pekee ndo aweze kuona leseni pale inapokamilika katika hatua ya Malipo.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)

Hoja imepokelewa, Mamlaka itahakikisha inaongeza udhibiti katika eneo la utoaji wa leseni kupitia mfumo kwa kuzuwia watendaji wa ndani wasione leseni hadi malipo yatakapokamilika. Hata hivyo, Mamlaka inaendelea na maboresho ya mfumo wa ZIRS na kuhakikisha mapungufu yote yaliyobanika na mkaguzi na wafanyakazi yanafanyiwa kazi ndani ya robo ya pili ya mwaka wa fedha 2024/2025.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba hoja hii bado haijafanyiwa kazi na Mamlaka, hivyo hoja hii inabaki kwa utekelezaji zaidi.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inaiagiza Mamlaka kuhakikisha inafuata ushauri uliotolewa na Mkaguzi kutoka kwa Afisi ya CAG ili kuweza kuifanyia kazi na kuiondoa hoja hii.

Hoja Nambari 4.1.14.11: Kujirudia kwa Taarifa zinazoingizwa kwenye Mfumo wa ZIRS (Data Redundancy)

Kujirudia kwa taarifa kwenye mfumo ni kitendo cha kuwepo kwa nakala nyingi za taarifa zinazofanana ndani ya Mfumo au Kanzidata. Hali hii inaweza kutokea kutokana na utaratibu mbaya wa kuhifadhi au kurekodi Taarifa ambapo taarifa hio hujirudia mara nyingi bila sababu ya msingi.

Ukaguzi umebaini baadhi ya taarifa za Mfumo wa ZIRS zinajirudia bila ya sababu maalum kama inavyoonekana katika picha hapo chini:-

Picha Nambari 13: Hali ya takwa la mfumo la kuingiza taarifa kuhusiana na kituo cha Mafuta wakati wa ukaguzi ingawa taarifa hizo zilishaingizwa katika mfumo wakati Kituo husika kinasajiliwa



Wingi wa taarifa zinazofanana ambazo zinajaza nafasi ya kuhifadhi taarifa katika Seva (storage) na kupelekea kuongeza gharama za uwendeshaji wa mifumo ya kielektroniki kwa kulazimisha manunuzi ya Seva kubwa zaidi ili kukabiliana na mahitaji makubwa ya nafasi za kuhifadhi taarifa bila sababu za msingi.

“Sloweness” ya mfumo mara kwa mara inayosababishwa na wingi wa taarifa ambazo hazina msingi katika mfumo pamoja na ugumu wa kusimamia ubora wa taarifa mbali mbali zinazopatikana katika mfumo ikiwa ni pamoja na kusasisha taarifa ikiwa kuna nakala nyingi za data inayohusiana na taarifa hiyo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kuhakikisha unaweka utaratibu bora wa kuhifadhi “re-use” taarifa mbali mbali ndani ya mfumo katika hatua tofauti za mfumo matumizi na uingizaji wa data.

Aidha, Ukaguzi unashauri ZURA kuhakikisha kwamba taarifa zote zinazoingizwa katika mfumo zinazingatia sifa ya ubora na ukamilifu (quality and complete data) ili zitumike kuisaidia Serikali kufanya maamuzi sahihi kwa wakati.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)

Hoja imepokelewa, Mamlaka inaendelea na utaratibu wa kuzipitia fomu zote za leseni kupitia mfumo wa ZIRS ili kuondosha taarifa zinazojirejea, hata hivyo zoezi hili linategemea kukamilika ndani ya robo ya pili ya mwaka wa fedha wa 2024/2025.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imepokea majibu ya Mamlaka. Aidha, Kamati inaibakisha hoja hii kwa utekelezaji kama majibu ya Mamlaka yanavonakili.

Hoja Nambari 4.1.14.12: Kuwepo kwa Taarifa zisizo sahihi ndani ya Mfumo (incorrect data)

Kwa kuzingatia kifungu nambari 4.1.1(c) cha muongozo wa Wakala wa Serikali Mtandao wa mwezi Machi, 2022, kinachozitaka Taasisi za Umma kuhakikisha uwepo wa utaratibu wa upatikanaji na uingizaji wa taarifa bora na sahihi ndani ya Mifumo ya TEHAMA. Ukaguzi umebaini uwepo wa baadhi ya taarifa zisizo sahihi ndani ya mfumo wa ZIRS kama ilivyoambatanishwa katika picha hapo chini.

Picha Nambari 14: Eneo la kijiografia kinapopatikana Kituo cha Mafuta cha Bavuai ambapo mfumo unaonesha Kituo hicho kikiwa karibu na eneo la “Chwaka Police Station” tofauti na uhalisia ambao ni kwamba

Kituo husika kinapatikana eneo la “Mombasa Unguja” umbali wa zaidi ya kilomita 34.5 kutoka eneo linalosomeka katika mfumo



Uwepo zo hazina usahihi unaweza kuathiri muzi yanayofanywa a taarifa zilizomo n no na kuondoa ute TEHAMA katika kuo a ufanisi. Aidha, rume na miongozo ha ali kama ilivyonuku

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kuhakikisha unaweka utaratibu bora wa kuthibitisha (review) usahihi wa taarifa zinazoingizwa kwenye mfumo kabla ya “posting” ili kuhakiki ubora na ukamilifu wa taarifa husika kila hatua ya matumizi ya mfumo.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)

Hoja imepokelewa na kufanyiwa kazi. Mamlaka kupitia kitengo cha TEHAMA kiligundua kwamba kuna changamoto katika matumizi sahihi “Global Positioning System -GPS” haswa pale wakaguzi “Inspector” wanapokuweko katika eneo la ukaguzi. Tatizo hili linatokana na eneo kuwa na miti mingi, majengo marefu, milima na vizuizi vingine vinaweza kuuzia utumaji wa GPS na kuharibu mawimbi “frequency”. Halikadhalika, Ubora wa kifaa ni mojawapo ya vipengele muhimu vinavyoathiri data ya GPS. Kifaa cha GPS kisichoaminika na cha bei nafuu mara nyingi kinaweza kutoa taarifa zisizo sahihi.

Hivyo, Mamlaka ipo katika harakati ya kuwapatia wataalamu vifaa bora “Intrisic devices” ambazo zitaengeza ufanisi katika utendaji kwa wataalamu haswa katika shughuli za ukaguzi wa mafuta. Kwa upande wa Kitengo cha TEHAMA inaendelea kuwajengea uwezo wakaguzi wa ZURA juu ya matumizi sahihi ya “Global Positioning System -GPS”.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imepokea majibu ya Mamlaka. Kamati inaibakisha hoja kwa ajili ya ufuatiliaji zaidi.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaiagiza ZURA kuhakikisha inanunua vifaa vilivyo bora ili kuleta ufanisi na tija kwa wakaguzi “inspectors” ambao wanakua katika maeneo yao ya ukaguzi.

Hoja Nambari 4.1.14.13: Mapitio ya Mfumo wa Usimamizi wa Malalamiko (Complaint Management System)

Mfumo wa CMS ni mfumo uliotengenezwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA) kwa lengo la kuiwezesha Mamlaka kuhifadhi na kufuatilia malalamiko ya Wananchi kuhusiana na changamoto za upatikanaji wa huduma za Maji na Nishati.

Kwa kuzingatia matakwa ya Miongozo ya Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar ya Machi, 2022 (ICT Guidelines), Miongozo ya Wakala wa Serikali Mtandao ya Utengenezaji wa Mifumo ya Kielekroniki pamoja na Viwango kubalifu (Best practice), Ukaguzi umebaini Dosari mbali mbali katika mfumo wa Usimamizi Malalamiko (CMS) kama ilivyoelezewa hapo chini:

1. Dosari katika utowaji wa Ripoti za Mfumo wa usimamizi wa malalamiko (CMS)

Ripoti za mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano TEHAMA ni nyenzo muhimu ambazo zinaweza kutoa ufahamu na taarifa kuhusu utendaji, usalama, na mwenendo wa mfumo na shughuli fulani ndani ya Taasisi.

Ripoti hizi zinaweza kutolewa kwa viongozi wa juu, timu za IT, na wadau wengine, na zinaweza kujumuisha Ripoti za Utendaji, Ripoti za Mafanikio na kadhalika.

Aidha, ukaguzi umebaini kutokupatikana kwa ripoti zilizo sahihi kutoka ndani ya mfumo wa Malalmiko wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati ambapo ripoti zinazopatikana ndani ya Mfumo haziakisi uhalisia na ripoti za utekelezaji wa kitengo cha Uhusiano wa Umma ZURA.

Hali hii inaenda kinyume na Matakwa ya Kifungu nambari 5.1 cha Muongozo wa TEHAMA wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA ICT GUIDELINE) kinachozitaka Taasisi kuweka utaratibu wa kuhakikisha upatikanaji wa Tarifa za Uhakika, Sahihi na zilizokamilika.

Jadweli Nambari 40: Utofauti baina ya ripoti zinazopatikana kutoka kwenye mfumo wa Malalamiko (CMS) na Taarifa zinazopatikana kutoka kwenye ripoti za Utekelezaji wa Kitengo cha Uhusiano wa Umma ZURA

	Idadi ya Malalmiko Yote Yaliyosajiliwa	Idadi ya Malalamiko Yaliyofanyiwa Kazi (Resolved)	Idadi ya Malamiko Yanayoendelea Kufanyiwa Kazi (On Progress)

Ripoti Kutoka Katika Mfumo	77	0	76
Ripoti Ya Utekelezaji Kutoka Kitengo Cha (Pr)	90	65	25
UTOFAUTI	**13**	**65**	**51**

Mchoro Nambari 3: Utofauti wa Ripoti za Mfumo wa (CMS) na Ripoti halisi za utekelezaji Kitengo cha (PR)



katika
Maji na



Kukosa Taarifa Muhimu za Uendeshaji: Ripoti za mfumo zinasaidia kutoa taarifa muhimu kuhusu uendeshaji wa mfumo na shughuli za uzalishaji na utendaji katika Taasisi. Kukosa ripoti kunaweza kufanya iwe vigumu kutambua hali ya uendeshaji, utendaji na ufuatiliji wa majukumu katika Taasisi.

Kukosa Kugundua Mapema Matatizo: Ripoti za mfumo zinaweza kutoa ishara za mapema kuhusu matatizo au makosa yanayotokea. Kukosa ripoti kunaweza kucheleweshe ugunduzi wa matatizo na hivyo kusababisha madhara makubwa baadae.

Ukaguzi unaishauri ZURA kuhakikisha mifumo inauwezo wa kutoa ripoti zenye uhalisia na Sahihi ili kuisaidia Serikali katika hatua za Kufanya Maamuzi kupitia Taarifa zinazopatikana kutokana na Mifumo ya TEHAMA.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)

Hoja imepokelewa na imeshafanyiwa kazi, aidha Mamlaka kupitia kitengo cha TEHAMA kimeshawajengea uwezo kitengo cha Uhusiano juu ya suala zima la utowaji wa ripoti sahihi kupitia mfumo. Mafunzo hayo yametolewa robo ya pili ya mwaka wa fedha 2024/2025.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imeridhika na hatua za utekelezaji ambazo zimechukuliwa na Mamlaka katika kuhakikisha hoja hii inafanyiwa kazi

Hoja Nambari 4.1.14.14: Kutofanya kazi ipasavyo “Logs/ Audit Trails” ndani ya Mfumo wa ZIRS

“Logs/ Audit trails” ni rikodi za kumbukumbu za matukio yanayofanyika katika mfumo yanayojumuisha usanidi na matumizi ya mfumo katika miamala mbali mbali muda wote mfumo unapotumika au kufanyiwa mabadiliko. “Audit trails” hutumika kama njia mbadala ya kusimamia Usiri, Uadilifu, Usalama na Upatikanaji wa taarifa za Serikali muda wote.

“Audit logs” zinahusisha nakala za taarifa za miamala yote inayofanyika katika mfumo ambazo zinaweza kuwa katika hatua ya kanzidata na programu tumizi, aidha, “audit trails” zinahusisha nakala za taarifa za mabadiliko yanayofanyika katika mfumo kwenye usanidi au kufuta (delete) taarifa fulani katika mfumo. Miongoni mwa taarifa zinazohifadhiwa kwenye “audit trails” ni pamoja na mtumiaji wa mfumo (user), aina na muamala/ mabadiliko ya yaliyofanyika, tarehe na muda, na mabadiliko yoyote yaliyofanywa kwenye kanzidata au programu tumizi (mfumo).

Ukaguzi umebaini kuwa mfumo wa ZIRS haujawezeshwa kikamilifu kuchukua na kutunza “audit trails” za maeneo mbali mbali kama vile “user logs” yaani “filter user logs based on the time frame”.

Aidha, ukaguzi umebaini mfumo kupitia kipengele cha “Logs” kilichowekwa hakina uwezo wa kuonyesha kumbukumbu zaidi ya rikodi 50, ambazo hazijitoshelezi katika kufuatilia tukio/ jambo fulani lililotokea katika mfumo kwa kipindi angalau cha mwaka mmoja.

Kukwamisha ufuatiliaji na tathmini ya matukio yanayoweza kutokea kwenye mfumo: Bila “logs/ audit trail” toshelevu zenye wigo mpana wa kupata nakala za matukio ya mfumo (event viewer logs) na matukio ya kanzidata (database logs) kwa kipindi cha angalu mwaka mmoja inakuwa

vigumu kufuatilia na kutathmini shughuli zilizofanyika katika mifumo na kanzidata. Hii inaweza kuchochea utendaji wa matukio maovu ya aina mbali mbali ikiwemo ubadhirifu wa fedha za umma katika mfumo pasipo kubainika.

Ukosefu wa Uwajibikaji: Uwepo wa audit trail husaidia katika kutambua ni nani aliyesababisha au kuhusika na shughuli ama ubadhirifu fulani. Bila rekodi hizi, uwajibikaji unakuwa mgumu kuthibitisha.

Kupungua kwa Usalama: Audit trail husaidia katika kugundua shughuli zisizotarajiwa au za kutiliwa shaka. Kutowezeshwa kwa kumbukumbu hizi kunaweza kusababisha hatari zaidi ya usalama kwani itakuwa vigumu kubaini shughuli za kushukiwa za kimtandao au udanganyifu.

Kukosa Uthibitisho kwa Madhumuni ya Kisheria: Katika mazingira mengi, kama vile kufuata sheria za ulinzi wa data au kanuni za usalama wa mifumo, audit trail ni muhimu kutoa uthibitisho kwa madhumuni ya kisheria. Kutoweka kwa rekodi hizi kunaweza kusababisha kutothibitisha kufuata kwa sheria na kanuni hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kutekeleza mgawanyo wa majukumu kwa mujibu wa matakwa ya viwango bora kubalifu vya TEHAMA pamoja na miongozo ya kitaifa ili kuhakikisha kwamba kila mtumiaji wa mfumo anapewa ufikiaji wa mfumo kwa kuzingatia majukumu yake ya msingi pamoja na “Segregation of Duties (SoD)” kwa lengo la kuimarisha usiri, uadilifu, upatikanaji wa taarifa pamoja na usalama wa mifumo ya TEHAMA.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)

Hoja imepokelewa, Mamlaka kupitia kitengo cha TEHAMA kiliuwezesha mfumo kuvuta taarifa mpya 50 za **“Logs/ Audit Trails”** ili kuupunguzia mzigo seva kuvuta taarifa zote kwa wakati mmoja “**Resource Optimization**”, hata hivyo Mamlaka imepokea ushauri uliotolewa na mkaguzi na tayari limeshafanyiwa kazi kwa kuondosha ukomo wa kuvuta taarifa za **“Logs/ Audit Trails”.**

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imeridhika na kupongeza Mamlaka katika kuitatua changamoto ambayo imeibuliwa na Mkaguzi

Hoja Nambari 4.1.14.15: Dosari ya kiusalama katika upatikanaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Malalamiko (SSL Certificate issue)

SSL (Secure Sockets Layer) Certificate, ni cheti cha kidigitali kinachothibitisha utambulisho wa tovuti au Mfumo na kutoa usimamizi wa uhusiano salama (encrypted) kati ya mtumiaji na seva ya Mfumo. SSL

hutumika kuboresha usalama wa mawasiliano kwenye tovuti na Mifumo ambapo huzuia uwezekano wa watu wasiokuwa na nia njema kusoma au kuharibu taarifa inayopitishwa baina ya mtumiaji na Seva.

Ukaguzi umebaini Mfumo wa (CMS) kutokuekewa SSL certificate ilio hai na hivyo kuhatarisha mawasiliano yanayofanyika baina ya Mtumiaji na Seva kupitia Mtandao.

Hali hii inaendana kinyume na kifungu **nambari 4.3.4** cha Muongozo wa Serikali Mtandao eGAZ wa mwezi machi, 2022, kinachohitaji uwepo wa utaratibu utakao hakikisha usalama wa Tarifa na mawasiliano baina ya Mtumiaji na Seva.

Picha Nambari 15: Upatikanaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Malalamiko (Complaint Managent system) kupitia mtandao (WAN) bila ya kua na "SSL certificate" iliokua hai



Ukosefu wa Usalama wa Mawasiliano: Mifumo isiyo na SSL certificate hutuma data bila ya kuwa na usalama imara (encryption) ambapo hali hii inaweza kufanya mawasiliano kati ya mtumiaji na Mfumo kuwa wazi kwa watu wa tatu (Third parties), ambapo watakua na uwezo wakuvuruga faragha na kudukua habari za watumiaji.

Kupungua kwa Imani ya Wateja: Watumiaji wanaweza kuwa na wasiwasi kuhusu kutoa taarifa zao za kibinafsi kwenye tovuti ambayo haioneshi ishara za usalama "SSL certificates" na "https://" kwenye URL. Hii inaweza kusababisha kupungua kwa imani na kuondoka kwa walalamikaji.

Ukaguzi unaishauri ZURA kuhakikisha inaweka utaratibu mzuri wa kiusalama katika kufikia mifumo yao, ili kuboresha usalama wa taarifa zinazosafirishwa baina ya mtumiaji na Seva.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)

Hoja imepokelewa, Mamlaka kupitia Kitengo cha TEHAMA kimeshaweka ulinzi katika mfumo wa malalamiko (CMS SSL certificate), na kwa sasa unapatikanwa kupitia linki https://cms.zura.go.tz:802.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya Mamlaka na kuridhika na hatua ilizochukua katika kuhakikisha mfumo wa CMS unawekewa SSL certificate.

Hoja Nambari 4.1.14.16: Kukosekana kwa zana za kisasa za kufuatilia utendaji wa Mtandao (Modern Network Monitoring Tools)

Zana za ufuatiliaji wa Mtandao ni zana zinazoweza kufuatilia Mtandao kwa wakati halisi (real time monitoring) na kutoa taarifa ya haraka juu ya utendaji kazi na hali ya Afya ya Mtandao (Network health) kwa muda wa masaa 24 siku 7 za wiki. Zana hizi huruhusu taasisi kufanya ufuatiliaji wa Mtandao na kudhibiti mapungufu mbali mbali kabla hayajatokea (pro-active measures) na kusaidia kuongeza ufanisi wa mtandao unaopelekea kuongeza tija katika utumishi kwa kutumia TEHAMA.

Kinyume na matarajio ya wadau wa ZURA nchini pamoja na miongozo ya viwango bora kubalifu **ISO/IEC 27001(A.18)** Ukaguzi umebaini kwamba ZURA haina zana za kufuatilia hali ya Mtandao wake (Network Monitoring system) yenye uwezo wa kuifahamisha hali halisi kwa wakati (real time) ya Mtandao.

Kwa kuzingatia umuhimu wa Mifumo pamoja na miundomimbinu ya kimtandao inayopatikana ndani ya ZURA mfano Mfumo wa HRMIS pamoja na CMS.

ZURA ilitarajiwa iwe na uwezo wa kufuatilia na kufahamu kwa wakati halisi hali ya upatikanaji wa mifumo husika ili kuhakikisha kwamba hakuna mfumo utakao kuwa “down” bila ya ZURA kuwa na taarifa ili kutoa taarifa stahiki kwa watumiaji wa mifumo hiyo kabla tatizo halijatokea na kuweka mikakati mahususi ya kupata ufumbuzi wake kwa haraka.

Ucheleweshwaji wa ugunduzi wa matatizo ya Mtandao na kupelekea kuchelewa kutoa ufumbuzi wa tatizo husika hali inayoweza kukwamisha utoaji wa huduma kwa jamii katika taasisi mbali mbali za umma.

Kukosa fursa za kufanya maboresho ya mfumo wa Mtandao kwa kukosa taarifa muhimu ambazo zingeweza kupatikana kupitia zana za ufuatiliaji wa Mtandao.

Kushindwa kubaini matatizo na kutoa ufumbuzi kabla hayajatokea (pro-active measures) na badala yake kungojea mpaka matatizo yatokee kisha

ndo ZURA ianze kutafuta chanzo na ufumbuzi wake hali inayochukuwa muda mrefu wakati taasisi za umma zikiendelea kukosa huduma muhimu za ufikiaji wa mifumo yao.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kuhakikisha unatenga bajeti ya kutosha ya kununua zana za kisasa za kusimamia mfumo wa Mtandao na Mifumo ya TEHAMA pamoja na miundombinu yake yote kwa wakati halisi (real time network monitoring tools) kwa haraka iwezekanavyo ili kuepusha athari zinazoweza kutokea kama zilivyoainishwa.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)

Hoja imepokelewa, Mamlaka iliandaa zabuni yenye nambari SMZ/F0118/NCB/G/2023-2024/15 kwa lengo kutafuta mtoa huduma wa kuboresha miundombinu ya Mtandao (Network Infrastructure) katika jengo la ZURA.

Zabuni tajwa hapo juu ilifutwa kutokana na watoaji huduma waliopatikana kutokukidhi matakwa na sifa zilizo orodheshwa kwenye zabuni hiyo, hata hivyo Mamlaka inaendelea na harakati ya kutangaza zabuni nyengine kwa ajili ya maboresho yote ya miundombinu ya mtandao ikiwemo yaliyotajwa katika hoja hii.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imeridhika na hatua za utekelezaji ambazo ZURA imechukua ili kuhakikisha zana za kisasa za kusimamia mifumo ya mtandao na mifumo ya TEHAMA pamoja na miundombinu yake zinanunuliwa. Aidha, Kamati imebaini kwamba Zabuni ya mwanzo ilifutwa kutokana na watoa huduma waliomba zabuni hawakua na sifa.

MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI ZANZIBAR (ZMA)

Hoja Nambari 4.1.26.1: Udhibiti duni katika chumba cha Seva cha Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA)

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa udhibiti duni wa chumba cha Seva ambapo chumba cha Seva hakina udhibiti wa moja kwa moja wa moto (automatic fire suppression system), vile vile kutokuwepo kwa Kamera za ulinzi (CCTV Camera) na mlango wa kuingilia katika chumba cha Seva upo katika hali dhaifu.

Hali hii ni kwenda kinyume na miongozo ya viwango bora kubalifu vya kimataifa. Vile vile hali hii inaweza kuleta athari mbalimbali ikiwemo hatari ya Upotezaji wa Vifaa, kuvuja kwa habari Nyeti, kuharibika na kupotea miundombinu na rasilimali za TEHAMA. Aidha, inaweza kusababisha kuongezeka kwa hatari za kiusalama wa taarifa na usiri.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA) kuchukuwa hatua ili kuweza kutatua changamoto hii iliyojitokeza.

Majibu ya Uongozi wa ZMA

Mamlaka imeshachukua hatua ya kuongeza usalama wa kuingilia chumba cha seva kwa kuweka ‘’two-way authentication” (biometric unlock + local key) pamoja na kuweka CCTV camera.

Hata hivyo kwa upande wa “Automatic fire suppression system” Mamlaka imepanga kuifanyia kazi katika mwaka wa fedha 2024-2025.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba Mamlaka kwa upande wa “Automatic fire suppression system” imeiandikia barua Kikosi cha Zimamoto Zanzibar yenye kumbukumbu namba JA.13/16/01/29 ya tarehe 16/07/2024 inayohusu “OMBI LA KUPATIWA HUDUMA NA VIFAA VYA KUZIMIA MOTO KATIKA AFISI YA MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI ZANZIBAR. Lengo kuu la barua hiyo ni kukaguliwa kwa ajili ya kuwekewa mfumo wa uzimaji moto ndani ya jengo hilo na jinsi ya kuweza kuutumia mfumo huo.

Hamkadhalika, Kikosi cha Zimamoto Zanzibar wamejibu barua yenye kumbukumbu namba ZM/HQ/I.M.SMZ/01/VOL.1/09 ya tarehe 24/07/2024 na kupangiwa kufanyiwa mafunzo siku ya tarehe 26/07/2024.

Aidha, hadi Kamati inamaliza uchunguzi, Kamati imebaini mafunzo hayo hayakutolewa licha ya kuwepo malipo ya Tsh 300,000 yaliyofanyika kwa ajili ya mafunzo hayo. Kamati pia imebaini kwamba mfumo huo mpaka uchunguzi unakamilika bado haukufungwa.

Kamati kimsingi imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Mamlaka, aidha hoja itaendelea kubakia kwa ajili ya ufuatiliaji.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inaielekeza Mamlaka kuhakikisha inafuatilia zaidi kwa Kikosi cha Zimamoto Zanzibar ufungaji wa mfumo huo wa uzimaji moto kiotomatiki "Automatic fire suppression system" pamoja na kupatiwa mafunzo kwa watendaji wanaoshughulikia mfumo huo.

Hoja Nambari 4.1.26.2: Udhaifu katika mfumo wa kusajili Meli na Mabaharia (Vessels & Seafarers Registration Systems)

Ukaguzi wetu umebaini uwepo wa udhaifu katika mfumo wa kusajili Meli na Mabaharia (Vessel & Seafarers Registration System) ambapo mapungufu hayo yameorodheshwa kama ifuatavyo:-

1. Kukosekana kwa mpangilio mzuri wa kutoa Ripoti za Vyombo vya Baharini

Ukaguzi umebaini Ripoti zinayotolewa katika mfumo wa Kusajili meli (Vessel Registration System) hazitenganishi Meli za ndani, Meli za nje na vyombo vidogo vidogo na badala yake hutoa ripoti mchanganyiko.

Hali hii inapelekea changamoto kubwa kwa watendaji pale wanapohitaji ripoti za vyombo mahsusi kutoka kwenye mfumo.

2. Ripoti haziwezi kuchuja (Filtering) meli zilizo Hai (Active) na zilizokwisha muda (Expired)

Ukaguzi umebaini kuwa Ripoti za ujumla za mfumo wa kusajili meli, haziwezi kuchuja meli zote zilizo Hai (Active) na zilizokwisha muda (Expired), meli zote zinaonekana katika hali mchanganyiko, ripoti hizi zinapatikana katika ripoti mjumuisho (Custom Report).

Changamoto hii inapelekea kushindwa kuweza kuchanganua ripoti hizi na kufatilia kwa hatua meli zilizokwisha muda.

3. Kuruhusu kujirejea kwa majina ya Meli ndani ya mfumo

Ukaguzi umebaini mfumo wa Usajili wa Meli kuruhusu kusajili Meli zenye majina sawa (Vessel Name Duplication).

Hali hii husababisha ndani ya mfumo kuwa na majina ya meli yaliyojirejea na hivyo kupelekea kwa mtumiaji kufanya makosa wakati wa ujazaji wa taarifa za meli husika au kutoa ripoti zenye makosa

4. Ripoti za mjumuisho haziwezi kutolewa "export" ndani ya mfumo wa kusajili meli

Ukaguzi umebaini kuwa mfumo wa kusajili meli, hauwezi kutoa “export” ripoti mjumuisho “custom report” ndani ya mfumo.

Watendaji wanapochuja na kupanga ripoti “Filtering & Sorting” ndani ya mfumo wanashindwa kuzitoa ripoti hizo baada ya kuzichuja.

Hali hii inapelekea watendaji na watumiaji wa mfumo kushindwa kuzitumia ripoti hizo nje ya mfumo kwa kufanya uchambuzi.

5. Mfumo kushindwa kutafuta taarifa za baharia (Searching) kwa kutumia Hati ya kusafiria (Passport)

Ukaguzi umebaini mfumo wa kusajili Mabaharia (Seafarers Registration System) kutoweza kutafuta taarifa za mabaharia kwa kutumia hati ya kusafiria (Passport).

Hali hii inaweza kuleta changamoto mbalimbali ikiwemo kushindwa kujua ni baharia gani anatumia hati ya kusafiria Fulani. Hii ilileta changamoto wakati tunasajili Baharia kwa kutumia hati ya kusafiria lakini zoezi letu halikufanikiwa kwa sababu nambari ya hati ya kusafiria tuliyoingiza tuliambiwa imetumika na Baharia mwengine. Hata hivyo Hatukuweza kujua namba hiyo hati ya kusafiria kama imetumika na Baharia gani ndani ya mfumo kwa sababu mfumo hauwezi kutafuta (Search) baharia kwa kutumia nambari ya hati ya Kusafiria.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA) kuchukuwa hatua ili kuweza kutatua changamoto hizo zilizojitokeza.

Majibu ya Uongozi wa ZMA

1. Ni kweli mfumo wa kusajili Meli na Mabaharia ulionekana una changamoto katika kutenganisha ripoti za meli za ndani, meli za nje na vyombo vidogo vidogo. Hata hivyo, Mamlaka tayari imeshafanya mawasiliano na Kampuni ya Ocean HQ na kupata maelekezo juu ya utatuzi wa suala hilo. Kwa sasa ripoti hizo zinapatikana bila ya mchanganyiko.
2. Mfumo hauchuji meli zilizo hai na zilizokwisha muda wake isipokuwa mfumo unachuja vyeti vya meli zilizosajiliwa vilivyo hai na vilivyokwisha muda wake.
3. Mfumo wa usajili wa meli hutoa indhari juu ya majina ya meli wakati wa usajili na hauruhusu kuendelea na hatua za kusajili meli kwa kutumia jina la meli ambalo limeshatumika.
4. Ni kweli mfumo ulikua hauwezi kutoa ripoti za mjumuisho (export) kwa baadhi ya taarifa, na kwa sasa Mamlaka imeshawasiliana na Kampuni ya Oceans HQ kwa ajili ya kurekebisha kasoro hiyo, hivyo mfumo tayari unatoa taarifa mjumuishi (export) ambapo watumiaji wa mfumo huo wanaweza kuzitumia nje ya mfumo huo kwa kufanya uchambuzi na kuzifanyia kazi.

5. Mamlaka inatoa hati ya kusafiri baharia (discharge book) Kwa nambari maalum ambayo hutumika kwa kutafuta (searching) uhalali wa taarifa ya baharia. Taarifa nyengine kama nambari ya pasi ya kusafiria au kitambulisho cha Taifa (NIDA au ZanID) huingizwa katika mfumo ili kupata taarifa za awali za baharia.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

1. Kamati imebaini kwamba mfumo wa Kusajili meli (Vessel Registration System) ni mfumo ambao ni "generic" na ilitakiwa watumishi wa kitengo cha TEHAMA cha ZMA wafanye "customization" kwa ajili ya mazingira na mahitaji ya ZMA.
   Kamati imebaini kwamba mfumo huo upo vizuri na changamoto ilikua kwa watumishi wa kitengo cha TEHAMA ambao hawakua na mafunzo ya jinsi ya kuutumia mfumo huo, licha ya kupata mafunzo ya awali.
   Mfumo huo ni "software as a lisence" na unatumika nan chi nyingi zikuwemo nchi za UK na Liberia.
2. Kamati imebaini katika uwezo wa mfumo kuchuja taarifa "filtering", njia bora na sahihi ni kuchuja kupitia vyeti "certificates" ambavyo vipo hai badala kuchuja meli "vessels" zilizohai. Hivyo, Kamati imeridhika na majibu ya Mamlaka.
3. Kamati imeridhishwa na majibu ya ZMA ambapo imebaini kwamba kutumia majina katika kutafuta vyombo ndani ya mfumo sio njia sahihi ukizingatia vyombo hivyo vinasajiliwa kwa kutumia "IMO Number" ambazo kila chombo inakua na namba ya kipekee.
4. Katika uwezo wa mfumo kutoweza kutoa ripoti za mjumuisho (export) kwa baadhi ya taarifa, Kamati ya PAC imeridhika na hatua zilizochukuliwa na Mamlaka na imeridhika na majibu ya Mamlaka
5. Kamati imebaini kwamba kwa upande wa mabaharia, "dispatch book" ndio inayotumika zaidi kwatika mfumo kuliko pasipoti "passport" ya kusafiria na inawezekana Baharia akapata "dispatch Book" mwanzo kabla hata ya pasipoti "passport". Hii ni kutokana na viwango vya kimataifa "international standards".

Kwa mnasaba huo, Kamati imeridhika na majibu ya Mamlaka.

Hoja Nambari 4.1.26.3: Udhaifu katika mfumo wa Bill Portal kutokuonesha Status za "Control Number" zilizoghairika (Cancelled) na zilizokwisha muda (Expired)

Ukaguzi umebaini mfumo wa Bill Portal unaweza kutoa "Status" za "Control number" katika hali mbili, zisizolipiwa yaani (Outstanding) na zilizolipiwa (Paid) tu. Hali hii inaleta changamoto ya kutoweza kujua control number zote zisizolipiwa yaani "Outstanding" ikiwa zimeghairishwa (cancelled) au zimeisha muda wa matumizi "Expired".

Hali ya kutokuwepo Status ya Control number zilizoghairishwa (Cancelled) au na zilizokwisha muda wa matumizi “Expired” kunaweza kuleta changamoto kwa upande wa Ripoti na kutaka kujua sababu ya kuwa na Control number zisizolipiwa, na ikiwa zimelipiwa controlled number zilizotolewa kimakosa basi zionekane zimeghairishwa ili zisiwemo katika “waiting list” ya Ripoti zisizolipiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA) kuchukuwa hatua ili kuweza kutatua changamoto hii iliyojitokeza.

Majibu ya Uongozi wa ZMA

Ni kweli Mfumo wa Bill Portal ulikuwa hauoneshi “status” za Control Number zilizoghairika (Cancelled) na zilizokwisha muda (Expired) kwa sasa Mamlaka tayari imesharekebisha changamoto hiyo katika mfumo wa Billing Portal na sasa “control numbers” zilizohairika (cancelled) na zilizokwisha muda (Expired) zinaonekana status yake.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilifanya uchunguzi wake na kuupitia mfumo na kujihakikishia kwamba hoja hii kwa sasa imeweza kufanyiwa kazi na changamoto iliyoonekana na mkaguzi imeweza kutatuliwa. Hivyo, Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya Mamlaka na kuiondoa hoja hii.

Hoja Nambari 4.1.26.4: Udhaifu katika mfumo wa kutoa Leseni wa Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA)

Ukaguzi umebaini kuwa mfumo wa kutoa Leseni wa ZMA umejitokeza mapungufu mbalimbali kama yafuatayo:-

1. Mfumo kuruhusu kupokea Nenosiri (Password) dhaifu

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo unaruhusu kusajili nenosiri (Password) dhaifu wakati wa kufungua “Account”.

Hali hii imebainika kwa kufungua “user account” na kuweka nenosiri (Password) isiyofuata mbinu za kiusalama za neno siri lakini kwa bahati mbaya neno siri hili iliruhusiwa na mfumo.

2. Mfumo Hauwezi kutoa Ripoti maalum (Custom Report) kwa baadhi ya taarifa

Tumebaini mfumo kutoweza kutoa ripoti maalum (Custom Report) kwa baadhi ya taarifa muhimu zinazopatikana ndani ya mfumo huo.

Mfano tulijaribu kutafuta ripoti maalum ya Kampuni kwa kutumia eneo husika “Location” ilipo Kampuni hiyo lakini hatukupata, vilevile tulijaribu kutafuta Kampuni zote zilizokuwa na leseni hai (Active License) lakini

hazikuweza kuonekana ndani ya mfumo na badala yake zinatokea ripoti ya leseni za Kampuni mchanganyiko yaani “Active & Expired”.

Majibu ya Uongozi wa ZMA

1. Ni kweli Mfumo ulikuwa unaruhusu Kupokea neno la siri (password) dhaifu na kwa sasa Mamlaka tayari imeshatatua chanagmoto hiyo kwa kuufanyia “updating” na kwa sasa mfumo hauruhusu Kupokea neno la siri (password) dhaifu.
2. Ni kweli Mfumo ulikuwa hauwezi kutoa ripoti maalum kwa baadhi ya taarifa, kwa sasa Mamlaka tayari imeshatatua chanagmoto hiyo kwa kuufanyia “updating” mfumo na sasa unaweza kutoa ripoti maalum (Custom Report) pamoja na kutoa ripoti zilizohai (Active) na zilizokwisha muda (Expired)

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC baada ya kujiridhisha, imebaini ni kweli changamoto ambazo zilibainishwa na Mkaguzi zilikuepo lakini Mamlaka kwa jitihada zao imeweza kuzifanyia kazi changamoto hizo na kuweza kuzitatua. Hivyo, Kamati ya PAC imeridhishwa na utekelezaji wa hoja hizi.

Hoja Nambari 4.1.26.5: Kuweza kusajili jina la Kampuni zaidi ya mara moja

Ukaguzi umebaini kuwa mfumo unaruhusu kusajili jina la Kampuni zaidi ya mara moja “Company Name Duplication”. Hali hii inaweza kuwachanganya watendaji/watumiaji wa mfumo pale wanapotaka kufanyia kazi Kampuni ambayo imejitokeza mara mbili, kujua ipi sahihi, vile vile kuna uwezekano mkubwa wa kutolewa Ripoti zisizokuwa na uhalisia baada ya Kampuni zilizochujwa wakati wa kutafuta (Searching) kujitokeza mara mbili.

Ukaguzi unauishauri uongozi wa Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA) kuchukuwa hatua ili kuweza kutatua changamoto hii iliyojitokeza.

Majibu ya Uongozi wa ZMA

Mfumo wa utoaji leseni wa Mamlaka unaruhusu kutoa leseni kwa jina moja la Kampuni zaidi ya mara moja kwa sababu Kampuni hizo zinajishughulisha na kutoa huduma tofauti zinazohitaji leseni.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba kutokana na uhalisia na shughuli za Mamlaka, kuna uwezekano mkubwa sana wa kampuni kusajiliwa kwa jina moja lakini ikawa inatoa huduma “services” tofauti kabisa na kampuni nyengine. Hivyo tofauti itaonekana katika aina ya huduma ambazo zinatolewa pamoja nae neo lao la kutoa huduma.

Kwa mnasaba huo, Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya Mamlaka.

Hoja Nambari 4.1.26.6: Kutotumika kwa mifumo ya Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA) kwa upande wa Pemba

Ukaguzi umebaini Mifumo yote inayopatikana Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA) haitumiki kwa upande wa Afisi za Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA) Pemba isipokuwa mfumo wa Bill Portal tu. Mteja akihitaji huduma ambayo inapatikana kupitia mifumo ya ZMA, itamlazimu taarifa zake zitumwe Makao Makuu Unguja kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Kuchelewa kutolewa kwa huduma ndani ya taasisi kunaweza kusababisha athari mbali mbali zinazoweza kuathiri sifa ya taasisi, ufanisi wa shughuli zake, na uzoefu wa watumiaji. Baadhi ya athari hizo ni pamoja na kucheleweshwa kukamilika kwa shughuli zinazohusiana na huduma hizo jambo ambalo linaweza kupunguza ufanisi wa kazi na kuathiri mzunguko wa kazi ndani ya taasisi.

Aidha, ikiwa huduma zinahusiana na Taasisi au mapato, kuchelewa kutolewa kwa huduma kunaweza kusababisha hasara ya mapato. Wateja wanaweza kukosa fursa za kuhudumiwa na kupelekea kuhama kwa washindani.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZMA kuhakikisha unazingatia umuhimu wa kutoa huduma kwa wakati na kuhakikisha michakato inaimarishwa ili kukidhi mahitaji ya wateja kwa ufanisi zaidi. Hii inaweza kujumuisha kuimarisha miundombinu, mafunzo ya wafanyakazi, na kutumia Teknolojia ili kuboresha mchakato wa utoaji wa huduma.

Majibu ya Uongozi wa ZMA

Ni kweli kwa Upande wa Pemba ilikua inatumia Mfumo moja tu wa Bill Portal kwa sasa Mamlaka tayari imeshapeka mifumo yote inayostahiki na kutumika katika Ofisi ya Mamlaka Usafiri Baharini – Pemba mifumo hiyo ni mfumo wa vyombo vidogo vidogo na mabaharia, na mfumo wa kutoa Leseni imeshaungwa na kuanza kutumika na sasa huduma zimerahisishwa na watumiaji wanaweza kusajili na kupatiwa certificate ndani ya dakika 15 baada ya kukamilika kwa malipo husika.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya Mamlaka. Aidha, katika uchunguzi wake, Kamati ya PAC ilitaka kujua sababu ambazo imepelekea kwa mifumo hiyo kuchelewa kupelekwa katika Afisi ya Mamlaka Pemba, na kubaini kwamba ni uwezo mdogo wa kipindi hicho kwa kitengo cha TEHAMA kwani mifumo hiyo inahitaji usalama na udhibiti wa hali ya juu.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaiagiza Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar kuhakikisha inazidi kuboresha huduma kwa upande wa Pemba na kuhakikisha wanawajengea uwezo wa kutosha wataalamu wa TEHAMA kwa upande wa Pemba ili kuweza kutoa huduma endelevu na yenye manufaa kwa jamii.

UCHUNGUZI WA KAMATI YA PAC KUHUSU UKAGUZI WA TAARIFA ZA SERIKALI KUU KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023

MFUKO WA FEDHA WA HUDUMA ZA AFYA ZANZIBAR (ZANZIBAR HEALTH BASKET FUND)

Hoja nambari 4.5.1.1: Kuchelewa kuingizwa kwa fedha za Mradi

Kifungu nambari 13 cha Makubaliano kinaelezea Usimamizi na utoaji wa fedha ambapo kifungu nambari 13.3 kinaelekeza kwamba washirika wa maendeleo wataingiza pesa za mradi kwenye akaunti ya pamoja mwezi wa kwanza wa robo ya kwanza wa mwaka wa fedha.

Ukaguzi umebaini kuchelewa kuingizwa kwa fedha za mradi kutoka kwa washirika wa maendeleo hali iliyosababisha kushindwa kutekeleza shughuli nyingi zilizopangwa. Hali hii inaweza kusababisha ucheleweshwaji wa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa za miradi na itapelekea matokeo yaliyokusudiwa kutofikiwa.

Ukaguzi unashauri washirika wa maendeleo kuingiza fedha za mradi kwa muda uliopangwa kwenye mwongozo wa utekelezaji wa mradi. Hii itarahisisha utoaji wa fedha kwa wakati kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi. Jadweli lifuatalo linaonyesha muda na kiasi cha fedha kilichotolewa na washirika wa maendeleo kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni, 2023.

Jadweli nambari 27: Fedha zilizoingizwa na Washirika wa Maendeleo

Washirika wa Maendeleo	Tarehe ya fedha zilivyoingizwa	Kiasi (Tsh.)
UNICEF	18/11/2022	232,300,000
HIPZ	27/06/2023	10,000,000
Jumla		**242,300,000**

Majibu ya Uongozi

Wizara itawashauri washirika wa maendeleo kusaini Makubaliano ya kuingizwa fedha (Side Agreement) kwa kipindi cha Aprili – Juni ya kila mwaka ilikuondosha changamoto ya ucheleweshaji wa uingizaji wa fedha ambapo kiutaratibu inatakiwa ziingizwe ndni ya mwezi wa kwanza wa robo ya kwanza wa mwaka wa Fedha.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba wakati Mkaguzi anatekeleza kazi za ukaguzi wa Mradi huu ni kweli fedha zilikuwa hazijaingizwa. Kamati ilitaka kujua fedha hizo zinatoka kwa Wahisani gani wa Maendeleo na kuelezwa kuwa hizi ni

fedha za pamoja katika ya Wahusani tofauti na Serikali ambapo tayari fedha zimeshaingizwa na Wahisani wawili kufikia jumla ya shilingi 400,000,000 lakini fedha za Serikali bado hazijaingizwa.

Sambamba na hilo, kamati imeelezwa kwamba hizi sio fedha za Miradi ya Maendeleo isipokuwa ni Mfuko wa fedha za pamoja kati ya Wahisani na Serikali ambapo hutumika kusaidia katika utekelezaji wa shughuli zilizoainishwa ndani ya Bajeti ya Wizara. Ili kuipatia ufumbuzi hoja hii, Kamati imeamua kukutana ba Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kujua changamoto iliyosababisha kuchelewa kuingizwa kwa fedha za Serikali hadi hivi sasa.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Wizara ya Afya ishirikiane na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ili fedha hizo ziweze kuingizwa na kufikia malengo yaliyopangwa.

Hoja nambari 4.5.1.2: Kuchelewa kuingizwa kwa fedha za Walengwa wa Mradi

Kulingana na Mpango wa Utekelezaji kila shughuli imepangwa kwa muda maalum wa kutekelezwa ndani ya kila robo mwaka. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2022/23. Ukaguzi umebaini kulikuwa na ucheleweshaji mkubwa wa kutolewa kwa fedha kutoka hesabu ya pamoja (JHA) kwenda kwenye hesabu za walengwa wa utekelezaji wa mradi.

Kuchelewa kuingiziwa fedha kwa walengwa kunaweza kusababisha kuchelewa kutimia kwa malengo ya mradi na kusababisha usumbufu katika utekelezaji wa mradi, na hatimaye kuathiri kufikia malengo ya mradi. Kuchelewa kuingiza fedha kwa watekelezaji wa mradi hupelekea kuharibu mipangilio ya uendeshaji wa kazi za mradi zilizopangwa kutekelezwa.

Ukaguzi unapendekeza kurahisisha mchakato wa utoaji wa fedha ili kuharakisha utoaji wa fedha kwa wanufaika wa mradi. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 28: Fedha iliyoingizwa kwenye akaunti za watekelezaji wa Mradi

Jina la Hesabu	Tarehe Fedha Iliyoingizwa	Kiasi (Shs)
Katibu Mkuu Wizara ya Afya	9/1/2023	45,513,503
MOH Central Medical Store	9/1/2023	146,190,000
District Health Services Pemba	9/1/2023	53,452,697
DHMT North 'A'	9/1/2023	14,115,774
DHMT North 'B'	9/1/2023	10,959,730
DHMT Central	9/1/2023	14,925,009

DHMT South	9/1/2023	8,259,763
DHMT Town	9/1/2023	27,001,101

Majibu ya Uongozi

Wizara itahakikisha fedha zitaanza kutumika mara tu baada ya kuingizwa katika mfuko wa Fedha za pamoja

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba bado fedha za hesabu ya pamoja hazijaingizwa na kusababisha kukwama utekelezaji wa shughuli za Wizara hususan shughuli za hospitali za Wilaya ambazo zilipangwa katika ununuzi wa vifaa tofauti.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inasisitiza kwa Serikali kufuatilia kutolewa kwa fedha hizo na kuingizwaji katika hesabu ya pamoja na kuwafikia walengwa.

Hoja nambari 4.5.1.3: Kutoingizwa kwa fedha za Mradi kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar shilingi 800,000,000

Kifungu nambari 6 cha Hati ya makubaliano (MoU) kinatafsiri majukumu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambapo kifungu nambari 6.1(i) kinaitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuchangia kiasi kilichokubalika kwenye mfuko wa Afya wa pamoja kwa mujibu wa hati ya makubaliano ya pamoja.

Ukaguzi umebaini kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliahidi kuchangia shilingi 800,000,000 kwenye mfuko wa Afya wa pamoja kupitia makubaliano ya pamoja na washirika wa maendeleo. Mpaka mwaka wa fedha unamaliza Serikali haijachangia fedha hizo ambapo itapelekea kutokutekelezwa kwa baadhi ya shughuli za mradi, aidha ni kwenda kinyume na makubaliano ya pamoja.

Ukaguzi unaishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuchangia fedha kwenye Mfuko wa Afya wa pamoja kama ilivyoahidi ili ziweze kutekeleza shughuli za mradi zilizopangwa.

Ukaguzi unaishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuchangia fedha kwenye Mfuko wa Afya wa pamoja kama ilivyoahidi ili ziweze kutekeleza shughuli za mradi zilizopangwa.

Majibu ya Uongozi

Wizara ya Afya iliandika barua tarehe 17.2.2023 kwenda Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ili kuomba kuingiza fedha shilingi milioni **800,000,000,** kwa bahati mbaya mpaka mwisho wa mwaka wa fedha 2022/2023, fedha hizo hazikuingizwa. Hata hivyo mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali

imeahidi kuchangia shilingi milioni 400,000,000, ambazo fedha hizo zimepatikana kwa asilimia 100.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imegundua kwamba ni kweli Mkaguzi alibaini kwambi jumla ya shilingi 400,000,000 bado hazijatolewa na Serikali kuingizwa katika Mfuko wa Afya wa Pamoja. Hivyo, Kamati itaendelea kuifuatilia hoja hii kama ilivyoelezwa katika hoja nambari 4.5.1.1.

Hoja nambari 4.5.1.4: Vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye daftari la ghalani shilingi 37,687,635

Kwa mujibu wa kifungu nambari 31 (2) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016, Afisa masuuli anatakiwa kuhakikisha anaanzisha mfumo wa uendeshaji na uwazi wa usimamizi wa fedha na vihatarishi na udhibiti wa ndani ili kusaidia usimamizi wa matumizi.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya shilingi 37,687,635 zilitumika katika ununuzi wa mafuta na vifaa mbalimbali kulingana na mahitaji ili kuwezesha shughuli za uendeshaji wa Mradi ambapo ukaguzi ulibaini uwepo wa bidhaa zilizonunuliwa ambazo hazikurikodiwa kwenye daftari la ghalani.

Kutokurikodiwa vifaa katika daftari la ghalani kunaweza kupelekea ukaguzi kuwa na mashaka na maamuzi hayo, aidha, ni kwenda kinyume na kifungu kilichonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZHBF kuimarisha udhubiti wa ndani kwa kurikodi bidhaa zote zinazonunuliwa kwenye daftari la ghalani kabla ya matumizi. Mchanganuo wa vifaa hivyo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 29: Vifaa ambavyo havijaingizwa kwenye daftari la ghalani

Kati ya mali			**Aliyelipwa**	**Maelezo**

1/418/4/2023	DHMT West 'A'	3,000,000	Salum TransportCompany	Ununuzi wa mafuta.
6/531/5/2023	Central Medicalstore (Un	3,130,300	Miembeni Lubricant Center	Ununuzi wa vifaa vya

	guja)			magari.
9/630/6/2023	CentralMedicalstore(Ungujа)	5,150,000	Tahfif Auto Works	



1/66/6/2023	Centralmedicalstore(Pemba)	15,000,000	Africom Ltd	Ununuziwavifaavyaya ICT
10/630/06/2023	Centralmedicalstore(Ung	1,500,000	Khamiar Enterprices Ltd	Ununuzi wa stationaries

	uja)			za ofisi
4/630/6/2023	DHMT Central	1,788,250	Adem Store	Ununuzi wa vifaa vya magari
23/6/2023	DHMT North ‘A’	1,632,000	G.M Traders	
3/623/6/2023	DHMT Central	2,000,000	Atlas Graphicsand Digital Advertisement	Ununuzi wa v

2/5/2023	DHMT West 'A'	1,987,085	Quality Trades	ifaa vya kuandikia.
2/6236/2023	DHMT Central	2,500,000	Atlas Graphic and Digital Advertisement	ununuzi wa vifaa vya magari se

				r v i c e s
		37,687,635		

Majibu ya Uongozi

Wakati ukaguzi unafanyika Kwa bahati mbaya kuna baadhi ya vielelezo vya vifaa havikuambatanishwa. Hata hivyo Wizara ilichukua hatua ya kuhakikisha vifaa vyote vimerikodiwa na vielezo vyote vimeambatanishwa na vipo tayari kwa ukaguzi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake, ni kweli vifaa alivyoviorodhesha vilikuwa havijaingizwa kwenye daftari la ghalani na kupelekea taratibu za manunuzi kukiukwa. Hata hivyo Kamati imefanikiwa kuviona vifaa hivyo vimeorodheshwa katika dadtari husika. Hivyo Kamati imeridhika na majibu ya hoja hii na kuiondosha.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Watendaji wa Wizara ya Afya Pemba wahakikishe wanahifadhi vizuri vielelezo vya vifaa walivgonunua katika utekelezaji wa Miradi yao na kuviingiz katika daftari la ghalaki kwa wakati. Hoja imeondolewa.

PROGRAMU YA CHANJO - EPI (GAVI)

Hoja nambari 4.5.2.1: Kutotelekelezwa kwa shughuli zilizopangwa zenye thamani ya shilingi 1,001,913,061.43

Wizara ya Afya Zanzibar ilipokea jumla ya shilingi 1,001,913,061.43 sawa na USD 432,978.85 kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za CDS kutoka Kitengo cha Idara ya chanjo kilicho chini ya Wizara ya Afya Tanzania Bara.

Ukaguzi ulibaini Mradi ulipitisha matumizi ya fedha hizo kwa mujibu wa barua yenye Kumb. namba CAC.261/433/03 ya tarehe 06 Machi, 2023 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi kwa mwaka 2022/2023, ambapo kiasi cha fedha cha shilingi 1,001,913,061.43 hakikuweza kutumika licha ya kupitishwa na kutengewa kiasi cha fedha katika utekelezaji wa shughuli za mradi. Mchanganuo wa shughuli za mradi zilipopangwa lakin hazikutekelezwa ni kama zinavyoonekana katika jedwali apo chini:

Jadweli Nambari 30: Shughuli za mradi ambazo zimepangwa na kutengewa fedha lakini hazikutekelezwa

Namba	Shughuli za Mradi	Kiasi kilichopangwa(Tsh.)
1.	**Uhamasishaji wa Jamii na Mawasiliano**	
	DSA kwa washiriki	6,100,000
	Viburudisho (PHCs)	1,200,000
	Kurushwa kwa Michezo ya Redio na TV	1,800,000
	Jumla Ndogo (A)	**9,100,000**
2.	**Usambazaji wa chanjo**	
	Usambazaji wa chanjo (Kutoka RVS hadi DVS)	13,370,000
	Jumla Ndogo (B)	**13,370,000**
3.	**Utekelezaji wa kampeni**	
	DSA kwa Wasimamizi wa Mikoa na Halmashauri	81,700,000
	Posho za Ushuru wa ziada kwa Watoa Chanjo	839,139,714
	Mafuta	58,603,347
	Jumla Ndogo (C)	**979,443,061**
Jumla Kuu (A+B+C)		**1,001,913,061**

Majibu ya Uongozi

Programu ilipanga kutumia fedha hizo kwa ajili ya utoaji wa chanjo za UVIKO 19. Wakatai wa utekelezaji tulipata wafadhili ambao ni (Zanzibar

Maisha Bora Foundation, Jhpiego, UNICEF). Hivyo Wizara iliamua kuzitumia fedha hizo kwa matumizi mengine. Hadi kufikia Juni 2023 jumla ya fedha **Tsh 842,857,000/-** na Fedha zilizobaki zilitumika kwa kipindi cha Julai hadi Agosti 2024 kupitia Huduma za Mkoba (Outreach).

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya fedha hizo kutumika. Kamati ilitaka kujua kuna vielelezo vyovyote vya kuthibitisha uhaulishaji wa matumizi yake lakini hakukuwa na kielelezo hicho.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Watendaji wa Wizara ya Afya wahakikishe wanapotumia fedha za Wahisani kutekelezea shughuli ambazo zimepangwa ndani ya bajeti yao wahaulishe vifungu vya fedha hizo.

Hoja nambari 4.5.2.2: kiasi cha dawa kilichokwisha muda wa matumizi

Kifungu cha 5(c) cha Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya Zanzibar ya 2006 kinasema kuwa "kulaani na kuamuru uharibifu au utupaji wa bidhaa yoyote iliyodhibitiwa chini ya Sheria hii inayoonekana kuwa haifai kwa matumizi yaliyokusudiwa".

Ukaguzi umebaini jumla ya dozi 834 za chanjo za MR na Covid 19 zilizoingia na kupokelewa Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ambazo zilikuwa zimeisha muda wake wa matumizi na wala hazikurikodiwa katika daftari lolote, licha ya dawa hizo kulimbikizwa katika duka la Ofisi ya Wilaya ya Kusini, ambapo hadi ukaguzi unamalizika Disemba, 2023 hakuna hatua zozote zilizochukuliwa juu ya Dawa hizo. Kuendelea kuwepo kwa Chanjo zilizokwisha muda wake wa matumizi kunaweza kukapelekea kuhatarisha maisha ya binadamu iwapo zitatolewa na zitatumika bila kujua muda wa matumizi ya dawa hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mradi kuhakikisha unafuatilia kwa karibu kutoka kwa Mamlaka inayohusika ili kupata kibali cha kuzitokomeza dozi 834 ya chanzo zinatolewa pamoja na kuanzisha daftari la kurekodi orodha za madawa yalikwisha pita muda wake wa matumizi pamoja na kutenga eneo maalum ya uwekaji wa madawa yaliyokwisha muda wa matumizi kwa binaadamu.

Jadweli Nambari 31: Chanjo zilizokwisha muda wake ambazo hazijateketezwa

Kipengele	Unit Dose	Tarehe yakumalizika muda wa matumizi
Chanjo ya MR	410	Septemba, 2023
Chanjo ya Sinovac COVID 19	330	Juni, 2023

Chanjo ya Sinopharm COVID 19	94	Agosti, 2023
Jumla	**834**	

Majibu ya Uongozi

Taratibu za zinazotakiwa kufuatwa za uangamizaji wa chanjo zilizoisha muda wake kama ifuatavyo: -

1. Chanjo zote lazima ziondolewe kwenye mnyororo baridi na kuwekwa mahali salama.

2. Kuzirekodi katika leja maalum ya chanjo zilizomaliza muda wake.

3. Kuwasilisha barua rasmi kwa Mamlaka ya Chakula na Dawa Zanzibar (ZFDA) kwa taratibu za uteketezaji.

4.Kuomba kibali Mamlaka ya usimamizi wa Mazingira Zanzibar.

Hatua zote hizo Wizara imezipitia na chanjo zilizomaliza muda ziliteketezwa chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Chakula na Dawa Zanzibar (ZFDA).

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imegundua kuwa wakati Mkaguzi anafika kukagua Mradi huu, ni kweli dawa zilikwishamaliza muda wa matumizi wala zilikuwa hazijatekelezwa. Hata hivyo, kwasasa tayari dawa hizo zimetekelezwa kwa mujibu wa sheria. Uteketezwaji huo ulifanyika tarehe 12/8/2024 ambapo Wakala wa Chakuka na Dawa umsthibitisha zoezi hilo kwa kutoa cheti chanye kumbukumbu nambari ZFDA/COD/0009/2024 cha tarehe 11/11/2024. Kwa vile zoezi hilo linefanyika kwa mafanikio, kamati imeiondoa hoja hii

Maagizo ya Kamati ya PAC

Wizara iwe makini kufuatilia dawa ambazo zimeisha muda wake wa matumizi na kuziteketeza kwa wakati ili kuzuia uwezekano wa kufumika kwake. Hoja nambari 4.5.2.3: Ushuru wa ongezeko la thamani kwa miamala ya banki ya shilingi 1,216,542.41

Hoja nambari 4.5.2.3: Ushuru wa Ongezeko la Thamani kwa miamala ya benkiyenye thamani ya shilingi 1,216,542.41

Kifungu cha 15 cha GAVI Alliance na Mkataba wa Mfumo wa Ubia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Chanjo na msaada wa fedha taslimu wa 2013 kinasema kuwa “Fedha za GAVI zitakazotolewa chini ya Mkataba huu hazitatumika kulipa kodi, forodha, ushuru, tozo au nyinginezo, gharama zinazotozwa kwa uingizaji wa chanjo na vifaa vinavyohusika. Serikali itatumia juhudi zake za kuridhisha kuweka utaratibu ufaao wa kuondoa ushuru na kodi kwenye manunuzi yote yanayofanywa ndani na nje ya nchi kwa fedha za GAVI”.

Ukaguzi ulipitia taarifa ya Kibenki za Mradi kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 na kubaini kuwa EPI Zanzibar wana akaunti katika benki ya PBZ yenye Namba 0404440000 ambapo benki ya PBZ inatoza VAT ya shilingi 1,216,542.41 kwa kila muamala unaofanywa na IVD ambapo ni kinyume na nukuu iliyonukuliwa hapo juu. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mradi kuchukua hatua zinazofaa ili kuhakikisha hakuna VAT inayolipwa kwa mujibu wa makubaliano kwa kutumia mfuko wa GAVI pamoja na kurejesha kiwango cha VAT cha shilingi 1,216,542.41 kilicholipwa kwa kila mwezi. Maelezo yanaonyeshwa kwenye jadweli hapo chini:

Jadweli nambari 32: kiasi cha VAT kilichotozwa kwa miamala ya kibenki kwa kila mwezi

Mwezi	Kiasi cha VAT Kilichotozwa (Tsh)
Julai	77,035.32
Agosti	457.62
Septemba	167,980.26
Oktoba	19,723.69
Novemba	6,406.77
Disemba	591,429.91
Januari	210,605.14
Februari	21,100.49
Machi	67,291.82
Aprili	37,608.01
Mei	9,797.96
Juni	7,105.42
Jumla	**1,216,542.41**

Majibu ya Uongozi

Wizara ya Afya imeamua kurudisha fedha hizo kwenye mfuko wa GAVI. Aidha, ili kuepusha kutokea tena tatizo hilo, Wizara ya Afya Zanzibar iliandika barua kwa Katibu Mkuu (OR) Fedha na Mipango kuomba kuingizwa katika utumiaji wa mfumo wa EPICOR ambao hauna makato wakati malipo. Hata hivyo (OR) Fedha na Mipango, ilibadilisha mfumo wa fedha kutoka EPICOR na kutumia BAMAS ambao hauwezi kutumika kwa fedha za nje ya bajeti ya Serikali. Hivyo, Wizara imeiandikia Wizara ya Afya Tanzania bara ili kuingizwa kwenye mfumo huo kwa vile wao bado wanaendeleo kuutumia.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imegundua kuwa fedha hizo zilitolewa na Wahisani wa Maendeleo zikiwa na masharti waliyokubaliana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa vile fedha hizo ndiko zilipotokea kwamba zisikatwe kodi. Hata hivyo, katika utumiaji wa fedha hizo, Wizara ya Afya Zanzibar ilikuwa ikizikata kodi ya ongezeko la thamani (VAT) pamoja na fedha ya huduma ya benki kwa pamoja (service charge) kimakosa.

Hadi Kamati inapokea majibu ya utekelezaji wa hoja hii, bado fedha hizo hazijarudishwa kwa Wahisani.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Watendaji wa Wizara ya Afya wawe makini kutekeleza makubaliano katika utekelezaji wa Miradi ya maendeleo inayodhaminiwa na Wahisani wa Maendeleo.
2. Watendaji wa Wizara ya Afya wahakikishe wanafuatilia fedha hizo Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ili kurekebisha changamoto iliyopo.
3. Barua ya tarehe 4/2024 yenye kumbukumvu nambari AB.244/455/12 kutoka Wizara ya Afya Kwenda kwa Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhusu kupokea fedha kutoka Shirika la GAVI zilizoingizwa kwenye Mfumo wa malipo unaosimamiwa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango.

Hoja nambari 4.5.2.4: Matumizi yaliyofanywa bila ya kuzingatia matumizi ya risiti za kielektroniki (EFD) shilingi 5,184,270

Kifungu nambari 23 (1) cha Sheria namba 7 ya Usimamizi wa Ushuru ya 2021 kinamtaka mtu anayesambaza bidhaa au kutoa huduma iwe kwa mkopo au pesa taslimu au anapokea malipo kuhusiana na bidhaa zinazotolewa au huduma iliyotolewa atatoa risiti ya kielektroniki kwa huduma. Aidha, barua yenye Kumb: Nam WN/ORFM/2022/VOL.V/20 ilitoa agizo la kuwataka wazabuni kuwasilisha stakabadhi za madai ya malipo (Invoice) na risiti kwa kutumia mashine za kielektroniki (EFD).

Ukaguzi uliofanyika katika Mradi wa IVD GAVI umebaini kuwa Mradi ulitumia shilingi 5,184,270 kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali bila kuzingatia matumizi ya risiti za kielektroniki kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli namba 33: Matumizi yaliyofanywa bila ya kuzingatia matumizi ya risiti za kielektroniki

Tarehe	Hati Namba	Ruzuku	Kiasi (Shs)	Aliyelipwa	Maelezo
30/01/23	V/HSS/01/14	HSS	1,959,020	BHCL Contractor Co Ltd	Maitenance of Store
25/05/23	V/HSS/05/07		3,225,250	Alim Consultant	Quick

					Book
Jumla			**5,184,270**		

Majibu ya Uongozi

Ni kweli wakati wa ukaguzi kuligundulika kwamba kuna malipo yalifanywa bila ya kuzingatia matumizi ya mfumo wa risiti za kielektroniki (EFD) badala yake zilitumika risiti za mkono, hii hali ilitokana na matatizo ya kimtandao kwa wakati ule wa utoaji risiti hizo. Hata hivyo kwa sasa malipo yote yanayofanywa na mradi yanazingatia utoaji wa risiti za kielektroniki (EFD).

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati katika kutathmini utekelezaji wa hoja hii ilibaini kwamba wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake ya kikatiba, Wizara ilitumia ilifanya malipo kwa bila ya kutumia risiti, a kielektroniki na badala yake walitumia risiti za mkono. Hali ilisababishwa na kujitokeza kwa kukwamakwama kwa mfumo wa kielektroniki jambo ambalo ni kinyume na sheria. Hata hivyo, kwasasa Wizara inaendelea kutumia risiti za kielektroniki ambapo kamati imefanikiwa kuona risiti ya aina hiyo ya tarehe 2/8/2024 yenye jumla ya shilingi 809,100 ikiwa ni malipo ya kodi kwa ajili ya zuio la kodi kwa supplier Alim Consultant na BHCL Construction Co. Ltd. Kwa vile Kamati imeridhika na utekelezaji wa hoja hii, Kamati ya PAC imeiondoa hoja hiyo.

Hoja nambari 4.5.2.5: Ununuzi uliofanywa bila ya kutumia mfumo wa E-Proz shilingi 39,340,503.78

Kifungu nambari 5(1) (i) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza “kuanzisha na kusimamia mfumo wa manunuzi wa kielektroniki”.

Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ) ilitoa taarifa kupitia barua yenye kumbukumbu namba MUUMU.BA.156/370/01/27 ya tarehe 12/8/2022 kuhusu Matumizi ya Mfumo wa Manunuzi wa Kielektroniki (e-PROZ) na kuzifahamisha taasisi zote za manunuzi za Serikali kutumia mfumo huo.

Ukaguzi umebaini kuwa manunuzi yaliyofanywa na Mradi wa IVD GAVI yenye thamani ya Shilingi 39,340,503.78 yamefanywa nje ya mfumo huo, jambo ambalo ni kinyume na kifungu nambari 5(1)(i) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya 2016.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Mradi kuzingatia miongozo iliyotolewa kwa kuhakikisha manunuzi yote yanafanyika kwa mfumo wa kielektroniki wa Ununuziwa Umma.

Jadweli namba 33: Ununuzi uliofanywa bila ya kutumia mfumo wa e-Proz

Tarehe	Hati Namba	Aliyelipwa	Maelezo	Kiasi (Shs)
30/01/23	V/HSS/01/14	BHCL Contractor Co Ltd	Maitenance Of Store	1,959,020.00
24/1//23	V/HSS/01/15	New Home Furniture	Office Equipment	980,000.00
24/01/23	V/HSS/01/16	Zan Printing	Stationary	768,627.00
24/01/23	V/HSS/01/17	Zanzibar Petroleum Ltd	Fuel EPI Pemba	6,000,000.00
24/06/23	V/HSS/01/18	Zanzibar Petroleum Ltd	Fuel EPI Unguja	12,000,000.00
Tarehe	Hati Namba	Aliyelipwa	Maelezo	Kiasi (Shs)
30/01/23	V/HSS/02/02	Jawaja Auto Parts	Vehicle Mentenance	865,340.00
30/01/23	V/HSS/02/03	Jawaja Auto Parts	Vehicle Mentenance	1,702,206.00
30/01/23	V/HSS/02/04	Jawaja Auto Parts	Vehicle Mentenance	1,110,340.00
22/03/23	V/HSS/04/02	Safia Shaibu Baki	Refreshment	4,582,941.18
23/03/23	V/HSS/04/03	Safia Shaibu Baki	Refreshment	759,019.60
10/05/23	V/HSS/05/02	Jawaja Auto Parts	Vehicle Mentenance	2,655,800.00
12/05/23	V/HSS/05/03	Coolpro Refrigeration And Engineering	Maintanance	931,960.00
28/04/23	V/HSS/05/04	Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni	Venue	600,000.00
28/04/23	V/HSS/05/05	ZSSF	Venue	1,200,000.00
25/05/23	V/HSS/05/07	Alim Consultant	Quick Book	3,225,250.00

Majibu ya Uongozi

Ni kweli kwamba TZS **39,340,503.78** za manunuzi yaliyofanywa bila kutumia Mfumo wa E-Proz kutokana na kitengo cha manunuzi kuwa na ufahamu kwamba, manunuzi ya serikali pekee ndio yanayopaswa kufanywa kwa kutumia Mfumo wa E-Proz. Lakini kitengo tayari kimeaanza kutumia mfumo huo E-Proz kwa manunuzi yote kama kilivyoelekezwa. Kwa sasa manunuzi yote ya kitengo yanayofanywa, yanaingizwa katika mfumo wa E-Pro.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa ni kweli kulikuwa na kasoro za kufanyika manunuzi bila ya kutumia mfumo wa E-Proz. Hali hiyo ilisababishwa na Watendaji wa Manunuzi wa Wizara ya Afya kutokuwa na uelewa kwamba matumizi ya mfumo wa E-Proz huwa yanafanyika kwa fedha za Serikà pekee. Hata hivyo, kwasasa wamejiandaa kutumia Mfumo huo hata katika fedha za Wahisani ambao hawajaweka masharti katika matumizi ya fedha wanazozitoa.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Watendaji wa Wizara waendee kutumia Mfumo wa E-Proz katika manunuzi ya Miradi yao ya maendeleo ili kuepusha kujitokeza hoja zisizo za msingi.

Hoja nambari 4.5.2.6: Upotevu wa ziada wa chanjo za Rotavan

Ukaguzi ulifanya uhakiki wa upotevu wa chanjo za Rotavac nakubaini uwepo wa upotevu wa Chanjo hizo kutokana na kutokufuatwa kwa Sera ya Vial Multidose ya chupa moja kwa dozi tano.

Pia, ukaguzi ulibaini sababu za upotevu wa chanjo ni kutokana na chanjo kutumia kiwango kidogo cha Multidose Vial Policy ambapo chanjo hiyo huisha muda wake wa matumizi kila baada ya saa Sita pindipo inapofunguliwa kwenye chupa yake.

Ukaguzi ulifanya ziara ya kutembelea maeneo ya Hospitali ya Wete na Chakechake - Pemba na kubaini uwepo wa upotevu wa chanjo ya Rotavac ya 7007 na dozi 2721 mfululizo kwa mwezi wa Januari, 2023 hadi Juni 2023 kama inavyoonyeshwa katika majadweli hapo chini. Kuendelea kuharibika kwa chanjo kunaweza kukapelekea hasara kubwa ya kifedha na lengo la Serikali la kuhakikisha Chanjo zilizoagizwa zinatumika kama ilivyokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mradi inaweka udhibiti mzuri wa uwagiziaji Chanjo mpya ya Rotavac ambayo zitamudu kukaa hadi siku 28 kutoka wakati wa ufunguzi wa chupa za chanjo pia kuhakikisha Wahudumu wa Afya wanapewa mafunzo kuhusu mbinu bora zaidi za kupunguza upotevu wa chanjo. Hali halisi ya upotevu wa Chanjo hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli zifuatazo:

Jadweli namba 35: Orodha ya chanjo ya Rotavac ya Wilaya ya Wete Pemba kutoka Jan, 2023 hadi Juni 2023

Vifaa vya Afya		Jumla ya kipimo kilichowekwa	Upotevu wa jumla wa	Asilimia (%)

			dozi	
Bwagamoyo PHCU	435	685	250	36.50
Chwale PHCU	275	555	280	50.45
Finya PHCU	367	585	218	37.26
Fundo PHCU+	325	510	185	36.27
Jadida PHCU	1360	2200	840	38.18
Jungu ni PHCU	554	865	311	35.95
Kambini PHCU	402	635	233	36.69
Kangagani PHCU	514	785	271	34.52

Kinyasini PHCU	584	960	376	39.17
Kisiwani PHCU	419	595	176	29.58
Kiungoni PHCU	1329	1940	611	31.49
Kojani PHCU+	519	815	296	36.32
Makongeni PHCU+	446	740	294	39.73

Mzambarauni Takao PHCU	329		321	49.38

Minungwini PHCU	683	1120	437	39.02
Pandani PHCU	655	1150	495	43.04
Ukunjwi PHCU	283	475	192	40.42
Uondwe PHCU	615	985	370	37.56
Vumba PHCU	555	855	300	35.09
Wete District Hospita	989	1540	551	35.78

l				
	11638	**18645**	**7007**	**37.58**

Jadweli Nambari 36: Data ya Chanjo ya Rotavac ya Wilaya ya Chake Chake Jan hadi Juni, 2023

Vifaa vya Afya	Rota 1	Rota 2	Rota 3	Jumla ya kipimo Chanjo	Jumla ya dozi zilizofunguliwa	Upotevu	Asilimia (%)
Ali Khamis Camp (JWTZ)	84	77	67	228	290	62	21.4
Chakechake District Hospital	506	418	325	1249	2940	1691	57.5
Chonga PHCU	244	210	141	595	610	15	2.5
Gombani PHCU	392	366	303	1061	1140	79	6.9
JKU Wawi	101	88	83	272	405	133	32.8
Kibokoni PHCU	50	33	34	117	170	53	31.2
Mbuzini PHCU	124	92	73	289	365	76	20.8
Mgelema PHCU	25	27	19	71	85	14	16.5
Mvumoni (Furaha) PHCU	92	59	42	193	240	47	19.6
Ndagoni PHCU	108	87	86	281	315	34	10.8
Ngomeni PHCU	10	9	7	26	35	9	25.7
Ole PHCU	112	95	68	275	285	10	3.5
Pujini PHCU+	323	277	269	869	875	6	0.7
SDA - Wawi Dispensary	70	63	40	173	215	42	19.5
Shungi PHCU	59	65	52	176	175	-1	-0.6
Tundauwa PHCU+	81	72	67	220	420	200	47.6
Uwandani PHCU	89	68	40	197	240	43	17.9
Vikunguni PHCU	67	49	32	148	160	12	7.5
Vitongoji Cottage Hospital	95	113	90	298	375	77	20.5
Wesha PHCU+	69	52	59	180	210	30	14.3
Ziwani PHCU	100	95	71	266	355	89	25.1
Jumla	**2801**	**2415**	**1968**	**7184**	**9905**	**2721**	**27.5**

Majibu ya Uongozi

Chanjo ya Rotavac ni kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa kuharisha kwa Watoto. ROTAVAC inapaswa kutolewa kwa dozi 3, katika wiki 6, wiki 10, na wiki 14 sambamba na Chanjo ya Polio ya Kunywa (OPV), chanjo ya Pentavalent na PCV-13.

ROTAVAC inahifadhiwa kwenye mnyororo baridi wa +2 ° C ± 8 ° C.

UTARATIBU WA MATUMIZI.

Chanjo hii mara tu baada ya kufunguliwa inapaswa kutumika ndani ya **saa sita tu na si zaidi ya hapo.** Kichupa kimoja kina dozi tano na ikatokea hawajatimia idadi hio ndipo inapokuwa na upotevu **usioepukika** kwa sababu dawa iliyobaki italazimika kutupwa baada ya masaa 6. Ununuzi na matumizi ya chanjo hii umezingatia mambo yote hayo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Ni kweli wakati Mkaguzi anafanya kazi za ukaguzi katika Mradi huu, kulikuwepo na chanjo za Rotavan ambazo zilikuwa za ziada. Hali hiyo ilikuwa haiwezi kuepukika kwa vile chanjo hizo zinakuwa zinakaa kwa muda mfupi usiozidi masaa sita. Hata hivyo, Kamati ilitidhishwa na utekelezaii wa hoja hii na kuiondoa.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Wizara ichukue tahadhari katika ununuzi na utumiaji wa chanjo za Rotavan kwa kuzingatia na mahitaji ili kuepusha kuharibika kwa wingi na kusababisha uwepo wa hoja za namna hii.

OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO

Hoja Namba 5.4.1.1 Ununuzi wa mafuta bila ya kuwepo mkataba shilingi 191,446,790.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 191,446,790 zimelipwa na Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa mtoa huduma United Group Limited. Kati ya fedha hizo shilingi 74,095,000 zilitumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya petroli na shilingi 117,351,790 zilitumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya dizel. Dosari ilyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa mkataba maalum wa ununuzi wa mafuta, jambo ambalo linaweza kupelekea kuzuka kwa migogoro baina ya wafanyabiashara hao na Wizara pale inapotokezea kutokufahamiana, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kuhakikisha unaongeza umakini katika kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo inayotolewa na Serikali ikiwemo kufunga mikataba kwa watoa huduma kama Sheria inavyoelekeza.

Majibu ya Uongozi wa Fedha na Mipango

Awali Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango ilikuwa ikinunua mafuta bila ya kuwa na framework contract kununua mafuta kwa kutumia (Local Purchase Order) na ililazimika kufanya hivyo kwa vile imekuwa ikipata changamoto kwa kampuni za mafuta juu ya kukamilisha taratibu za manunuzi ikiwemo kutowasilisha nyaraka za zabuni pindi unapowapatia. Aidha, hakukuwa na muongozo uliotolewa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma (ZPPDA) juu ya mifumo ya Mikataba Maalum “Frame Work Contract”.

Hata hivyo, kwa sasa Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango imeshafanya mchakato wa zabuni na hivi karibuni utakamilika na kwa kuzingatia muongozo uliotolewa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma (ZPPDA) juu ya mifumo ya Mikataba Maalum “Frame Work Contract” ili kuweza kwenda sambamba na taratibu zilizowekwa juu ya ununuzi wa mafuta.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Baada ya kamati ya PAC kupata ufafanuzi wa hoja hii, Kamati emebaini kuwa Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kweli haikufuata utaratibu wa miongozo inapaswa katika kuhakikisha kuwa ununuzi wote wa mafuta unafanyika kwa kufuata sheria na taratibu, ikiwa ni pamoja na kuandaa mikataba rasmi na watoa huduma ili kuepusha migogoro na kuhakikisha uwazi katika matumizi ya fedha za umma.

Hata hivyo kamati ya PAC imeridhika na hatua za utekelezaji wa hoja hii.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauagiza Uongozi Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kuhakikisha inafuata miongozo na taratibu zote za kuimarisha uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika ununuzi wa mafuta kwa taasisi za umma.

Hoja Namba 5.4.1.2 malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslim shilingi 107,451,300

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango imefanya malipo yenye jumla ya shilingi 107,451,300 kwa njia ya fedha taslimu jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za umma, aidha ni kwenda kinyume na kanuni. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kuhakikisha unafuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kufanya malipo kupitia benki.

Majibu ya Uongozi wa Fedha na Mipango

Katika kukamilisha taratibu za malipo ikiwa ni maposho ya safari au mengineyo kuna njia tofauti za kulipa ikiwemo malipo ya moja kwa moja kutoka kwenye mfumo kwa kutumia (vendor) na kuhaulisha kutoka kwenye mfumo kupitia benki nyengine kwenda kwenye akaunti ya mtu husika. Hivyo hoja iliyoainishwa na wakaguzi malipo yake yamelipwa kwa njia ya pili ambayo ni kutoka kwenye mfumo kupitia benki nyengine kwenda kwenye akaunti ya muhusika**.**

Hili ni kwa mujibu muongozo uliotolewa na Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) ya kwamba Ofisi inaweza kufanya malipo ya si zaidi ya Tsh. 15,000,000 kwa mwezi kwenda kwa walipwaji ambao hawamo kwenye mfumo wa malipo ya Serikali. Mahitaji ya kutumia utaratibu huo hutokezea pale ambapo Ofisi imeendesha mafunzo/semina/kikao na kuwa na idadi kubwa ya washiriki ambao ni vigumu kuwalipa mmoja mmoja kwa mujibu wa mfumo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Baada ya kupokea ufafanuzi wa kina kuhusu hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa malipo yalifanyika kinyume na miongozo ya ufungaji wa hesabu, kwani baadhi ya manunuzi hayakuwa ya dharura kiasi cha kuhalalisha kutotumia mifumo rasmi ya ununuzi.

Hata hivyo, baada ya kupitia jitihada zilizochukuliwa na **Wizara**, Kamati imeridhika na hatua zilizofanyika katika kurekebisha kasoro hiyo

Hoja Namba 5.4.1.3: Malipo yaliyofanyika kinyume na miongozo ya ufungaji wa hesabu shilingi 248,361,770

Ukaguzi umebaini kwamba Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango imefanya malipo yenye thamani ya shilingi 248,361,770 kwa ajili ya kulipia huduma mbali mbali. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kufanyika kwa malipo kinyume na toleo lililobainishwa hapo juu jambo ambalo huenda likapelekea kujitokeza kwa changamoto katika ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kuhakikisha kwamba unasimamia na kutekeleza miongozo ya kifedha wanayoitoa ili kuwa ni kigezo kwa Taasisi nyengine.

Majibu ya Uongozi wa Fedha na Mipango

Kwa kawaida kila ifikapo mwisho wa mwaka tunapewa toleo linaloonyesha mwisho wa matumizi lakini kutokana na shughuli muhimu za Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango inatulazimu kuendelea na matumizi hata baada ya tarehe hiyo na malipo haya yamelipwa kwa kufuata taratibu zote za malipo. Hata hivyo, Uongozi unaahidi kufuata miongozo yote inayotolewa.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Baada ya kufanya uchunguzi wake kwa kina, Kamati ya PAC imebaini kuwa changamoto hii inatokana na hulka ya kiutendaji ya Wizara ya Fedha pamoja na mfumo wake wa matumizi ya fedha. Asili ya majukumu ya wizara hii, ikiwa ni pamoja na usimamizi wa rasilimali za umma na mchakato wa ununuzi, imechangia kutokea kwa changamoto hii. Hali hii inadhihirisha umuhimu wa kuimarisha mifumo ya ununuzi na utekelezaji wa matumizi ya fedha ili kuhakikisha kuwa taratibu zote zinafuatwa ipasavyo kwa mujibu wa sheria na miongozo inayotolewa.

Kwa mnasaba huo kamati ya PAC imeibakisha hoja hii kwa ajili ya utekelezaji zaid.

Hoja Namba 5.4.1.4 Malipo yaliyolipwa kinyume na utaratibu shilingi 35,000,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango iliidhinisha utoaji wa fedha mnamo tarehe 23/06/2023 na kukabidhiwa Msaidizi Mshika Fedha Mkuu kuzihifadhi katika maduhuli kinyume na utaratibu wa muongozo wa ufungaji wa hesabu. Aidha, ukaguzi ulipitia hati mbalimbali zinazohusiana na malipo ya mwaka wa fedha unaoishia Juni, 2023 na kubaini uwepo wa hati za malipo zilizoambatishwa na barua za maombi ya fedha za mwaka 2022/2023, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuambatanishwa kwa vielelezo vya matumizi hayo na uhaulishaji wa fedha uliofanywa kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Vile vile, katika tathmini iliyofanyika ukaguzi umebaini kwamba malipo hayo ya fedha hayakuwa

katika orodha ya fedha zenye dhamira maalum (commitments). Hii ni kwenda kinyume na kanuni nambari 21(1)(a)(b) ya kanuni za fedha za 2021. Aidha, ukaguzi haukupatiwa vielelezo vinavyohusiana na maombi na ruhusa (approval) ya kutumia fedha za mwaka husika kwenye mwaka unaofuata vilivyopelekwa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kutoka kwa afisa masuuli, jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu namba 21(2) cha kanuni za fedha za mwaka 2021. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kuhakikisha kuwa unafuata kikamilifu sheria, kanuni na miongozo mbalimbali inayohusiana na fedha pale wanapotekeleza majukumu yao ya kiutendaji ya kila siku.

Majibu ya Uongozi wa Fedha na Mipango

Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango imepokea ushauri na kuahidi kufuata sheria na miongozo yote.

Aidha, Ofisi ina jukumu la kuhakikisha kwamba serikali inapata fedha za matumizi kwa wakati, hivyo ililazimika kutenga fedha hizo kwa matumizi lakini taratibu za malipo zilikuwa hazijakamilika. Fedha hizi zilikuwa ni masurufu kwa ajili ya safari ambazo taarifa zake zilikuwepo lakini zilishindwa kulipwa kwa mwaka husika kwa sababu utaratibu wa malipo ulikuwa bado haujakamilika.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Wakati kamati ikufuatilia utekelezaji wa hoja hii, Kamati imebaini kuwa Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango imekiri kutokea kwa dosari ya Malipo yaliyolipwa kinyume na utaratibu na kuahidi kuwa kufuata sheria na miongozo yote ya ununuzi.

KAMISHENI YA UTALII ZANZIBAR

Hoja nambari 5.8.2.1: Tofauti iliyojitokeza baina ya Hesabu ya Mwisho wa mwaka na Mikataba halisi iliyofungwa shilingi 87,126,930

Kwa mujibu wa muongozo nambari 2 wa mwaka 2022/2023 wenye kumbukumbu nambari ACGEN/BC.195/393/01/01 wa tarehe 13/06/2023 kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango unaohusiana na zoezi la kufunga hesabu la mwaka wa fedha 2022/2023 ikisisitiza ufungaji wa hesabu uzingatie muongozo uliotolewa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 wenye kumbukumbu nambari AD.5/184/01/08/90 uliotolewa na (OR) Fedha na Mipango Zanzibar tarehe 9/6/2022 unazitaka Taasisi za Serikali kutayarisha taarifa sahihi za mapato na matumizi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokuwepo kwa uwiyano wa taarifa za fedha baina ya taarifa za fedha zilizoripotiwa katika Hesabu za Mwisho wa mwaka na taarifa zilizomo katika mikataba halisi iliyofungwa na Kamisheni jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa tofauti ya shilingi 87,126,930 baina ya taarifa hizo. Aidha, inapelekea taarifa za Hesabu zilizoandaliwa na kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi kutokuonyesha sura halisi na sahihi kulingana na vigenzo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa ikiwemo toleo la ufungaji wa Hesabu nililolinakili hapo juu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii kuhakikisha unaingiza taarifa sahihi za mapato na matumizi katika Taarifa za Hesabu za mwisho wa mwaka ili kuweza kuonyesha sura sahihi na halisi kwa mujibu wa viwango vya ufungaji wa Hesabu vya Kitaifa na Kimataifa. Hali halisi ya tofauti hiyo ni kamainavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 78: Tofauti kati ya Hesabu za Mwisho wa mwaka na Taarifa katika Mikataba

Kifungu cha matumizi	**Fedha za Mikataba iliyoainishwa katika Hesabu ya mwisho wa mwaka (Tshs)**	**Aina ya Mikataba iliyofungwa 2022/2023**	**Thamani (Tshs)**	**Tofauti (Tshs)**
Contracting fees	90,945,000	Mkataba wa utunzaji wa bustani Bungi kwa Bihole 600,000 kwa	7,200,000	

		mwezi		**87,126,930**
		Mkataba wa huduma ya ulinzi (Bungi) Tzs 1,200,000 kwa mwezi	14,400,000	
		Mkataba wa hudumaya ulinzi Kamisheni shs 1,020,000 kwa mwezi	12,240,000	
		361 Degrees Africa(SMS-Private) Ltd	68,960,950	
		Tea Party Zanzibar (TPZ)	73,370,980	
		Tea Part Zanzibar addendum	1,900,000	
Jumla	**90,945,000**		**178,071,930**	**87,126,930**

Majibu ya Uongozi wa Kamisheni

Ni kweli kuna tofauti iliyotokea baina ya hesabu za mwisho wa mwaka na mikataba halisi. Hii inatokana na Kamisheni kuangalia kwenye shughuli ambazo zinafanywa zinahusika na vifungu gani badala ya kuangalia uhalisia wa mkataba walioingia. Hivyo basi Kamisheni ilihaulisha vifungu mbali mbali ambavyo vinaendana na mazingira ya Tamasha vikiwemo ADVERTISING CHARGES, HIRING OF CONFERENCE FACILITIES, CONTRACTING FEES, TRANSPORT ALLOWANCE, FOOD AND REFRESHMENT, PATROL na SECURITY SERVICES kwani uhalisia ulikuwa kuhaulisha vifungu vyote ili viingie kwenye kifungu cha contract. Naambatanisha na vocha husika.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katia kufuatilia majibu ya hoja hii, Kamati ya PAC ilibaini kwamba ni kweli Mkaguzi aligundua kasoro ya kuwepo tofauti baina ya Hesabu ya Mwisho wa mwaka na Mikataba halisi iliyofungwa yenye jumla ya shilingi 87,126,930. Hali hiyo ilitokana na Kamisheni kukabiliwa na shughuli ya Tamasha la ZTITE Lakini ilikuwa halijapangiwa bajeti yake awali. Kutokana na uwepo wa uhitaji wa kufayika Tamasha hilo kwa maslahi ya Zanzibar. Kamisheni ilichukua maamuzi ya kuiandikia barua Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kupitia Idara ya Bajeti kuomba kufanyiwa uhaulishaji wa vifungu

vyake vya bajeti ilivyonavyo bila ya kuongeza fedha kwa barua ya tarehe 23 Januari, 2023 yenye kumbukumbu nambari CAB.115/306/01/ ambayo iliomba uhaulishwaji wa shilingi milioni mia mbali ambayo pamoja na matumizi mengine yaliyofanyika, mlikuwa pia na jumla ya shilingi 87,126,930 zilioinishwa na Mkaguzi.

Kutokana na uchunguzi huo, Kamati imegundua kuwa wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake katika Kamisheni hii, hakuweza kupatiwa kielelezo hicho. Hili linathibitishwa na majibu ya 'Management letter' ya Kamisheni kwamba walikubali uwepo wa hoja hiyo. Kwa msingi huo, hoja hii inabakia hadi Mkaguzi atakapoenda kujiridhisha.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Kamisheni ya Utalii uhakikishe unaingiza taarifa zote za mapato na matumizi katika Taarifa za Hesabu za mwisho wa mwaka ili kuweza kuonyesha sura sahihi na halisi kwa mujibu wa viwango vya ufungaji wa Hesabu vya Kitaifa na Kimataifa.

Hoja nambari 5.8.2.2: Tofauti iliyobainishwa kati ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka na Taarifa za Mapato shiling 724,427,202

Kwa mujibu wa muongozo nambari 2 wa mwaka 2022/2023 wenye kumbukumbu nambari ACGEN/BC.195/393/01/01 wa tarehe 13/06/2023 kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango unaohusiana na zoezi la kufunga hesabu la mwaka wa fedha 2022/2023 ikisisitiza ufungaji wa hesabu uzingatie muongozo uliotolewa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 wenye kumbukumbu nambari AD.5/184/01/08/90 uliotolewa na (OR) Fedha na Mipango Zanzibar tarehe 9/6/2022 unaeleza kwamba taarifa zote za mapato yatokanayo na vyanzo mbalimbali ziingizwe katika Taarifa za Hesabu ya Mwisho wa Mwaka (Financial Statement)". Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa tofauti ya taarifa za fedha za Kamisheni ya Utalii baina ya taarifa ya mapato zilizoripotiwa katika Hesabu za Mwisho wa Mwaka ambazo ni shilingi 5,710,528,729 na taarifa za makusanyo ya leseni zilizoripotiwa kupitia kumbukumbu za mapato ya Kamisheni yenye jumla ya shilingi 4,986,101,527 jambo ambalo limepelekea kuwepo kwa tofauti ya mapato yenye jumla ya shilingi 724,427,202 kati ya taarifa hizo. Kufanya hivyo kunapelekea taarifa za Hesabu za Mwisho wa mwaka kutokuonyesha Sura halisi na Sahihi kulingana na muongozo wa ufungaji wa Hesabu uliounakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni kuhakikisha unaingiza taarifa sahihi katika Hesabu za mwisho wa mwaka zinazolingana na Taarifa za Mapato zilizobainishwa kupitia kumbukumbu za mapato sambamba na kufanya usuluhishi wa kibenki ili kuweza kubaini tofauti zinazoweza kujitokeza katika taarifa za mapato.

Majibu ya Uongozi wa Kamisheni

Ni kweli kuna tofauti kati ya mapato yaliyoonyeshwa. Kwenye Hesabu za mwisho wa mwaka “Financial Statement” jumla ya shilingi 5,710,528,729 na kwenye Zan Malipo ni jumla ya shilingi 4,986,101,527 na kufanya tofauti ya ongezeko katika hesabu ya mwisho wa mwaka yenye jumla ya shilingi 724,427,202. Aidha uwepo wa tofauti hio ni kutokana na changamoto zinazojitokeza katika Benki mbali mbali za kuhaulisha fedha za wateja wao ambao miongoni mwao ni wadau wa Kamisheni bila kunakili malipo ya mfumo wa Control Number ijapokua mtaka huduma husika hujaza na kunakili maelezo ya Control Number katika kukamilisha taarifa na kutoa idhini ya kufanyika hamisho la kiwango husika kwenda katika Akaunti za Kamisheni ya Utalii. Kutokana na changamoto hii mawasiliano baina ya Mfumo wa Zan-Malipo na Mfumo wa Benki husika hukosekana na kupelekea Benki kuwa na taarifa ya fedha kamili zilizopokelewa na kwa upande wa mfumo wa Zan-Malipo kuwa na taarifa pungufu katika kumbu kumbu zake. Kamisheni inasimamia makusanyo yake kwa kupitia mfumo wa Zan-Malipo na kwamba hakuna mtaka huduma wa Kamisheni ambae anaeweza kufanya malipo bila ya kupatiwa Control number husika kutoka Kamisheni ya Utalii. Kamisheni imepanga kufanya mazungumzo baina ya Benki husika na uongozi unaosimamia mfumo wa ZanMalipo ili kutatua changamoto hii. Hata hivyo changamoto hii itaendelea kujitokeza kutokana na mapungufu yaliyopo katika mfumo wa ZanMalipo na Bank.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kwamba kuna baadhi ya wateja wa Kamisheni huwa wanafanya malipo kupitia mtandao (internet) moja kwa moja kutoka huko walipo katika nchi zao. Malipo hayo hufanyika kwa kutumia hesabu ya Benki (account number) ya Benki ya Watu wa Zanzibar na sio kutumia ‘control number’ inaytotolewa na mfumo wa ZanMalipo. Hali hiyo hupelekea tofauti ya fedha zilizopo benki ukilinganisha na miamala iliyopitia katika mfumo wa ZanMalipo.

Aidha, Kamati imebaini kwamba suala hili ni endelevu ambapo linategemewa kujitokeza hoja kwa mara nyengine kwasababu Wateja wengine hawaelewi kama malipo yanatakiwa yafanyike kwa mfumo wa ZanMalipo.

Kamati imebahatika kuoneshwa miamala kadhaa iliyofanywa kupitia mitandao kwenda Benki ya Watu wa Zanzibar na kuridhika nayo. Hata hivyo, kuna haja ya Wakaguzi kukaa pamoja na Watendaji kuona namna ya kuitatua kasoro hii. Hivyo, hoja inabakia kwa hatua za utekelezaji.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inautaka uongozi wa Kamisheni ya Utalii kuhifadhi vielelezo vyote vya malipo yanayofanyika kwa njia ya mtandao na kumpatia Mkaguzi wakati anapotekeleza majukumu yake.

Hoja nambari 5.8.2.3: Kutokuingizwa kwa makusanyo yatokanayo na Tamasha la ZTITE katika Taarifa za Hesabu za Mwisho wa Mwaka U$D 3,465

Kwa mujibu wa muongozo nambari 2 wa mwaka 2022/2023 wenye kumbukumbu nambari ACGEN/BC.195/393/01/01 wa tarehe 13/06/2023 kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango unaohusiana na zoezi la kufunga hesabu la mwaka wa fedha 2022/2023 ikisisitiza ufungaji wa hesabu uzingatie muongozo uliotolewa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 wenye kumbukumbu nambari AD.5/184/01/08/90 uliotolewa na (OR) Fedha na Mipango Zanzibar tarehe 9/6/2022 unaeleza kwamba taarifa zote za mapato yatokanayo na vyanzo mbalimbali ziingizwe katika Taarifa za Hesabu ya Mwisho wa Mwaka (Financial Statement)".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kamisheni ya Utalii ilikusanya jumla ya USD 3,465 zinzotokana na Tamasha la Utalii la ZITITE. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokuainishwa kwa mapato hayo pamoja na matumizi yake katika Taarifa za Hesabu za Kamisheni jambo ambalo linapelekeaTaarifa za Hesabu zilizowasilishwa kutokuonyesha Sura halisi na sahihi, aidhani kwenda kinyume na muongozo niliounakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni kuhakikisha unasimamia utaratibu unaohusiana na ukusanyaji wa mapato, ufungaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka pamoja na utayarishaji wa usuluhishi wa kibenki ili kuweza kubaini tofauti ya mapato na kufanya marekebisho katika Hesabu za Mwisho wa Mwaka.

Majibu ya Uongozi wa Kamisheni

Ni kweli Kamisheni ya Utalii haikuingiza makusanyo ya tamasha la ZTITE ilipopeleka hesabu za mwisho wa mwaka 2022-2023. Kwa sasa tayari mapato hayo yameshaingizwa katika kitabu cha mwisho wa mwaka 2022-2023 katika kipengele cha "disclosure note" kwa kurudia barua kumbukumbu namba HA.5/26/01 ya tarehe 17/01/2024 ripoti imewasilishwa kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali. Kivuli cha barua hiyo kimeambatanishwa.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika uchunguzi wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa ni kweli wakati wa Ukaguzi kulikuwa na kasoro hiyo. Hali hiyo ilijitokeza kutokana na Kamisheni kupata Mfadhili wa Tamasha ambae alitaka kuingiza fedha

kwako lakini Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango iliwaelekeza kwamba kiutaratibu fedha hizo zinatakiwa kupitia Hazina kwanza kabla ya kufika Kamisheni. Hivyo, Kamisheni hawakulazimika kuzionesha katika hesabu yao ya mwisho wa mwaka fedha hizo badala yake kuziwekea 'disclusure note'. Kamati imepitia Hesabu ya Mwisho wa Mwaka na kugundua kufanyika kwa marekebisho hayo. Kwa msingi huo, hoja hii imeondolea.

Hoja nambari 5.8.2.4: Kutoonekana kwa maeneo halisi ya miradi 10 ambayo imepata lesseni kutoka Kamisheni ya Utalii

Ukaguzi ulikaguwa majalada ya miradi arobaini na tisa (49) kati ya majalada mia saba na kumi (710) ya miradi iliyopewa leseni na Kamisheni ya Utalii, baada ya kutembelea maeneo iliyopo miradi hiyo ukaguzi umebaini kwamba kati ya miradi hiyo 49 uliyoitembelea miradi kumi (10) haikuonekana kwa ajili ya ukaguzi ili kuweza kujiridhisha na uwepo wa miradi hiyo.

Kutoa leseni kwa miradi ambayo haipo katika maeneo husika ni matumizi mabaya ya rasilimali za Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii kuhakikisha kwamba ukaguzi wa awali unafanyika katika maeneo ya mradi kabla ya utoaji wa leseni haujafanyika ili kuweza kujiridhisha na maeneo sahihi yaliopo miradi hiyo. Miradi yenyewe ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 79: Miradi ambayo haijaoonekana katika maeneo yake

Namba	Jina la mradi	Eneo ulipo
1.	Cinnamon Hotel Lited (Marafiki Bungalows (***)	Kiwengwa
2.	Shelly Bungallows (A)	Bwejuu
3.	Nakupenda Stone town (*)	Hurumzi
4.	PPBD Work's Limited (AA)	Bwejuu
5.	Fesste Company Limited (Bondeni Beach House (*)	Jambiani
6.	Zawadi House (APP)	Jambiani
7.	K – Consaltant	Mjini
8.	Grass Root Travel Ltd	Kiembesamaki
9.	G. P Selena (*)	Forodhani
10.	Arco Zanzibar Ltd (*)	Kiembesamaki

Majibu ya Uongozi wa Kamisheni

Ni kweli wakati wa ukaguzi Miradi hiyo haikuonekana katika maeneo yake halisi kutokana na kubadilishwa majina, kuhama na kufunga ofisi bila ya kutoa taarifa rasmi Kamisheni ya Utalii. Hata hivyo maofisa wa Kamisheni na Wakaguzi wa nje waliweza kufika katika 6 lesseni kutoka Kamisheni ya Utalii katika maeneo ya mradi kabla ya utoaji wa leseni haujafanyika ili

kuweza kujiridhisha na maeneo sahihi yaliopo miradi hiyo. maeneo hayo na kujiridhisha uwepo wake.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, Kamati ya PAC imegundua mambo yafuatayo:

1. Kuna baadhi ya Wateja wa Kamisheni ya Utalii ambao hufanya marekebisho ya majina ya Kampuni bila ya kufika au kuieleza Kamisheni;
2. Kuna baadhi ya Wateja hufanya marekebisho ya eneo lao la Kampuni bila ya kufika au kuieleza Kamisheni; na
3. Kuwepo usimamizi na ufuatiliaji mdogo kwa Wateja wanaobadilisha eneo au majina ya Kampuni zao. Hili limebainika kwa kutathimni utendaji kazi wa Kamisheni katika utekelezaji wa mabadilko ya Kampuni yanayofanywa na Wateja wao kwani haiwezekani hayo yatokee hasa ukizingatia kwamba Kamisheni ndio Taasisi inayoshughulikia mabadiliko ya majina au eneo la Kampuni (ni lazima anayefanya mabadiliko aende Kamisheni).
4. Kuwepo kwa mashirikiano madogo baina ya Mkaguzi na Wakaguliwa. Hili limebainika kwa kuzingatia kwamba kuna baadhi ya Hoteli zinaendelea kufanya kazi lakini zimeainishwa kwamba zimebadilisha majina zikiwemo Cinnamon Hotel Limited (Marafiki Bungalows na Nakupenda Stone town

Maagizo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Kamisheni ya Utalii uhaskikishe unafuatilia kwa karibu hoteli zote zinazofanya marekebisho ya majina yao au kuhama eneo lililokuwemo katika usajili.

Uongozi wa Kamisheni ya Utalii uhakikishe unawapatia adhabu na ikiwezekana kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria wote watakaobainika kushindwa kuwasilisha taarifa za kubadilisha eneo la kazi Kamisheni.

Hoja nambari 5.8.2.5: Dosari katika uazishwaji wa kikosi cha Polisi Utalii pamoja na matumizi yaliyofanyika shilling 181,691,420

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kamisheni ya Utalii imefanya matumizi ya jumla ya shilingi 181,691,420 kwa ajili ya kuwalipa maposho Kikosi cha Police Utalii kwa ajili ya kusaidia kuimarisha ulinzi na usalama wa wageni (watalii). Katika kupitia kumbu kumbu zinahusiana na ulipwaji wa fedha hizo ukaguzi umebaini uwepo wa dosari zifuatavyo:-

- Kukosekana kwa nyaraka za maandishi ya kupata Baraka ya uanzishwajiwa Kikosi cha Police Utalii.

- Kukosekana kwa barua kutoka katika Taasisi zilizotoa watendaji waokwa ajili ya kuunda kikosi cha Police Utalii.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kukosekana kwa uhalali wa malipo yaliyofanyika sambamba na uwepo viashiria vya ubadhirifu wa fedha za Umma.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Kamisheni kuhakikisha unasimamia na kutekeleza matakwa ya kisheria juu ya uwekwaji wa kumbukumbu za Uanzishwaji wa Kikosi cha Polisi Utalii ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo yanayofanyika kwa ajili ya kikosi hicho.

Majibu ya Uongozi wa Kamisheni

Ni kweli wakati wa ukaguzi zilikosekana nyaraka za maandishi ya kupata Baraka ya uanzishwaji wa Kikosi cha Polisi Utalii. Pia Kukosekana kwa barua kutoka katika Taasisi zilizotoa watendaji wao kwa ajili ya kuunda kikosi cha Polisi Utalii. Hii ni kutokana na Kikosi cha Polisi Utalii na Diplomasia kimeundwa kutokana na agizo la Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi tarehe 21/09/2021 ambapo tarehe 19/11/2021 kikosi hicho kilizinduliwa rasmi na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kikiwa na askari 150. Aidha nyaraka zote zinazohusiana na kikosi hicho zinapatikana Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kwamba ni kweli wakati wa ukaguzi hakukuwa na kielelezo (nyaraka) cha uanzishwaji wa Kikosi cha Polisi Utalii. Hili lilitokana na kwamba mara baada ya Rais kutoa taarifa ya uhitaji wa kuwepo kwa chombo hicho, Taasisi husika zililazimika kuchukua hatua ipasavyo za uanzishwaji wake. Hata hivyo, hivi sasa nyaraka hiyo (legal notice) ipo na Kamati kufanya maamuzi ya kiondoa hoja hii.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Kamisheni ya Utalii uhakikishe unafuatilia kwa haraka sehemu husika nyaraka za uanzishwaji wa Vyombo kama hivyo mara tu baada ya kutolewa agizo la kuanzishwa kwake ili kuepuka hoja kujitokeza.

Hoja nambari 5.8.2.6: Mapungufu katika Mpango wa Manunuzi wa Mwaka (Annual Procurement Plan)

Kwa mujibu wa kifungu nambari 29(e) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 linaelekezea juu ya kupanga mipango yaUnununzi na uondoshaji wa mali za umma za Taasisi ya Ununuzi na Uondoshajiwa Mali za Umma.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Kamisheni ya Utalii imeandaa Mpango wa Manunuzi kwa ajili ya matumizi ya mwaka wa Fedha 2022/2023. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokuingizwa fedha za Tamasha la ZITITE zenye jumla ya shilingi 133,110,038.18 katika Mpango wa Manunuzi wa Mwaka jambo ambalo linapelekea kufanya ununuzi wa bidhaa na huduma bila ya kuwa na mpangilio maalum, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii kuhakikisha taarifa zote za manunuzi yanayofanyika zinainishwa katika Mpango wa Manunuzi wa mwaka kwa mujibu ya sheria na miongozo iliyowekwa na Serikali.

Majibu ya Uongozi wa Kamisheni

Ushauri umepokelewa na umeshafanyiwa kazi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa wakati Mkaguzi anafika Kamisheni kutekeleza majukumu yake ni kweli kulikuwa hakuna Mpango wa Manunuzi wa Tamasha la ZITITE zenye jumla ya shilingi 133,110,038.18. hali hiyo ilitokana na kutokuwepo kwa bajeti ya Tamasha hilo tangu hatua za awali na kusababisha Watendaji wa Kamisheni kutokufanya mapitio ya Mpango wa Manunuzi walionao ili uendane na uhalisia wa matumizi wanayoyafanya. Kwa msingi huo, hoja hii inaendelea kubakia kwa hatua za utekelezaji ili kurthibitisha kama kweli katika kasoro hiyo haijirudii tena.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Kamati inaushauri Uongozi wa Kamisheni ya Utalii kuhakikisha wanafanya mapitio ya Mpango wao wa Manununuzi hususan wanapofanya matumizi yaliyopo nje ya bejeti zao.
2. Kamati inaushauri Uongozi wa Kamisheni ya Utalii uhakikishe taarifa zote za manunuzi yanayofanyika zinainishwa katika Mpango wa Manunuzi wa mwaka kwa mujibu ya sheria na miongozo iliyowekwa na Serikali

Hoja nambari 5.8.2.7: Malipo kwa watoa huduma ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 136,536,485. 62

Kifungu nambari 23(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba “kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi. Aidha kifungu namba 23(2) kinafafanua kuwa zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa nataasisi ya ununuzi”.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kamisheni ya Utalii Zanzibar limefanya malipo yenye jumla ya shilingi 136,536,485.62 kwa wafanyabiashara ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kama watoa huduma jambo ambalo ni kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na usajili huo, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kununua bidhaa au huduma kwa wafanyabiashara au watoa huduma waliosajiliwa na Mamlaka husika. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli namba 80 linahusika. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 80: Watoa huduma ambao hawakusajiliwa

Namba	**Hati namba**	**Aliyelipwa**	**Thamani (Shs)**	**Maelezo**
1.	J02Pv0358 ya 10/2/2023	Tea party Zanzibar	24,486,797	Malipo kwa ajili ya shughuli za Maonyesho ya ZITITE
2.	J02Pv0356 ya 9/2/2023		4,104,000	
3.	J02Pv0354 ya 9/2/2023		35,995,592.24	
4.	J02Pv0464 ya 17/3/2023		5,720,000	
5.	J02Pv0509 ya 25/03/2023	361 Degrees Africa Ltd	33,115,048.19	
6.	J02Pv0510 ya 25/3/2023		33,115,048.19	
Jumla			**136,536,485.62**	

Majibu ya Uongozi wa Kamisheni

Ni kweli watoa huduma walikuwa hawajasajiliwa wakati Kamisheni ilipokuwa inataka huduma kutoka kwao. Aidha Kamisheni ilifanya malipo kwa watowa huduma hao pale ambapo tayari wameshasajiliwa kama ifuatavyo: 361 Degree Afrika (SMS - Private) amesajiliwa BPRA kwa nambari Z0000183371 na ZPPDA kwa nambari NC001437 na Tea Party Zanzibar amesajiliwa BPRA kwa nambari Z0000118471 na Mamlaka ya Manunuzi ZPPDA kwa nambari NC001358. Kamisheni ipo tayari kwa ukaguzi. Naambatanisha na nyaraka za usajili wa watoa huduma hao.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya PAC imegundua kuwa wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake katika Kamisheni hii, ni kweli cheti cha usajili wa Kampuni zilizopewa kazi na Kamisheni hakuoneshwa Mkaguzi. Hata hivyo, Kamati ya PAC imekiona cheti cha Mamlaka ya Ununuzi na uondoshaji wa Mali za Umma cha Kampuni ya 361 Degree Afrika (SMS - Private) kilishosajili cha tarehe 17 Febuari, 2022 na kumaliza muda wake tarehe 17 Febuari, 2023 kilikuwepo. Kwa msingi huo, Kamati imeridhika na majibu ya hoja hii na kuiondosha.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inautaka uongozi wa Kamisheni kuongeza ushirikiano na Mkaguzi ili hoja za namna hii zisiweze kujitokeza katika Ripoti ya Mkaguzi.

Hoja nambari 5.8.2.8: Matumizi yaliyokiuka Taratibu za Manunuzi Shilingi 136,536,485. 62

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Kamisheni ya Utalii Zanzibar imefanya matumizi yenye jumla ya shilingi 136,536,485.62 kwa ajili ya kupatiwa huduma mbali mbali katika Tamasha la ZITITE. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokufuatwa kwa taratibu za manunuzi kama ifuatavyo:-

a) Kukosekana kwa ripoti ya tathmini kinyume na kifungu nambari 29(g) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.
b) Kutotangazwa kwa Zabuni kinyume na kifungu nambari 29(j) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.
c) Kukosekana kwa idadi ya Wazabuni walioomba zabuni kinyume na kifungu nambari 29(l) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.
d) Kupata taarifa ya ruhusa ya kutumia njia mbadala kama kifungu nambari 45 (3)(a) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.
e) Kutokujumuisha bajeti ya ununuzi na mipango ya ununuzi kinyume na kifungu nambari 42 (d) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.
f) Kugawa ununuzi wa bidhaa kwa lengo la kutokutumia utaratibu wa ununuzi kinyume na kifungu nambari 42 (c) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.
g) Kutoingizwa katika mpango wa Manunuzi kinyume na kifungu nambari 29(e) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016

h) Kushindwa kupatiwa taarifa za maandishi kabla ya kuanza manunuzikinyume na kifungu nambari 43(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzina Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.
i) Kukosekana kwa Baraka ya Mwanasheria Mkuu ya kuridhia Mkataba.
j) Kukosekana kwa hati za Madai ya Malipo kutoka kwa Mtoa huduma. Kufanya hivyo kunapelekea kuwepo kwa viashiria vya ubadhirifu wa fedha zaUmma unaosababishwa na uvunjwaji wa vifungu vya Sheria katika kufanya manunuzi ya Umma jambo ambalo linaweza kupelekea kuitia hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii kuhakikisha kwamba unasimamia na kutekeleza matakwa ya Sheria na miongozo iliyopo katika kufanya manunuzi ya bidhaa na huduma kwa ajili ya kuimarisha maendeleo. Mchanganuo wa matumizi yaliyofanyika bila kufuata utaratibu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 81: Malipo ambayo hayakufuata taratibu za manunuzi

Namba	Hati namba	Aliyelipwa	Thamani (Shs)	Maelezo
1.	J02Pv0358 ya 10/2/2023	Tea party Zanzibar	24,486,797	Malipo kwa ajili ya shughuli za Maonyesho yaZITITE
2.	J02Pv0356 ya 9/2/2023		4,104,000	
3.	J02Pv0354 ya 9/2/2023		35,995,592.24	
4.	J02Pv0464 ya 17/3/2023		5,720,000	
5.	J02Pv0509 ya 25/03/2023	361 Degrees AfricaLtd	33,115,048.19	
6.	J02Pv0510 ya 25/3/2023		33,115,048.19	
Jumla			**136,536,485.62**	

Majibu ya Uongozi wa Kamisheni

Ni kweli Kamisheni ya Utalii ilikiuka taratibu za manunuzi hii ni kutokana na mabadiliko ya uongozi kwa kipindi hicho ambapo kulikuwa hakuna Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni na Wajumbe pia walikuwa pungufu. Aidha, Kamisheni ya Utalii ilipeleka muundo wa Bodi ya Zabuni mnamo tarehe 24/10/2023 kwa barua yenye kumbukumbu nambari IA.212/235/07. Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma iliridhia muundo huo tarehe 27/10/2023 kwa barua yenye kumbukumbu nambari E.A 26/177/01/205. naambatanisha na vivuli vya barua hizo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kiujumla, Kamati ya PAC imegundua kuwa mchakato mzima wa ufanyikaji wa Tamasha la ZITITE tangu hatua za awali haukufuata taratibu na ulikosa usimamizi mzuri unaoendana na utekelezaji wake kwa mujibu wa Sheria na Miongozo iliyopo hasa ukizingatia shughuli hiyo haikuwemo katika bajeti ya msingi ya Kamisheni. Kwa mnasaba huo, yale yote ambayo Mkaguzi ameyaeleza katika hoja hii ni kweli yalijitokeza. Hivyo, hoja hii inaendelea kubakia kwa hatua za utekelezaji katika shughuli nyengine ili Mkaguzi aweze kujiridhisha kwamba kasoro kama hizo hazijitokezi tena kwa Kamisheni.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inautaka Uongozi wa Kamisheni ya Utalii kuhakikisha kwamba Matamasha yanafanywa yanatekelezwa kwa kufuata Sheria na mongozo iliyopo ili kuepukana na kujitokeza kasoro katika utekelezaji wake.

Hoja nambari 5.8.2.9: Kukosekana kwa nyaraka za makubaliano ya kuwasafirisha wageni kutoka Arusha shilingi 6,814,800

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Kamisheni ya Utalii Zanzibar imefanya malipo yenye jumla ya shilingi 6,814,800 kupitia hati namba J02Pv0509 kwa ajili ya kuwasafirisha wageni 19 kutoka Arusha kuja Zanzibar kwa lengo la kushiriki katika Tamasha la ZITITE.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa nyaraka ya makubaliano ya kuwasafirisha wageni hao kutoka Arusha kuja Zanzibar ikiwemo hati ya makubaliano yenye kuonyesha muhusika mwenye jukumu la kuwasafirisha wageni pamoja na Barua ya mualiko jambo ambalo linapelekea kutokuthibitikakwa uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa viashiria vya ubadhirifu wa fedha za umma, aidha ni kwenda kinyume na kanuni nambari 57(1)(2)(b) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar kuhakikisha unaandaa na kuweka kumbukumbu zote za matumizi yaliyofanyika kama kanuni inavyoelekeza.

Majibu ya Uongozi wa Kamisheni

Kamisheni ya Utalii iliomba udhamini kutoka kwa Shirika la Ndege la Air Tanzania (ATC) lakini siku moja kabla ya kuwasili wageni, mhusika wa ATC alienda likizo na kutokupatikana kwa simu. Hali hii ilipelekea Uongozi wa Kamisheni ya Utalii kutafuta njia mbadala ya kuwafikisha wageni hao Zanzibar bila kuharibu ratiba ya Tamasha la ZTITE. Nakala ya email ya maongezi baina ya Kamisheni na Air Tanzania ATC inaambatanishwa.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya juhudi ambazo Kamisheni ya Utalii ilichukua katika kuhami mazingira yaliyojitokeza, Kamati ya PAC imegundua kuwa hakukuwa na mawasiliano y kiutendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar na Kampuni ya ATC hasa ukizingatia Sheria ya Utumishi wa Umma, Nambari 2 ya 2011 inaelekeza kwamba mawasiliano ya Taasisi au Ofisi ya Umma yafanywe kwa maandishi kupitia Mkuu wa Taasisi. Kilichoonekana kufanyika ni kama mazungumzo ya mtu na mtu na sio mazungumzo rasmi ya kiofisi jambo lililopelekea kutaka kutokea maharibiko katika Tamasha lililopangwa.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Kamisheni ya Utalii uhakikishe unapofanya mawasiliano yaliyo rasmi hususan wanapohitaji huduma kutoka nje ya Ofisi yao ili hata kama kutajitokeza changamoto iwe rahisi kufuatilia na kuchukua hatua stahiki haraka iwezeanavyo.

Hoja nambari 5.8.2.10: Fedha zilizotumika bila ya kuidhinishwa katika Mpango kazi wa Mwaka shilingi 247,706,500

Kifungu nambari 41(2)(c) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaelezea kuwa “Taasisi zinazohusika na bajeti ya Serikali zitawasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali bajeti zao za mwaka na zitajumuishampango kazi na mpango wa manunuzi”.

Katika kufanikisha shughuli za maonyesho ya Utalii na Uwekezaji zilizofanyikakatika mwaka wa fedha 2022/2023 Kamisheni ya Utalii ilitumia jumla ya shilingi 247,706,500 kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya maonyesho hayo.

Ukaguzi ulipitia kumbukumbu na nyaraka mbali mbali pamoja na mpango kazi wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar na kubaini kuwa fedha zilizotumika kwa ajili ya maonyesho hayo hazikuingizwa katika mpango kazi wa Kamisheni wa mwaka na kuwasilishwa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali jambo ambalo linaonyesha kutekelezwa kwa shughuli ambazo hazikupangwa katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kutokutekelezeka kwa shuguli zilizopangwakatika mpango kazi kutokana na kutumika kwa fedha hizo kwa ajili ya maonyesho ya Utalii na Uwekezaji na hatimae kupelekea kutokufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar kuhakikisha unasimamia matumizi yote ya fedha za Umma ili kuhakikisha yanafanywa kulingana na mpango kazi wa mwaka kwa lengo la kuepuka kutumika kwa fedha kinyume na mipango ya Kamisheni iliyowekwa.

Majibu ya Uongozi wa Kamisheni

Ni kweli fedha zilitumika bila ya kuidhinishwa katika Mpango kazi wa Mwaka. Aidha Ushauri umepokelewa na utafanyiwa kazi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Uongozi wa Kamisheni kukiri kujitokeza kwa hoja, Kamati ya PAC imebaini kuwa kati ya hizo shilingi 247,706,500, kulikuwa na shilingi milioni 200 zilizokuwa zimepangwa kutumika kwa ajili ya kufanikisha shughuli za Tamasha la ZITITE na shilingi 247,706,500 zilikuwa ni kwa ajili ya uandaaji wa Kanuni ambazo zilikuwa zikijadiliwa katika ngazi tofauti. Hata hivyo, Watendaji wa Kamisheni walifanya matumizi ya fedha hizo bila ya kuhakikisha kwanza wanafanya mapitio ya Mpango Kazi wao hasa ukizingatia fedha hizo zilikuwa hazimo katika bajeti yao ya awali. Kwa msingi huo, hoja hii inabakia kwa hatua za utekelezaji.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inautaka Uongozi wa Kamisheni kuhakikisha unafanya mapitio ya Mpango Kazi wao kabla kufanya matumizi ya fedha kama zinavyoelekeza Sheria za fedha.

Hoja nambari 5.8.2.11: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu shilingi 27,570,000

Kanuni ya 58(1) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaelezakwamba malipo yote ya matumizi ya Taasisi za Kibajeti na Serikali za Mitaa lazima yafanywe kwa kutumia njia za kielektroniki.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kamisheni ya Utalii Zanzibar imefanya malipo yenye jumla ya shilingi 27,570,000 kwa njia ya fedha taslimu jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa viashiria vya matumizi mabayaya fedha za umma, aidha ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar kuhakikisha unafuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kufanya malipo kupitia benki. Mchanganuo wa malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu ni kama inavyoonekana katika jadweli namba 82. Mchanganuo wa malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu ni kamainavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 82: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu

Namba	Hati Namba	Aliyelipwa	Thamani (Tshs)	Maelezo
1.	PV 16/04	Pili Juma	4,900,000	
2.	PV 02/6 ya		1,700,000	

	02/06/2023	Suleiman		Malipo ya posho mbali mbali
3.	PV 02/6 ya 07/06/2023		4,680,000	
4.	PV 03/6 ya 12/06/2023	Amina Alawi Yussuf	3,710,000	
5.	PV 04/6 ya 12/6/2023	Pili Juma Suleiman	5,020,000	
6.	PV 04/6 ya 06/06/2023		4,680,000	
7.	PV 06/6 ya 17/06/2023		2,880,000	
Jumla			**27,570,000**	

Majibu ya Uongozi wa Kamisheni

Ni kweli Kamisheni ya Utalii imefanya malipo kwa njia ya fedha taslimu Tsh. 27,570,000 katika vocha mbali mbali kama inavyojionesha katika jadweli Nambari 82. Kwa mujibu wa barua ya tarehe 06/02/2023 yenye kumbukumbu namba DC.184/199/01/05/1031 ya muongozo kutoka Afisi ya Rais Fedha na Mipango inayotupa ruhusa ya kufanya malipo ya cash hadi milioni 15. Mchanganuo wa malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu ni kama inavyoonekana katika jadweli namba 82. jumla ya Tsh. Million Kumi na Tano kwa kila mwezi, hivyo kutokana na barua hiyo Vocha ya 16/4 yenye thamani ya Tsh. 4,900,000 itakuwa imefuata muongozo uliotolewa wa matumizi ya fedha taslimu.

Aidha vocha za mwezi wa sita PV 02/6 ya tarehe 07/06/23 yenye thamani ya Tsh. 4,680,000 PV 03/6 ya tarehe 12/6/2023 yenye thamani ya Tsh. 3,710,000 PV 04/6 ya tarehe12/06/2023 yenye thamani ya Tsh. 5,020,000 PV 06/6 ya tarehe 17/06/2023 yenye thamani ya Tsh. 2,880,000. Vocha hizi zina jumla ya Tsh 16,410,000 na hazipo katika uhalisia. Hata hivyo uhalisia wa vocha za mwezi wa sita zilizoainishwa katika jadweli 82 ni kama ifuatavyo: Hivyo Kamisheni pia imefuata muongozo uliotolewa wa matumizi ya fedha taslimu.

PV aliyelipwa Kiasi 2/6 ya tarehe 6/6/23 Pili Juma 1,700,000 3/6 ya tarehe 6/6/23 Pili Juma 6,090,000 4/6 ya tarehe 6/6/23 Pili Juma 4,680,000 6/6 ya tarehe 8/6/23 Asha Haji 850,000 Jumla 13,320,000 11 Naambatanisha na vocha husika pamoja na muongozo wa Afisi ya Rais, Fedha na Mipango wa tarehe 06/02/2023 kumbukumbu nambari DC.184/199/01/05/1031.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kuchunguza hoja hii, Kamati ya PAC iligundua yafuatayo:

1. Fedha ambazo Mkaguzi amezionesha ni fedha ambazo zililipwa kwa Pili Juma (Mshika Fedha) na Amina Alawi Yussuf (Msaidizi Mhasibu) zilikuwa ni kwa ajili ya kuwalipa Wadau walioshiriki katika mchakato

wa uandaaji wa Kanuni ya Kamaisheni wakiwemo Masheha zaidi ya 100 ambao hawakuwemo katika mfumo wa malipo.

2. Ni kweli kuna muongozo wa matumizi uliotolewa na Afisi ya Rais, Fedha na Mipango ulioitaka Kamisheni kutumia si zaidi ya milioni 15 kwa mwezi lakini kwa mujibu wa vocha zilizopo imeonekana Kamisheni imetumia jumla ya shilingi 17,260,000 kinyume na muongozo huo.
3. Ni kweli kulikuwa na vocha ziliwekwa kimakosa na Mkaguzi kwani zilikuwa zikijrudia na kufanya shilingi 27,570,000.
4. Matumizi hayo yalitokea katika kipindi cha mwisho wa kufunga hesabu ya mwaka.

Kwa msingi huo, hata kama Kamaisheni ilipaswa kutumia kwa fedha taslim ilitakiwa kufuata muongozo uliopo na sio kuukiuka. Hoja inabakia kwa hatua za utekelezaji wa baadae.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Kamisheni uhakikishe unafanya matumizi yake kwa kufuata sheria na miongozo iliyopo ili kujiepusha na hoja za Mkaguzi.

Hoja nambari 5.8.2.12: Kutelekezwa kwa majengo ya Mradi wa Bi Khole yaliyogharimu shilingi 1,791,715,81 5.36

Kifungu nambari 61(2) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinawata maafisa masuuli kuhakikisha kwamba mali za Umma zinatumika kwa tija na manufaa kulingana na jukumulitakalo tekelezwa.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 1,791,715,815.36zilitumika kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya mradi wa Utalii kwa wote (Bi Khole) ambao ulitekelezwa kwa kipindi cha Aprili, 2019 hadi 2022 katika maeneo yaBungi.

Pamoja na ujenzi uliofanyika ambao umegharimu fedha nyingi za Serikali, ukaguzi umebaini kutokuanza kutumika kwa mradi huo jambo ambalo huwenda likapelekea kutukufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa na hatimae kukosekana kwa tija pamoja na kuingizia hasara Serikali kutokana na gharama kubwa ya fedha za ujenzi zilizotumika.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba Kamisheni ya Utalii Zanzibar inaendelea kutumia fedha za ziada kwa ajili ya kuwalipa walinzi pamoja na watunza Bustani katika maeneyo ya majengo hayo ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Kamisheni imelipa jumla ya shilingi 28,380,000 jambo ambalo ni kuiongezea Serikali gharama bila ya kufikiwa kwa mafanikio yaliokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar kuhakikisha jitihada za makusudi zinachukuliwa ili kuendana na uhalisia wa thamani ya fedha iliyotumika na tija itakayopatikana kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali, vyenginevyo kama hali itaendelea kama ilivyo sasa kuna uwezekano mkubwa wa majengo hayo kuchakaa kabla ya gharama zilizotumika kuweza kurejeshwa kupitia mapato yaliyotarajiwa kupatikanwa katika maeneo hayo

Majibu ya Uongozi wa Kamisheni

Ni kweli jumla ya shilingi 1,791,715,815.36 zilitumika kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya mradi wa Utalii kwa wote (Bi Khole) na kutoanza kutumika kwa mradi huo ni jambo ambalo huwenda likapelekea kutokufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa. Hata hivyo Kamisheni ya Utalii imefanya jitihada ya kutafuta Mwekezaji wa eneo hilo ambae ni Halmashauri ya Wilaya ya Kati (U). Kwa sasa wapo katika hatua ya kusaini mkataba baina ya Kamisheni na Halmashauri ya Wilaya ya Kati (U).

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya mpango uliopo kwa Kamisheni ya Utalii wa kuingia Mktaba wa Uwekezaji wa eneo la kwa Bi Khole, Kamati imependekeza kwamba ni busara uwekezaji huo ungefanywa na Kamisheni yenyewe hasa ukizingatia kwamba wao ndio wenye upeo mkubwa wa kuyatangaza maeneo ya Utalii Zanzibar. Aidha, kuliendeleza eneo hilo kwa shughuli za utalii kutaleta tija zaidi kwa Kamisheni. Kwa vile Mkataba walioingia na Halmashauri ya Wilaya ya Kati ni wa mwaka mmoja, utkapomaliza Kamisheni wafanye utaratibu wa kulichukua eneo hilo na kulendeleza kwa shughuli za utalii kwa maslahi ya Zanzibar.

Aidha, Kamati imebaini kwamba Miradi mikubwa kama huu unapotekelezwa, kufanyike upembuzi yakinifu ili kuweza kutathmini mapema faida na changamoto na jinsi gani zitaweza kutatuliwa. Hoja hii imebakia kwa hatua za utekelezaji.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Kamati inautaka Uongozi wa Kamisheni ya Utalii kuhakikisha unafanya upembuzi yakinifu kabla ya kutekeleza Miradi yake.
2. Uongozi wa Kamisheni kwa kushirikiana na Wizara ya Utalii na mambo ya kale uchukue juhudi za makusudi kuhakikisha mkataba uliopo ukimalizika unalichukua eneo hilo na kuliendeleza kwa shughuli za utalii.

Hoja nambari 5.8.2.13: Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia Mfumo wa kielektroniki (e-Proz) shilingi 38,835,048

Kwa mujibu wa barua kutoka Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar la tarehe 12/08/2022 lenye kumbukumbu nambari MUUMU. BA.156/370/01/27 inazitaka taasisi zote za Serikali kufanya manunuzi kupitiamfumo wa e-proz kuanzia tarehe 15/08/2022.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kamisheni ya Utalii Zanzibar imefanya manunuzi yenye thamani ya shilingi 38,835,048 kwa wafanyabiashara mbali mbali bila ya kutumia mfumo wa kielektroniki ujulikanao kama e-Proz, jambo ambalo linaweza kupelekea kununua bidhaa zenye viwango duni na hatimae kuitia hasara Serikali, aidha ni kwenda kinyume na muongozo niliounakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar kuhakikisha kwamba manunuzi yote yanayofanyika yafuate utaratibu wa kutumia mfumo wa Manunuzi kwa mujibu wa Toleo la Barua hiyo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 83: Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa e-Proz

Namba	Hati Namba	Hundi Namba	Aliyelipwa	Thamani (Tshs)	Maelezo
1.	J02PV0509 ya 25/3/2023	TISS	361 Degrees AfricaLtd	33,115,048	Fedha kwa ajili ya maonesho ya ZITITE
2.	J02PV0464 ya 17/3/2023		Tea Party Zanzibar	5,720,000	
Jumla				**38,835,048**	

Majibu ya Uongozi wa Kamisheni

Ni kweli Kamisheni ilifanya manunuzi bila ya kutumia mfumo huo. Hii ni kwa sababu matumizi yalikuwa ya haraka na kwa kipindi hicho wakati mtandao wa mfumo ulikuwa unasumbua kupatikana kutokana na upya wake. Sambamba na hayo Kamisheni imechukua ushauri na kuufanyia kazi katika mwaka wa fedha ujao. Na kwa sasa manunuzi yote yanafanyika kwa kutumia mfumo

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Uongozi wa Kamisheni kukiri uwepo wa dosari ya kutotumia Mfumo wa kielektroniki (e - Proz) shilingi 38,835,048. Hata hivyo, Kamati ya PAC imebaini mambo yafuatayo:

1. Uongozi wa Kamisheni ya Utalii uliamua kufanya matumizi hayo kwa

njia taslim ili kuhami mazingira yaliyojitokeza ya kuandaa Tamasha la ZITITE.

2. Kulikuwa hakuna ushindani uliofanyika katika kazi hiyo.
3. Maumbile ya huduma zilizokuwa zinahitajika zilikuwa hamna Kampuni yenye kutoa huduma hizo ambazo zimesajiliwa kwenye Mfumo wa e – Proz. Huduma zenyewe zilikuwa kuwatafuta 'exbitors' na pamoja na mtu wa kufanya ujenzi wa mabanda.
4. Uongozi wa Kamisheni ya Utalii haikuomba ruhusa ya matumizi nje ya Mfumo kwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Kwa mazingira hayo, Kamati imeibakisha hoja hii kwa hatua za utekelezaji wake.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Uongozi wa Kamisheni ya Utalii uhakikishe unafanya manunuzi kwa kutumia Mfumo wa Kielektroniki.
2. Kamati inautaka Uongozi wa Kamisheni ya Utalii kufuatilia Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma iwapo kutatokea jambo lenye mahitaji ya kufanyika manunuzi nje ya Mfumo ili kuepusha hoja za Mkaguzi.

KAMISHENI YA UTALII - PEMBA

Hoja nambari 5.8.2.14: Mtumishi anaekaimu nafasi kinyume na utaratibu

Kwa mujibu wa kanuni nambari 20(6) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya 2014 inaeleza kwamba "kwa kuzingatia masharti ya kifungu hiki hakuna nafasi ya kukaimu zaidi ya muda wa miezi kumi na mbili (12) mfululizo kutoka tarehe ya uteuzi wa kukaimu isipokuwa muhusika atathibitishwa katika wadhifa huo au mwenye dhamana atakaporejea."

Ukaguzi umebaini kwamba kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu nambariAC.161/383/01/70 ya tarehe 22/07/2019 kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar inaelezea kuhusu kupewa Mtumishi jukumu la kukaimu kwa nafasi ya Uratibu katika Kamisheni ya Utalii Pemba, lakini hadi ukaguzi huu unakamilika bado Mtumishi huyo anaendelea kukaimu nafasi hiyoambapo ni kipindi cha zaidi ya miaka minne (4) tangu kukaimishwa kwake.

Kufanya hivyo kunapelekea mtumishi huyo kukosa moyo wa kuitendea haki nafasi hiyo kwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi uliokusudiwa, aidha nikwenda kinyume na kanuni iliyonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha mtumishi huyo anathibitishwa au anateuliwa mtumishi mwengine mwenye sifa toshelevu za kushika nafasi hiyo.

Majibu ya Uongozi wa Kamisheni

Ushauri umepokelewa na umeshaanza kufanyiwa kazi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa ni kweli kuna mfanyakazi ambae amekaimu nafasi ya Mratibu wa Kamisheni ya Utalii Pemba lakini kwa muda wa miaka minne hakuweza kuthibitishwa kwenye nafasi hiyo kwasababu alikuwa hana sifa za kuweza kuthibitishwa. Kamati ilitaka kujua kwa kipindi chote ambacho Mfanyakazi huyo alikuwa anakaimu maslahi yake amepatiwa na kuelezwa kwamba kwa mujibu wa Sheria za Utumishi anastahiki kulipwa maslahi ya mwaka mmoja ambao tayari ameshapatiwa.

Katika kulitafutia ufumbuzi suala hilo, Manao tarehe 01/10/2024 Bodi ya Kamisheni ya Utalii imeiandikia barua Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa barua yenye kumbukumbu nambari KA.36/306/01 kupendekeza majina ya Wafanyakazi watatu wenye sifa ambao wanaweza kuteuliwa kushika nafasi hiyo.

Kwasasa Mfanyakazi huyo anaendelea kutumikia nafasi hiyo hadi Kamati inakamilisha uchunguzi wake katika Taasisi hiyo bado alikuwa hajaondolewa. Hata hivyo, Kamisheni kupitia maelekezo kutoka Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Kamati imeelezwa kwamba kwa vile Mtumishi huyo katika muda wake wote aliokaimu alikuwa hana sifa, hivyo hastahiki kulipwa maslahi yoyote kitu ambacho Kamati ilishindwa kukikubali na kueleza kwamba kwa vile Mtumishi huyo ametumikia bila ya kuwepo kasoro yoyote, Kamisheni inawajibu wa kuhakikisha maslahi yake yanalipwa. Kwa msingi huu, Kamati haikuridhishwa na majibu yaliyotolewa na uongozi wa Kamisheni na kuibakisha hoja hii kwa hatua za utekelezaji.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inautaka Uongozi wa Kamisheni ya Utalii kutafuta njia mbadala kuhakikisha Mfanyakazi aliyekuwa anakaimu anapatiwa maslahi yake hasa ukizingatia uzembe wa kuendelea kumwacha akaimu ulifanywa na Ofisi na sio kwa matakwa yake mwenyewe.

UCHUNGUZI WA KAMATI YA PAC KUHUSU UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023

MRADI WA MAENDELEO WA ZESTA

Hoja nambari 4.1.1.1: fedha za mradi ambazo hazikutolewa USD 2,401,605.98

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23 Mradi wa ZESTA ulipanga kutumia kiasi cha USD 3,079,147 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 kiasi cha USD 677,541.02 zilikuwa zimepokelewa sawa na asilimia 22 na kupelekea USD 2,401,605.98 sawa na asilimia 78 ya fedha zilizoidhinishwa katika bajeti kutopokelewa.

Shughuli za mradi zenye jumla ya USD 2,401,605.98 zilizopangwa hazikufanyika na hivyo kusababisha malengo yaliyopangwa kutotekelezwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mradi wa ZESTA kuhakikisha unafanya ufuatiliaji ili kuhakikisha kuwa fedha zilizoidhinishwa kwenye bajeti zinatolewa. Pia, uongozi wa Mradi unashauriwa kuweka vipaumbele katika utekelezaji wa shughuli za mradi. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 18: Fedha za mradi ambazo hazikutolewa

Nam	Maelezo	Bajeti iliyoidhinishwa(USD)	Kiasi kilichotumika(USD)	Kiasi kisichotolewa(USD)
1.	Msaada wa kiufundi na msaada wa utekelezaji wa mradi	2,149,147	620,301.35	1,528,845.65
2.	Uboreshaji wa ufanisiwa nishati	860,000	0	860,000
3.	Kuondoa Tofauti ya Jinsia katika sekta yanishati	70,000	57,239.67	12,760.33
Jumla		**3,079,147**	**677,541.02**	**2,401,605.98**

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Kuchelewa utekelezai wa Shughuli za mradi zenye jumla ya USD 2,401,605.98 kulisababishwa kwa kubadilishwa kwa watendaji wa kada ya manunuzi na kuchangiwa zaidi kwa hatua za upatikanaji wa ridhaa (No

objection) kutoka Benki ya Dunia juu ya shughuli zilizopangwa za manunuzi

Hata hivyo, Uongozi wa mradi wa ZESTA unaendelea kufuatilia kwa karibu shughuli zote zilizopangwa ili kuongeza ufanisi na ufikiwaji wa malengo yalowekwa, hivyo, changamoto hiyo kwa sasa haipo na hatua zote za manunuzi zimekamilika kwa kuanza utekelezaji wa mikataba ambapo baaadhi ya mikataba imeshakamilika utekelezaji wake na mengine ipo katika hatua za mwisho ya kukamilika kwake.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii imebaini kuwa utekelezaji wa mradi huu ulikuwa katika kipindi cha miaka miatatu ambapo hadi kamati inapokea majibu ya hoja hii ni asilimia 28 tu ya utekelezaji umefanyika.

Kamati ilipochunguza kwa kina iligundua kuwa afisa manunuzi aliyeteuliwa kwa awamu ya pili alikuwa hana utaaluma wa usimamizi wa mardi, matumizi ya mfumo ambao bank ya Dunia unatumika, kuchelewa kuwasilishwa barua ya no objection kutoka banka ya dunia na kutokuwemo katika mpango kazi wa manunuzi hali iliyosabaisha kuchelewa kwa asilimia 78 ya utekelezaji kutokutekelezeka kwa mradi.

Sambamba na hilo, kamati imeelezwa kwa sasa changamoto zote tayari zimeshafanyiwa kazi zikiwemo kuandaliwa kwa mikataba, kupatikana kwa barua ya no objection na Afisa manunuzi tayari ameshapatiwa mafuzo kwa ajili ya utekelezaji wa maradi

Kwa msingio huo kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa hoja hii.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Kamati ya PAC inaushauri Uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa miradi inayotekelezwa NA SERIKALI iwemo kwenye mpango wa manunuzi wa wizara ili kuondokana na changamoto ya matumizi mabaya ya fedha za Serikali.
2. Kamati ya PAC inaushauri uongozi kabla ya utekelezaji wa mradi wowote wa Wizara kuwepo kwa wataalam ambao wana ujuzi na uledi wa miradi ili kupatikana kwa ufanisi na uwajibikaji.

Hoja nambari 4.1.1.2: kuchelewa kuwasilishwa kwa Rasimu ya Mkataba kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kwa mujibu wa Kanuni ya 47(1)(2) ya Kanuni ya Ununuzi na Undoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2020 inataka makubaliano yoyote yanayohusiana na manunuzi ambayo thamani itakuwa na kiwango cha juu yatathibitishwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya kusainiwa na wahusika ambapo Afisa Masuuli ndani ya siku saba (7) baada ya kutoa uamuzi

atawasilisha kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali rasimu ya mkataba ili kuthibitishwa.

Ukaguzi ulipitia Mikataba mbalimbali ya miradi ya ZESTA inayohusiana na usambazaji wa bidhaa na kubaini uwepo wa ucheleweshaji wa kuwasilisha rasimu ya mkataba kwa Mwanasheria Mkuu kabla ya kusainiwa na wahusika. Ucheleweshaji wa mikataba hiyo ni kama inavyonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 19: Ucheleweshaji wa mikataba kwa Mwanasheria Mkuu

Kumbukumbu za Mkataba	**Kiasi cha Mkataba(USD)**	**Tarehe yaTuzo ya Mkataba**	**Tarehe ya uwasilishaji Ofisi ya Mwanasheria aMkuu**	**Idadi ya siku zilizochelewa**
Ununuzi wa Kompyuta na Vifaa kwa mkataba namba TZ-MOWEM-292675- GO-RFQ	40,181.21	22/08/2022	04/10/2022	33
Ununuzi wa Gari kupitia mkataba namba TZ-MOWEM-292723 -GO-RFQ	81,356.96	22/08/2022	04/10/2022	33

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Kwa mujibu wa kanuni ya manunuzi kipengele namba 48.1 kinaelezea utaratibu wa kisheria ni kuwasilisha rasimu za Mkataka kwa maafisa wa Sheria wa ndani ya Taasisi nunuzi kabla ya kuwasilisha kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Changamoto yakuchelewa kuwasilisha mikataba kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali imetatuliwa kwavile mradi umeongeza ufanisi kwa watendaji hususan wanasheria kwa lengo la kuhakikisha Rasimu za mikataba zinapitiwa mapema na wanasheria wa ndani. Kwa sasa Mikataba yote inawasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu kwa wakati

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC katika kufuatilia utekelezaji wa majibu ya hoja hii imebaini kuwa mkataba uliwasilishwa kwa mwanasheria wa wizara ambaye hakuwasilisha rasimu hiyo ya mkataba katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu

wa Serikali kama Sheria na Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2020

Baada ya majadiliano ya kina kuhusiana na majibu ya hoja hii, kamati imeelezwa kuwa kwa sasa mikataba yote kabla ya kuanza utekelezaji wake inawasilishwa katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya mapitio ya kisheria na kupata maoni.

Kwa mzingi huo, kamati ya PAC imeridhishwa na utekelezaji wa hoja hii.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inashauri Uongozi wa Wizara Maji, Nishati na Madinikuhakikisha mikataba yote inawasilishwa katika Afisi ya Mwanasheria mkuu wa Serikali ili kuepusho hoja zisizo za msingi.

MRADI WA MAENDELEO WA ZESS

Hoja nambari 4.1.2.1: upungufu wa fedha za kugharamia shughuli za mradi

Ukaguzi ulipitia ripoti za mpango wa mradi pamoja na kufanya majadiliano na wasimamizi wa Mradi na kubaini kwamba baadhi ya shughuli za Mradi ambazo zilipaswa kutekelezwa kwa mujibu wa fedha zilizolengwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 hazikuweza kutekelezeka kutokana na uhaba wa fedha za Mradi.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 ukaguzi ulibaini Mradi ulikuwa na bakaa ya shilingi 128,719,936 katika Akaunti za benki za mradi wakati shughuli zilizopangwa kutekelezwa zilighariimu jumla ya shilingi 154,314,132.40 jambo ambalo limepelekea shughuli za mradi kutotekelezwa.

Kutokuwepo kwa fedha za kutosha za kugharamia shughuli za mradi kunaweza kusababisha uwepo wa madai kwa shughuli zilizokwisha kutekelezwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini kuhakikisha unafanya ufuatiliaji wa karibu kwa washirika wa maendeleo ili fedha iliyopangwa na kuidhinishwa ipatikane kwa wakati kutekeleza shughuli za Mradi zilizokusudiwa.

Hali halisi ya shughuli za Mradi pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa ni kamainavyonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 20: Fedha za Mradi ambazo hazijalipwa na Washirika wa Maendeleo

Nam	Jina la Mfadhili	Maelezo	Kiasi cha Fedha (SEK/USD)	Kiasi cha fedha (TZS)
1.	Mult Consult	Fedha ambazo hazijalipwa	SEK 196,000	46,209,158.8
2.	Hexing ElectricalCo. Ltd	Malipo ya mwisho ya mkataba wa usambazaji wa mitaza AMR	USD. 46,456.8	108,104,973.6
Jumla				**154,314,132.4**

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Washirika wa Maendeleo wameshatoa fedha hizo na tayari ziko katika Akaunti ya Wizara ya Fedha.

Wizara ya maji Nishati na Madini imeshaziomba ilii ziingizwe katika akaunti ya mradi wa ZESS ili kuwalipa wanaohusika. ***Kiambatanisho nambari 1 kinahusika.***

Kiambatisho Nambari 1: Fedha za Mradi ambazo hazijalipwa na Washirika wa Maendeleo

Nam	Jina la Mfadhili	Maelezo	Kiasi cha Fedha (SEK/USD)	Kiasi cha Fedha (TZS)
1.	Mult Consult	Fedha ambazo hazijalipwa	SEK 196,000	46,209,158.8
2.	Hexing Electrical Co. Ltd	Malipo ya mwisho ya mkataba wa usambazaji wa mita za AMR	USD. 46,456.8	108,104,973.6
Jumla:				**154,314,132.4**

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Wakati kamati ikipitia utekelezaji wa hoja hii, kamati ya PAC imebaini kuwa tofauti ya fedha za bakaa iliyojitokeza imetokana kuwepo kwa mabadiliko ya thamani ya fedha (exchange rate). Hata hivyo, kamati ya PAC imeelezwa kuwa fedha hizo tayari zimeshaingizwa katika Akaunti ya hesabu ya Wizara ya Nchi, Afisi ya Raisi, Fedha na Mipango ambapo Wizara ya Maji, Nisharti na Madini imewasilisha barua ya maombi ya fedha kwa ajili ya kuingizwa kwenye Akaunt ya hesabu ya mradi wa Wizara kwa ajili ya utekelezaji wa mardi huo.

Sambasamba na hilo, hadi kamati inakamalisha uchunguzi wa hoja hii hakuna kilelezo cha barua kutoka wizara ya maji, nisharti na madini kilichowasilishwa mbele ya kamati iliyopelekwa wizara ya fedha kwa ajili ya kujirisha hatua za utekelezaji wa maombi ya fedha hizo na kupelekea kubakia kwa hoja hii.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inashauri Wizara ya maji, Nishati na Madini kuandaa utaratibu mzuri wa uwekaji wa nyaraka za Serikali vizuri ili zinapohitaji wakati wa ukaguzi zipatikane.

Hoja nambari 4.1.2.2: ukaguzi katika maeneo ya utekelezaji wa mradi

Ukaguzi ulifanya ziara ya kutembelea maeneo tofauti ya utekelezaji wa shughuli za mradi za uwekaji wa mita za AMR kwa upande wa Unguja na Pemba katika maeneo yafuatayo Wesha, Shumba, Makangale, Wete, Tibirinzi kwa upande wa Pemba na maeneo ya Nungwi, Matemwe, Pwani Mchangani, Michamvi, Chwaka, Pongwe, Paje, Makunduchi, Chukwani, Fumba na Kiembe Samaki kwa upande wa Unguja.

Aidha, ukaguzi umebaini Uwekezaji wa Mita aina AMR zilizowekwa hazikuwekewa Ulinzi kwa ajili ya kulinda uharibifu au madhara yanayoweza kutokea katika maeneo yaliyofungwa Mita hizo.

Maeneo yaliyowekwa Mita hizo ni Jadida Wete Pemba ambapo ufungaji wa Mita kwenye maeneo ya Barabara Kuu pamoja na eneo la Michamvi Unguja katika Hoteli ya Karafuu iliwekwa kwenye nguzo za Umeme ambazo watu hutumia kamasehemu za kutupa taka.

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Mita ya Umeme iliyoko Matemwe Karafuu Hotel imefungwa juu ya nguzo za umeme ambapo chini kuna jaa. Jaa limeshasafishwa na hairuhusiwi kutupa taka tena katika eneo hilo.

Kwa upande wa Mita ya AMR iliyoko Jadida Wete Pemba imefungwa juu ya Nguzo ambayo ipo karibu na barabara kuu. Mita hiyo iko ndani ya boksi maalum ambapo sio rahisi kuharibika. Kwa mujibu wa wataalamu wetu ndio mahala pa usalama zaidi kwa mujibu wa mazingira ya eneo hilo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, mebaini kuwa nguzo za mita za umeme zilifungwa kabla ya kuwepo kwa jaa katika maeneo ya Matemwe (Unguja)na Jadida kwa upande wa (Pemba). Hata hivyo, jukumu la usafi wa maeneo ya jaa ni jukumu la Manispaa ya wilaya husika na sio Shirika la Umeme.

Kwa msingi huo, Kamati ya PAC haikuona haja ya kuwepo kwa hoja hii katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kupelekea hoja hii kuondoka.

MRADI WA UIMARISHAJI WA ELIMU YA SEKONDARI ZANZIBAR (ZISP)

Hoja nambari 4.3.1.1: Fedha za mradi zilizokopwa ambazo hazijarejeshwa U$D 130,464

Fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka kwa Washiriki wa Maendeleo zinaongozwa na makubaliano ya ufadhili wa kifedha ambayo inawataka watekelezaji wa mradi kuhakikisha fedha zinazotolewa zinatumika kikamilifu katika shughuli za mradi zilizopangwa.

Ukaguzi ulipitia taarifa za fedha za Mradi wa ZISP na kubaini uwepo wa kiasi cha U$D 130,464 hadi tarehe 30 Juni, 2023 zilikuwa ni bakaa ya fedha ambazo hazijatumika ambapo ukaguzi ulibaini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar mnamo tarehe 28 JUNI, 2023 ilianza mchakato wa marejesho ya fedha hiyo (U$D) 130,464).

Lakini hadi ukaguzi unakamilika bado kiasi hicho cha fedha hakijarejeshwa. Hali hii ni kwenda kinyume na matakwa yaliyopo kwenye hati ya mradi husika, kama vile Mkataba wa fedha, miongozo mingine inayosimamia uendeshaji wa mradi, pia pamoja na uwepo wa mapungufu katika udhibiti wa ndani kwenye usimamizi wa fedha za mradi. Kutokurejeshwa kwa fedha zilizokopwa kunaathiri utekelezaji wa shughuli zilizopapangwa za mradi huo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa mradi kuhakikisha fedha zilizokopwa zinarejeshwa mara moja kwenye mradi husika ili kukwepa madhara ya kutotekelezeka kwa shughuli zilizopangwa.

Majibu ya Uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Uongozi wa Wizara inakubaliana na hoja ya mkaguzi kwa kipindi cha ukaguzi fedha hizo zilikuwa bado hazijarudishwa bali Uongozi wa Wizara ulikwisha chukua hatua ya kuzirejesha fedha hizo kwa kuandika barua kwenda Benki ya Watu wa Zanzibar yenye kumbukumbu namba AD.5/37/01/09/94 ya tarehe 28 Juni 2023 na barua kumb AD.5/37/01/09/95.Ucheleweshwaji wa urudishwaji wa fedha hizo haukusabishwa na Wizara isipokuwa baada ya Benki (PBZ) kupokea barua ya kurejesha fedha hizo kwenda Benki ya Dunia walitaka kuomba kibali kinachoruhusu kurejeshwa kwa fedha hizo kutoka Wizara ya Fedha kufuatia uhaba wa fedha za kigeni. Wizara ilifanya hivyo kupitia barua yenye kumbukumbu namba AB/74/72/02/A/19 ya tarehe 1 Septemba 2023. Kwasasa tayari fedha hizo zimerudishwa tokea tarehe 18 Disemba 2023.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kwamba Mradi huo ulikuwa na jumla ya Shilingi za Tanzania 35 Bilioni ambazo zilitumika katika utekelezaji wa Mradi huo wa ZISP na kubakia jumla ya Shilingi 130,464 ambazo wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake ya kiukazi, Wizara ilikuwa bado haijakamilisha taratibu za kuzirudisha Banki ya Dunia kama ilivyoelekezwa na Makubaliano ya utumiaji fedha hizo. Hata hivyo, Kamati imechunguza nyaraka za urudishaji wake na kubaini ni kweli fedha hizo zimerudishwa tarehe 18 Disemba, 2023 muda ambao Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilikuwa imeshatolewa kwa umma. Hivyo, Kamati imeamua kuiondosha hoja hii.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Wizara ya Elimu ihakikishe inachukua juhudi za makusudi kurudisha fedha za Miradi zinazobakia kwa wakati ili kuepusha kuwa na uhusiano usioridhisha na Washirika wetu wa Maendeleo.

Hoja nambari 4.3.1.2: Fedha ya mradi ambazo hazikutumika U$D 140,399.97

Kwa mujibu wa Mkataba wa Fedha kutoka Benki ya Dunia inawataka watekelezaji wa mradi kuhakikisha kuwa fedha zilizotolewa zinatumika katika shughuli za mradi zilizokusudiwa.

Ukaguzi ulipita kumbukumbu za matumizi ya fedha za mradi na kubaini jumla ya fedha za kimarekani USD 140,399.97 kutoka Benki ya Dunia ambapo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar imeshindwa kutumia fedha hizo kama zilivyotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi, hali hii imesababishwa na kuchelewa kwa fedha hizo kutoka Benki ya Dunia kutokana na kipindi cha janga la Uviko - 19 na kusababisha ugumu kwa baadhi ya shughuli kutotekelezwa jambo ambalo limesababisha kiasi hicho cha fedha kurejeshwa Benki ya Dunia ili kuzingatia masharti yaliyowekwa katika hati husika ya mradi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mradi wa ZISP kuhakikisha inachukua jitihada za makusudi za kuharakisha matumizi ya fedha za mradi kwa shughuli zilizopangwa kwa wakati.

Majibu ya Uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Uongozi wa Wizara umekubaliana na hoja ya Mkaguzi, kwa kipindi hicho cha ukaguzi fedha hizo zilichelewa kutumika kwa sababu uingizwaji wa fedha kutoka Benki ya Dunia zilichelewa kuingizwa katika kipindi cha janga la UVIKO - 19 ambapo hali hii ilipelekea baadhi ya shughuli kutoweza kutekelezwa. Kutokana na kukamilika kwa muda wa mradi, Wizara iliweza

kurudisha fedha hizo kwa Wahisani Kama ilivyoanisha katika hoja namba 4.3.1.1.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya fedha hizo kurudishwa kwa Wahisani wa Maendeleo, Kamati ya PAC ilitaka kujua kwanini jumla ya fedha iliyomo katika hoja 3.4.1.1 inatofautina na kuelezwa kwamba Mkaguzi Mradi ulikuwa na hesabu (account) ya Kigeni yenye jumla ya U$D 9,992.13 na hesabu ya fedha za Tanzania ambazo Mkaguzi alizibadilisha na kupata jumla ya U$D 130,464. Kamati pia imebaini kuathirika kwa baadhi ya shughuli zilizokuwa zimepangwa zikiwemo utoaji wa mafunzo kwa Walimu wa Wizara.

Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya uongozi wa Wizara na kuamua kuiondosha hoja hii.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha inaharakisha matumizi ya fedha za mradi kwa shughuli zilizopangwa kwa wakati husika ili kuepusha kutokutekelezeka kwa baadhi ya shughuli zilizoainishwa ndani ya Miradi hiyo.

Hoja nambari 4.3.1.3: Dosari iliyojitokeza katika kituo cha Limbani - Pemba

Ukaguzi ulitembelea Kituo cha Ubunifu wa Sayansi na cha Limbani - Pemba kilichojengwa kupitia mradi wa ZISP na kubaini uwepo wa dosari iliyojitokeza katika kituo hicho ambayo ilisababisha na bomba la kuteremshia maji lililofungwa vibaya kwa ajili ya ukusanyaji wa maji ya mvua ili kuruhusu mwelekeo wa mtiririko wa maji ya mvua kutoka nje ya eneo la kituo, ambalo limeweza kusababisha mmongonyoko wa ardhi katika eneo la mradi. Kuendelea kujitokeza kwa dosari katika utekelezaji wa shughuli za mradi kunaweza kusababisha hatari za usalama na uimara wa jengo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mradi kusimamaia vizuri shughuli za mradi zilizopangwa ili malengo ya mradi yafikiwe ikiwemo tija, usalama na ubora kwa watumiaji.

Majibu ya Uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Uongozi wa Wizara umekubaliana na hoja ya Mkaguzi Kuhusu dosari ya kituo cha Limbani kwa kipindi cha ukaguzi. Uongozi wa Wizara uliahidi kuwaagiza Watendaji wake kumsimamia Mkandarasi HOME AFRICA kwenda kufanya marekebisho ya sehemu zenye dosari na kuweka uimara zaidi na kwasasa dosari hiyo imefanyiwa kazi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya hoja hii kufanyiwa kazi na uongozi wa Wizara. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba kulikuwepo na usimamizi usioridhisha katika utekelezaji wa Mradi huu na kupelekea kujitokeza kwa changamoto ya uvujaji wa maji ya mvua.

Kamati imekubaliana na Wizara kwamba kabla ya kufikia maamuzi ya kuthibitisha utekelezaji wa hoja hii, ifanye ziara katika jengo hilo ili kubaini kwa kiasi gani maelezo yaliyotolewa yana ukweli.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Wizara uhakikishe unasimamia vyema utekelezaji wa Miradi yake ya Maendeleo ili kuweza kutambua changamoto zitakazoweza kujitokeza katika hatua ya awali na kuchukua hatua za kuzirekebisha.

MRADI WA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA WA ELIMU AWAMU YA PILI (GPE II)

Hoja nambari 4.3.2.1: Kasoro zilizobainika katika utekelezaji wa Mradi

Ukaguzi ulifanya ziara katika maeneo ya Mradi kwa ajili ya kuhakiki kazi za ukamilishaji wa madarasa kumi (10) ya awali, kati ya hayo jumla ya madarasa matano (5) yalijengwa ambayo ni Pagali, Guruweni, Pangani, Uwandani, Kibonde Mzungu na Kibubwi kwa upande wa Unguja na madarasa matano (5) kwa upande wa Pemba ambayo ni Chanjaani, Chanjamjawiri, Ngombeni, Ngagu na Ndagoni na kubaini uwepo wa dosari katika utekelezaji wa mradi huo.

Hali hii ilisababishwa na kutokuwepo kwa usimamaizi wa kutosha wa timu ya kutathmini zabuni za mradi ili kupata Mzabuni anaefaa kwa mujibu wa makubaliano. Kukosekana kwa usimamizi wa kutosha wa kazi za ukarabati zilizofanywa shuleni kulisababisha kasoro mbali mbali ambazo zilitakiwa kurekebishwa wakati wa usimamaizi wa kila siku.

Ukaguzi unashauri uongozi wa mradi kuhakikisha kuwa unafanya jitihada za makusudi za kufuatilia shughuli za ukarabati kwa madhumuni ya kugundua kasoro yoyote iliyojitokeza wakati wa shughuli za ujenzi.

Majibu ya Uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Uongozi wa Wizara unakubaliana na hoja ya Mkaguzi kwa kasoro zilizojitokeza katika Skuli zote zilizojengwa kupitia mradi wa GPE II kwa kipindi cha ukaguzi. Hata hivyo, Wizara ilichukuwa jitihada za kuhakikisha marekebisho yanafanywa kwa sehemu zilizobainika kuwa na kasoro. Kwa sasa tayari marekebisho yamefanyika kwa maeneo yaliyokuwa na kasoro.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika uchunguzi wa hoja hii, Kamati ya PAC iligundua mambo yafuatayo:

1. Kutokuwepo kwa usimamizi mzuri katika utekelezaji wa Mradi huu wa wa Ushirikiano wa Kimataifa wa Elimu Awamu ya Pili (GPE II).
2. Kuvunjwa kwa taratibu za Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, Namba 11 ya 2016. Hili lilibainishwa na Kamati baada ya kutaka kujibiwa kwamba marekebisho ya ujenzi yalifanywa na Kampuni nyengine ya BHCL Contractor Ltd kwa jumla ya shilingi 14,975,000 (VAT inclusive) ambapo upatikanaji wa Kampuni hiyo haukufuata taratibu ya kuwepo kwa Ripoti ya Tathimini iliyowasilishwa katika Bodi ya Zabuni kwa kuidhinishwa, badala

yake Uongozi wa Wizara ulifanya maamuzi ya kuitumia Kampuni hiyo baada ya Kampuni ya awali (M/S Sainath Builders Company Limited) kushindwa kukamilisha kazi na kuamua kuvunja mkataba nae.

3. Gharama ya matengenezo hazikuongekeza kwani Uongozi wa Wizara ulitumia bakaa ya fedha ambazo Mjenzi wa awali alikuwa hajalipwa. Gharama zote za ujenzi zilikuwa shilingi 244,221,000 (VAT inclusive).
4. Mradi ulitekelezwa na mafundi Wazawa ambao hawakusimamiwa ipasavyo na uongozi wa Wizara na kupelekea kujitokeza kwa kasoro za kiujenzi.

Kwa vile hoja hii imeshatekelezwa, Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya Uongozi wa Wizara na kuamua kuiondosha hoja hii.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Licha ya kwamba Mradi huu umetekelezwa na Wkandarasi Wazawa, uongozi wa Wizara unatakiwa kuchukua juhudi za makusudi kuhakikisha Mkandarasi huyo anasimamiwa vyema.
2. Uongozi wa Wizara utekeleze Miradi yake ya Maendeleo kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, Namba 11 ya 2016 ikiwemo kuidhinishwa kwa Ripoti ya Tathmini na Bodi ya Zabuni.

MRADI WA ELIMU YA JUU KWA MABADILIKO YA KIUCHUMI (HEET)

Hoja nambari 4.3.3.1: Fedha za mradi ambazo hazikutumika shilingi 3,140,485,688

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi (HEET) ulipanga kutumia jumla ya Shilingi 7,171,630,333 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi.

Ukaguzi ulipitia nyaraka za mradi na kubaini jumla ya shilling 3,870,897,961 zimeingizwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za miradi zilizopangwa kwa kipindi cha miezi sita, ambapo mradi uliweza kutumia jumla ya shilingi 730,412,273 sawa na asilimia 18.87 ya fedha zilizopokelewa na kupelekea uwepo wa jumla ya shilingi 3,140,485,688 ambazo hazikutumika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa mradi kuhakikisha kunakuwa na usimamizi mzuri wa matumizi ya fedha za miradi juu ya kutekeleza shughuli zote za mradi zilizopangwa kwa mwaka husika kwa mujibu wa bajeti iliyopangwa. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli namba 24 katika kitabu.

Majibu ya Uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Uongozi utachukua juhudi zote zinazofaa za kuhakikisha fedha za mradi zinatumika kutokana na kazi zilizopangwa na kuongeza kasi ya utekelezaji kwenda na wakati ili kuepuka kuongezeka kwa muda au kutowezekana kukamilika kwa utekelezaji wa kazi hizo.

Chuo kilipanga kutumia shilingi 2,082,731,131 kwa ajili ya ujenzi au ukarabati wa miundombinu. Uongozi ulifuatilia kwa karibu zoezi la ukamilishaji wa mchakato wa kumpata Mshauri Elekezi wa maswala ya kijamii na mazingira, Mshauri Elekezi wa usimamizi wa ujenzi na Mkandarasi wa Ujenzi pamoja na ununuzi wa vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu na TEHAMA pamoja na mafunzo ya kuwasimamia wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Uongozi wa SUZA uliweza kuongeza nguvu zaidi ya utekelezaji wa shughuli za maandalizi ya ujenzi na kumpata Mshauri Elekezi wa maswala ya kijamii na mazingira, kumpata Mashauri Elekezi wa kusimamia ujenzi na kukamilisha michoro ya ujenzi, ununuzi wa vifaa vya TEHAMA na vya Wanafunzi wenye mahitaji maalumu pamoja na kutoa mafunzo.

Hadi kufikia Juni 2024, jumla ya shilingi 1,096,947,328.2 ambazo ni wastani wa asilimia 53 ya bajeti ya 2022/2023 zilitumika. Kutokamilika kwa matumizi hayo kumetokana na kuchelewa kumpata Mkandarasi wa

ujenzi na kuanza kazi za ujenzi. Hali hii ilisababishwa na utaratibu wa manunuzi wa Benki Kuu ya Dunia kuchukua muda zaidi ya uliotarajiwa.

Chuo kilipanga kutumia shilingi 114,700,000 kwa ajili ya kukuza mitaala na kuanzisha mbinu bunifu za ufundishaji. Uongozi wa Chuo uliongeza nguvu ya ufuatiliaji. Hii ilitokana na kubadilika mara kwa mara kwa taratibu za utayarishaji wa mitaala kulikosababishwa na mabadiliko ya matakwa ya Benki ya Dunia na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kulikopelekea kuchelewa matumizi ya fedha zilizotengwa kwa kazi hiyo.

Uongozi wa SUZA ulifanikisha kukamilishwa kwa mitaala iliyopangwa kuandaliwa kwa mwaka 2023 na kuweza kuwasilishwa TCU kwa ajili ya ithibati Mwezi wa Oktoba, 2023. Hadi kufikia Juni 2024, jumla ya shilingi 114,700,000 zilizotengwa kwa mwaka 2022/2023 zimetumika kwa asilimia 100.

Chuo kilipanga kutumia shilingi 161,720,830 kwa ajili ya Kuimarisha matumizi ya teknolojia ya kidijitali. Uongozi ulifanya ufuatiliaji wa kutatua changamoto zilizokwamisha na kuchelewesha taratibu za manunuzi kwa baadhi ya vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya Maabara za Kompyuta na Kituo cha Elimu kwa njia za Kidijitali (CDL) kutokana na malalamiko kwa baadhi ya Wazabuni kutoridhika na mchakato huo (Super Enterprises) kwa barua nambari SUP/SUZA/2023/4/1 ya tarehe 25/4/2023 na SUP/ZAPDD/2023/03 ya tarehe 29/5/2023 na (ZANIT) kwa barua nambari TZ-SUZ-263540-GO-RFB ya tarehe 20/4/2023. Uongozi ulisitisha zoezi hilo na kurudiwa kwa mchakato wa kumpata Mzabuni wa ununuzi wa vifaa hivyo. Hata hivyo uongozi ulisimamia vyema zoezi hilo na kukamilika kwa ufanisi. Hadi kufikia June 2024, jumla ya shilingi 139,161,950.50 ambazo ni wastani wa asilimia 86 zimetumika kwa ajili ya kuimarisha mifumo ya kidijitali, ununuzi wa vifaa vya kidigitali na mafunzo ya kidigitali kwa wanataaluma na mafundi.

Chuo kilipanga kutumia shilingi 1,511,746,000 kwa ajili ya kuwajenga uwezo wafanyakazi wa kitaaluma na uongozi wa Chuo Kikuu, Uongozi wa SUZA ulisimamia kumaliza changamoto ya upatikanaji wa idadi ndogo ya maombi ya mafunzo ya muda mrefu kwa kupitia upya vipaumbele vya Mradi. Baada ya kuruhusu maombi kwa kufungua vipaumbele vyote 14 vya mafunzo vilivyoainishwa na mradi, kulikopelekea ongezeko la idadi ya maombi ya nafasi za masomo. Hadi kufikia Juni 2024, tatizo hilo limetatuliwa kwa kuwapeleka masomoni jumla ya watumishi 38 kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Aidha, Uongozi wa SUZA ulisimamia uimarishaji na uanzishwaji wa mifumo ya kitaaluma na kiutawala, kuimarisha masuala ya kijinsia, zoezi la ununuzi wa vifaa na samani mbali mbali za Ofisi, ununuzi wa magari pamoja na gharama nyengine za uendeshaji wa mradi. Hadi kufikia Juni,

2024 kazi zote zimefanyika na fedha zote zilizopangwa shilingi 1,511,746,000 kwa mwaka 2022/2023 zimetumika sawa na asilimia 100.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kwamba wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake katika Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA), ni kweli chuo hicho kilikuwa kinakabiliwa na kasoro zilizobainishwa na Mkaguzi katika utekelezaji wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi (HEET). Hata hivyo, Kamati imebaini Uongozi wa SUZA umechukua juhudi za kutosha kuzifanyia kazi kasoro zilizobainika. Kiujumla, Kamati imebaini yafuatayo katika utekelezaji wa hoja hii:

1. Licha ya kuchelewa, Mkandarasi wa Mradi huo ameshapatikana mwezi wa Novemba, 2024 ambaye ni Mohammed Builders chini ya Kampuni ya ZABACCO na Mshauri Elekezi AKIS.
2. Bado fedha kwa ajili ya kazi za ujenzi hazijatumika kwa ukamilifu wake. Hali hiyo imesababishwa na kuchelewa kupatikana kwa Mkandarasi wa ujenzi.
3. Kutokutumika kwa wakati kwa fedha hizo pia kulichangiwa na kutokuwepo kwa uelewa wa taratibu za manunuzi zinazotumiwa na Benki ya Dunia kwa Watoaji huduma wetu.
4. Kwa upande wa mitaala ya wanafunzi kulihitajika Mwekezaji wa kuingiza taarifa za ufundishaji kwa kutumia 'ICT'.
5. Kwasasa Chuo kinao mtandao wa 'internet' kupitia Ternet.

Pamoja na utekelezaji wa hoja ya Mkaguzi, Kamati imeamua kufanya ziara katika Mradi huu ili kujionea uhalisia wa mambo yaliyotekelezwa na ikiridhika, kuiondoa hoja hii.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Uongozi wa Chuo uharakishe hatua za ujenzi wa Mradi huu ili kuepusha kuchelewa zaidi katika utekelezaji wa Mradi.
2. Uongozi wa Chuo uhakikishe unamsimamia vyema Mkandarasi aliyepewa kazi ya ujenzi ili kubaini mapema kasoro zitakazojitokeza na kuzifanyia marekebisho.
3. Kamati inakiagiza Chuo cha SUZA kufuata taratibu za kisheria hususan katika utekelezaji wa Miradi yake ya Maendeleo ili kijiepusha na changamoto za kiukaguzi.

MRADI WA UJENZI WA KITUO CHA MABASI KINOWE (HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI)

Hoja nambari 5.1.4.1: Kukosekana kwa Ripoti ya Utekelezaji Mradi

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imesaini hati ya makubaliano ya mkataba wa Ujenzi wa Kituo cha Mabasi Kinowe na Kampuni ya M/S Comfi x & Engineering Co. Ltd wenye nambari SMZ/D11-212/W/DP/2021-2022/15 wa tarehe 13/5/2022 wenye thamani ya shilingi 1,046,224,500.

Katika kupitia kumbukumbu mbali mbali za mradi ukaguzi umeshindwa kuona na kupitia ripoti ya utekelezaji ya mradi huo hali iliyopelekea kushindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa mwenendo wa utekelezaji wake, kukosekana kwa uwazi katika taarifa za kifedha na kutokubainika kwa changamoto na mafanikio yaliyofikiwa katika kipindi cha utekelezaji. Hali hii inaweza kupelekea ugumu katika kufanya tathmini ya maendeleo ya mradi na pia ni kwenda kinyume na kanuni ya 57(1)(2)(b) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri kuhakikisha unatayarisha na kuhifadhi vielelezo vyote vinavyohusiana na uendeshaji wa kazi za Afisi ya Halmashauri.

Majibu ya uongozi wa Halmashauri

Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imekua ikiandaa ripoti mbali mbali za utekelezaji wa miradi inayotekelezwa na Ofisi. Kupitia mradi wa ujenzi wa Kituo cha Mabasi wa Kinowe Konde Ofisi imeandaa ripoti za utekelezaji ambazo zimeweza kuwasilishwa katika ngazi husika. Aidha Ofisi inatunza na kuhifadhi vielelezo vyote vinavyohusiana na mradi huu na miradi mengineyo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia ukweli wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kwamba ni kweli hakukuwa na Ripoti ya Utekelezaji Mradi wakati Mkaguzi anafanya kazi zake za ukaguzi katika Mradi huu. Hali hiyo ilitokana na Watendaji wa Halmashauri kushindwa kumsimamia ipasavyo Mshauri Elekezi aliyekabidhiwa kazi ya kushughulikia Mradi huu.

Kamati iliyabaini hayo baada ya kujua kwamba Ripotivzilikuwepo ila alikuwa nazo Mshauri Elekezi na hakuziwasilisha wakati wa ukaguzi.

Kamati ya PAC imefanikiwa kuiona Ripoti hiyo na kuridhika nayo. Kwasasa, Halmashauri inaandaa na kuhufadhi Ripoti za utekelezaji wa Miradi mimgine tofauti ya maendeleo kama ilivyofanyika katika Mradi wa Usambazaji maji Micheweni. Kwa msingi huo, Kamati imeiondoa hoja hii.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inautaka uongozi wa Halmashauri ya Wilayacya Wete kuwafuatilia na kuwasimamia kwa karibu Washauri Elekezi wanaowapa kazi za kushughulikia Miradi yao.

Hoja nambari 5.1.4.2: Kukosekana kwa Ripoti ya Mkaguzi wa Ndani

Kwa mujibu wa kifungu nambari 117(5) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 inasema kwamba "Katika kutekeleza majukumu yao, wakaguzi wa ndani watatoa kwa maandishi taarifa za ukaguzi wa ndani pamoja na mapendekezo kwa Maafi sa Wahasibu."

Ukaguzi umebaini kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni hawakuandaa taarifa za ukaguzi wa ndani zinazohusu mradi wa ujenzi wa Kituo cha Mabasi. Hali inayopelekea Halmashauri kutokupata ushauri wa kitalaam unauhusiana na masuala ya kifedha na mambo mengine kwa wakati. Aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kuhakikisha kuwa Mkaguzi wa Ndani anakagua na kutoa ripoti kwa kazi zote zinazohusiana na Halmashauri ikiwemo kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa lengo la kutoa ushauri wa kitaalam kwa wakati.

Majibu ya uongozi wa Halmashauri

Katika ukaguzi uliofanywa na mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za serekali umebaini **Kukosekana kwa ripoti ya mkaguzi wa ndani**, hii ilitokana na Mkaguzi wa ndani kwenda kujiendeleza kimasomo nchini China na kwa kipindi hicho hapakuwa na mkaguzi mwengine jambo ambalo lilipelekea kuzorota kwa kazi za mkaguzi, hata hivyo tulipokea mkaguzi mwengine kutoka ofisi ya Rais fedha na mipango tarehe 16/05/2023 ambapo ni mwezi mmoja kabla ya mwaka wa fedha kumalizika kwa kuwa muda ulikuwa umeshakuwa mrefu alilazimika kufanya ukaguzi wa jumla kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni inaupokea na kuufanyia kazi ushauri wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali wa kuhakikisha kuwa Mkaguzi wa Ndani anakagua na kutoa ripoti kwa kazi zote zinazohusiana na Halmashauri ikiwemo kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa lengo la kutoa ushauri wa kitaalam kwa wakati.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kukubaliana na hoja ya Mkaguzi ya kukosekana Ripoti ya Mkaguzi wa Ndani wakati wa

ukaguzi. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba kulikuwa na Mkaguzi wa Ndani wa Wizara ambae pia alikuwa akifuatilia utekelezaji wa Mradi huu lakini hakuwa akiwasilisha Ripoti yake katika uongozi wa Halmashauri.

Kadhalika, kwa wakati huo hakukuwa na Kamati ya Ukaguzi wa Ndani iliyokuwa inazipitia Ripoti ya Makguzi. Kwasasa kasoro hizo zimerekebishwa na Ripoti za ukaguzi wa ndani zinakuwepo. Kwa vile hoja hii imetekelezwa, kamati imeamua kuiondosha.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Halmashauri uhakikishe unamtumia vyema Mkaguzi aliyekuwepo na kuzifanyia kazi hoja anazoziibua kwacmujibu wa sheria ili kuondokana na hoja za ukaguzi.

Hoja nambari 5.1.4.3: Kutokuwasilishwa kwa hati ya dhamana ya utendaji kazi (Performance security) shilingi 104,622,450

Kwa mujibu wa kanuni nambari 29(4) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya 2020 inamtaka mzabuni aliyeshinda kuwasilisha hati ya dhamana pamoja na hundi ambazo zimethibitishwa na benki anayotumia kwa Kitengo cha Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma. Aidha, kifungu nambari 55.1 cha masharti maalum ya mkataba (SCC) cha mkataba wa Ujenzi wa Kituo cha Mabasi kinamtaka Mkandarasi kuwasilisha hati ya dhamana ya utendaji kazi ya asilimia 10 ya bei ya mkataba.

Katika kupitia kumbukumbu za mradi wa ujenzi wa Kituo cha Mabasi, ukaguzi umebaini kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni iliingia katika mkataba wa Ujenzi wa Kituo cha Mabasi na M/S Comfi x & Engineering Co. Ltd bila ya kuwasilishwa kwa hati ya dhamana (Performance Security). Kutokuwasilishwa kwa hati ya dhamana ni kwenda kinyume na kanuni na kifungu cha masharti maalum ya mkataba nilivyovinakili hapo juu.

Kutokuwasilishwa kwa hati ya dhamana ya utendaji kazi kunaweza kuisababishia hasara Serikali kwa kutokupata marejesho ya fedha zake pale ambapo mzabuni atashindwa kuwasilisha vifaa alivyotakiwa kuwasilisha au kushindwa kazi aliyopewa kwa mujibu wa mkataba, aidha hupelekea uwezekano wa kuisababishia Halmashauri hasara na Serikali kwa ujumla pindipo Mkandarasi huyo akishindwa kufanya kazi kama inavyotakiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kuhakikisha wanasimamia vyema matakwa ya Sheria na masharti ya mkataba ili kuiepushia Serikali hasara inayotokana na upotevu wa fedha za Serikali.

Majibu ya uongzi wa Halmashauri

Katika ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serekali imeripotiwa **Kutokuwasilishwa kwa hati ya dhamana ya utendaji kazi (Performance Security),** hii ilitokana na kuwa Mradi huo wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ulikuwa ni miongoni mwa mradi unaotekelezwa kimkakati, kituo cha Mabasi cha Konde kilikuwa ni kimoja miongoni mwa ahadi za Mh. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kukuza miundo mbinu mbali mbali hapa nchini. Uharaka wa utekelezaji wa kazi hiyo ulisababisha kutokupatikana kwa hati ya dhamana ya utendaji kazi (Performance security), hata hivyo ushauri wa mkaguzi umechukuliwa na tutaufanyia kazi kwa miradi ambayo tunaendelea kuitekeleza.

Aidha kutokana na changamoto ya uhaba wa fedha za kutekeleza mradi huo Mkandarasi alikubali kutekeleza mradi huo kwa kumlipa kwa mujibu wa utekelezaji wa mradi na kwa mujibu wa kiwango cha fedha tulichonacho na fedha itakayobakia atalipwa kidogo kidogo kwa mujibu wa uwezo na upatikanaji wa fedha za makusanyo ya Halmashauri.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Ki kweli kwamba Mkaguzi alibaini kwamba wakati anakagua Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni haikuwasilishiwa dhamana ya utendaji kazi na kampuni ya M/S Confi and engineering Co. LTD. Kamati imegundua hilo lilisababishwa na usimamizi mdogo wa uliofanywa kwa Mkandarasi.

Kwasasa, Kamati imejirodhisha kwamba kasoro hiyo imesharekebishwa kwani Miradi mingi imeonekana hati ya dhamana ya utendaji kazi ipo. Hilo limethibitishwa na Kamati baada ya kuchunguza utekelezaji wa Mradi wa Ufungaji wa Mashine wa Kuchakata Mwani ambao una hati ya dhamana ya shilingi 3,000,000 ya tarehe 5/3/2024 kwa Shirika la Bima la Zanzibar na Mradi wa Usambazaji Maji Micheweni wenye hati ya dhamana ya shilingi 1,500,000 kwa Benki ya Watu wa Zanzibar ya tarehe 22/5/2024. Kwa msingi huo, hoja hii imeomdolewa na Kamati.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni uhakikishe unafuata Sheria katika utekelezaji wa Miradi yake hususan kwa kuwa nayo hati ya dhamana ya itendaji kazi, kuihifadhi vizuri na kuiwasilisha katika wakati wa ukaguzi.

Hoja nambari 5.1.4.4: Kutokufanyika kwa upembuzi yakinifu kabla ya utekelezaji mradi

Katika kupitia kumbukumbu za mradi wa ujenzi wa Kituo cha Mabasi ukaguzi umebaini kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni

haikufanya upembuzi yakinifu wa kubaini asili ya udongo na vipengele vingine vinavyohitajika kabla ya ujenzi wa Kituo cha Mabasi Kinowe.

Dosari iliyobainika ni kuchelewa kwa kazi ya ujenzi kutokana na uwepo wa udongo dhaifu unaokaa maji kwa kiwango kikubwa pindi mvua inaponyesha katika eneo lililoteuliwa kujengwa Kituo cha Mabasi. Hali hii inaweza kupelekea kuitia Serikali hasara kutokana na ucheleweshwaji wa mradi na upandaji wa bei za vifaa. Kutokufanyika kwa upembuzi yakinifu ni kwenda kinyume na kifungu nambari 2.3 cha Mwongozo wa Upangaji wa Miradi na Majadiliano ya Kuongeza Mikopo, Kutoa Dhamana na Kupokea Ruzuku ya Novemba, 2020.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kuhakikisha unafanya upembuzi yakinifu kabla ya kuanza kwa miradi ya ujenzi ili kuepusha kuisababishia Serikali kutumia gharama kubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo bila ya uwepo wa ulazima wa kufanya hivyo.

Majibu ya uongozi wa Halmashauri

Katika ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serekali haukupata taarifa za**kufanyika kwa upembuzi yakinifu kabla ya ujenzi wa mradi wa kituo cha mabasi Kinowe,** hii ilitokana na kuwa Mradi huo wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ulikuwa ni miongoni mwa mradi unaotekelezwa kimkakati, kituo hichi kilikuwa ni miongoni mwa ahadi za Mh. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kuwatengenezea wananchi miundo mbinu muhimuikiwemo ya usafiri. Kutokana na uharaka wa kazi hio, Halmashauri haikupata muda wa kutosha wa kufanya upembembuzi yakinifu, hata hivyo Mkandarasi kwa usimamizi wa Mshauri elekezi alichukua hatua zote zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuupima udongo, na kuuondoa udongo usio stahiki pamoja na kuweka na kushindilia udongo mwengine kwa viwango vinavyohitajika ili kuepusha athari zinazoweza kutokea.

Ushauriwa mkaguzi tumeuchukuwa na kuufanyia kazi kwa miradi mengine itakayotekelezwa na ofisi, na hasa ukizingatia kwamba mradi huu ni wa mwanzo mkubwa kutekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni.

Uchungiwa Kamati ya PAC

Licha ya Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kukiri kuwepo kwa kasoro ya kutokufanyika kwa upembuzi yakinifu. Hata hivyo, Kamati ilitaka kujua shida ilikuwa nini na kubaini kwamba Halmashauri kwa wakati huo ilikuwa haina wataalam wa kufanya kazi hiyo na ilishindwa kutafuta Wataaalam kutokana na uharaka wake kwani vile huu ulikuwa ni Mradi wa Kimkakati.

Kamati ya PAC imegundua kwamba uongozi wa Halmashauri haukuzingatia matakwa ya sheria katika utekelezaji wa Mradi huu kwani Mradi kuwa ni wa Mkakati hauzuii kutekelezwa bila ya kufuata sheria na taratibu za ujenzi.

Kaasasa, Kamati imeelezwa kwamba Halmashauri inafanya upembuzi yakinifu katika Miradi yake. Hivyo, hoja hii inabakia kwa hatua za utekelezaji na kujiridhisha kwa miradi ijayo.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Halmashauri y Wilaya ya Micheweni ihakikishe inafanya upembuzi yakinifu katika Miradi yake ya Maendeleo ili kuepusha kujitokeza athari za baadae hususan wakati wa matumizi ya miradi hiyo.

Hoja nambari 5.1.4.5: Malipo ya awali yaliyolipwa kinyume na utaratibu

Kwa mujibu wa kifungu cha 54.1 cha masharti ya jumla ya mkataba (GCC 54.1) kikisomwa pamoja na kifungu cha 25 cha masharti maalum ya mkataba (SCC 25) namba SMZ/D11-212/W/DP/20212022/15 wa tarehe 13/5/2022 baina ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kama mwajiri na Kampuni ya Comfix & Engineering Co. Ltd kama Mkandarasi vinaeleza kwamba, kiwango cha juu cha malipo ya awali kitakua asilimia 20 ya thamani ya mkataba chini ya kiasi cha muda kinacholipwa na mwajiri baada ya kuwasilisha hati ya dhamana ya kibenki bila masharti.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imefanya malipo ya awali ya shilingi 209,244,900 sawa na asilimia 20 ya thamani ya mkataba kwa Mkandarasi kabla ya Mkandarasi huyo wa ujenzi wa Kituo cha Mabasi Kinowe kuwasilisha hati ya dhamana ya benki kwa mujibu wa matakwa ya mkataba wao. Hali hii inaweza kupelekea Afisi ya Halmashauri kuitia hasara Serikali pindipo mkandarasi akiamua kuiwacha kazi husika, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kuhakikisha wanafuata kikamifu Sheria, Kanuni na Matakwa ya mkataba ili kuepukana na hasara inayoweza kujitokeza pindipo Mkandarasi akiamua kuacha kazi.

Majibu ya uongozi wa Halmashauri

Katika ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serekali imegundulika kuwepo kwa **Malipo ya awali yaliyolipwa kinyume na utaratibu shilingi 209,244,900,**Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ilifanya juhudi kubwa kuhakikisha kuwa Mkandarasi anawasilisha hati hiyo ya dhamana kabla ya kufanyiwa malipoikiwa ni pamoja na kumuandikia barua Mkandarasi yenye kumb. Nambari

OH/WM/OR/TB/74/VOL.1/29 ya tarehe 01/06/2022 ya kumtaka awasilishe hati hiyo ili aweze kufanyiwa malipo hayo ya awali. Tarehe 02/06/2022 alijibu barua na kutueleza kuwa bank yake imo kwenye utaratibu wa kukamilisha na kuiwasilisha kwetu pindipo itakapopatikana.

Aidha kutokana na uharaka wa utekelezaji wa mradi huu, na kuepusha ucheleweshaji wa utekelezaji wa mradi huku Ofisi ikiamini kuwa Mkandarasi atawasilisha hati hiyo; Ofisi ilichukua maamuzi ya kumlipa Mkandarasi fedha hizo ili aweze kuendeleza mradi huo huku tukizingatia kuwa atajenga na kukamilisha kazi yote bila ya kumlipa fedha zote za mkataba (ambapo hadi kufikia sasa ameshakamilisha ujenzi ila bado hatujamalizia malipo yake).

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya ilibaini kuwa ni kweli Mkandarasi alilipwa malipo ya awali bila ya kufuata utaratibu wa kuweka hati ya dhamana. Hali hiyo ilijitokeza kwa vile Halmashauri ilikuwa haina fedha za kutosha za kumlipa Mkandarasi kwani alikuwa akitumia fedha zake mwenyewe katika utekelezaji wa Mradi huo na kutegemea kukamilishiwa malipo yake baada ya kukamilika Mradi huo (Halmashauriilikuwa na shilingi milioni 70 wakati Mradi unahitaji Bilioni moja). Kutokana na hilo, hivi sasa Mradi umekamilika tangu tarehe 13/5/2023 lakini Mkandarasi anadai shilingi milioni 89.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inaitaka Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kuhakikisha wanatekeleza sheria na masharti ya mikataba wanayoingia ili kuepusha kuwepo kwa malalamiko wakati wa utekelezaji na ukamilikaji wa Miradi hiyo.

Hoja nambari 5.1.4.6: Kutokukatwa malipo ya kitangulizi katika vyeti vya malipo (interim payment certificate) shilingi 128,050,000

Kwa mujibu wa kifungu cha 54.1 cha masharti ya jumla ya mkataba (GCC 54.1) kikisomwa pamoja na kifungu cha 25 cha masharti maalum ya mkataba (SCC 25) namba SMZ/D11-212/W/DP/20212022/15 wa tarehe 13/5/2022 baina ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kama mwajiri na Kampuni ya M/S Comfi x & Engineering Co. Ltd kama Mkandarasi vinaeleza kwamba, kiwango cha juu cha malipo ya awali kitakua asilimia 20 ya thamani ya mkataba chini ya kiasi cha muda kinacholipwa na mwajiri baada ya kuwasilisha hati ya dhamana ya benki bila masharti na malipo hayo yatarejeshwa asilimia 20 kwa kila cheti cha malipo (interim payment certifi cate).

Ukaguzi umebaini kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imefanya malipo ya shilingi 640,250,000 kwa awamu mbili tofauti ikiwa awamu ya

mwanzo wamelipa shilingi 408,250,000 kwa ajili ya malipo ya cheti cha mwanzo na shilingi 232,000,000 ikiwa ni kwa ajili ya malipo ya cheti cha pili bila kukata asilimia 20 ya kurejesha malipo ya kitangulizi (Advance Payment) ambayo kwa ujumla wake ni shilingi 128,050,000 kama masharti ya mkataba yanavyoelekeza.

Kutokukatwa malipo ya kitangulizi katika vyeti vya malipo (Interim payment certificate) kunaweza kupelekea hasara kwa Serikali pindipo Mkandarasi akiamua kuacha kazi, aidha ni kwenda kinyume na kifungu tajwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kuhakikisha unasimamia vyema makubaliano ya mkataba kama Sheria zinavyoelekeza.

Majibu ya uongozi wa Halmashauri

Katika ukaguzi uliofanywa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serekali imeonekana **Kutokukatwa kwa malipo ya kitangulizi katika vyeti vya malipo (Interim payment Certificate) Shilingi 128,050,000,** hii ilitokana na mshauri elekezi kutokuanisha moja kwa moja kukatwa kwa Advance payment kwa Certificate ya mwanzo aliyotupatia; kwa certificate ya pili kazi ilikuwa imeshafikia asilimia 88 ya utekelezaji ilhali malipo yaliyokuwa yamefanyika ni asilimia 39 tu, hivyo Ofisi iliona ipo haja ya kuendelea kumlipa kiasi hicho ili kuepusha ongezeko la deni kwa mwaka wa fedha unaofuata na kwa kuzingatia kwamba kwa mujibu wa makubaliano yetu Mkandarasi atakamilisha kazi yote na baadaye ataendelea kuidai Ofisi, na malipo yake atalipwa kwa mujibu wa upatikanaji wa fedha. Hata hivyo uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni unauchukua ushauri waMdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serekalikuhakikisha tunasimamia vyema makubaliano ya mkataba kama Sheria zinavyoelekeza.

Uchungi wa Kamati ya PAC

Ni kweli uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ilikiri kuwepo kwa kasoro hizo. Hali hiyo ilitokana na ukweli kwamba utekelezaji wa Mradi huo ulikuwa unafanyika kwa utaratibu wa Mkopo yaan Mkandarasi atumie pesa zake na kulipwa kidogo kidogo. Kamati imebaini kuwa malipo ya Mkandarasi yalikuwa yakilipwa kinyume na masharti ya Mkataba. Hili hiyo imepelekea Mradi kukamilika lakini Mkandarasi bado anadai shilingi milioni 89. Kwa mnasaba huu, Kamati imeibakisha hoja hii kwa hatua za kujiridhisha utekelezaji wa miradi ya baadae.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kuhakikisha unasimamia ipasavyo Miradi yake kama inavyoelekezwa na masharti ya Mikataba yao.

Hoja nambari 5.1.4.7: Mapungufu katika Mkataba wa Ujenzi wa Kituo cha Mabasi Kinoe

Baada ya kupitia nyaraka mbali mbali za mradi ukaguzi umebaini uwepo wa barua ya malalamiko yenye kumbukumbu nambari Mac/com/23/315/50 ya tarehe 22/5/2023 kutoka Kampuni ya M/S Comfix Engineering limited kwenda Afisi ya Halmashauri ikilalamikia kupokea malipo yaliyokatwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kutoka katika bei ya mkataba ya shilingi 1,046,224,500.

Dosari iliyobainika katika mkataba wa Ujenzi wa Kituo cha Mabasi wenye kumbu kumbu nambari SMZ/D11-212/W/DP/2021-2022/15 wa tarehe 13/5/2022 uliosainiwa baina Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kama mwajiri na Kampuni ya M/S Comfix Engineering Co. Ltd kama Mkandarasi ni kutokuanisha iwapo malipo ya mkataba ya shilingi 1,046,224,500 yanajumuisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) au vyenginevyo. Hali hii imepelekea kutokea kwa tofauti ya uwelewa baina ya mwajiri na mkandarasi jambo lililopelekea kiashiria cha kutokea kwa mgogoro baina yao.

Kuwepo kwa mapungufu katika mkataba wa ujenzi wa Kituo cha Mabasi Kinowe kunaweza kupelekea uwezekano wa kutokea kwa migogoro baina ya muajiri na mkandarasi na pia inaweza kupelekea kuitia hasara Serikali, aidha ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri kuhakikisha mikataba yote wanayoingia wanaipeleka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kupata maoni ya kitaalamu na hivyo kuingia mikataba ambayo haitaleta migogoro na pia yenye kuleta tija kwa taifa.

Majibu ya uongozi wa Halmashauri

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ilikubaliana na Kampuni ya M/S Comfix Engineering limited kujenga Kituo cha Mabasi cha Kinowe Konde kwa kufunga Mkataba wenye kumbu kumbu nambari SMZ/D11-212/W/DP/2021-2022/15 wa tarehe 13/5/2022 uliotayarishwa kwa kufuata vigezo vyote vinavyo hitajika. Mkataba huo uliwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu mnamo tarehe 28/04/2022 na kujibiwa tarehe 05/05/2022 ambapo ushauri wote wa kisheria uliotolewa ulifanyiwa kazi na Ofisi yetu. Aidha kuhusu lalamiko la Mkandarasi kuhusiana na Ongezeko la thamani (VAT) halikuwa la msingi hii ni kwa mujibu wa sheria ya usimamizi wa kodi (tax Administration and Procedures Act no. 7 of 2009. Kifungu cha 50(1),(2), (3) kinatuwajibisha kuzuia kodi kwa mtoa huduma aliesajiliwa katika kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT);hivyo Mkandarasi huyo analazimika kukatwa Kodi ya ongezeko la thamani (VAT) hata kama mkatabaumekaa kimya.

Uchungi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia ukweli wa hoja hii, Kamati imebaini kuwa Uongozi wa Halmashauri ilikutakiwa kuainisha katika Mkataba wake malipo ya utekelezaji Mradi huo yatajumuisha kodi au vyengine licha ya sheria kodi inatambua kuwa Taasisi za Serikali ni Wakala katika ukusanyaji kodi. Kungekuwepo sharti hilo kungeepusha Mkandarasi kilaumu kwamba malipo aliyolipwa yanaupungufu.

Kwa msingi huo, hoja hii inaendelea kubakia kwa hatua za utekelezaji ili kubaini kama mikataba ijayo imezingatia uwepo wa kifungu cha kukatwa kodi.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Halmashauri uhakikishe unaweka kifungu cha ukataji kodi katika malipo ya Miradi yao ya maendeleo.

Hoja nambari 5.1.4.8: Mradi kutekelezwa bila ya uwepo wa hati ya dhamana ya benki.

Kwa mujibu wa kanuni nambari 29(4) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya 2020 inamtaka mzabuni aliyeshinda kuwasilisha hati ya dhamana pamoja na hundi ambazo zimethibitishwa na benki anayotumia kwa Kitengo cha Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Katika kupitia kumbukumbu za mradi wa ujenzi wa Kituo cha Mabasi Kinowe, ukaguzi umebaini kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni iliingia katika mkataba wa Ujenzi wa Kituo cha Mabasi na Kampuni ya M/S Comfi x & Engineering Co. Ltd wenye kumbu kumbu nambari SMZ/D11-212/W/DP/2021-2022/15 bila ya kuwasilishwa kwa hati ya dhamana (Performance Security). Kutokuwasilishwa kwa hati ya dhamana ya benki ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Hali hii huenda imesababishwa na Halmashauri kuchagua mkandarasi asiyekuwa na uwezo wa kutosha na hivyo kupelekea uwezekano wa kuisababishia hasara Halmashauri na Serikali kwa ujumla. Kufanya hivyo kunapelekea kuitia hasara Serikali kwa kutokupata marejesho ya fedha zake pale ambapo mzabuni atashindwa kuwasilisha vifaa alivyotakiwa kuwasilisha au kushindwa kazi aliyopewa kwa mujibu wa mkataba

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kuhakikisha kuwa wanasimamia vyema Sheria, Kanuni na Miongozo inayotolewa na Serikali ikiwa ni pamoja na kutokuanza kazi za ujenzi wa miradi mikubwa bila ya kuwepo kwa hati ya dhamana ya benki.

Majibu ya uongzi wa Halmashauri

Katika ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serekali imeripotiwa **Mradi kutekelezwa bila ya uwepo wa hati ya dhamana ya benki,** hii ilitokana na kuwa Mradi huo wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ulikuwa ni miongoni mwa mradi unaotekelezwa kimkakati, kituo cha Mabasi cha Konde kilikuwa ni kimoja miongoni mwa ahadi za Mh. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kukuza miundo mbinu mbali mbali hapa nchini. Jambo ambalo lilisababisha kutokupatikana kwa hati ya dhamana ya utendaji (Performance security) kutokana na uharaka wa kazi hio, hata hivyo ushauri wa mkaguzi umechukuliwa na tutaufanyia kazi kwa miradi ambayo tunaendelea kuitekeleza

Aidha kutokana na changamoto ya uhaba wa fedha za kutekeleza mradi huo Mkandarasi alikubali kutekeleza mradi huo kwa kumlipa kwa mujibu wa utekelezaji wa mradi na kwa mujibu wa kiwango cha fedha tulichonacho na fedha itakayobakia atalipwa kidogo kidogo kwa mujibu wa uwezo na upatikanaji wa fedha za makusanyo ya Halmashauri.

Uchunguzi na Maagizo ya Kamati

Kamati katika Uchungizi wake imebaini Mkaguzi amefanya kosa kuingiza hoja hiyo kwani inalingana na hoja nambari 5.1.4.3. Hivyo hoja hii imeondolewa.

UCHUNGUZI WA KAMATI YA PAC KUHUSU UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA NA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023

SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR

Hoja nambari 4.1.1.1: ukosefu wa mita inayotumika kupima umemem unaoingia na kutoka katika vituo vidogo vya usambazaji umeme na transfoma

Ukaguzi ulifanya mapitio ya ufanisi wa uendeshaji wa vituo vidogo (sub stations) vya usambazaji wa umeme pamoja na transfoma na kubaini kukosekana kwa mita ya kusoma umeme wa laini kuu unaoingia na kutoka katika vituo vidogo pamoja na Transfoma. Kupitia majadiliano na uongozi wa Shirika la Umeme, ukaguzi ulibaini sababu iliyopelekea dosari hiyo ni ukosefu wa fedha kwa ajili ya mita ya laini kuu na kuchelewa kuwekwa kwa mfumo wa kusoma mita moja kwa moja.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa haikuwezekana kufuatilia usomaji wa mita kwa umeme ulioingia na kusambazwa (wakiwemo watumiaji wakubwa wa umeme) na vituo vidogo vya umeme kutokana na kukosekana kwa usomaji mita ya laini kuu au katika vituo vidogo vya usambazaji wa umeme.

Kukosekana mita ya laini kuu na vituo vidogo vya usambazaji umeme kwa ajili ya kusoma umeme unaoingia na kutoka kunaweza kusababisha Shirika kushindwa kuelewa umeme unaopotea kutokana na wizi katika eneo maalum na kwa wakati.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Umeme Zanzibar uwasiliane na Serikali Kuu ili kupata fedha za ziada kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya usambazaji wa umeme pamoja na kuhakikisha kuwa mita zote za laini kuu au vituo vidogo vya usambazaji umeme zinapatikana na zinawekwa katika vituo husika ili kuongeza ufanisi katika kubaini wizi au upotevu wa umeme.

Majibu ya Uongozi

Shirika limeshafanya utaratibu wa kibajeti kwa kutenga fedha katika mwaka wa fedha 2024/25 kwa ajili ya manunuzi ya Transformer Management Unit (TMU) mia tatu (300) na hatua iliopo hivi sasa ni kutangaza tenda ya ununuzi wa vifaa hivyo ambapo kila transfoma itawekewa kifaa hicho ili taarifa za mwenendo wa matumizi ya transfoma ziweze kupatikana kwa ajili ya kuchukua hatua stahiki.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, Kamati imebaini kuwepo kwa ucheleweshaji wa utekelezaji wa hoja hii na kugundua kuwa Uongozi wa Shirika la Umeme ilitenga bajeti ya shillingi bilioni 5.8 kwa ajili ya ununuzi wa mita za kupimia umeme TMU kwa mwaka wa fedha 2022/2023, hata hivyo manunuzi hayo hayakuweza kufanyika kutokana na kukosekana kwa bajeti. Pia, Kamati ya PAC imeelezwa kuwa Serikali imepanga ununuzi wa mita kutekelezwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025.

Wakati wa majadiliano Kamati ya PAC imegundua mambo yafuatayo:-

- Machakato wa zabuni ulifanyika kwa kutumia njia ya “direct procurement” na mita 53 zilinunuliwa ambapo 13 (11kv) na 40 (33kv) kupitia mzabuni wa Osaju Company Limited. Kamati ilielezwa kwamba mita zote 53 ziliopo maeneo ya saateni hazikuweza kufanya kazi (mbovu).
- Upatikanaji wa technical team haukufuata taratibu wa Sheria ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.
- Kukosekona kwa mita katika vituo vidogo vya usambazaji umeme na transfoma kunapelekea kuwepo kwa hasara ya shilingi bilioni 3.9 kwa mwezi .
- Kutokana na ukosefu wa kifaa cha TMU kunapelekea kuwepo kwa wimbi kubwa la wizi wa unit za umeme.
- Osaju Company Limited imelipwa fedha zote za ununuzi wa vifaa vya mita za umeme na trasfoma.

Uongozi wa Shirika la Umeme umechukua hatua ya kuwasilisha dai hilo kwa Mamlaka husika kwa ajili ya uchunguzi. Kwa sasa Shirika limeanza na mchakato mpya wa tenda kwa ajili ya ununuzi wa vifaa 500 vya Umeme.

Sambamba na hilo, Kamati ilihitaji kupatiwa vielelezo kwa ajili kujiridhisha kuhusiana na hoja hii lakini hadi inakamilisha uchunguzi wake vielelzo hivyo havikuweza kuwasilishwa mbele ya kamati na kupelekea hoja hii kubakia kwa ufuatiliaji.

Magizo ya Kamati ya PAC

- Kamati ya PAC inashauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhakikisha katika bajeti ya mwaka 2024/2025 fedha hiyo inapatika ili kunusuru upotevu mkubwa wa mapato ya Serikali yatokanayo na Umeme.
- Uongozi wa Shirika la Umeme unashauriwa kufuata masharti ya Sheria ya Manunuzi na Uondowaji wa Mali za Umma nambari 11 ya 2016 katka mchakato wa zabuni za manunuzi.
- Kamati inashauri watendaji wa Shirika la Umeme kuwa waaminifu katika kutekeleza majukumu yao kwa maslahi ya Serikali.

Hoja nambari 4.1.1.2: ucheleweshaji mkubwa wa kushughulikia malalamiko ya wateja

Ukaguzi ulipitia ufanisi wa uwezo wa Shirika la Umeme Zanzibar katika kushughulikia malalamiko ya wateja kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na kubaini kuwa kati ya malalamiko 20,348 yaliyosajiliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2023 malalamiko 6,163 ya wateja (sawa na asilimia 30) hayakuhudumiwa ndani ya kipindi cha kuanzia siku 1 hadi siku 363, malalamiko 6,794 (sawa na asilimia 33) yalihudumiwa kwa kuchelewa kwa kiasi kikubwa kuanzia muda wa siku 7 hadi siku 355**.**

Kuchelewa kushughulikia malalamiko ya wateja ni kinyume na aya ya 5.1, 5.2 na 5.3 ya Mkataba wa Wateja wa Shirika la Umeme. Ucheleweshaji wa utatuzi wa malalamiko kunaweza kusababisha kutoridhika kwa wateja na kuharibu hadhi ya Shirika pamoja na uaminifu wa wateja.
Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Umeme Zanzibar kufanya mapitio ya kina ya michakato ya ushughulikiaji wa malalamiko ya wateja na kufanya maboresho ili kuhakikisha ufanisi na kutathmini mahitaji ya rasilimali, ikiwa ni pamoja na wafanyakazi na teknolojia, ili kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye ya wingi wa malalamiko.

Majibu ya Shirika la Umeme

Shirika limeshachukua kwa kuwapatia mafunzo watendaji wake wa kituo cha kupokeleea miito ya simu pamoja na kuandaa watendaji maalumu quality assuarance team) wanao fanya kazi ya kuskiliza miito ya simu pamoja na kushughulikia malalamiko yote ya wateja ya kuhakikisha yanafungwa kwa wakati.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa hoja hii, kamati imebaini kuwa changamoto hiyo imetokana na uhaba wa watendaji kwa wakati huo, jumla ya watendaji 16 tu walikuwepo katika kitengo cha ushughulikiaji wa malalamiko ya wateja.

Baada ya kamati kufanya uchunguzi kuhusiana na hoja hii ilielezwa kwamba kwa sasa hatua mbali mbali zimechukuliwa na Uongozi wa shirika ikiwemo kuajiri watendaji wapya saba katika kituoa cha mamalamiko kwa wateja na kituo hicho kinafanyakazi masaa 24. Ambapo Kituoa hicho cha mito ya simu kinasimamiwa na wataalumu ambao wanapitia malalamiko yote yanayowasilishwa na wateja na kuyafanyia kazi kwa wakati na kuyafunga yanapokamilika na kila mwisho wa mwezi ripoti huwasilishwa wa uongozi.

Aidha, Uongozi wa Shirika imeeleza kamati kwamba imenzisha utaratibu maalum wa kushughulikia mito ya simu ya dharura kwa kupitia mfumo wa wateja. Kwa mnasaba huo, Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa hoja hii.

Hoja nambari 4.1.1.3: kutokukusanywa kwa mwaka mzima madeni ya wateja wanaolipa baada ya kutumia umeme shilingi bilioni 7,596,399,436.42

Kifungu nambari 7.3(c) cha Muongozo wa Sera na Taratibu za Uhasibu na Fedha wa Shirika la Umeme wa mwaka 2004 unampa mamlaka Meneja Biashara kufuatilia kikamilifu ulipaji wa madeni ya wateja wenye madeni makubwa na kuanzisha taratibu za kukata huduma ya umeme kwa mujibu wa sera zilizowekwa.

Ukaguzi umebaini uwepo wa wateja 42 wanaofanya malipo baada ya matumizi ya umeme (postpaid) ambao hawakufanya malipo yoyote kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa madeni yao wanayodaiwa yenye thamani ya shilingi 7,596,399,436.42.

Ukaguzi ulifanya uchambuzi kwa kulinganisha baina ya bili zote zilizotolewa katika mwaka wa fedha 2022/2023 na muda ziliokaa bila ya kulipwa (age analysis). Uwepo wa wateja hawa kunaibua wasiwasi juu ya kufuata kifungu nilichokinakili hapo juu.

Aidha, ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ina deni kubwa lenye jumla ya shilingi 54,216,259,718. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 13 (shilingi 6,237,350,092.51) kutoka deni la mwaka jana la shilingi 47,978,909,625. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wa mwaka jana kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022, ilielezwa wasiwasi juu ya madeni haya na kati ya mapendekezo tuliyoyatoa ni umuhimu wa Shirika la Umeme Zanzibar kushirikiana kikamilifu na Mamlaka ya Maji Zanzibar ili kutafuta hatma ya malimbikizo ya madeni yaliyopita na yajayo.

Ukaguzi unapendekeza kwa uongozi wa Shirika la Umeme Zanzibar kuimarisha utaratibu madhubuti wa ukusanyaji wa madeni na hatua za ukataji wa huduma ya umeme kama ilivyoelekeza kifungu 7.3 (c) cha mwongozo wa Shirika pamoja na kuanzisha vipimo vya utendajikazi na taratibu za uwajibikaji kwa ajili ya kufuatilia na kuboresha ufanisi wa ukusanyaji wa madeni.

Mchanganuo wa wateja 42 wanaofanya malipo baada ya matumizi ya umeme (postpaid) ambao hawakufanya malipo yoyote kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa madeni yao wanayodaiwa ni kama inavyoonekana hapo chini:-

Jadweli Nambari 23: Madeni ya muda mrefu yanayodaiwa kwa wateja wa ZECO

Namba	Nambari ya	Jumla ya Deni	Bakaa ya Deni hadi Tarehe	Kiasi kilicholipwa ndaniya Mwaka

	Hesabu	(Tsh.)	30/06/2023 (Tsh.)	2022/2023
1.	D000039252	164,676,159.62	164,676,159.62	0
2.	D000021488	115,994,487.77	115,994,487.77	0
3.	D000039254	102,524,849.59	102,524,849.59	0
4.	D000037345	56,922,862.27	56,922,862.27	0
5.	D000037710	56,671,807.52	56,671,807.52	0
6.	000000015N	51,739,296.81	51,739,296.81	0
7.	000000003K	51,057,039.61	51,057,039.61	0
8.	D000039271	42,328,917.84	42,328,917.84	0
9.	000001023N	37,630,944.58	37,630,944.58	0
10.	D000037429	35,864,370.57	35,864,370.57	0
11.	D000039138	29,118,327.21	29,118,327.21	0
12.	D000039180	29,072,302.79	29,072,302.79	0
13.	D000039439	18,839,952.19	18,839,952.19	0
14.	D000008233	14,360,149.65	14,360,149.65	0
15.	D000038625	14,096,899.32	14,096,899.32	0
16.	D000039311	6,413,982.83	6,413,982.83	0
17.	D000014171	5,551,664.40	5,551,664.40	0
18.	D000038952	4,481,620.58	4,481,620.58	0
19.	D000039431	4,248,944.57	4,248,944.57	0
20.	D000039126	3,917,657.15	3,917,657.15	0
21.	D000039461	3,745,329.47	3,745,329.47	0
22.	D000021266	3,582,358.23	3,582,358.23	0
23.	D000039465	3,576,370.70	3,576,370.70	0
24.	D000039459	3,353,603.16	3,353,603.16	0
25.	D000039441	3,280,324.35	3,280,324.35	0
26.	D000039462	2,864,963.55	2,864,963.55	0
27.	D000039440	2,678,105.07	2,678,105.07	0
28.	D000013047	2,560,630.92	2,560,630.92	0

29.	D000039336	1,983,209.52	1,983,209.52	0
30.	000030219W	1,755,000.78	1,755,000.78	0
31.	D000039442	1,690,305.05	1,690,305.05	0
32.	D000039463	1,548,024.75	1,548,024.75	0
33.	000000113M	210,783,282.59	210,783,282.59	0
34.	D000039307	44,596,583.58	44,596,583.58	0
35.	D000039443	47,472,859.05	47,472,859.05	0
36.	D000039448	8,174,460.00	8,174,460.00	0
37.	D000039348	23,173,991.01	23,173,991.01	0
38.	D000021626	16,357,368.49	16,357,368.49	0
39.	D000039310	12,434,330.03	12,434,330.03	0
40.	000000106O	43,693,786.48	43,693,786.48	0
41.	D000039153	74,232,219.77	74,232,219.77	0
42.	ZAWA	6,237,350,092.51	6,237,350,092.51	0
Jumla		**7,596,399,435.93**	**7,596,399,435.93**	**0**

Majibu ya Shirika la Umeme

Shirika limechukua juhudi mbalimbali ikiwemo kuwaandikia notisi, wadaiwa ambao hawajalipa madeni yao. vile vile Shirika limefanya mikutano mbalimbali na taasisi husika ili kuhakikisha wanalipia madeni yao kwa wakati. Aidha, kwa sasa Shirika lipo katika hatua ya ununuzi wa mita za *prepaid* zenye uwezo mkubwa kwa ajili ya kuwafungia wateja wakubwa ili kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato. Ufungaji wa mita hizo za prepaid utaliwezesha shirika kukusanya madeni hayo kwa makato ya asilimia 50% kwa kulipia deni la nyuma kila anaponunua umeme

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa hoja hii, kamati ya PAC imegundua deni la shilingi bilioni 7,596,399,436.42 liliorodheshwa na mkaguzi hadi sasa asilimia 13% tu ya deni limeshalipwa, hata hivyo, kamati imebaini kuna changamoto kubwa kwa upande wa Taasisi za Serikali kwa kutokulipa kwa madeni yao kwa wakati.

Wakati wa uchunguzi kamati pia imebaini kuwa kuna utofauti wa deni ambalo mkaguzi amelionesha katika ripoti yake na taarifa ya hesabu ya

mwisho wa mwaka (financial statement). Deni halisi ambalo linaonekana katika taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka 2022/2023 ni jumla ya shilingi bilioni 65,164,171,512 (Note 8) deni ambalo kamati imeelezwa kuwa linajumuisha na madeni wanaodaiwa shirika na watoa huduma (suppliers).

Sambamba na hilo, Kamati imeelezwa kwa upande wa Mamlaka ya maji zanzibar Serikali imechukua juhudi ya kuanza kulipa deni la kila mwezi shilingi bilioni 1.5.

Maagizo ya Kamati ya PAC

kamati ya PAC inazishauri Taasisi na Mashirika ya Serikali kuaanda mapango madhubuti wa ulipaji madeni ili shirika liondokane na hoja zisizo na lazima.

Kamati ya PAC inashauri Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kuaanda utaratibu maalum kwa Taasisi na Mashirika ya Serikali yanayodaiwa madeni ya muda mrefu ya umeme kukatwa moja kwa moja kupitia matumizi mengineo (OC) katika bajeti zao.

Kamati ya PAC inawashauri Wahasibu kutumia ujuzi na uweledi katika uandaaji wa taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka ili kuondokana na mapungu yanayojitokeza katika taarifa za hesabu.

Hoja nambari 4.1.1.4: kuchelewa kwa kiasi kikubwa kwa huduma ya unganishaji umeme kwa wateja

Kifungu namba 2.1 cha Mkataba wa Huduma kwa wateja wa Shirika la Umeme Zanzibar (Customer Charter) wa mwaka 2015 kinaelezea muda unaotarajiwa kwa kila hatua ya mchakato wa uunganishaji huduma ya umeme kwa wateja wapya ili kuhakikisha utoaji wa huduma kwa wakati. Hatua za mchakato huo ni pamoja na usajili, upimaji, makisio ya gharama, malipo, ufungaji mita na uboreshaji wa mfumo.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, ukaguzi ulibaini kuwepo kwa ucheleweshaji mkubwa katika huduma ya uunganishaji umeme kwa wateja wapya kutoka siku 97 hadi siku 238. Muda huu ni kinyume na Mkataba wa Huduma kwa wateja kama ilivyoainishwa katika kifungu namba 2.1 kinachohusiana na ufanisi wa shughuli za uunganishaji umeme kwa wateja.

Baada ya kufanya mahojiano na Uongozi wa Shirika, ukaguzi umebaini kuwa changamoto ya kutofikia muda uliowekwa inatokana na uhaba wa vifaa vya kuunganisha umeme.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Umeme Zanzibar kuhakikisha unafuata muda wa Mkataba wa Huduma kwa wateja kwa kufanya tathmini ya mara kwa mara ya vifaa vinavyohitajika ili kuzuia uhaba wa baadaye

katika kukidhi mahitaji ya wateja pamoja na kufanya tathmini na kuwasiliana na mamlaka husika kuhusu uhaba wa wafanyakazi

Majibu ya Shirika la Umeme

Shirika limepokea maombi mengi ya uunganishaji wa umeme kutokana na kupungua kwa gharama za uunganishaji umeme kutoka wastani wa 460,000/= hadi 200,000/= kwa wateja wa kawaida na wastani wa 1,600,000/= kwa nguzo moja hadi 200,000/=. Aidha, shirika limeomba kibali cha kuajiri wafanyakazi 120 wa muda kuongeza nguvu katika kushughulikia maombi ya wateja mapya. kwa sasa Shirika linawaunganishia wateja wapya 150 kwa wiki na usajili wa wateja wapya 200 kwa mwezi na mategemeo ikifika mwishoni mwa oktoba 2024 hakutakuwa na maombi ya zamani

Uchunguza wa Kamati ya PAC

Baada ya Kamati ya PAC kupata majibu ya utekelezaji wa hoja hii, Kamati imebaini kuwa ucheleweshaji huu umetokana na mtoa huduma aliyepewa kazi hiyo kuwasilisha asilimia 20% ya nguzo ambazo hazina viwango vilivyoainishwa kwa mujibu wa mkataba husika.

Licha ya changamoto iliyojitokeza Uongozi wa Shirika imechukua juhudi mbali mbali zikuwemo kuanzisha mkachato mpya wa manunuzi ya nguzo ili kupunguza ucheleweshaji wa unganishaji wa umeme kwa wateja ambapo kwa sasa malalamiko yamepungua kwa asilimia kubwa kama majibu yanavyojieleza.

Kwa mnasaba huo, Kamati ya PAC imeridhika na hatua za utekelezaji wa hoja hii.

Hoja nambari 4.1.1.5: Ucheleweshaji mkubwa wa kutafuta ufumbuzi wa miamala isiyo ya kawaida iliyomo katika taarifa ya usuluhishi wa kibenki

Ukaguzi ulipitia taarifa za usuluhishi wa kibenki (bank reconciliation statements) na kubaini uwepo wa miamala isiyo ya kawaida ambayo imeshindwa kutafutiwa ufumbuzi kwa zaidi ya miezi miwili (2) ambapo ni kinyume na kifungu nambari 9.8 (c) cha Muongozo wa Sera na Taratibu za Uhasibu na Fedha wa Shirika la Umeme wa mwaka 2004. Miamala hiyo inajumuisha hundi zilizokwishafanyiwa malipo ambazo bado hazijalipwa benki, pamoja na fedha zilizopelekwa benki ambazo bado hazijaingizwa katika hesabu. Kiasi kinachohusika ni kikubwa na kinatia wasiwasi juu ya usahihi wa taarifa za kifedha za Shirika la Umeme.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Umeme Zanzibar kuboresha udhibiti wa ndani unaohusiana na mchakato wa usuluhishi wa kibenki ili kupunguza vihatarishi vya kupata tofauti pamoja na kuhimiza mapitio ya

mara kwa mara ya taarifa za usuluhishi wa kibenki ili kugundua na kushughulikia tofauti zinazojitokeza kwa wakati.

Majibu ya Shirika la Umeme

Shirika limechukua hatua ya kupitia miamala iliyokaa muda mrefu bila ya kutoka au kuingia benki (unpresented and uncredited) na kwa miamala ambayo haikutoka benki kwa muda mrefu tayari imeshafanyiwa usuluhishi. Na miamala ambayo haikuonekana kuingia benki katika ripoti ya usuluhishi Shirika limepitia miamala hiyo na kugundua kuwa imetokanana kutofautiana kwa senti au kwa makisio na nambari(approximation) mfano 3,714,935.18/= na benki kulipwa 3,715,000/= hali hii inasababisha mfumo kutoweza kufanya usuluhishi wa miamala hiyo kwani usuluhishi hio hufanyika kiotomatiki katika mfumo wa SAP.

Uchunguza wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa wateja wa Serikali walikuwa wanalipa moja kwa moja kwa kupitia Ankara za benki na kupelekea kujitokeza kwa utofauti wa taarifa ya usuluhishiji wa kibenki hali hii imetokana na baadhi ya control number haoneshi uhaliasia kwa sababu miamala mingi.

Kwa sasa changamoto hiyo tayari umeshafanyiwa kazi Uongozi wa Shirika na kupelekea hoja kuondoka.

Hoja nambari 4.1.1.6 mchakato wa ununuzi usio wa ushindani wenye thamani ya shilingi 3.24 bilioni na USD milioni 138.07.

Ukaguzi ulipitia majalada 17 ya michakato ya manunuzi na nyaraka nyengine zinazohusiana na mikataba ya manunuzi hayo na kubaini uwepo wa mikataba sita iliyotolewa kwa wazabuni mbalimbali bila kufanya taratibu za ununuzi wa ushindani. Uongozi wa Shirika uliandaa na kutoa tu taarifa za kushinda zabuni (notification of award) au taarifa ya kukubalika kwa zabuni (letter of acceptance) kulikofuatiwa na uingiaji wa mkataba. Hakukuwa na mwaliko wa maombi ya ushindani wala nyaraka za zabuni zilizotumwa kwa wazabuni. Aidha, hakukuwa na michakato ya tathmini ya zabuni wala mazungumzo ya mapatano kabla ya kuingia mkataba. Hii ni kinyume na kifungu cha 66(1)(a)(b) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

Kushindwa kufuata taratibu za manunuzi za ushindani kunapunguza uwezo w**a** Shirika kufaidika na bei ya ushindani na pia kukosa thamani halisi ya fedha (Value for Money) katika shughuli za manunuzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Umeme Zanzibar kuzingatia taratibu zote za ununuzi wa bidhaa kwa kutumia taratibu husika kama

zilivyoelezwa katika kifungu nilichokinakili hapo juu. Mchanganuo wa manunuzi yaliyobainika kutokuwa na ushindani ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Majibu ya Shirika la Umeme

Majibu ya hoja hii yameambatanishwa katika **kiambatanisho B**.

Jadweli Nambari 24: Manunuzi ya Shirika la Umeme yaliyokosa ushindani Kiambatanisho B:

No.	Namba ya Zabuni/ Mkataba	Maelezo	Jina la Mzabuni	Kiasi cha Fedha	
				Shs.	USD
1.	No. Contract preparedby ZECO	Provision of Software Assurance Agreement	LANDIS + Gyr (Pty) Ltd SA	-	138,000,000
2.	ZECO/CW/01/2023/09	Repair of House NoS1	Isadeco Construction Zanzibar	35,697,438.00	-
3.	ZECO/GR/12/2022/26	Supply of WoodenPoles	Poles (T) Limited	-	70,924.61
4.	ZECO/GR/10/2022/17	Supply of High Tension &Low Tension Materials	VOLEX Electrical & Decorators Co. LTD	3,121,100,000	-
5.	ZECO/SR/01/2023/01	Provide Support& Maintenance for callcenter System	Soft Net Technologies Limited	31,049,112	-
Jumla				**3,238,096,950**	**138,070,925**

	Nambari ya Mkataba	Maelezo	Majibu ya Menejimenti

1	Mchakato wa Mkataba huu	Provision of Software	haya yalikua ni malipo ya leseni

	haukuanzishwa na Shirika	Assurance Agreement	ya kampuni (inayoendelea kutoa huduma) ya uuzaji wa umeme kwa kampuni ya LANDIS + Gyr (Pty) Ltd .
2	ZECO/CW/01/ 2023/09	Matengenezo ya Nyumba nambari S1	Haya yalikuwa ni manunuzi ya moja kwa moja kwa ajili ya matengenezo ya ofisi za Mradi wa ZESTA. Na taratibu za manunuzi zilizotumika ni za mradi wa benki ya dunia ambazo haziendani na taratibu za manunuzi ya sheria iliyopo.
3	ZECO/GR/12/ 2022/26	Usambazaji wa Nguzo	Ununuzi wa nguzo ulifanyika kwa kutumia njia ya manunuzi ya moja kwa moja (direct procurement) na njia hii ilichaguliwa ili kuhakikisha upatikanaji wa nguzo hizo kwa ufanisi na kwa wakati kwa kuwa Shirika lilikuwa katika hali ngumu ya uhitaji na mazingira hayakuwa mazuri kwa njia ya zabuni ya ushindani.
4	ZECO/GR/10/ 2022/27	Usambazaji wa vifaa vya Umeme Mkubwa na vya Umeme Mdogo.	Ununuzi wa nguzo ulifanyika kwa kutumia njia ya manunuzi ya moja kwa moja (direct procurement) na njia hii ilichaguliwa ili kuhakikisha upatikanaji wa nguzo hizo kwa ufanisi na kwa wakati kwa kuwa

			Shirika lilikuwa katika hali ngumu ya uhitaji na mazingira hayakuwa mazuri kwa njia ya zabuni ya ushindani. Kwa sasa, Zabuni zinatangazwa kupitia mfumo ya e-proz kupitia njia ya ushindani.
5	ZECO/SR/01/2 023/01	Kutoa Huduma ya Usaidizi na Matengenezo kwa Mfumo wa kituo cha simu (Call Center).	Shirika liliingia mkataba na kampuni ya SOFTNET TECHNOLOGIES LIMITED kwa mkataba wa TSH: 81,716,000 kwa ajili ya ufungaji wa mfumo wa kituo cha simu(Call Center System). Na kwa kuwa kulikuwa na mahitaji ya utoaji wa Msaada na Matengenezo kwa mfumo huo wa kituo cha simu na
			kampuni ya SOFTNET TECHNOLOGIES LIMITED ilikuwa na uwezo wa kutoa aina hii ya huduma. Kwa hivyo, kulifanyika nyongeza ya mkataba (addendum) na kampuni ya SOFTNET TECHNOLOGIES kwa mkataba wa jumla ya TZS 31,049,112. Kwa hiyo, kwa kuwa kulifanyika nyongeza ya mkataba hakukuwa na haja ya kuanzisha mchakato mwingine wa manunuzi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, Kamati ya PAC haikuridhishwa na majibu ya utekelezaji yaliotolewa na Uongozi wa Shirika la Umeme katika kadhia ya manunuzi ya Shirika la Umeme yaliyokosa ushindani kwa Kampuni zilizotajwa katika hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambazo hazikufuata taratibu za Manunuzi kama Sheria inavyoelekeza na kupelekea Kamati kushindwa kuiondoa hoja hii.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauagiza Uongozi wa Shirika la Umeme wanapofanya manunuzi ya ndani ni vyema kuhakikisha Sheria, Kanuni na Miongozo inayohusiana na Manunuzi inafuatwa kikamilifu ili kuondokana na upotevu wa fedha za Serikali**.**

Hoja nambari 4.1.1.7: Kutumia njia ya ununuzi isiyosahihi shilingi bilioni 11.63

Jadweli la Tano la Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 linataja viwango vya ukomo vinavyopedekezwa kwa kila njia ya manunuzi vinavyotakiwa kufuatwa na Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji ya Mali za Umma wakati wa mchakato wa zabuni za bidhaa, kazi na huduma za Ushauri elekezi. Kwa upande wa njia ya manunuzi ya maombi ya ushindani, jadweli linaweka wazi kuwa kwa bidhaa, ukomo ni baina ya shilingi milioni 15 hadi shilingi milioni 50, kwa kazi ni baina ya shilingi milioni 20 hadi shilingi milioni 100 na kwa huduma za ushauri elekezi ukomo ni kutoka shilingi milioni 5 hadi shilingi milioni 75.

Kifungu nambari 72(1) – (3) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma inaweza kununua na kuuza kwa njia ya manunuzi ya maombi ya ushindani kwa bidhaa, kazi na huduma za ushauri elekezi zinazopatikana na zilizo tayari. Endapo thamani inayokadiriwa ya mkataba imezidi kizingiti cha zabuni Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma itapata uthibitisho wa awali wa Mamlaka kwa ajili ya kushiriki katika ununuzi na uondoshaji wa mali za umma kwa njia ya uanishaji.

Ukaguzi ulipitia majalada 17 ya mchakato wa manunuzi na nyaraka nyengine zinazohusiana namikataba na kubaini kuwa uongozi wa Shirika ulinunuwa bidhaa kwa njia ya maombi ya ushindani (open quotation) zenye jumla ya shilingi 11,627,929,490 ambayo ni zaidi ya kizingiti cha juu kinachotakiwa kwa ajili ya kutumia njia hii. Kizingiti cha juu kwa njia hii ya ushindani wa wazi ni shilingi milioni 50. Aidha, ukaguzi haukupata ushahidi wa maombi ya Uongozi wa Shirika kuomba ruhusa kutoka kwa

Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA) kwa ajili ya kutumia njia ya maombi ya ushindani.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 72(1)-(3) na jadweli la Tano la Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 na kunazuia ushindani mpana na uwazi na hatimae kukosekana kwa ufanisi wa bei.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Umeme Zanzibar kuhakikisha kuwa manunuzi yote ya Shirika yanafanywa kwa mujibu wa Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 na Kanuni zake za 2020. Mchanganuo wa manunuzi yaliyofanyika kwa njia iliyozidi kizingiti kilichowekwa ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 25: Manunuzi yaliyofanywa kwa njia iliyozidi kizingiti kilichowekwa

Namba	**Namba ya Mkataba**	**Maelezo**	**Jina la Mzabuni**	**Kiasi (Shs.)**
1.	ZECO/GR/09/2022/16/17	Supply of Fuel	GAPCO Zanzibar Limited	4,239,648,000
2.	ZECO/GR/45/2021/72	Supply of Miters	BAOBAB Energy SystemTanzania	7,388,281,490
Jumla				**11,627,929,490**

Majibu ya Shirika la Umeme

Kupitia mkataba nambari (ZECO/GR/09/2022/16/17), Shirika lilitumia mbinu za Ushindani wa Kitaifa wa Zabuni (Restricted National CompetitiveBidding RNCB)) kutangaza mchakato wa zabuni na ikisha zabuni ilitekelezwa kwa njia ya nukuu zilizofungwa (sealed quotations) kwa wasambazaji wa mafuta wakubwa hapa Zanzibar kwani bidhaa hiyo ya mafuta tayari imeshapangiwa bei elekezi na mamlaka husika.

Vilevile, kwa mkataba nambari (ZECO/GR/45/2021/72), utekelezaji ulifanyika kwa njia ya 'framework contract' ambapo utaratibu wake ni kwamba, pale Shirika linapohitaji vifaa hivyo hutoa nukuu (quotation) kwa wasambazaji waliotambuliwa kwa ajili ya kuleta ofa zao na baadae huchaguliwa yule aliekidhi vigezo kwa hatua zaidi. Njia hii ilitumika ili

kuokoa muda kwani vifaa hivyo vilihitajika kwa haraka kutokana na uhitaji uliopo kwa wakati huo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii imebaini Uongozi wa Shirika la Umeme kuwa tokea hatua za awali taratibu za Sheria ya Manunuzi zilikiukwa pamoja na kutolewa kwa Adendum nyengine bila ya kuitisha Kikao cha Tender Board.

Kwa mnasaba huo, Kamati ya PAC haukuridhishwa na utekelezaji wa hoja hiina kupelekea kubakia hoja hii

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauagiza Uongozi wa Shirika la Umeme wanapofanya manunuzi ya ndani ni vyema kuhakikisha Sheria, Kanuni na Miongozo inayohusiana na Manunuzi inafuatwa kikamilifu ili kuondokana na upotevu wa fedha za Serikali**.**

SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR (ZPC)

Hoja nambari 4.1.2.1: Kukosekana kwa Mshauri Elekezi katika miradi ya ujenzi ya Shirika la Bandari yenye thamani ya shilingi 12,500,530,762

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kuwa Shirika la Bandari Zanzibar limeingia mikataba ya kazi za ujenzi na wakandarasi mbali mbali yenye thamani ya shilingi 12,500,530,762 bila ya kuwepo au kuchelewa kuajiriwa kwa mshauri elekezi jambo ambalo linaweza kupelekea kutekelezwa kwa miradi chini ya kiwango kilichopangwa au kuchelewa kukamilika kwa miradi iliyokusudiwa kwa wakati. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kuhakikisha wanatafuta washauri elekezi wa miradi ya ujenzi mapema iwezekanavyo kabla ya kuanza kazi za ujenzi kwani ushauri wao unaweza kusaidia katika kutathmini uwezo wa wakandarasi na kutatua mapema changamoto katika miradi hiyo. Mchanganuo wa miradi ya ujenzi iliyotekelezwa bila ya kuwepo kwa Mshauri Elekezi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli nambari 26: Miradi ya Ujenzi iliyoanza kutekeleza bila ya kuwepo kwa Mshauri Elekezi

Jina la Mkataba wa Mradi	Jina la Mkandarasi	Jina la Mshauri elekezi	Thamani ya Mradi (Tshs.)	Tarehe ya Kuanza kwa Mradi	Tarehe ya kuajiriwa Mshauri elekezi
Mkataba wa Ujenzi wa Eneo la kusubiri,Gala na njia Ya Watembea kwa Miguu katika Bandari ya Mkokotoni	Edge Engineering and Consulting (T) Limited	Hakukua na Mshauri Elekezi	1,106,822,520	21/6/2022	--
Mkataba wa kuendeleza Bandari ya Mkoani	China Railway Major Bridge Engineering Group Co. Ltd	Anova Consul-tant Company Limited	5,778,594,226	27/6/2022	22/5/2023
Mkataba wa Ujenzi wa Bandari ya Shumba	Comfix and Engineering Limited	--	5,615,114,016	27/6/2022	3/6/2023
Jumla			**12,500,530,762**		

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Ni sahihi wakati wa ukaguzi Shirika halikua na Mshauri elekezi wa Miradi hio, hata hivyo kabla ya kuanza ujenzi wa baadhi ya miradi hiyo alitafutwa Mshauri Elekezi M/S Anova Consultant kutoka Dar es Salaam wa kusimamia mradi wa Shumba na Mkoani.

Kwa mradi wa Mkokotoni Awamu ya I, kulikua na mshauri elekezi ambaye ni Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA). kwa Awamu ya II ambayo ilikua ni muendelezo (extension) wa Awamu ya I, hakukua na Mshauri elekezi. Aidha, kutokana na changamoto hizo, Shirika limefanya mabadiliko ya watendaji waliokua wakisimamia miradi hiyo.

Aidha, ZPC imekataa kuupokea mradi wa Mkokotoni awamu ya pili na imekubaliana na Mkandarasi wa mradi huo Edge Engineering kufanya marekebisho ya kasoro zote bila ya gharama za ziada kwa Shirika. Pia, Shirika lipo katika hatua za kumuajiri mshauri elekezi kwa ajili ya kusimamia na kuhakikisha kuwa kasoro zote za mradi huo zinarekebishwa bila ya gharama za ziada. Kwa upande wa Mradi wa Mkoani, mshauri alichelewa ila baadae alipatikana na alianza kuupitia hatua zilizofikia hadi kumalizika kwake ambae ni Anova Consultant.

Kwa Mradi wa Shumba, mshauri elekezi alianza nao toka hatua za awali hadi sasa anaendelea nao.

Pamoja na maelezo ya hapo juu, Shirika la Bandari limepokea ushauri wa kumtafuta mshauri elekezi kwa ajili ya kusimamia mradi wa ujenzi wa bandari ya Mkokotoni kwa awamu ya II.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia ukweli wa hoja, Kamati ya PAC imebaini mambo yafuatayo:

1. Ni kweli kwamba wakati wa ukaguzi hakukuwa na Mshauri Elekezi wa Mradi wa Shumba katika kipindi cha Mkataba wa awali hadi Mkataba unamaliza muda wake isipokuwa kulikuwa na Kamati ya Ufundi (Technical Team) ambayo iliundwa na Uongozi wa Shirika la Bandari kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Gati ya Bandari ya Shumba Pemba. Hata hivyo, Kamati ya PAC ilitaka kupatiwa uthibitisho (Barua au Minutes) za kuteuliwa kwa Wajumbe wa Kamati ya Ufundi lakini hadi Kamati inakamailisha kazi zake hakuna kielelezo kilichowasilishwa mbele ya Kamati. Kutokana na kukosekana kwake, Kamati imepata mashaka juu ya usahihi na ukweli wa taarifa zilizotolewa na Uongozi wa Shirika.
2. Kamati imebaini kwamba kulikuwa na ukiukwaji wa masharti yaliyoelezwa ndani ya Mkataba kwamba Mshauri Elekezi alitakiwa atoke nje ya Ofisi badala yake Uongozi wa Shirika ulitumia Watendaji wake wa ndani kuwa ndio Kamati ya Ufundi ya utekelezaji wa Mradi huo.
3. Mradi wa Ujenzi wa Gati ya Bandari ya Shumba haukuweza kukamilika ndani ya muda uliopangwa na kumpelekea Mkandarasi kuongoezewa siku za kufidia muda uliopotea kutokana na changamoto ya kushindwa kufika vifaa kwa wakati na kufanyika malipo kwa wakati uliopangwa.

4. Kutokana na kukosa ufanisi katika utekelezaji wa Mradi huo, Uongozi wa Shirika ulichukua hatua ya kuwaondoa Wajumbe wa Kamati ya Ufundi na kuwapeleka katika Taasisi tofauti za Serikali.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Kamati inaitaka Shirika la Bandari kuhakikisha inaajiri mshauri elekezi kwanzia hatua za awali za mardi hadi kukamilika.
2. Shirika la Bandari lihakikishe linatekeleza kikamilifu masharti ya mkataba.
3. Shirika la Bandari lihakikishe linakamilisha miradi yake kwa wakati kwa mujibu wa mikataba ya utekelezaji wa miradi husika.

Hoja nambari 4.1.2.2: Kuchelewa kuanza kwa mradi wa ujenzi wa bandari ya Shumba

Shirika la Bandari Zanzibar lilingia mkataba wenye kumbukumbu namba SMZ/F123/W/IRB/2021- 2022/44 na kampuni ya M/s Comfix Engineering Limited uliosainiwa tarehe 27 Juni, 2022 kwa thamani ya shilingi 5,615,114,016 pamoja na VAT kwa ajili ya kazi ya usanifu na ujenzi wa Bandari ya Shumba. Kwa mujibu wa kifungu cha 20 cha Masharti Maalum ya Mkataba (SCC), ilibainishwa kuwa utekelezaji wa mradi huo utakuwa ni wa kipindi cha mwaka mmoja (1) kuanzia tarehe 11 Julai, 2022 na kukamilika tarehe 26 Juni, 2023. Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa pamoja na kwamba mkataba wa ujenzi ulishasainiwa lakini hadi ukaguzi unakamilika mnamo tarehe 8 Septemba, 2023 mradi huo bado haujaanza kutekelezwa kama ilivyokubalika. Kuchelewa kuanza kazi za ujenzi wa Bandari ya Shumba kunapelekea kuchelewa kuondosha kero inayowakabili wananchi pamoja na Shirika kushindwa kufikia malengo iliyojiwekea katika mradi huo. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kuendelea kusimamia na kufuatilia kwa karibu kazi za ujenzi wa Bandari ya Shumba ili malengo yaliyokusudiwa yaweze kufanikiwa.

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Pamoja na maelezo ya ukaguzi yanayoonesha kuwa Shirika limechelewa kuanza mradi wa ujenzi wa Bandari ya Shumba, usahihi ni kwamba, mradi wa ujenzi wa Bandari ya Shumba una awamu mbili, ambazo ni usanifu wa michoro na ujenzi, (design and build), hivyo wakati wa ukaguzi, mradi huu ulikuwa umeanza katika hatua ya awali ya usanifu wa michoro ambapo pamoja na usanifu huo, kazi za tafiti (geotechinical investigation, topographic survey na bathymetic survey) zilikuwa tayari zimekamilika na matayarisho ya eneo la ujenzi ‘site preparation’, na uwekaji wa zana na vifaa

vya ujenzi 'Equipment mobilization' zilikua zinaendelea kufanyika. kazi hizo ni sawa na asilimia 30 ya fedha za mradi

Nikweli kuchelewa kuanza kwa miradi kunapelekea kuchelewa kuondosha kero inayowakabili wananchi, pamoja na Shirika kushindwa kufikia malengo iliyojiwekea katika mradi huu, hata hivyo, kuchelewa kuanza kwa awamu ya pili ambayo ni ujenzi wa gati hio, kulitokana na mabadiliko ya michoro ya awali ya gati. Mapendekezo ya michoro mipya yalipelekea ongezeko la gharama za ujenzi. Ili kuepusha ongezeko hilo, Shirika liliamua kuendelea na michoro ya awali hali iliyopelekea kuchelewa kuanza kwa ujenzi wa gati hiyo.

Pamoja na maelezo yaliyoelezwa hapo juu, Shirika limechukua hatua mbalimbali kuharakisha kukamilika kwa mradi huo ikiwemo kuwa na vikao vya mara kwa mara na mshauri elekezi, mkandarasi na uongozi wa Shirika kwa lengo la kuhakikisha mradi huo unakamilika ndani ya wakati.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Baada ya kupokea majibu ya hoja hii, Kamati ya PAC imegundua kwamba katika hatua ya awali Mkataba wa Ujenzi wa Gati ya Bandari ya Shumba ulikuwa na muda wa utekelezaji wa siku 300 kuanzia Juni, 2022 hadi Septemba 2023 lakini Mradi huo haukuweza kutekelezeka. Mnamo mwezi wa Febuari, 2024 Mradi huo uliingia katika utekelezaji halisi ambapo Mkandarasi aliwasilisha ongezeko la gharama za utekelezaji wa Mradi huo kutoka bilioni 5.6 hadi bilioni 12. Hata hivyo, Serikali kupitia Afisi ya Mwanasheria Mkuu ilitoa ushauri wa kuendelea na utekelezaji wa Mradi huo kwa gharama za awali za bilioni 5.6.

Aidha, maelezo mengine kuhusiana na hoja hii ni kama yanavyojieleza katika uchunguzi wa Kamati nambari 4.1.2.1.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Shirika uhakikishe unafuatilia kwa karibu utekelezaji wa Mradi huo ikiwa ni pamoja na kumsimamia Mkadandarasi ili aweze kumaliza utekelezaji wa Mradi huo kwa wakati (ndani ya siku za 'compensation days').

Hoja nambari 4.1.2.3: Kumaliza muda wa dhamana ya Utendaji kazi (Performance security)

Kanuni ya 29(6) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za 2020 inasema "dhamana ya utendaji (Performance Security) itahifadhiwa na taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma hadi kukamilika kwa mkataba na itatolewa baada ya kutolewa kwa cheti cha kukubali ripoti ya mwisho au cheti cha kukamilika kwa kazi au huduma ikiwa hakuna madai yaliyowasilishwa dhidi ya mzabuni, Mdhamini wa mkataba au kampuni ya

udhamini". Mnamo tarehe 27 Juni, 2022 Shirika la Bandari Zanzibar lilisaini mkataba wa shilingi 5,615,114,016 na kampuni ya M/S Comfix and Engineering Limited kwa ajili ya Usanifu na Ujenzi wa Bandari ya Shumba ambao ulitarajiwa kukamilika tarehe 26 Juni, 2023. Kwa mujibu wa mkataba huo Shirika la bandari lilipaswa kulipa malipo ya awali ya shilingi 1,731,752,064 ambapo kampuni ya M/S Comfix and Engineering Limited ilipaswa kutoa dhamana ya utendaji kazi kwa kiasi hicho hicho. Mnamo tarehe 30 Juni, 2022 Kampuni ya M/S Comfix and Engineering Limited iliwasilisha dhamana ya utendaji kazi kutoka KCB Bank Limited kwa ajili ya mkataba huo ambapo Shirika la Bandari pia limefanya malipo ya awali ya shilingi 1,731,752,064 kwa mkandarasi kama inavyotakiwa na mkataba. Ukaguzi ulibaini kuwa dhamana ya utendaji kazi iliyoletwa na kampuni ya M/S Comfix and Engineering Limited kupitia Benki ya KCB ilimaliza muda wake tarehe 25 Juni, 2023 hata kabla ya kazi ya ujenzi kuanza. Kumaliza muda wa dhamana ya utendaji kazi kunaweza kusababisha Shirika la Bandari Zanzibar kutorudishiwa malipo ya awali yaliyolipwa endapo kutatokea madai dhidi ya mkandarasi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kuhakikisha unasimamia kikamilifu mchakato wa ujenzi wa bandari ili hatua za ujenzi zianze kutekelezwa kwa mujibu wa makubaliano yaliyoanishwa katika mkataba pamoja na kuhakikisha kwamba Mkandarasi anawasilisha dhamana mpya ya utendaji kazi kama inavyotakiwa katika mkataba.

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Ni sahihi, wakati ukaguzi unaendelea Dhamana ya utendeji kazi (Performance security) pamoja na dhamana ya malipo ya awali (Advance payment security) ya Mkandarasi ilikua imemalizika muda wake kabla ya ujenzi kuanza. Changamoto hiyo imetokana na mabadiliko ya michoro ambayo haikupata idhini kwa wakati. Hata hivyo, Shirika kabla ya kumalizika kwa mda wa dhamana hizo lilichukua hatua ya kumuandikia barua yenye kumbu kumbu ZPC/BYS/C.125/VOL.1/48 ya tarehe 7/06/2023 na barua ya tarehe 15/05/2023 yenye kumbu kumbu nambari ZPC/BYS/C.125/VOL1 zilizomtaka Mkandarasi kuhuisha nyaraka hizo kabla ya mda wake kuisha.

Pia, Mshauri elekezi alimtaka Mkandarasi kuongeza muda wa dhamana hizo kwa ajili ya muendelezo wa ujenzi ili kukamilisha matakwa ya mkataba kupitia barua yenye kumbu nambari ACC/277/ZPC/SBA/22/KRK/nm-23 ya tarehe 22/09/2023. Aidha, ushauri umepokelewa na Shirika la Bandari Zanzibar linaendelea kuufanyia kazi ambapo imeshamuandikia barua Mkandarasi yakuwasilisha dhamana mpya ya utendaji kazi kama inavyotakiwa katika mkataba.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia ukweli wa majibu ya hoja hii, Kamati imebaini kwamba ni kweli Mkandarasi hakuweza kuwasilisha dhamana ya utendaji kazi (Performance security) pamoja na dhamana ya malipo ya awali (Advance payment security). Hata hivyo, uongozi wa Shirika ulichukua hatua ya kufuatilia kadhia hiyo kwa kumuandikia barua Mkandarasi 'M/S Comfix and Engineering Limited' barua ya tarehe 15/05/2023 yenye kumbu kumbu nambari ZPC/BYS/C.125/VOL1 na barua ya tarehe 7/06/2023 yenye kumbu kumbu ZPC/BYS/C.125/VOL.1/48 zilizomtaka Mkandarasi kuhuisha nyaraka hizo kabla ya muda wake kuisha.

Licha ya juhudi ambazo uongozi wa Shirika ulizichukua dhidi ya Mkandarasi husika, hakuna majibu yaliyowasilishwa na Mkandarasi huyo. Kwa msingi huo, Kamati ya PAC haikuridhika na utekelezaji wa hoja hiyo na kupelekea hoja hii kubakia kwa hatua za ufuatiliaji zaidi.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inautaka Uongozi wa Shirika kuwa makini kabla na wakati wa kuingia makubaliano na Wakandarasi ili kuepusha usumbufu wa kutokukamilishwa kwa baadhi ya matakwa ya sheria zinazosimamia utekelezaji wa Miradi yetu ya Maendeleo nchini.

Hoja nambari 4.1.2.4: Kutokujumuishwa kwa maoni ya Mwanasheria Mkuu katika mkataba wa ujenzi wa Bandari ya Shumba

Kanuni nambari 47(4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za 2020 inaeleza kuwa "Afisa Masuuli atakapo pokea maoni juu ya rasimu ya mkataba kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, atayajumuisha katika rasimu ya mkataba huo". Ukaguzi ulibaini kuwa tarehe 23 Juni, 2023 Shirika la Bandari Zanzibar ilipokea barua kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali yenye kumbukumbu namba L.D902VOL.IV/5 kwa ajili ya rasimu ya mkataba wa ujenzi wa bandari ya Shumba ambayo ilijumuisha maoni sita. Miongoni mwa maoni hayo ni kama ifuatavyo:

a) Shirika inabidi liandae rasimu ya mkataba mpya kwa kutumia hati ya kawaida iliyotolewa na Mamlaka ya Manunuzi Zanzibar. Pia rasimu ya mkataba ieleze kazi mahususi itakayofanywa na mkandarasi na sio kubuni michoro na kujenga.
b) Shirika linapaswa kujiridhisha iwapo mkandarasi aliyepewa kazi hiyo ana uwezo wa kukamilisha kazi hiyo kisheria na kutimiza taratibu za usajili na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar.
c) Shirika hilo lishirikishe kikamilifu Wakala wa Majengo Zanzibar katika ujenzi huo. Baada ya kupitia mkataba kati ya Shirika la

Bandari Zanzibar na kampuni ya M/S Comfix and Engineering Limited unaohusu Usanifu na Ujenzi wa Bandari ya Shumba kwa jumla ya shilingi 5,615,114,016, ukaguzi haukupata ushahidi unaoonyesha kuwa maoni ya Mwanasheria Mkuu yameingizwa kwenye mkataba uliosainiwa. Kutokutekelezwa kwa mapendekezo kutoka kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa rasimu ya mikataba liyowasilishwa kunaweza kusababisha Shirika kuingia katika makubaliano ya mikataba isiyo na tija na hatimae linaweza kupata hasara isiyo ya lazima

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kuhakikisha kuwa mikataba yote ya manunuzi inawasilishwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kabla ya kusainiwa kama inavyotakiwa na kanuni 47(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya 2020 na mapendekezo ya Mwanasheria Mkuu yanafanyiwa kazi na kuingizwa katika mikataba ili kupunguza hatari ya kuingia katika makubaliano ya mikataba ambayo haina tija kwa Serikali.

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Ni sahihi, Shirika la Bandari halikujumuisha maoni ya Mwanasheria Mkuu katika mkataba wa ujenzi wa Bandari ya Shumba. Hata hivyo, Shirika liliyafanyia kazi maoni hayo yote kama ifuatavyo:-

a) Shirika lilitaka ushauri kwa Mamlaka ya Manunuzi juu ya aina ya mkataba wa kusanifu na kujenga (design and Building) kupitia barua yenye kumbu kumbu nambari MUUMU.BA.140/463/09/11 ya tarehe 1/3/2022 waliotujibu ambapo baada ya kukaa nao tuliweza kuwaelezea kwa mradi wa shumba na Mkoani na ilipata maelekezo na ruhusa ya kuweza kutumiaaina hio ya zabuni ijapokuwa wao walitujibu kwa Mkoani tu katika barua yao na hii imetokana na sehemu zote mbili za ujenzi zinaenda sambamba.
b) Shirika lilijiridhisha kwa kwenda kuangalia kazi alizozifanya ikiwemo ujenzi wa gati ya Lindi na ikaridhishwa na kazi waliyoifanya.
c) Ni sahihi Shirika halikumshirikisha ZBA kutoa maoni ya kitaalamu. Hata hivyo, Shirika liliwasilisha nyaraka hizo za usarifu kwa Mshauri elekezi Anova kwa ajili ya kutoa maoni ya kitaalamu, kusimamia pamoja na kufanikisha mradi huu wa ujenzi wa Shumba.

Pamoja na maelezo haya tumeambatahisha ridhaa kutoka mamlaka ya manunuzi (ZPPDA). Uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar umeupokea ushauri na inahakikisha kuwa mikataba yote ya manunuzi inawasilishwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Uongozi wa Shirika la Bandari kukiri kwamba ni kweli ushauri wa Mwanasheria Mkuu haukuingizwa katika Mkataba wa awali wa Ujenzi wa

Gati ya Bandari ya Shumba. Hata hivyo, Mkataba wa awamu ya pili baada ya Mkataba wa awali kumaliza muda wake na kushindwa kutekelezeka, Shirika limeweza kuzingatia ushauri na maoni ya Mwanasheria Mkuu.

Kamati pia imebaini kwamba utekelezaji wa Mradi wa Shumba haukuwemo katika Mpango kazi wa Shirika kwa mwaka 2022/2023. Hata hivyo, Mradi huo uliibuka wakati wa majadiliano ya Watendaji wa Shirika la Bandari pamoja na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma juu ya utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Mkoani. Kupitia kikao hicho, iliamuliwa itumike michoro ya Mradi wa Mkoani katika utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Gati ya Bandari ya Shumba.

Kutokana na maelezo hayo, Kamati ya PAC ilitaka ipatiwe vielelezo vya uamuzi uliofanyika katika kikao hicho lakini kwa bahati mbaya hadi Kamati inakamilisha kazi zake, hakuna kielelezo kilichowasilishwa mbele ya Kamati. Kwa mnasaba huo, Kamati inaendelea kuibakisha hoja hii.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar uhakikishe mikataba yote ya manunuzi inawasilishwa kwa wakati katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu kabla ya kusainiwa kama inavyoelekezwa na Kanuni za Manunuzi ya Umma ya 2020.
2. Uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar uhakikishe Ushauri na Mapendekezo ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu yanafanyiwa kazi ipasavyo na kuingizwa katika mikataba husika ili kuepusha kuingia katika makubaliano ya mikataba ambayo haina tija kwa Serikali.

Hoja nambari 4.1.2.5: Kutokuwepo kwa usimamizi mzuri wa madeni ya wadaiwa wa Shirika shilingi 1,692,860,807.5

Kifungu nambari 30(1)(2) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa Afisa Masuuli atahusika na usimamizi wa mapato ya Taasisi ya Umma na atachukua hatua zinazofaa kuhakikisha uanzishaji na uendeshaji wa mfumo bora na wa ufanisi wa ukusanyaji na wa uhifadhi wa mapato. Aidha, kanuni ya 23(1)(a) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inasisitiza ukusanyaji wa mapato kwa kueleza kuwa Afisa Masuuli atahakikisha kuwa watu wote wanaopaswa kulipa fedha yoyote kama mapato ya Serikali au stahiki yoyote ya Taasisi ya Umma wanapewa notisi ya madai au notisi yoyote ile ya madeni yanayodaiwa kwa wakati huo. Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kuwa Shirika la Bandari Zanzibar linadai jumla ya shilingi 1,692,860,807.5 zitokanazo na utolewaji wa huduma mbalimbali kwa kampuni mbalimbali pamoja na watu binafsi jambo ambalo limepelekea kutokufikiwa kwa malengo yaliokusudiwa. Hali hii imesababishwa zaidi na

kutokuwepo kwa sera za usimamizi wa madeni (receivable management policies) katika Shirika.

Aidha, ukaguzi umebaini kuwa licha ya wadaiwa hao kutokulipa madeni yao ya muda mrefu wanaendelea kupata huduma zote wanazohitaji kutoka kwa Shirika la bandari. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kuanzisha sera za usimamizi wa madeni pamoja na kuzisimamia ili kuboresha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na madeni hayo. Mchanganuo wa baadhi ya wafanyabiashara wanaodaiwa na Shirika la Bandari Zanzibar ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli nambari 27: Wadaiwa wa Shirika la Bandari Zanzibar

Jina la Mdaiwa	**Tarehe ya Ankara**	**Muda wa deni tokea kutolewa Ankara (invoice) hadi tarehe 30 Juni, 2023 (Siku)**	**Bakaa ya deni (Tsh)**
Alghubra			
General Journal	30/06/2022		4,497,090.00
Ankara	30/07/2022	335	2,010,660.00
	30/08/2022	304	578,940.00
	31/10/2022	242	559,606.10
	29/11/2022	213	4,112,836.00
	30/12/2022	182	2,446,872.00
	31/01/2023	150	1,715,889.70
	28/02/2023	122	1,087,164.00
	29/03/2023	93	2,053,233.00
Jumla ndogo(A)			**19,062,290.80**
ALI SALAMA SHIPPING LINE			
General Journal	30/06/2022		2,078,628.00
Ankara	30/07/2022	335	435,714.30
	31/01/2023	150	647,519.00
	28/02/2023	122	565,561.95

	28/02/2023	122	6,323,850.00
	45126	115	8,046,090.00
	29/03/2023	93	1,047,100.30
Jumla Ndogo(B)			**19,144,463.55**
AZAM MARINE PEMBA			
Ankara	30/08/2022	304	4,948,922.00
	30/08/2022	304	1,698,205.00
	30/09/2022	273	5,347,132.00
	30/09/2022	273	2,344,528.00
	31/10/2022	242	1,567,427.00
	31/10/2022	242	5,220,172.00
	31/10/2022	242	664,424.00
Payment	21/11/2022		-78,821.00
Jumla Ndogo(C)			**21,711,989.00**
Jumla kuu(A+B+C)			**59,918,743.35**

Aidha, ukaguzi umebaini uwepo wa madeni ya muda mrefu ambayo yanatia shaka juu ya ulipwaji wake kutokana na wadaiwa kutokufanya juhudi za ulipaji wa madeni yao jambo ambalo limepelekea kuwepo kwa kiwango kikubwa cha fedha zinazodaiwa na Shirika. Hali hii inaweza kupelekea kukosekana kwa baadhi ya huduma muhimu ambazo zingeweza kutekelezeka iwapo fedha zinazodaiwa zingeweza kulipwa kwa wakati. Mchanganuo wa madeni ambayo yanatia shaka juu ya ulipwaji wake ni kama inavyooneakana katika jadweli hapo chini:

Jadweli nambari 28: Wadaiwa wa muda mrefu

Jina la Mdaiwa	**Tarehe iliyotolewa huduma.**	**Kiasi cha deni (Tshs)**

Anna Shipping	30/06/2022	94,629,415.16
Azam Marine		52, 334, 394.25
BP Ltd		37,608,470.35
Jack Enterprises		156,608,868.00
Kamal		57,357,105.75
Kilimanjaro First Feries		29,672,626.25
Nanai Co Ltd		41,718,154.00
Saqar General Trader		29,686,440.00
Sohar General Trader		173,303,007.00
Tropical Air		91,642,505.20
United Trader Enterprises Tzs		438,412,069.00
Mansour Abeid	27/06/2023	39,436,824.60
K.F.F Marine Services	22/06/2023	29,255,284.00
Saqar General Trader	30/03/2023	508,240,710.00
Jumla ndogo		**1,632,942,064.15**

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Ni sahihi kwamba Shirika la bandari halina sera na miongozo ya usimamizi wa madeni. Hata hivyo Shirika limekua likifanya juhudi mbali mbali za kufuatilia madeni ya Shirika. Miongoni mwa juhudi hizo ni

- Kuwepo kwa rasimu ya sera ya madeni
- Kuundwa kwa kamati maalumu ya ufuatiliaji wa madeni
- Shirika kupeleka watendaji wake TPA kwa lengo la kuwapatia elimu ya namna bora ya kukabiliana na madeni.
- Kuwaandikia barua wadaiwa wa Shirika la Bandari kupitia Kamati ya madeni kwa lengo kuwakumbusha madeni yao na kuwashauri juu ya namna bora ya ulipaji wa madeni yao.
- Kuchukua mshauri elekezi kwa ajili ya kuja kutengeneza utaratibu wa utoaji wa Ankara pamoja na ufuatiliaji wa huduma zinazotolewa kwa wateja.

Kwa juhudi hizo zilizozochukuliwa, tumeweza kupunguza baadhi ya madeni. Pia, Shirika linaendelea kufanya vikao vya pamoja na wateja wake kwa lengo la kuangalia jinsi gani watayalipa madeni yao pamoja na kuandaa mikataba ya ulipaji wa madeni hayo. Vilevile, Shirika limeandaa utaratibu wa mteja kufanya malipo kwanza (Interim payment) kabla ya kupatiwa huduma kwa lengo la kuepusha usumbufu.

Aidha, Shirika limechukua juhudi za makusudi kwa kuiomba Bodi ya Wakurugenzi kutoa msamaha kwa madeni yasiolipika ili kuweka sawa hesabu za Shirika. Pamoja na Maelezo haya, kumeambatanishwa barua za kukumbushia madeni na hadidu rejea za kamati ya kufuatilia madeni.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika uchunguzi wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini mambo makubwa yafuatayo:

1. Kwa kupitia Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka, Kamati imegundua kuwa Shirika linadai kwa Wadaiwa wa ndani jumla ya shilingi bilioni 15 na sio bilioni 1.7 kama ilivyooneshwa katika hoja ya Mkaguzi ambapo hadi kamati inakamilisha kazi zake, jumla ya bilioni 3.2 zimelipwa.
2. Shirika la Bandari halina sera ya usimamizi wa madeni kwa Wadaiwa wao.
3. Faida ya Shirika la Bandari imeshuka kutoka bilioni 12 kwa mwaka 2022 ukilinganisha na bilioni 7 kwa mwaka 2023. Hali hiyo imetokana na kuewepo kwa deni kubwa ambalo Bandari inadaiwa.
4. Shirika limepanga kuanzisha mfumo wa kufanya malipo kwanza kabla ya kupatia huduma.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Shirika lihakikishe linafatilia kwa karibu madeni yake inayodai kwa taasisi nyengine na kuchukua hatua za kisheria endapo italazimika kufanya hivyo.
2. Shirika la Bandari ihakikishe inaanda Sera ya Usimamizi wa madeni yake.
3. Kamati inaiagiza Shirika la Bandari kuhakikisha inalipa madeni inayodaiwa ili kuweza kuengeza ufanisi katika utekelezaji wa shughuli zao za kila siku.
4. Shirika lihakikishe linachukua juhudi za haraka kutekeleza mpango wa kuhakikisha malipo yanafanywa kabla ya kukatiwa huduma.

Hoja nambari 4.1.2.6: Kukosekana kwa kumbukumbu za vikao vya kamati ya misamaha na madai

Kanuni nambari 40(2) ya Kanuni za Fedha za Shirika la Bandari Zanzibar kinaeleza kuwa Mkurugenzi wa Fedha kwa kushauriana na Mkurugenzi Mkuu wanaweza kusamehe kiasi kisichozidi asilimia 25 ya deni la huduma ya tozo ya uhifadhi wa mzigo. Ikiwa msamaha ulioombwa ni zaidi ya asilimia 25 ya deni hilo, maombi hayo yatafikishwa kwa kamati ya madai na misamaha kwa kujadiliwa na kupatiwa maamuzi.

Ukaguzi umepitia taarifa mbalimbali zinazohusiana na msamaha wa tozo za uhifadhi zilizotolewa kwa wafanyabiashara tofauti na Shirika la Bandari Zanzibar na kukosa uthibitisho kuwa misamaha hiyo ilitolewa baada ya idhini ya kamati husika. Aidha, tuliona udhaifu katika udhibiti wa ndani kutokana na ukweli kuwa Mkurugenzi Mkuu na Mkurugenzi wa Fedha wamepewa uwezo wa kusamehe hadi asilimia 25 ya tozo ya uhifadhi wa mzigo. Hii inaweza kutumika kama mwanya iwapo Mkurugenzi Mkuu na Mkurugenzi wa Fedha watakuwa na mgongano wa kimaslahi katika ombi la msamaha wa kodi husika. Aidha, ukaguzi umekosa taarifa juu ya kiasi halisi kilichosamehewa kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Hali hii inaweza kupelekea Shirika kukosa mapato kutokana na kuwepo kwa mianya ya kusamehe tozo ya uhifadhi wa mzigo. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kuweka udhibiti mzuri wa utoaji wa misamaha ya tozo ya uhifadhi mizigo ikiwa ni pamoja na kuweka vizuri kumbukumbu za taarifa zote zinazohusu misamaha hii. Aidha Shirika ni vyema likaainisha mapema sababu zinazofaa kuzingatiwa katika kutoa misahama ya tozo na misamaha mengineyo. Mchanganuo wa baadhi ya makampuni yalioomba misamaha ya tozo ya uhifadhi mizigo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli nambari 29: Orodha ya walioomba misamaha ya tozo

Jina la kampuni.	Kiwango anachodaiwa (Tshs)	Kiwango cha asilimia iliyosamehewa (%)
Salalah Investment Ltd Company	5,597,280.00	15
Hamza Brother General Supply	8,684,800.00	25
Darajani General Tyres	1,736,960.00	25
Khamis Ali Khamis	7,518,700.00	Haijaainishwa
Abrahmani Ali Juma	2,583,360.00	25
Hafidh Talib Omar	22,066,200.00	25
Iri Clearing And Forward	3,437,120.00	25
Muslih Ali Ali	24,274,660.00	Haijaainishwa
Mourib And Mouhib	14,392,940.00	Haijaainishwa
Milan Heilmann	8,163,160.00	Haijaainishwa
Turky Petroleum	43,314,750.00	50

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Ni sahihi Kanuni za fedha ya Shirika imeweka utaratibu wa namna ya kusamehe madeni yatokanayo na huduma ya uhifadhi wa mizigo. Kwa

kawaida Shirika lina utaratibu wa kupokea maombi ya wateja wake wanaomba misamaha ya ada ya uhifadhi wa mizigo, utaratibu huo Mteja anapowasilisha ombi la msamaha wa tozo za uhifadhi wa mizigo, uongozi wa Shirika kupitia kitengo cha fedha na mkurugenzi mkuu wanatathmini maombi hayo, ikiwa mteja maombi yake yapo chini ya asilimia 25 mkuu wa kitengo cha fedha kwa kushauriana na Mkurugenzi Mkuu wana uwezo wa kumsamehe mteja huyo pasi na kuwasilishwa maombi hayo kwenye Kamati ya Msamaha, barua ya Mkurugenzi Mkuu inatosha kukamilisha msamaha wa tozo iliyoombwa.

Aidha, maombi ya mteja yanapozidi asilimia 25, kamati ya msamaha inakaa na kutathmini maombi ya msamaha yaliyoombwa. Kupitia orodha ilioneshwa na Mdhibiti asilimia 90 ya maombi yalioneshwa yapo chini ya asilimia 25, kwa maana maombi hayo yalitekelezwa kwenye ngazi ya Mkurugenzi wa Fedha akishauriana na Mkurugenzi Mkuu, hakukuhitajika kuwekwa kumbukumbu za vikao kudhibitisha idhini ya Kamati kwani barua za viongozi hao zilitosheleza. Ombi moja la Turkey Petroleum ndio lilizidi asilimia 50, kupitia ombi hilo Kamati ya msamaha ilikaa kikao kujadili ombi lake na kufanya maamuzi pamoja na kuweka kumbu kumbu za kikao hicho.

Shirika linaungana na maelezo ya ukaguzi kuhusiana na udhaifu uliopo katika kanuni kwa kumpa mamlaka Mkurugenzi Mkuu na Mkurugenzi wa Fedha kwa kufanya maamuzi ya maombi ya msamaha kwa kiwango kisichozidi asilimia 25 kwa kuzingatiwa changamoto hiyo Shirika linaipitia upya Kanuni yake ili kuondoa mamlaka waliyopewa Mkurugenzi Mkuu na Mkurugenzi fedha ya kusamehe tozo hadi asilimia 25.

Aidha Uongozi wa Shirika ulikuwa na utaratibu wa kuwasilisha taarifa za msamaha kwenye bodi ya wakurugenzi hata hivyo Shirika linakiri kutowasilishwa kwa taarifa za msamaha kwa kipindi cha mwaka mmoja wa fedha 2022/2023.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa kwa vile shughuli za uendeshaji wa Bandari umeamuliwa kukabidhiwa kwa Muwekezaji binafsi ambapo kumbukumbu za vikao vya Kamati ya misamaha na madai inafanywa na kuhifadhiwa na Mwekezaji huyo. Hivyo, Shirika la Bandari Zanzibar halikuwa na kumbukumbu hizo. Hata hivyo, Kamati ya PAC ilihitaji kupatiwa asilimia ya misamaha ya tozo pamoja na madai iliyotolewa pamoja na maoni na ushauri wa Mwanasheria Mkuu kuhusiana na makubaliano yaliopo ya SHirika na Mwekezaji juu ya misamaha na madai iliyokuwepo kabla ili iweze kujiridhisha kuhusiana na uhalisia wa hoja hii lakini hadi Kamati inakamilisha kazi zake haikuweza kupatiwa kielelezo hicho. Kwa vile Shirika hivi sasa halishughulikii misamaha na madai, Kamati imeiondoa hoja hii.

Hoja nambari 4.1.2.7: Kushindwa kukusanya tozo ya mizigo na ada ya kukodisha ghala shilingi 546,795,243.75

Kifungu nambari 57(1-3) cha Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2004 kinataka wakati bidhaa yoyote itauzwa kwa mnada wa umma, basi mapato ya mauzo hayo yatatumika kwa utaratibu uliowekwa hapa chini katika utekelezaji wa ushuru, gharama za mauzo, kodi mbalimbali, tozo za forodha pamoja na ushuru wa bandari

Ukaguzi ulibaini kuwa, mnada wa hadhara unaofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) haukuzingatia utaratibu uliotajwa na Sheria, kwani Shirika la Bandari Zanzibar limekuwa halirejeshewi mapato wanayodai kutokana na mizigo iliyopigwa mnada ikiwemo gharama za kodi ya ghala na uhifadhi za mizigo. Ukaguzi umebaini kuwa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2023,

Tokea Septemba 2023 baada ya Shirika kusaini mkataba na Kampuni Endeshaji ya ZMT huduma za uhifadhi wa mizigo zimehamishiwa kwa muwekezaji huyo. Shirika la Bandari lilikuwa linadai malipo yenye jumla ya shilingi 546,795,243.75 kutoka kwa wafanyabiashara walioshindwa kutoa mizigo yao mapema na kulazimu Mamlaka ya Mapato Tanzania kupiga mnada wa mizigo yao. Hali hii inalifanya Shirika kushindwa kupata mapato yake stahiki licha ya kutoa huduma kwa wafanya biashara wenye mizigo husika. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kukaa pamoja na uongozi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania tawi la Zanzibar kwa ajili ya kujadili na kutafuta namna bora ya kutatua tatizo hili kwa maslahi ya pande zote mbili. Mchanganuo wa Madeni yaliyoshindwa kulipwa kutokana na kupigwa mnada na Mamlaka ya Mapato Tanzania ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli nambari 30: Orodha ya madeni yaliyoshindwa kulipwa

Namba ya Kontena	Ukubwa (ft)	Siku	Gharama za Storage (Tshs)	Gharama za Liftings (Tshs)	Jumla (Tshs.)
DFSU 773821-6	40	105	20,962,200	227,268.75	21,189,468.75
CLHU 904320-0	40	105	20,962,200	227,268.75	21,189,468.75
TCHU 881341-9	40	105	20,962,200	227,268.75	21,189,468.75
AMFU 878152-0	40	105	20,962,200	227,268.75	21,189,468.75
DSAU 949686-1	40	105	20,962,200	227,268.75	21,189,468.75
APZU 321336-0	20	139	14,117,400	133,687.50	14,251,087.50
DFSU 771716-8	40	139	28,234,800	227,268.75	28,462,068.75
CMAU 698686-2	40	158	32,298,900	227,268.75	32,526,168.75
MRSU 309393-4	40	153	31,229,400	227,268.75	31,456,668.75
MSKU 870976-5	40	122	24,598,500	227,268.75	24,825,768.75
TCNU 414739-8	20	210	21,710,850	133,687.50	21,844,537.50
TCKU 207477-7	20	210	21,710,850	133,687.50	21,844,537.50
DRYU 291366-0	20	210	21,710,850	133,687.50	21,844,537.50
TCKU 218493-1	20	179	18,395,400	133,687.50	18,529,087.50
DFSU 307830-4	20	169	17,325,900	133,687.50	17,459,587.50
DFSU 619132-0	40	154	31,443,300	227,268.75	31,670,568.75
RFCU 501377.3	40	154	31,443,300	227,268.75	31,670,568.75
DFSU 752799-9	40	120	24,170,700	227,268.75	24,397,968.75
FCIU 820678-6	40	120	24,170,700	227,268.75	24,397,968.75
ESPU 801922-8	40	120	24,170,700	227,268.75	24,397,968.75
RFSU 501643-2	40	120	24,170,700	227,268.75	24,397,968.75
DRYU 966710-5	40	120	24,170,700	227,268.75	24,397,968.75
DRYU 994833-4	40	111	22,245,600	227,268.75	22,472,868.75
Jumla					**546,795,243.75**

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Shirika la Bandari lilifanya jitihada ya kuwaandikia TRA taarifa za makontena yaliyokaa mda mrefu bandarini na kupelekewa kwao saateni. Katika barua hio kulikuwa na madai ya lifting charges za kubebea kontena hilo kutokea Malindi kwenda saateni.
Pamoja na madai ya storage ya makontena hayo kipindi yapo Bandari ya

Malindi Shirika halikupata mrejesho wa madai hayo likafanya jitihada nyengine ya kikao baina yao na baadhi ya wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Bandari ili kusainiana kuhusu ugawaji wa fedha zinazopatikana baada ya mnada wa makontena hayo.

Zoezi hilo halikuendelea kutokana na uwekezaji wa bandari katika usimamizi wa makontena kuhamia kwa muekezaji ZMT. Pamoja na maelekezo haya naambatanisha na list ya makontena tulodai na barua iliopelekwa ya madai.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

1. Shirika la Bandari hupata shida katika kukusanya tozo za kukaa kwa mizigo kwa muda mrefu Bandarini (overstay storage) kwa vile Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hupiga mnada na kufidia gharama zao bila kuzingatia tozo za ghala ambazo Shirika la Bandari linatakiwa kukusanya.
2. Shirika la Bandari limeshandaa utaratibu wa kuwa na sehemu yake ya kuhifadhia mizigo ambapo minada yote ya mizigo iliyokaa Bandarini kwa muda mrefu itaweza kufanyiwa mnada hapo na Shirika la Bandari litaweza kupata tozo zake linalostahiki.
3. Hakuna mashirikiano baina ya Shirika la Bandari na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) katika utaratibu mzima wa mgawanyo wa tozo za “overstay storage”.
4. Shirika la Bandari linaidai TRA jumla ya Tsh 546,795,243.75 ikiwa ni malipo ya sehemu ya fedha yanayotokana na mnada wa mizigo inayopigwa mnada na Mamlaka ya Mapato Tanzania ambapo Shirika mnamo tarehe 15/08/2022 iliiandikia barua Mamlaka ya Mapato Tanzania kuhusu ulipaji wa deni hilo, na hadi Kamati inamaliza uchunguzi wake, deni hilo bado halijalipwa.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Kamati inalitaka Shirika la Bandari pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania, kushirikiana kwa karibu katika utekelezaji wa majukumu yao hususani katika mgawanyo wa tozo za mizigo inayopigwa mnada.
2. Shirika la Bandari kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na Afisi ya Rais, Fedha na Mipango zikutane kujadili na kuhakikisha deni ambalo TRA inadaiwa na Shirika la Bandari linalipwa.
3. Shirika la Bandari lihakikishe minada yote ya mizigo iliyokaa muda mrefu inapigwa ndani ya eneo ambalo limeliandaa na linalimiliki.

SHIRIKA LA BANDARI PEMBA

Hoja nambari 4.1.2.8: Malimbikizo ya Madeni ya Mapato shilingi 226,165,354.96

Kifungu nambari 29(1)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa “Afisa Mhasibu wa Taasisi ya Umma atahusika na kusimamia madeni ya Taasisi ya Umma”. Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Bandari Tawi la Pemba linazidai Kampuni Binafsi za Usafirishaji na baadhi ya taasisi za Serikali jumla ya shilingi 226,165,354.96 kutokana na utoaji wa huduma mbali mbali bandarini. Madeni hayo ni ya muda mrefu na hakuna hatua zilizobainika na ukaguzi ambazo zimechukuliwa na Shirika katika kudai madeni hayo, jambo ambalo ni kuikosesha Serikali mapato ambayo yangetumika katika utekelezaji wa shughuli za Serikali ikiwemo miradi ya maendeleo, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria kilichonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari Pemba kuongeza umakini katika kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kufanya ufuatiliaji wa madeni ili yaweze kuongeza mapato Serikalini. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli nambari 31: Malimbikizo ya madeni ya mapato ya muda mrefu

Namba	Mdaiwa	Deni halisi (Tshs)
1.	Wakala wa Barabara	198,375.00
2.	ZIPA	2,415,690.00
3.	GAPCO	9,255,080.26
4.	Shirika la Meli Zanzibar	40,675,392.20
5.	Azam Marine	117,520,296.90
6.	Zanzibar Fast Feries	56,100,520.60
Jumla		**226,165,354.96**

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Shirika la bandari umeandaa team ya kufuatilia na kuhakikisha madeni haya yanalipwa kwa yale yanayolipika na kwa yale yasiyolipika kutokana na sababu tofauti yatafutwa kupitia waraka utakao wasilishwa kwenye bodi ya wakurugenzi ya Shirika.

Pia, Shirika limeandaa sera ya mikopo (credit policy) ambayo vitasaidia udhibiti wa madeni, Hata hivyo Shirika kupitia kitengo cha fedha kinafuatilia madeni kwa kuwaandikia barua wadaiwa na kuwafata ana kwa ana na kwa sasa tumejipanga kufanya mikakati ya malipo kwa wadaiwa wote wa Shirika. Deni ni malimbikizo ya madeni za zamani, baadhi ya madeni hayo uwezekano wa kuyalipa ni mdogo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya juhudi ambazo Uongozi wa Shirka la Bandari Pemba za kuwaandikia barua na kufanya vikao vya pamoja na Wadaiwa wa madeni ya Shirika. Kamati imebaini kuwa hakuna deni lolote ambalo Mkaguzi ameliainisha katika Ripoti yake ya mwaka 2022/2023.

SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA ZANZIBAR

Hoja nambari 4.1.5.1: Mkataba unaotekelezwa bila ya kuwasilishwa dhamana ya utendaji kazi (perfomance Security)

Kanuni namba 29(1) ya kanuni za Ununuzi ya Umma ya 2020 inamtaka Mzabuni aliyeshinda zabuni kuwasilisha gharama ya utendaji kazi (Performance Security) ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa mkataba wake.

Shirika la Meli la Zanzibar limeingia mkataba na kampuni ya Zanzibar Agency Tally (ZAG-TAC) kwa ajili ya Utoaji wa Huduma za Ufuatiliaji wa mwenendo wa makontena (tracing and tracking), huduma za ulinzi pamoja na uthibitishaji wa taarifa za makontena (Tallying) katika bandari ya Malindi Zanzibar.

Kifungu cha 28 cha mkataba kati ya Shirika la Meli la Zanzibar na Zanzibar Agency Tally (ZAG-TAC) kinaeleza kuwa Mtoa Huduma (ZAG-TAC) atawasilisha dhamana ya utendaji kazi kwa mwajiri (Shirika la Meli la Zanzibar) kabla ya tarehe iliyoainishwa katika barua ya kukubali zabuni hiyo. Dhamana ya utendaji kazi itatolewa katika kiasi, aina na benki au mdhamini anayekubalika kwa mwajiri, na kujumuishwa katika aina na uwiano wa sarafu ambayo bei ya mkataba inayolipwa.

Ukaguzi umebaini kuwa Mtoa huduma (ZAG-TAC) hakuwasilisha dhamana ya utendaji kazi (Performance Security) kwa Mwajiri (Shirika la Meli la Zanzibar) licha ya ukweli kuwa Mtoa Hudumabado anendelea na utekelezaji wa majukumu yake.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 28 cha mkataba baina ya Shirika la Meli la Zanzibar na Kampuni ya Zanzibar Agency Tally (ZAG-TAC) na kupelekea Shirika kukosa kidhibiti endapo Mtoa Huduma atashindwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar kuzingatia miongozo ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya 2020 pamoja na masharti ya Mkataba ili kuhakikisha maslahi ya Serikali yanapatikana katika utekelezaji wa mikataba.

Kifungu cha 28 cha mkataba kati ya Shirika la Meli la Zanzibar na Zanzibar Agency Tally (ZAG-TAC) kinaeleza kuwa Mtoa Huduma (ZAG-TAC) atawasilisha dhamana ya utendaji kazi kwa mwajiri (Shirika la Meli la Zanzibar) kabla ya tarehe iliyoainishwa katika barua ya kukubali zabuni hiyo. Dhamana ya utendaji kazi itatolewa katika kiasi, aina na benki au mdhamini anayekubalika kwa mwajiri, na kujumuishwa katika aina na uwiano wa sarafu ambayo bei ya mkataba inayolipwa.

Ukaguzi umebaini kuwa Mtoa huduma (ZAG-TAC) hakuwasilisha dhamana ya utendaji kazi (Performance Security) kwa Mwajiri (Shirika la Meli la Zanzibar) licha ya ukweli kuwa Mtoa Huduma bado anendelea na utekelezaji wa majukumu yake.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 28 cha mkataba baina ya Shirika la Meli la Zanzibar na Kampuni ya Zanzibar Agency Tally (ZAG-TAC) na kupelekea Shirika kukosa kidhibiti endapo Mtoa Huduma atashindwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar kuzingatia miongozo ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya 2020 pamoja na masharti ya Mkataba ili kuhakikisha maslahi ya Serikali yanapatikana katika utekelezaji wa mikataba.

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Shirika lilichukua hatua ya kuwaeleza Kampuni ya ZAG-TAC kuwasilisha Dhamana ya utendaji kazi. Kampuni hiyo imejibu kwa barua ya tarehe 12/02/2024 wakieleza kuwa wataiwasilisha Dhamana hiyo. Hata hivyo, katika barua yao Kampuni hiyo imeeleza kuwa hawakuwasilisha dhamana ya utendaji kazi baada ya kuona kuwa katika Mkataba kuna 'Perfomance penalty' hivyo waliona kuwa 'performance' hiyo inachukua jukumu la dhamana ya utendaji kazi. Kampuni hiyo imesema itawasilisha Dhamana hiyo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, Kamati imebaini kwamba wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake ni kweli Mkataba unaotekelezwa bila ya kuwasilishwa dhamana ya utendaji kazi (perfomance Security) kama ilivyoelekezwa na kifungu cha 28 cha mkataba baina ya Shirika la Meli la Zanzibar na Kampuni ya Zanzibar Agency Tally (ZAG-TAC). Hata hivyo, kazi hiyo tayari imeshakamilisha kwani ilianza tarehe 25/4/2022 hadi tarehe 25/4/2024. Aidha, kwa bahati nzuri Kampuni hiyo ilikamilisha kazi bila ya kuwepo kwa kasoro yoyote.

Kwa vile Mkataba huu umeshakamilika, Kamati imelielekeza Shirika kuhitaji cheti cha kukamilisha utekelezaji wa kazi iliyopewa Kampuni ili Mkaguzi aweze kujiridhisha na kuiondoa hoja hii.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Kamati inalitaka Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar kutekeleza vifungu vya Mkataba yake hususan vinavyohusiana na dhamana ya utendaji kazi ili kuepuka changamoto katika utekelezaji Mkataba inajitokeza.

2. Shirika lihakikishe linawasilisha na kutekeleza ushauri unaotolewa na Mwanasheria Mkuu kwa vile ndio muhusika Mkuu wa mikataba ya Serikali na Taasisi zake.
3. Shirika lihakikishe linafuatilia cheti cha kukamilisha kazi aliyopewa (certificate of completion) kwa Kampuni ya Zanzibar Agency Tally (ZAG-TAC) ili Shirika liwe na ithibati ya utekelezwaji wa kazi ya Utoaji wa Huduma za Ufuatiliaji wa mwenendo wa makontena (tracing and tracking).

Hoja nambari 4.1.5.2: Wasiwasi juu ya ulipwaji wa deni kutoka Kampuni ya GBP Tanzania shilingi 1,406,195,716.28

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar limeingia katika makubaliano ya mikataba ya ukodishwaji wa meli yake ya MT UKOMBOZI na Kampuni ya GBP TANZANIA. Makubaliano hayo yalikuwa ni ya ukodishwaji meli kwa kodi ya safari (voyage charter) ambapo malipo ya ukodishwaji hulipwa kwa kuzingatia uzito wa mzigo (wa mafuta) uliobebwa katika safari husika.

Wakati wa ukaguzi wetu, ilibainika kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 kampuni ya GBP Tanzania ltd ilikuwa inadaiwa na Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar deni lenye jumla ya shilingi 1,406,195,716.28 ambalo limebakia bila ya kulipwa kwa muda wa zaidi ya mwaka mmoja. Ukaguzi umebaini kuwa deni hili limesababishwa kutokana na kutokukubaliana baina ya Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar na Kampuni ya GBP juu ya vipimo vinavyotumika katika upimaji wa uzito wa mafuta.

Uwepo wa deni hili kumesababisha Shirika kukosa fedha ambazo zingelisaidia Shirika katika uendeshajiwa kazi zake za kila siku.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar kwa kushirikiana na taasisi nyengine za Serikali ikiwemo ZURA na ZBS kukaa pamoja na Kampuni ya GBP ili kutafuta ufumbuzi wa suala hili ili hatimae fedha ya deni la Shirika iweze kukusanywa.

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Kampuni ya Gulf Bulk Petroleum (GBP) ilikuwa ikipeleka madai yake ya upotevu wa mafuta kupitia meli ya MT Ukombozi II juu yatofauti ya kipimo cha mafuta kati ya bandari ya Tanga, Dar na Zanzibar. Wakati huo hakukuwa na makubaliano ya kulinganisha kipimo kitakachotumika katika kupima mafuta ambacho ni UTI au Radar. Kipimo kilichokuwa kikitumika wakati wa kupakia mafuta melini, kilikuwa tofauti na kipimo kilichotumika wakati wa kushusha mafuta Zanzibar. Pamoja na kuripoti jambo hili kwa Uongozi wa meli, Kampuni ya GBP ilipaswa kuujulisha Uongozi wa Shirika la Meli juu ya changamoto hiyo ya nani anayepunguza kiwango cha malipo kwa mujibu wa upotevu wa mafuta uliotokea.

Wakati wa malipo, Shirika lilikuwa linapokea malipo pungufu ikilinganishwa na Ankara zilizotolewa na Shirika bila ya kuwa na maelezo ya ziada juu ya mapungufu hayo. Katika kulitafutia ufumbuzi wa suala hili, Shirika lilianza kwa kuwasiliana na GBP ili kupata maelezo ya kina kwanini wanafanya malipo pungufu. Kampuni ya GBP ilieleza kuwa wanalipa kwa mujibu wa kipimo cha UTI ambacho ndicho kilichokubalika na ZURA.

Shirika lilikuwa likiwasiliana mara kwa mara na ZURA kwa kuwa ni Msimamizi wa usafirishaji wa mafuta na pia ndio mwenye Mkatabana GBP.

Shirika halikuridhika na jawabu hilo na likachukua hatua ya kutaka kuwa na kikao cha pamoja ili kutatua changamoto hiiya malipo iliyojitokeza bila ya mafanikio. Shirika likaiomba ZURA waitishe kikao cha pamoja baina ya SHIPCO, GBP na ZURA akiwakamaMsuluhishi.Hatahivyo, kikaohichohakijafanyika. Kablayahatuahii, Shirikaliliwasilianana ZURAna ZBS ili kuona uhalisia wa kadhia hiyo na kwamba Shirika kama linaweza kuokoa sehemu ya malipo hayo.

Shirika pia liliandika ZURA barua yenye Kumb. No. AB.244/252/01/45 ya tarehe 15/07/2023 yenye lengo la kukumbushia kikao cha pamoja kilichoombwa na Shirika kwa barua nambari AB.244/252/01/31 ya tarehe 04/01/2023 na barua AB.244/252/01/35 tarehe 07/02/2023.

Aidha, Shirika liliandikia ZURA barua yenye Kumb. No. AB.244/252/01/46 ya tarehe 02/03/2023 likiomba kikao cha pamoja baina ya ZURA, ZBS, SHIPCO, ZAWEMA na GBP kufanya mkutano kwa kutumia 'ZOOM' katika Mamlaka ya ZURA ifikapo tarehe 07/09/2023 saa 4 kamili asubuhi. Hata hivyo, barua hiyo haikujibiwa na ZURA.

Shirika pia katika kutafuta haki yake liliiandikia ZURA barua yenye Kumb. No. AB.244/252/01/47 ya tarehe 05/10/2023 kuomba iridhie wazo la Shirika la kutuweka pamoja na GBP ili kutafuta Msuluhishi. Hata hivyo, hakuna majibu ya ZURA katika ombi hilo la Shirika.

Katika kuendelea kulitafutia ufumbuzi deni hili, Shirika liliwasiliana na CAG kuhusu suala hili kwa barua yenye Kumb No.AC.19/272/01/52 ya tarehe 01/01/2024 yenye kuomba ushauri juu ya deni ambalo Shirika linaamini linadai Kampuni ya GBP. Kwa sasa Shirika linasubiri kupata majibu ya barua hiyo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kwamba ni kweli Shirika linaidai Kampuni ya GBP jumla ya shilingi 1,406,195,716.28 ikiwa ni deni lililotokana na kuwepo utofauti katika vipimo vipimo vilivyokuwa vikitumika wakati wa upakiaji na ushushaji wa mizigo. Licha ya juhudi zilizochukuliwa na Shirika na ili kulipatia ufumbuzi suala hili na Shirika kupata haki yake ya kulipwa deni inalodai, Kamati imepanga kufaya kikao na ZURA, SHIPCO pamoja na

kampuni ya GBP kulizungumzia kwa udani suala hili na kulipatia ufumbuzi. Kwa msingi huu, hoja hii inaendelea kubakia hadi Kamati itakapopata majibu kutoka pande zote mbili na kujiridhisha kufanyika kukamilishwa malipo ya deni la Shirika.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inaitaka ZURA kwa kushirikiana na Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar kuhakikisha wanahakikisha deni la shilingi 1,406,195,716.28 linafuatiliwa na kulipwa.

Hoja nambari 4.1.5.3: Kutokuwepo kwa Mkataba baina ya Shirika la Meli Zanzibar na Kampuni ya ZALAGACO

Kanuni ya 83(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya 2020 inaeleza kuwa Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za umma itawajibika kwa usimamizi mzuri wa mkataba wa ununuzi wowote wa bidhaa, huduma au kazi za ujenzi. Aidha, kifungu nambari 63(3) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba "kukubaliwa kwa zabuni kutaidhinishwa kwa mkataba wa maandishi utakaosainiwa na pande zote mbili Mtoa huduma na Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji …"

Ukaguzi umebaini kuwa Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar lilikuwa likiilipa kampuni ya ZALAGACO kwa huduma mbalimbali wanazozitoa za ufungaji na ufunguaji makontena ya Shirika pasi na kuwepo kwa makubaliano halali ya mkataba kwani mkataba uliopo tayari umeshapita muda wake.

Kwa kukosekana makubaliano baina ya pande hizo mbili kuna uwezekano huduma zisitolewe kama Shirika linavyotarajia. Aidha huwa ni vigumu kwa Shirika kuweza kutatua mgogoro pindi utakapoibuka.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar kuhakikisha kunakuwepo mkataba halali baina yake na Mtoa huduma ili kuhakikisha Mtoa huduma anatoa huduma kwa mujibu wa makubaliano.

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Kampuni ya ZALAGACO ambayo kwa kipindi kirefu ndio inayotekeleza shughuli za kufunga na kufungua makontena kwenye meli inafanya shughuli hizo bila kuwa na mkataba kwa sababu ifuatayo; Kimsingi, Shirika la Meli halikutaka kuendesha mchakato wa ununuzi wa kazi hii kutokana na Mzabuni kuonesha kuwa hana imani na Shirika kushughulikia ununuzi huu. Hivyo, Shirika lilitoa taarifa kwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZAPPDA) kwamba linaomba kujitoa kushughulikia ununuzi huu na Mamlaka hiyo ilikubali na kuiteua Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi (WUMU) kuwa ndio wakala wa ununuzi wa kazi hii. Wizara

ilitekeleza mchakato wa ununuzi na Kampuni ya ZALAGACO ilishinda Zabuni hiyo na kuingia Mkataba na WUMU. Hata hivyo, kimsingi, Shirika ndio Muajiri wa kazi hiyo, hivyo lilipaswa kuwa sehemu ya Mkataba huo na ZALAGACO na sio WUMU. Hatua ya kuubadilisha Mkataba zinaendelea na kwasasa suala hili lipo kwa Mwanasheria Mkuu.

Kwa kipindi chote hicho, Shirika limeshindwa kuizuia ZALAGACO kutekeleza kazi za kufunga na kufungua makontena kwa sababu kufanya hivyo kungepelekea hasara kubwa kwa Makampuni ya Meli na Serikali ya Zanzibar.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imegendua kwamba ni kweli wakati Maguzi anafika katika Shirika hili kutekeleza majukumu yake ya kikatiba hakukuwa na Mkataba. Hilo lilisababishwa na kusitishwa kwa Zabuni ya awali na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma (ZPPDA) kulazimika kuingilia suala hilo na kuipa Mamlaka Wizara ya Ujenzi, Mawasiiano na Uchukuzi kusimamia kurejewa kwa Zabuni nyengine ambapo Kampuni ya mwanzo iliendelea kushinda Zabuni hiyo.

Hata hivyo, Kamati ya PAC ilitaka kujua kwanini Shirika lilishindwa kuwa na imani na Kampuni ya ZALAGACO na kuelezwa kwamba kulikuwa na utofauti katika masharti ya Mkataba wa awali ulioweka vigezo vya wafanyakazi wawe kidato cha nne kitu ambacho katika Mkataba mpya kimerekebishwa. Kamati pia imeelezwa kwamba hivi sasa Mkataba mpya umeshaandaliwa na umepelekwa kwa Mwanasheria Mkuu lakini huduma zinaendelea kutolewa na Kampuni ya ZALAGACO chini ya usimamizi wa Wizara hadi hapo Mkataba utakapokamilika. Kwa mnasaba huu, hoja hii inaendelea kubakia hadi Mkaguzi atakapojiridhisha katika ukaguzi unaofuata kwamba Mkataba husika upon a unatekelezwa.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar lihakikishe linafuatilia Mkataba uliopo kwa Mwanasheria Mkuu ili huduma ziweze kutolewa kwa mujibu wa masharti ya Mkataba huo.
2. Mkataba utakapmalizika, Wizara iondoe mikono yake katika utendaji na uendeshaji wa shughuli za ufungaji na ufunguaji makontena na badala yake shughuli hizo zifanywe kwa mujibu wa makubaliano yaliopo baina ya Shirika na Kampuni husika.

Hoja nambari 4.1.5.4: Malipo yaliyofanywa bila ya upatikanaji wa huduma zilizokusudiwa Shilingi TZS 32,260,00

Jumla ya shilingi 32,260,000 zililipwa kwa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (e-GAZ) kwa ajili ya ununuzi wa Mfumo wa Uhasibu katika Shirika la Meli.

Hata hivyo hadi ukaguzi unakamilika mfumo huo ulikuwa haujakamilika wala kufanya kazi kama ilivyotarajiwa na Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar. Aidha, ilibainika kuwa hakukuwa na mkataba kati ya Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar na Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar hali iliyopelekea Shirika kushindwa kutatua changamoto ilizokabiliana nazo katika ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar uwasiliane na Wakala wa Serikali Mtandao ili kuweza kupata mfumo huo wa uhasibu na kuweza kutumika kama ilivyotarajiwa.

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Shirika limelifanyia kazi suala hili kwa kuwaandikia Wakala wa Serikali Mtandao kupatiwa mkataba wa kuunganishwa mfumo wa ERMS kwa barua yenye Kumb. No. CA.244/281/01/34 ya tarehe 09/02/2024. Hata hivyo, Wakala huo haujajibu barua hiyo mpaka wakati huu. Shirika limefuatilia Serikali Mtandao na limefahamishwa kuwa hawatoi mikataba kwa michango inayotolewa na taasisi kupatiwa mfumo wa ERMS.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imegundua kuwa ni kweli Mkaguzi alikutana na kasoro ya kufanywa malipo bila ya upatikanaji wa Mfumo wa Uhasibu katika Shirika la Meli kwa Shilingi TZS 32,260,00. Hata hivyo, kwasasa Kamati imehiridhisha kwamba Mfumo huo wa ERM ipo na huduma yake inapatikana ipasavyo. Kwa msingi huo, hoja hii imeondolewa na Kamati kwa vile imeshatekelezwa.

Hoja nambari 4.1.5.5: Malipo yaliyofanyika kinyume na bajeti iliyoidhinishwa shilingi 174,865,205

Kanuni ya 22 ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021 inaeleza kuwa “Afisa Masuuli hatoingia dhima au kulipa deni lolote ambalo fedha zake hazikuwemo katika bajeti”.

Katika ukaguzi wetu wa Shirika la Meli na Uwakala kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ukaguzi umebaini kuwa Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar lilitumia jumla ya shilingi 174,865,205 ikiwa ni zaidi ya fedha zilizoidhinishwa katika bajeti ambapo ukaguzi umekosa ushahidi wa uwepo wa idhini ya Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika juu ya uhaulishaji wa fedha kuruhusu malipo hayo.

Kufanya matumizi zaidi ya bajeti iliyopitishwa ni kwenda kinyume na Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021 na kunapelekea udhibiti dhaifu wa matumizi ya fedha za umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar kuimarisha udhibiti wa bajeti utakaohakikisha kunakuwepo na uwiano kati ya matumizi halisi na bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka husika. Aidha, uongozi wa Shirika uhakikishe hakuna matumizi yanayofanywa zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa pasi na kupata idhini ya Bodi ya Wakurugenzi au mamlaka nyengine husika.

Mchanganuo wa vifungu vilivyobainika kuzidi bajeti iliyoidhinishwa ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 38: Matumizi ya Shirika la Meli yaliyozidi bajeti iliyoidhinishwa

Maelezo	Kiasi cha Bajeti (Tsh.)	Matumizi Halisi (Tsh.)	Tofauti (Tsh.)	Asilimia ya Matumizi Halisi(%)
Printings & Stationeries	24,451,600	32,775,120	-8,320,520	134
Staff Transport Office	72,885,000	212,751,685	-139,866,685	292
Public relation	10,000,000	18,000,000	-8,000,000	180
Donations	6,000,000	24,678,000	-18,678,000	411
Jumla	**113,336,600**	**288,204,805**	**-174,865,205**	

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Shirika linakubaliana na ushauri wa Mkaguzi. Vifungu hivi viliongezeka kutokana na kutokea matumizi yasiyoepukika ikiwemo fedha zilizohitajika na Serikali kuchangia shughuli maalum ya Serikali. Pamoja na hilo, Shirika halijapitiliza bajeti (over budget) ya jumla ya mwaka.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imegundua kuwa ni kweli Mkaguzi alikutana na kasoro ambayo inaonesha yalifanyika malipo ya shilingi 174,865,205 kinyume na bajeti iliyoidhinishwa. Hali hiyo ilisababishwa na kufanyika matumizi bila ya kufuata utaratibu wa kuhaulisha vifungu vya matumizi. Hata hivyo, Kamati imebaini licha ya kuwepo kwa kasoro hiyo lakini hakukuwa na matumizi aliyofanywa nje ya bajeti kuu iliyoidhinishwa na Bodi.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Shirika lihakikishe linafuata taratibu za matumizi ya fedha za Serikali ikiwemo kuhaulisha vifungu vya matumizi kwa idhini ya Bodi ili kujiepusha na hjoja kutoka kwa Mkaguzi.

SHIRIKA LA NYUMBA (ZHC)

Hoja nambari 4.1.7.1: Kutokuchukuliwa hatua za kisheria kwa Wapangaji wenye malimbikizo ya madeni ya muda mrefu shilingi 833,023,000

Kifungu cha 33(2) na 34(4) vya Sheria nambari 6 ya Shirika la Nyumba Zanzibar ya 2014 vinalitaka Shirika la Nyumba Zanzibar kumuondosha mpangaji ndani ya nyumba na linaweza kumfikisha mahakamani kudai deni lake iwapo mpangaji atashindwa kulipa kodi ya nyumba kama ilivyokubaliwa kwenye mkataba.

Aidha, mikataba yote ya muda mfupi ya upangishaji nyumba imeeleza wazi katika vifungu vya adhabu kwamba “ikiwa kwa namna yoyote kodi haijalipwa kwa kipindi cha siku thelathini (30) kutoka tarehe ya mwisho aliyoishia kulipa kodi hiyo, Mpangishaji atalazimika kumpa mpangaji notisi ya indhari ya kufuta mkataba wa upangishaji ya siku thalathini (30), na ikiwa kodi itakuwa haijalipwa kwa kipindi cha siku 30 kutoka tarehe ya notisi hiyo, mpangishaji atalazimika kumhamisha mpangaji kupitia kwa dalali wa mahakama bila kumpa notisi nyingine na mpangishaji atampeleka mpangaji mahakamani kudai deni lake”. Ukaguzi umepitia taarifa za mapato pamoja na mikataba ya upangishaji na kubaini uwepo wa idadi kubwa ya wapangaji wenye madeni ya muda mrefu ambao bado wanaendelea kukaa kwenye nyumba za Shirika bila kuchukuliwa hatua zozote za kisheria kwa mujibu wa Sheria na mikataba ya upangishaji. Ukaguzi umebaini kuwa sababu mojawapo ya kasoro hii ni na kuingiliwa kwa maamuzi ya uongozi wa Shirika la Nyumba Zanzibar kwa kupewa maagizo ya mamlaka nyengine za Serikali. Kutokuchukuliwa hatua za kisheria kwa wapangaji wenye malimbikizo ya madeni ya muda mrefu kunapelekea kudhoofika kwa juhudi za Shirika katika kutoa huduma bora za makazi kwa wananchi. Aidha, kunaweza kusababisha kuongezeka kwa idadi ya wapangaji wanaokaidi kulipa malimbikizo ya madeni yao. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Nyumba Zanzibar pamoja Serikali Kuu kwa ujumla kuhakikisha kuwa huduma za upangishaji wa nyumba za Shirika zinatolewa kwa mujibu wa masharti ya Sheria nambari 6 ya Shirika la Nyumba la Zanzibar ya 2014. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 44: Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu kwa wapangaji wa nyumba za Serikali

Namba	Mtaa	Idadi ya	Idadi ya	Asilimia	Deni halisi

		Wapangaji	**Wadaiwa**	**(%)**	**linalodaiwa (Tsh.)**
ENEO LA NG'AMBO YA MJI					
1.	MICHENZANI BLOCK 1	104	26	25	11,670,000
2.	MICHENZANI BLOCK 3	70	11	16	1,975,000
3.	MICHENZANI BLOCK 4	30	4	13	6,211,000
4.	MICHENZANI BLOCK 5	57	11	19	6,500,000
5.	MICHENZANI BLOCK 6	70	8	11	4,850,000
6.	MICHENZANI BLOCK 7	85	13	15	6,900,000
7.	MICHENZANI BLOCK 8	161	29	18	10,475,000
8.	MICHENZANI BLOCK 9	108	26	24	21,614,000
9.	MICHENZANI BLOCK 10	54	15	28	8,460,000
10.	MOMBASA	92	24	26	17,800,000
11.	SAATENI	32	15	47	15,230,000
12.	KIKWAJUNI	98	27	28	20,915,000
13.	KILIMANI	13	5	38	1,300,000

14.	GAMBA	136	107	79	86,250,000
15.	MPAPA	70	59	84	103,045,000
16.	MAKUNDUCHI	96	71	74	56,330,000
17.	CHUKWANI	2	2	100	4,525,000
18.	**Jumla Ndogo (A)**	**1,283**	**454**	35	**384,050,000**

ENEOLAMJIMKONGWE					
19.	MALINDI	69	37	54	65,898,500
20.	KIPONDA	154	74	48	64,386,000
21.	VUGA	34	11	32	60,293,000
22.	S/MUHOGO	28	9	32	11,735,000
23.	DARAJANI	44	10	23	18,755,000
24.	FORODHANI	21	2	10	24,700,000
25.	SHANGANI	54	16	30	54,207,500
26.	HURUMZI	58	17	29	15,240,000
27.	BAGHANI	9	4	44	1,490,000
28.	KOKONI	16	6	38	6,932,500
29.	M/ WIMA	12	1	8	1,000,000
30.	GIZENGA	49	14	29	15,160,000
31.	MKUNAZINI	68	24	35	45,620,500
32.	KAJIFICHENI	44	20	45	36,340,000
33.	MCHANGANI	46	6	13	7,295,000
34.	MBUYUNI	19	2	11	3,220,000
35.	MLANDEGE	14	2	14	780,000
36.	K/TUMBO	11	6	55	6,510,000
37.	MTENDENI	18	4	22	9,160,000

38.	MNAZIMMOJA	3	1	33	250,000
39.	**JumlaNdogo(B)**	**775**	**266**	34	**448,973,000**
40.	**JUMLAKUU(A+B)**	**2,058**	**720**	35	**833,023,000**

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Katika kuhakikisha deni hilo linapungua, hatua kadhaa zimechukuliwa na Shirika ikiwemo:

- Kufanya zoezi maalum la kuhakiki wapangaji.
- Kuwapa barua za ukumbusho
- Kuwatumia ujumbe kupitia simu
- Barua za indhari ya kushtakiwa na kufuta mkataba
- Kufunga nyumba (ambapo idadi ya nyumba ishirini na tano (25) zilifungwa)
- Kuwapeleka mahakamani baadhi ya wapangaji sugu (idadi ya kesi nane (8) za wapangaji zipo mahakani).

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Uongozi wa Shirika kuchukua juhudi mbali mbali za kuhakikisha deni hilo linapungua kutoka 833,023,00 hadi kufikia526,000,000.Kamati ya PAC imebaini Shirika katika utekelezaji wa ufuatiliaji wa madeni hayo ya muda mrefu kuwa halina Sera ya Usimamizi madeni jambo lililopelekea kuwepo kwa malimbikizo ya madeni makubwa ya idadi ya wapangaji ya muda mrefu.

Hata hivyo, kamati imeibakisha hoja hii kwa ufuatiliaji zaid wa madeni.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauangiza Uongozi wa Shirika la Nyumba kuuanda Sera Maalum ya Ulipaji wa Madeni ili kuepusha kulimbikizika madeni ya muda mrefu na kuikosesha mapato Serikali.

Hoja nambari 4.1.7.2: Uwepo kwa idadi kubwa ya wapangaji ambao hawana mikataba halali

Kifungu nambari 1(ii) cha mikataba yote ya muda mfupi ya ukodishaji nyumba kinamtaka mpangaji kuomba kwa maandishi mkataba mpya ndani ya kipindi cha miezi mitatu kabla ya kumalizika muda wa mkataba ulio hai. Aidha, kifungu cha 8 cha mikataba yote ya muda mfupi ya ukodishaji nyumba kinaeleza mazingira yanayopelekea kuvunjika kwa mikataba hiyo ambayo ni pamoja na kukamilika kwa muda wa mkataba. Ukaguzi umepitia

orodha za mikataba ya muda mfupi ya ukodishaji nyumba za biashara na makazi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023 na kubaini uwepo wa idadi ya wapangaji 616 kati ya wapangaji 2,058 wa nyumba za Shirika wanaendelea kunufaika na matumizi ya nyumba za Shirika bila ya kuwa na mikataba halali ya upangishaji. Kuwepo kwa idadi kubwa ya wapangaji ambao hawana mikataba halali ya upangishaji kunaweza kukapelekea Shirika kushindwa kuwashurutisha kisheria wapangaji hao endapo watashindwa kutekeleza masharti ya matumiziya nyumba hizo. Aidha kunaweza kupelekea upotevu wa mapato ya Serikali. Kiambatisho Nambari 1 Kinahusika

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Nyumba la Zanzibar kuhakikisha kuwa huduma za kupangisha nyumba zinatolewa kwa kufuata Sheria nambari 6 ya Shirika la Nyumba ya 2014. Aidha, Serikali iangalie namna bora ya kuwasaidia wananchi wasio na uwezo katika kuwahakikishia wanapata makaazi bora kwa gharama nafuu.

Majibu ya uongozi wa Shirika

Ni kweli suala hilo lilikuwepo kwa sababu ya kuwa na madeni makubwa na kesi ambazo zimepelekea kucherewa kupatiwa mikataba.

Hata hivyo idadi hiyo imepungua kutokana na hatua zilizochukuliwa na kwenda kuondoa tatizo hilo kwa kiasi kikubwa ikiwemo kufanya uhakiki na kuweka mifumo ya kisasa katika eneo la upangishaji.

Jitihada hizo zimesaidia kupunguza idadi ya wapangaji ambao hawana mikataba na wananufaika na nyumba za shirika kutoka **616** hadi kufikia **416.**

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuati utekelezaji wa hoja hii. Kamati ya PAC imebaini kuwa Shirika halina Mikata kwa baadhi ya Wapangaji, isipokuwa kwa badhi ya Wapanga wanayo makubaliano baina yao na shirika na kupelekea kuwepo na changamoto mahakamani

Hata hivyo, Shirika limechukua juhudi za kuzifungia baadhi ya Nyumba za shirika ili kuhakikisha changamoto hiyo inatatuka.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inashauri Uongozi Shirika la Nyumba Zanzibar kuhakikisha kuwa huduma za kupangisha nyumba zinatolewa kwa kufuata Sheria nambari 6 ya Shirika la Nyumba ya 2014.

Hoja nambari 4.1.7.3: Kukosekana kwa sera za bima (insurance policies) kwa nyumba za biashara zenye mikataba ya upangaji wa muda mrefu (long lease contracts)

Kifungu cha 7 (ii) cha mikataba ya upangishaji nyumba wa muda mrefu kinaeleza kwamba “Mpangaji atakata bima ya mwaka kwa jengo alilopanga na atawasilisha sera ya bima hiyo (insurance policy) kwa Mpangishaji kila mwaka katika kipindi cha mkataba husika”. Katika kuthibitisha utekelezaji wa kifungu cha 7 (ii) cha mikataba ya upangishaji nyumba wa muda mrefu, ukaguzi uliomba kupatiwa nakala za sera za bima zilizokatwa na kuwasilishwa na wapangaji wa muda mrefu. Hata hivyo ukaguzi ulipatiwa bima za nyumba kwa mikataba miwili (2) kati ya mikataba 36 ya upangaji wa muda mrefu ambazo zimekatwa na kuwasilishwa na wapangaji wa muda mrefukatika shirika. Kukosekana kwa bima za majengo kwa wapangishaji wa muda mrefu ni kwenda kinyume na mikataba ya upangishaji na kunaweza kusababisha athari za kifedha kwa Mpangaji na Mpangishaji pindi yakitokea majanga kama ya moto na matukio mengine hatarishi. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Nyumba Zanzibar kuwasiliana na wapangaji wa muda mrefu kuhusu ukataji na uwasilishaji wa Bima za nyumba Shirikani.

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Shirika limechukuwa juhudi za kuwaandikia barua wapangaji wenye mikataba ya muda mrefu (long lease contracts) na tayari wapangaji saba (7) wamewasilisha nakala (Copy) za bima zao,

Aidha kuna majengo kumi na mmoja (11) ambayo yana mkataba wa muda mrefu ila ipo katika hatua za ujenzi kiasi cha kukosa bima hizo na pindi tu itakapomalizika tutawataka wapangaji hao kukata bima za majengo hayo. Aidha baadhi ya wanapangaji ambao bado hawajawasilisha bima zao, Shirika linaendelea kuwahimiza na kuwakubusha kukata na kuwasilisha nakala za bima zao Ofisini kwetu.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa Shirika la Nyumba katika mkataba wa awali wa ukodishaji ulikuwa hauna kipengele kinachohusiana na ukataji wa bima za majengo ya muda mrefu (long lease contracts). Aidha, kwa sasa Uongozi wa Shirika umechukua juhudi za kuhakikisha kipengele hicho kinakuwemo katika mkataba yote ya ukodishaji nyumba.

Kwa msingi huo, Kamati ya PAC baada ya kupitia nakala ya Mkataba wa sasa imeridhika na utekelezaji wa hoja hii na kuiondoa.

Hoja nambari 4.1.7.4: Kutotenganishwa kwa thamani ya Ardhi na Majengo katika kutafuta gharama za uchakavu

Aya ya 45 ya Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa (IAS 16) inaeleza kuwa Kila sehemu ya thamani ya Mali ya Kudumu ambayo ina thamani kubwa ikilinganishwa na thamani ya jumla ya mali hiyo, italazimika kufanyiwa uchakavu peke yake. Aidha, aya ya 58 ya Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa (IAS 16) inaeleza kuwa Ardhi na jengo ni mali zinazotenganishika na utafutaji wa uchakavu wao hufanyika kwa kutenganishwa hata kama vyote vimenunuliwa au kupatikana kwa pamoja. Ukaguzi umepitia taarifa za fedha za mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2023 za Shirika la Nyumba Zanzibar na kubaini kuwa kiasi cha shilingi 3,290,829,902 za majengo kilichoonyeshwa katika taarifa ya fedha hakikutenganishwa na gharama ya ardhi kinyume na miongozo ya aya ya 58 ya Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa (IAS 16). Ukaguzi unahusisha dosari hii kuwa inatokana na Shirika kushindwa kufanya uthamini wa majengo yake. Kutotenganishwa kwa thamani ya Ardhi na Majengo katika kutafuta gharama za uchakavu kunaweza kusababisha gharama za uchakavu kuwa kubwa zaidi ya uhalisia na hatimae kupelekea Taarifa ya Fedha ya mwisho wa mwaka ya Shirika kutokutoa sura sahihi na halisi. Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Shirika la Nyumba Zanzibar kuboresha vizuri taarifa za Daftari la Mali na kufanya uthamini wa kitaalamu kwa majengo yake ili kuweza kujua thamani halisi ya Majengo na Ardhi wanayomiliki.

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Shirika lilishindwa kutofautisha thamani ya Ardhi na Majengo ambapo kiuhalisia sehemu kubwa ya ardhi ya Shirika ina majengo ambayo yanamilikiwa na Shirika na mengine yanamilikiwa na watu binafsi.

Hivyo katika kuhakikisha kunapatikana thamani ya ardhi na majengo, Shirika limeshaanza kufanya uthamini wa nyumba 350 (nyumba 300 Unguja na nyumba 50 Pemba) zinazomilikiwa na Shirika kwa asilimia mia kwa awamu ya kwanza. Kazi hiyo inafanywa na Mtaalamu wa ndani wa Shirika, ambaye ameteuliwa kufanya kazi hiyo kwa barua ya tarehe 01/02/2024. Kwa sasa ripoti ya kazi hiyo imeshawasilishwa kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kwa barua yenye kumbukumbu namba CA.29/70/01/07 ya tarehe 30/10/2024.

Aidha gharama ya uchakavu iliyoainishwa katika ripoti ni kwa majengo tu kwa vile majengo yanapungua thamani na ardhi inaongezeka kadri miaka inavyokwenda.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii imegundua kuwa licha ya juhudi za Shirika za kumuandikia barua Mthamini Mkuu wa

Serikali yenye kumbukumbu namba CA.29/70/01/07 ya tarehe 30/10/2024 ya kumtaka kutoa majibu ya kazi ya ripoti ya tathmini iliyofanywa na mtaalam wao wa ndani wa Shirika ili kuweza kujua thamani halisi ya Majengo na Ardhi wanayomiliki.

Aidha, Kamati hadi inakamilisha uchunguzi wake hakuna majibu ya barua hiyo kutoka kwa Mthamini Mkuu wa Serikali na kupelekea hoja hii kubakia kwa hatua za utekelezaji zaidi.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauagiza Uongozi wa Shirika kuhakikisha unautekeleza kikamilifu ushauri uliotolewa na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu kuboresha vizuri taarifa za Daftari la Mali na kufanya uthamini wa kitaalamu kwa majengo yake ili kuweza kujua thamani halisi ya Majengo na Ardhi wanayomiliki.

Hoja nambari 4.1.7.5: Kushindwa kuondoa thamani ya majengo mawili yaliyobomolewa katika taarifa za mwaka wa fedha 2022/2023

Aya ya 66 ya Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa (IAS 40) inaeleza kuwa Mali ya Uwekezaji (Investment Property) inapaswa kuondoshwa katika taarifa ya hali kifedha (statement of fi nancial position) wakati itakapouzwa au Mali hiyo itakapoondolewa kwa kudumu katika kutumika na kwamba hakuna maslahi ya kiuchumi yanayotarajiwa kupatikana baadae kwa kuondolewa kwake. Katika kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2023 Shirika laNyumba Zanzibar liliyabomoa majengo yake mawili yaliyokuwa maeneo ya Darajani Unguja na Mkungu Malofa - Chake Chake Pemba ambayo yalikuwa yakitumika kama ni Mali ya Uwekezaji (Investment Property) ili kupisha ujenzi wa majengo mapya ya uwekezaji katika maeneo hayo ya Darajani Unguja na Mkungu Malofa - Chake Chake Pemba. Ukaguzi umebaini kuwa Shirika la Nyumba Zanzibar limeshindwa kuondoa thamani ya mwisho yaliyokuwa nayo majengo hayo (carrying value) katika taarifa ya hali ya fedha jambo lililosababishwa na kutokufanyiwa kwa uthamini wa majengo hayo kabla ya kubomolewa. Kutokuondoshwa kwa thamani ya majengo hayo katika taarifa ya Hali ya Kifedha ya mwaka 2022/2023 kumepelekea thamani ya Mali za Uwekezaji zilizoonyeshwa katika taarifa ya hali ya Kifedha kuwa zaidi ya kiwango halisi cha Mali hizo. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Nyumba Zanzibar kufuata miongozo ya Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa (IAS 40) katika kuondosha thamani ya mali za uwekezaji zilizobomolewa kutoka taarifa ya hali ya kifedha ya mwaka.

Majibu ya Uongozi Wa Shirika

Katika kuhakikisha thamani ya majengo hayo mawili yanaondoshwa katika taarifa za fedha. Shirika linakamilisha kazi ya uthamini wa majengo hayo kwa lengo la kuyaondoa katika taarifa za fedha. Kazi hiyo inafanywa na mtalaamu wa ndani wa Shirika na ripoti imeshawasilishwa kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kwa barua yenye kumbukumbu namba CA.29/70/01/07 ya tarehe 30/10/2024

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Baada ya Kamati ya PAC kupata majibu ya utekelezaji wa hoja hii imebaini kuwa kweli Shirika la Nyumba Zanzibar limeshindwa kuondoa thamani ya mwisho yaliyokuwa nayo majengo hayo (carrying value) katika taarifa ya hali ya fedha jambo lililosababishwa na kutokufanyiwa kwa uthamini wa majengo hayo kabla ya kubomolewa.

Hali hii imetokana awali Shirika lilikuwa halina utaratibu wa usajili wa mali zake katika Daftari la Usajili wa Mali za Umma (Fixed Asset Register) jambo lililopelekea kutokujumuishwa taarifa za mali hizo katika taarifa za hali ya fedha na kupelekea kushindwa kutambua thamani halisi ya majengo hayo.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauagiza Uongozi wa Shirika la Nyumba Zanzibar kuhakikisha mali zote zinazomilikiwa na Shirika linafuata miongozo ya Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa (IAS 40) katika kuondosha thamani ya mali za Shirika katika taarifa ya hali ya kifedha ya mwaka.

SHIRIKA LA NYUMBA PEMBA

Hoja Nambari 4.1.7.6: Malipo yaliyofanywa nje ya mfumo wa manunuzi shilingi 17,310,740

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba MUUMU.BA.156/370/001/27 ya tarehe 12/08/2022 kutoka Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar kwenda kwa wakuu wa taasisi inaeleza kwamba kuanzia tarehe 15/08/2022 manunuzi yote ya Serikali yanatakiwa yafanywe kwa kutumia mfumo wa ununuzi wa kielektroniki (e-PROZ). Ukaguzi umebaini kwamba Shirika la Nyumba Pemba limetumia jumla ya shilingi 17,310,740 kwaajili ya manunuzi mbali mbali pasipo kutumia mfumo wa kielektroniki wa manunuzi bila ya kuweposababu maalum ya kufanya hivyo. Kufanya manunuzi bila kutumia mfumo ni kwenda kinyume namaelekezoya barua niliyoitajahapo juu. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirikala Nyumba Pemba kuhakikisha manunuzi yote yanayofanyika yanapitia katika mfumo wa manunuzi.

Mchanganuo wa manunuzi yaliyofanywa nje ya mfumo wamanunuzini kama ufuatao:-

Jadweli Nambari 45: Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa kielektroniki (e-Proz)

Namba	**Hati Namba**	**Hundi Namba**	**Kiasi cha FedhaKilicholipwa(Tshs)**	**Aliyelipwa**	**Maelezo**
1.	1/10ya04/10/2022	000350	980,000	AbrahmanHajiAbdallah	Malipo kwa ajili yagharamaza ufundi.
2.	3/9ya2/09/2022	TT	6,913,919.60	SalimHamdanMaalim	Malipokwaajiliyaununuziwavifaavyaujenzi.
3.	16/9ya21/09/222		504,210	Masoud GeneralSupplier	Malipo kwa ajili yamatengenezo yagari.
4.	4/4ya2/09/2022		8,912,610	AsaaKheriAsaa	Malipoyaununuziwavifaavyaujenzi.
Jumla			**17,310,740**		

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Shirika lilifanya manunuzi yaliyotajwa kabla ya toleo la tarehe 12/08/2022 la kuzitaka Taasisi zote za serikali kufanya manunuzi kupitia mfumo wa e-proz kuanzia tarehe 15/08/2022 lakini malipo ya huduma husika ndio yalifanyika miezi ya mbele (invoice za malipo pamoja na delivary notes zipo kwa ajili ya uhakiki kutokana na malipo husika)

Aidha, kutokana na changamoto za mfumo wa manunuzi wa e- proz kuwa mpya mafunzo yake yalifanyika tarehe 24/09/2022 na tarehe 25/09/2022 na kupelekea baadhi ya huduma kufanyika nje ya mfumo kama vile matengenezo ya gari. (barua yenye kumbukumbu namba

BF.209/406/01A/5 ya tarehe 21/09/2022 ya kushiriki mafunzo ya mfumo wa manunuzi (e- proz) ipo kwa ajili ya kujiridhisha)

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, Kamati ya PAC imegunduwa kuwa Shirika la Nyumba lilifanya matumizi nje ya Mfumo wakati mfumo huo ushaanza kutumika kwa taasisi zote za Serikali kama Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Nambari 11ya Mwaka 2016 inavyoelekeza.

Kamati wakati ikiendelea na uchunguzi wa hoja hii, ilitaka kujua ni sababu zipi zilizopelekea Uongozi wa Shirika la Nyumba Zanzibar kufanya matumizi yenye jumla ya shilling 17,310,740 nje ya mfumo mpya wa Manunuzi na kuieleza Kamati kuwa kutokana na ukosefu wa elimu juu ya matumizi ya Mfumo wa Eproz kwa maafisa wa manunuzi na uhaba wa wataalam ndio sababu ilipelekea kutotumia mfumo wa Eproz.

Hata hivyo, Uongozi wa Shirika umechukua juhudi mbali mbali za kuwapatia mafunzo Maafisa Manunuzi na kwa sasa matumizi yote yanayofanyika katika Shirika yanapitia katika Mfumo wa Manunuzi ya Serikali (Eproz) na kwa hatua hiyo Kamati ya PAC imeridhishwa na utekelezaji wa hoja hii na kupelekea kuondoka kwa hoja.

Hoja Namabari 4.1.7.7: Kutokununua vifaa vya kuandikia kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji shilingi 3,419,504.70

Kifungu nambari 35 cha Sheria nambari 12 ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar ya 2018 kimezitaka Taasisi zote za Serikali kupeleka kazi zake zote za Uchapaji na Mahitaji ya vifaa vya Afisi na vifaa vya kuandikia kwa wakala wa Uchapaji wa Serikali Zanzibar.

Ukaguzi umebaini kwamba Shirika la Nyumba Pemba limefanya ununuzi wa vifaa vya kuandikia vyenye thamani ya shilingi 3,419,504.70 kutoka kwa Wasambazaji bila ya kuwepo kwa ruhusa kutoka kwa Wakala kama utaratibu unavyoelekeza jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo ikiwemo kununua vifaa kwa Wakala husika au kuomba ruhusa kwa Wakala ili kuweza kununua vifaa hivyo kwa wasambazaji wengine pale inapotokezea Wakala kutokuwa na vifaa vinavyohitajika kununuliwa. Mchanganuo wa vifaa vilivyonunuliwa nje ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji Pemba ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 46: Kutonunua vifaa kutoka kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji

Namba	Hati Namba	Hundi Namba	KiasichaFedhaKilicholipwa(Tshs)	Aliyelipwa	Maelezo
1.	11/12ya20/12/2022	TT	1,231,232.80	AdultTrainingCentre	Ununuziwavifaavyakuandikia
2.	13/9ya16/9/2022		2,002,914.20	HalimEnterprises	
3.	22/7ya27/7/2022		185,357.70	CapitalTecnologyCentre	
Jumla			**3,419,504.7**		

Chanzo: Uchambuzi wa Hati za malipo

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Shirika lilipeleka LPO ya tarehe 22/5/2022 kwa ajiliya kupatiwa vifaa vya kuandikia kwa Wakala wa serikali wa Uchapaji. Hata hivyo Shirika halikupata marejesho kutoka Wakala.

Kwa sasa Shirika linafanya manunuzi yake yote ya vifaa vya kuandikia kupitia Wakala wa Uchapaji wa Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilipokuwa ikihoji utekelezaji wa hoja hii, Shirika limekiri kufanya manunuzi ya vifaa vya kuandikia bila ya kupata kibali kutoka kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji yenye jumla ya shilling 3,419,504.70kutoka kwa Wasambazaji Binafsi.

Wakati Kamati ikiendelea na mahojiano ilielezwa kuwa Uongozi wa Shirika la Nyumba liliandikia barua Wakala wa Serikali wa Uchapaji (LPO) kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandika vya Ofisi ambapo kamati iliomba kuwasilishwa ithibati ya barua hiyo, cha kushangaza hadi Kamati inakamisha uchunguzi wake katika hoja hii barua hiyo kushindwa kuwasilishwa.

Kwa msingi huo, Kamati imeibakisha hoja hii kwa ajili ya utekelezaji Zaidi.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Shirika unaagizwa kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo ikiwemo kununua vifaa kwa Wakala husika au kuomba ruhusa kwa Wakala ili kuweza kununua vifaa hivyo kwa wasambazaji wengine pale inapotokezea Wakala kutokuwa na vifaa vinavyohitajika kununuliwa.

Hoja nambari 4.1.7.8: Hali ya Uchakavu wa majengo ya Shirika

Kifungu nambari 66(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba “Kutakuwa na mpango wa matengenezo ya mali utakaoandaliwa na Taasisi ya Umma unaohakikisha kwamba mali zinabaki katika ubora kwa matumizi yaliyokusudiwa”.

Shirika la Nyumba Pemba linamiliki majengo katika maeneo mbalimbali yakiwemo maghala na vituo vya kuuzia karafuu.

Ukaguzi umebaini kuwa majengo mengi yapo katika hali ya Uchakavu mkubwa uliosababishwa na kutokufanyiwa ukarabati kwa wakati jambo ambalo linaweza kupelekea kuzidi kuchakaa kwa majengo hayo na hatimae kubomoka na kuanguka na kuisababishia hasara Serikali jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Nyumba Pemba kuyafanyia ukarabati kwa wakati majengo ili kuepusha athari zinazoweza kujitokeza baadae.

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Shirika linaendelea na utekelezaji wake wa mpango wa matengezo wa mwaka 2019/20-2023/24 kwa kuzifanyia matengenezo nyumba zake ambazo zipo katika hali ya uchakavu.

Miongoni mwa miradi mipya iliyotokana na kuvunjwa kwa nyumba chakavu ni:-

Mradi wa Jengo la Biashara na Makaazi Mkungu Malofa

Chake-chake Pemba (upo katika hatua ya utekelezaji)

Mradi wa Jengo la Biashara na Makaazi Kilima-tinde Chake-chake Pemba (Utekelezaji wa mradi huo unategemewa kufanyika mwaka wa fedha 2025/2026).

Ukarabati wa ujenzi wa paa la jengo la Makaazi Tibirinzi (ZHC.19/02 a-d) umekamilika. Aidha, pia shirika liliweza kuyatengeza mashimo ya Jengo hilo.

Ukarabati wa ujenzi wa nyumba zilioko madungu.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Baada ya Kamati kupata majibu ya hoja hii, Kamati ya PAC imeridhishwa na utekelezaji na hatua mbali mbali zilizochukuliwa na Uongozi wa Shirika la Nyumba Zanzibar juu ya Mpango wa matengenezo wa Nyumba za Maendeleo na uanzishwaji wa utekelezaji wa miradi ya kimkakati kwa Unguja na Pemba.

Kamati imeridhishwa na hatua za utekelezaji na kupelekea hoja kuondoka.

Hoja nambari 4.1.7.9: Kukosekana kwa hatimiliki kwa baadhi ya mali za Shirika

Kifungu nambari 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya mwaka 2021 kinaeleza kwamba “Taasisi ya Umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali”.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa mali nyingi za Shirika la Nyuma Pemba ambazo hazina hati miliki, miongoni mwa mali hizo ni baadhi ya majengo ya Afisi, nyumba za kupangisha pamoja na vyombo vya moto jambo ambalo linaweza kupelekea upotevu wa mali hizo kutokana na Serikali kutokuwa na umiliki halali, aidha ni kwenda kinyume na Kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani pamoja na kutokuongeza umakini kwa watendaji wenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo inayotolewa na Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika kuongeza umakini katika kufuata Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kuzitafutia hati miliki mali za Shirika. Orodha ya mali ambazo hazina hatimiliki

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Shirika limeshaanza kuchukua hatua za awali za kuomba hati miliki kutoka Mamlaka huzika. Kwa upande wa chombo cha moto vespa SMZ 316C hati miliki yake imeshafuatiliwa na kupatikana kutoka Mamlaka ya Mapato Zanzibar (hati miliki ipo kwa ajili ya kuhakikiwa).

Aidha, kwa upande wa majengo ya Shirika hatua za kuomba hati miliki zimeshachukuliwa kwa kuwaandikia barua Kamisheni ya Ardhi kupitia **barua** zenye kumbukumbu namba ZHC/P/M.90/4VOLII/60 ya tarehe 21/06/2019, ZHC/P/90/4VOLII/150 ya tarehe 31/08/2021, ZHC/P/KA/10/01 ya tarehe 09/02/2023. Barua zeneye kumbukumbu zilizoorodheshwa zimehifadhiwa kwa ajili ya kujiridhisha.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilipokuwa kifuatikllia utekelezaji wa hoja hii, imebaini kuwa Shirika limeshaanza kuchukua hatua za awali za kuomba hati miliki kutoka mamlaka husika. Aidha, kamati PAC iliomba kupatiwa vielelezo pamoja na barua kwa ajili ya uchunguzi ni kama viuatavyo…….

Kwa mnasaba huo, kamati ya PAC baada ya kupitia vielelezo hivyo imeridhishwa na juhudi zilizochukuliwa na Uongozi wa Shirika katika

upatikanaji wa hati miliki katika nyumba za maendeleo zinazomilikiwa na Shirikakwa Unguja na Pemba na kupelekea kuiondoka hoja hii.

Hoja nambari 4.1.7.10: Deni la Mapato la ukarabati wa nyumba zilizotolewa fidia shilingi 57,900,000

Kutokana na makubaliano ya vikao vilivyofanyika baina ya uongozi wa Shirika la Nyumba Pemba na wamiliki wa nyumba za fidia zilizopo katika majengo ya Nyumba za maendeleo zilizofanyiwa matengenezo “wamiliki wa nyumba za fidia wanatakiwa kuchangia gharama za matengenezo ya nyumba hizo ili kuendana na muonekano wa pamoja baina ya nyumba za Shirika na zile zilizotolewa fidia”.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kufanyika kwa matengenezo ya nyumba za fidia zilizoko katika maeneo mbali mbali ili ziweze kuwa na muonekano wenye kufanana na nyumba za Shirika ikiwa ni njia mojawapo ya kuzitunza na kuziboresha nyumba hizo lakini hadi ukaguzi unakamilika imebainika wamiliki wa nyumba hizo hawajachangia gharama za matengenezo yaliyofanyika katika nyumba zao jambo ambalo ni kulibebesha Shirika mzigo mkubwa wa gharama za matengenezo na hatimae kuitia hasara Serikali**.**

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika kuweka sera na miongozo bora ya kushughulikia nakuzitunza nyumba za maendeleo za Shirika na zile za watu binafsi. Baadhi ya nyumba hizo ni kamazinavyoonekanakatika jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 47: Nyumba za fidia zilizofanyiwa matengenezo

Namba	**Namba yaNyumba**	**EneoIlipo**	**Deni linalodaiwa(Tshs)**	**Fedha iliyolipwa(Tshs)**	**Bakaa ya Deni(Tshs)**
1.	BL-5/1	Madungu	2,000,000	1,200,000	800,000
2.	BL-5/2		2,000,000	0	2,000,000
3.	BL-5/3		2,000,000	400,000	1,600,000
4.	BL-5/4		2,000,000	0	2,000,000
5.	BL-5/5		2,000,000	0	2,000,000
6.	BL-3/3		8,500,000	0	8,500,000
7.	BL-4/14		8,500,000	0	8,500,000

8.	BL-4/15		8,500,000	0	8,500,000
9.	BL-4/1	Mtemani	3,000,000	0	3,000,000
10.	BL-4/2		3,000,000	0	3,000,000
11.	BL-4/4		3,000,000	0	3,000,000
12.	BL-4/7		3,000,000	0	3,000,000
13.	BL-4/8		3,000,000	0	3,000,000
14.	BL-4/11		3,000,000	0	3,000,000
15.	BL-4/12		3,000,000	0	3,000,000
16.	BL-4/22		3,000,000	0	3,000,000
Jumla			**59,500,000**	**1,600,000**	**57,900,000**

Chanzo: Uchambuzi wa taarifa za madeni ya Shirika

Majibu ya Uongozi wa Shirika

Shirika limeshaanza kuchukua hatua za awal i za kuomba hati miliki kutoka mamlaka husika.

Kwa upande wa chombo cha moto vespa SMZ 316C hati miliki yake imeshafuatiliwa na kupatikikana kutoka Mamlaka ya Mapato Zanzibar (hati miliki ipo kwa ajili ya kuhakikiwa).

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwepo kwa ucheleweshaji wa ulipaji wa fidia kwa watu binafsi walifanyiwa matengenezo ya nyumba zao zilizokuwemo katika block 5 za nyumba za maendeleo za Madungu.Licha juhudi mbali mbali ambazo shirika imechukua kufuatilia urejeshaji wa fiadia hizo kamati imebaini kuwa wamiliki binafsi 2 wa nyumba hizo ndio waliochangia gharama za matengenezo hayo. Hivyo, Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa hoja hii na kuibakisha kwa utekelezaji zaidi.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauagiza Uongozi wa Shirika kuhakikisha unaanda utaratibu maalum wa usimamizi wa ilipaji wa madeni yatokanayo na fidia ya matengenezo ya Nyumba za Maendeleo Madungu ili kusaidia Serikali kuongeza pato lake la ndani.

MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR (ZAA)

Hoja nambari 5.1.3.1: Kutowasilishwa katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa Tozo ya Usalama (Safety Fee) inayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kwa niaba ya Mamlaka, shilingi 684,050,000

Kwa mujibu wa Sheria nambari 2 ya Kodi za Huduma za Bandari na Viwanja vya Ndege ya 1999 (Port Service Charge Act no.2, 1999), abiria yeyote anaesafiri ndani ya Tanzania kupitia viwanja vya ndege, anapaswa kutozwa shilingi 2,000 na wale wanaosafiri nje ya Tanzania kutozwa USD 9. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, Mamlaka ya Mapato Zanzibar, huzikusanya fedha hizo kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na baadae kuziwasilisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.

Katika kupitia Bajeti ya Mamlaka ya Viwanja vya ndege Zanzibar ya mwaka wa fedha 2022/2023, ukaguzi umebaini kwamba, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 406,215,357 kutokana na tozo ya usalama (safety fee).

Ukaguzi ulipitia Ankara za madai zenye thamani ya shilingi 684,050,000 ambazo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ilizituma kwenda Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili ya kurejeshewa fedha za tozo ya usalama wa abiria za Viwanja vya Ndege zilizokusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar. Hata hivyo fedha hizo hazikuwasilishwa katika Mamlaka ya Viwanja vya ndege Zanzibar. Aidha ukaguzi umebaini kwamba kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa tozo hizo hazijawasilishwa katika Mamlaka yay a viwanja vya ndege Zanzibay shilingi 1,257,606,000 zinazotokana na deni la tozo ya usalama wa abiria.

Kutokuwasilishwa kwa tozo ya usalama kwa Mamlaka ya Viwanja vya ndege kunapunguza uwezo wa Mamlaka katika kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato hayo katika uwezo wa kuboresha usalama wa abiria.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya ndege Zanzibar kuendelea na jitihada za kuishawishi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwasilisha mapato yanayotokana na tozo ya usalama wa abiria kama inavyotakiwa na Sheria.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Mamlaka inaendelea kuchukua juhudi za kukutana nakuiandikia Ofisi ya Raisi Fedha na Mipango juu ya kurejeshwa fedha za tozo ya usalama (Safety fee) ambazo zinakusanywa na Mamlaka ya mapato Zanzibar (ZRA), pamoja na jitihada hizo, Mamlaka bado haijafanikiwa kuzipata fedha hizo.

Hivyo Mamlaka iniomba kamati yako tukufu kuisaidia Mamlaka juu ya suala hili.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia majibu ya hoja hii, Kamati ya PAC imegundua kwamba ni kweli Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) haikuweza kuwasilishiwa Tozo ya Usalama (Safety Fee) inayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kwa niaba ya Mamlaka, shilingi 684,050,000. Hali hiyo imetokana na makusanyo hayo yanaingizwa moja kwa moja katika Mfuko Mkuu wa Seriakli (Hazina) baada ya kukusanywa. Hata hivyo, Kamati ilitaka kujua juhudi ambazo Mamlaka imezichukua katika kuhakikisha makusanyo hayo yanaingizwa katika hesabu zao na kubaini kwamba Mamlaka tayari imeshafanya vikao mbali mbali na Watendaji wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango pamoja na kuwaandikia barua zenye azma ya kutatua changamoto hiyo bila ya kuwepo mafanikio.

Miongoni mwa vielelezo ambavyo Mamlaka iliipatia Kamati ni barua ya tarehe 18 Agosti, 2021 yenye kumbukumbu nambari ZAA/WF/01/03/VOL.1/ inayohusiana na uhaulishaji wa shilingi 244,994,000 pamoja na barua ya tarehe 13/12/2022 yenye kumbukumbu nambari ZAA/WF/01/03/VOL.1/ kuhusiana na uhaulishaji wa shilingi 1,027,986,000.

Kutokana na uchunguzi wa Kamati ya PAC, hili ni suala ambalo linapatikana ufumbuzi wake baada ya kupata maelezo kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kupitia Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ambao ndio wanaoingiziwa fedha hizo. Kwa mnasaba huo, kuna haja kwa Kamati kuifuatilia zaidi hoja hii hasa ukizingatia Sheria za kiamatifa za usimamizi na uendeshaji wa Viwanja vya Ndege zimeelekeza fedha hizo zibakie Mamlaka husika kwa ajili ya kusaidia matumizi ya iendelezwaji wa viwanja husika.

Kamati pia iligundua uwepo wa tofauti ya fedha zilizooneshwa na Mkaguzi katika Ripoti yake (Tzs. 684,050,000) na Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka (Tzs. 499,680,000) na kubaini kwamba tofauti hiyo imesababishwa na kutumika kwa utaratibu wa ufungaji hesabu wa Mamlaka (Acrual Basis) ambao unaruhusu kuyajumuisha matumizi hata kama hayajafanyika.

Kamati imeridhishwa na majibu ya Mamlaka. Hata hivyto, hoja hii inaendelea kubakishwa kwa ufuatiliaji zaidi.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inaitaka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kupitia Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kuruhusu fedha zinazokusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar kubakishwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ili ziweze kuviendeleza Viwanja hivyo.

Hoja nambari 5.1.3.2: Kutowasilishwa katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa Tozo ya Huduma kwa abiria (Passenger Service Charge) inayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kwa niaba ya Mamlaka

Kwa mujibu wa Sheria nambari 2 ya Kodi za Huduma za Bandari na Viwanja vya Ndege ya 1999 (Port Service Charge Act no.2, 1999), abiria yeyote anaesafiri ndani ya Tanzania kupitia Viwanja vya Ndege, anapaswa kutozwa shilingi 10,000 na wale wanaosafiri nje ya Tanzania kuchajiwa USD 40 kwa ajili ya tozo ya huduma kwa abiria (Passenger Service Charge). Kwa mujibu wa sera za kimataifa za usafiri wa Anga (International Civil Aviation Organization Policies), fedha zote zinazokusanywa kupitia huduma za abiria, zinatakiwa zirudishwe kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege husika kwa ajili ya kuboresha huduma za Viwanja vya Ndege kwa ajili ya abiria wanaotumia viwanja hivyo.

Ukaguzi umebaini kwamba tozo ya huduma kwa abiria haijawahi kuwasilishwa kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kama zinavyoelekeza sera za kimataifa za usafiri waanga.

Kutowasilishwa katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa tozo ya huduma kwa abiria kunaweza kuzorotesha matengenezo na maboresho ya huduma za viwanja vya ndege vya Zanzibar kwa ajili ya abiria wanaotumia viwanja hivyo jambo linaloweza kupelekea uwezekano wa kushuka A hadhi kwa Viwanja vya Ndege vya Zanzibar kwa mujibu wa viwango za kimataifa za usafi ri wa anga.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuishawishi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango juu ya umuhimu wa kurejesha fedha za makusanyo ya tozo ya huduma kwa abiria katika Mamlaka ya Viwanja vya ndege Zanzibar ili ziweze kusaidia katika kuboresha huduma za Viwanja vya Ndege kwa ajili ya abiria wanaotumia viwanja hivyo.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Mamlaka imefanya juhudi za kuwasiliana na wadau wakiwemo ZRA, Wizara, Hazina juuu ya kuishawishi Ofisi ya Raisi Fedha na Mipango juu ya kurejeshwa fedha za tozo ya huduma kwa abiria (Passenger Service Charge) ambazo zinakusanywa na Mamlaka ya mapato Zanzibar (ZRA), pamoja na jitihada hizo, Mamlaka bado haijafanikiwa kuzipata fedha hizo.

Hivyo Mamlaka inaiomba kamati yako tukufu kuisaidia Mamlaka juu ya upatikanaji wa fedha hizo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati baada ya kuchunguza hoja hii, imebaini yafuatayo:

1. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar haijawahi kukusanya aina hiyo ya tozo pamoja na kwamba sheria yao inaelekeza kufanya makusanyo ya tozo hiyo.
2. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar pia haijawahi kukiingiza chanzo hicho kuwa ni miongoni mwa makusanyo yao ndani ya bajeti yao.
3. Mamlaka takriban zote Ulimwnguni huwa haizichukui ada za utoaji huduma (Service charge) badala yake ama hukusanywa na Mamlaka za Mapato husika na kuzirudisha Mamlaka za Viwanja vya Ndege husika.

Zaidi ya hayo, maelezo mengine ya uchunguzi wa Kamati yaliyotolewa katika hoja nambari 5.1.3.1 ikiwemo juhudi walizochukua Mamlaka katika kuitafutia ufumbuzi hoja hii yanahusika. Kwa mnasaba huo, hoja hii inaendelea kubakia hadi Kamati itakapokutana na watendaji wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ili kujua changamoto ya utekelezaji wake.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ihakikishe inaanzisha chanzo kipya cha mapato kuhusiana na tozo ya huduma kwa abiria (Passenger Service Charge) pamoja na kukiingiza ndani ya bajeti yao.

Hoja nambari 5.1.3.3: Malipo ya kukodi mabasi manne kwa ajili ya wafanyakazi bila ya kuzingatia thamani ya fedha (Value for money), shilingi 237,600,000

Kwa mujibu wa kifungu nambari 37(c)(e) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016, inelezea kwamba ununuzi na uondoshaji wa mali za Umma unatakiwa kufanywa kwa mujibu wa misingi ya kuwepo ushindani na kuhakikisha thamani ya fedha (Value for Money) inapatikana pamoja na kuzingatia hali ya uchumi na ufanisi.

kaguzi umebaini kuwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imekodi mabasi manne (4) kwa ajili ya wafanyakazi wake kwa gharama za shilingi 237,600,000 kwa mwaka ambazo ni sawa na wastani wa shilingi 4,950,000 kwa mwezi kwa kila basi bila ya kuzingatia thamani halisi ya fedha zinazolipwa kwa Mkodishaji.

Utaratibu wa Mamlaka kukodi mabasi hayo bila ya kuzingatia thamani halisi ya fedha inaibua wasiwasi kuhusu matumizi bora ya fedha za umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kufanya tathmini ya kina kabla ya kuanza na utaratibu wa kukodi mabasi kwa ajili ya wafanyakazi wake na kuja na namna ya uboreshaji wa huduma za usafiri kwa wafanyakazi kwa kuzingatia thamani halisi ya fedha (Value for Money), hali ya uchumi na ufanisi.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Kwa kuzingatia ushauri wa Mkaguzi, Mamlaka imenunua mabasi mawili aina ya Tata kupitia Ofisi ya Raisi Fedha na Mipango kwa ajili ya kubeba wafanyakazi ili kuondokana na kukodi mabasi

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kutathmini thamani halisi ya fedha iliyokuwa ikitumika katika kukodi mabasi manne kwa shilingi 4,950,000 kwa kila mwezi ambayo yalikuwa yakichukua wafanyakazi waliokuwa wakiingia na kutoka Mamlaka kwa takriban mara tatu au nne kwa siku (shift of work). Kamati imebaini kuwa thamani halis ya fedha iliyokuwa ikilipwa ilikuwepo kutokana na sababu zifuatazo:

1. Huduma zote za Mabasi hayo ikiwmo matengenezo makubwa na madogo (service) zilikuwa zikifanywa na Mmiliki wa mabasi hayo. Hivyo, Mamlaka ilikuwa haina wajibu (liability) yoyote zaidi ya kupata huduma.
2. Kutokana na fedha iliyokuwa ikilipwa, Kamati imebaini kwamba gharama za malipo ya kodi ni shilingi 165,000 kwa siku. Fedha hiyo ni kidogo hasa ukizingati mabasi hayo yalikuwa yakifanya kazi (route) si chini ya mara tatu.

Kwasasa, Kamati imebaini kwamba tayari Mamlaka imeshachukua juhudi za kununua gari mbili (Mabasi) na tayari Mkandarasi wa Mabasi wameshamalizana nae Mkataba na huduma hivi sasa inaendelea kutoklewa na Mamlaka yao. Kwa mnasaba huo, Kamati imeridhika na majibu na kukubaliana na Mkaguzi kuiondoa hoja hii.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Mamalak ihakikishe inazisimamia ipasavyo gari hizo na kuendelea na juhudi za kufanya ununuzi wa gari nyengine zitakazotatua changamoto ya usafiri kwa mujibu wa majukumu ya watendaji wake.

Hoja nambari 5.1.3.4: Kutokuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Viwanja vya Ndege

Kifungu nambari 20 cha Sheria nambari 9 ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ya 2011 (Aerodrome Act), kinahitaji kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Viwanja vya Ndege (Airport Development Fund) utakaojumuisha fedha zitakazoamuliwa kwa pamoja na Waziri anaeshuhulika na Viwanja vya Ndege pamoja na Waziri anehusika na masuala ya Fedha. Kwa mujibu wa kifungu hicho, fedha zinazowekwa katika Mfuko huo zinatakiwa zitumike kwa ajili ya uwekezaji, uendelezaji au ujenzi wa Viwanja vya Ndege.

Ukaguzi umebaini kwamba Mfuko wa Maendeleo ya Viwanja vya Ndege haujawahi kuanzishwa tangu kusainiwa kwa Sheria hiyo ya Viwanja vya Ndege mwaka 2011.

Kutokuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Viwanja vya Ndege ni kwenda kinyume na Sheria ya Viwanja vya Ndege jambo ambalo linapelekea kukosekana kwa fedha maalum zinazotengwa na Serikali kwa ajili ya uwekezaji, uendelezaji au ujenzi wa viwanja vya ndege Zanzibar.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuhakikisha unafanya ufuatiliaji ikiwa ni pamoja na kufanya vikao kwa lengo la kujadili namna bora ya kuweza kuhuisha mfuko ulioasisiwa katika sheria ili kuhakikisha utekelezaji wa shughuli za uwekezaji, uendelezaji au ujenzi wa viwanja vya ndege Zanzibar.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Mamlaka imeanzishwa kwa sheria namba 8 ya mwaka 2011, jukumu lake kubwa ni kutoa kuduma za uendeshaji viwanja kwa mujibu wa kifungu namba 5 (1) (a-r) cha sheria hiyo.

Serikali imeanzisha sheria nambari 9 ya mwaka 2011 (Aerodrome Act), ambayo inasimamiwa na Wizara ya Miundombinu, Ujenzi na Usafirishaji yenye jukumu la kudhibiti viwanja vya ndege Zanzibar. Pia kifungu nambari 20 (1-3) cha sheria hiyo, kinahitaji Wizara kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Viwanja vya Ndege (Airport Development Fund).

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, Kamati ya PAC ilikiangalia kifungu cha 20 cha sheria ya Viwanja vya Ndege, Namba 9 ya 2011 na kubaini kuwa kinahitaji kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Viwanja vya Ndege (Airport Development Fund) utakaojumuisha fedha zitakazoamuliwa kwa pamoja na Waziri anaeshuhulika na Viwanja vya Ndege pamoja na Waziri anehusika na masuala ya Fedha.Kwa mnasaba huo, Kamati imegundua kuwa mwenye jukumu la kuanzishwa Mfuko wa Maendeleo ya Viwanja vya Ndege ni Wizara inayohusiana na Mawasiliano akishirikiana na Waziri anayehusika na Fedha na sio Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar. Kufuatia ukweli huo, Kamati imamua kuiondoa hoja hii kwa vile haina misingi kisheria.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Wizara inayohusiana na Mawasiliano na Waziri anayehusika na Fedha kukaa pamoja kuhakikisha wanaanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Viwanja vya Ndege ili uweze kuwa muwarubaini wa changamoto zitakazojitokeza.

Hoja nambari 5.1.3.5: Kutokuwepo kwa Sera na Miongozo ya Uendeshaji na Usimamizi wa Mamlaka

Kwa mujibu wa viwango bora vinavyokubalika vya uendeshaji na usimamzi wa Viwanja vya Ndege, ni muhimu kuandaa sera na miongozo itakayofafanua na kuweka kumbukumbu za viwango vya utendaji na taratibu ambazo ni muhimu kwa ajili ya kupunguza vihatarishi katika usimamizi na uendeshaji wa wafanyakazi wa Mamlaka.

Lengo kuu la kuwepo sera katika usimamizi na uendeshaji wa Mamlaka ni kuweka usawa katika shughuli za utendaji ndani ya Mamlaka na katika Idara zote. Uwepo wa sera na miongozo ya uendeshaji na usimamizi wa shughuli za Mamlaka kunaongeza nguvu za udhibiti wa ndani katika usimamizi wa shughuli za kila siku za Mamlaka.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Viwanja vya Ndege haina miongozo na sera za uendeshaji na usimamizi wa shughuli zake muhimu ikiwemo:

a. Sera ya usimamizi wa mali (Asset Management Policy),

b. Kanuni za Fedha (Financial Regulations),

c. Kanuni za Utumishi (Staff Regulations),

d. Sera za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT Policies)

Kutokuwepo kwa sera na miongozo ya uendeshaji na usimamizi wa Mamlaka kunaweza kupelekea kuongezeka kwa vihatarishi vinavyoikabili Mamlaka katika usimamizi bora wa shughuli za kiutendaji za Mamlaka.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kuweka kipaombele katika uanzishaji wa sera na miongozo inayogusa maeneo muhimu ya uendeshaji wa Mamlaka ikiwemo usimamizi wa mali, usimamizi wa fedha, usimamizi wa rasilimali watu na usimamizi wa teknolojia ya habari na mawasiliano. Aidha ni vyema kwa uongozi wa Mamlaka kuhakikisha kuwa miongozo hiyo inaendana na viwango bora vinavyokubalika vya sekta ya Viwanja vya Ndege na inaendana na R matakwa ya kisheria.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Uongozi wa Mamlaka umeanza mataarisho ya kutaarisha miongozo hiyo ikiwemo “Sera ya TEHAMA, Kanuni za fedha na kanuni za kiutumishi Mmamlaka.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, ni kweli nyaraka ya Sera ya usimamizi wa mali (Asset Management Policy), Kanuni za Fedha (Financial Regulations) na Sera za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT Policies)

zilikuwa hazijaandaliwa. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba Kanuni za Utumishi (Staff Regulations) ilikuwepo na zilikuwa zikitumika tangu mwaka 2016 lakini inaonekana Mkaguzi hakuoneshwa na Watendaji. Sambamba na hilo, Mamlaka imeanzisha mchakato wa kuandaa Sera za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT Policies) ambapo tayari Zabuni ya kutafuta Mtaalamu wa kuandaa Sera hiyo ambapo mwakani 2025 inategemewa itakuwa tayari.

Kamati pia imetilia nguvu uanzishwaji wa Idara ya Huduma kwa Wateja (Customer Service Department) kwa kupelekea Serikalini maombi ya kufanyiwa marekebisho Muundo wao wa Utumishi ili uweze kuruhusu uanzishwaji wa Idara hiyo muhimu kwa Mamlaka hii.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Mamalaka ihakikishe inaandaa Sera ya usimamizi wa mali (Asset Management Policy), Kanuni za Fedha (Financial Regulations).
2. Mamlaka ihakikishe inakamilisha mchakato wa Zabuni wa kumpa Mtaalamu atakaeandaa Sera za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT Policies) kwa vile shughuli nyingi za Viwanja vya Ndege vinaendeshwa kwa kutumia tecknolojia.
3. Mamlaka ichukue juhudi za makusudi kufuatilia Kamisheni ya Utumishi wa Umma marekebisho ya muundo wao ili Idara ya Huduma kwa Wateja iweze kuanzishwa na kutatua changamoto za utoaji huduma zinazojitokeza.

Hoja nambari 5.1.3.6: Kutokuwepo kwa usimamizi mzuri wa madeni ya Mamlaka

Kifungu nambari 30(1)(2) vya Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa Afi sa Masuuli atahusika na usimamizi wa mapato ya Taasisi ya Umma na atachukua hatua zinazofaa kuhakikisha uanzishaji na uendeshaji wa mfumo bora na wa ufanisi wa ukusanyaji na wa uhifadhi wa mapato. Aidha, Kanuni ya 23(1)(a) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inasisitiza ukusanyaji wa mapato kwa kueleza kuwa Afisa Mas-uuli atahakikisha kuwa watu wote wanaopaswa kulipa fedha yoyote kama mapato ya Serikali au stahiki yoyote ya Taasisi ya Umma wanapewa notisi ya madai au notisi yoyote ile ya madeni yanayodaiwa kwa wakati huo.

Ukaguzi umebaini kuongezeka kwa madeni yanayodaiwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa ongezeko lenye jumla ya **shilingi 2,945,599,832** kutokana na kuwepo wadaiwa wenye jumla ya **shilingi 10,407,989,440** katika mwaka 2022/2023 ikilinganishwa na wadaiwa wenye jumla ya **shilingi 7,462,389,608** kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Ukaguzi umebaini kuwa hali hii imesababishwa zaidi na kutokuwepo kwa sera nzuri ya usimamizi wa madeni (Receivable Management Policies) katika Mamlaka.

Kukosekana kwa usimamizi mzuri wa madeni ya wadaiwa wa Mamlaka kunaathiri mtiririko wa fedha za Mamlaka jambo linaloweza kupelekea Mamlaka kushindwa kukimu mahitaji ya fedha kwa muda mfupi

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kuanzisha sera za usimamizi wa madeni ili kuboresha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na madeni hayo.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Sera ya usimamizi wa madeni tayari imeshataarishwa.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imegundua kuwa wakati Mkaguzi alipotkua akitekeleza kazi yake ya ukaguzi katika Mamlaka hii, Sera ya Usimamizi wa Madeni ilikuwa haijaandaliwa. Hata hivyo, kwasasa Sera hiyo imeshakamilika na inatumika ipasavyo tangu mwezi Disemba, 2023. Licha ya kuwepo kwa Sera hiyo, Kamati ilitaka kujua madeni inayodai kwa Taasisi, Kampuni na Watu binafsi na kuelezwa kwamba kwa mwaka 2023/2024 deni hilo limepungua.

Kwa vile hoja ya Mkaguzi iliyotaka kuwepo kwa Sera ya Usimamizi wa Madeni imetatuliwa, Kamati imeamua kuiondoa hoja hii.

MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE PEMBA

Hoja nambari 5.1.3.7: Kutokukamilika kwa Ufungaji wa Taa za kuongozea Ndege (Approach light)

Kwa mujibu wa miongozo ya kimataifa ya usimamizi wa viwanja vya ndege Annex 14 inaeleza kwamba Taa za kuongozea ndege (Approach light) ni taa ambazo zinatakiwa kuwepo katika kiwanja cha ndege kwa lengo la kumuongoza rubani katika njia sahihi wakati wa kutua.

Ukaguzi umebaini kwamba katika Kiwanja cha Ndege cha Pemba runway 2 Kusini na runway 20 Kaskazini kunatakiwa kuwepo taa 17 kila upande. Hadi ukaguzi huu unakamilika mnamo mwezi wa Disemba, 2023 runway 2 ni taa 15 pekee zinafanya kazi na hivyo kuweka tofauti ya taa 2 ambazo hazifanyi kazi na runway 20 zipo taa 11 zinafanya kazi na kuweka upungufu wa taa 6 ambazo hazifanyi kazi. Hali hii ikiendelea inaweza kusababisha kutokea kwa ajali pale ambapo itatokezea taa nyengine zaidi kuharibika na hivyo rubani kushindwa kuona vyema.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Pemba kuchukua jitihada za haraka za kuziweka taa hizo ili kuondoa usumbufu

kabla hazijasababisha madhara kwa watumiaji wa uwanja huo, aidha ukaguzi unashauri kuimarisha ulinzi na kuweka uzio ulio imara.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Kwa saa Uongozi wa Mamlaka Pemba umechukua hatua ya kuweka taa 14 za kuongozea ndege (Approach light) kila upande wa RAN WAY badala ya taa 17 kwa mujibu wa muongozo ambazo zote zinafanyakazi kwa mpangilio maalum ambao unafanya kutokuwepo na athari yoyotekatika hatua za utuaji wa ndege, kwani hakujatolewa ripoti yoyote kutoka kwa marubani kuhusiana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na upungufu wa taazo chache.

Hata hivyo, taa zilizopungua zitakamilishwa mara tu baada ya ujenzi wa uwanja utakapo kamilika ujenzi ambao utaanza unatarajiwa kuanza hivi karibuni.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kuchunguza utekelezaji wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kwamba kwa mujibu wa Sheria za Usimamizi na Uendeshaji wa Viwanja vya Ndege Ulimenguni, inaelekeza idadi ya taa zinazotakiwa kuwekwa katika kiwanja cha ndege cha Pemba kwasasa ni taa 14. Hali hiyo inatokana na ukubwa wa kiwanja pamoja na urefu wa njia ya kurukia na kutulia ndege. Kwa msingi huo, Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa hoja hii na kuamua kuiondoa.

MAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI ZANZIBAR (ZIPA)

Taarifa fupi kuhusu utekelezaji wa Kazi za Kamati kwa Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA)

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ya PAC ilipanga kufanya kazi na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) mnamo tarehe 14 Agosti, 2024. Kwa bahati mbaya, Kamati ilishindwa kupata majibu ya hoja nambari 5.1.5.1 inayohusiana dosari zilizojitokeza katika manunuzi ya Ujenzi wa Barabara yenye urefu wa kilomita 13.5 iliopo Micheweni. Kamati iliielekeza Mamlaka ihakikishe inatafuta majibu sahihi ya matumizi ya jumla ya shilingi 6,984,145,000 ili Kamati iweze kujiridhisha kama fedha hizo zilitumika kwa mujibu wa utaratibu kwa kumuelekeza Mkurugenzi wa Mamlaka ua Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) kufuatilia kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ambae ndio aliyekuwa Mkurugenzi wakati wa matumizi ya fedha hizo pamoja na Waziri Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na Katibu Mkuu wake ili kubaini fedha hizo ziliweza kutolewa vipi Hazina na kutumika kama taratibu za kisheria zinavyoelekeza lakini hadi Kamati inawasilisha Ripoti yake hii haijapatiwa utekelezaji wake.

Kamati yako ya PAC haikuishia hapo bali ilichukua juhudi za makusudi za kuandikia barua nyengine ya tarehe 2 Disemba, 2024 yenye kumbukumbu nambari CE.81/204/02A/44 kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji na nakala kuziwasilisha kwa Waziri Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na Katibu Mkuu wake pamoja na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar ikiwa ni ukumbusho lakini hakuna majibu ya barua hiyo wala utekelezaji wake uliofanyika.

MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA ZANZIBAR UNGUJA

Hoja nambari 5.1.9.1: Mapato yaliyokusanywa nje ya mfumo shilingi 70,989,688

Kwa mujibu wa Muongozo nambari 2 (2022/23) – wa kufunga hesabu za mwaka wa fedha 2022/23 sehemu ya 6 Mapato ya kodi (Tax Revenue) na yasio ya kodi (Non Tax Revenue) inataka mapato yote yanayokusanywa na Taasisi kutokana na vyanzo mbalimbali Maafisa Masuuli wahakikishe taarifa za makusanyo ya Mapato ya Kodi (Tax Revenue) na yasio ya kodi (Non Tax Revenue) ziwe zimeingizwa katika mfumo wa ukusanyaji wa mapato wa IFMIS pamoja na kufanyiwa Usuluhishi (Reconciliation) kwa fedha zilizohamishiwa katika Hesabu ya Mfuko Mkuu wa Serikali na taarifa za IFMIS pamoja na kuhakikisha fedha zote zimehamishwa ndani ya mfumo kutoka katika Vote kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali.

Katika kufanya mapitio ya hesabu za benki za Mamlaka, hesabu nambari 406448000 yenye jina Uendeshaji wa Miradi ya Kidimni na hesabu nambari 0827932001 yenye jina Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya Zanzibar, ukaguzi ulibaini kwamba Mamlaka ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 70,989,688 kupitia vyanzo vyake mbalimbali vya mapato bila ya kuzingatia utumiaji wa mfumo wa ukusanyaji wa mapato wa IFMIS.

Ukusanyaji wa mapato nje ya mfumo unaweza kupelekea kukosekana kwa usahihi katika Taarifa za Fedha za Mwisho wa Mwaka zinazoandaliwa na Mamlaka na hatimae kupelekea kuathiri maamuzi ya watumiaji wa Taarifa hizo.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuhakikisha makusanyo yote yanafanyika kupitia mfumo uliowekwa na Serikali. Aidha ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha unazisimamia na kuzifuatilia Taasisi zote zinazokusanya mapato nje ya mfumo ili kuweza kujua changamoto inayowakabili kwa lengo la kuchukuwa hatua za haraka za utatuzi wa changamoto hizo ikiwemo Taasisi hizo kuunganishwa na Mfumo Mkuu wa Serikali ili kuweza kupata taarifa kamili na sahihi za ukusanyaji wa mapato kwa mwaka. Mchanganuo wa mapato yaliyokusanywa nje ya mfumo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 74: Mapato yaliokusanywa nje ya Mfumo wa IFMIS

Chanzo	Nambari ya Hesabu	Kias i

		(Tsh)
Miradi ya Mamlaka	406448000	34,068,854
	0827932001	36,920,834
	Jumla	**70,989,688**

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Ni kweli kua Mamlaka ilikusanya jumla ya fedha **Tzs. 70,989,688** katika Hesabu zake mbili yaani Hesabu ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ambayo ilikusanya jumla ya **Tzs. 36,920,834** na Hesabu ya Uendeshaji wa miradi ya Kidimni ambayo ilikusanya jumla ya **Tzs. 34,068,854**. Katika Hesabu ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za kulevya fedha zilizokusanywa katika Hesabu hii sio i mapato ya serikali ni michango ya waraibu kwaajili ya matibabu mbalimbali pale ambapo ofisi haina fedha za kuwatibu. Hata hivyo matumizi ya fedha hizo yanafuata taratibu zote za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia utekelezaji wa majibu ya hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa ni kweli Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya wamekusanya fedha jumla ya shilingi 70,989,688 nje ya mfumo sababu kuu ya kufanya hivyo ni kuwa fedha hizo zilikuwa zinatokana na michango ya hiari kutoka kwa wananchi wanaoleta waraibu kwa ajili ya kusaidia kupatiwa matibabu pale inapohitajika na kuingia katika Akaunti yao moja kwa moja ya Mamlaka bila ya kupita katika Mfuko Mkuu wa Serikali kama utaratibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nambari 12 ya Mwaka 2016 inavyoelekeza.

Kwa msingi huo, Kamati baada ya kupitia vilelezo vilivyowasilishwa mbele yake imeridhishwa na hatua ilivyochukuliwa na Mamlaka na kuiondoa hoja hii.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauagiza Uongozi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa fedha yote inayokusanywa kutoka katika michango ya hiari ya waraibu kufunguliwa Akaunti maalum na kuwekewa cash book yake ili anapokuja Mkaguzi kuja kufanya ukaguzi fedha hiyo iweze kukaguliwa kama Sheria inavyoelekeza

Hoja nambari 5.1.9.2: Kushindwa kuthibitisha uwepo wa mali za ghalani za jumla ya shilingi 52,059,922.59 zilizoainishwa katika Taarifa za Fedha za Mwisho wa Mwaka

Muongozo nambari 2 (2022/23) – wa kufunga hesabu za mwaka wa fedha 2022/23 sehemu ya 7(c) ya Ufafanuzi wa Taarifa za Fedha (Disclosures) inaeleza kwamba Taasisi zitalazimika "kufanya Stock taking ya mali za mpito (Current Asset), na kuziainisha mali hizo zilizopo hadi kufikia 30 Juni 2023 kwa kuainisha bakaa ya Inventories na Receivables".

Katika kipindi cha ukaguzi, ukaguzi uliomba ripoti ya stock taking kuweza kuvitambua vifaa vilioainishwa ili kuweza kujiridhisha juu ya thamani ya vifaa ilioanishwa katika Taarifa za fedha za mwisho wa mwaka 2022/2023 ambapo Mamlaka waliainisha bakaa la mali za ghalani (Inventory) la jumla ya shilingi 52,059,922.59. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya iliainisha bakaa ya mali za ghalani (Inventories) yenye thamani ya shilingi 87,049,814.70 ambapo imebainika ni pungufu kwa thamani ya shilingi 34,989,892 kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa taarifa za uondoshwaji wa mali zenye thamani ya shilingi 34,989,892 pamoja na kukosekana kwa ripoti ya hesabu za mali zenye thamani ya shilingi 52,059,922.59 iliyoripotiwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka wa fedha 2022/2023.

Pamoja na uwepo wa dosari hizo ukaguzi umeshindwa kuthibitisha uhalali wa taarifa iliyowasilishwa katika ufungaji wa hesabu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jambo ambalo limepelekea kushindwa kutoa maoni sahihi ya ufungaji wa hesabu iliyowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Kushindwa kutambua thamani ya shilingi 34,989,892 ya mali zilizoondoshwa kwenye vitabu vya hesabu kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na thamani halisi ya fedha ya shilingi 52,059,922.59 iliyobainishwa katika vitabu vya hesabu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umetia shaka juu ya usahihi wa taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka zilizowasilishwa na Mamlaka kuonyesha sura sahihi na halisi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuhakikisha unatekeleza miongozo ya Ufungaji wa Hesabu ili taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka ziweze kuonyesha sura sahihi na halisi pamoja na kuweza kufahamu idadi ya mali zilizopo, gharama za mali hizo, mahala zilipo, pamoja na hali ya uchakavu ili kuweza kutoa taarifa za kuziondosha katika vitabu vya hesabu Mali zilizopitwa na muda wa matumizi.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Wakati huo ripoti haikupatikana lakini kwa sasa ripoti hiyo ipo tayari kwa ajili ya ukaguzi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii imegundua kuwa watendaji wa Mamlaka walikuwa wakifanya zoezi la utambuzi wa mali zake zilizopo ghalani “Stock Taking” kinyume na utaratibu wa Sheria inavyoelekeza, hii ilitokana na kukosa uelewa kwamba mwenye Mamlaka ya kufanya utambuzi wa mali za ghalani na kuthibitisha ni Mkaguzi kutoka Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na sio watendaji wa ndani.

Ila kwa sasa hatua iliyochukuliwa na Mamlaka ni kuwa utaratibu wa Sheria unafuatwa ipasavyo na Kamati baada kupitia vielelezo vya barua yenye kumbukumbu namba MKKDF/UK.GS/VOL.1 ya tarehe 04/07/2024 ya kuomba kwa CAG kufanyiwa ukaguzi wa utambuzi wa mali imeridhishwa na hatua za utekelezaji na kuiondoa hoja hii.

Hoja nambari 5.1.9.3: Kukosekana kwa Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi (Risk Management Framework)

Kwa mujibu wa kanuni nambari 154, 155 na 156 za Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021, Afisa Masuuli wa Taasisi ya Umma anapaswa kutengeneza, kutekeleza na kuimarisha Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi (Risk Management Framework). Aidha, Afisa Masuuli anapaswa kuhakikisha kuwa ripoti za usimamizi wa vihatarishi (risk management reports) zinawasilishwa katika kamati ya ukaguzi angalau mara nne (4) kwa mwaka.

Ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya bado haina Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi (Risk management Framework) sambamba na kukosa kuwasilishwa ripoti za usimamizi wa vihatarishi katika kamati ya ukaguzi. Hali hii inaweza kupelekea Mamlaka kushindwa kutambua na kuingiza katika mikakati na mipango ya Taasisi vihatarishi vilivyopo na vinavyoweza kuwepo katika utendaji kazi wa Taasisi hiyo ikiwemo vihatarishi vya kisheria (legal risks), vihatarishi vya uhalifu mitandaoni (cyber security risks), na vihatarishi vya mazingira ya utendaji kazi (operational risks).

Kutokuanzisha, kutekeleza na kuimarisha Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi ni kwenda kinyume na kanuni nambari 154, 155 na 156 za Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuhakikisha unaanzisha, unatekeleza na kuimarisha

Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi (Risk Management Framework) kwa mujibu wa Kanuni

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Mamlaka katika hatua za kuhakikisha inaanzisha mfumo wa usimamizi wa vihatarishi, imewapeleka maofisa wake kupata mafunzo katika taasisi ambazo zimeanzisha mfumo huo, jumla ya wafanyakazi watatu wanaendelea na mafunzo hayo kwa ajili ya kuja kushughulikia mfumo huo**.**

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilipokuwa ikifanya uchunguzi wake juu ya utekelezaji wa majibu ya hoja hii imebaini wakati wa ukaguzi ulipofanyika ni kweli Mamalaka ya Kudhibiti na kupambana na Dawa za Kulevya ilikuwa haina wataalam wanaohusiana na Usimamizi Viashiria Hatarishi "Risk Management". Ila juhudu mbali mbali walichukua za kuhakikisha upatikanaji wa wataalam hao kwa kuandika barua za maombi kwa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kujibiwa kuwa hawana wataalam hao,

Kamati imeelezwa kwa sasa wanapatiwa mafunzo hayo na wataalam kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF isipokuwa lengo la Mamlaka ni kuajiri wataalam wao wa ndani ili kuweza kufikia dhumuni la kuanzishwa kwa mfumo huu wa Usimamizi Viashiria Hatarishi.

Kwa mnasaba huo, Kamati ya PAC imeridhishwa na hatua za utekelezaji walizochukua Mamlaka na kupelekea hoja hii kuondolewa.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauagiza Uongozi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuhakikisha wanasimamia kikamilifu upatikanaji wa ajira za wataalam hao ili kusaidia uanzishwaji, utekelezaji wa Mfumo huu wa Usimamizi wa Vihatarishi kama Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Mwaka 2021 inavyoelekeza

Hoja nambari 5.1.9.4: Kuchelewa kukamilika kwa mradi wa ujenzi

Katika ukaguzi wa 2022/2023 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar kupitia Miradi ya Maendeleo ilipanga kukamilisha jengo na huduma nyengine za jengo ambapo Mamlaka ilipanga bajeti ya shilingi 5,000,000,000 fedha yote hii ni kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Ukaguzi wa Mradi wa kukamilisha jengo umefanywa kwa lengo la kuangalia hali halisi ya utekelezaji wa mradi pamoja na tija inayopatikana kutokana na mradi huo. Aidha, ukaguzi umekagua taratibu mbali mbali zinazohusiana na utekelezaji wa mradi ikiwa ni pamoja na kupima kiwango

cha ufanisi kilichofikiwa kutokana hatua zilizochukuliwa kwa lengo lililokusudiwa katika utekelezaji wa mradi huo

Kupitia Taarifa za Fedha za Mwisho wa Mwaka 2022/2023, ukaguzi ulibaini kwamba kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Mamlaka ilifanya malipo ya jumla ya shilingi 2,075,254,873 kwa ajili ya kuendeleza shughuli za mradi wa Ujenzi. Mnamo tarehe 2 Februari 2024 ukaguzi ulitembelea maeneo mbalimbali ya mradi na kubaini kuwa mkandarasi ameshindwa kukamilisha kazi kwa wakati kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba pamoja na makubaliano wa muda nyongeza, ambapo kwa mujibu wa barua ya tarehe 8 Machi 2023 kuhusiana na nyongeza ya mkataba wa Ujenzi yenye kumbukumbu nambari MKKDK/U.10/VOL.2/… kwenda kwa kampuni ya M/S AZHAR Construction Co. Ltd ujenzi ulitakiwa kukamilika tarehe 30 Novemba 2023 huku muda wa uangalizi ukiwa ni mwaka mmoja, aidha hadi ukaguzi unafanya kikao cha kufunga Ukaguzi tarehe 05/2/2024 shughuli za Ujenzi zilikua bado zinaendelea ikiwemo ukarabati wa maeneo mbalimbali kama upakaji rangi jengo la Mnara wa mbao na kushindwa kufunga milango pamoja na CCTV Camera kwa jengo la Kidimni na shughuli za usafishaji wa eneo kwa Kidimni na Mnara Mbao.

Kushindwa kukamilisha kwa makubaliano ya utekelezaji wa miradi kwa wakati kunaweza kusababisha uwepo wa matumizi ya ziada ambayo sio ya msingi yanayoweza kusababishwa na kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa mradi huo kunakosababishwa na mfumko wa bei ya vifaa vya ufundi. Aidha, kunaweza kupelekea kushindwa kunufaika na kipindi cha uangalizi kilichowekwa (Defect Liability Period)

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar kufanya ufuatiliaji wa vipengele vyote vya mikataba ili kuweza kufikia viwango vya ubora wa kazi iliyokusudiwa, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba mradi unatekelezwa ndani ya muda uliopangwa kwa kuhakikisha bajeti iliyopo inatosha ndipo ifunge mkataba

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Mamlaka imechukua ushauri wa Mkaguzi na kwa sasa mradi umeshakamilika na tumeshakabidhiwa rasmi kupitia certificate iliyotolewa tarehe 22 Machi, 2024

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imeridhishwa na utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Kidini na hatimae kuiondoa hoja hii.

Hoja nambari 5.1.9.5: Dosari katika mradi wa Ujenzi Kidimni

Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 inataka manunuzi yote kufanyika kwa kuzingatia thamani halisi ya fedha (Value For Money).

Kupitia Taarifa za Fedha za Mwisho wa Mwaka Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya iliainishwa malipo ya jumla ya shilingi 3,141,798,476 kwa ajili ya maboresho na Ujenzi kwa kituo cha Kidimni ikiwa ni utekelezaji wa mkataba nambari SMZ/C0401/W/ICB/2021-2/21 uliosainiwa tarehe 16 Machi 2022 baina ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar na mkandarasi M/S AZHAR Construction Co. Ltd.

Kupitia ziara ya Ukaguzi kwenye maeneo ya mradi, ukaguzi ulibaini uwepo wa dosari mbalimbali katika utekelezaji wa mradi huo ikiwemo kuharibika kwa maeneo mbalimbali ya majengo yaliojengwa ikiwemo tiles za kingo za chini ya kuta kabla ya hata majengo hayo kuanza kutumika.

Kuwepo kwa dosari hizi katika miradi ya ujenzi kunaweza kupelekea kukosekana kwa uimara wa majengo pamoja na kushindwa kuzingatia thamani halisi ya fedha katika ujenzi uliojengwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar kuhakikisha unaboresha na kusimamia ipasavyo majengo yaliojengwa na kuhakikisha majengo yote yamejengwa kwa ubora unaotakiwa katika maeneo yote ya mradi kabla kukamilisha malipo kwa mkandarasi.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Dosari zote zimeshaondoshwa kwa kufanya marekebisho kwa gharama za mjenzi kwa kutumia kipindi cha “Defect Liability Period”

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC baada ya kupokea majibu ya utekelezaji wa hoja hii imeridhishwa na maboresho yaliofanyika katika Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Kidini na kupelekea kuiondosha hoja hii,

Hoja nambari 5.1.9.6: Uhifadhi usioridhisha wa vielelezo vya dawa za kulevya zilizokamatwa

Kifungu cha 50(e) cha Sheria nambari 8 ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar ya 2021 inaitaka Mamlaka kutunza vyema vifaa vilivyozuiliwa ili kuepuka uwezekano wa kupotea, kuibiwa, kusinyaa, kushuka kwa ubora au thamani yake.

kaguzi ulifanya ziara katika maeneo ya kuhifadhia dawa za kulevya yaliofanikiwa kukamatwa (Kidimni) na kubaini kwamba Mamlaka imeshindwa kuanzisha utaratibu mzuri wa uhifadhi wa dawa hizo hali inayoweza kupelekea upotevu wa madawa hayo (Kuibiwa) na hata kuhatarisha usalama wa wanaohusika katika uhifadhi wa dawa hizo.

Miongoni mwa dosari zilizobainika ni pamoja na;

- Kukosekana kwa 'CCTV Camera' katika jengo na chumba cha uhifadhi wa dawa za kulevya.
- Uhifadhi usioridhisha wa dawa za kulevya zilizokamatwa kutokana na kuchanganya dawa zinazotakiwa kuangamizwa pamoja na vielelezo vinavyohifadhiwa.
- Uwepo wa vifungashio vya kuhifadhia dawa za kulevya vilivyochanika hali inayopelekea dawa hizo kupotea.

Uwepo wa uhifadhi usioridhisha wa dawa za kulevya unaweza kuhatarisha usalama wa wahusika wanaosimamia uhifadhi wa dawa za kulevya lakini pia kunaweza kupelekea upotevu wa dawa za kulevya na kushindwa kubaini muhusika wa upotevu huo kutokana na kutokuepo kwa uhifadhi mzuri pamoja na CCTV camera.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar kuhakikisha wanaboresha njia za uhifadhi wa dawa za kulevya ili kuepusha kujitokeza kwa vitendo vya ukosefu wa maadili kwa baadhi ya watumishi kuweza kutumika kupoteza ushahidi au kufanya utoroshaji wa dawa hizo kwa maslahi binafsi

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Mamlaka tayari imekamilisha ujenzi wa Jengo la Utawala katika ofisi zake za Kidimni. Katika jengo hilo kuna sehemu maalumu ya uhifadhi wa vielelezo, na kwa sasa vielelezo vyote vimeshahamishiwa katika chumba maalumu ambacho ni salama kwa vielelezo hivyo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, imebaini kuwa Mamlaka tayari imeshakamilisha ujenzi wa jengo la Utawala katika eneo la kidini pamoja na kuwepo kwa taaribu maalum wa uhifadhi wa vielelezo vinavyohusiana na Dawa za Kulevya.

Kwa Msingi huo, Kamati imeridhishwa na hatua za utekelezaji wa hoja hii na kuiondoa.

Hoja nambari 5.1.9.7: Malimbikizo ya Madeni ya muda mrefu shilingi 55,421,635

Ukaguzi umepitia na kukagua nyaraka mbali mbali ikiwemo hesabu ya mwisho wa mwaka na kubaini kwamba jumla ya taasisi 2 za Serikali zinaidai Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar kiasi cha shilingi 55,421,635 kutokana na huduma mbali mali alizopatiwa na taasisi hizo.

Kutokana na uwepo wa deni hilo ukaguzi umefanya tathmini ya kina na kubaini kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Mamlaka ilikuwa ikidaiwa jumla ya shilingi 10,296,505 na Mfuko wa Maendeleo – JKU pamoja na Shirika la Bima la Zanzibar.

Aidha kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi umebaini uwepo wa ongezeko la deni hilo na kufikia jumla ya shilingi 55,421,635 inalotokana na Mamlaka kuendelea kupatiwa huduma na taasisi hizo bila ya kuonyesha juhudi za kupunguza ukuaji wa deni hilo ambalo limeongezeka kwa wastani wa asilimia 438.26

Kuendelea kuongezeka kwa deni hilo kunaweza kupelekea kusuasua kwa utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka hivyo kuzotesha utekelezaji wa mpango waliojipangia na hatimae kutokufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar kuweka mikakati maalum na kuchukuwa hatua madhubuti katika kusimamia ulipaji wa madeni ili kufikia malengo yaliowekwa na kuongeza ufanisi kwa Mamlaka na Serikali kwa ujumla.

Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Malimbikizo ya Madeni hayo yemesababishwa na uingizwaji mdogo wa Fedha za Matumizi mengineo kutoka Serikali Kuu, hata hivyo Mamlaka inajitahidi kupunguza madeni hayo kadiri ya fedha zinavyoingia**.**

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, ilibaini kwamba kweli wakati mkaguzi anatekeleza majukumu yake katika Mamlaka kulikuwepo na malimbikizo ya Madeni ya muda mrefu yaliofikia jumla ya shilingi 55,421,635. Hata hivyo, Kamati ilipohoji ni juhudi gani Mamlaka imechukua ya kuhakikisha madeni hayo yamepunguzwa na kueleza kwamba Mamlaka itawasilisha taarifa hizo ambapo hadi Kamati inakamilisha kazi ya uchunguzi wake taarifa hizo hazikuwasilishwa.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauagiza Uongozi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuhakikishwa kunakuwepo na utaratibu mzuri wa uhifadhi wa vielelezo ili wakati wa ukaguzi vinapohitajika viweze kupatikana.

Hoja Nambari 5.1.9.8: Dosari zilizobainika katika utekelezaji wa Sheria

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya inaendelea na utekelezaji wa majukumu yake kama yalivyotajwa katika Sheria nambari 8 ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya 2021, katika vifungu mbalimbali ambapo katika utekelezaji wa kazi hizo ukaguzi umebaini uwepo wa kesi mbalimbali zilizoripotiwa, kuwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na kuchukuliwa hatua za Mahkama kama ifuatavyo:-

- Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya kesi 498 ziliripotiwa ambapo kesi 354 majalada yake yamefikishwa Mahkamani na kesi 72 bado zinaendelea na hatua za upelelezi, kesi 41 vielelezo vyake havikutambulika kuwa ni dawa za kulevya na kesi 31 zimefungwa na Mkurugenzi wa Mashtaka.

- Uwepo wa ongezeko la kesi zilizofikia 498 ukilinganisha na kesi zilizoripotiwa mwaka uliopita ambazo zilikuwa kesi 312. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 59.6 ya ongezeko la kesi zote.

Aidha, katika hatua za upelelezi wa Tuhuma mbalimbali zilizowakabili watuhumiwa wa dawa za kulevya ukaguzi umebaini uwepo wa tuhuma 103 ambazo ziliendelea kuchukuliwa hatua mbali mbali za ukusanyaji wa vielelezo, uchukuwaji wa maelezo ya mashahidi, pamoja na upitiaji wa taarifa zinazohusiana na tuhuma hizo ili kuweza kuwasilishwa Mahkamani kwa ajili ya kutolewa hukumu. Miongoni mwa tuhuma hizo ni kama zilivyobainshwa katika jadweli liliopo hapo chini:-

Jadweli Nambari 75: Idadi ya Tuhuma katika hatua ya upelelezi hadi Oktoba, 2023

Aina ya Dawa	Jumla ya Kesi	Mamlaka	Mkurugenzi wa Mashtaka	Mkemia	Zilizofungwa na DPP
Heroin	25	10	1	5	9
Kokeni	2	-	-	2	

Bangi	74	34	8	10	22
Valium	1	1	-	-	
Mirungi	1	1	-	-	-
Jumla	**103**	**46**	**9**	**17**	**31**

Pamoja na uwepo wa tuhuma 103 zinazoendelea katika hatua mbalimbali za uchunguzi ukaguzi umebaini hadi kufikia Oktoba, 2023 jumla ya majalada 286 ya kesi za dawa za kulevya yamefikishwa katika Mahkama mbalimbali za Unguja na Pemba. Mchanganuo wa majalada hayo ni kama unaonekana katika jadweli kama ifuatayo:-

Jadweli Nambari 76: Idadi ya majalada ya kesi zilizofikishwa Mahkamani hadi Oktoba2023

Mahkama Unguja	Idadi	Mahkama Pemba	Idadi
Mahkama Kuu Tunguu	111	Mahkama Kuu Chake Chake	7
Mahkama ya Mkoa-Vuga	85	Mahkama ya Mkoa Wete	8
Mahkama ya Mkoa-Mwera	25	Mahkama ya Mkoa Chake Chake	18
Mahkama ya Mkoa-Mahonda	32	--	--
Jumla	253		33

Katika ufuatiliaji wa mwenendo wa mashauri ya kesi Mahkamani ukaguzi umebaini jumla ya kesi 354 ziliripotiwa Mahkamani ambapo kati ya kesi hizo jumla ya kesi 206 ziliachiwa huru kutokana na sababu mbalimbali zilizopelekea watuhumiwa kutokuwa na kesi ya kujibu na hatimae Mahkama kuamuru watuhumiwa hao kuachiwa huru kwa mujibu wa taratibu za kimahakama. Aidha, jumla ya kesi 122 bado zinaendelea na hatua ya kujiridhisha kutokana na vielelezo vilivyowasilishwa Mahkamani pamoja na hatua za kuwasikiliza mashahidi. Vile vile jumla ya kesi 26 zilitolewa hukumu kwa watuhumiwa kuweza kutiwa hatiani ima kwa kulipa fidia, kutumikia kifungo au mambo yote mawili kwa pamoja.

Kutokana na idadi kubwa ya kesi zilizoachiwa huru ukaguzi umebaini pamoja na uwepo wa sababu nyenginezo suala la upatikanaji wa shahidi huru, utambuzi wa watuhumiwa, watuhumiwa kutokupewa haki, mashahidi kushindwa kufika mahkamani huwenda ikawa ni kichocheo pekee kilichopelekea kukosekana kwa nguvu ya kisheria na hatimae Mahkama kuamuru kuwaachia huru watuhumiwa.

Pamoja na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ikiwemo kufanya maboresho na mapitio mapya ya Sheria nambari 8 ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya 2021 ukaguzi unaushauri ni vyema suala la upatikanaji wa shahidi huru kutizamwa kwa upana wake kwani ni miongoni mwa sababu zinazopelekea idadi kubwa ya kesi kuachiwa huru hivyo ni vyema shahidi huru kutumika wakati wa upekuzi wa madawa ya kulevya kwa watuhumiwa. Mchanganuo wa mwenendo wa kesi hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 77: Hatua za kesi zilizofikishwa Mahkamani hadi Oktoba,2023

Aina ya dawa	**Jumla ya kesi**	**Zilizoachwa huru**		**Zinazoendelea Mahkamani**		**Zilizopata hatia**	
		Unguja	**Pemba**	**Unguja**	**Pemba**	**Unguja**	**Pemba**
Heroine	146	63	24	38	10	6	5
Kokeni	4	2	-	1	-	1	-
Bangi	201	105	10	57	15	5	9
Mirungi	1	-	-	1	-	-	-
Valium	2	1	1	**-**	**-**	**-**	**-**
Jumla	**354**	**171**	**35**	**97**	**25**	**12**	**14**
		206		**122**		**26**	

Majibu ya Uongozi wa Tume

Sheria imefanyiwa marekebisho kwa kuondoa dosari zote zilizojitokeza kutokana na suala zima la shahidi huru, aidha marekebisho hayo yameenda na maamuzi ya Mahkama ili kuhakikisha kesi za dawa za kulevya zinapata hatia, ambapo jumla ya vifungu 18 vya sheria vimefanyiwa marekebisho, na tayari vimeshapitishwa na Baraza la Wawakilishi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kwamba kasoro zote zilizoorodheshwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali kuhusu mapungufu yaliomo katika utekelezaji wa Sheria iliopita tayari mapungufu hayo yote yameshafanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali Namba 5 ya Mwaka 2024.

Kwa Msingi huo, Kamati ya PAC imeridhishwa na hatua za utekelezaji na kuiondoa hoja hii.

MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA ZANZIBAR - PEMBA

Hoja nambari 5.1.9.9: Kukosekana kwa usafiri wa uhakika wa ufuatiliaji wa kazi za mamlaka za utoaji taaluma kwa wananchi

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Pemba inalojukumu la kutembelea katika skuli na shehia mbalimbali ili kutoa taaluma kwa wanafunzi, vijana na jamii kwa ujumla juu ya athari za dawa za kulevya na kufuatilia taarifa za utumiaji, uuzaji, usambazaji na usafirishaji wa dawa hizo.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka inamiliki gari moja ambayo ni chakavu na inayoigharimu Mamlaka fedha nyingi kwa ajili ya matengenezo hali inayoweza kupelekea kuzorota kwa shughuli nyengine muhimu za Mamlaka. Kukosekana kwa usafiri wa uhakika kunaweza kusababisha kutokutolewa elimu kwa wakati kwa wanafunzi, vijana na jamii hali inayoweza kupelekea Mamlaka kushindwa kufikia lengo lililokusudiwa**.**

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Pemba kuhakikisha wanatenga fedha za kutosha kwa lengo la kununua vyombo vya usafiri ili kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi**.**

Majibu ya Uongozi wa Tume

Ofisi ya Mamlaka Pemba tayari imepokea gari mbili kwa ajili ya shughuli za ufuatiliaji wa kazi pamoja na utoaji wa elimu badala ya gari moja iliyokuwepo awali. Licha ya kupatiwa gari hizo bado ipo haja ya kupatiwa gari nyingine kwa ajili ya kuendesha shughuli za Operesheni

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika ufuatiliaji wa majibu ya hoja hii, kamati imebaini kuwa licha ya Mamlaka ya kudhibiti na kupambana na madawa ya kulenya kukiri kupatiwa gari mbili kwa ajili ya kusaidi shughuli za utekelezaji wa

majukumu yao ya kazi bado Mamlaka inauhitaji kupatiwa usafiri, rasilimali na vifaa vya kutendea kazi ili kusaidia kufanyika kwa doria kwa ufanisi ili kundoa janga la Taifa.

Pamoja na kupatika kwa gari hizo kamati ya PAC imebaini kuwa gari aina ya Prado ilitaifishwa kutoka kwa mtuhumiwa kwenda kwa mamlaka Ofisi ya Pemba kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za operesheni, bado Gari hiyo haijawa na umiliki halali na kuoneka katika Fixed Asset Register kama utaratibu wa sharia ya Msajili wa Hazina inavyoeleza.

Kwa Msingi huo, kamati ya PAC imeibakisha hoja hii kwa ajili ya ufuatiliaji wa hatua za utekelezaji.

Magizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauagiza Uongozi wa Mamlaka ya kudhibiti na kupambana na madawa ya kulenya kuhakikisha Mali zote wanazozimiliki zinasajiliwa katika daftari la usajili wa Mali za Serikali (Fixed Asset Register) ili kuepusha upotevu wa mali za Serikali.

Hoja nambari 5.1.9.10: Kukosekana kwa usiri katika utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Afisi ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Pemba siyo tu kwamba imezungukwa na taasisi nyengine bali imo katika jengo moja na Afisi ya Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu pamoja na Afisi ya Tume ya Haki za Binadamu.

Hali hii inaweza kupelekea kukosekana kwa usiri katika utekelezaji wa majukumu yao ambapo kwa uhalisia wa kazi zake inahitaji kuwepo katika Afisi iliyojitenga na ofisi nyengine ili kuweza kufanya kazi zake ipaswavyo na kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuhakikisha wanapeleka pendekezo maalum Serikalini la kupatiwa Afisi ya faragha ili kuweza kutekeleza majukumu yao kwa usiri mkubwa.

Majibu ya Uongozi wa Tume

Kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 ni kweli Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ilikuwa inakabiliwa na suala la kutokuwa na usiri kutokana na jengo la ofisi limezungukwa na taasisi nyengine pia jengo hilo moja linatumiwa na Ofisi ya Baraza la Watu wenye Ulemavu na Ofisi ya Tume ya Haki za Binaadamu ila kwa sasa Ofisi ya Mamlaka ya Pemba mnamo tarehe 01/11/2024 imepata eneo na jengo la ofisi ambalo lilikuwa linamilikiwa na Wizara ya Kilimo,Umwagiliaji na Maliasili Zanzibar.

Jengo hilo la ofisi lipo katika shehia ya Pujini, wilaya ya Chake Chake Pemba.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC baada ya kupokea majibu ya utekelezaji hii, imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Mamlaka ya kudhibiti na kupambana na madawa ya kulenya ya kupatiwa jengo katika eneo la Pujini liliokuwa la Wiara ya kilimo, umwagiliaji, maliasili na Mifugo ili kusaidia kufanya kazi zao katika mazingira ya usiri kama Mkaguzi alivyoshauri.

Aidha, wakati wa majadiliano Kamati imegundua licha ya kupatiwa jengo hilo ila bado halimo katika Daftari la Usajili wa Mali zao za Mamlaka. Kamati imeondosha hoja.

Magizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauagiza Uongozi wa Mamlaka ya kudhibiti na kupambana na madawa ya kulenya kuhakikisha Mali zote wanazozimiliki zinasajiliwa katika daftari la usajili wa Mali za Serikali (Fixed Asset Register) ili kuepusha upotevu wa mali za Serikali

Hoja nambari 5.1.9.11: Kukoseka kwa vifaa vya kisasa vya ukaguzi wa Dawa za Kulevya.

Kwa mujibu wa kanuni nambari 126 ya Kanuni ya utumishi wa umma ya mwaka 2014 inaeleza kwamba “Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi atalazimika kuhakikisha kuwa mtumishi anaefanya kazi katika mazingira yanayohitaji vifaa maalum vya kutendea kazi anapatiwa vifaa hivyo”.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Pemba haina vifaa vya kisasa, mfumo mzuri na imara wa ukaguzi wa mizigo na abiria katika bandari na uwanja wa ndege Pemba ili kuweza kubaini dawa za kulevya zinazoingia au kutoka katika kisiwa cha Pemba. Hali hii inaweza kupelekea watu wasiowaadilifu kuingiza au kutoa dawa za kulevya katika kisiwa cha Pemba kwa urahisi. Ukaguzi unaishauri Serikali kupitia Mamlaka kuhakikisha inaipatia vitendea kazi vyenye ubora na vya kisasa ili kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi

Majibu ya Uongozi wa Tume

Suala la vifaa vya ukaguzi wa Dawa za Kulevya katika maeneo ya uingiaji na utokaji Pemba limewasilishwa katika kikao cha Baraza la Taifa la Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, na tayari Mwenyekiti ametoa maagizo kwa wizara inayoshughulika na Bandari na Viwanja vya ndege kununua vifaa vitakavyoweza kugundua Dawa za Kulevya. Kwa sasa vipo vifaa vya ukaguzi vya kawaida tu.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya juhudi mbali mbali ambazo Mamlaka wamechukua za kufanya vikao vya pamoja na Mamlaka ya Uwanja wa Ndege na Shirika la Bandari juu ya Umuhimu wa uwekaji wa vifaaa vya ukaguzi wa madawa katika maeneo ya usafiri kamati ya PAC imebebaini jukumu la uwekaji wa vifaa vya ukaguzi ni la Mamlaka ya husika za usafirishaji na sio jukumu ya Mamlaka ya kudhibiti na kupambana na madawa ya kulenya ambapo hadi kamati inakamailisha uchunguzi wake vifaa hivo havijanunuliwa.

Kwa mnasaba huo, kamati ya PAC haijaridhishwa na hatua za utekelezaji wa hoja hii na kupelekea kubakia kwa hoja.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauagiza Uongozi wa Tume ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuhakikisha wanafanya kikao cha pamoja na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kulitafutia ufumbuzi wa haraka suala la ununuzi wa vifaa vya ukaguzi wa dawa katika maeneo yote ya Viwanja vya Ndege pamoja na Bandari ili kuondokana na upitishaji wa dawa ndani ya nchi yetu kiholela.

MAMLAKA YA MAWASILIANO ZANZIBAR (ZICTIA)

Hoja nambari 6.1.2.1: Dosari katika uandaaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka

Kwa mujibu wa miongozo ya ufungaji Hesabu ya IPSAS Cash Basis 1.3.26 inaeleza kwamba, taarifa za awali za mapato na matumizi pamoja na taarifa nyenginezo za fedha kutolewa mchanganuo wake katika taarifa za uchanganuzi (Notes of the financial statement). Aidha, IPSAS Cash Basis 1.3.25 (b) kinasisitiza taarifa za Hesabu kuwasilishwa kwa kuzingatia usahihi na usawa.

Ukaguzi ulipitia taarifa za fedha za mwaka 2022/2023 zilizowasilishwa na Wakala na kubaini uwepo wa baadhi ya vifungu vilivyoainishwa katika taarifa ya mapato na matumizi ya fedha (Statement of Cash Receipts and Payments) pamoja na taarifa ya mtiririko wa fedha (Statement of Cashflow) zilibainisha uwepo wa kifungu cha mapato mengineyo (other receipts) chenye jumla ya shilingi 4,227,531,817 ambazo hazijabainishwa mchanganuo wake katika taarifa zilizoainishwa katika maelezo ya taarifa ya fedha (Notes of the Financial Statement).

Uandaaji wa Taarifa za Fedha za Mwisho wa mwaka bila ya kuzingatia miongozo ya ufungaji wa Hesabu ya IPSAS Cash Basis inaweza kupelekea kuathiri maamuzi ya watumiaji wa Taarifa za Fedha.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA kufanyia mapitio Taarifa zake za fedha za mwisho wa mwaka na kuhakikisha taarifa zinaandaliwa kwa kuzingatia usawa na usahihi.

Majibu ya Uongozi ZICTIA.

Kwa mujibu wa taarifa za fedha za mwaka 2022/2023 zilizowasilishwa kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), nathibitisha kwamba taarifa za awali za mapato na matumizi pamoja na taarifa nyenginezo za fedha zenye jumla ya Shilingi 4,227,531,817 mchanganuo wake ulitolewa katika taarifa za uchanganuzi (Notes to the FINANCIAL STATEMENT) kwa mujibu wa miongozo ya ufungaji Hesabu ya IPSAS Cash Basis 1.3.26 kama inavyoonekana katika ukurasa wa 19 wa taarifa hiyo (Note 14).

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, Kamati ya Hesabu za Serikali imebaini yafuatayo:

1. Kuwepo kwa kasoro katika uainishaji wa taarifa za ufafanuzi wa mapato na Matumizi (Note). Kwa mfano taarifa za ‘Note’ nambari 15 zilitakiwa ziwe za nambari 14.

2. Kuwepo tofauti ya fedha zilizobainika katika usuluhishi wa kibenki ambapo taarifa za benki zimeonekana kuwa shilingi Bilioni 4.06 wakati katika vitabu kuna bilioni 4.22. hili limetokana na kujitokeza makosa katika 'note' nambari 11 ya 'other receipt' ambapo Mamlaka imerekebisha.
3. Kujitokeza kwa taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka tatu tofauti, kulikuwa na ya awali ambayo ilipekewa kwa Mkaguzi kwa ukaguzi na kurudishwa ili ifanyiwe marekebisho, ya pili iliyofanyiwa marekebisho lakini ilichelewa kurudishwa kwa Mkaguzi na ya tatu iliyopewa Kamati.
4. Kuwepo kwa 'note' ambazo zimejumuisha vitu vingi na tofauti vinavyotakiwa kuwemo katika katika 'note' nyengine.

Kwa vile changamoto iliyojitokeza iliwahi kurekebishwa, Kamati ya PAC imeamua kuiondoa.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Kamati inaiagiza Mamlaka ya Mawasiliano kufunga taarifa zake za hesabu ya mwisho wa mwaka kwa mujibu wa viwango vya kitaifa, kimataifa na miongozo kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango
2. Mamlaka ya Mawasiliano Zanzibar ihakikishe inawasilisha taarifa zake za hesabu za mwisho wa Mwaka kwa Mkaguzi kwa wakati.

Hoja nambari 6.1.2.2: Tofauti iliyojitokeza katika taarifa za fedha shilingi 2,672,032,699

IPSAS Cash Basis 1.3.27 inaeleza kwamba, taarifa za fedha za mwisho wa mwaka zitalazimika kuwa zenye kueleweka, taarifa zenye usahihi, zilizokamilika, zisizo na makosa, zenye uwiano kwa vipindi tofauti na pia ambazo zitaweza kuthibitishwa.

Ukaguzi ulipitia Taarifa za Fedha za Mwisho wa Mwaka 2022/2023 na kubaini jumla ya shilingi 4,063,749,680.39 ziliripotiwa katika taarifa hizo na shilingi 6,735,811,870.87 ziliripotiwa katika daftari Kuu la Mapato na kupelekea uwepo wa tofauti katika taarifa za fedha jumla ya shilingi 2,672,032,699 jambo ambalo limetia shaka juu ya uwepo wa tofauti hiyo ambapo hadi ukaguzi unamalizika maelezo ya tafauti hiyo hayajapatikana.

Kushindwa kuainisha makusanyo ya jumla ya shilingi 2,672,032,699 katika taarifa za fedha za mwisho wa mwaka kunaweza kupelekea kuathiri maamuzi ya watumiaji wa Taarifa za Fedha za Mwisho wa Mwaka kwa kushindwa kubaini kiasi halisi cha fedha kilichokusanywa.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA kuhakikisha unazifanyia mapitio taarifa za fedha za mwisho wa mwaka kwa

kulinganisha na taarifa zilizomo katika daftari la mapato ili kuweza kuhakikisha upatikanaji wa taarifa zilizokamilika na zenye usahihi.

Hali halisi wa mapato kwa mujibu wa Cash book ni kama inayoonekana katika jadweli hapo chini:

Taarifa za Mapato kwa Tanzania Shilingi

Tarehe	**Jina**	**Nambari ya bili**	**Kiasi kilicholipwa (Tshs)**
7/6/2022	Katibu Mkuu Wizara ya Maji Nishati (Michenzani Mall)	188	3,961,500
7/6/2022	Commissioner ZRA	189	36,320,400
7/8/2022	M/Mtendaji Mamlaka ya M/Amali (Vitongoji)	191	9,269,000
18/7/2022	The Institute Of Public (IPA)	193	11,536,800
19/7/2022	Katibu Mkuu Wizara ya Elimu Na M/Amali (Elimu FM)	195	5,448,800
26/7/2022	Kamishna Bodi ya Mapato Zanzibar (Gombani PBA)	196	7,521,000
8/3/2022	Kamishna Idara ya Michezo (Viwanja Vya Mpira)	199	9,960,000
8/4/2022	Dhiabu Moh'd Dhiabu wa Mbeleo	200	6,000,000
8/9/2022	Wakala wa Maendeleo ya Viwanda SMIDA	201	4,665,000
8/9/2022	Chief Executive Officer Zanztel (AUG)	202	34,951,122
8/11/2022	Mamlaka ya Viwanja Vya Ndege (Terminal III)	205	15,092,000
29/8/2022	Taasisi ya Elimu Zanzibar	208	3,076,250
9/5/2022	Megha Engineering	211	12,000,000
9/7/2022	Estim Enterprises Ltd	212	17,629,500

9/7/2022	Chief Executive Officer Zantel (Sept)	213	34,967,427
9/7/2022	Katibu Mkuu Wizara ya M/Jamii Zanzibar (Sebleni)	215	6,618,250
15/9/2022	Kamishna Zimamoto (Ofisi Kuu)	217	6,710,250
16/9/2022	M/Mtendaji Mamlaka ya M/Amali (Beit-El-Rais)	218	4,749,500
19/9/2022	M/Mtendaji Kampuni ya Uvuvi (Ofisi za ZAFICO)	219	2,265,500
21/9/2022	M/Mkuu Taasisi ya Utafiti (Kizimbani)	221	3,478,261
21/9/2022	Mkurugenzi Mtendaji Mfuko Wa Barabara	222	1,345,500
26/9/2022	Zanzibar Bureau Of Standards (ZBS)	223	3,184,279
26/9/2022	Mrajis Bodi ya Kondonominia (Sensa) (Shangani)	225	3,363,000
30/9/2022	Mkurugenzi Matrekta (Mbweni)	226	2,687,650
30/9/2022	M/Mtendaji Idara Ya Kilimo (Mbweni)	227	4,408,000
10/4/2022	Ofisi ya Wakala wa Vipimo Pemba	229	3,473,000
10/4/2022	Wakala Wa Usalama/ Barabarani Pemba (M/Usafiri PBA)	230	3,343,500
10/4/2022	Karakana Kuu ya Magari - Pemba (Ofisi Kuu)	231	4,266,250
10/4/2022	Usajili Wa Biashara na Mali - Pemba (Ofisi Kuu)	232	2,570,750
10/6/2022	M/Mtendaji Mamlaka ya M/Amali (Makunduchi)	234	8,630,750

10/6/2022	Chief Executive Officer Zantel (OC)	235	34,967,427
17/10/2022	Mkuu wa Skuli ya Sheria Zanzibar	240	3,126,000
27/10/2022	Mkurugenzi Salem Contruction	246	16,663,500
28/10/2022	Management & Development Health PBA	247	5,272,750
11/2/2022	Wakala Wa Usajili Wa Matukio	248	19,377,500
11/2/2022	Wakala Wa Usajili Wa Matukio	249	3,967,500
11/10/2022	Kamishna Bodi Ya Mapato Zanzibar	250	8,320,250
11/10/2022	Kamishna Bodi Ya Mapato Zanzibar	251	5,313,000
11/11/2022	Taasisi Ya Utafiti Wa Mifugo	253	4,248,300
14/11/2022	Wakala Wa Majengo Zanzibar	254	3,082,000
15/11/2022	Wakala Wa Matukio Ya Kijamii	255	4,105,500
16/11/2022	Shirika La Bima Zanzibar	258	6,755,000
17/11/2022	Katibu Mkuu Wizara Ya Afya	259	4,105,500
21/11/2022	Mkurugenzi Mtendaji Zura	260	3,777,750
23/11/2022	Katibu Mkuu W/Watoto	261	3,887,000
25/11/2022	Mkurugenzi Baraza Ka Jiji	262	2,314,000

28/11/2022	Mkurugenzi Mtendaji ZEMA	263	1,385,750
29/11/2022	Mkurugenzi Idara ya M/Mifugo	264	4,324,000
12/1/2022	Mthamini Mkuu wa Serikali	265	2,345,000
12/3/2022	Katibu Mkuu Wizara ya Afya	266	30,479,400
12/5/2022	Quality Building Contractor Ltd Kitogani	267	345,000
12/6/2022	Kamishna Bodi ya Mapato Zanzibar	275	13,978,250
14/12/2022	Wakala Wa Huduma za Matrekta Pemba	276	3,620,100
12/8/2022	Chief Executive Officer Zantel (Nov,2022)	277	34,967,427
12/8/2022	Chief Executive Officer Zantel (Dec,2022)	278	34,967,427
13/12/2022	Mratibu Wakala wa Barabara Pemba	282	3,851,400
14/12/2022	Quality Building Constractor Ltd Kitogani	283	9,188,500
14/12/2022	Rans Company Ltd – Dimani	284	66,907,000
14/12/2022		286	17,249,400
14/12/2022	CRJE (East Africa Ltd) – DSM	287	31,079,400
14/12/2022		288	22,235,700
14/12/2022	Salem Contruction Ltd Dsm	291	7,969,500

1/3/2023	Zmux July- Dec,2022	292	69,000,000
1/4/2023	Viettel Tanzania Plc (April-March,2023)	293	87,000,000
1/4/2023	Htt Infraco Limited (July - Dec,2022)	294	175,917,644
1/4/2023	Chief Executive Officer Zanztel (July June2023)	295	367,500,000
1/10/2023	The Institute Of Public (Ipa)	296	34,610,400
1/10/2023	Chief Executive Officer Zantel (Jan-2023)	297	34,967,427
1/10/2023	Wcfc (Hospital) Limited	299	77,878,500
24/01/2023	Mazrui Building Contractors Ltd	301	17,549,400
24/01/2023	Tume ya Ushindani wa Biashara - Pemba	303	1,610,000
30/01/2023	Mamlaka ya Udhibiti Nishati Zura	304	3,120,750
30/01/2023	Tupo Pamoja Zanzibar	306	3,000,000
30/01/2023	Limbani Wete Hub	307	4,000,000
30/01/2023	Mamlaka ya Huduma ya Nishati (ZURA)	308	2,179,250
2/7/2023	Idara ya Habari Maelezo	310	1,500,000
2/7/2023	Zanzibar Water Authority (ZAWA)	312	5,397,187
2/7/2023	Zanzibar Housing Corporation (ZHC)	313	3,691,800
13/02/2023	Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha	320	8,322,000

13/02/2023	Mkuu Wa Kikosi Cha Valantia	321	7,000,000
21/02/2023	Zanzibar Housing Corporation (ZHC)	347	3,691,800
21/02/2023	Zanzibar Housing Corporation (ZHC)	349	9,237,375
21/02/2023	Bodi ya Mikopo Elimu ya Juu Zanzibar	350	2,413,000
27/02/2023	Commissioner ZRA	351	36,320,400
27/02/2023		352	36,474,300
27/02/2023	Karume Institute of Science and Technology (KIST)	371	6,130,350
14/03/2023	Zanzibar Fisheries and Marine Resources Research	378	2,332,155
27/02/2023	The State University of Zanzibar (SUZA)	389	66,587,400
15/03/2023	Meneja Mkuu Shirika la Umeme Zanzibar	390	4,910,000
24/03/2023	Mkuu wa Kikosi cha Valantia	392	7,000,000
28/03/2023	Karume Institute of Science and Technology (KIST)	393	3,083,270
13/04/2023	Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini “A”	402	2,556,522
14/04/2023	Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Mali Asili	403	17,226,270
14/04/2023	Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Ofisi za Maruhubi	404	6,002,713

18/042023	Mkurugenzi Mkuu Tume ya Ushindani Halali Zanzibar	405	1,610,000
18/042023	Group Six International Ltd (GSI)	420	36,891,400
5/4/2023	Katibu Mkuu Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji	421	5,855,500
5/4/2023	The State University of Zanzibar (SUZA)	425	22,148,775
15/03/2023	Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Jozani	442	8,737,126
18/05/2023	Mkurugenzi Mtendaji Taasisi ya Elimu Zanzibar	447	2,621,500
14/06/2023	Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini “A”	452	2,433,809
15/06/2023	Mkaguzi Mkuu wa Elimu Zanzibar	453	3,567,400
30/06/2023	Htt Infraco Limited (Jan - Juni 2023)	456	176,250,000
	Jumla Ndogo Tsh. (A)		**2,056,008,388**

Taarifa za Mapato kwa Fedha za Kigeni

Tarehe	**Jina**	**Nambari ya Bili**	**Kiasi kilicholipwa**
			(USD)
7/5/2022	Chief Executive Officer Zantel (July)	187	15,000
7/6/2022	Zanzibar Social Security Fund (ZSSF)	190	3,825
18/7/2022	Zanzibar Electricity Corporation (ZECO)	192	1,530

16/8/2022	China Medical Team (CMT)	206	4,600
12/6/2022	Managing Director Zanlink	268	17,920
12/6/2022	Managing Director Zanlink	269	124,200
12/6/2022	Managing Director Zanlink	270	49,680
12/6/2022	Managing Director Zanlink	271	24,840
12/6/2022	Mic Tanzania Limited Plc Tigo	272	320,784.20
12/6/2022	Management & Development For Health (MDH)	273	5,175
1/11/2023	Zanzibar Connecting Company	298	13,378
1/11/2023	Zanzibar Airport Authority (ZAA)	315	15,075
1/11/2023	Zanzibar Airport Authority (ZAA)	322	15,075
1/11/2023	Zanzibar Airport Authority (ZAA)	323	15,075
1/11/2023	Zanzibar Utility Regulatory Authority Zura	330	16,500
1/11/2023	People's Bank of Zanzibar Ltd (PBZ)	336	2,880
1/11/2023	People's Bank of Zanzibar Ltd (PBZ)	337	8,640
20/03/2023	Account Payable Finance Mic Tanzania PLC	340	207
20/03/2023	Zanzibar Social Security Fund	343	15,300
27/02/2023	Chief Executive Officer Zantel (February, 2023)	353	15,000
27/02/2023	Chief Executive Officer Zantel (March,2023)	354	15,000
28/02/2023		357	3,918.75
28/02/202	Zanzibar Ports Corporation (ZPC)	358	4,743.75

3			
28/02/2023		359	4,743.75
28/02/2023		360	4,743.75
28/02/2023	Zanzibar Shipping Corporation	365	3,960
3/2/2023		366	2,070
3/2/2023	Zanzibar State Trading Corporation (ZSTC)	367	2,070
3/2/2023		368	2,070
3/2/2023		369	2,070
3/3/2023	Zanzibar Electricity Corporation	372	1,453.50
3/8/2023	Managing Director Zanlink Limited	376	24,840
3/8/2023	Managing Director Zanlink Limited	377	133,750
15/03/2023		381	6,969
15/03/2023	Zanzibar Road Transport Safety Authority	382	6,969
15/03/2023		383	6,969
15/03/2023	People's Bank Of Zanzibar Ltd (Pbz)	407	6,624
27/04/2023	Zanzibar Utility Regulatory (Zura)	408	4,125
5/4/2023	Chief Executive Officer Zantel (April,2023)	422	15,000
5/4/2023	China Medical Team (Cmt)	423	2,300

5/4/2023	Zanzibar Social Security Fund (Zssf)	424	4,398.75
5/10/2023	Mic Tanzania Limited Plc Tigo	427	728,379.25
	Managing Director Zanlink	429	144,900
5/11/2023	Zanzibar Shipping Corporation (Shipco)	433	1,138.50
5/11/2023	Zanzibar Housing Corporation (Zhc)	434	1,811.25
5/11/2023	Deep Sea Fishing Authority (Dspa)	438	14,250
5/12/2023	Chief Executive Officer Zantel (May,2023)	440	15,000
15/05/2023		444	84,146.63
15/05/2023	Managing Director Zanlink	445	4,140
15/05/2023		446	82,146.64
26/06/2023	Karume Institute Of Science And Technology	455	1,552.50
	Jumla Ndogo (USD)		**2,020,937.22**
	Jumla ndogo (Tsh.) (B) 1 USD = Tsh. 2315.66		**4,679,803,483**
Jumla Kuu (A+B)			**6,735,811,870.87**

Majibu ya uongozi wa ZICTIA

ZICTIA ilipitia na kujiridhisha kuwa hesabu zilizofanyika za mwaka 2022/2023 ziko sawa, kwa kuwa kiasi cha shilingi 4,063,749,680.39/- ni kiwango cha fedha taslimu (cash revenue) ambacho kimekusanywa. Hivyo tofauti ya kiasi cha shilingi 2,672,032,699/- ni deni ambalo lilikuwa

halijakusanywa. Hivyo, hoja inaonesha kuwa fedha zilijumuuishwa zote ambazo ni “cash” na deni na kupelekea jumla ya shilingi 6,735,782,379.39/-. Aidha, ukaguzi huu ni “cash based” ambao haujumuishi madeni.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC baada ya kuchunguza hoja hii imebaini yafuatayo:

1. Tofauti liliyojitokeza ilisababishwa na kwamba wakati wa ukaguzi Mamlaka ilikuwa ikitumia mfumo wa ‘cash basis’
2. Tofauti ilionekana baada ya Mkaguzi kuangalia ‘cash book’ akilinganisha na taarifa za benki.
3. Kukosekana kwa vielelezo wakati wa ukaguzi hususan ‘invoice’ za shilingi milioni 861 zilizojumuisha madeni tofauti. Hata hivyo, wakati Kamati inatekeleza majukumu yake ‘invoice’ hizo zimeonekana.

Kwa msingi huo, Kamati iliridhika na majibu yaliyotolewa na kuiondoa hoja hii.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Kamati ya PAC inautaka uongozi wa Mamlaka kuhifadhi vielelezo vya matumizi inayoyafanya ili viweze kupatikana wakati wa ukaguzi.
2. Uongozi wa Mamlaka uhakikishe unafanya usuluhishi wa kibenki kwa taarifa zake za fedha kwa kila mwezi ili kuepusha changamoto ya kutofautiana kwa fedha zake.

Hoja nambari 6.1.2.3: Uwepo wa deni la shilingi 2,605,582,800 ambalo halijalipwa

Ukaguzi ulipitia Taarifa za Fedha za Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA pamoja na Ankara zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi na kubaini uwepo wa deni la shilingi 2,605,582,800 kwa taasisi za Serikali ambalo halijalipwa ,deni ambalo mbali na jitihada zilizochukuliwa na Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA kwenda kwa wateja waliowapatia huduma halijalipwa.

Kutokulipwa kwa deni hilo kunaweza kuathiri malengo ya ukusanyaji wa Mapato ya Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA .

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA kuhakikisha wanachukua jitihada za makusudi kwa taasisi hizo juu ya ulipaji wa madeni kwa wakati.

Mchanganuo wa deni ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 83: Orodha ya Deni kwa mujibu wa Ankara

Tarehe	Jina	Nambari ya Bili	Deni (Tsh.)
29/7/2022	M/Mkuu Mamlaka ya Maji (Marekebisho Mradi)	197	37,077,500
8/3/2022	Kamishna Idara ya Michezo (Viwanja vya Mpira)	199	20,244,750
17/8/2022	Katibu Mkuu Wizara ya Biashara na Viwanda (Kinazini)	207	4,290,075
31/8/2022	Mamlaka Ya Viwanja Vya Ndege (Terminal III)	209	17,710,000
9/2/2022	Katibu Mtendaji Maji Nishati (Ofisi Ya Crc)	210	3,921,500
20/9/2022	M/Mkuu Mamlaka Ya Viwanja Vya Ndege (Terminal III)	220	17,710,000
26/9/2022	Katibu Mkuu Ofisi Ya Rais (Uwekaji Wa Lan)	224	13,386,000
30/9/2022	Mkurugenzi Matrekta (Mbweni)	226	3,850,100
30/9/2022	M/Mtendaji Idara Ya Umwagiliaji Maji (Mbweni)	228	5,336,000
25/10/2022	Mkurugenzi Idara Ya M/Ualimu	243	1,138,500
25/11/2022	Mkurugenzi Baraza La Jiji	262	2,251,500
25/11/2022	Kampuni Ya Bench Mark Dsm	289	4,807,000
1/2/2023	Ofisi Ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar	290	5,669,500
23/01/2023	Taasisi Ya Viwango Zanzibar	302	1,610,000
23/01/2023	Ofisi Ya Mkurugenzi Wa Mashtaka	309	6,808,000

2/7/2023	Idara Ya Habari Maelezo	310	3,939,500
20/02/2023	Mic Tanzania Limited Plc Tigo	339	6,621,700
3/3/2023	Katibu Mkuu Wizara Ya Afya Zanzibar	374	3,542,000
16,03/2023	Meneja Mkuu Shirika La Umeme Zanzibar	391	10,137,250
29/03/2023	Kamishna Mkuu Uhamiaji Tanzania (Miaka Miwili)	396	99,360,000
27/04/2023	Afisa Mdhamini Ofisi Ya Makamo Wa Pili Pemba	411	11,321,750
27/04/2023	Mkaguzi Mkuu Wa Elimu Zanzibar	426	4,174,500
5/12/2023	Zmux --January - June 2,023,	441	69,000,000
6/7/2023	Meneja Mkuu Shirika La Umeme Zanzibar	451	63,145,000
15/06/2023	Mkaguzi Mkuu Wa Elimu Zanzibar	453	4,174,500
22/06/2023	Mratib Mamlaka Ya Mafunzo Ya Amali Pemba	454	4,370,000
	Jumla (TZS)		**425,596,625**
Tarehe	**Jina**	**Nambari ya Bili**	**Deni (USD)**
18/7/2022	Zanzibar Utility Regulatory (ZURA)	194	4,743.75
10/11/2022	Com.Net Compant Ltd	237	14,283.00
10/11/2022	Com.Net Compant Ltd	238	14,283.00
17/10/2022	Zanzibar Fisheries And Marine	239	1,207.50

12/6/2022	Mic Tanzania Limited Plc Tigo	272	320,784.20
12/6/2022	Zanzibar Water Authority (ZAWA)	312	5,175.00
12/6/2022	Director G. Z'bar Road Transport (ZANROAD)	314	6,969.00
9/2/2023	Z'bar Investment Promotion Authority (ZIPA)	316	4,398.00
9/2/2023	Zanzibar Airport Authority (ZAA)	323	17,336.00
13/02/2023	Tanzania Telecommunication Corporation	324	76,848.00
13/02/2023	Tanzania Telecommunication Corporation	325	97,881.00
13/02/2023	Tanzania Telecommunication Corporation	326	15,369.00
13/02/2023	Zanzibar Water Authority (ZAWA)	331	5,175.00
13/02/2023	Zanzibar Water Authority (ZAWA)	332	5,175.00
13/02/2023	Zanzibar Water Authority (ZAWA)	333	5,175.00
20/03/2023	Account Payable Finance Mic Tanzania Plc	340	207
21/02/2023	Zanzibar Investiment Promotion Authority (ZIPA)	344	4,398.75
21/02/2023	Zanzibar Investiment Promotion Authority (ZIPA)	345	4,398.75
21/02/2023	Zanzibar Investiment Promotion Authority (ZIPA)	346	4,398.75
21/02/2023	Zanzibar Housing Corporation (ZHC)	348	1,811.25
21/02/2023	Zanzibar Housing Corporation (ZHC)	349	1,811.25

27/02/2023	Alfa Care Group Limited	355	1,139.54
27/02/2023	Alfa Care Group Limited	356	1,139.54
27/02/2023	Zanzibar Electricity Corporation (ZECO)	373	1,759.50
15/03/2023	Zanzibar Broadcasting Corporation (ZBC)	384	9,660.00
15/03/2023	Zanzibar Broadcasting Corporation (ZBC)	385	9,660.00
15/03/2023	Zanzibar Broadcasting Corporation (ZBC)	386	9,660.00
28/03/2023	Zanzibar Broadcasting Corporation (ZBC)	394	9,660.00
28/03/2023	Zanzibar Water Authority (ZAWA)	395	5,175.00
29/03/2023	Zanzibar Electricity Corporation (ZECO)	397	1,759.00
4/11/2023	Zanzibar Investiment Promotion Authority (ZIPA)	400	2,673.75
27/04/2023	Zanzibar Bureau Of Standards (ZBS)	409	1,656.00
27/04/2023	Zanzibar Revenue Authority (ZRA)	410	18,630.00
27/04/2023	Zanzibar Airport Authority (ZAA)	412	17,336.25
27/04/2023	Zanzibar Airport Authority (ZAA)	413	17,336.25
27/04/2023	Zanzibar State Trading Corporation (ZSTC)	414	2,070.00
27/04/2023	Zanzibar Investiment Promotion Authority (ZIPA)	415	3,536.25
27/04/2023	Zanzibar Investiment Promotion Authority (ZIPA)	416	3,536.25

27/04/2023	Zanzibar Investiment Promotion Authority (ZIPA)	417	3,536.25
27/04/2023	Zanzibar Investiment Promotion Authority (ZIPA)	418	4,398.75
27/04/2023	Zanzibar Road Transport Safety Authority	419	6,969.00
27/04/2023	Zanzibar Housing Corporation (ZHC)	434	1,811.25
5/11/2023	Zanzibar Ports Corporation (ZPC)	439	4,743.75
5/12/2023	Chief Executive Officer Zantel (May,2023)	440	15,000.00
15/05/2023	Managing Director Zanlink	444	84,146.63
15/05/2023	Managing Director Zanlink	445	4,140.00
15/05/2023	Managing Director Zanlink	446	82,146.64
31/05/2023	The Public Helth Laboratory (PHL)	449	3,750.00
25/05/2023	Mandlethu	450	1,000.00
26/06/2023	Karume Institute of Science andTechnology	455	1,552.50
Jumla (USD)			**941,410.30**

Majibu ya Uongozi wa ZICTIA

Ili kuhakikisha madeni hayo yanalipwa kwa wakati, Taasisi iliendelea kuchukua hatua za kuwasiliana na wadaiwa kwa kutumia njia mbalimbali za mawasiliano kama vile kuwatumia barua, barua pepe au kuonana nao ana kwa ana katika ofisi zao. Aidha, bado kuna changamoto kubwa ya ulipaji wa madeni kutoka kwa wadaiwa, ambapo ZICTIA ilifanya mawasiliano na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango juu ya kuyakusanya madeni ya ZICTIA kabla ya kugaiwa (OC) kwa taasisi hizo. Hata hivyo, muelekeo wa Shirika kwa sasa ni kuwa na mfumo wa usimamizi wa wateja (billing and customer management system) utakaosaidia katika ukusanyaji wa mapato yanayotokana na huduma zinazotolewa.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa ni kweli ZICTIA inakabiliwa na madeni inayodai kwa Mashirika na Taasisi tofauti za Serikali kufuatia utoaji wa huduma zake kwa mujibu wa Sheria. **Hata hivyo, Kamati yetu ilitaka** kujua juhudi ambazo Mamlaka imezichukua na kueleza wanakumbusha wahusika kuhusiana na kukamilisha malipo yao lakini bado madeni hayo hayajalipwa yote hususan kwa Taasisi zinazopokea ruzuku Serikalini. Kwa msingi huo, hoja hii inaendelea kubakia kwa hatua za ufuatiliaji zaidi.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inaitaka Mamlaka ihakikishe inafuatilia kwa karibu madeni hayo ili yaweze kulipwa kwa haraka.

Hoja nambari 6.1.2.4: Kushindwa kukusanya jumla ya shilingi 44,007,687 kutokana na usimamizi usioridhisha wa Mkataba baina ya Wakala na TTCL

Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA waliingia katika makubaliano ya mkataba na Tanzania Telecommunications Corporation Limited (TTCL) ambapo utekelezaji wake ulianza rasmi mnamo tarehe 1 Septemba, 2022 kwa ajili ya kupatiwa huduma ya Fiber (Zanzibar Submarine Fiber Network) kwa ada ya USD 432,000 kwa mwaka kwa huduma za kutoka Dar es Salaam kuja Zanzibar, na jumla ya USD 129,257.4 kwa huduma za kutoka Tanga kwenda Pemba na kufanya jumla ya malipo yote kuwa ni USD 561,257.

Ukaguzi ulibaini Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA waliwasilisha Ankara yenye thamani ya USD 190,098 ambayo ni sawa na shilingi 440,076,870 kwa kutumia kiwango kilichotolewa na BoT tarehe 30 Juni, 2023 cha shilingi 2,315 kwa TTCL kwa ajili ya kuweza kufanyiwa malipo pamoja na uwasilishwaji wa bili hizo kwa TTCL. Aidha, hakukua na malipo yoyote yaliofanikiwa kufanywa au kupokelewa na Wakala hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 ambapo Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA hawakuweza kuchukua hatua yoyote kwa TTCL pamoja na ucheleweshwaji wa malipo hayo, ambapo kwa mujibu wa sehemu ya 13.3 ya mkataba inaeleza kwamba endapo kutakua na ucheleweshwaji wa malipo kwa zaidi ya siku 30 kuanzia tarehe ya kuwasilishwa kwa bili, Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA atalazimika kuhakikisha anawasilisha taarifa ya ukumbusho wa deni kwa awamu mbili kwa TTCL kabla ya kujumuisha asilimia 10 ya deni ikiwa ni fidia ya ucheleweshwaji wa malipo.

Kushindwa kusimamia vyema vifungu vya mkataba kunaweza kupeleka upotevu wa mapato, aidha kushindwa kukumbushia deni kwa TTCL

kunapelekea Wakala kushindwa kudai nyongeza ya asilimia 10 inayotokana na kucheleweshwa kwa malipo.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Wakala kuhakikisha unasimamia vyema matakwa ya mkataba kwa manufaa ya Wakala na Serikali kwa ujumla. Mchanganuo wa deni ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Namba	**Nambari Ankara**	Kiasi (USD)	Kiasi kilichoshindwa kudaiwa (Asilimia kumi ya bili katika USD)	Kiasi kilichoshindwa kudaiwa (Asilimia kumi katika Tsh iliobadilishwa kupitia Rate ya BoT 30/06/2022 1USD=TZS **2,315)**	Miezi iliotolewa Ankara
	324	76,848	7,684.8	17,790,312	Julai – Septemba 2022
	325	97,881	9,788.1	22,659,451.5	Oktoba – Disemba 2022

	326	15,369	1,536.9	3,557,923.5	Malipo ya mwaka ya huduma ya O & M
Jumla		**190,098**	**19,009.8**	**44,007,687**	

Majibu ya Uongozi wa ZICTIA

Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar imepokea ushauri huo na inatambua uwepo wa ongezeko la fedha za adhabu (penalt)kutokana na ucheleweshaji wa malipo kwa TTCL kama ilivyo katiaka mkataba. Aidha, ZICTIA ilichukua hatua zakufatilia deni hilo kwa kushirikisha Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar pamoja na Wizara ya habari na Teknolojia ya Habari Tanzania. Hata hivyo, makubaliano ya vikao tofauti yaliridhia kuzingatia deni mama ambalo ni la muda mrefu na kuendelea kujadili adhabu hio ikiwa malipo ya awali yatakamilika. Aidha kutozingatiwa kwa deni hilo kulitokana kuwa ZICTIA inapokea baadhi ya huduma kutoka kwa TTCL bila malipo yoyote ikiwemo uwekaji wa vifaa katika ofisi za TTCL Kijangwani na huduma ya mkonga kutoka TTCL house hadi Tanesco, jambo ambalo linaonesha mashirikiano baina ya pande mbili. Hata hivyo, ZICTIA itasaini mkataba wa kulisamehe deni hilo punde baada ya TTCL kukamilisha Deni mama wanalodaiwa.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa ni kweli kuna changamoto inayoikabili Mamlaka ya kushindwa kukusanya jumla ya shilingi 44,007,687 kutokana na usimamizi usioridhisha wa Mkataba baina ya Wakala na TTCL. Suala hili limekuwa gumu kiutekelezaji kwani TTCL inatoa huduma katika Taasisi nyeti za Serikali kitu ambacho huwawia ugumu ZICTIA kuchukua hatua stahiki. Kwa mnasaba huo, ZICTIA inaendelea kutumia njia za kidiplomasia katika kulitafutia ufumbuzi changamoto hiyo. Kwa mnasaba huo, hoja hii inaendelea kubakia kwa hatua za utekelezaji zaidi.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Mbali njia ZICTIA kuendelea kutumia njia za kidiplomasia kwa kukaa na kuzungumza na TTCL mara kwa mara lakini iwe na utaratibu wa kudai deni lake kwa njia ya maandishi ili kuwepo kielelezo cha hatua inazozichukua.

Hoja nambari 6.1.2.5: Kutokulipwa kwa kiasi cha shilingi 859,233,085 kutoka kwa Mteja TTCL

Kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba baina ya Wakala wa Miundmbinu ya TEHAMA na Tanzania Telecommunications Corporation Limited (TTCL) ambapo utekelezaji wake ulianza rasmi mnamo tarehe 1 Septemba, 2022 kwa ajili ya kupatiwa huduma ya Faiba (Zanzibar Submarine Fiber Network). Mkataba uliainisha kuwa ada ya mwaka kwa huduma zinazotolewa na Wakala kwa TTCL ni USD 561,257 ambapo USD 432,000 ni kwa ajili ya huduma kutoka Dar es Salaam kuja Zanzibar na Dola za Marekani 129,257.4 kwa huduma kutoka Tanga kwenda Pemba.

Ukaguzi ulibaini kwamba hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022 Wakala waliwasilisha bili zenye thamani ya USD 190,098 ambayo ni sawa na shilingi 440,076,870 kwa kutumia kiwango kiliotolewa na BoT tarehe 30 Juni 2022 ya shilingi 2,315, ambayo ilikuwa ni kuanzia Julai 2022 hadi Disemba, 2022 kwa huduma za Faiba na kwa M/S O & M waliwasilisha bili ya mwaka na kushindwa kuwasilisha bili kwa miezi iliobakia yenye thamani ya USD 371,159 ambayo ni sawa na shilingi 859,233,085

Kushindwa kulipwa kwa bili kwa huduma wanazowapatia TTCL kunapelekea Wakala kushindwa kukusanya mapato kupitia huduma iliyotolewa kwani kiasi kingeleiweza kutumika kwa shughuli za uendeshaji wa shughuli za Maendeleo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kuhakikisha kwamba unafatilia fedha zake kutokana na huduma walizowapatia TTCL. Mchanganuo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 85: Kiasi kilichoshindwa kudaiwa (Unbilled Amount)

Kiasi kilichostahiki kudaiwa kwa mujibu wa Mkataba		**Kiasi kilichodaiwa kwa mujibu wa makubaliano ya Mkataba**		**Kiasi kilichoshindwa kudaiwa kwa mujibu wa Mkataba**	
Dola ya Marekani	Shilingi ya Tanzania	Dola ya Marekani	Shilingi ya Tanzania	Dola ya Marekani	Shilingi ya Tanzania

561,257	1,299,309,955	190,098	440,076,870	371,159	859,233,085

Maijbu ya Uongozi wa ZICTIA

Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar imeendelea na juhudi katika kuhakikisha inakusanya mapato kutoka kwa kampuni zote zinazopata huduma ikiwemo TTCL. Aidha, ZICTIA inatambua uwepo wa changamoto ya ucheleweshaji wa malipo ya huduma zinazotolewa kwa TTCL ambapo hatua zilichukuliwa kuhakikisha madeni hayo yanalipwa. Taasisi ilitumia njia mbalimbali za kulidai Shirika hilo, kama vile mawasiliano ya barua, barua pepe pamoja na watendaji kufikaka katika Ofisi za TTCL. Zaidi ya hayo, ZICTIA iliwaandikia barua Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais Zanzibar na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Tanzania na kuelezea juu ya changamoto hiyo na kuahidi kulifanyia kazi suala hilo. Aidha malipo ya deni hilo yameanza kulipwa na hadi sasa tayari ZICTIA imepokea shilingi 300,000,000/-.

Uchunguzi na Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa unchunguzi na Maagizo ya hoja hii unafanana na hoja nambari.

Hoja nambari 6.1.2.6: Malipo yenye vielelezo pungufu shilingi 89,032,790

Kifungu nambari 34(1) cha Sheria, Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinamtaka Afisa Mhasibu kuweka kumbukumbu zinazohusiana na masuala ya fedha za Idara, taasisi za biashara au taasisi za kikatiba kulingana na masharti na viwango na kanuni ya 55(1) pamoja na kanuni ya 57(2) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inataka malipo yote yanayofanywa na taasisi ya Serikali kuhakikisha yanaambatanishwa na marejesho yaliokamilika.

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala ilifanya matumizi ya jumla ya shilingi 89,032,790 kwa matumizi mbalimbali bila ya kuzingatia upatikanaji wa marejesho ya kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Kukosekana kwa marejesho ya malipo yaliotajwa hapo juu kumepelekea ukaguzi kushindwa kuthibitisha uhalali wa malipo yaliofanywa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kuhakikisha kwamba malipo yote yanayofanywa yanawekewa viambatanisho halali vya matumizi yaliyofanyika. Mchanganuo wa malipo hayo unaonekana katika Jedwali lifuatalo:-

Jadweli Nambari 86: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu

Nambari ya Hati	Kiasi Kilicholipwa (shs)	Aliyelipwa	Maelezo
2/7 ya 8-Julai-2022	3,660,000	Wakala wa Mkonga	Malipo kwa ajili ya safari ya kikazi Tanga kwenda kufanya marekebisho ya Mkongo njia ya Tanga Pemba
3/7 ya 8-Julai-2022	9,205,396	Wakala wa Mkonga	Malipo baada ya saa za kazi kwa wafanyakazi wa Wakala
13/10 ya 13-Okt-2022	900,000	Wakala wa Mkonga	Malipo ya fedha kwa ajili ya kupatiwa posho walinzi watatu wanaofanya kazi ya Ulinzi
21/10 ya 17-Okt-2022	630,000	Wakala wa Mkonga	Malipo ya fedha kwa ajili ya safari ya Dar es salaam kikazi kwa mk Ufundi ndg Frank N Kagoma
22/10 ya 17-Okt-2022	790,000	Wakala wa Mkonga	Malipo ya fedha kwa ajili ya safari ya Dar es salaam kikazi kwa mtendaji Mkuu

			Ndg Shukuru A. Suleiman
24/10 ya 18-Okt-2022	150,000	Wakala wa Mkonga	Malipo ya kukodi gari na wachukuzi wa kubeba nguzo
26/10 ya 18-Okt-2022	2,400,000	Stone Town Trader Ltd	Malipo ya fedha kwa ajili ya marejesho ya gharama za wino zilizotumika katika kazi za Wakala wa miundombinu ya Tehama Zanzibar
31/10 ya 31-Okt-2022	560,000	Wakala wa Mkonga	Malipo ya fedha kwa ajili ya marejesho ya gharama ya upakaji rangi kwenye jengo la Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wakala wa miundombinu ya Tehama Zanzibar
12/11 ya 25-Nov-2022	680,000	Saidi Hadadi Makame	Malipo ya fedha kwa ajili ya kukodi gari na wachukuzi wa kubeba nguzo

15/11 ya 30-Nov-2022	250,000	Wakala wa Mkonga Zanzibar	Malipo ya fedha kwa ajili ya marejesho ya fedha zilizotumika kwa ajili ya ununuzi wa betri ya gari SMZ 501 B
6/12 ya 6-Dise-2022	270,000	Wakala wa Mkonga Zanzibar	Marejesho ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa wino kwa matumizi ya Ofisi ya Mhasibu
4/1 ya 5-Jan-2023	2,950,000	Saidi Hadadi Makame	Malipo ya fedha kwa ajili ya uchukuzi na usambazaji wa nguzo 254 pamoja na uunganishaji mkonga wa mawasiliano katika hospitali za wilaya sita (6) na mkoa moja (1) kwa upande wa Unguja
5/1 ya 6-Jan-2023	570,000	Miriam Stanley Mwaitumile	Malipo ya fedha kwa ajili ya malipo ya upambaji wa banda katika Tamasha la Tisa la Biashara (9 Zanzibar Shoopping Festival)
9/1 ya 6-Jan-	630,000	Wakala wa	Malipo ya fedha kwa ajili

2023		Mkonga Zanzibar	ya safari ya kikazi kwa nd Muhamed Juma Muhamed
13/1 ya 13-Jan-2023	1,065,000	Wakala wa Mkonga Zanzibar	Malipo ya fedha kwa ajili ya safari ya kikazi Dar es salaam kwa Mkurugenzi Mtendaji wakala wa miundombinu ya TEHAMA Zanzibar
22/1 ya 23-Jan-2023	170,000	Said Hadadi Makame	Malipo ya fedha kwa ajili ya kukodi gari na wachukuzi wa kubeba nguzo
3/2 ya 3-Feb-2023	600,000	Wakala wa Mkonga Zanzibar	Malipo ya fedha kwa ajili ya posho la walinzi wawili
6(B)/2 ya 10-Feb-2023	1,931,950	Island Refregeration & Electricity	Bakaa la malipo ya Ununuzi wa vifaa vya matengenezo ya vipoza hewa

12/2 ya 14-Feb-2023	300,000	Wakala wa Mkonga Zanzibar	Malipo ya fedha kwa ajili ya kukodi gari na wachukuzi kubeba nguzo
13/2 ya 14-Feb-2023	120,000	Wakala wa Mkonga Zanzibar	Malipo ya fedha kwa ajili ya kukodi gari na wachukuzi kubeba nguzo
14/2 ya 14-Feb-2023	230,000	Haroub & sons decoration	Marejesho ya fedha zilizotumika kwa ajili ya matengenezo madogo ya ofisi
14/2 ya 15-Feb-2023	5,439,448	Mwinyi Building Contractors Ltd	Bakaa ya malipo ya awamu ya kwanza (50%) ya kazi ya upakaji wa rangi katika majengo ya Ofisi za ZICTIA
24/2 ya 24-Feb-2023	1,108,270	Azam Marine Ltd	Malipo ya fedha kwa ajili ya kukodi gari kubeba nguzo
1(A)/4 ya 31-Machi-2023	588,235	Azam Marine	Malipo ya kukodi gari kwa ajili ya kubeba mzigo Unguja kwenda

			Pemba
10/5 ya 9-Mei-2023	1,200,000	Wakala wa Mkonga Zanzibar	Malipo ya fedha kwa ajili ya posho maalum kwa walinzi mwezi Machi na April
11/5 ya 9-Mei-2023	2,550,000	Wakala wa Mkonga Zanzibar	Malipo ya fedha kwa ajili ya posho la kujikimu na nauli Pemba
19/5 ya 22-Mei-2023	1,098,000	Wakala wa Mkonga Zanzibar	Malipo ya fedha kwa ajili ya posho la kujikimu na nauli ya kwenda Dar es salaam kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA
20(A)/5 ya 26-Mei-2023	1,950,000	Chukwani Catering Supplier	Malipo ya fedha kwa ajili ya kugharamia chakula kitakachotumika katika mafunzo kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ya Mswada wa Sheria ya kuanzishwa kwa shirika la mawasiliano

			Zanzibar
2/6 ya 7-Juni-2023	7,698,429	Double Plus Company Ltd	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia (stationary)
3/6 ya 7-Juni-2023	3,170,185	Rahisi Auto Spare	Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya matengenezo ya majenereta (betri)
11/6 ya 13-Juni-2023	9,367,608	Kheri Mohd Mhema	Malipo kwa ajili ya malipo mbalimbali yanayohusiana na uunganishaji wa Mkonga
16/6 ya 20-Juni-2023	100,000	Saidi Hadadi Khamis	Malipo ya fedha kwa ajili ubebaji wa vifaa vya mkonga katika gari la Azam
21/6 ya 21-Juni-2023	7,413,726	Kheri Mohd Mhema	Malipo kwa ajili ya malipo mbalimbali yanayohusiana na uunganishaji wa Mkonga
19-Oktoba-2022 (Dola)	6,252,282	AFRINIC	Malipo ya fedha kwa ajili ya kulipia IP Block

			mpya tulizoziomba kutoka AFRINIC
07-Machi-2023 (Dola)	694,698	AFRINIC	Malipo ya fedha kwa ajili ya malipo ya Ada ya mwaka kwa AFRINIC
1/7 ya 30-Juni-2022 (Pemba)	9,514,563	Iddi Mohammed Salim	Malipo ya fedha kwa huduma ya kutengeneza vyumba vya aluminium katika Ofisi za ZICTIA iliopo jengo la ZSSF Tibirinzi Chake Chake Pemba
1/8 ya 11-Agos-2022 (Pemba)	640,000	Wakala wa Mkonga Pemba ChakeChake	Malipo ya fedha za nauli na posho la safari kikazi kwenda Unguja mratibu Wakala wa Mkonga Pemba, ndg. Abbass Fadhil Abbass
3/3 ya 23-Feb-2023 (Pemba)	1,005,000	Wakala wa Mkonga Pemba	Malipo ya fedha kwa ajili ya posho na nauli kwa mratibu wa Wakala wa Mkonga Pemba kwenda Unguja kikzi kushiriki kikao cha kuwasilisha makadirio ya

			bajeti ya mwaka 2023/2024
2/5 ya 15-Mach-2023 (Pemba)	1,180,000	Wakala wa Mkonga Pemba	Malipo ya fedha kwa ajili ya posho na nauli kwa Mratibu wa Wakala wa Mkonga Pemba kwenda Unguja kikazi kushiriki kikao cha kujadili na kupitia bajeti ya Shirika la Mawasiliano Zanzibar
Jumla	**89,032,790**		

Majibu ya Uongozi wa ZICTIA

ZICTIA iliwasilisha vielelezo husika, ingawa baadhi ya vielelezo viliendelea kufuatiliwa. Hata hivyo vielelezo hivyo vipo na tayari vimepatikana.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati imebaini mambo yafuatayo:

1. ZICTIA inachelewa kupata vielelezo vyake kutokana na kwamba huwa inafanyakazi na Wateja wake ambao wapo nje ya nchi. Hata hivyo, umakini unahitaji hasa ukizingatia malipo siku hizi yanafanyika kwa mifumo.
2. Kamati ya PAC imegundua kuwa licha ya kuwepo sababu ya baadhi ya Wateja wapo nje ya nchi. Hata hivyo, Kamati imelibaini suala la Malipo yenye vielelezo pungufu shilingi 89,032,790 katika RIpoti ya Mkaguzi wa ndani.
3. Saini za 'Head of Account' zimeonekana kuwa tofauti katka vocha namba 2/7 na 26/10.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inautaka uongozi wa ZICTIA kuhakikisha mara baada ya malipo kufanyika, vielelezo navyo vinapatikana ili kuweza kutumika wakati vitakapohitajika.

Hoja nambari 6.1.2.7: Malipo yaliofanywa kwa njia ya Fedha Taslim (Cash Payment) shilingi 39,925,000

Kanuni Namba 58 ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inataka matumizi yote kufanyika kwa mfumo wa Kielektroniki.

Ukaguzi ulibaini kwamba Wakala ilifanya matumizi ya jumla ya shilingi 39,925,000 kwa njia ya fedha taslim (Cash) bila ya kuzingatia mfumo wa ulipaji wa Kielekroniki. Kufanya malipo kwa njia ya fedha taslimu kunaweza kupelekea kujitokeza kwa upotevu wa fedha za umma kunakotokana na kushindwa kuzuia tozo za kodi mbalimbali na kuisababishia Serikali hasara.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kuhakikisha kwamba hakuna malipo yanayofanywa kwa njia ya fedha taslimu. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama unavyoonekana katika Jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 87: Malipo yaliofanywa kwa fedha Taslim

Hati namba	**Aliyelipwa**	**Kiasi kilicholipwa (Tsh)**	**Maelezo**
1/7 ya 8/7/2022	Wakala wa Mkonga	200,000	Malipo kwa ajili ya ununuzi wa chakula.
2/7 ya 8/7/2022		3,660,000	
20/10 ya 17/10/2022		3,000,000	

5/12 ya 5/12/2022		1,590,000	
5/12 ya 5/12/2022		1,590,000	
8/4 ya 13/12/2022		360,000	Malipo ya kwa ajili posho
12/4 ya 13/4/2023 13/4 ya 14/4/2023		1,700,000 3,750,000	mbalimbali.
20B/4 ya 26/5/2023		18,975,000	
20/6 ya 26/6/2023		4,600,000	
22/6 ya 30/6/2023		500,000	
		39,925,000	

Majibu ya Uongozi wa ZICTIA

ZICTIA inatambua na kuheshimu miongozo, sheria na kanuni za matumizi ya fedha za umma. Aidha wakati wa utekelezaji wa shughuli mbalimbali za taasisi kulijitokeza hali ya dharura iliyopelekea kufanyika kwa matumizi ya fedha taslimu ikiwemo gharama za mafunzo ya wajumbe kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar juu ya mswada wa sheria ya kuanzishwa kwa Shirika la Mawasiliano Zanzibar, ambapo kabla ya malipo hayo kulikuwa na

majadiliano kati ya Wizara ya Miundombinu, Mawasilano na Uchukuzi, ZICTIA na Baraza la Wawakilishi. Aidha malipo hayo yote yaliyolipwa kwa “cash”, vielelezo vyake vimewasilishwa.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kulifuatilia suala hili, Kamati imebaini kwamba kuna changamoto ya ZICTIA kufanya malipo yaliofanywa kwa njia ya Fedha Taslim (Cash Payment) shilingi 39,925,000 jamba ambalo ZICTIA inatakiwa kuchukua juhudi za makusudi kurekebisha suala hilo. Hoja hii inaendelea kubakia.

Maagizo ya Kamati ya PAC

ZICTIA ihakikishe inafanya malipo yake kwa kutumia mfumo wa kielektroniki.

Hoja nambari 6.1.2.8: Ongezeko la matumizi kwa baadhi ya vifungu vya bajeti shilingi 932,427,527

Kanuni ya 20(1) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaelezea kwamba uhaulishaji wa fedha za vifungu usizidi asilimia kumi na tano (15%) ya kiasi chote cha programu husika.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya taarifa za fedha za mwisho wa mwaka kwa kulinganisha bajeti na Matumizi halisi yailioidhinishwa na kubaini uwepo wa ziada ya matumizi ya shilingi 932,427,527 kwa matumizi yaliyofanyika bila ya kuzingatia kiasi kilichoidhinishwa katika bajeti.

Kufanya matumizi ya ziada kwa baadhi ya programu kunaweza kuathiri shughuli nyenginezo zilizotengewa bajeti na hatimae kupunguza ufanisi wa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kuhakikisha matumizi yote yanafanyakia kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa na endapo italazimika kufanya uhaulishaji ni vyema kufuatwa taratibu zilizoainishwa katika sheria nambari 12 ya usimamizi wa fedha za umma ya 2016 na kanuni zake. Hali halisi ni kama inavyonekana katika jadweli hapo chini: -

Jadweli Nambari 88: Mlinganisho wa matumizi na bajeti iliyoidhinishwa

Kifungu	Maelezo	Makadirio	Matumizi Halisi	Ongezeko la matumizi	Asilimia ya Ongezeko

		(Tshs)	(Tshs)	(Tshs)	(%)
6112246	Purchase of Fiber Equipments	230,480,500	370,997,736	140,517,236	61
6112227	Purchase of Moving camera	6,000,000	7,205,882	1,205,882	20
2209003	Tuition Fees	6,200,000	18,976,040	12,776,040	206
2206025	Burial Activities	2,100,000	2,900,000	800,000	38
2206001	Stationery Supplies	14,000,000	16,374,429	2,374,429	17
2206001	Sitting Allowance	79,927,500	97,743,400	17,815,900	22
2204001	Petrol	77,795,000	158,000,000	80,205,000	103
2202003	Gift	500,000	4,600,000	4,100,000	820
2202001	Security services	20,000,000	115,500,000	95,500,000	478
2201012	Fiber Network Maintainance	29,000,000	135,863,294	106,863,294	368
2112616	Special Allowance	1,500,000	17,600,000	16,100,000	1073
2112610	Over time	103,000,000	120,590,704	17,590,704	17

2112606	Transport Allowance	12,600,000	17,688,570	3,888,300	40
2821022	Tax Refund	-	432,690,742	432,690,742	Haimo katika bajeti
Jumla		**583,103,000**	**1,516,730,797**	**932,427,527**	

Majibu ya Uongozi wa ZICTIA

Ingawa kwa ujumla wake ZICTIA haijakiuka kiwango cha bajeti kilichopangwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ongezeko hilo la matumizi, kwa sehemu kubwa lilitokana na miradi mipya kutoka kwa wateja wa ZICTIA na Ujenzi wa barabara, ambayo iliibuka bila kutarajia. Hivyo kupelekea ongezeko la gharama za mahitaji ya vifaa, malipo ya ziada, usafirishaji wa vifaa pamoja na gharama tofauti zilizotumika katika matengenezo ya miundombinu ya miradi inayotekelezwa nchini hususan ujenzi wa barabara ambapo kwa kiasi kikubwa iliathiri miundombinu ya mawasiliano.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, Kamati ya PAC ilitaka kujua kama ongezeko la fedha zilizotumika zimefanyiwa uhaulishaji (reallocation) na Bodi ya ZICTIA na kuelezwa kwamba ziliidhinishwa na Bodi yao lakini hakukuwa na kikao ambacho Kamati imeoneshwa kielelezo chake na kutia shaka juu ya ukweli wa jibu hilo.

Kwa msingi huo, hoja hii imebakia kwa hatua za utekelezaji zaidi.

Maagizo ya Kamati ya PAC

1. Uongozi wa ZICTIA uhakikishe unapeleka maombi yake ya mabadiliko ya matumizi ya fedha zilizoongezeka kwa Bodi yake ili ziweze kutumika kwa misingi ya Sheria.
2. Uongozi wa ZICTIA uhakikishe unahifadhi vizuri kumbukumbu zake ili ziweze kupatikana zitakapohitajika.

WAKALA WA KARAKANA KUU YA MAGARI YA ZANZIBAR

Hoja nambari 6.1.8.1: Dosari katika utayarishaji wa Hesabu za Mwisho wa mwaka

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi umepitia taarifa za fedha zilizotayarishwa na kuwakilishwa na Wakala na kubaini uwepo wa dosari mbali mbali ambazo zimepelekea kutokuoneshwa sura sahihi na halisi ya hesabu zilizowasilishwa. Miongoni mwa dosari hizo ni kama zifuatazo:

Kutokubainishwa kwa mishahara yenye jumla ya shilingi 1,030,189,053 katika hesabu za mwisho wa mwaka ambapo ni kwenda kinyume na muongozo wa ufungaji wa hesabu kwa Taasisi za Umma kipengele namba 1.7 (IPSAS)

Kutowasilishwa kwa taarifa ya hesabu kwa ajili ya kupitiwa na kutolewa maoni kwa kamati ya ukaguzi na kitengo cha ukaguzi wa ndani ili kuweza kubainishwa dosari zilizopo kabla ya kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Jambo ambalo ni kwenda kinyume na kanuni ya 149(1)(m) ya Kanuni za usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021.

Kujitokeza kwa upotoshwaji wa taarifa za salio la hesabu ya mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo jumla ya shilingi 68,120,326 zilibainika kuwa ni salio anzia kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na sio shilingi 77,121,256 zilizoripotiwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jambo ambalo ni kwenda kinyume na miongozo ya ufungaji wa hesabu IPSAS Cash Basis 1.3.27 pamoja na kanuni ya 127 ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Karakana Kuu ya Magari kuhakikisha unafuata miongozo ya ufungaji na utayarishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka ikiwemo kuziwasilisha hesabu hizo kwa Mkaguzi wa ndani kwa lengo la kuzipitia na kuzitolea ushauri kabla ya kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi ili kuepusha kujitokeza kwa dosari nyingi wakati wa ukaguzi

Majibu ya Uongozi wa Karakana

Kutokubainishwa kwa mishahara yenye jumla ya shilingi 1,030,189,053 katika hesabu za mwisho wa mwaka kumetokana na ukweli kuwa kwa kipindi hicho mchakato wote wa uandaaji wa mishahara ya wafanyakazi wa Wakala ulikuwa ukisimamiwa na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, hivyo hatukujumuisha mishahara ya watumishi wa Wakala katika kitabu cha Hesabu za mwisho wa mwaka. Hata hivyo, baada ya kupata ushauri wa Wakaguzi kuhusiana na muongozo wa ufungaji wa

hesabu wa taasisi za Umma tayari tumerekebisha changamoto hiyo kwa kubainisha mishahara katika kitabu kilichowasilishwa cha Hesabu za mwisho wa mwaka uliofuatia (2023/2024).

Taarifa za hesabu hazikuwasilishwa kwa ajili ya kupitiwa na kutolewa maoni na kamati ya ukaguzi na kitengo cha ukaguzi wa ndani kwa sababu Wakala wa Karakana Kuu ya Magari haina Kamati ya ukaguzi wa ndani hadi sasa. Hii ni kutokana na kukosa Bodi ya Ushauri ya Wakala ambayo ndiyo yenye mamlaka ya kupitisha majina ya wateule wa Kamati hiyo ya ukaguzi wa ndani. Bodi ya Ushauri ya Wakala imemaliza muda wake tangu tarehe 31/07/2023. Wakala imepeleka taarifa Wizarani ya kumalizika kwa muda wa bodi ya ushauri na kuomba uundwaji wa bodi mpya ya ushauri kwa barua ya tarehe 10/07/2023 yenye kumbukumbu namba AC.5/93/01/18

Salio la Hesabu za WakalawaKarakana Kuu yaMagari Zanzibar linaloishiamwaka 2022/2023 ni TZS 77,121,256 nasio TZS 68,120,326 ambazo ni tofauti ya fedha kati ya salio la mwanzo “Cash at begin” na salio la mwisho “Cash at the end”.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika uchunguzi wake, Kamati ya PAC kwenye hoja hii imebaini yafuatayo:

1. kwa upande wa rosario zilizobainika katika mishahara ya Wakala kutokubainishwa kwa mishahara yenye jumla ya shilingi 1,030,189,053. Kamati imegunda kuwa ni kweli wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake katika Wakala huu kulikuwa na kasoro hiyo. Hilo lilijitokeza kutokana na Muhasibu kushindwa kufuata ipasavyo miongozo ya ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka. Kamati ilitaka kujua chanzo cha kuwepo dosari hii na kubaini kuwa kwa vile mishahara ya Watendaji wa Wakala ilikuwa ikilipwa na Wizara, Muhasibu alifaelewa kwamba itaonekana katika hesabu za Wizara na sio katika hesabu yao. Kwa mnasaba huu, hoja bado haijatekelezwa kwa ufanisi, hivyo Kamati imeibakisha.
2. kwa upande wa kutokuwasilishwa kwa taarifa ya hesabu kwenye Kamati ya Ukaguzi na Kitengo cha Ukaguzi kwa ajili ya kupatiwa maoni. Kamati ya PAC imegundua kuwa ni kweli kasoro hiyo ipo. Hilo limesababishwa na kutotekelezwa ipasavyo muundo wa utumishi (Organization structure) ya Wakala huo. Wakala unao muundo wake wa utumishi ambapo ndani yake mna kitengo cha Ukaguzi lakini hadi kamati inakamilisha majukumu yake katika Wakala huo, hakuna Mkurugenzi aliyechaguliwa kusimamia masuala ya ukaguzi. Kadhalika, Wakala haukuwa na Bodi yake ya Ushauri iliyokamilika. Hilo limetokana na Mwenyekiti wa Bodi hiyo kumaliza muda wake yangu mwaka 2022 lakini hakuna Mwenyekiti mwengine aliyechaguliwa. Hata hivyo majukumu ya Wakala yalikuwa

yakitekelezwa kwa kusuasua kwani iliwalazimu wamtumie Waziri katika kupata ushauri juu ya mambo tofauti wanayopanga kuyatekeleza. Hoja hii inabakia kwa hatua za utekelezaji.

3. Kuhusiana na suala la kujitokeza upotoshwaji wa taarifa za salio la hesabu ya mwisho wa mwaka 2022/2023. Kamati imebaini kuwa kulijitokeza makosa yaliyofanywa na Mkaguzi kwa kusahau kujumuisha ipasavyo kwa kiasi cha fedha kilichokusanywa na kili chotumika na kupelekea kujitokeza tofauti iliyoelezwa. Kwa msingi huu, hoja hii imeondolewa.

Hoja nambari 6.1.8.2: Kukosekana kwa makadirio ya mapato ya shilingi 55,340,658

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi umefanya mapitio ya taarifa za fedha za mapato na matumizi kwa lengo la kupima ufanisi wa ukusanyaji wa mapato unaotokana navyanzo mbali mbali vya kibajeti. Kutokana na tathmini iliyofanyika imebainika kutokukadiriwa kwa mapato kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na kubainishwa katika hesabu za mwisho wa mwaka jambo ambalo ukaguzi umetia shaka juu ya usahihi wa mapato ya shilingi 55,340,658 yaliyobainishwa katika taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka ambayo hayakukadiriwa kwa mujibu wa utaratibu wa ufungaji wa hesabu.

Kutokana na dosari hiyo ukaguzi umeshindwa kutathmini hali halisi ya makusanyo kupitia makadirio ambayo hayakuainishwa mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2022/2023 jambo ambalo ni kwenda kinyume na kanuni ya 28(1) ya Kanuni za Usimamiziwa Fedha za Umma ya 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Karakana Kuu ya Magari kuweka makadirio ya mapato ili kuweza kupima na kutathmini uwezo wa ukusanyaji wa mapato kupitia vyanzo vya mapato vilivyobainishwa na Wakala wa Karakana Kuu ya Magari.

Majibu ya Uongozi wa Karakana

Kama ilivyo kwa Taasisi nyengine za Serikali kabla ya kuanza kwa mwaka husika wa fedha, Taasisi zote hupangiwa makadirio ya matumizi na mapato kama Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inavyoelekeza. Hivyo Wakala kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 100,000,000, mapato ambayo ndiyo yaliyotumika katika kupimiana kutathmini hali ya makusanyo ya Wakala kwa mwaka huo wa fedha.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Baada ya Kamati ya PAC kupitia kwa makini hesabu ya mwisho wa mwaka ya Wakala huu, Kamati imebaini hesabu hiyo ilikuwa na makosa kwa kutokuingizwa kwa makisio ya bajeti ya mapato ya mwaka 2022/2023

(estimated budget) wala bajeti halisi iliyopo (original budget). Kwa msingi huo, hesabu hizo haziwezi kutoa taswira halisi na sahihi hususan kwa watumiaji wa hesabu hizo.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Wakala wa Karakana Kuu ya Magari ya Serikali ihakikishe inapondaa hesabu zake za mwisho wa mwaka waingize na makadirio ya bajeti ya mapato ili waweze kujipima katika utekelezaji wa malengo yao na kwenda sambamba na vigezo vya uandaaji vya kitaifa na kimataifa.

Hoja nambari 6.1.8.3: Dosari katika uwasilishaji wa taarifa za fedha shilingi 12,066,650

Ukaguzi ulifanya mapitio ya taarifa za fedha za Wakala wa Karakana Kuu ya Magari zitokanazo na ruzuku inayopokelewa kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Juni, 2023 na kubaini jumlaya shilingi 357,904,600 zimepokelewa ikiwa ni ruzuku ya uendeshaji wa shughuli zilizopangwa na Wakala wa Karakana Kuu ya Magari.

Katika taarifa za hesabu za Wakala zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi zimebainisha jumla ya shilingi 369,971,250 ni fedha iliyopokewa kwa ajili ya matumizi ya shughuli za uendeshaji zilizopangwa na kupelekea uwepo wa tofauti ya shilingi 12,066,650 jambo ambalo linapelekea kutokuonesha sura sahihi na halisi ya taarifa za hesabu zilizowasilishwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Karakana Kuu ya Magari kuongeza umakini katika uandaaji na utayarishaji wa taarifa za hesabu ili kuweza kuakisi miongozo ya kitaifa na kimataifa.

Majibu ya Uongozi wa Karakana

Kwa mujibu wa akaunti yetu ya matumizi, fedha tulizopokea kutoka Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Juni, 2023 ni TZS 369,971,250 ambazo katika hizo kiasi cha TZS 357,904,600 ni ruzuku ya uendeshaji wa shughuli za Wakala, na TZS 12,066,650 ni malimbikizo ya stahiki za maposho ya kukaimu kwa watendaji wa Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar. Hivyo tofauti hiyo ya TZS 12,066,650 haikujumuishwa kwenye hesabu ya ruzuku ya uendeshaji wa shughuli za Wakala.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kushughulikia hoja hii, Kamati ya PAC imegundua kuwa ni kweli kiasi cha shilingi 12, 066,650 hazikuwasilishwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka. Hali hiyo ilitokana na Watendaji wa Wakala kushindwa kujumuisha fedha hizo ambazo zilipokelewa na Wakala kutoka Wizarani kama ni matumizi mengineyo ikiwa ni stahiki za posho la kukaimu Ofisi na

kupelekea hesabu zilizowasilishwa kwa Mkaguzi na Wakala kuwa shilingi 357,904,600 badala ya 369,971,250 na kupelekea kuwepo tofauti ya shilingi 12,066,650

Maagizo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Wakala wa Karakana Kuu ya Magari ya Serikali uwe makini katika uandaaji wa hesabu zake za mwisho wa mwaka kwa kujumisha taarifa zote zinazohitajika ili kwenda sambamba na miongozo iliopo.

WAKALA WA KARAKANA YA MAGARI YA SERIKALI- PEMBA

Hoja nambari 6.1.8.4: Ukosefu wa mafundi wenye taaluma ya kutosha.

Kukosekana kwa Mafundi wenye taaluma ya kutosha kumepelekea Taasisi nyingi za Umma, Taasisi za Binafsi na Wananchi kwa jumla kushindwa kupeleka gari zao katika Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Pemba kwa ajili ya kufanyiwa matengenezo jambo ambalo linaweza kukosesha mapato Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Karakana kufanya jitihada za kuwasomesha mafundi waliopo pia kuajiri mafund iwenye taaluma ya kutosha.

Majibu ya Uongozi wa Karakana

Wakala wa Karakana Kuu Pemba imeanza kuwawezesha mafundi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbali mbali kutegemea na uwezo wa mafundi wenyewe kuweza kusomesheka pamoja na upatikanaji wa fedha.

Kwa sasa fundi mmoja Ndg. Omar Hamad Hamad anaendelea na masomo katika Chuo cha Ufundi Arusha chini ya ufadhili wa Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Pemba.

Aidha, Wakala imeendesha mafunzo ya ndani (on job training) kwa kutoa Wakufunzi kutoka Makao Makuu ya Wakala wa Karakana Kuu ya Magari, Unguja kwenda kutoa mafunzo ya ufundi kwa wafanyakazi wake wa Pemba ili kuwajengea uwezo wa kiutendaji na kiufundi na kuongeza ufanisi kwa huduma zinazotolewa.

Vile vile, katika hatua za kupunguza changamoto hizi, Wakala tayari imeshaajiri mfanyakazi mmoja wa ngazi ya ‘Certificate’ katika fani ya Ufundi wa umeme wa magari.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

KAmati ilipitia majukumu ya msingi ya Wakala na kubaini kuwa ina kazi kubwa yackufanya matengenezo ya gari za Serikali. Ili hilo litekelezeke, ni lazima Wakala uwe na Watendaji wenye utaalamu wa kisasa hasa

ukizingatia gari za Serikali za siku hizi zinakuwa zimetengenzwa kwa tekbolojia ya hali ya juu.

Katika kutathimini hoja hii, Kamati imebaini kuwa hauna Watendaji wenye utaalamu wa kutosha wala hakuna mpango madhubuti wa kuwaendeleza Wataalamu walionao ili waweze kwenda samabamba na mabadiliko ya kiteknolojia ya magari ya kisasa. Hata hivyo, Serikali baada ya kuliona hilo imekuja na njia mbadala ya kuuimarisha utendaji wa Wakala kwa kuingia ubia na Kampuni binafsi ya ..... kwenye masuala mazima ya utoaji huduma za matengenezo ya gari za Serikali.

Pamoja na nia njema ya Serikali, Kamati imepata mashaka kwenye mambo yafuatayo:

1. jinsi mchakato ulivyofanyika wa kumpata Mbia huyo.Kamati imebaini kwamba Wakala unaonekana haukuwa na maandalizi yaliyo imara kwani Kamati ilishindwa kupata concept note.
2. Hadi Kamati inakamilisha kazi zake, imeshindwa kupata Mkataba wa makubaliano ya awali ya ubia huo ili kuweza kujua kama mambo ya msingi yakiwemo Mpango uliomo wa Matengenezo ya gari za Serikali. Kamati ilielezwa kwamba Ubiya huo umefanywa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Wakala huu pamoja na kujua uzoefu wa kazi kama hizo uliofanywa na Kampuni hizo katika Taasisi tofauti.
3. Hivi sasa Kampuni inajiandaa kuja Zanzibar muda wowote kuanzia sasa kwa kuanza kazi za majaribio.
4. Watendaji wa Wakala hawajafanya tathmini inayotakiwa ikiwemo kwenda kutembelea Kampuni hiyo ili kujua uwezo wake halisi ulionao (due delegence). Hilo limebainika baada ya Kamati kuomba ipatiwe ripoti na kushindwa kupatikana.
5. Serikali itanufaika na mkataba huo kwa kupata asilimia 25 ya biashara iliyofanyika na sio Friday inayopatikana na asilimia iliyobakia kampuni itanufaika nayo.
6. kamati ilitaka kujua hesabu (account) ya pamoja kama ipo na kuelezwa kwamba kumeundwa kamati maalum itakayokuwa na jukumu la kufungua hesabu hiyo.
7. Mkataba wa utekelezaji kazi hiyo kamati nao haujapatiwa.

Hoja nambari 6.1.8.5: Uwepo wa upungufu wa watumishi

Ukaguzi ulibaini kwamba Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Pemba ina upungufu wa watumishi muhimu ambao wangeliwezesha wakala kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Upungufu huu unaathiri Wakala ikiwani pamoja na utoaji duni wa huduma, mrundikano wa majukumu na kupunguza hamasa ya utendaji kwa watumishi waliopo, hali inayoweza kupelekea ucheleweshaji wa utoaji huduma kwa taasisi za Umma na jamii kwa jumla.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba Sheria, Utumishi na Utawala Bora kulipa kipaumbele suala la uajiri ili kupunguza changamoto za utendaji zinazokabili Taasisi**.**

Majibu ya Uongozi wa Karakana

Wakala tayari imepeleka maombi ya kupatiwa kibali cha ajira mpya kwa nafasi 7 kwa upande wa Ofisi ya Pemba kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kupitia mpango wa Nominal Roll ya mwaka 2023/2024 kwa lengo la kuajiri mafundi wataalamu. Hata hivyo, nafasi hizo hazikupatikana zote kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wetu na badala yake zilipatikana nafasi tatu (3). Maombi hayo yaliombwa kwa barua yenye kumbukumbu nambari WKKM/UW/15/VOLI/15 ya tarehe 7/08/2023 na AC.58/116/01 ya tarehe 13/02/2024 kiambatanisho cha maombi hayo kinajieleza.

Aidha, ruhusa ya kufanya ajira kwa mfumo wa ‘outsource’ iliombwa kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa barua yenye kumbukumbu nambari AC.22/58/01 ya tarehe 10/05/2024.

Tulipokea barua ya kibali cha ajira kutoka Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba Sheria, Utumishi na Utawala Bora yenye kumbukumbu namba DB.117/157/07/32 ya tarehe 27/02/2024 kwa nafasi tatu (3) ambazo ni (fundi magari 1, afisa sheria 1 na afisa mfumo 1). Hata hivyo, hadi leo imeshindikana kuajiri kutokana na changamoto ya kutokuwepo Bodi ya Ushauri ya Wakala.

Uchunguzi na Maagizo ya Kamati.

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati imebaini kwamba uchunguzi na maagizo yake ni kama yanavyoonekana katika hoja nambari 6.1.8.4

Hoja nambari 6.1.8.6: Kutokuuzwa au kufanyiwa matengenezo kwa gari chakavu

Ukaguzi umebaini kua Wakala wa Karakana Kuu ya Magari inamiliki gari aina ya Toyota yenye namba za usajili SLS 137 ambayo ipo maneo ya Ofisi Kuu ya Wakala Wilaya ya Chakechake Pemba. Gari hii haitumiki kwa muda mrefu sasa bila kufanyiwa matengenezo au kuiondowa kama inavyotakiwa na Sheria.Hali hii inaweza kupelekea gari hii kushuka thamani na Serikali kushindwa kunufaika nayowakati ingeweza kunufaika iwapo Wakala ingeamua kifanyia matengenezo au kuiondowa mapema inavyowezekana.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala kuhakikishaunaweka Mpango mzuri wa matumizi ya Rasilimali zake ikiwa ni pamoja na mali zilizochakaa au kuharibika kwa muda mrefu kuziombea ruhusa Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa ajili ya kuuzwa**.**

Majibu ya Uongozi wa Karakana

Ni kweli gari iliyotajwa imekaa muda mrefu bila kutumika. Hata hivyo Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Pemba pamoja na kuchukuwa juhudi za maksudi kuifanyia matengenezo gari hiyo, imeshindwa kuirejesha gari hiyo kuweza kutumika. Hivyo Wakala imechukuwa hatua ya kumuandikia barua Afisa Mdhamini wa Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi ili na yeye amuandikie barua Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi ili kupelekwa maombi kwa msajili wa Hazina kwa ajili ya kuondolewa (kuuzwa).

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Ni kweli wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake katika Wakala huu kulikuwa na gari ambayo hakuna hatua za kuiondosha iliyochukuliwa. Hilo pia limeshuhudiwa na Kamati kwamba licha ya Afisa Mdhamini wa Mawasiliano kuandika barua ya tarehe 18/1/2024 yenye kumbukumbu nambari WUMUP/M.84/VOL. XI/17 kwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo juu ya uondoshaji wa gari chakavu ya Wakala yenye nambari za usajili SLS 137A, bado gari hiyo haijaondolewa na lakushangaza zaidi ni kwamba hata barua husika haikujibiwa.

Kamati pia imebaini Wakala huu una ukosefu mkubwa kupata bajeti yake inayopelekea kushindwa kutekeleza kazi zake na kufikia malengo yake. Hili limebainika kwani hizo gari 3 walizozipata zilitokana na mchakato uliofanywa na ZAECA wakati wa uchukuaji wa magari yaliyokuwa yamekaa bila ya kufanyiwa matengenezo. Kwa msingi huo, hoja hiyo inabakia hadi hapo Wakala utakapokamilisha taratibu zacuuuzwaji wa gari hiyo.

Hoja nambari 6.1.8.7: Kukosekana kwa kitengo cha unyoshaji, upigaji rangi na usafishaji wa magari

Ukaguzi ulibaini kua hadi sasa Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Pemba haijaanzisha kitengo cha unyooshaji na upigaji rangi wa magari wala kuanzisha huduma ya kuosha magari hali inayoweza kuondoa dhana halisi ya kuwa na Karakana Kuu ya matengenezo ya magari na hivyo kukosesha Serikali Mapato.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Karakana Kuu ya Magari Pemba kufanya jitihada zitakazowezesha kuanzisha vitengo vyote muhimu vinavyohusiana na ufundi wa Magari.

Majibu ya Uongozi wa Karakana.

Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Pemba inayo matarajio ya kuanzisha kitengo hicho, changamoto inayotukabili ni kukosekana kwa wafanyakazi wa kuweza kukifanyia kazi kitengo hicho na pia kukosa kabisa kwa mafundi wa kuweza kuwapatia mafunzo yanayohusiana na kitengo hicho.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kwamba Wakala hauna Kitengo hicho ambacho ni miongoni mwa kitengo muhimu mno katika utekelezaji wa kazi za Wakala. Kadhalika, Kamati imegundua kwa vile Waziri hayupo katika kikao kilichofanyika, ni busara Kamati ikasikia mipango ya Waziri katika kuitekeleza hoja hii. Hivyo, hoja imebakia kwa hatua za utekelezaji.

Hoja nambari 6.1.8.8: Kutokutayarishwa kwa Mpango wa Matengenezo ya Mali

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Pemba haina utaratibu wa kutayarisha mpango rasmi wa matengenezo wa mali zilizo chini ya umiliki wake hali iliyosababisha baadhi ya mali inazozimiliki ikiwemo jengo linalotumika kwa kutengenezea magari kuwa katika hali isiyoridhisha kwa utoaji wa huduma kutokana na uchakavu wake, hali hii imesababishwa na Wakala kutolipa kipaombele suala la utengenezaji wa jengo hilo katika bajeti yake ya mwaka**.**

Ukaguzi unashauri uongozi wa Karakana Kuu ya Magari kuandaa mpango wa matengenezo ya mali na kutenga fedha za kutosha katika bajeti ya mwaka ili kuboresha mazingira ya Karakana utakaoendana na wakati.

Majibu ya Uongozi wa Karakana

Wakala wa Karakana Kuu ya Magari imechukua hatua stahili za kuhakikisha inakuwa na uwelewa mzuri na wakutosha kuhusiana na mpango rasmi wa matengenezo ya mali zilizo chini ya umiliki wake. Miongoni mwa hatua hizo ni kushiriki katika timu ya uandaaji wa Muongozo wa Serikali wa kuandaa Mpango wa Matengenezo ya Mali za Umma. Aidha, kutokujumuishwa kwa matengenezo ya jengo la kutengenezea magari katika bajeti ya mwaka ni kutokana na ufinyu wa bajeti tunaokabiliana nao katika Taasisi yetu.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia maiibu ya hoja hii, Kamati ya PAC ilitaka kujua kwamba Wakala unao Mpango wa Matengenezo ya magari na kuelezwa Mpango upo na umeingizwa katika katika Mkataba wa Ubia. Hivyo Kamati hailiweza kuthibitosha hilo mpaka Kamati itakapopata fursa na kukutana na Waziri husika.

Hoja nambari 6.1.8.9: Uwepo wa muitiko mdogo wa Taasisi za Umma wa kufanya Matengenezo ya magari ya karakana Kuu.

Ukaguzi ulibaini kwamba muitikio wa Taasisi za Serikali kupeleka gari wanazomiliki karakana Kuu kwa ajili ya matengenezo ni mdogo hali

iliyosababishwa na kukosekana kwa nguvu ya kisheria katika kuhakikisha magari yote ya Serikali yanapeleka magari yao kufanyiwa matengenezo Karakana Kuu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Karakana Kuu kufanya maboresho ya Sheria yake katika baadhi ya vifungu au kuingiza vifungu vipya na pia kufanya uhamasishaji kwa kutoa uelewa kwa Taasisi za Umma

Majibu ya Uongozi wa Karakana.

Wakala inafanya juhudi kubwa za kuzihamasisha Taasisi za Umma na Jamii kwa jumla juu ya uwepo wa Karakana Kuu ya Serikali na umuhimu wa Taasisi za Serikali kuitumia Wakala kwa ajili ya kuyafanyia matengenezo magari yao. Miongon imwa juhudi hizo ni Ushiriki wa Wakala Katika maonyesho mbali mbali ya kitaifa na kimataifa yakiwemo maonesho ya Siku ya chakula Duniani ambayo hufanyika katika viwanja vya Chamanangwe Pemba. Na pia Wakala wa Karakana kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imewahi kuzitaarifu Wizara zote na Taasisi zao juu ya hatua ya kufanyiwa matengenezoya gari zake zote chini ya Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Pemba.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imegundua kuwa Agizo la Serikali la kutaka gari zote za Serikali zifanyiwe matengenezo kwa Wakala lakini bado agizo halijatengenezwa. Hivyo Kamati imeendelea kuibakisha hoja hii kwa hatua za utekelezaji hasa ukizingatia maamuzi ya Serikali ya gari za Serikali kufanyiwa .matengenezo kupitia Ubia wa Wakala na Kampuni.

WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA MALI (BPRA)

Hoja Nambari 6.1.9.1: Dosari katika Uandaaji wa Taarifa za Hesabu za Mwisho wa Mwaka shilling 15,495,019.86

Kwa mujibu wa IPSAS Cash Basis 1.7 inaelezea juu ya uandaaji wa taarifa za ulinganishi wa Bajeti na utekelezaji ambapo taarifa hizo zitalazimika kuwa ni taarifa sahihi na zisizo na makosa.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya taarifa za ulinganishi wa Bajeti na utekelezaji halisi na kubaini jumla ya shilingi 2,391,798,241.71 hazikuwa na uwiano na taarifa za Mapato na Matumizi ambazo ziliripotiwa kuwa ni shilingi 2,376,303,221.85 na kupelekea uwepo wa tofauti ya shilingi 15,495,019.86 katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka zilizowasilishwa kwa ukaguzi.

Pamoja na uwepo wa taarifa za maboresho ya hesabu iliyowasilishwa kwa mara ya pili kwa ajili ya ukaguzi bado ilibainika uwepo wa tofauti ya shilingi 15,495,019.86 baina ya matumizi halisi yaliyoainishwa katika taarifa za bajeti na utekelezaji halisi dhidi ya matumizi yaliyoainishwa katika taarifa za mapato na matumizi jambo ambalo limepelekea ukiukwaji mkubwa wa miongozo ya Ufungaji wa Hesabu za Taasisi za Umma (IPSAS Cash Basis) na hatimae taarifa hizo kutokuonesha sura sahihi na halisi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar kuhakikisha taarifa za fedha zinawasilishwa kwa Kamati ya Ukaguzi ya Wizara pamoja na Kitengo cha Ukaguzi wa ndani kwa kuweza kupitiwa na kufanyiwa maboresho kabla ya kuwasilishwa kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi.

Majibu ya Uongozi

Ni kweli kulikuwa na tofauti ya fedha jumla ya shilingi 15,495,019.86 kulikosababishwa na makosa ya kutokuingizwa kwa fedha za vifungu vya Note No 19.0 Supplies and consumable goods kwenye taarifa za fedha za mwaka 2022/2023. Vifungu hivyo ni kama ifuatavyo:

a)	Policy and law stakeholders	4,475,019
b)	Risk allowance	1500,000
c)	Brocasting charges	18,000,000
d)	Sundry expenses	2,000,000
e)	Commettee setting allowance	5,720,000
Jumla		**15,495,018**

Sababu: Hali hii ilichangiwa kwa kiasi kikubwa na kukosekana kwa taarifa muhimu za fedha kutoka kwa mhasibu aliyesimamishwa kazi ghafla. Hivyo ilimlazimu Mhasibu aliyefunga hesabu kwa wakati huo kukosa muda wa

kutosha wa kupitia taarifa za fedha za mwisho wa mwaka kabla ya kuziwasilisha kwa ukaguzi.

Hatua ya Utekelezaji: Baada ya Kamati iliyoundwa kuwasilisha ripoti yake, Uongozi wa BPRA ulifanikiwa kuzipitia taarifa zake za fedha za mwisho wa Mwaka 2022/23 na kuzifanyia maboresho.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Uongozi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA) kukiri kuwepok wa utofauti wa hesabu katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka, kamati PAC wakati wa uchunguzi imebaini kuwa kasoro hiyo imesababishwa na watendaji wa kitengo cha uhasibu kutokuwa na uwelewa wa uwandaaji wa taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka na kupelekea kujitokeza kwa mapungufu mengi kama yalivoonesha katika majibu yao.

Kutokana na kasoro hiyo, kamati imegundua pia yapo mapungufu mengine ya kutokufuata sharia ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016 inayoeleza kwamba tarifa zote za fedha baada ya kukamilika ziwasilishwa kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili Ukaguzi, ambapo wakala baadaya kufanya marekebisho ya taarifa ya fedha haikuwasilisha mamlaka husika kama sharia inavyoelekeza.

Wakati wa uchunguzi ukiendelea taarifa hiyo ambayo iliyofanyiwa marekebisho kwa ajili ya ukaguzi

Iliwasilishwa mbele ya kamati na kupitiwa pamoja na mkaguzi kutoka Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na baada ya kuridhiwa hoja hiyo imeondolewa.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauagiza Uongozi wa Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhakikisha kuwa inaendelea kuwapatia mafunzo wahasibu wote wa Serikali juu ya namna bora ya uandaaji wa taaifa za Hesabu za Mwisho wa Mwaka ili kuondokana na matumizi mabaya ya fedha za Serikali**.**

Hoja Nambari 6.1.9.2: mapato yaliyokusanywa nje ya mfumo wa ZanMalipo Shillingi 726.954,846

Kifungu nambari 55(a) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaelezea kwamba “Fedha zote za Umma zitakusanywa kupitia mfumo wa malipo wa kielektroniki uliowekwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali”. Katika kutekeleza agizo hilo la Serikali ilianzisha rasmi mfumo wa ‘ZanMalipo’ ili kuweza kukusanya fedha zote za Serikali kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mapato ya Serikali.

Ukaguzi ulipitia taarifa za mapato za Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar na kubaini uwepo wa makusanyo yenye jumla ya shilingi

726,954,846 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yaliyokusanywa nje ya mfumo wa malipo (ZanMalipo).

Kufanya makusanyo nje ya mfumo kunaweza kupelekea viashiria vya upotevu wa mapato ya Serikali pamoja na kwenda kinyume na Kifungu cha 55 (a) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar kuhakikisha fedha zote zinakusanywa kupitia mfumo wa malipo wa kielektroniki kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mapato ya Serikali.

Majibu ya Uongozi

Mnamo mwaka 2018, Serikali iliridhia BPRA kuanzisha Mfumo wa Usajili Mtandaoni (Online Registration System (ORS)). Mfumo huo ulilenga kufanya usajili wa biashara (kampuni na majina ya biashara) pamoja na kukusanya mapato yanayotakana na usajili huo. Mwaka 2021, Serikali ilianzisha mfumo wa Zanmalipo uliokusudiwa kukusanya malipo yote yanayofanyika serikalini. Kwa kuwa BPRA tayari ilikuwa na mfumo wa ORS unaosajili na kukusanya mapato, na kwa kuwa mnamo mwaka 2019 mara baada ya kuanza kufanya kazi mfumo wa ORS kutokana na ufanisi wake, Serikali kupitia Wizara ya Fedha iliridhia kuanzishwa mfumo wa National Online Business System (NOBS) uliolenga kutanuwa mawanda ya mfumo wa ORS ili kuongeza wigo katika usajili wa biashara, utolewaji wa vibali, leseni, na ruhusa katika masuala ya biashara kwa taasisi mbali mbali zikiwemo BPRA yenyewe, ZIPA, Kamisheni ya Utalii, Baraza la Udhiniti wa Leseni (BLRC) na taasisi inazozimamia. Kwa ujio wa mfumo wa NOBS iliamulika katika vikao mbali mbali kwamba utaratibu wa malipo kwa BPRA uendelee hadi utakapokamilika mfumo wa NOBS.

Kwa kuwa mfumo wa NOBS hadi kufikia mwaka 2022/2023 haukuwa umeanza kufanya kazi licha ya kuwa ulikabidhiwa rasmi kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GAZ), BPRA iliendelea kukusanya mapato kupitia mfumo wake wa ORS. Hali iliopelekea fedha 726,954,846 kukusanya nje ya mfumo wa Zanmalipo ingawa fedha hizo zilikuwa zinaenda kwenye Mfuko wa Hazina kila mwezi kupitia Bank ya PBZ.

Kwa kuwa jambo hilo limekuwa la muda mrefu BPRA tumechukuwa hatua mbali mbali kama zilivyoainshwa hapo chini.

Sababu: Huduma za usajili wa makampuni na majina ya biashara hufanyika katika mfumo wa ORS ambao unazalisha Namba ya Udhibiti (Control Number) iliyopelekea fedha shilingi 726,954,846 zilizokusanywa kutoonekana katika mfumo wa ZanMalipo.

Hatua za Utekelezaji: Kwa vile dosari hii ni ya msingi na ya muda, Uongozi wa BPRA umechukuwa hatua mbali mbali baada ya kuona mfumo wa NOBS umeshindwa kufanya kazi kama ilivyotarajiwa. Hatua hizo ni pamoja na:

a. Kukutana na kufanya mazungumzo na uongozi wa Mamlaka Serikali Mtandao Zanzibar yenye jukumu la kusimamia mifumo yote Zanzibar, kufanya mawasiliano kupitia barua mbali mbali, barua pepe, vikao katika mitandao ya kijamii (skype na WhatsApp) kwa uratibu wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ili kuisaidia kuondokana na dosari hii. Ushahidi wa hayo ni vielelezo vilivoambatanishwa. Hata hivyo, bado jambo halijaweza kupatiwa ufumbuzi.

b. BPRA kwa nia njema kabisa ya kuondokana na dosari hii imeanza kufanya mazungumzo na mkandarasi wa mfumo wa ORS/NOBS ambaye ni NRD baada ya kupokea barua kutoka eGAZ yenye kumbukumbu namba CA.109/351/01-M/80 ya tarehe 22 Oktoba 2024 ili kuweza kuunganisha mfumo wa ORS na mfumo wa ZanMalipo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa Hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa licha ya kuwepo wa muongozo kutoka kwa Wakala wa Serikasli Mtandao (e-gaz) wa utumiaji wa mifumo wa ZanMalipo kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa Taasisi zote zinazokusanya,

Kamati hadi inakamilisha uchunguzi wake Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali bado inaendelea kutumia mfumo wake wa Online Registration System (ORS) jambo ambalo ni kwenda kinyume na agizo la Serikali na kupelekea hoja kubakia kwa ajili ya hatua za utekelezaji.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauagiza Uongozi za Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali za Serikali kuhakikisha fedha zote zinazokusanywa zinapitia katika mfumo wa Kieletronic ZanMalipo kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Hoja Nambari 6.1.9.3: Kukosekana kwa Taarifa ya Mapato shilingi 2,693, 743 638 katika mfumu wa ZanMalipo

Kwa mujibu wa kanuni ya 25(1) ya Kanuni ya Usimamizi wa fedha za Umma ya 2021 inamtaka Afisa Masuuli kuhakikisha anasimamia vyema taarifa za fedha za taasisi.

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ukaguzi ulifanya mapitio ya taarifa za fedha za mwisho wa mwaka za Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali

Zanzibar na kubaini jumla ya shilingi 2,693,743,638 zilikusanywa kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato.

Aidha, ukaguzi haukuweza kuthibitisha usahihi wa taarifa hizo za mapato kutokana na kukosekana kwa taarifa muhimu za mapato yaliyokusanywa kupitia mfumo wa ZanMalipo kwa kipindi cha mwezi wa Julai 2022 hadi Disemba, 2022.

Kukosekana kwa taarifa za mfumo wa ZanMalipo kwa ukaguzi juu ya makusanyo ya shilingi 2,693,743,638 yaliyokusanywa na BPRA , ukaguzi haukuweza kuthibitisha usahihi wa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar kuhakikisha unafanya usuluhishi wa taarifa za fedha kabla ya ufungaji wa hesabu na ni vyema taarifa hizo kupitiwa na vitengo vya ndani vya ukaguzi wa hesabu ili kuweza kutolewa maoni na mapendezo kuhusiana na usahihi wa hesabu hizo kabla ya kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Majibu ya Uongozi

Ni kweli katika kipindi cha ukaguzi kulikuwa na changamoto ya upatikanaji wa taarifa za makusanyo kutoka katika mfumo wa ZanMalipo kwa upande wa BPRA. Dosari hiyo ilichangiwa kwa kiasi kikubwa na kukosekana kwa makabidhiano (handover) rasmi ya ofisi baina ya Mhasibu aliyesimamishwa kazi na Mhasibu aliyechukuwa nafasi yake hali iliyomfanya Mhasibu mpya kukosa *credentials* za kuingia katika mfumo wa ZanMalipo.

Sababu: Taarifa za Mfumo wa ZanMalipo kwa upande wa BPRA zilizuiwa baada ya baadhi ya watendaji wa BPRA kusimamishwa kazi ili kupisha uchunguzi.

Hatua za Utekelezaji: BPRA imefanya jitihada za kutosha kuweza kuwashirikisha Mamlaka ya Serikal Mtandao katika kutatua changamoto hii; na kwa sasa taarifa zote za mapato ya shilingi 2,693,743,638 zilizokusanywa kupitia mfumo wa ZanMalipo zimepatikana.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, imebaini kuwa hoja hii inaenda sambamba na uchunguzi wa hoja Nambari 6.1.9.2.

Hoja Nambari 6.1.9.4: Usimamizi usioridhisha wa Fedha za TIRKA

Tirka ni Mali au haki ya kimali aliyoiwacha mtu baada ya kufariki dunia. Ukaguzi ulifanya mapitio ya taarifa mbalimbali za fedha ili kuweza kutathmini endapo usimamizi wa fedha zinazotokana na Tirka

zinasimamiwa ipasavyo na kubaini kwamba kwa mwaka wa fedha 2022/2023 usimamizi wa fedha hizo haukua wa kuridhisha.

Kutokana na taarifa za fedha zilizoandaliwa na kuwasilishwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar zilibainisha jumla ya shilingi 632,875,323.59 zilipokelewa kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) kwa ajili ya kulipa Tirka. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 jumla shilingi 299,939,887.99 zilitumika kulipa Tirka na kupelekea uwepo wa bakaa ya shilingi 332,935,435.60 jambo ambalo linatofautiana na taarifa za fedha za shilingi 317,440,415.74 zilizoripotiwa kama bakaa ya fedha ya Tirka kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na kupelekea uwepo wa tofauti ya shilingi 15,495,019.86. Mchanganuo wa taarifa hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 104: Mchanganuo wa fedha za Tirka

Bakaa ya Fedha za Tirka 2022/2023 (Tsh.)	Bakaa ya Fedha za Tirka kabla ya kujumuishwa kwa bakaa yafedha la 2021/2022 (Tsh.)	Tofauti (Tshs)
332,935,435.60	317,440,415.74	15,495,019.86

Pamoja na uwepo wa tofauti hiyo ukaguzi ulifanya ufuatiliaji wa majibu ya hoja na kubainika kupitia taarifa za fedha zilizofanyiwa maboresho na kuwasilishwa kwa mara ya pili ilibainika kujitokeza kwa tofauti ya shilingi 31,210,168.93 baina ya bakaa la fedha iliyoainishwa katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka ukilinganisha na bakaa la fedha lililoainishwa mara ya pili katika hesabu za Wakala jambo ambalo limepelekea kushindwa kujiridhisha juu ya usahihi wa taarifa zilizowasilishwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar kuhakikisha hauchanganyi fedha za Tirka na fedha za matumizi mengineyo ili kuepusha uwezekano wa uwepo wa matumizi mabaya ya fedha ambayo yatapelekea kushindwa kuwalipa warithi kwa wakati. Mchanganuo wa taarifa hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini

Jadweli Nambari 105: Tofauti ya fedha za Tirka baina ya hesabu za benki na Taarifa yaUfungaji wa Hesabu

Bakaa la Fedha 2022/2023 Kwa Mujibu wa Hesabu za Wakala (Bank Statements) **(A)**	**Bakaa la Fedha 2022/2023 Kwa mujibu wa Taarifa za Fedha za mwisho wa mwaka** **(Financial Statement)** **(B)**	**Tofauti** **(A-B)**

Nambari ya Hesabu	Kiasi (Tsh)	Kiasi (Tsh)	Kiasi (Tsh)
0404422000	100,000	**383,756,402**	**31,210,168.93**
0404063000	414,866,570.93		
Jumla	**414,966,570.93**		

Majibu ya Uongozi

Dosari hii ilichangiwa na kutopatikana kwa taarifa za matumzi ya fedha hizo shilingi 15,595,019.86 kutokana na makosa ya kujumlisha katika taarifa za fedha kutokupata ushirikiano kutoka kwa Muhasibu aliyeondoka baada ya kusimamishwa kazi. Mawasiliano yalifanyika kwa njia ya simu na Mhasibu mpya na akaeleza kwamba hawezi kuja ofisini kwa mujibu wa maelekezo yaliyokuwemo katika barua yake ya kusimamishwa kazi.

Sababu:

Majibu: Tofauti ya shilingi 31,210,168

Tofauti ya shilingi 31,210,168 iliyojitokeza mara ya pili ilisababishwa na kukosekana kwa taarifa za malinganisho ya benki (bank statement) zizoishia tarehe 27/6/2023 wakati ukaguzi unafanyika, ambapo taarifa za malinganisho ya tarehe 28-30 Juni 2023 hazikupatikana kwa ukaguzi kwa kuwa ziliwasilishwa pungufu. Taarifa za fedha za tarehe hizo zikijumuishwa na shilingi 15,595,019.86 tofauti ya fedha za Tirka kunafanya jumla kuu ya tofauti ya shilingi 31,210,168.

Hatua za Utekelezaji: BPRA imefanikiwa kufungua nambari ya hesabu mpya ya matumizi iliyotafautisha na nambari ya hesabu ya tirka ili kuondosha dosari hiyo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC katika ufuatiliaji wa hoja hii imegundua kuwepo kwa usimamizi usioridhisha kwa Akaunti ya fedha za TIRKA uliotokana na kutokuwepo kwa Mhasibu Husika wakati wa ukaguzi. Kutokana na hali hiyo, Uongozi wa Wakala ulipeleka Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka ya tarehe 27/06/2022 badala ya Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka tarehe 30/06/2023 na kupelekea kujitokeza kwa utofauti huo. Hata hivyo, Uongozi wa Wakala umeshachukua juhudi za ila kwa sasa Wakala umechukua juhudi za kufanya marekebisho ya kasoro hizo ili siweze kujirudia tena katika Ripoti zijazo.

WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA MALI (BPRA) - PEMBA

Hoja nambari 6.1.9.5: Dosari Uwepo wa upungufu wa watumishi

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Pemba ina upungufu wa watumishi muhimu ambao wangaliwezesha Wakala kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Upungufu huu unaathiri utendaji wa jumla wa Wakala ikiwa ni pamoja na utoaji duni wa huduma, mrundikano wa majukumu, na kupunguza hamasa ya utendaji kazi kwa watumishi waliopo. Hali inayoweza kupelekea ucheleweshwaji wa utoaji huduma kwa taasisi za umma na jamii kwa ujumla na pia ni kuikosesha mapato Serikali.

Kutokufanya uajiri kwa mujibu wa nafasi zilizowazi ni kwenda kinyume na kanuni nambari 6(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kulipa kipaombele suala la uajiri ili kupunguza changamoto za kiutendaji zinazoikabili taasisi husika. Mchanganuo wa upungufu wa watumishi ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 106: Upungufu wa Watumishi

Namba	Kada	Waliopo	Wanaohitajika	Upungufu
1.	Afisa Mipango	0	1	1
2.	Afisa IT	1	2	1
3.	Afisa Masjala	0	1	1
	Walinzi	1	2	1
Jumla		**2**	**6**	**4**

Majibu ya Uongozi wa Wakala

Ni kweli kumekuwepo na upungufu wa watumishi katika Wakala hali ambayo inaathiri utekelezaji wa kila siku wa majukumu ya taasisi yetu. Kwa kipindi cha ukaguzi, Wakala ilikuwa ipo chini ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ambayo ndio ilikuwa ikisimamia suala zila zima la utumishi katika Wakala. Kuanzia Julai 2023, Serikali iliamuwa kuwa Wakala iwe ni miongini mwa taasisi zinazojitegemea ikiwemo kusimamia masuala ya kiutumishi. Katika kufanyia kazi hoja ya upungufu wa watumishi, Wakala imejumuisha suala la uajiri wa watumishi wapya katika

Mpango Kazi wa Mwaka 2024/2025 na tayari tumeshawasilisha ombi la kupatiwa Kibali cha Uajiri katika Wizara inayosimamia utumishi kwa nafasi za Unguja na Pemba.

Hali hii imesababishwa na kukosekana kwa kibali cha uajiri kutoka Wizara inayohusiana na utumishi kwa taasisi nzima ya Wakala.

Hatua ya Utekelezaji:

Wakala imeweza kufanya jitihada kubwa katika kutatua changamoto hii. Kwa sasa, Wakala imefanikiwa kupata watumishi wawili wa kuazima kwa muda ambao ni:

1. **Ndg. Hafidh Khatib Iddi, Dereva**: Ameazimwa kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kusaidia katika usafirishaji na majukumu mengine yanayohusiana na usafiri ndani ya Wakala.

2. **Ndg. Abdulwahid Mohd Khalid, Afisa wa Tehama**: Ameazimwa kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba ili kusaidia katika masuala ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), ambayo ni muhimu kwa ufanisi wa shughuli za Wakala.

Licha ya kupatikana kwa watumishi hao wawili, Wakala iliendelea, na inaendelea, na juhudi za kuazima watumishi akiwemo afisa mipango katika taasisi nyengine za Serikali kama Mamlaka ya Madawa ya kulevya na ZAWA ambako kulionekana kuwepo watumishi wa kada hio wengi lakini maombi hayakufanikiwa.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Wakati ikifuatilia utekelezaji wa hoja hii Kamati ya PAC imebaini kuwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA) imekiri kuwepo kwa kasoro hiyo kwa muda mrefu ya ukosefu wa watumishi wa kada mbali mbali, licha ya kupatiwa watumishi kutoka katika taasisi nyengine za Serikali bado Wakala inakabiliwa na changamoto ya uhaba ya watumishi kama ilivoripotiwa katika ripoti ya mdhibiti.

Licha ya Uongozi wa Wakala kuchukua juhudi mbali mbali za kuomba kibali cha uajiri kutoka Tume ya Utumishi Serikalini hadi Kamati inakamilisha uchunguzi wake ruhusa hiyo ya uajiri haikupatikana. Aidha, Kamati iliomba kupatiwa baadhi ya vielelezo kwa ajili ya uchunguzi ikiwemo Mpango wa Uajiri wa Mwaka wa Wakala pamoja Mpango wa Urithishaji wa Uongozi ambapo hadi Kamati inakamilisha uchunguzi wake vielelezo hivyo havikuwasilishwa.

Kutokana na changamoto hiyo, kamati ya PAC imeibakisha hoja hii kwa ajili ya hatua za utekelezaji.

Magizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauagiza Uongozi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali kuhakikisha inafuatilia kwa karibu utekelezaji wa upatikanaji wa kibali cha uajiri kutoka Tume ya Utumishi Serikali ili kuondokana na changamoto za kiutendaji.

Ili kuondoa changamoto iliopo ya uhaba wa wafanyakazi Kamati ya PAC inautaka Uongozi wa Wakala kutafuta Wafanyakazi wenye kada zinazolingana na mahitaji yao kutoka katika taasisi yengine za Serikali zenye kada kama hizo wanazozihitaji.

Hoja Nambari 6.1.9.6: Kukosekana kwa gari kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za wakala

Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali inajukumu la kusajili na kushajihisha wananchi kusajili biashara na mali zao kwa lengo la kuongeza pato la Taasisi na Serikali kwa ujumla.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Pemba haina vyombo vya usafiri (Gari) hali iliyopelekea kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu ya kushajihisha wananchi wa maeneo mbali mbali katika kisiwa cha Pemba juu ya umuhimu wa kuwa na nyaraka za biashara na mali wanazozimiliki.

Kukosekana kwa vyombo vya usafiri kunaweza kupelekea Wakala kushindwa kufikia malengo yake iliyojiwekea.

Ukaguzi unaishauri Serikali kuandaa mpango wa dharura wa kuipatia Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Pemba vyombo vya usafiri ili viweze kusaidia katika kufikia lengo la uhamasishaji wananchi juu ya umuhimu wa utafutaji, umiliki na utunzaji wa nyaraka.

Majibu ya Uongozi wa Wakala

Wakala inakiri kuwa ilikuwa na tatizo la kukosekana kwa gari katika ofisi yetu ya Pemba lakini kwa sasa tatizo hilo limeondoka kulingana na uhitaji wa gari uliokuwepo.

Hapo awali bajeti ya Wakala ilikuwa ipo chini ya Wizara hali ambayo ununuzi wa gari ilikuwa changamoto kutokana na upatikanaji wa fedha uliokuwa ukitegemea uingizwaji wa ruzuku kutoka serikalini, kwa Wizara.

Hatua za Utekelezaji: Ofisi ya Wakala Pemba kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imeweza kupata gari moja mpya Toyota Hilux yenye namba SMZ 732B na bodaboda moja mpya yenye namba SMZ 2217C ambazo zinasaidia

kutekeleza kikamilifu majukumu yetu ikiwemo ya kushajihisha wananchi kufanya usajili wa mali na biashara zao, katika maeneo mbali mbali.

Hata hivyo, Wakala imepanga kuongeza zaidi vyombo vya usafiri vitakavyotumika kwa ajili ya kupata ufanisi katika shughuli zetu za usajili kwa siku za usoni.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika ufuatiliaji utekelezaji wa hoja hii, Kamati ya PAC imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa za upatikanaji wa usafari kwa Ofisi ya wakala Pemba na baada ya kamati kupitia vielelezo vya ununuzi wa gari na pikipiki kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yao Kamati imeiondoa hoja hii.

BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ)

Hoja nambari 7.1.1.1: Kutokuripotiwa kwa orodha kamili ya mikopo iliyofanyiwa maboresho

Ukaguzi ulifanya mapitio ya mikopo na malipo ya awali kwa wateja waliokopa benki ya PBZ na kubaini kwamba kulikuwa na mkopo kwa mteja aliyefariki dunia, ambao ulifanyiwa marekebisho mwezi wa Machi, 2023 na kubainika uwepo wa bakaa la deni linalodaiwa la shilingi 909,814,450. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuripotiwa kwa orodha kamili ya mikopo iliyofanyiwa maboresho awali jambo ambalo lilipelekea kutokuonekana kwa deni linalodaiwa.

Kushindwa kuonyesha kwa deni hilo kwenye orodha kamili ya mikopo iliyorekebishwa inaweza kusababisha kukosekana kwa faida au kupatikana kwa hasara kwenye mikopo iliyorekebishwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuhakikisha kuwa unaandaa na kusimamia orodha iliyokamilika ya mikopo iliyofanyiwa marekebisho katika mwaka wa fedha na kuijumuisha wakati wa kufanya ukokotoaji wa faida/ hasara kwenye mikopo iliyorekebishwa.

Majibu ya Uongozi wa PBZ

Uongozi wa Benki unakubalina na hoja hii, hata hivyo orodha kamili iliwasilishwa kwa wakaguzi na hoja hii haikujumuishwa katika ripoti ya mwisho.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia ukweli wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa hoja hii haikuwa ni miongoni mwa hoja zilizowasilishwa katika hati ya mwisho ya majibu 'Management letter' kutoka Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Taasisi ya Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ). Hata hivyo, hoja hiyo imeingizwa kwenye kitabu cha Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka unaoishia Julai, 2023.

Kutokana na changamoto hiyo, Kamati ilitaka kupatiwa ufafanuzi kutoka kwa Mkaguzi na kuelezwa kwamba kwa vile ukaguzi huo ulifanywa kwa pamoja na Mkaguzi aliyepewa kazi hiyo (Joint Audit), Mkaguzi hakuwa na majibu sahihi kwa Kamati hadi atakapofanya mawasiliano na Mkaguzi aliyekaguwa katika Taasisi hiyo. Kwa mnasaba huo, Kamati ilishindwa kuendelea kuchunguza hoja hiyo hadi yatakapopatikana majibu yaliyo sahihi.

Hoja nambari 7.1.1.2: Dosari zilizobainika katika majalada ya mikopo (PBZ Convetional)

Ukaguzi ulifanya mapitio ya majalada ya mikopo na kubaini uwepo wa dosari zifuatazo:-

a) Kulingana na sera ya Benki ya Utoaji wa Mikopo imebainisha ukomo wa Ripoti za Tathmni kwa miaka mitatu, ukaguzi ulibaini uwepo wa ripoti za tathmini zilizopitwa na wakati kwa zaidi ya miaka mitano nyuma jambo ambalo ni kwenda kinyume na sera ya Benki ya Utoaji wa Mikopo. Mchanganuo wa ripoti za tathmini zilizopitwa na wakati ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli nambari 115: Ripoti za Tathmini zilizopitwa na wakati kwa mujibu wa sera ya Benki

Customer name	**currency**	**Product name**	**Total exposure in TZS**	**Valuation report issue from**	**Valiation report issued date**
The heritage Zanzibar Company Ltd usd	USD	TL	144,694,572.25	Stan Property	30/06/2018
Sabah Store Limited LTD.	USD	TL	113,128,860.97	Stan Property	02/03/2017
Urban and Rural Engeering Service	TZS.	OD	2,690,369,686.25	Stan Property	30/06/2016

Majibu ya Uongozi wa PBZ

1. The Heritage Zanzibar ni Kampuni ambayo mbia wake mkubwa Bw. Said Idd Ndombugani ambaye alikuwa anamiliki asilimia 90 ya hisa za kampuni hiyo alifariki mapema mwaka 2023 na Uongozi kulikuwa na majadiliano na uongozi wa kampuni hiyo ambao hawakuonyesha nia ya kuendelea na mkopo huo badala yake kusubiri kukamilika kwa mchakato wa kisheria wa kuhamisha hisa za marehemu kwa wanufaika wake na baada ya hapo wataondoa mkopo huo, Hii ndiyo sababu hatukuithamini mali hiyo.

2. Kuhusu Sabah Store, Uongozi pia ulijadiliana na mmiliki kuhusu hesabu yake, anakubali na tuko katika mchakato wa kuthamini mali hiyo.
3. Kwa upande wa Urban and Rural valuations' zao zilikua ziko sawa mpaka muda wa mkopo wao kumalizika muda mwaka 2022 kwa sasa mkopo wao haujafunguliwa hadi pale atakapotimiza masharti tuliomuwekea ikiwa ni pamoja na kuhuisha taarifa za hesabu ili mkopo wake wa muda mfupi urudishwe tena (renewed).
4. Dhamana zilizothaminiwa na wakadiriaji ambao hawajaidhinishwa na benki, Ukaguzi ulifanya mapitio ya majalada ya Mikopo na kubaini uwepo wa vifaa (dhamana) ambavyo vimefanyiwa tathmini na wakadiriaji (wathamini) waliokuwa hawakuidhinishwa na Benki, ambapo kwa mujibu wa kumbukumbu na sera za benki zilizotolewa Juni, 2022 imebainika kuwa PBZ iliidhinisha wathamini wawili kutekeleza uthamini wa dhamana ambao ni M/S Nasia Consults na M/S Lipaz Mthamini ambaye hakuidhinishwa na benki ni Consultants

Hii ni kwamba mthamini aliyeidhinishwa alimpatia kazi mthamini mwengine kufanya tathmini kwa niaba ya Benki ya Watu wa Zanzibar kwa kua hakuepo nchini.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya uongozi wa PBZ kukiri kuwepo kwa hoja hii, hata hivyo Kamati ya PAC imebaini mambo yafuatayo:

1. Kuna baadhi ya wakopeshwaji (The Heritage Zanzibar Company Limited ikiongozwa 'share' na Ndugu Said Idd Ndombugani) alikopeshwa mkopo na PBZ lakini alifariki kabla ya kufanywa marejesho ya Mkopo husika. Kufariki kwa muhusika huyo kumeipelekea Benki kukosa kurejeshwa kwa Mkopo kwa vile wanahisa wengine hawakutaka kuendelea na mkopo huo hadi watakapomaliza harakati za usimamizi wa mali za marehemu.
2. Tathmini iliyofanyika awali, Mtathmini hakuwa miongoni mwa Watathmini wanaotambuliwa na Serikali na kupelekea tathmini ya awali kushindwa kukubaliwa.
3. Kukosekana kwa umakini wa Watendaji wa PBZ katika ufuatiliaji na usimamizi wa mkopo wanayoitoa kwa vile walishindwa kutambua mapema kwamba Mtathmini aliyetumika hakuwa anatambuliwa na Serikali.
4. PBZ ilitekeleza majukuu yake kinyume na sera iliyopo ambayo iliwataka ukomo wa ripoti ya tathmini kwa utoaji wa mikopo usizidi miaka mitatu. Hata hivyo, PBZ ilichelewa kufanya tathmini hiyo kwani mkopo ulitolewa mwaka 2018 lakini tathimini imefanywa mwaka 2023.
5. Hatua iliyofikiwa kwasasa ni kufanyika kwa tathmini ya pili ya deni hilo na kinachosubiriwa na kufanyika kwa marejesho.

6. Kwa upande wa Sabaha Store, Kamati imegundua kwamba tathmini tayari imeshafanyika ambayo imewasilishwa kwa Mtathmini Mkuu wa Serikali na muda wowote itawasilishwa kwao.
7. Kwa upande mkopo wa 'Urban and Rural Engineering Services'. Kamati imegundua kuwa mkopo wake ulikuwa umemaliza muda wake ulioanza tangu 2016 ambapo PBZ ilimtaka apunguze deni lake na afanye tathmini ya mkopo husika lakini alishindwa kutekeleza sharti la kufanya tathmini.

Kufuatia uchunguzi huo, Kamati ya PAC imeshindwa kuiondoa hoja hiyo kwa hatua za ufuatiliaji za baadae.

Hoja nambari 7.1.1.3: Dosari zilizobainishwa katika Shariah (PBZ Islamic)

Wakati wa mapitio ya mafaili ya Mikopo, ukaguzi umebaini dosari zifuatazo:

a) Dhamana zilizothaminiwa na wakadiriaji ambao hawajaidhinishwa na benki

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na benki ya Juni, 2022 iliwaidhinisha M/S Nasia Consults na M/S Lipaz Consultants kuwa wathamini wa dhamana za benki. Katika ukaguzi uliofanyika ulipitia majalada mbali mbali na kubaini uwepo wa tathmini za dhamana zilizowasilishwa ambazo hazikutathminiwa na wathamini walioorodheshwa kwa mujibu wa toleo la Juni 2022, miongoni mwa wathamini hao ni kama inavyoonekana katika jadweli japo chini:

Jadweli nambari 116: Mthamini ambae hakuidhinishwa na Benki

Customer Name	Currency	Product name	Total exposure in TZS	Valuation report issue from	Valiation report issued date
Kendwa Limited	USD	Overdraft	167,314.17	LP Consultants	01/12/2022

Majibu ya Uongozi wa PBZ

(a) Salum Omar Simba ndiye Mthamini wa mwanzo aliyeidhinishwa na Benki ingawaje mkataba wake ulimalizika mnamo mwaka 2022 na tayari amepewa mkataba mwengine ambao utamalizika mnamo mwezi wa nne mwaka 2026.

(b) Kwenye orodha hii ya TZS 175,909,398.54 mikopo yenye thamani ya TZS 25,006,976.69 ilipata idhini ya kuondolewa kwenye vitabu na kufikia robo mwaka ya mwanzo wa mwaka 2024 mikopo hiyo iliondolewa kwa mujibu wataratibu za Benki kuu na mikopo yenye thamani ya TZS 56,220,530.81 imeshalipwa yote na wateja husika na mikopo iliyobakia ya TZS

94,681,891.06 benki inaendelea na kufuatilia kwa karibu ili nayo iweze kulipwa kama inavyotakiwa.

Benki imeupokea ushauri wa CAG na kuufanyia kazi kama ilivyoelekezwa na itahakikisha taarifa zote zinawekwa vizuri ili kuendana na matakwa ya sharia za usimamizi wa mikopo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kushughulikia hoja hii, Kamati ya PAC imebaini mambo yafuatayo:

1. Kwamba shilingi milioni 175,909,398.54 zilikuwa ni mikopo iliyomaliza muda wake kwa Wateja ambayo ilipangwa kuondolewa (written off) mwezi wa Disemba, 2023. Hata hivyo, Mikopo hiyo ilifutwa bila ya kupata idhini ya Bodi ya Wakurugenzi ambayo ndio yenye mamlaka ya kufanya maamuzi ya utendaji wa Benki.
2. Kamati ilitaka kujua sababu ya kufutwa kwa mikopo hiyo na kuelezwa kwamba kwa kufuatia kikao cha Kamati Tendaji mikopo iliamuliwa kufutwa ili kukidhi masharti ya Kanuni ya Benki Kuu ya Tanzania inayoelekeza mikopo inayozidi miaka mitatu iondolewe katika orodha ya mali za benki.
3. Kamati imebaini kwamba utaratibu wa kufutwa kwa mikopo hiyo haukufutwa kama ilivyoeleza na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nambari 12 ya Mwaka 2016 ambayo imeelekeza Bodi ya Wakurugenzi ndio yenye mamlaka ya kufutwa kwa mikopo na sio kamati Tendaji kama ilivyoelezwa na uongozi wa PBZ. Kamati ilitaka ipatiwe kielelezo cha Bodi ya Wakurugenzi (Minutes) iliyoridhia ufutwaji wa mikopo hiyo lakini hadi Kamati inakamilisha kazi zake kielelezo hicho hakikuweza kupatikana.
4. Kwa upande wa Mkataba wa Mwinyi Building Contractor Company Limited ambayo ilifanyiwa tathmini ya Simba Salum, Kamati imebaini kuwa alipatiwa kazi wakati Mkataba wake ulikuwa umeshamaliza muda wake. Kamati ilitaka kujua sababu ya kufanya hivyo ilitokana na kuchelewa kukamilika kwa tathmini yake ndio wakaamua kumruhusu kuendelea na kazi. Hata hivyo, hivi sasa mkataba wake umeshafanyiwa mapitio.

Hoja nambari 7.1.1.4: Kutokuzingatiwa kwa matakwa ya kisheria katika utoaji wa mikopo

Kwa mujibu wa kanuni ya 9 ya Kanuni za Usimamizi wa Mali hatarishi za Benki na Taasisi za Fedha za 2014. Benki au taasisi ya fedha italazimika, katika kila uhakiki wa robo mwaka, kulipia gharama zote za malipo ya mikopo na mali nyingine hatarishi ambazo zimebakia katika kitengo cha hasara kwa robo mwaka mfululizo.

Ukaguzi ulibaini kuwa kuna mikopo ambayo imekuwa katika makundi ya hasara kwa zaidi ya robo mwaka mfululizo na mikopo hii haijatozwa kulingana na mahitaji ya BoT. Hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2022, jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 2.725 ilikuwa ni mikopo ya

muda mrefu iliyochelewa kulipwa. Kati ya mikopo hiyo ukaguzi umebaini kwamba jumla ya bakaa ya shilingi bilioni 2.636 ilikuwa ni mikopo kwa benki ya PBZ Conventional na shilingi milioni 89 kwa benki ya Kiislamu ya PBZ.

Kutokana na kutokufuatwa kwa misingi ya kanuni niliyoinakili hapo juu kunaweza kupelekea kujitokeza kwa vikwazo vinavyoweza kutolewa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kutokana na dosari ya kutokukidhi matakwa ya kanuni hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuhakikisha unafuata na kutekeleza vigezo na masharti yaliyowekwa na Benki Kuu ya Tanzania ili kuepuka kujiingiza katika migongano ya kisheria ambayo inaweza ikashusha hadhi ya benki ya PBZ katika taratibu za utoaji wa mikopo ikiwa ni pamoja na kulipa fidia.

Majibu ya Uongozi wa PBZ

Kwa upande wa Benki ya Kiislamu, mikopo miwili iliyoorodheshwa kwenye kiambatanisho Nambari 3 (TZS 89 milioni) imeshalipwa yote kwa ujumla wake ndani ya mwaka 2023. Benki inaendelea kusimamia na kuhakikisha mikopo yote inalipwa kwa wakati na kwa mujibu wa kanuni na miongozo ya Benki. Vile vile inahakikisha kila robo mwaka inaipitia mikopo hiyo na kuiondoa kwenye vitabu mikopo yote inayostahili kuondolewa kwa mujibu wa taratibu zinavyoelekeza.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa kuna tofauti ya kiwango cha fedha ambacho kiliainishwa katika na Mkaguzi ambacho ni bilioni 2.725 ambayo ilikuwa ni mikopo ya muda mrefu iliyochelewa kulipwa na PBZ wakati uongozi wa PBZ jumla ya shilingi bilioni 1.6 waliyoainishiwa katika hati yao ya majibu ya mwisho 'Management letter'. Kutokana na kasoro hiyo, Kamati imeshindwa kuendelea na uchunguzi wa hoja hii hadi Mkaguzi atakapotoa ufafanuzi baada ya kufuatilia kwa Mkaguzi aliyefanya ukaguzi katika Taasisi hiyo.

Hoja nambari 7.1.1.5: Kutokufanyika kwa marekebisho ya thamani ya mikopo iliyorekebishwa

Kwa mujibu wa aya ya 5.4.3 ya Vigezo vya Kimataifa vya Ufungaji wa Hesabu (IFRS 9) "Marekebisho ya mtiririko wa pesa za kimkataba" inaeleza kwamba Wakati wa kufanya majadiliano kuhusu mtiririko wa kifedha au kufanya marekebisho ya mali kwa mujibu wa vigezo haitopelekea kutokutambuliwa kwa mali iliyojadiliwa pamoja na kiwango cha mali hiyo. Taasisi itatakiwa kuhesabu upya na kufanya utambuzi wa mali pamoja na kubaini uwepo wa faida au hasara unaoendana na thamani halisi ya wakati uliopo au italazimika kufanyika upya kwa majadiliano pamoja na marekebisho ya

mtiririko wa fedha utakaozingatia hali halisi ya wakati uliopo pale itakapohitajika.

Faida au hasara itakayopatikana itazingatia hali halisi ya wakati uliopo na itathaminishwa kwa kuangalia bakaa ya muda wa matumizi wa mali ya benki.

Kiasi cha jumla cha kubeba cha mali ya kifedha kitahesabiwa upya kama thamani ya sasa ya mtiririko wa fedha wa mkataba uliojadiliwa upya au uliorekebishwa ambao umepunguzwa kwa kiwango cha awali cha riba cha mali ya kifedha (au kiwango cha riba kinachofaa kilichorekebishwa kwa mkopo kwa kununuliwa au asili ya kifedha iliyoharibika. mali) au, inapotumika, kiwango cha faida kilichorekebishwakinachokokotolewa na aya ya 6.5.10. Gharama au ada zozote zinazotozwa hurekebisha kiasi cha kubeba cha mali iliyorekebishwa na hupunguzwa kwa muda uliosalia wa mali iliyorekebishwa.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya taarifa za benki na kubaini kuwa kulikuwa na mikopo mitatu iliyopewa jinala Freedom Logistics, Tropical Air na Wakala wa Serikali wa Uchapaji ambayo ilifanyiwa marekebisho kwa kubadilishiwa utaratibu kutoka overdraft hadi muda wa mkopo wa kawaida pamoja na kufanyiwa marekebisho muda wa ulipwaji wa mikopo hiyo jambo ambalo lilipelekea kufanyiwa marekebisho ya mtiririko wa fedha na baadae ulijadiliwa upya bila ya kuzingatia matakwa ya viwango vya kimataifa vya ufungaji wa hesabu (IFRS-9) inayotambua kigezo cha faida na hasara ya utoaji wa mikopo.

Kutokana na mapitio ya taarifa za kibenki pamoja na ukokotoaji uliofanywa imebainika kwamba benki ilitakiwa kupata hasara ya shilingi 327,842,419.35 kutokana na kutofuatwa kwa vigezo na viwango vya Kimataifa vya Ufungaji wa Hesabu (IFRS 9).

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuhakikisha inabaini faida au hasara yamarekebisho kwenye mikopo iliyorekebishwa na kutambua faida au hasara ipasavyo kulingana na kiwango.

Majibu ya Uongozi wa PBZ

Hili ni jambo jipya kwa sababu hakuna mwongozo katika kanuni kuhusu hili wala katika sera yetu. Uongozi umezingatia ushauri wa wakaguzi na itaanza kuifanyia kazi kama inavyotakiwa na kiwango cha IFRS 9.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya uongozi wa PBZ kukiri juu ya uwepo wa hoja hiyo, Kamati imebaini suala la kufanyika kwa maboresho ya thamani ya mikopo ni jambo jipya kwa PBZ. hata hivyo, Kamati ilitaka kujua kwanini PBZ ilishindwa kufuata utaratibu huo ambao umeainishwa katika muongozo wa vigezo na viwango

vya kimataifa vya ufungaji wa hesabu wa (IFRS 9) ambao upo tangu mwaka 2009 ambapo Tanzania umeridhia mwaka 2017 na kuanza kazi kidogo kidogo mwaka 2018.

Uonogozi wa PBZ ulieleza kwamba ulishindwa kutekeleza muongozo huo kwa vile walikuwa wapo katika hatua ya kujenga uwezo wa watendaji wao pamoja na kuweka sawa mfumo wao ili uweze kuendana na mabadiliko hayo. Kwasasa, PBZ wamezungumza na Mshauri Elekezi (IWA) kwa lengo la kukipatia mafunzo kitengo cha mikopo ili kiweze kutekeleza muongozo husika.

Hoja nambari 7.1.1.6: Uwepo wa Akaunti za dharura katika matawi ya benki

Ukaguzi ulifanya mapitio ya vitabu vya kumbukumbu za benki na kubaini uwepo wa akaunti za dharura zinazotumika kuwekea kumbukumbu za miamala isiyohusiana na matawi ya benki ambapo ukaguzi umeshindwa kupata ufafanuzi juu ya uwepo wa akaunti hizo.

Uwepo wa akaunti za dharura inapelekea uwezekano wa kurikodi miamala ya uwongo ambayo inaweza kusababisha kuongezeka kwa mtaji wa benki au kupungua pamoja na kutokuzingatiwa kwa madeni ya benki.

Ukaguzi ulibaini kwamba PBZ ina akaunti mbalimbali za dharura ambazo zinapelekea uwepo wa mali na madeni kutokupitiwa kwa wakati, na bakaa ya fedha kuhaulishwa katika daftari kuu la benki jambo ambalo linaweza kupelekea benki kua katika hali ya hatari ya kuzidisha thamani ya mali ambayo itaenda kuathiri taarifa ya bakaa itakayoainishwa katika hesabu za mwisho wa mwaka.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kufanya mapitio ya sera ya upatanisho ili kuweza kuendana na wakati kwa kufanya upatanisho wa taarifa za fedha pamoja na taarifa za benki kwa lengo la kuonesha usahihi wa taarifa hizo kwa wakati. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 118: Taarifa za akaunti za dharura

GL code	Amount	Amount (Tsh.)
1921	INTERBRANCH CLRG A/C FOR CENTRAL BR SUSP	213,957,725.96
415	INTERBRANCH SUSPENSE ACCOUNT	3,157,127.66
1913	SUSPENSE INTERBRANCH- OTHER BANKS POS	(304,183.35)
1911	SUSPENSE INTERBRANCH- OTHER BANKS ATMS	557,719.80
1921	INTERBRANCH CLRG A/C FOR CENTRAL BR SUSP	9,875.22

Majibu ya Uongozi wa PBZ

Akaunti zinaonyesha miamala inayofanywa nje ya mtandao wakati wa kufungwa hesabu za siku, ambayo yote husawazishwa mara tu mfumo unapofunguliwa siku inayofuata ya kazi. Kufungwa kwa mfumo mwisho ni mwa siku hufanywa tawi kwa tawi, hali inayosababisha ucheleweshaji wa miamala kutoka tawi moja lililofunguliwa na lingine lililofungwa, mfanowamiamalahiini “standing orders”, miamalaya ATM. Uongozi unalifanyia kazi na kuwasiliana na “vendor” ili kutoa ripoti inayoonyesha miamala yote inayofanywa nje ya mtandao inayohusiana na akaunti za dharura.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC haikuridhishwa na majibu yaliyowasilishwa hasa ukizingatia kwamba hakua mfumo unaotambua miamala inayofanyika nje ya wakati wa benki kutekeleza majukumu yake. Jambo ambalo ni hatari na linaweza kuitia hasara benki. Katika kutatua changamoto hiyo, PBZ imeahidi kulitatua hilo katika kipindi kifupi kijacho kwa vile hivi sasa tayari wanaendelea kufanya kazi na ‘vendor’ ambae ameuandaa mfumo huo.

Kwa mnasaba huo, Kamati imeibakisha hoja hii na kuifuatilia katika kikao kinachofuata cha Kamati.

Hoja nambari 7.1.1.7: Kutokutambulika kwa ada ya upangaji wa mikopo na mapato

Kutokana na utaratibu wa upangaji wa mikopo imebainika ya kwamba Mikopo yote itatozwa asilimia 1 ikiwa ni ada za upangaji na uchakataji ambapo kwa upande wa “letter of Credit” na “Letter of Guarantee” itatozwa asilimia 1 na kwa upande wa mikopo ya nyumba “mortgages” itatozwa asilimia

0.75 kwa thamani halisi ya bima.

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Disemba, 2023 ilibainika uwepo wa gharama za uchakataji wa mikopo zilizofikia shilingi bilioni 5.9 ambazo zilitambulika kikamilifu katika kipindi cha mwaka wa utoaji wa mikopo, ambapo kwa mujibu wa viwango vya ufungaji wa hesabu vinahitaji gharama za uchakataji wa mikopo ziweze kutambuliwa kulingana na muda wa mkopo husika.

Aidha, malipo ya ujira yatokanayo na “letter of Credit” na “Letter of Guarantee” yalibainika kufikia shilingi milioni 479 ambayo yalitambulika kikamilifu kwa mwaka 2023 na kuhitajika kugawanywa katika kipindi chote cha huduma ya mkopo.

Kutokufanyika kwa tathmini vizuri kunaweza kupelekea kujitokeza kwa ongezeko la mikopo pamoja na kushindwa kusimamia vizuri taratibu za utoaji wa mikopo kwa wateja.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuhakikisha unazingatia tathmini ya gharama za uchakataji wa mikopo katika kipindi chote cha muda wa utolewaji wa mkopo, vile vile si vyema kufanya utambuzi wa ukataji wa mikopo kwa muda wa mwaka mmoja. Hata hivyo, uongozi wa benki ni vyema kuhakikisha unazingatia Viwango vya Kimataifa vya Ufungaji wa Hesabu (IFRS) pamoja na viwango kubalifu vya kiuhasibu (GAAP).

Majibu ya Uongozi wa PBZ

Uongozi unafanya mazungumzo na "vendor" ili kupata njia bora zaidi ya kutambua ada zote na kuzigawa kwa muda wote wa uhai wa huduma iliyotolewa.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kwamba ni kweli PBZ inatoza asilimia moja ikiwa ni ada ya upangaji na uchakataji wa utoaji kwa kila huduma ya mikopo, rehani na dhamana. Kwa mujibu wa utaratibu uliopo, PBZ inatoza mara moja tu katika hatua za awali za utoaji huduma husika.

Kwa mujibu wa maoni ya Mkaguzi, PBZ imetakiwa itoze asilimia hiyo iliyoelezwa katika kila mwezi kwa kipindi chote cha utoaji huduma husika jambo ambalo linaweza kuleta usumbufu katika utekelezaji wa majukumu ya kibenki. Kwa vile hakuna muongozo unaoelekeza wakati wa utozaji wa asilimia ya huduma husika, Kamati ya PAC imeushauri uongozi wa PBZ kuendelea kutumia njia ya kutoza awali ada ya upangaji wa mikopo na mapato ili isijiingize katika gharama zaidi za kufanya marekebisho katika Mfumo wake na kuondosha changamoto zinazoweza kujitokeza. Kwa mnasaba huo, Kamati imeiondoa hoja hiyo.

Hoja nambari 7.1.1.8: Kutokuzingatiwa kwa utaratibu wa kushughulikia Malalamiko ya Wateja

Kwa mujibu wa kanuni za Benki ya Tanzania (BoT) zinazohusu ulinzi wa taarifa za fedha kwa watumiaji zimebainisha mambo mbalimbali yanayopaswa kuzingatiwa kama ifuatavyo:

- Kila mtoa huduma za kifedha atapaswa kumfahamisha mtumiaji utaratibu unaotumika wa kushughulikia malalamiko ya wateja.
- Taarifa inayorejelewa chini ya kanuni ndogo (b) utaratibu wa utatuzi wa malalamiko ya wateja kwa benki.

Ukaguzi umebaini kutokuandaliwa kwa utaratibu wa ukusanyaji wa malalamiko kwa wateja na hatua zinazochukuliwa kushughulikia malalamiko ya wateja. Kutokana na hali hiyo benki inapaswa kuwa na utaratibu wa pamoja wa upokeaji wa malalamiko na ushughulikiaji wa malalamiko ya wateja ili iweze kuboresha utoaji wa huduma kwa wateja wake na hatimae kuweza kuboresha ufanisi wa huduma zinazotolewa.

Aidha, ukaguzi uliomba kupatiwa kumbukumbu za taarifa za malalamiko ya wateja kuhusiana na utoaji wa huduma na kubaini uwepo wa mkanganyiko wa taarifa zilizopokelewa ambazo bado hazijafanyiwa kazi, ingawa mtendaji mwenye dhamana ya kushughulikia malalamiko ya wateja alibainisha kwamba malalamiko yote yamefanyiwa kazi. Mchanganuo wa taarifa hizo ni kama unavyoonekana katika Kiambatisho Nambari 6.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuzingatia upokeaji wa malalamiko kwa wakati na kuyafanyia kazi kwa lengo la kuboresha huduma za benki zinazotolewa ili kuweza kupatikanwa kwa ufanisi wa huduma hizo ikiwa ni pamoja na kuharakisha upatikanaji wa mrejesho kwa wateja kuhusiana na malalamiko yote yaliyowasilishwa na kufanyiwa kazi.

Majibu ya Uongozi wa PBZ

Imetekelezwa. Uongozi tayari umeweka mfumo kwa ajili ya kushughulikia malalamiko ya wateja.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya PAC ilitaka kujua ni utaratibu gani ambao PBZ huutumia katika kushughulikia malalamiko ya Wateja wao na kuelezwa kwamba PBZ imeanzisha kitengo cha 'Customer Experience' ambacho huwasiliana na Wateja kuwasilikiza changamoto zinazowakabili. Vile vile, PBZ imeanzisha mfumo wa CRM ambao unawawezesha Wateja kupiga simu na kutuma meseji. PBZ pia wanatoa matangazo na elimu kwa njia tofauti kwa Wateja wao pamoja na kuwatembelea.

Awali PBZ ilikuwa ikitumia njia ya 'manual' katika kuhifadhi kumbukumbu zake lakini mwezi wa 8/2023, imeanzisha mfumo wa kielektroniki ambapo kwasasa changamoto nyingi zimeweza kurekebishwa. Hata hivyo, Kamati ilitaka kujua hatua iliyofikiwa ya ushughulikiaji wa malalamiko ya wateja yaliyoorodheshwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo hadi Kamati inakamilisha kazi zake haijapatiwa mchanganuo wa malalamiko hayo kama yalivyooneshwa katika kiambatanisho husika.

Hoja nambari 7.1.1.9: Malipo ya posho la usumbufu yaliyolipwa bila ya kuzingatia taratibu za kiutumishia shilingi 30,000,000

Kwa mujibu wa kanuni nambari 89(1) ya Kanuni ya Utumishi wa Umma ya 2014 inaeleza kwamba mtumishi atakaepewa uhamisho kutoka Unguja kwenda Pemba, Tanzania Bara au kinyume chake atapaswa kulipwa posho la usumbufu litakalokuwa sawa na posho la siku saba (7) pamoja na usafiri wa ndani kwa kufidia usumbufu atakaoupata katika kutekeleza amri hiyo ya uhamisho.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Benki ya Watu wa Zanzibar imefanya malipo yenye thamani ya shilingi 30,000,000 kwa ajili ya kuwalipa watumishi walioajiriwa kwa ajira ya mkataba kwa vipindi vya rejewa rejewa kwa muda wa miaka mitatu (3) jambo ambalo haliendani na Kanuni ya Utumishi wa Umma kwa mazingatio ya kwamba watumishi hao ni waajiriwa wapya na sio waliohamishwa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine ambao ndio wanaopaswa kulipwa posho la usumbufu.

Kufanya malipo ya fedha za umma bila ya kuzingatia Kanuni za Utumishi kunaweza kupelekea uwepo wa matumizi mabaya ya fedha ambayo yataisababishia hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Bodi ya Benki ya Watu wa Zanzibar kuhakikisha unasimamia taratibu za urejeshwaji wa fedha za umma kwa kutoa miongozo kwa uongozi wa benki hiyo ili kuhakikisha wanakatwa wanufaika wote waliolipwa kinyume na utaratibu na kuweka nidhamu ya utekelezaji wa kanuni za utumishi wa Umma. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 119: Malipo ya posho la usumbufu yaliyolipwa bila ya kuzingatia taratibu za kiutumishi

Namba	Jina la Mtumishi	Kiwango cha fedha alicholipwa (Tsh.)
1.	Abdul Bilal Kandoro	5,000,000
2.	Eddie Edward Muhina	5,000,000
3.	Kassim Salim Said	5,000,000
4.	Hilal Said Amour	5,000,000
5.	Harith Habib Fentu	5,000,000
6.	Dkt. Issa Salim Mohamed	5,000,000
Jumla		**30,000,000**

Majibu ya Uongozi wa PBZ

Wafanyakazi hao waliotajwa katika jadweli wamelipwa kiwango TZS 4,260,000 kila mmoja ikiwa ni kiwango cha kuwawezesha wale waliokuwa

nje ya Zanzibar kuweza kuhamia Zanzibar kwa kuwa tayari walikuwa ni waajiriwa wa mashirika na taasisi nyinginezo nje ya Zanzibar.

Uongozi wa PBZ umepokea maelekezo ya Mkaguzi Mkuu na utahakikisha unaongeza umakini katika kufuata na kusimamia miongozo ya Utumishi wa Umma kikamilifu kama ilivyoelekeza miongozo na Kanuni za Utumishi wa umma.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia hoja hii nambari 7.1.1.9, Kamati imebaini kuwa hoja hii ni miongoni mwa hoja iliyowasilishwa katika hati ya mwisho ya majibu (Management letter) kutoka Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Taasisi ya Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ). Hata hivyo, hoja hii imeingizwa kwenye kitabu cha Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka unaoishia Julai, 2023.

Kutokana na changamoto hiyo, Kamati ilitaka kupatiwa ufafanuzi kutoka kwa Mkaguzi na kuelezwa kwamba kwa vile ukaguzi huo ulifanywa kwa pamoja na Mkaguzi aliyepewa kazi hiyo (Joint Audit), Mkaguzi hakuwa na majibu sahihi kwa Kamati hadi atakapofanya mawasiliano na Mkaguzi aliyekaguwa katika Taasisi hiyo. Kwa mnasaba huo, Kamati ilishindwa kuendelea kuifanyia uchunguzi hoja hii hadi itakapopatikana majibu yaliyo sahihi. Hivyo, Kamati imelizingatia hilo na itahakikisha inalifuatilia suala hilo katika wakati mwengine wa ukaguzi ujao.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauelekeza uongozi wa PBZ kuwa na mashirikiano ya karibu na uongozi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili changamoto za namna hii zisiweze kujitokeza.

Hoja nambari 7.1.1.10: Kutokufuatwa kwa taratibu za utoaji wa mikopo kwa watumishi waliopo katika muda wa majaribio (probation Period) shilingi 1,036,785,631

Kwa mujibu wa Muongozo wa Mtumishi aliye katika kipindi cha majaribio wenye kumbukumbu namba CAB.78/388/01/6 wa tarehe 21/02/2022 umeeleza kwamba Mtumishi wa Umma ambae yupo katika kipindi cha majaribio pamoja na mambo mengineyo hastahiki kupatiwa au kunufaika na kudhaminiwa mkopo.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi 1,036,785,631 kwa wafanyakazi wake bila ya kufuata Miongozo ya Utumishi ambapo wakati wa utoaji wa mikopo hiyo wafanyakazi hao walikuwa hawajathibitishwa kazini jambo ambalo ni kwenda kinyume na toleo nililolinakili hapo juu. Aidha,

ukaguzi umebaini mikopo hiyo ilitolewa kinyume na utaratibu wa Sera ya Mikopo ya PBZ na bila ya kuidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya PBZ.

Kutoa mikopo kwa wafanyakazi waliokuwepo katika muda wa majaribio kunaweza kupelekea kuisababishia Serikali hasara pindipo mtumishi huyo atakaposhindwa kutekeleza majukumu yake au kutokuwa na ufanisi wa utekelezaji wa kazi zake na Serikali kuamua kusitisha ajira yake.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa PBZ kuhakikisha unaongeza umakini katika kufuata na kusimamia miongozo ya Utumishi wa Umma kikamilifu ili kuweka nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali. Mchanganuo wa watumishi hao na thamani ya mikopo waliyochukuwa ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 120: Mikopo iliyotolewa kwa watumishi walio katika kipindi cha majaribio

Nam	Jina la Mtumishi	Kiwango cha Mkopo (Tsh.)	Benki (PBZ)
1.	Abdul Bilal Kandoro	206,205,000	Conventional Bank
2.	Eddie Edward Muhina	102,881,631	Conventional Bank
3.		149,000,000	Islamic Bank
4.	Kassim Salim Said	150,000,000	Conventional Bank
5.	Hilal Said Amour	150,000,000	Conventional Bank
6.	Harith Habib Fentu	83,000,000	Conventional Bank
7.	Mohamed Yussuf Nuh	70,500,000	H/O Mkopo wa Gari
		125,199,000	Islamic Bank
Jumla		**1,036,785,631**	

Majibu ya Uongozi wa PBZ

Wafanyakazi husika waliajiriwa kwa utaratibu maalumu kupitia kuchukua wataalamu katika soko (Poaching) na hivyo kusababisha kuchukuliwa pamoja na mikopo yao na ilikubalika kipindi cha makubaliano cha waajiriwa hao kujiunga na Benki ya Watu wa Zanzibar.

Aidha katika wafanyakazi wafuatao walipewa mikopo baada ya kumalizika kwa kipindi chao cha majaribio ambao ni Hilal Said Amour, Kassim Salim Said.

Aidha Uongozi wa PBZ utahakikisha kuongeza umakini katika kufuata na kusimamia miongozo ya Utumishi wa Umma kikamilifu kama ilivyoelekeza miongozo na Kanuni za Utumishi wa umma.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia hoja hii nambari 7.1.1.10, Kamati imebaini kuwa hoja hii ni miongoni mwa hoja iliyowasilishwa katika hati ya mwisho ya majibu (Management letter) kutoka Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu

za Serikali kwa Taasisi ya Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ). Hata hivyo, hoja hii imeingizwa kwenye kitabu cha Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka unaoishia Julai, 2023.

Kutokana na changamoto hiyo, Kamati ilitaka kupatiwa ufafanuzi kutoka kwa Mkaguzi na kuelezwa kwamba kwa vile ukaguzi huo ulifanywa kwa pamoja na Mkaguzi aliyepewa kazi hiyo (Joint Audit), Mkaguzi hakuwa na majibu sahihi kwa Kamati hadi atakapofanya mawasiliano na Mkaguzi aliyekaguwa katika Taasisi hiyo. Kwa mnasaba huo, Kamati ilishindwa kuendelea kuifanyia uchunguzi hoja hii hadi itakapopatikana majibu yaliyo sahihi. Hivyo, Kamati imelizingatia hilo na itahakikisha inalifuatilia suala hilo katika wakati mwengine wa ukaguzi ujao.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauelekeza uongozi wa PBZ kuwa na mashirikiano ya karibu na uongozi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili changamoto za namna hii zisiweze kujitokeza.

Hoja nambari 7.1.1.11: Mikopo iliyotolewa bila ya kuzingatia kizingiti cha ukomo wa Utumishi shilingi 1,036,785,631

Kwa mujibu wa mazingatio ya ajira za watumishi walioajiriwa kwa kipindi cha mkataba na kwa mazingatio ya mkataba wa kuingizwa kazini mtumishi wa kujaribiwa anaweza kutolewa kazini kwa kupewa taarifa ya mwezi mmoja au anaweza kutoka kazini kwa kutoa taarifa ya mwezi mmoja au kwa kulipa mshahara wa mwezi mmoja pindipo atakapokosa kutoa taarifa hiyo.

Vile vile, ikiwa muda wa kujaribiwa na kabla ya kuthibitishwa kwake kazini imeonekana kuwa hana uwezo wa kazi au amefanya kosa au amepinga amri ya kazi basi anaweza kuachishwa kazi hapo hapo (bila ya kupewa taarifa).

Ukaguzi umebaini uwepo wa mikopo yenye thamani ya shilingi 1,036,785,631 iliyotolewa kwa watumishi sita (6) wa PBZ ambayo haiendani na muda wa mkataba wa ajira ambapo ajira zilizotolewa zilikuwa na ukomo wa mkataba wa miaka mitatu (3) lakini mikopo iliyotolewa ilikuwa na kikomo baina ya miaka mitano (5) hadi saba (7) jambo ambalo ni kinyume na sera ya mikopo ya benki.

Kutoa mikopo bila ya kuzingatia kizingiti cha ajira ya mtumishi kunaweza kupelekea kusababisha hasara kwa Serikali pindipo mtumishi huyo atakaposhindwa kurejesha mikopo kwa kusimamishwa au kuondoshwa kazini kabla ya ukomo wa kizingiti cha utumishi wake.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuongeza umakini katika kusimamia misingi ya haki na taratibu za utumishi ili

kujiepusha kujitokeza kwa vitendo vya uvunjwaji wa sheria na hatimae kuibebesha Serikali mzigo wa deni usio wa lazima.

Aidha, uongozi wa Bodi ya Wakurugenzi ya PBZ kuhakikisha unatoa miongozo kwa uongozi wa PBZ ili wanufaika wote wa mikopo iliyotolewa kinyume na kuzingatia kizingiti cha utumishi wao wanawasilisha dhamana ya mikopo yao ili kuwe na kidhibiti cha kushika pindipo watakaposhindwa kulipa mikopo yao au watakaposhindwa kupewa mikataba ya nyongeza inayoendana na ukomo wa muda waliopewa kurejesha mikopo yao.

Mchanganuo wa mikopo iliyotolewa bila ya kuzingatia kizingiti cha ukomo wa utumishi ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 121: Mikopo iliyotolewa kwa watumishi walio katika kipindi cha majaribio

Namba	Jina la Mtumishi	Kiwango cha Mkopo(Tsh.)	Benki (PBZ)	Ukomo wa ajira	Muda wa kurejesha Mkopo
1.	Abdul Bilal Kandoro	206,205,000	Conventional Bank	Miaka 3	Miaka 7
2.	Eddie Edward Muhina	102,881,631	Conventional Bank	Miaka 3	Miaka 7
3.		149,000,000	Islamic Bank		
4.	Kassim Salim Said	150,000,000	Conventional Bank	Miaka 3	Miaka 5
5.	Hilal Said Amour	150,000,000	Conventional Bank	Miaka 3	Miaka 5
6.	Harith Habib Fentu	94,012,739.92	Conventional Bank	Miaka 3	Miaka 7
7.	Mohamed Yussuf Nuh	70,500,000	H/O Mkopo wa Gari	Miaka 3	Miaka 7
		125,199,000	Islamic Bank		
Jumla		**1,036,785,631**			

Majibu ya Uongozi wa PBZ

Kanuni za Utumishi za wafanyakazi wa Benki ya Watu wa Zanzibar ya mwaka 2022 ambayo imeruhusu wafanyakazi wote kupata mikopo na kulipika ndani ya miaka mitano kwa mujibu wa kipengele cha 5.3 (h) (ii) ambapo baadae kilifanyiwa marekebisho na kuwa miaka saba.

Aidha Uongozi wa PBZ utahakikisha kuongeza umakini katika kufuatana kusimamia miongozo ya Utumishi wa Umma kikamilifu kama ilivyoelekeza miongozo na Kanuni za Utumishi wa umma.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia hoja hii nambari 7.1.1.11, Kamati imebaini kuwa hoja hii ni miongoni mwa hoja iliyowasilishwa katika hati ya mwisho ya majibu (Management letter) kutoka Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Taasisi ya Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ). Hata hivyo, hoja hii imeingizwa kwenye kitabu cha Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka unaoishia Julai, 2023.

Kutokana na changamoto hiyo, Kamati ilitaka kupatiwa ufafanuzi kutoka kwa Mkaguzi na kuelezwa kwamba kwa vile ukaguzi huo ulifanywa kwa pamoja na Mkaguzi aliyepewa kazi hiyo (Joint Audit), Mkaguzi hakuwa na majibu sahihi kwa Kamati hadi atakapofanya mawasiliano na Mkaguzi aliyekaguwa katika Taasisi hiyo. Kwa mnasaba huo, Kamati ilishindwa kuendelea kuifanyia uchunguzi hoja hii hadi itakapopatikana majibu yaliyo sahihi. Hivyo, Kamati imelizingatia hilo na itahakikisha inalifuatilia suala hilo katika wakati mwengine wa ukaguzi ujao.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauelekeza uongozi wa PBZ kuwa na mashirikiano ya karibu na uongozi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili changamoto za namna hii zisiweze kujitokeza.

Hoja nambari 7.1.1.12: Mikopo iliyoidhinishwa kinyume na sera ya mikopo ya Benki shilingi milioni 458,086,631

Kwa mujibu wa utaratibu wa watumishi wanaoajiriwa kutoka sekta nyengine ya benki ambao wanakuja na mikopo yao uongozi wa PBZ unatakiwa uwataarifu Bodi ya Wakurugenzi ya PBZ ili kutoa maamuzi sahihi ya ajira za watumishi hao pamoja na kufanya maamuzi ya kina juu ya uhitaji wa mtumishi huyo kwa lengo la kuinunua mikopo hiyo kutoka benki wanazotoka.

Aidha, kwa mujibu wa sera ya mikopo ya 2023 iliyotolewa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ lending Policy, 2023) iliweka ukomo wa kiwango cha uidhinishwaji wa mkopo kwa watumishi kwa kiwango cha ukomo wa mkopo wenye thamani ya shilingi 200,000,000 ambao utaidhinishwa na Mkurugenzi mtendaji wa Benki ya PBZ, na pindipo kiwango hicho kitakapozidi kwa mtumishi wa PBZ italazimika kuombwa ridhaa kwa Bodi ya Wakurugenzi ya PBZ.

Ukaguzi umebaini uwepo wa watumishi wawili waliochukuwa mkopo binafsi (personal loan) ima kwa kuajiriwa nao au kwa kuomba Benki ya Watu wa Zanzibar uliozidi ukomo wa kiwango kubalifu kwa mujibu wa Sera za Mikopo ya PBZ, 2023 ambao umeidhinishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa PBZ bila ya kutolewa taarifa na kuidhinishwa kwenye Bodi ya Wakurugenzi

ya PBZ jambo ambalo ni kwenda kinyume na Sera hiyo pamoja na kukengeuka maamuzi ya Bodi ya Wakurugenzi ya PBZ.

Kufanya maamuzi ya uajiri wa watumishi wenye mikopo mikubwa au kuruhusiwa kuchukuwa mikopo mikubwa yenye ukomo wa idhini ya uongozi wa PBZ bila ya kushirikishwa maamuzi ya Bodi ya PBZ kunaweza kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya matumizi mabaya ya Ofisi kutokana na kufanyika maamuzi kwa maslahi binafsi na yenye kuzingatia utashi wa mtu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa PBZ kuhakikisha maamuzi yoyote wanayoyatoa ambayo yapo nje ya mamlaka ya uongozi wa PBZ ni vyema kushirikishwa Bodi ya Wakurugenzi wa PBZ ili kuweza kupata ridhaa ya maamuzi ya pamoja.

Miongoni mwa wanufaika wa mikopo hiyo iliyoidhinishwa kinyume na sera ya PBZ ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 122: Mikopo iliyoidhinishwa kinyume na sera ya mikopo ya Benki

Namba	Jina la Mtumishi	Kiwango cha Mkopo (Tsh.)	Benki (PBZ)	Ukomo wa ajira	Muda wa kurejesha Mkopo
1.	Abdul Bilal Kandoro	206,205,000	Conventional Bank	Miaka 3	Miaka 7
2.	Eddie Edward Muhina	102,881,631	Conventional Bank	Miaka 3	Miaka 7
		149,000,000	Islamic Bank		
Jumla		**458,086,631**			

Majibu ya Uongozi wa PBZ

Uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar uliitarifu Bodi ya Wakurugenzi ya Watu wa Zanzibar kupitia ripoti ya utekelezaji iliyowasilishwa kwa kipindi cha robo mwaka ya mwisho ya 2022 ambayo ilianisha kuchukuliwa kwa mikopo ya wafanya kazi (loan take over) ambayo tayari wanayo kutoka kwa waajiriwa wao wa awali na kwa kipindi cha malipo ya miaka saba.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa ni kweli mikopo ilitolewa kinyume na uaratibu wa sera za Benki ambayo inaitaka Bodi ya Wakurugenzi ya PBZ kuidhinisha mikopo yote inayotaka kutolewa. Hata hivyo, Kamati imegundua kuwa PBZ iliitumia Kamati Tendaji kuidhinisha mikopo jambo ambalo kinyume na utaratibu wa Sera na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nambari 12 ya mwaka 2016. Kutokana na kujitokeza kwa kasoro hiyo, Kamati ya PAC imeshindwa kuiondoa hoja hiyo.

Taarifa za ukaguzi wa Benki ya Mucoba kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba, 2022

Katika mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba, 2022 ukaguzi ulifanya mapitio ya taarifa za ufungaji wa hesabu wa Benki ya MuCoBa ambayo ni sehemu ya Benki ya PBZ kutokana na benki hiyo kuuza hisa nyingi kwa PBZ. Katika mapitio hayo imebainika uwepo wa dosari mbalimbali ambazo zimepelekea benki ya MuCoBa kupata Hati Yenye Shaka kutokana na uwasilishaji wa taarifa za ufungaji wa hesabu ambazo zilitolewa maoni ya ukaguzi na kubainika uwepo wa dosari mbalimbali ambazo zimepelekea kutokuonesha sura sahihi na halisi ya taarifa za hesabu zilizoandaliwa. Miongoni mwa dosari zilizobainika na kupelekea kutolewa kwa hati hiyo ni kama zifuatazo:

- **Mikopo ya wateja na malipo ya awali yenye thamani ya shilingi bilioni 4.35 kutokuendana na hali halisi ya orodha ya wateja wanaodaiwa na benki**

Kutokana na dosari hiyo ukaguzi umebaini mikopo ya wateja na malipo ya awali kwa bakaa ya fedha iliyoripotiwa katika taarifa ya fedha ni kubwa kuliko jumla ya kiasi cha mikopo na malipo ya awali kwa wateja katika vitabu vya hesabu (General Ledgers) ambayo inakubaliana na kiasi kilichobainishwa katika vitabu vya mikopo.

Kutokana na hali hiyo jumla ya shilingi bilioni 4.35 za mikopo na malipo ya awali kwa bakaa iliyowasilishwa katika hesabu ya mezania si katika deni ya bakaa ya wadaiwa iliyoripotiwa na uongozi wa benki jambo ambalo hakukuwa na hatua zilizochukuliwa kwa kulifuta au kuliondoa katika taarifa za hesabu.

- **Kutokuendana kwa orodha ya mali nyenginezo zilizobainishwa katika hesabu ya mezania zenye thamani ya shilingi bilioni 1.27**

Ukaguzi umebaini uwepo wa taarifa za mali nyenginezo (other assets) zilizobainishwa katika hesabu za mezania ambazo haziendani na uhalisia wa taarifa hizo katika orodha ya taarifa nyenginezo ambapo kiasi hicho kitapatikana na wala hakuna ushahidi wa kwamba faida za kiuchumi za baadae zitaingia Benki kuhusiana na mali hii. Licha ya hayo, wasimamizi na wakurugenzi wa Benki hawakuchukuwa hatua za kulifuta au kuondoa taarifa za mali nyenginezo katika vitabu vya benki.

Kutokana na uwepo wa dosari zilizobainishwa hapo juu imebainika mali zinazowiana zimezidishwa (overstated) kwa kiasi kilichoonyeshwa vile vile hasara ya ujumla iliyobainishwa ilipunguzwa na kufikia shilingi bilioni 5.62. Iwapo makosa yalisahihishwa, kiwango cha kodi kilipaswa kulipwa zaidi kwa shilingi bilioni 1.7 na uwiano wa msingi na jumla wa utoshelevu wa

mtaji unapaswa kuwa hasi asilimia 21.61 na asilimia 16.50 badala ya chanya asilimia 11.88 na asilimia 15.58.

- Kiasi cha Amana kinachodaiwa chenye thamani ya shilingi bilioni 1.22 kilichobainishwa katika rejista ya amana hakikubainishwa katika hesabu za mezania.
- Kiasi linganishi cha mtaji wa hisa na masalio ya mali nyingine yaliyoripotiwa katika taarifa za fedha za mwaka wa ukaguzi zinatofautiana na kiasi husika kilichoripotiwa katika taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita kwa thamani ya shilingi bilioni 1.13. Aidha, taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita zilionyesha kuwa mtaji wa hisa na mali nyinginezo ni shilingi bilioni 7.04 na shilingi bilioni 3.31. Kinyume chake, taarifa linganishi za fedha katika taarifa za fedha za mwaka huu zinaonyesha shilingi bilioni 8.17 na shilingi bilioni 4.44 mtawalia.
- Ukaguzi ulifanya mapitio ya taarifa za fedha za benki na kubaini uwepo wa shilingi milioni 598 ambazo zimetambuliwa kwa mwaka uliopita kama marekebisho ya mwaka katika taarifa ya mabadiliko ya mtaji (statement of changes in equity), hata hivyo msingi wa marekebisho hayo na maingizo ya taarifa za fedha zinazokubaliana (contra entry) hazijalingana. Aidha, mahitaji ya uwasilishaji na ubainishaji yanayohusiana na marekebisho ya mwaka uliopita kama ilivyobainishwa katika IAS 1 Uwasilishaji wa taarifa za fedha na Sera za Uhasibu na IAS 8 Mabadiliko katika Makadirio ya Uhasibu na Hitilafu hazijazingatiwa katika taarifa za fedha.
- Ukokotoaji wa mahesabu ya upotevu wa mikopo unaotarajiwa yalionyesha mikopo na malipo ya awali kwa wateja yenye jumla ya shilingi bilioni 11.19 ambayo ilikuwa chini ya kiasi kilichotambulika katika Kielelezo nambari 17 (Note 17) cha taarifa za ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kwa shilingi bilioni 15.69.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa benki kuzingatia vigezo vya mtazamo wa mbele vya uchumi mkuu (macro-economic variable) katika kukokotoa upotevu wa mikopo unaotarajiwa pamoja na kufanya mazingatio ya viwango vya kimataifa vya ufungaji wa hesabu (IFRS 9).

Majibu ya Uongozi wa PBZ

Suala la benki ya MUCOBA, hili suala halikuwa katika ukaguziwa mwaka 2023, iligundulika hali hii wakati wa ukaguzi wa mwaka 2022 iliopelekea PBZ kutakiwa kuongeza mtaji zaidi kwa benki ya MUCOBA, benki ikalipeka suala hili mbele ya Baraza la Mapinduzi, maamuzi yalitoka kwa PBZ isiongeze mtaji na kuiomba BOT kuruhusu MUCOBA iipitishe hasara hiyo kidogo kidogo kwa miaka kumi katika hesabu zake.

Na pia PBZ itafute namna ya kuziuza hisa zake kwa muekezaji mwengine hata kwa bei ya hasara. Hadi sasa PBZ ishapitisha kama tengo (provision) kwenye vitabu vyake kwa kiwango chote cha uwekezaji katika MUCOBA, TZS 5 bilioni.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kwamba PBZ imenunua hisa za asilimia 75 katika benki ya Jamii ya Mucoba ya Mufindi inayofanyakazi zake kwa hasara katika kanda ya Kusini mwa Tanzania (Iringa). Kamati ilitaka kujua hali halisi ya usimamizi na uendeshaji wa benki hiyo na kuelezwa kwamba PBZ imewekeza jumla ya shilingi bilioni 5 ambapo kutokana na hasara iliyopo, PBZ imeshapata maelekezo kutoka Baraza la Mapinduzi ya kuuza hisa zao kwenye benki hiyo ili iachane na biashara isiyo na tija.

Hadi sasa PBZ bado haijafanikiwa kuuza hisa zake kwani ilitoa nafasi kwa wale ‘minority shareholders’ wanunue hisa zake hadi Disemba 2024, lakni ilipofika muda huo ‘minority shareholders’ hao hawakuweza kupata fedha kama walivyokubaliana na PBZ. Kwa sasa PBZ inawatafuta wanunuzi wengine na iwapo ‘minority shareholders’ atapata fedha, PBZ itakuwa tayari kuwauzia hisa hizo.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati inaitaka PBZ kuhakikisha inaongeza juhudi zitakazopelekea kupata Wanunuzi wengine wa hisa zake ili kujiondoa kuendelea kufanya biashara isiyokuwa na tija.

CHUO KIKUU CHA TAIFA ZANZIBAR (SUZA)

Hoja nambari 7.1.9.1: Manunuzi wa vifaa vya kuandikia kinyume na sheria ya wakala wa Serekali wa Uchapaji Zanzibar shilingi 34,579,297

Kifungu nambari 35(1) cha Sheria nambari 12 ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji ya 2018 kinahitaji kila Taasisi ya Serikali kupeleka kazi zake zote za uchapaji na mahitaji ya vifaa vya ofisi na vya kuandikia kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji.

Ukaguzi umebaini kuwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kimefanya manunuzi ya vifaa vya ofisi na vya kuandikia nje ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji pasi na kupata idhini ya maandishi kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala kuruhusu kuchapisha au kununua vifaa vya kundikia na vifaa vya ofisi nje ya Wakala kama ilivyonakiliwa katika kifungu cha sheria hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo cha Taifa cha Zanzibar kuhakikisha unafuata miongozo ya Sheria nambari 12 ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji ya 2018 katika ununuzi wa huduma za uchapaji na ununuzi wa vifaa vya ofisi na vya kuandikia. Mchanganuo wa vifaa vya ofisi na vya kuandikia vilivyonunuliwa nje wa Wakala ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 134: Vifaa vya kuandikia vilivyonunuliwa nje ya Wakala wa Serikali waUchapaji Zanzibar

Hati Namba	Kiasi (Tshs.)	Aliyelipwa	Maelezo
PY004441 ya 3/01/2023	19,898,899	Multi-Color Printers ltd	Ununuzi wa vifaa vya kuandikia
PY004885 ya 5/11/2023	7,340,199		
PY004885 ya 5/11/2023	7,340,199		
Jumla	**34,579,297**		

Majibu ya Uongozi wa SUZA

Uongozi wa SUZA unakubaliana na hoja ya CAG kuhusiana na manunuzi ya vifaa vya kuandikia kinyume na sheria ya wakala wa Serikali wa

Uchapaji Zanzibar. Hali iliyosababishwa na changamoto kwa Wakala kutokujibu kupitia mfumo wa E-proz ambapo na changamoto kwa Wakala kutokujibu kupitia mfumo wa E-proz ambapo ilipelekea Chuo kutumia njia mbadala kununua vifaa hivyo vya kuandikia.

HATUA ZILIZOCHUKULIWA BAADA YA UKAGUZI

Katika kukabiliana na changamoto hiyo katika mwaka wa fedha 2023/2024 Chuo kilipeleka maombi kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar ya kuomba kuruhusiwa kufanya manunuzi ya vifaa kwa wasambazaji wengine kutokana na uwezo mdogo wa Wakala wa kutoa huduma hiyo kwa barua yenye Kumb. Nam. AH.17/141/01/02 ya tarehe 11/3/2024na kuruhusiwa kwa barua ya tarehe 13/3/2024 yenye Kumb. Nam. ZGP/CA.327/334/A/8Manunuzi ya vifaa hivyo yamefanyika, jumla ya shilingi 862,036,385 zimetumika sawa na wastani wa asilimia 72.1 ya fedha zilizotengwa na zilizobaki ni 333,481,815. ya shilingi 862,036,385 zimetumika sawa na wastani wa asilimia 72.1 ya fedha zilizotengwa na zilizobaki ni 333,481,815.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Pamoja kwa kukiri kwa Uongozi wa Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ya kufanya manunuzi ya vifaa nje ya mfumo wa Serikali bila ya idhini kutoka kwa Wakala wa Uchapaji wa Serikali kama Kifungu nambari 35(1) cha Sheria nambari 12 ya mwaka 2018 inavyoelekeza.

hata hivyo, wakati wa majidiliano Kamati ya PAC ilibaini kuwa Chuo hawakufanya ufuatiliaji wa barua ya ruhusa ya kutokufanya manunuzi nje ya mfumo na hatimae kufanya manunuzi kwa kampuni Binafsi, baada ya utekelezaji huo kamati imeiondoa hoja hii.

Hoja nambari 7.1.9.2: Matumizi madogo ya Fedha za Skuli ya Biashara

Kwa mujibu wa taratibu za kifedha za Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Skuli ya Biashara (Chwaka) inaandaa na kupeleka Makao Makuu ya Chuo, mtiririko wa fedha unaoonyesha mahitaji na matumizi ya fedha kwa kila robo mwaka pamoja na shughuli zote zilizopangwa kutekelezwa, kwa ajili ya kupata idhini na kuingiziwa fedha.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi umebaini kuwa Skuli ya Biashara ilikuwa na bakaa ya fedha ambayo haikutumika yenye jumla ya shilingi 532,048,298.32 jambo linalomaanisha kuwa kuna shughuli nyingi zilizopanga kutekelezwa ama hazikutekelezwa au zimetekelezwa kwa kiasi kidogo.

Ukaguzi umebaini kuwa sababu kubwa iliyopelekea kutokutumika kwa fedha hizo ni kuchelewa kukamilika kwa michakato ya manunuzi pamoja na taratibu za uidhinishaji kutoka Makao Makuu ya Chuo.

Kuwepo kwa matumizi madogo ya fedha za Skuli ya Biashara kunapelekea kuchelewa kukamilika kwa malengo yaliyowekwa na Skuli kwa wakati uliotarajiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kuweka mfumo madhubuti utakaosaidia kuharakisha michakato ya manunuzi na taratibu za uidhinishaji kutoka Makao Makuu ya Chuo ili kuziwezesha Skuli kutekeleza shughuli zao kwa ufanisi.

Majibu ya Uongozi wa SUZA

Uongozi wa SUZA unakubaliana na angalizo la CAG kuhusiana na matumizi madogo ya fedha katika Skuli ya Biashara. Hali iliyosababishwa na changamoto iliyowakabili watumishi katika matumizi ya mfumo mpya wa manunuzi (Eproz) iliyopelekea kuchelewa kwa manunuzi.

HATUA ZILIZOCHUKULIWA BAADA YA UKAGUZI

Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Uongozi wa Chuo kwa kushirikana na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar katika kukabiliana na changamoto hiyo umetoa mafunzo na uelewa kwa Uongozi wa Skuli ya Biashara kuhusiana na manunuzi ya pamoja na matumizi ya mfumo wa Manunuzi (eproz) na kuhakikisha fedha zote zinazohitajika kwa manunuzi ya pamoja zinabakishwa Makao Makuu kutoka katika bajeti zao.

Chuo pia kimechukuwa hatua ya kukagua akiba ya Skuli ya Biashara kwa kuomba “Bank Statement” ili kujua kiwango cha fedha kilichopo wanapoomba bajeti ya kila robo mwaka na kulipa tofauti wanapoomba kuidhinishiwa fedha hizo ili kupunguza limbikizo katika hesabu zao. Kuanza kwa matumizi ya *e-office* pia kumerahisisha uidhinishaji wa matumizi yanayohitajika kwa wakati. Fedha hizi zimetumika, hadi kufikia Novemba, 2024 akaunti ya Skuli ya Biashara ilikuwa na shilingi 100,801,883.49 tu.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) licha ya kukiri kuwepo kwa bakaa hiyo kama ilivyoainishwa na hoja ya Mkaguzi, wakati wa uchunguzi Kamati ya PAC imebaini kuwa sababu iliyopelekea kubakia kwa fedha hiyo katika akaunti bila kufanyika kwa matumizi yoyote kwa muda mrefu, Makao Mkauu ya Chuo iliingia makubaliano ya mkataba wa frame work contract na ndio sababu iliyopelekea kuchelewa kutumika kwa fedha hiyo.

Kwa Mnasaba huo, Kamati ya PAC baada ya kujiridhisha na vielelezo vinavyohusika na matumizi ya fedha hiyo hoja hii imeondoka.

Hoja nambari 7.1.9.3: Malipo ya fedha taslim kwa wafanyakazi wa kigeni 163,944,000

Kwa mujibu wa Kanuni namba 58(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021, “Malipo yote ya matumizi ya Taasisi ya Kibajeti na Serikali za Mitaa yatafanyika kwa mfumo wa uhaulishaji fedha”.

Katika mwaka 2022/2023 ukaguzi umebaini kuwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kimefanya malipo ya fedha taslim yenye jumla ya shilingi 163,944,000 kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi wakigeni kutoka nchini Cuba wanaofanya kazi katika Chuo hicho.

Kufanya malipo kwa fedha taslim ni kwenda kinyume na Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za2021 na kunaweza kupelekea upotevu wa fedha za umma kunakotokana na kurundikana kwa fedhataslim.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kufuata miongozo ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na Kanuni zake katika kufanya malipo ikiwemo kufanya malipo kwa njia za kibenki. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 135: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha Taslimu

Namba	**Mwezi**	**Kiasi cha Mshahara (Shs.)**
1.	Julai, 2022	14,904,000
2.	Agosti, 2022	14,904,000
3.	Septemba, 2022	14,904,000
4.	Oktoba, 2022	14,904,000
5.	Novemba, 2022	14,904,000
6.	Disemba, 2022	14,904,000
7.	Januari, 2023	13,041,000
8.	Febuari, 2023	14,904,000
9.	Machi, 2023	14,904,000
10.	Aprili, 2023	5,589,000
11.	Mei, 2023	13,041,000
12.	Juni, 2023	13,041,000

Juml a	**163,944,000**

Majibu ya Uongozi wa SUZA

Uongozi wa SUZA unakubaliana na angalizo la CAG kuhusiana na malipo ya fedha taslimu kwa wafanyakazi wa kigeni. Hali hii inasababishwa na Sera za Kimataifa zinazoizuia Cuba kufungua akaunti za benki katika nchi

HATUA ZILIZOCHUKULIWA BAADA YA UKAGUZI

Kuwepo kwa malipo taslimu kwa wafanyakazi kutoka Cuba kumetokana na nchi ya Marekani kuijumuisha Cuba katika orodha ya nchi zinazounga mkono ugaidi kwa kuiwekea vikwazo vya kiuchumi (Embargo). Vikwazo ambavyo vimepelekea na benki kuwekewa zuio la kufanya biashara na miamala ya kifedha na wananchi wa Cuba kulikopelekea kunyimwa fursa ya kufungua Hesabu (Bank Accounts) katika benki yoyote kwa ajili ya kufanyiwa malipo ya posho zao. Kwa ufafanuzi zaidi fungua link zifuatazo.

https://oncubanews.com/en/cuba-usa/obstacles-to-cuban-banking-operations-increase-due-to-u-s-sanctions-according-to-official/

"Obstacles to Cuban banking operations increase due to U.S. sanctions, according to official"

In the last three years, "more than 850 actions have been registered to prevent operations with foreign banks," according to Juan Jorge Galego, official of the Central Bank of Cuba.

https://www.wola.org/analyss/human-cost-cuba-state-sponsor-of-terrorism-list/

Tunaomba hoja hii iondolewe kwa vile ipo nje***to official"***

In the last three years, "more than 850 actions have been registered to prevent operations with foreign banks," according to Juan Jorge Galego, official of the Central Bank of Cuba.

https://www.wola.org/analyss/human-cost-cuba-state-sponsor-of-terrorism-list/

Tunaomba hoja hii iondolewe kwa vile ipo njeya uwezo wetu na nje ya uwezo wa Serikali. Hakuna uwezekano wa kuwafungulia akaunti za benki kwa sasa na bado tunawahitaji ili kuongeza nguvu katika kada za afya.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini pamoja na Uongozi wa Chuo kukubaliana na hoja ya Mkaguzi ya kufanyika kwa malipo kwa njia fedha taaslim kwa wataalam wa afya kutoka Cuba kinyume na utaratibu wa malipo kwa kutumia njia ya mifumo.

Kamati ya PAC imeelezwa kuwa Chuo hakina uwezo wa kufungua akaunti kwa wataalama kutokana na sera za kimataifa zinazoizuia cuba kufungua akaunti za benki katika nchi.

Kutoka na kadhia hiyo, Chuo kimechukua juhudi za kuaandika barua Kamesheni ya Kazi mnamo tarehe 03 Febuari 2023, ili kupatiwa ushauri na Muongozo juu ya hatua stahiki ya waajiriwa hao wa kigeni.

Kwa msingi huo, Kamati ya PAC imeibakisha hoja hii kwa ajili ya hatua zaidi za utekeleza.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauagiza Uongozi wa Chuo cha SUZA kufanya kikao cha pamoja na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na Afsi ya Rais, Fedha na Mipango kulitafutia ufumbuzi changamoto hiyo ya malipo ya fedha Taslim kwa waatakum kutoka Nchini Cuba.

Hoja Nambari: 7.1.9.4 Changamoto zinazolikabili eneo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lilioko Wilaya ya Bagamoyo

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, inamiliki eneo la shamba la Ranchi ya Zanzibar Bagamoyo (RAZABA) lenye ukubwa wa zaidi ya hekari 6,000 liliopo Makurunge katika Wilaya ya Bagamoyo Tanzania Bara lililopatikana mwaka 1976 baada ya kupata kibali kutoka kwa Kamishna wa Ardhi chenye kumbumbukumbu nambari LD/70254/12/TBR cha tarehe 24Septemba,1971.

Kupitia mazungumzo na watendaji mbalimbali wa Chuo, ukaguzi umebaini kuwa shamba hilo linakabiliwa na changamoto ya kuvamiwa na watu wanaoishi karibu nalo kunakotokana na kukosekana kwa mipango madhubuti ya kuliendeleza pamoja na kukosekana kwa hatua za kulilinda eneo hilo dhidi ya uvamizi.

Aidha ukaguzi umebaini kuwa Chuo hakina Hati ya umiliki inayothibitisha umiliki halali na haki ya matumizi ya shamba hilo.

Kukosekana kwa hati ya umiliki wa shamba hilo kunaweza kukapelekea Serikali kupoteza sehemu ya shamba au shamba lote kutokana na vitendo vinavyoendelea vya uvamizi na uharibifu unaofanywa na wananchi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kwa kushirikiana na viongozi wa Serikali kuchukuwa jitihada za haraka za kuhakikisha kunakuwa na umiliki halali wa eneo hilo ili kuweza kulidhibiti na kulizuia dhidi ya uharibifu unaoendelea kufanywa na wananchi.

Majibu ya Uongozi wa SUZA

Uongozi wa SUZA unakubaliana na angalizo la CAG kuhusiana na changamoto zinazoikabili Ranchi ya Zanzibar iliyopo Bagamoyo (RAZABA) chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Uongozi wa SUZA unaendelea kuchukua hatua kadhaa za kuhakikisha shamba hilo liko kwenye mikono

salama ikiwa ni pamoja na kuwasiliana rasmi na Wizara zinazohusika na ardhi Zanzibar na Tanzania Bara, kujadiliana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais mara kadhaa ili kufanya ufuatiliaji wa upatikanaji wa hati miliki na kukodisha kwa matumizi ya ardhi. Pamoja na Ofisi ya Rais kupitia ZIPA kutafuta muwekezaji muhimu wa kuwekeza kwenye shamba hilo.

HATUA ZILIZOCHUKULIWA BAADA YA UKAGUZI

Uongozi wa Chuo ulifanya jitihada za kupata hati ya matumizi ya eneo la RAZABA kwa kuwasiliana na Serikali ya Mkoa wa Bagamoyo na pia kuliwasilisha suala hilo Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili liweze kuratibiwa kwa ngazi ya mambo ya Muungano. Kwa barua ya tarehe 3 Februari, 2022 Kumb. **SUZA/OVC/CON.4/043** pamoja na barua ya tarehe 16 Juni, 2022 Kumb. **SUZA/OVC/CON.4/440**.

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ilitujulisha kwa barua ya tarehe 30 Juni, 2022 Kumb. **OMPR/E.10/C.6/VOL.1/27** kuwa swala hilo limepokelewa na litafanyiwa kazi. Uongozi wa SUZA ulialikwa katika kikao cha Kamati za Baraza la Wawakilishi ambapo taarifa ya ufuatiliaji wa jambo hilo liliwasilishwa. Kwasasa suala hili lipo kwa Makamu wa Pili wa Rais ingawa SUZA inaendelea kulitunza eneo hilo kwa ulinzi. Kuna wafanyakazi 15 wa SUZA waliopo RAZABA kwa lengo hilo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa changamoto hiyo ni ya muda mrefu ya kukosekana kwa hati miliki katika eneo la RAZABA liliopo (Bangamoyo), kutoka na kuchelewa kupatika kwa hati hiyo Kamati ya PAC imeibakisha hoja hii kwa ajili ya ufuatiliaji wa utekelezaji.

Hoja nambari 7.1.9.5: Kutokutumika kwa mashine na vifaa vya jikoni kwa muda mrefu

Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar moja katika jukumu lake ni kutoa taaluma kwa wanafunzi wanaojifunza fani ya mapishi, vyakula na vinywaji ambapo wanafunzi hao husoma kwa nadharia na vitendo pamoja na kujifunza mbinu za kuhudumia vikao na mikutano mikubwa kwa kutoa huduma za chakula, vinywaji, usafi na mambo mengineyo.

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 wakaguzi pamoja na mambo mengineyo walitembelea eneo la Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar kwa lengo la kutathmini shughuli za utunzaji na uimarishaji wa mali za Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar katika tawi la Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar.

Ukaguzi umebaini uwepo wa vifaa mbalimbali vya jikoni pamoja na mashine ambazo kwa muonekano ni vifaa vipya vilivyopatikana kwa muda mrefu ambavyo hadi ukaguzi unakamilika vifaa hivyo bado havijaanza kutumika

jambo ambalo linaweza kusababisha vifaa hivyo kupotea au kuharibika uimara wake kutokana na kutokufanya kazi kama vilivyokusudiwa na hatimae kupelekea uwepo wa hasara kwa Chuo na kukosekana tija iliyokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kuhakikisha unachukuwa jitihadaza makusudi kuvitumia vifaa na mashine zilizopo kwa ajili ya mafunzo ya wanafunzi, ikiwemo kuanzisha utoaji wa huduma za ufuaji wa nguo (laundry) ili mashine hizo ziweze kutumika kwa lengo la kumudu gharama ndogo ndogo za upatikanaji wa malighafi za kuwafundishia wanafunzi wanaochukuwa taaluma mbali mbali katika chuo hicho.

Majibu ya Uongozi wa SUZA

Uongozi wa SUZA unakubaliana na hoja ya CAG kuhusu kuwepo kwa vifaa mbalimbali vya jikoni na mashine ambavyo havijatumika tangu kununuliwa. Vifaa na mashine hizo zilikuwa ni sehemu ya mradi uliojenga jengo jipya lakini hakuna maelezo ya matumizi ya vifaa vilivyotolewa kwa Idara tumizi. Wakati Taasisi ilitaka kutumia vifaa na mashine hizo, iligundulikaya vifaa vilivyotolewa kwa Idara tumizi. Wakati Taasisi ilitakakutumia vifaa na mashine hizo, iligundulika (kulingana na mafundi wa Taasisi) kwamba mfumo wa umeme uliopo hauendani na mfumo wa umeme wa vifaa hivyo.

Kwa kutambua umuhimu wa kushughulikia suala hilo ili kuboresha matumizi ya rasilimali hizo, IoT inapanga kufanya ukaguzi wa kina (kwa kutumia fundi wa nje) ili kugundua tatizo mahususi la kiufundi linalohusiana na vifaa na mashine hizo na kujua njia inayowezekana ya kuhakikisha matumizi bora ya vifaa hivyo. Endapo tatizo lililokuwepo halitaweza kutatuliwa Uongozi wa SUZA utawasiliana na Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa ajili ya mnada wa vifaa na mashine hizo.

A. Uongozi ulilifanyia kazi suala la vifaa vilivyokuwa havijatumika na kubaini kuwa baadhi ya vifaa hivyo vina mapungufu ya kimifumo na kiufundi ikiwemo kutokukubaliana kwa mfumo wa umeme tunaoutumia na ule uliopo katika mashine husika na kushindwa kutumika. Kwa kushirikiana na Msajili wa Hazina iliamua kuviuza vifaa vyote vilivyokuwa na hitilafu za kiufundi ikiwemo mashine ya kukandia unga na jiko la kuokea, na “Under-counter chiller 3 door” ambacho kina matumizi zaidi ya moja (ikiwemo kuhifadhia bidhaa kwa baridi.

B. Ukarabati wa jiko la kusomeshea unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi wa Disemba, 2024. Hii itawezesha kutumika kwa vifaa ambavyo havijatumika kwa muda mrefu.

C. Kukamilisha ukarabati wa sehemu ya kufulia “laundry” na kukabidhiwa rasmi kwa barua Kumb. Nam. MF./M.6/VOLXV ya tarehe 18/05/2024 na kuzifunga mashine za kufulia kutakiwezesha Chuo kuongeza mapato yake yanayotokana na udobi.

Aidha, Chuo kinaendelea na utayarishaji wa mpango wa uwekezaji wa Chuo ili kutoa fursa ya kufanyakazi kibiashara.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC wakati wa kufuatilia Utekelezaji wa hoja hii, imegundua kasoro hizo zimetokana na kuwepo kwa mkandarasi aliyeopewa kusimamia kazi za ujenzi wa jengo hilo kutokuwa na utaalamu na uwezo wa kusimamia ujenzi hali iliyopelekea kukosekana kwa ufanisi na kusababisha kujitokeza kwa mapungufu mengi katika Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Utalii Maruhubi.

Pia, Kamati ilipokuwa ikiendelea na uchunguzi wa majibu ya hoja hii imebaini hadi sasa jengo la Chuo cha Utalii Maruhubi halijakabidhiwa Rasmi kwa Uongozi wa SUZA licha ya Chuo hicho kuwepo chini ya Uongozi wa SUZA kama Sheria inavyoelekeza na kupelekea kubakia kwa hoja hii.

Maagizo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inauagiza Uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuharakisha ukabidhishwaji wa Chuo hicho kwa SUZA ili Sheria iweze kutekelezeka

HITIMISHO

Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) ni Kamati inayosimamia masuala ya kifedha, hufanya kazi zake za uchunguzi kwa kupitia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuchunguza hoja mbali mbali zilizojitokeza katika Ripoti hizo pamoja na kuchunguza kwa njia yoyote inayofaa mambo yote yanayohusu Hesabu za Mawizara, Mashirika pamoja na Taasisi za Serikali kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Toleo la 2024.

Katika kutekeleza hayo, Kamati ya PAC ilieleza mambo ambayo imeyabaini kupitia majibu ya Watendaji na kutoa Maagizo mbali mbali kwa Wahusika kwa lengo la kuimarisha utendaji wa Mawizara, Mashirika na Taasisi za Umma. Kwa mnasaba huo, Kamati hii inaliomba Baraza lako Tukufu, kuipitia, kuijadili na hatimaye kuiridhia Ripoti hii kwa lengo la kufanyiwa kazi na Serikali.

Pamoja na maelezo hayo, Kamati ya PAC inapenda kutoa shukurani za dhati kwa Mawizara, Mashirika pamoja na Taasisi zake kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati hii wakati inatekeleza majukumu yake ya Kikatiba. Shukurani pia ziwafikie Watendaji wote wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali(CAG) kwa mashirikiano yao ya dhati kwa Kamati hii wakati wa utekelezaji wa majukumu.

Mwisho kabisa na kwa umuhimu wa pekee, tunatoa shukurani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Baraza pamoja na Watendaji wote wa Afisi ya Baraza kwa mashirikiano yao ya dhati waliyoyaonesha katika muda wote ambao Kamati hii ilipokuwa ikiwajibika.